# JINSI YA KUOMBEA WATOTO WADOGO & WATOTO WAKUBWA

Maombi ya Mwangalizi
Huu ni Urithi wa Maisha,
Neema na Mafanikio



Tena amewaambia, Mwacha watoto wadogo,
wala msiziuzie kuja kwangu; kwa maana
Ufalme wa Mungu ni wao.

Marko 10:14

MaarifaMtandaoni.com | RohoYaUnabii.Org

**JINSI YA KUOMBEA WATOTO WADOGO**

**&**

**WATOTO WAKUBWA**

**Uhamishoni Ughaibuni Mtandaoni Majumbani**



*Mimina moyo wako kama maji mbele za uso wa Bwana.*

*Inua mikono yako Kwake kwa ajili ya maisha ya watoto wa wadogo na wakubwa*

**MAOMBOLEZO 2:19**

Maombi ni Machozi yamiminikayo.

(Tears are liquid prayers)


**Shukrani kwa Baba wa Mbinguni, kwa wema na uwezeshaji Wake. Shukrani pia kwa Wasomaji, Watafsiri, Wahariri, Wahakiki, Waombaji, Washauri, Wanateknolojia nk**

1. Grace Momadi Masaka-Jersey, Marekani
2. Eline Mrema-Kilimanjaro, Tanzania
3. Elias Luwela-Rukwa, Tanzania
4. David Masaka-Kyoto, Japan
5. Stormie Omartian-Tennessee, Marekani
6. Sandra Barron-North Carolina, Marekani


How To Pray For Kids
Question: What can I pray about?
Answer: ANYTHING! God wants you to talk to Him about everything in your life. Nothing is too big or too small to talk to God about.
Question: When and where should I pray?
Answer: ANYTIME and ANYWHERE! It doesn't matter where you are; you can always talk to God. He is always with you.
Question: How long should my prayer last?
Answer: You can pray for one second or for hours. God is always listening! He loves for you to talk to Him.
Question: Can I pray with my friends?
Answer: ABSOLUTELY! Praying with your friends will make your faith and your friendships stronger.
Question: Should I always fold my hands?
Answer: Folding your hands and closing your eyes may help you to concentrate on your prayer, but you don't have to. You can talk to God while riding your bike or just sitting quietly.
Question: Should I pray out loud?
Answer: God hears you whether you pray out loud or silently. Sometimes praying out loud helps you to stay focused on your prayer. Praying silently can be done wherever you are. God hears your prayers no matter how you say them!

# UTANGULIZI

Wengi wetu tunaweza kusema kwamba mama zetu au baba zetu wamekuwa nguzo kwetu kwa ajili ya maombi yao, hakika wametutia moyo kwa maombi yao. Wakati mama yangu alipofariki nilisikitika sana kwamba sikujua ni nani atakayekuwa ananiombea kila siku! Hakika tunashukuru maombi ya wazazi pamoja na upendo wao. Na Tumeruka viunga vingi kwa ajili ya maombi yao, nao hata wametutia moyo kwa mambo mengi iwe ni shule, ndoa, taaluma au hata huduma. Maombi ya wazazi wetu yamefanya tofauti kwetu, na kwa sababu yao, tuko hai katika dunia hii.

Baba yetu wa mbinguni anajua yote kuhusu hali za familia yetu ya hapa duniani, Naye anataka tushirikiane Naye katika kuumba maisha ya watoto wetu, si tu kwa ajili ya maisha marefu, yenye maana duniani, bali pia kwa umilele katika dunia mpya. Sisi tunapaswa kuwaelimisha kwa umilele. Kitabu hiki kizuri ni msaada mkubwa katika kupata mashauri ya kuombea watoto wako, nacho kinatia moyo sana, mawazo mengi, mambo ya kuombea, na unahamasishwa kurekodi matumaini yako na maombi kwa ajili ya watoto wako wa umri wowote. Sala za kweli si kurudia-rudia maneno bila kufanya kazi yoyote au kushauri watoto. Jiunge na safari hii ya maombi unaposhughulikia mawazo ya maombi kwa ajili ya hatua mbalimbali za maisha wanazokutana nazo watoto wako wa kimwili, wa kuasili au wa kiroho, mkao wa maombi, kufunga na kuomba na kumngoja Mungu.

Kuna wakati nikiwa Shule ya Sekondari nilipenda sana kwenda Ulaya au Magharibi kusoma na mama alisema “mbona hilo jambo ni rahisi tu, hata

nauli mimi naweza kukupa, mwombe Mungu tu liwezekane, hilo ni rahisi kabisa! Ila jambo kubwa ambalo ni mtihani mgumu kwa wengi ni kumpenda Mungu, kuwa na tabia njema na kuingia malango ya mbinguni". Hakika nilipata nafasi ya kwenda kusoma Shahada ya Elimu ya viumbe Baiolojia, nami huwapa watu moyo na kuwaombea wapate vibarua na hata shule za kusoma.

Daima tunaendelea kutiwa moyo na maombi ya shangazi, wajomba, baba wakubwa, baba wadogo, mama wakubwa, mama wadogo, bibi zetu na watu wazima katika jumuiya ya Israeli ya Kiroho yaani wakina baba na mama katika Jumuiya ya imani (Fathers and Mothers in Israel). Maombi hayo mengi yametimia bila hata sisi kujua masikini. Maana kuna wakati mwingine tunapitia ujinga na ujana, na tunatanga kutoka njia ile nyofu, hapa ndiyo maombi ya wazazi na walezi yametubeba. Ila hata Mungu Mwenyewe anapenda sote tufikie wokovu, na wakati mwingine kibao huwa kinageuzwa, kwani kuna watoto wanaompenda Mungu na wapo tayari kutwaliwa kwenda mbinguni kwa neema ya Mungu ila wazazi wao hawajui wanachokifanya, hivyo ni kikwazo kwa uzoefu wa watoto kwa kuasili tabia ngumu kama vile uasherati, ugomvi, ulevi na kadhalika. Yule mwenye hekima katika familia ya kumjua Mungu, iwe mtoto au mzazi au mjukuu aendelee kuombea wengine. Sote tunabebana, tukitaka kwenda kwa haraka, tunaenda wenyewe, ila tukitaka kwenda mbali tunaenda pamoja. Mungu ametupa familia kwa sababu kama hizo, mbali na kusaidiana kwa mahitaji mengine: kimwili, kiakili, kijamii, na kiuchumi.

Nilipokuwa mdogo kule Tarime nilimtembelea bibi mzaa mama na kuishi naye kwa muda kwa vile baba alikuwa ameenda kusoma nje Uingereza, nilimsikia bibi akisali baada ya kuamka saa kumi usiku “Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo…….”. Sauti kwenye mabati yasiyo na ceiling board. Kisha akaombea watoto na wajuu wake, ila sikutambua wakati huo maombi ya bibi huyu wa Imani, kama alivyokuwa Loisi bibi wa Timotheo, maombi yake yalifunika mambo mengi, ujinga wa wajomba, na upumbavu wetu—Maombi ya wazee wa Imani yameishikilia familia pamoja. Adui hupenya kwa kiasi kikubwa kwa watoto wetu hata Shetani akijaribu kuharibu, endapo sisi tutawaombea watoto wetu, nasi tujiombee pia tutafanikiwa kwa neema ya Bwana. Twapaswa kumlilia Mungu kwa huzuni wakati wa shida tukimweleza kila kitu, hata hivyo Yeye anajua kila kitu. Ninaweza kuona sasa kile ambacho kingetokea ikiwa wazazi wangu hawangekuwa wakiniombea muda wote huo, na hasa wakati huo wa shida maishani mwangu.

Maombi yao wazazi, bibi na babu yametulinda, yametupa nguvu, na kutuongoza, hata wakati hatukung’amua kwamba tulihitaji ulinzi, nguvu, au mwongozo. Siku moja mbinguni nina hakika kwamba tutagundua uzoefu, furaha na matumaini yetu yalitokana na maombi haya yenye furaha na matumaini. Maombi yamekuwa sehemu muhimu sana ya maisha ya wengi wetu hasa baada ya Korona, nchi zimeomba na kufunga kwa miongozo ya wakina baba au mama wa taifa, tunajua kwamba maombi ni kitu ambacho hatuwezi kuishi pasipo kuwa nacho.

Wakati ulipofika wa kuoa au kuolewa wazazi wetu walianza kutuombea kwamba tufanye maamuzi sahihi ya kupata wenza sahihi wa maisha.

Mtu mmoja alisema hivi, kwamba sikuwa na papara ya kuingia kwenye ndoa. Haikutokea tu bila kutarajia nikiwa na umri wa miaka 35, niliolewa na mtu ambaye alikuwa bora kupita matarajio yangu ya maisha yote katika mambo mengi.

Najua mama yangu aliomba kwa ajili ya mume wangu mwema na kwa ajili ya maisha yangu. Ni jambo zuri kiasi gani kuwa na mama ambaye haachi kamwe kujali juu ya mambo ambayo wakati mwingine sina hata nguvu ya kushughulikia kwa vile sijayafikiria au sijafikia hatua hiyo! Jambo lingine aliloombea ni kwamba niwe na kazi ninayoipenda inayolingana na haiba na uwezo wangu na kuniletea shangwe. Nilikuwa mchanga sana katika karibu kila eneo la maisha yangu kiasi kwamba nilihisi kana kwamba siku hiyo isingekuja kwangu pia.

Lakini kama vile kupata mwenzi wa maisha katika miaka ya thelathini, kazi yangu pia ilianza wakati huo na milango ilifunguliwa kwa ajili yangu. Nilifurahia kile ninachofanya, na hilo ni jibu la maombi mengi. Ninamshukuru Mungu—kwa mama na baba yangu kwa kuwa na bidii sana kupigana kwa niaba yangu, kusali bila kukoma na kutumaini kwamba Mungu angenifikisha mahali nilipohitaji kwenda.

Mifano hii ni ya watoto mbalimbali au wazazi mbalimbali.

## Ushuhuda wa *Binti yangu* (akiwa na umri wa miaka 32)

Kiukweli, lazima niseme kwamba kwa kweli nimebarikiwa na wazazi kadhaa ambao ni wenye upendo sana na wanaojali, waelewa, na, naam, wachangamfu mno kwangu. Lakini kati ya sifa nyingi za ajabu ambazo wazazi wangu wanazo, mojawapo ninayoheshimu zaidi ni kuendelea kwao katika sala kwa ajili yangu na ndugu zangu na maisha yetu ya kila siku. Ikiwa ningekuambia jinsi maombi yao yalivyo na maana kubwa kwangu na kuleta mabadiliko katika maisha yangu, labda ningeishia kuandika zaidi ya mama yangu. Lakini kwa vile umechukua kitabu hiki kusoma maandishi yangu, nitabainisha wakati wa kukumbukwa zaidi maishani mwangu ambapo kuwa na wazazi wanaoomba kulilipa sana.

Katika muda wote wa miaka yangu kumi na minane, wazazi wangu wote wawili wamekuwa katika maombi kila mara kwa ajili ya usalama wangu. Nilipokuwa nikikulia katika jiji kubwa, sala hizo zilinilinda kutokana na hatari. Ninakumbuka waziwazi wakati fulani katika mwaka wangu wa kwanza katika shule ya upili wakati Mungu alinilinda katika ajali mbaya ya gari. Mimi na ndugu wengine wawili tulikuwa tukiendesha gari kuelekea shuleni asubuhi moja na hatukuwa tumefunga mikanda tulipogongana uso kwa uso na gari lingine lililokuwa likiingia kushoto kwenye makutano. Rafiki yangu mmoja alijeruhiwa vibaya sana aliporushwa na kupitia dirisha mbele ya gari, na yule mvulana mwingine akagonga usukani kwa uso wake. Nilikuwa kwenye kiti cha nyuma na kuishia na jeraha dogo tu, kwenye sehemu ya chini ya

mgongo wangu. Katika hali ambayo kila mtu angeweza kufa, Mungu aliweka ulinzi Wake juu ya gari na kutuokoa sisi sote watatu. Ilikuwa wakati huo maishani mwangu nilipotambua jinsi sala ilivyo muhimu, na nilipata mtazamo wazi zaidi wa uwezo wa ajabu wa Mungu katikati ya hali mbaya.

Ninawashukuru milele wazazi wangu kwa kuendelea kuombea maisha yangu. Kwa kweli imefanya tofauti sio kubwa katika kuniepusha na hatari, lakini pia kuniweka kwenye njia sahihi kama mtu wa imani, mwenye maadili.

***Ushuhuda wa Kazimoto akiwa na miaka 10***

Ninapotazama nyuma katika miaka kumi iliyopita, siwezi kukataa nguvu ya ajabu ya maombi na mahali nilipo leo kama matokeo yake. Bado nimebarikiwa na wazazi wale wale wanaonipenda na wanaojali na, ndiyo, bado wanajitahidi kuwa wacheshi. Lakini najua zaidi ya hapo awali kwamba kuwa na wazazi ambao walijali vya kutosha kuchukua wakati wa kusali daima kwa ajili ya ustawi wangu kumethibitika kuwa muhimu sana kwangu. Bila maombi ya wanafamilia wangu, ambao walifafanua nini maana ya kuomba bila kukoma, sijui mimi ningekuwa wapi jamani.

**Ushuhuda wa Rehema akiwa chuoni**

Miaka michache iliyopita, nilijikuta katika mahali pagumu. Muda niliokuwa nikiutumia katika Neno na maombi ulikuwa umekuwa wa mazoea na ratiba tu. Na kwa sababu hiyo, kulikuwa na upungufu mkubwa

katika maisha yangu. Nilikwama katika changamoto ya kifedha. Pia nilikuwa nimechomwa kisu mgongoni na mtu niliyemwamini kwa miaka mingi-kumbe alikuwa mnafiki tu. Lakini muhimu zaidi, nilikuwa nimepoteza furaha na amani yangu. Nakumbuka nilimpigia simu mama yangu usiku mmoja nikimweleza hali yangu na kumwomba aniombee. Alinijibu kwa kuniambia kwamba Mungu amenileta mahali hapa kwa sababu fulani na kwamba alikuwa akijaribu kupata usikivu wangu.

Siku iliyofuata nilipofungua Neno, nilistaajabishwa na Maandiko "Utafuteni kwanza ufalme wa Mungu, na haki Yake, na hayo yote mtazidishiwa" (Mathayo 6:33). Nilikuwa nimeisoma mara nyingi sana hapo awali lakini sikuwahi kutambua urahisi wa kina wa Fungu hilo. Nilikuwa nimekengeushwa sana na changamoto zangu binafsi kiasi kwamba nilikuwa nikimwomba Mungu mara kwa mara afanye jambo fulani litokee maishani mwangu badala ya kumtafuta Roho wa Mungu kwa kweli ili *aongoze* maisha yangu. Ilikuwa ni wakati huo nilianguka kifudifudi mbele za Bwana bila ajenda nyingine zaidi ya kumtafuta Yeye.

Haya yote ni kusema kwamba Mungu mara nyingi ataturuhusu kucheua mambo katika hali zetu zilizojaa dhiki huku tukingojea kwa subira na hivyo tutakubali mapenzi Yake kwanza kabisa ambayo ni msaada kwetu na wanadamu wenzetu pia. Na nyakati hizo za taabu, huwa chombo kilichonolewa haswa, ambacho Mungu hutumia kutuleta katika uhusiano wa ndani zaidi Naye.

Mungu amenimiminia kwenye kikombe changu zaidi ya kile ninachostahili

na ninaweza kusema kweli kwamba maombi ya dhati ya wazazi wangu kwa ajili yangu, yamekuwa msaada ili niweze kutembea kwa kina zaidi na Bwana, hakika ndiyo yamefanikisha yote. Bila shaka, ninamrejelea hasa mama yangu kwani nusu ya maombi ya baba yangu yalitengwa kuelekea mafanikio ya timu yake ya mpira.

**Ushuhuda wa Rajabu akiwa na miaka 28**

Nimebahatika kulelewa na mama na baba wanaoamini katika nguvu ya maombi. Katika maisha yangu yote, wazazi wangu walisali ili nigundue na kukumbatia kusudi ambalo Mungu alikuwa nalo kwangu hata kabla sijazaliwa. Kudumu kwao katika kumtafuta Bwana na mapenzi Yake kwa maisha yangu kulinielekeza kutoka kwa maumivu mengi ya moyo zaidi ya miongo mitatu na kubadilisha maisha yangu kwa njia za kimiujiza kweli. Tangu nilipokuwa mdogo, wazazi wangu wote wawili walisali kwamba nipate mke mwenye tabia nzuri. Waliona umuhimu wa kumwomba Mungu amlinde na kumwandaa jinsi alivyokuwa akinitayarisha. Na lazima niseme sikuweza kuwa na furaha zaidi na jinsi mambo yalivyotokea. Leo, nimeoa mke wangu mwema aitwaye Neema. Yeye ndiye mwanamke mrembo zaidi, na mcha Mungu ambaye mwanamume yeyote angeweza kumshukuru Mungu kumpata……mwenzi ambaye hunijenga katika imani, akitafuta daima kuishi maisha yanayompendeza Bwana. Yeye ni jibu la moja kwa moja kwa maombi.

Wakati fulani huko nyuma, nilipohangaika au kupambana na maisha yangu ya maombi, sikuwahi hata mara moja kuusukumilia mbali mfano

uliowekwa na wazazi wangu wawili waliojitolea sana katika sala. Katika kipindi cha maisha yangu, nimejifunza kwamba kuwa mwaminifu kwa kuomba bila kukoma ndiko kunakopelekea mambo makubwa kutokea. Ni kama saa! Najua kwamba siku moja nitawaombea watoto wangu kama baba yangu na mama yangu walivyokuwa wakiniombea.

Nina hakika nitahisi kulemewa nyakati fulani na imani yangu, nayo itachukua njia mpya. Hata hivyo, nina hakika kwamba Mungu Yule-yule aliyejibu maombi ya wazazi wangu kwa niaba yangu atakuwa mwaminifu kwa mke wangu na mimi tunapotafuta mapenzi yake kwa familia yetu.

Natumai hili litakuwa jambo la kutia moyo kwa wazazi kupanda mbegu za maombi katika maisha ya watoto wao na kumtazama Mungu akifanya mambo yote pamoja kwa wema.

## YALIYOMO

UTANGULIZI ........................................ 4
YALIYOMO ........................................ 14
SEHEMU YA KWANZA ........................................ 25
JINSI YA KUOMBEA WATOTO WADOGO ........................................ 25
Sura ya kwanza ........................................ 25
KUWA MZAZI MWENYE MAOMBI ........................................ 25
MAOMBI NI NINI NA HUWA YANAFANYAJE KAZI? ........................................ 31
Anza na Orodha Iliyobinafsishwa ........................................ 33
NENO LA MUNGU NI SILAHA YAKO ........................................ 35
Mfano Mzuri wa Maombi Yanayojibiwa ........................................ 39
Wakati Majibu Hayaji ........................................ 42
Nilisema “Kuomba,” Sio kuleta “Ukamilifu” ........................................ 43
Sura ya pili ........................................ 48
KUMWACHILIA MTOTO KATIKA MIKONO YA MUNGU, MDONDOSHE ........................................ 48
Sura ya tatu ........................................ 56
ULINZI DHIDI YA MADHARA ........................................ 56
Sura ya nne ........................................ 65
KUHISI KUPENDWA NA KUKUBALIKA ........................................ 65
Sura ya tano ........................................ 74
KUANZISHA WAKATI UJAO WA MILELE ........................................ 74
Sura ya sita ........................................ 80

KUWAHESHIMU WAZAZI NA KUPINGA UASI ........................................80
Sura ya saba ........................................................................................................ 86
KUDUMISHA UHUSIANO WA FAMILIA BORA MAHUSIANO ..................86
Sura ya nane .........................................................................................................91
KUVUTIA MARAFIKI WACHA MUNGU NA MIFANO YA KUIGWA ........91
Sura ya tisa ..........................................................................................................96
KUKUZA NJAA KWA AJILI YA MAMBO YA MUNGU ..............................96
Sura ya kumi .....................................................................................................101
AWE MTU MUNGU ALIYEMUUMBA .................................................... 101
Sura ya kumi na moja ...................................................................................... 107
KUFUATA UKWELI, KUKATAA UONGO ................................................107
Sura ya kumi na mbili .......................................................................................113
KUFURAHIA MAISHA YA AFYA NA UPONYAJI ....................................113
Sura ya kumi na tatu .........................................................................................118
KUWA NA MOTISHA YA KUTUNZA FAMILIA ....................................... 118
Sura ya kumi na nne ..........................................................................................124
KUWEKA HAMU YA KUJIFUNZA ............................................................124
Sura ya kumi na tano ....................................................................................... 128
KUTAMBUA VIPAWA NA VIPAJI VILIVYOTOLEWA NA MUNGU ....... 128
Sura ya kumi na sita ..........................................................................................134
KUJIFUNZA KUZUNGUMZA MAISHA .................................................... 134
Sura ya kumi na saba ....................................................................................... 139
MKAO WA KUVUTIWA NA UTAKATIFU NA USAFI ............................. 139
Sura ya kumi na nane ....................................................................................... 145
KUOMBA KUPITIA CHUMBA CHA MTOTO ............................................ 145
Sura ya kumi na tisa ..........................................................................................150
KUFURAHIA UHURU KUTOKA KWA HOFU .......................................... 150
Sura ya ishirini .................................................................................................. 154
KUPOKEA AKILI TIMAMU .........................................................................154
Sura ya ishirini na moja .................................................................................... 159

KUALIKA FURAHA YA BWANA .......... 159
URITHI .......... 163
Sura ya ishirini na tatu .......... 171
KUEPUKA POMBE, MADAWA YA KULEVYA NA MADAWA MENGINE .......... 171
Sura ya ishirini na nne .......... 175
KUKATAA UASHERATI .......... 175
Sura ya ishirini na tano .......... 179
KUPATA MWENZI MWEMA .......... 179
Sura ya ishirini na sita .......... 185
KUISHI BILA KUTOSAMEHE .......... 185
Sura ya Ishirini na Saba .......... 192
KUTEMBEA KATIKA TOBA .......... 192
Sura ya ishirini na nane .......... 197
KUVUNJA MAHUSIANO NA WASIOMCHA MUNGU .......... 197
Sura ya ishirini na tisa .......... 203
KUTAFUTA HEKIMA NA UTAMBUZI .......... 203
Sura ya thelathini .......... 207
KUKUA KATIKA IMANI .......... 207
Sura ya thelathini na moja .......... 215
KUPITIA MAISHA YA UJANA KWA MAFANIKIO .......... 215
SEHEMU YA PILI .......... 225
JINSI YA KUOMBEA WATOTO WAKUBWA .......... 225
Sura ya thelathini na mbili .......... 226
KUWAOMBEA WATOTO WAKO WAKUBWA .......... 226
Jinsi Ya Kuombea Watoto Wako Wakiondoka Nyumbani .......... 228
Omba Maombi Yafuatayo kwa WATOTO WAKO WAKUBWA .......... 229
1: Kujiombea kama Mzazi .......... 229
2: Kumwachilia Mtoto Wangu Mikononi mwa Mungu .......... 229
3: Kujikinga dhidi ya hatari .......... 230

4: Kujisikia Kupendwa na Kukubaliwa ....................................................230
5: Kuanzisha Wakati Ujao wa Milele ....................................................231
6: Kuwaheshimu Wazazi na Kupinga Uasi ..........................................231
7: Kudumisha Uhusiano Mzuri wa Kifamilia .......................................231
8: Kuvutia Marafiki Wacha Mungu na mifano ya kuigwa .................... 232
9: Kukuza Njaa ya Mambo ya Mungu ..................................................232
10: Awe Mtu ambaye Mungu Alimuumba ........................................... 232
11: Kufuata Ukweli, Kukataa Uongo ...................................................233
12: Kufurahia Maisha ya Afya na Uponyaji ......................................... 233
13: Kuwa na Motisha ya Utunzaji Sahihi wa Mwili ............................. 234
14: Kuweka Tamaa ya Kujifunza ..........................................................234
15: Kutambua Talanta Na Vipawa Vilivyotolewa Na Mungu .................. 234
16: Kujifunza Kuhusu Maisha ................................................................235
17: Kukaa Kuvutiwa na Utakatifu na Usafi ............................................235
18: Kuomba Kupitia Chumba cha Mtoto ................................................236
19: Kufurahia Uhuru kutoka kwa Hofu ...................................................236
20: Kuwa Na Akili Nzuri ....................................................................... 236
21: Kualika Furaha ya Bwana ................................................................ 237
22: Kuharibu Urithi wa Utumwa wa Familia ..........................................237
23: Kuepuka Pombe, Madawa ya Kulevya, na Uraibu Mwingine ........ 238
24: Kukataa Uasherati ............................................................................ 238
25: Kutafuta Mpenzi Mwaminiifu ...........................................................238
26: Kuishi Bila kinyongo na kusamehe .................................................. 239
27: Kutembea katika Toba ...................................................................... 239
28: Kuvunja Ngome Zisizomcha Mungu .................................................240
29: Kutafuta Hekima na Utambuzi ..........................................................240
30: Kukua katika Imani ...........................................................................240
31: Kuvuka Miaka ya Ujana kwa Mafanikio ..........................................241
Nyongeza ..........................................................................................................241
KUOMBA PAMOJA NA WENGINE WAZAZI ............................................241

NGUVU YA KUMWOMBEA MTOTO WAKO ........................................ 244
SAHAU! HILO HALITATOKEA! .............................................................245
MAMBO SABA AMBAYO KILA MZAZI WA MTOTO MKUBWA ANATAKIWA KUJUA. ..........................................................................246
1. Uzazi Hauna Mwisho ........................................................................246
2. Kuna changamoto Huwezi Kuzirekebisha ...............................................250
3. Mungu Anaweza Kubadilisha Kila Kitu ...................................................254
4. Unatakiwa Kujua Lazima Uache Kulaumu ............................................ 260
5. Jua Kwamba Unatakiwa Kusamehe ....................................................... 263
UJUMBE WA KWANZA KWAKE MWENYEWE: ................................ 264
UJUMBE WA PILI KWAKE MWENYEWE: ............................................266
UJUMBE WA TATU KWAKE MWENYEWE: ........................................ 268
UJUMBE WA NNE KWAKE MWENYEWE: ..........................................269
6. Unatakiwa Kujua Kuna Mzazi Mmoja Tu Mkamilifu Naye Ni Mungu Wa Mbinguni ................................................................................. 270
7. Unahitaji Kujua Unaweza Kusema Kwa Moyo Wote, ......................... 273
NGUVU YA MAOMBI ...........................................................................278
OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE KUMTAZAMA MUNGU AKIMIMINA ROHO WAKE JUU YAO. .......................................281
OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE KUSITAWISHA MOYO WA MUNGU, NENO LAKE, NA NJIA ZAKE MIOYONI MWAO . 285
OMBA ILI WATAMANI KUMJUA MUNGU .......................................... 286
OMBA ILI WATAMANI KUWA NA MOYO WA TOBA ........................292
OMBA ILI WATAMANI KUJUA KILE MUNGU AMEFANYA ..............297
OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUE KATIKA HEKIMA, UTAMBUZI, NA UFUNUO ......................................................................................303
NJIA SABA ZA KUFAA ZA KUOMBEA HEKIMA ....................................306
OMBEA MTOTO WAKO MTU MZIMA APATE UFUNUO KUTOKA MUNGU ..........................................................................................313
SABABU NNE ZA KUMWOMBA MUNGU UFUNUO .............................. 314
OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE KUTAFUTA

UHURU, UREJESHO, NA UKAMILIFU .................................................... 320
UHURU NA KUWA HURU ...................................................................... 321
UKOMBOZI NA UREJESHO ...................................................................328
MABADILIKO NA UKAMILIFU ............................................................ 334
OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE KUELEWA KUSUDI LA MUNGU KWA MAISHA YAO ............................................ 340
IKIWA MTOTO WAKO MKUBWA HANA MAANA YA KUSUDI ........345
IKIWA MTOTO WAKO MKUBWA ANAHITAJI MWELEKEO ............. 349
IKIWA MTOTO WAKO MKUBWA TAYARI ANA HISIA YA KUSUDI351
OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE FANYA KAZI KWA MAFANIKIO NA UWE NA UTULIVU WA KIFEDHA ................. 354
OMBA ILI WAWE NA BIDII NA KUFANYA KAZI KWA BIDII ........... 356
MAMBO MATANO AMBAYO BIBLIA INASEMA KUHUSU WATU WENYE KUFANYA KAZI KWA BIDII ...................................................357
IKIWA UNA MTOTO AMBAYE HAWEZI—KUTUNZA KAZI YAKE ANAACHA HAPA ANAENDA KULE. .................................................... 358
OMBEA WAWEZE KUWA NA HALI NJEMA KIUCHUMI .....................361
NJIA NANE ZA KUOMBEA USALAMA WA KIFEDHA ........................ 364
JINSI YA KUOMBEA MTOTO MTU MZIMA ALIYE NA MATATIZO YA KIFEDHA ..........................................................................................367
OMBA ILI WATOTO WAKO WATU WAZIMA WAWE NA AKILI TIMAMU ZENYE HEKIMA NA MTAZAMO MWEMA WA MAMBO. . 373
MAMBO AMBAYO NI KWELI KUHUSU AKILI YA MUUMINI .......... 377
MAMBO MATATU YA MAOMBI KWA AKILI ZA WATOTO WETU WAZIMA ........................................................................................... 378
OMBA ILI WAFANYE MAAMUZI SAHIHI KUHUSU NINI WANARUHUSU KINGIE AKILINI MWAO ............................................381
KUONDOA MTAZAMO MBAYA ........................................................ 382
HISIA TANO HASI NA MITAZAMO MBAYA YA KUEPUKA ..............384
SIFA HUPONYA AKILI, HISIA, NA MITAZAMO ...................................... 385
OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE KUZUIA USHAWISHI MWOVU NA TABIA ZENYE KUHARIBU. .......................391

WAKATI SIO KOSA LAO ........ 394
WAKATI NI KOSA LAO ........ 397
NJIA SABA ZA KUMWOMBEA MTOTO WAKO MKUBWA ILI KUPINGA ATHARI ZA UOVU ........ 400
IKIWA UNAHISI KUWA UNASHINDWA VITA ........ 401
OMBA ILI MUNGU AANGAMIZE ROHO YOYOTE YA UASI ........ 404
USISITE KUPIGA SIMU KWA UIMARISHAJI ........ 407
OMBA MTOTO WAKO MKUBWA ARUDI KWA BWANA ........ 410
WAKATI UNACHOHITAJI KUSEMA NI KIGUMU KWAO KUSIKIA ........ 413
OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE KUEPUKA UCHAFUZI WOTE WA NGONO NA VISHAWISHI ........ 420
NJIA KUMI ZA KUOMBEA WATOTO WAKO WAKUBWA KUPINGA UCHAFUZI WA NGONO ........ 424
OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE KUFURAHIA AFYA NJEMA NA UPONYAJI WA MUNGU ........ 430
KUJIFUNZA KUDUMISHA AFYA BORA ........ 437
KUMJUA YESU KAMA MPONYAJI WAO ........ 437
NJIA TANO ZA KUOMBEA AFYA NA UPONYAJI KWA WATOTO WAKO WAKUBWA ........ 441
OMBA UJASIRI WA KUZUNGUMZA NENO LA MUNGU LA UPONYAJI ........ 442
UNAPOKABILIANA NA VITISHO VIKUBWA VYA AFYA ........ 443
OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE KUFURAHIA NDOA YENYE MAFANIKIO NA KULEA WATOTO WACHA MUNGU ........ 449
OMBA MTOTO WAKO WAKUBWA AOLEWE NA MTU MWENYE TABIA YA KIUNGU ........ 457
OMBEA WATOTO WAKO WATU WAZIMA KUWA NA UHUSIANO MZURI NA WAKWE ZAO. ........ 459
OMBA KWAMBA KWAMBA AWE NA NGUVU NA KUWA NA UHUSIANO NA BWANA. ........ 461
NJIA TANO ZA KUOMBEA WATOTO WAKO WAKUBWA WAWE

WAZAZI WAZURI ....................................................................................461
NJIA KUMI ZA KUWAOMBEA WAJUKUU ZAKO ................................462
OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE KUWA NA MAHUSIANO MEMA ..........................................................................467
OMBEA MAHUSIANO MEMA NA MARAFIKI WACHA MUNGU .......468
OMBEA MAHUSIANO MEMA NA WAFANYAKAZI WENZAO .......... 470
OMBEA MAHUSIANO MEMA NA NDUGU NA DADA ........................ 472
OMBEA MAHUSIANO MEMA NA WAZAZI .........................................475
OMBA ILI WATOTO WAKO WALINDWE NA KUOKOLEWA NA NYAKATI NGUMU ............................................................................ 481
NJIA KUMI ZA KUOMBEA ULINZI KWA WATOTO WAKO WAKUBWA ........................................................................................ 484
OMBA MUNGU AMZINGIRE MTOTO WAKO NA MALAIKA .............487
OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE KUSTAHIMILI NYAKATI NGUMU ............................................................................ 494
OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAELEWE WEMA WA MUNGU ...............................................................................................497
OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WATAMBUE WANAVYOMHITAJI MUNGU ..................................................................503
OMBA ILI WATOTO WAKO WATU WAZIMA WATEMBEE KATIKA WAKATI WOTE UJAO NA MUNGU .......................................................514

## *Utangulizi*

Niliposoma mara ya kwanza Vitabu kadhaa vya wazazi kuwaombea watoto wao na nguvu inayopatikana katika kufanya hivyo, sikuwahi kuota ndoto kwamba ningeweka mkusanyiko wa shuhuda mbali mbali ambazo zingegusa maisha ya wengi katika ulimwengu wa Kiswahili. Nilichofikiria tu ni jinsi Bwana alikuwa amenifundisha njia ya kuwaombea watoto wangu kwa njia ambayo ina nguvu na yenye ufanisi—na kwamba nilitaka kushiriki hili na wazazi wengine. Kile ambacho kilikuwa kimeanza kama kikundi cha marafiki wa Magomeni Prayer group na wakina Rosemary Mwakipunda na Nsanji Mwamkonda, au Baraton Power hour Kenya, au Hamburg Prayer group of Pennslyvania, au The Carribean Prayer group in New Jersey, au Mbaki and Ngulu Prayer group au Women Prayer Warriors of Tanzania and Kenya in USA, na makundi mengine ya nchi zingine ambao walikusanyika pamoja kila siku mbashara au kwa zoom na mtandao wa WhatsaApp ili kuombea watoto, kazi na shule, kabla ya ulimwengu wa Korona kutokea hapa duniani, na hata baadaye ilikuwa safari iliyokuwa na msaada mkubwa. Hatimaye hata Makanisa pamoja na mashule yalifungwa, na zoom ikawa njia ya maisha kwa ajili yetu sote. Tulihisi nguvu ya

maombi yetu na kuona matokeo yake ya ajabu na kushangaza. Majibu ya maombi tuliyoomba kwa miaka hii mitano yalichochea imani yetu na kututia moyo kuwa na bidii ya *kuendelea* kuomba hata kama, mtoto wetu mmoja baada ya mwingine, walikua na kuondoka nyumbani ili kujenga maisha yao wenyewe.

Mwishoni, tumejumuisha sura za ziada zinazohusisha "Kuombea Watoto Wako walio watu Wazima." Sehemu hii inajumuisha maombi rahisi ya kukusaidia kuombea uzao wako kwa njia bainishi au mahususi. Hiyo ni kwa sababu wewe kama mzazi hutaacha kuwaombea watoto wako, haijalishi wana umri gani au wanaishi wapi. Watoto ni urithi, na Mungu ametupa waendeleze kuishi njozi yetu wazazi, ya kumtumikia Mungu, na kuhudumia watu na kusaidiana. Kipande hiki tutakiita *Nguvu ya Kuombea Watoto Waliofikia utu uzima.* Hata kama watoto wako tayari wamekua watu wazima nawe hujawahi kuwaombea kwa kuwa ulikuwa mtu wa dunia, asiye na imani, au kwa ujinga na hivyo kwa kutojua hukufanya vile, bado unaweza kutumia kitabu hiki kuwaombea leo. Kisha ongeza kitabu mahususi kwa ajili ya watoto watu wazima, wakati uko tayari kwa jambo la kina zaidi. Watoto wangu wana miaka ishirini na kitu sasa, na ninaendelea kutumia vitabu vyenye mawazo ya nini cha kuombea watoto na hivi vimekuwa kwangu kama mwongozo wa maombi. Basi hebu hiki kitabu kiwe mwongozo wako wa kuombea watoto., kwani hata hivyo ni msimu wa kuombea watoto, wajukuu na vitukuu sasa.

Kuna sura pia ya "Kuvuka Miaka ya Ujana kwa mafanikio.

Katika nyakati hizi nzito za ujana, ni wazi kwamba hatuwezi kumudu kusubiri hadi watoto wetu wakue na wafikie ujana (utineja au umri wa balehe, ili kushughulikia sehemu hiyo muhimu ya maisha yao katika sala. Natumaini sura hii itakukumbusha mambo ya kuombea ambayo huenda usikumbuke kuyaombea hadi yawe masuala ya dharura.

Unapoanza safari hii ya kuwaombea watoto wako, utaona kuwa ni tabia isiyoisha ndani ya moyo wako. Kuweza kuathiri vyema watoto wako katika maombi kutakuweka katika mawasiliano ya karibu nao na kushiriki kikamilifu katika maisha yao, hata baada ya wao kuondoka nyumbani. Na itachangia daima furaha yako kama mzazi. Tena itakusaidia kuanza kuombea watoto wa wengine kwa bidii, wajua mtu anakuwa na upendo wa kweli na mpendwa hasa wa Mungu pale anapoombea wanadamu wengine pia na kushugulika na wokovu wao kama vile Nuhu alivyofanya!

# SEHEMU YA KWANZA

# JINSI YA KUOMBEA WATOTO WADOGO

## Sura ya kwanza

## KUWA MZAZI MWENYE MAOMBI

Ni kazi bora zaidi. Ni kazi ngumu zaidi. Ila inaweza kukuletea furaha kuu inaweza kusababisha maumivu makubwa zaidi. Hakuna kitu cha kuridhisha na kufurahisha kama kazi hii. Hakuna kitu kinachofanya utindikiwe na kuchoka kama shuguli hii. Hakuna sehemu ya maisha yako inayoweza kukufanya ujisikie kuwa umefanikiwa zaidi wakati kila kitu kinakwenda sawa kama kusali. Hakuna sehemu ya maisha yako inayoweza kukufanya

ujisikie kuwa mtu aliyefeli kuliko mambo yanapoenda mrama wakati unaomba.

## UZAZI!

Neno lenyewe linaweza kuleta hisia zinazopingana juu ya uso wako. Tunajaribu kufanya kila tuwezavyo ili kuwalea watoto wetu. Pengine pale tunapofikiria kuwa tumeelewa kikamilifu eneo la malezi, tunajikuta kwa ghafula katika eneo jipya tena. Kila hatua ya ukuaji na kila jukwaa linawasilisha changamoto nyingine. Wakati mwingine tunapita mahali kwa urahisi. Wakati mwingine tunakutana na tufani na mawimbi ya maji. Wakati fulani tunachoka sana kiasi kwamba tunataka kukata tamaa na kukaa chini, ili tulie machozi haswa—tukijisemea moyoni, acha tufani itufikishe mahali pale itakapotupeleka, sisi hatujali, wacha mambo yawe yalivyo tu. Lakini nina habari njema. Hatutakiwi kurushwa na kugeuzwa na dhoruba hizi za mabadiliko. *Maisha ya watoto wetu si lazima yaachwe kuwa yya kubahatisha tu au pata-potea.*

Hatuhitaji kutembea tukiwa tunahema kwa wasiwasi, tukiuma kucha, tukiguguna vifundo vyetu, tukiogopa watu wawili wabaya au watesi.

Haifai kuishi kwa hofu ya kile ambacho kila awamu mpya ya maendeleo ya mtoto inaweza kuleta, na kukodolea macho hatari gani zinazoweza kuvizia kila kona. Wala si lazima tuwe wazazi wakamilifu. Tunaweza kuanza sasa hivi—dakika hii hii, kwa kweli— na hakika kuweza kuleta mabadiliko chanya katika siku zijazo za mtoto wetu. Haijawahi kuwa mapema sana na

wala kuchelewa sana. Haijalishi ikiwa mtoto ana umri wa siku tatu na mkamilifu, au umri wa miaka thelathini na anapitia talaka ya tatu kwa sababu ya tatizo la pombe au ni mwizi sokoni. Katika kila hatua ya maisha yao, watoto wetu wanahitaji na watafaidika sana na maombi yetu. Jambo kuu si kujaribu kufanya yote peke yetu kwa wakati mmoja, lakini badala yake ni kumgeukia Mzazi Mbobezi katika nyakati zote—**Baba yetu wa mbinguni**—ili kupata msaada. Ndipo, tukichukua hatua moja baada ya nyingine, ni lazima tufunike kila jambo la maisha ya mtoto wetu kwa sala. Kuna *nguvu* kubwa katika kufanya hivyo, zaidi ya vile watu wengi wanavyofikiri. Kwa kweli, usithubutu kudharau uwezo wa mzazi. Mama mmoja alisema- Sikuwa na mfano bora wa malezi kwa sababu nililelewa na mama ambaye alikuwa mgonjwa wa maradhi ya akili na mnyanyasaji sana. Niliwasimulia wenzangu kanisani kuhusu unyanyasaji huo na kupona kwangu kimiujiza kutokana na athari zake. Naam waweza kuwa na baba anayebagua watoto, kwa kupenda wengine zaidi ya wengine, ila usikate tamaa.

Pia nilisimulia jinsi kujifungua mtoto wangu wa kwanza, mwanetu Mushi kulivyonifanya nitambue kwamba nilikuwa na hatari ya kuwa mzazi mnyanyasaji kama mama yangu, ikiwa ningechagua kufuata yale niliyoyapata kwa mzazi wangu. Hapa ndiyo niligundua kwamba ikiwa tunalea watoto bila Mungu, basi tumekusudia kurudia makosa yetu ya zamani na kuiga yale ambayo tumeona kwenye kabila letu, kijijini au kwa wazazi wetu. Tukio la tokea utotoni linaweza kumulika katika akili yako na kujicheza lenyewe kichwani, kama mkandwa wa video, kwenye jukwaa la

maisha yako katika wakati wa udhaifu—kabla hata hujatambua kilichotokea. Linaweza kutokea haraka sana kiasi kwamba unahisi huna uwezo wa kulidhibiti, na linaweza kukufanya ufanye na kusema mambo yenye kuharibu watoto wako. Hili huchangiwa na hatia ambayo bila shaka hukita mizizi na kukua hadi kufikia kiwango cha kupooza au kufisha ganzi yale yaliyo mema.

Nashukuru nilikuwa na ushauri mzuri na msaada na niliweza kuondokana na tatizo hili kabla ya uharibifu wowote haujatokea kwa mtoto wangu, lakini watu wengi hawajabahatika kwa hili.

Kwa sababu nilijua kwa uchungu kwamba sikuwa na uzoefu mzuri wa mzazi wa kuiga kwake, nilikuwa na woga na wasiwasi mtoto wangu wa kwanza alipozaliwa. Niliogopa ningemfanyia yale niliyofanyiwa mimi. Nilisoma kila kitabu kilichopatikana kuhusu malezi na kuhudhuria kila semina ya Kikristo ya kulea watoto niliyoweza kupata. Nilijaribu kufanya kwa ubora nilioweza na habari hii yote nzuri na ya kusaidia, lakini haikutosha kamwe. Nilikuwa na mahangaiko mengi sana kwa ajili ya makuzi ya kijamii, kiroho, kihisia-moyo na kiakili kwa wanangu, lakini jambo la kushangaza zaidi niliogopa kwamba huenda angepatwa na jambo baya. Utekwaji nyara, kuzama majini, ajali za kuharibikiwa, majeraha yasiyoweza kurekebishwa, magonjwa, unyanyasaji wa kingono, dhuluma, ubakaji, au kifo-haya yote yalijitokeza akilini mwangu kama yenye uwezekano wa kutokea katika maisha yake ya baadaye. Kadiri nilivyojaribu kutokuwa mzazi mwenye mihemko yenye kupitiliza, kila

makala ya gazeti, au habari za televisheni kuhusu uhalifu zilinifanya nihangaikie zaidi kuhusu ustawi wa mtoto wangu.

Kwa vile tuliishi katika jiji kubwa ambalo uhalifu ulikuwa umeenea. Ilikuwa zaidi ya ambavyo ningeweza kushughulikia. Siku moja katika maombi nilimlilia Mungu, nikisema, "Bwana, hili limenishinda. Siwezi kumwekea mwanangu ulinzi wa masaa ishirini na nne kwa siku, kila wakati mpaka zifike siku 365. Je, ninawezaje kuwa na amani basi?"

Kwa majuma machache yaliyofuata Bwana alizungumza na moyo wangu kuhusu kumkabidhi mtoto wangu Kwake. Mume wangu na mimi tulikuwa tumemweka wakfu mtoto wetu kwa Mungu katika ibada ya kuwabariki watoto kanisani, lakini Mungu alitaka zaidi ya hilo. Alitaka tuendelee kumkabidhi mtoto wetu Tumaini, Kwake Yeye kila siku. Hii haikumaanisha kwamba sasa tungetelekeza wajibu wetu wote kama wazazi.

Badala yake, tungejitangaza kuwa katika ubia kamili na Mungu katika malezi. Yeye *Angekuwa na* mabega makubwa ya kuweza kubeba mzigo wa kutoa hekima ya namna ya kulea, nguvu, ulinzi, na uwezo wa juu zaidi ya sisi wenyewe. Tungefanya kazi *yetu* kuadabisha, kuadilisha, kuadhibu, kufundisha, kukuza, na "kumlea mtoto katika njia impasayo" tukijua kwamba "hata atakapokuwa mzee hataiacha njia" (Mithali 22:6). Tulipaswa kumtegemea Mungu atuwezeshe kumlea mtoto wetu ifaavyo, Naye angehakikisha kwamba maisha ya mtoto wetu yanabarikiwa.

Sehemu muhimu ya kazi yetu ilikuwa kuweka maelezo ya maisha ya

mtoto wetu katika sala. Kwa kufanya hivi, nilijifunza kutambua kila wasiwasi, woga, tashwishi, au hali yenye mashaka ambayo ilikuja akilini mwangu kama msukumo wa Roho Mtakatifu kuombea jambo hilo. Naam tulimweka mtoto wakfu, sasa tungemwomba Mungu atusaidie kumfanya asiishe maisha ya mtu mwingine, bali yale alitaka mtoto wetu aishi.

Nilipomfunika mwanangu Nyafanga katika maombi na kumwachilia mikononi mwa Mungu, Mungu aliyaacha huru mawazo yangu kuwa kutoka katika wasiwasi huo. Hii haimaanishi kwamba mara nilipoomba kwa ajili ya jambo fulani sikushugulika na kusali kuhusu jambo hilo tena, lakini angalau kwa muda niliondolewa mzigo huo. Na hali hiyo ilipojitokeza tena, nilisali kuhusu hilo tena.

Mungu hakuahidi kwamba kamwe jambo lolote baya lisingemfikia mtoto wangu, lakini kuomba kuliachilia nguvu ya Mungu ya kufanya kazi katika maisha yake, na nikaweza kufurahia amani zaidi. Pia nilijifunza kwamba nisijaribu kulazimisha mapenzi yangu kwa mtoto wangu katika sala. Mfano 'ningependa mwanangu awe mwanasheria tu' Hii inasababisha tu kufadhaika na kukata tamaa kwa wote wanaohusika, yaani mtoto na mzazi na hata ndugu wengine. Nafikiri umeona na kujua sasa aina za sala ninazomaanisha, kwa sababu sisi sote tuna jaribu hilo, wacha nitoe mifano tena: "Mungu, naomba kwamba mwanangu akue na kuoa binti ya rafiki yangu mkubwa." *(Wazazi wake wangekuwa wakwe zake.)* Au, "Bwana, ruhusu binti yangu akubalike kusajiliwa katika chuo

cha Uhamiaji." *(Kisha naweza kujisikia vizuri zaidi kuhusu nafsi yangu.)* Bila shaka hatuwezi kamwe kukiri kwa uangalifu maneno yaliyo kwenye mabano, lakini yapo nyuma ya akili zetu, yakituchochea kwa hila, na kulazimisha mapenzi yetu katika sikio la Mungu. Nimeona ni bora zaidi kuomba kwa kufuatana na mapenzi Yake- "Bwana, nionyeshe jinsi ya kumwombea mtoto huyu. Nisaidie kumwinua na kukaa katika njia yako, na mapenzi Yako yatimizwe katika maisha yake.".

Kufikia wakati binti yetu, Fatuma, alipozaliwa miaka minne na nusu baada ya kijana wangu wa kiume kuzaliwa, Mungu alikuwa amenifundisha maana ya kusali kwa kina na kuombea maisha ya mtoto wangu.

Katika miaka kumi na miwili iliyofuata Mungu alijibu maombi yangu kwa njia nyingi za ajabu, na leo ninaona matokeo.

Mume wangu na mimi tunatambua mkono wa Mungu juu ya maisha ya watoto wetu, na wao hukubali kwa urahisi pia. Maana ni nguvu ya Mungu inayopenya kwenye maisha ya mtoto, mzazi anapoomba.

## MAOMBI NI NINI NA HUWA YANAFANYAJE KAZI?

Maombi ni zaidi ya kutoa tu orodha ya matamanio kwa Mungu, kana kwamba alikuwa ni ndugu milionea. Maombi ni kukiri na kuhisi uwepo wa Mungu na kualika uwepo Wake katika maisha na hali zetu. Ni kutafuta *uwepo* wa Mungu na kuachilia *nguvu* ya Mungu ambayo inatupa njia ya kushinda shida yote. Maombi ni kumruhusu Mungu atuumbie moyo safi na kutusaidia kufanya tuishi kwa kile alichotuitia, kwani mafanikio ni kufanya

kile Mungu anataka tufanye, na kuishi pale Mungu anataka tuishi.

Biblia inasema, “Lolote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni, na lolote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni” (Mathayo 18:18). Mungu anatupa mamlaka duniani. Tunapochukua mamlaka hayo, Mungu hutupatia nguvu kutoka mbinguni. Kwa sababu ni nguvu *za Mungu* na si zetu, basi sisi tunakuwa chombo ambamo nguvu Zake hutiririka. Tunapoomba, tunaleta uwezo huo juu ya kila kitu tunachoombea, na tunaruhusu nguvu za Mungu kufanya kazi kupitia kutokuwa na uwezo kwetu. Tunapoomba, tunajinyenyekeza mbele za Mungu na kusema, “Ninahitaji uwepo Wako na nguvu Zako, Bwana. Siwezi kufanya hivi bila Wewe.” Wakati hatuombi, ni kama tunasema hatuna haja ya kitu chochote nje ya nafsi zetu. Kama sisi wazazi hatuwapi watoto wetu ng’e au mawe wanapoomba mkate, Naye Bwana hatawapa vitu vibaya wanapoomba hekima ya Roho Wake.

Kuomba katika Jina la Yesu ni ufunguo mkuu wa nguvu za Mungu. Yesu alisema, “Amin, amin, nawaambia, lolote mtakalomwomba Baba kwa Jina Langu, atawapa” (Yohana 16:23). Kuomba katika Jina la Yesu hutupatia mamlaka juu ya adui na inathibitisha kwamba tuna imani katika Mungu kufanya kile ambacho Neno lake linaahidi. Kuomba katika Jina la Yesu siyo ndumba au hirizi fulani, bali kuamini tabia, uwezo, na sifa Zake.

Mungu anajua mawazo yetu na mahitaji yetu, na Yeye anajibu maombi yetu. Hiyo ni kwa sababu sikuzote Yeye anatupa uchaguzi kuhusu kila jambo, na kutuongoza kwa undani ikiwa tutamwamini na kumtii kwa kuomba katika

Jina la Yesu.

Kuomba hakutuathiri sisi pekee tu, bali pia kunawafikia na kuwagusa wale tunaowaombea. Tunapowaombea watoto wetu, tunamwomba Mungu afanye uwepo wake kuwa sehemu ya maisha yao na kufanya kazi kwa nguvu kwa niaba yao. Hiyo haimaanishi kutakuwa na jibu *la papo hapo* kila wakati. Wakati mwingine inaweza kuchukua siku, wiki, miezi, au hata miaka. Lakini maombi yetu hayapotei wala hayapotezi maana yake. Ikiwa tunaomba, basi jambo fulani linatokea, iwe tunaweza kuliona au la. Biblia inasema, “Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii” (Yakobo 5:16).

Yote ambayo yanahitaji kutokea katika maisha yetu na maisha ya watoto wetu hayawezi kutokea bila uwepo na nguvu za Mungu. Maombi hualika na kuhusisha yote mawili.

**Anza na Orodha Iliyobinafsishwa**

Mimi nilianza kuombea kila mmoja wa watoto wangu tangu walipotungwa mimba kwa sababu Biblia inasema, Bwana “Amewabariki watoto wako ndani yako” (Zaburi 147:13). Niliamini katika nguvu ya maombi. Kile ambacho *sikutambua* wakati huo ni jinsi kila sehemu ya maisha yetu ni muhimu Kwake Bwana. Haitoshi kuombea tu mahangaiko ya wakati huu; tunahitaji kusali kwa ajili ya wakati ujao, na tunahitaji kuomba dhidi ya madhara ya matukio ya zamani. Mfalme Daudi alipokuwa amehuzunika kwa sababu ya kile alichokifanya, na kilichotokea katika maisha yake na kuogopa matokeo ya wakati ujao (Zaburi 143), hakusema tu, “Loo,

chochote kitakachokuwa kitakuwa basi, wacha mambo yaende tu." Hapana, yeye alimlilia Mungu kuhusu wakati uliopita, wa sasa, na wakati ujao wa maisha yake. Aliomba juu ya *kila kitu.* Na hivyo ndivyo tunapaswa kufanya nasi.

Ili kufanya hivyo kwa ufanisi, niliona nililazimika kutengeneza orodha binafsi pana kwa kila mtoto. Huu haukuwa mtazamo fulani wa kufuata sheria ambao ulisema, "Ikiwa sitaomba kila jambo mahususi, Mungu hatalifunika." Nilikuwa na amani zaidi nilipojua kwamba Mungu alikuwa amesikia kila mojawapo ya mahangaiko yangu mengi na Roho Wake anatuomba kwa kuugua kusikotamka, katika mengi zaidi tusiyojua kwamba tunayahitaji. Kwa hiyo mara moja kwa mwaka, tulipoenda ufuoni mwa bahari kwa ajili ya likizo ya familia yetu, nilitumia saa hizo nilizozipenda asubuhi na mapema kabla mtu mwingine yeyote hajaamka ili kuwa na wakati pamoja na Mungu kutengeneza orodha kuu ya maombi.

Ningeketi na kutazama nje baharini, nikiwa na penseli na karatasi mkononi, na kumwomba Mungu anionyeshe jinsi ya kuombea kila mtoto katika kipindi cha miezi kumi na miwili ijayo. Kwani baada ya yote, Yeye peke yake Ndiye aliyejua kwa hakika kile ambacho kila mtoto alihitaji na changamoto ambazo wangekabili katika siku zijazo. Biblia inasema, "Siri ya BWANA iko kwao wamchao" (Zaburi 25:14). Yeye Anatufunulia mambo tunapoomba. Mungu kila mara alikutana nami pale na mausia mazuri, na nilirudi nyumbani na orodha za maombi kwa kila mmoja wa watoto wangu. Kisha, mwaka mzima, niliendelea kuongeza mambo mengine,

wakati wowote nilipohitaji kufanya hivyo.

Nimezihifadhi nyingi za orodha hizo, na ninapozitazama sasa na kuona majibu yote ya maombi yangu, ninatekewa na uaminifu wa Mungu wa kufanya kazi katika maisha ya watoto wetu.

## NENO LA MUNGU NI SILAHA YAKO

Vita vya maisha ya watoto wetu vinapiganwa magotini. Tusipoomba, ni sawa na kukaa pembeni na kuwa watazamaji tu wakati watoto wetu wapo katika eneo la vita, wakipigwa risasi kutoka kila pembe. Tunapoomba, tuko kwenye vita pamoja nao, tukibeba nguvu za Mungu kwa niaba yao. Ikiwa pia tunatangaza Neno la Mungu katika maombi yetu, basi tunachukua silaha yenye nguvu ambayo hakuna adui anayeweza kushinda. Biblia ina zaidi ya ahadi 10,000 za kuombea watoto wetu, kitabu cha Isaya kina zaidi ya ahadi 1000, kitabu cha Yeremia kina zaidi ya ahadi 1000 na vitabu hivi vina ahadi za ajabu kwa wana wetu wa kiroho na kimwili!

Neno la Mungu "li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili" (Waebrania 4:12) na huchoma kila kitu linachogusa. Mungu anasema Neno Lake, "halitamrudia bure, bali litatimiza mapenzi Yake, nalo litafanikiwa katika mambo yale aliyoyatuma" (Isaya 55:11). Kwa maneno mengine, Neno Lake kamwe halifanyi kazi bila ya kuleta matunda. Ndiyo maana nimejumuisha mistari kadhaa ya Biblia kufuatia kila moja ya mifano ya maombi.

Unapomwombea mtoto wako, jumuisha mstari wa Maandiko unaofaa katika sala yako. Ikiwa huwezi kufikiria mstari wakati unaomba, usiruhusu hilo likuzuie, wewe nukuu mstari mmoja au miwili kila unapoweza na utaona mambo makubwa yakitokea.

Unaposoma Neno wakati wa ibada yako na unapowaombea watoto wako kwa uongozi wa Roho Mtakatifu, utapata Maandiko mengi zaidi ya kujumuisha. Na sio lazima uwe na aya tofauti kwa kila sala. Unaweza kuwa na aya moja au mbili tu, unazotumia mara kwa mara wakati wa msimu maalum wa maombezi kwa mtoto wako. Kwa mfano, binti yangu alipokuwa na matatizo shuleni, kila mara tuliposali kuhusu jambo hilo pamoja nilimtia moyo anukuu hivi: “Naweza kufanya mambo yote kupitia Kristo anayenitia nguvu” (Wafilipi 4:13). Nilipoomba kuhusu jambo hilo peke yangu, niliweka ndani mstari huo wa ahadi, “Wenye haki wanalia, Naye BWANA akasikia, na kuwaponya na taabu zao zote” (Zaburi 34:17).

Tunapotumia Neno la Mungu katika maombi, tunashikilia ahadi anazotupa na kuziweka katika maisha ya watoto wetu.

Kupitia Neno Lake, Mungu hutuongoza, huzungumza nasi, na kutukumbusha kuwaYeye ni mwaminifu. Kwa njia hiyo, Yeye hujenga imani ndani ya mioyo *yetu* na kutuwezesha kuuelewa moyo *Wake.* Hii inatusaidia kuomba kwa ujasiri katika imani, tukijua hasa Ukweli W*ake,* mapenzi Y*ake ,* na mamlaka *yetu* ni nini.

Yesu alipozungumza na Shetani, alimkemea. Wakati fulani katika kufanya hivi alinukuu Maandiko. Kwa mfano, Shetani alipomwambia Yesu, “Ikiwa utanisujudia, yote yatakuwa yako,”

Yesu akajibu, “Nenda nyuma Yangu, Shetani! Kwa maana imeandikwa, ‘Msujudie Bwana Mungu Wako, umwabudu Yeye peke yake” (Luka 4:7,8). Yesu Ndiye kielelezo chetu. Tunapaswa kumtazama kwa makini na kufanya kile Anachofanya Yeye. Alisema, “Amin, amin, nawaambia, Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya; na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba Yangu” (Yohana 14:12). Pia alisema, “Ninyi mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa” (Yohana 15:7). Tunaweza kumpinga Shetani kwa ufanisi zaidi ikiwa tunaomba kwa Mungu kulingana na maagizo Yake yanayopatikana katika Maandiko, na ikiwa tunaelewa uwezo na mamlaka tuliyopewa kupitia Yesu Kristo. Ikiwa sisi…

*TUNAMTAZAMA,*

*TUNATEMBEA* pamoja Naye, TUNAMNGOJEA*,*

*TUNAMWABUDU* na

*kuishi* katika *NENO Lake, NI HAKIKA*

*TUTASHINDA* vita hivi kwa ajili ya watoto wetu.

Wakati wowote unapomuombea mtoto wako, fanya hivyo kana kwamba

unaombea maisha yake, YALIYO HATARINI—kwa sababu ndivyo hasa unavyofanya. Kumbuka kwamba ingawa Mungu ana mpango kamili kwa maisha ya watoto wetu, Shetani ana mpango kwa ajili yao pia. Mpango wa Shetani ni kuwaangamiza, na atajaribu kutumia njia yoyote iwezekanavyo kufanya hivyo: madawa ya kulevya, ngono chafu au kinyume na maumbile, uzinzi, uasherati, chuki, kutofundishika, kukataa shule, kutopenda kazi, pombe, uasi, ajali, kutoa mimba, magonjwa na kadhalika. Lakini hataweza kutumia kwa mafanikio chochote kati ya vitu hivyo ikiwa nguvu zake zimetawanywa kwa maombi. Biblia inasema, "Awezaje mtu kuingia katika nyumba ya mtu mwenye nguvu na kuteka mali yake, asipomfunga kwanza yule mwenye nguvu? (Mathayo) 12:29). Kwa maneno mengine, hatuwezi kuathirika kwa njia yoyote katika eneo la Shetani ikiwa tutachukua mamlaka juu yake na kupinga mamlaka yake yoyote hapo. Hivyo, tunaweza pia kumkataza kupata maisha ya watoto wetu. Bila shaka, Shetani anaweza kuleta madhara mengi ikiwa hatuwafundishi watoto wetu njia za Mungu na Neno la Mungu na kuwasaidia waheshimu sheria za Mungu, na ikiwa hatuwaadabishi, hatuwaelekezi, na kuwasaidia wajifunze kumcha Mungu. Chaguzi ni muhimu. Biblia inatuambia, "Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee." (Mithali 22:6) Tusipofanya mambo hayo, watoto wetu wanaweza kuanguka katika uasi na kufanya maamuzi ambayo yatawaondoa chini ya mwavuli wa ulinzi wa Mungu. Maombi na mafundisho sahihi katika njia na Maneno ya Mungu yatahakikisha hilo halifanyiki na kwamba mpango wa Mungu unafanikiwa—na sio wa Shetani. Biblia inasema, "Mpingeni Shetani naye

atawakimbia” (Yakobo 4:7). Kufunga mipango ya Shetani katika maombi ni sehemu ya kumpinga Shetani. Kumpinga kwa niaba ya watoto wetu kunaweza kuwaweka huru kufanya maamuzi ya Kiungu. Shetani atajaribu daima kufanya kesi dhidi ya watoto wetu ili aweze kupata njia ya kuingia katika maisha yao. Iwapo tumejizatiti kwa Maandiko hata hivyo, adui atalazimika kushindana na Neno la Mungu. Biblia inasema, “Sasa kumekuja wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo Wake; kwa maana ametupwa chini mshitaki wa ndugu zetu, yeye ambaye huwashitaki mbele za Mungu mchana na usiku.” 12:10). Kifo cha Yesu msalabani kilivunja mgongo wa mshtaki, lakini yule mwovu bado atawasumbua wote wasiojua mamlaka waliyopewa na Mungu juu yake. Hapa ndipo maombi yetu yanapoingia. Watoto wetu watasimama na kushtakiwa na adui hadi tutakapovunja ngome ya mshtaki kwa maombi, tukitumia Neno la Mungu kama ushahidi mgumu dhidi yake.

**Mfano Mzuri wa Maombi Yanayojibiwa**

Tangu wakati mwana wetu alipokuwa na umri wa miaka miwili hivi, mimi na mume wangu tulikuwa na vikundi vya maombi vya kawaida nyumbani mwetu.

Kanisa letu lilikuwa limepanga vikundi vidogo vya nyumbani na tuliongoza mojawapo ya makundi hayo. Hatua kwa hatua tukitambua kwamba mahitaji ya kikundi chetu yalikuwa makubwa sana kuweza kushughulikia katika mkutano mmoja wa kila mwezi, kwa hiyo tuliongeza usiku mwingine kila mwezi kwa ajili ya sala tu pamoja na watu. Wakati huo tuliomba kwa kila

aina ya hitaji, lakini wingi wa maombi ya watoto wetu ulikuwa mkubwa sana. Kwa sababu hiyo, nilihisi kwamba tulihitaji kuwa na siku nzima iliyotengwa hasa kwa ajili ya kusali pamoja na kwa ajili ya kila mmoja wa watoto wetu. Wakati huu wa maombezi, tuliouita "Kuombea Maisha ya Watoto Wetu," wakati huu, ukawa unapendwa na kuwa maarufu sana kiasi kwamba watu waliomba tena na tena. Kwa hakika, msingi wa kitabu hiki umetokana na vikundi hivyo vya maombi. Tumekuwa na kufunga pia kwaajili ya kuwaombea watoto wetu kwa ujumla. Hakuna hata mmoja wetu aliyekuwa na wazo lolote jinsi ambavyo vikundi hivi vingekuwa muhimu. Tulijua tu tulikuwa tukifuata mwongozo wa Bwana tulipojifunza jinsi ya kufanya maombezi, na tulifurahi pamoja tuliposhuhudia majibu mengi kwa maombi yetu. (Angalia jinsi ya, "Kusali Pamoja na Wazazi Wengine," ili kupata madokezo ya jinsi ya kupanga wakati wako mwenyewe wa maombezi ya kikundi kwa ajili ya watoto.) Habari njema ni kwamba katika miaka hiyo yote tangu tusali kwa ajili ya watoto hao, hatukuwahi kupoteza mtoto hata mmoja; — si kwa magonjwa, ajali, uasi, kutomcha Mungu, au kwa mipango ya adui. Hiyo ni miujiza ya Bwana.

Biblia inasema, "Ikiwa wawili wenu watapatana duniani katika jambo lolote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni" (Mathayo 18:19). Pia, mtu mmoja anaweza kukimbiza elfu na wawili wanaweza kukimbiza elfu kumi (Kumbukumbu la Torati 32:30) umoja au 'synergy' wazungu wasemavyo. Haihitaji akili nyingi ya hisabati kufahamu hili, basi ni jinsi gani wazazi kumi hadi kumi na wawili wanaweza kuwa na nguvu wanapojiunga katika maombi na kumlilia Mungu kwa ajili ya watoto

wao.

Katika Maandiko niliyotumia kama mstari wa mwongozo wa kitabu hiki chote, Mungu anaamuru, “Mimina moyo wako kama maji mbele za uso wa Bwana. Mwinulie mikono yako kwa ajili ya uhai wa watoto wako” (Maombolezo 2:19). Je, mstari huu unaweza kuwa wazi zaidi kiasi gani kwamba tunapaswa kuomba kwa *bidii* na *shauku* kwa ajili ya vijana wetu, na kutazamia kwa hamu kubwa maombi hayo kujibiwa?

Tumekuwa na majibu mengi kwa maombi yaliyotolewa wakati wa nyakati za kikundi katika kipindi cha miaka kadhaa iliyopita, kwamba ningeweza kuandika kitabu juu ya wale pekee, yale yaliyoshuhudiwa na wazazi na watoto ambao walihusika. Hata hivyo, tukio moja mahususi linajitokeza akilini mwangu kwa sababu lilikuwa ni matokeo ya moja kwa moja ya wakati wetu wa kwanza *wa* maombi na lilikuwa ombi la lazima kwetu sote katika kikundi.

Agatha, mama asiye na mwenzi, aliomba maombi kwa ajili ya binti yake, Janet, ambaye alimjua Bwana lakini alikuwa akimwacha Bwana taratibu kwa sababu ya kukatishwa tamaa na kuumia kwa talaka ya wazazi wake. Mojawapo ya mambo mahususi tuliyoomba ni ulinzi kwa Janet, kwa kuwa tulijua kwamba watoto wanaochagua kutoka chini ya mwavuli wa baraka za Mungu, hujianika kwa kila aina ya madhara. Ndani ya wiki chache za wakati huo wa maombi, Janet alikuwa akiendesha gari kwenye barabara kuu usiku sana na aligongwa uso kwa uso na dereva mlevi ambaye alikuwa ameendesha barabara kuu na alikuwa akisafiri kwa mwendo wa kasi

kuelekea upande usiofaa. Madaktari walisema ulikuwa muujiza kwamba hakuuawa, lakini alikuwa na majeraha mabaya kichwani, shingoni, mabegani na mgongoni.

Hatimaye, kupitia maombi ya kuendelea na matibabu ya kimwili, Janet alipona kabisa, kimwili na kiroho. Yeye na mama yake na sisi sote tulioomba tunaamini hangekuwa hai tusingeombea maisha yake kabla ya ajali. Leo, Janet ana ndoa yenye furaha, na binti yake mwema, naye ni mwanamke Mkristo aliyejitoa wakfu kwa Bwana. Alikua katibu na msaidizi wetu kwa miaka minane, na daima atakuwa ukumbusho wetu wa ajabu wa uwezo wa mzazi anayeomba.

## Wakati Majibu Hayaji

Inawezekana sehemu ngumu zaidi ya kuwaombea watoto wetu ni kungoja maombi yetu kujibiwa. Wakati mwingine majibu huja haraka, lakini mara nyingi haiwi hivyo. Isipokuwa hivyo, sisi tunaweza kukata tamaa, kuacha imani au kumkasirikia Mungu. Kila kitu kinaonekana kutokuwa na tumaini, na tunataka kukata tamaa. Wakati mwingine, licha ya yote ambayo Mungu ametufanyia na sala zetu zote kwa ajili yao, Hata pale watoto wetu hufanya maamuzi mabaya na kisha kuvuna matokeo. Nyakati hizo ni ngumu kwa mzazi kutazama, haijalishi mtoto ana umri gani.

Ikiwa mtoto wako amefanya maamuzi mabaya, usijilaani na kuacha kuomba. Usimlaani mtoto, ila weka njia za mawasiliano wazi na mtoto wako, endelea kumwombea, na utangaze Neno la Mungu. Badala ya kukata tamaa, azimia kujitolea *zaidi* kwa maombi. Omba pamoja na waumini

wengine. Simama imara na useme, “Nimeanza tu kupigana,” ukikumbuka kwamba sehemu *yako* ya vita ni kuomba. Ukweli ni *Mungu Ndiye* anapigana vita. Kumbuka pia kwamba vita yako si na mtoto wako, ni pamoja na Shetani. Yeye ni adui yako, sio mtoto wako. Simama imara katika maombi hadi uone mafanikio katika maisha ya mtoto wako.

Mojawapo ya Maandiko yenye kutia moyo sana ambayo nimesoma kuhusiana na ustahimilivu huo ni pale Daudi aliposema, “Nimewafuatia adui zangu na kuwapata; wala sikurudi nyuma hata walipoangamizwa. Nimewatia jeraha, wasiweze kuinuka; wameanguka chini ya miguu yangu. Kwa maana Bwana umenitia nguvu kwa vita” (Zaburi 18:37-39). Hakusimama hadi kazi ilipokamilika na sisi pia hatupaswi kufanya hivyo.

Tunapaswa kuomba hadi tuone jibu la Mungu. Isaya 43 ina mafungu mengi ya kutia moyo, mfano “Usiogope; maana Mimi ni pamoja nawe; nitaleta wazao wako toka mashariki, nitakukusanya toka magharibi.”

Ikiwa una hasira au kutomsamehe mtoto wako—ndiyo, hata wazazi wenye upendo wanaweza kuwa na hisia hizi—mwambie Mungu kwa uaminifu kamili, usiwe mnafiki au feki, Yeye anajua moyo. Ikiwa unahisi kukata tamaa na kuachia kila kitu, sema wazi. Usiishi na hisia hasi na hatia ambazo zinaweza kukutenganisha na Mungu. Shiriki hisia zako zote kwa uaminifu na kisha umwombe Mwenyezi Mungu akusamehe na akuonyeshe hatua yako inayofuata inapaswa kuwa nini. Zaidi ya yote, usiruhusu kuudhika kokote juu ya maombi ambayo haijajibiwa na kukufanya uache kuomba.

## Nilisema “Kuomba,” Sio kuleta “Ukamilifu”

Mambo yanapoharibika katika maisha ya watoto wetu, tunajilaumu wenyewe. Tunajipiga konzi kwa kutokuwa wazazi wakamilifu. Lakini sio kuwa mzazi mkamilifu ndiyo huleta mabadiliko katika maisha ya mtoto katika hatua hii, kwa sababu hakuna wazazi wakamilifu. Hakuna hata mmoja wetu ambaye ni mkamilifu, kwa hiyo tunawezaje kuwa wazazi wakamilifu basi? Ni kuwa mzazi *anayeomba* ndiko kunaleta tofauti. Kuwa mzazi ni hali ya mwenye dhambi mmoja kumkuza na kumlea mwenye dhambi mwingine (parenting is one sinner, raising another sinner). Na hilo ndilo jambo ambalo *sote* tunaweza kuwa, wana maombi, au hata mashujaa wa maombi kama wasemamavyo Waingereza “Prayer Warrior”.

Kwa kweli, hata hatuhitaji kuwa wazazi au walezi ili kumuombea mtoto. Tunaweza kuwa rafiki, mwalimu, babu na nyanya, shangazi, binamu, jirani, mlezi, au hata mtu baki mwenye moyo wa huruma au kumjali mtoto.

Mtoto anaweza kuwa mtu tunayesikia au kusoma habari zake kwenye gazeti; unapoona mambo kwenye taarifa ya habari unaweza kumwombea mtoto au mtu papo hapo, badala ya kukodoa macho tu na kuona maovu au maafa ya mtu au mtoto wa mtu. Hakika mtoto anaweza hata kuwa mtu mzima ambaye sisi wenye huruma na moyo wa mama au baba tukasukumwa tumwombee. Mtoto wa jirani, mzazi jirani nk

Ikiwa unafahamu mtoto ambaye hana mzazi anayeomba, wewe unaweza kuingia katika pengo hilo sasa hivi na kujibu hitaji hilo la maombezi (Intercessory prayer). Unaweza kuleta mabadiliko katika maisha ya mtoto yeyote unayemjali. Hata yule uliyemwona sokoni kwa dakika

chache tu, ambaye ananyanyasika au ana huzuni, au hafanyi vizuri kitaaluma. Kinachohitajika ni moyo unaosema, ***“Mungu, nionyeshe jinsi ya kuomba kwa njia ambayo italeta mabadiliko katika maisha ya mtoto huyu.”*** Kisha anza na maombi katika kitabu hiki na uone mahali ambapo Roho Mtakatifu anakuongoza. Kwani Roho Mtakatifu anatuombea kwa kuugua kwingi kusikoweza kutamkika. Mwishoni mwa kila sura nimekuwekea maombi ili uombe. Unaweza kutaka kusali hata moja ya hilo kila siku kwa mwezi mmoja, au kusali sala moja mahususi kwa juma moja, au kukazia katika fikira juu ya mahangaiko yako makubwa zaidi ya wakati huo hadi uhisi kufunguliwa ili kuendelea na lingine.

Rudia maombi haya mara nyingi upendavyo. Mungu hakusema, “Usije Kwangu tena na tena na ombi lile lile.” Kwa kweli, Alisema “Ombeni bila kukoma”.

Na kumbuka, sio lazima ufuate ratiba yoyote au uombe maombi haya mahususi. Kwani haya ni mwongozo tu wa kukufanya uendelee na safari ya maombi. Anza kwa kujinyenyekeza kwa Mungu na kumwomba akusaidie kuwa mzazi na mwombezi ambaye anataka wewe uwe. Omba jinsi Roho Mtakatifu anavyokuongoza unaposikiliza maongozi yake moyoni *mwako* kwa ajili ya mtoto *wako. Msifu Mungu, omba msamaa, mshukuru, mwombe!* Ninatazamia kwa shauku kusikia kuhusu majibu ya maombi yako.

***Maombi***

*Bwana,* najisalimisha Kwako. Ninatambua kwamba kulea mtoto kwa njia ambayo ungenitaka nifanye, ipo nje ya uwezo wangu wa kibinadamu. Najua kuwa nahitaji Wewe unisaidie. Ninataka kushirikiana na Wewe na kushiriki katika karama Zako za hekima, ushauri, utambuzi, ufunuo, na mwongozo. Pia ninahitaji nguvu na subira Yako, pamoja na sehemu ya ukarimu ya upendo Wako inayotiririka kupitia kwangu. Nifundishe jinsi ya kupenda jinsi Wewe Bwana unavyopenda. Mahali ninapohitaji kuponywa, kutolewa dhabihu, kubadilishwa, kukomaa, au kufanywa mzima, ninakualika ufanye hivyo ndani yangu. Nisaidie nienende katika haki na uadilifu mbele zako. Nifundishe njia zako, niwezeshe kutii amri zako na kufanya yale tu yapendezayo machoni pako.

Uzuri wa Roho Wako na uwe dhahiri ndani yangu, kwamba nitakuwa kielelezo cha mbingu hapa duniani. Nipe ujuzi wa mawasiliano, ufundishaji, na kulea, stadi ambazo ni lazima niwe nazo. Nifanye kuwa mzazi Unayetaka niwe na unifundishe jinsi ya kuomba na kuombea kweli maisha ya mtoto huyu/watoto hawa. Bwana, ulisema katika Neno lako, "Lolote mtakaloomba katika sala, mkiamini, mtapokea" (Mathayo 21:22). Katika Jina la Yesu naomba uniongezee imani ya kuamini mambo yote uliyoweka moyoni mwangu kuyaombea kuhusu mtoto huyu/watoto hawa katika jumuiya, kanisani, shuleni au nyumbani.

Katika Jina la Yesu ninaomba. Amen

**SILAHA ZA VITA**

Si ninyi mlionichagua Mimi, bali ni Mimi niliyewachagua ninyi na kuwaweka mwende mkazae matunda; na matunda yenu yapate kukaa; ili kwamba lolote mmwombalo Baba kwa Jina Langu awapeni.

**YOHANA 15:16**

Mwenye haki huenenda katika unyofu wake; watoto wake wamebarikiwa baada yake.

**MITHALI 20:7**

Nanyi mkiomba lolote kwa Jina Langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lolote kwa Jina Langu, nitalifanya.

**YOHANA 14:13-14**

Msiwachokoze watoto wenu, bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana.

**WAEFESO 6:4**

Pokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni Neno la Mungu; kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote.

**WAEFESO 6:17-18**

## Sura ya pili

## KUMWACHILIA MTOTO KATIKA MIKONO YA MUNGU, MDONDOSHE

Sikuwa na amani wakati mtoto wangu wa kwanza, toka akiwa tumboni nilikuwa na wasiwasi kama atatoka salama, na kuwa na afya njema, kwa vile nilikuwa mwenye umri wa miaka 38, ila pia ni hofu tu ya mzazi. Nilifuata maelekezo ya kuweka nyimbo nzuri za tenzi na Biblia ya kusikiliza kwani niliambiwa na wengi kwamba itamfanya mtoto alipende Neno atakapozaliwa na kupenda nyimbo zilizo na amani moyoni na mionjo ya kiroho, badala nyimbo nyingi za matusi kwenye televisheni za mabasi yetu, na zile zenye maadili mabaya za ukatili. Na nikafikiri atakapozaliwa Je, atampenda Mungu na watu pia?

Je, atakuwa mkarimu kwa watu, mwenye adabu njema, anayeweza kujifunza na kujitegemea mwenyewe. Sikupenda mtoto ambaye atakuwa mzembe na kunitegemea maisha yake yote, ndiyo anaweza akae nyumbani kwa muda kwani hata Masihi aliishi kwao mpaka alipofika miaka 30, ila alisaidia nyumbani mwao. Kwa sababu nilihangaika kuhusu kila kipengele. Niliogopa hata kwamba mtu angemwangusha chini naye akadhurika, au angezama kwenye beseni la kuogea, au atapata ugonjwa wa kufa, au naweza nisahau kumlisha, au ataweza kuumwa na mbwa au mbu na kupata malaria, kujeruhiwa katika ajali ya gari, kutekwa nyara, au kupotea. Katika moyo uliokata tamaa zaidi kuliko utii, nilimlilia Mungu kuhusu hili. Mara moja alinikumbusha kwamba Mtoto wangu Daudi alikuwa zawadi kwetu kutoka Kwake na kwamba Yeye *Alijali hata zaidi,* kuhusu mwana wetu kuliko sisi. Nilikumbushwa kuhusu maagizo ya Biblia ya kumtwika Bwana "Fadhaa na mahangaiko yetu yote" (1 Petro 5:7), ni jambo halisi, na ndivyo nilivyofanya.

"Bwana, mwanangu ndiye 'tuzo' kubwa niliyo nayo, na ninamwachilia mikononi Mwako. Ni Wewe pekee unaweza kumlea sawa na kumweka salama kweli. Sitajitahidi tena kufanya yote peke yangu bali nitaingia katika ushirikiano, yaani ubia kamili na Wewe."

Kuanzia wakati huo na kuendelea, kila nilipokuwa na hofu juu ya jambo lolote, mara moja nililichukulia kama ishara ya kuomba hadi nilipohisi amani. Yaani pale tu nilipopata hofu kuhusu mwanangu, nilijua hiyo ni

ishara kwamba napaswa kumwombea papo hapo. Ikiwa sikuwa na amani mara moja nilipoomba, basi niliomba juu ya jambo hilo na mwenzangu mmoja au zaidi, hadi nipate amani moyoni. Kila siku nilimwachilia mwanangu kwa Mungu na kumwomba awe msimamizi wa maisha yake. Hili liliondoa shinikizo kwangu na uzazi ukawa jukumu la kufurahisha zaidi. Waswahili husema mzazi jalala, hebu isiwe hivyo kwetu, chochote kinachokuja kuhusu mwanetu tuombee. Wajerumani husema watoto wadogo changamoto ndogo, watoto wakubwa, changamoto kubwa! Maadamu tunapumua hatutaacha kuwapenda watoto wetu, na kusononeka wakipata shida! Upendo hutufanya tuumie moyoni sana mambo ya watoto wetu yanapoenda vibaya. Marafiki zangu wenye miaka 90+ wameonekana kuwa na changamoto hii zaidi kwani wengi wao wamezika watoto wao, na kuwa na wasiwasi na watoto wao kwa miaka mingi zaidi ya wengine. Rafiki yangu mwenye miaka 94 ana watoto wa miaka 72 ambao huwafikiria daima!

Kwa miaka mingi nimeomba aina hii ya maombi ya wakfu kwa ajili ya kila mmoja wa watoto wangu. Niliomba Jumamosi asubuhi kwanza, kabla ya kwenda naye kanisani, nami nikawaacha kwenye chumba cha mafundisho ya watoto cha kanisa (shule ya Sabato ya watoto), nilimwombea alipokaa na yaya wa watoto siku nzima, nikaomba siku ambayo alianza shule ya chekechea, mara nyingine nililazimika kumwacha kwenye chumba cha upasuaji ili daktari aweze kushona mguu wake uliokuwa umechanika. Niliomba nilipomwacha kwenye nyumba ya rafiki au mama yangu, niliomba aliposafiri kwa ndege hadi Maryland kwaajili ya programu ya watafuta njia au Pathfinder ya Biblia – (Bible ball), nilimwombea alipoenda

katika safari ya vijijini/mashambani, nikaomba kila walipoenda kambini, nilimwombea alipokuwa anajifunza kuendesha gari, nilimwombea asubuhi alipoanza kuendesha gari la familia peke yake, na kila wakati alipoenda kucheza mpira na wenzake.

Ilibidi nimwachie mwanangu mikononi mwa Mungu ulipofika wakati wa kuondoka na kwenda chuo kikuu. Nililia mara nyingi katika miezi iliyotangulia wakati huo kwa kufikiria tu kuhusu kutengana kipindi kirefu, kwa maana nilitambua kwamba maisha yetu hayangekuwa vilevile tena. Kisha, kabla tu ya ile siku kuu ya kuagana, kwamba anaenda kwingine kujitegemea na kufanya kazi, Mungu alinihuisha na Maneno haya, “Kwa maana mtatoka kwa furaha, na kuongozwa nje kwa amani; milima na vilima vitatoa nyimbo mbele yenu” (Isaya 55:12). Pamoja na hayo, Bwana alinipa ujuzi na uhakikisho kwamba baada ya kupatwa na maumivu ya awali ya kuwaachilia watoto wetu inakuja furaha na amani, kwao na kwetu sisi wazazi. Kwa sababu tunajua haijalishi watoto wetu wapo katika hatua gani ya maisha, sisi tunapowaachilia kwa Mungu hao wanakuwa kwenye mikono ya wema na huruma nyororo, naam upendo mwanana kuliko wetu. Tunajua kwamba watatoka kwa amani na furaha na Mungu atawatengenezea njia. Kwani Yeye Ndiye aliyewaumba kwa utukufu Wake, Naye anawapenda kuliko sisi au wao wenyewe wanavyojipenda. Kisha Bwana Atatufanyia vivyo hivyo nasi pia. Kuna faraja gani kubwa zaidi ya kufikiria huu upendo mwororo wa Bwana? Kwa sababu ya hili, siku tulipoendesha gari hadi chuo kikuu ili kumpeleka Daudi katika bweni lake la wanafunzi wa mwaka wa kwanza, nilikuwa na furaha na amani ambayo

Mungu pekee Ndiye awezaye kutoa, na nilikuwa karibu hakika kusikia milima na vilima vikiimba. Kila ninapofikiria jambo hili, nakumbuka kisa cha Hana, ambaye aliomba kwa Mungu kwa ajili ya mwana. Bwana alijibu maombi yake na akamzaa Samweli. Baadaye akasema, Naliomba kwa ajili ya mtoto huyu, Naye BWANA amenipa dua yangu niliyomwomba, kwa sababu hiyo mimi nami nimempa Bwana huyo mtoto; muda wote atakaokuwa hai amepewa BWANA" (1 Samweli 1:27-29).

Hana alifanya kazi kubwa sana ya kumkopesha Bwana mtoto, kiasi kwamba Samweli lipoachishwa kunyonya, alimpeleka nyumbani kwa Bwana ili akaishi na kuhani Eli japokuwa alijua Eli na watoto wake walikuwa waovu na wakorofi. Alifanya hivyo ili kutimiza nadhiri aliyoweka kwa Mungu kuhusu Samweli, kwa hiyo wewe usijali (wala usifanye moyo na matumaini yako kufadhaika, kama itakavyokuwa); Mungu hatakuomba wewe leo, umwache mtoto wako katika ofisi ya kanisa ili mchungaji na mke wake wamlee pamoja na watoto wao waovu. Jambo kuu ni kwamba, Hana alimwachilia kikamilifu mtoto wake kwa Mungu na kufanya kama Mungu alivyomwagiza. Matokeo yakawa kwamba Samweli akawa mmoja wa manabii wakuu wa Mungu ambao ulimwengu umewahi kuwa nao. Kwa uhalisia nabii wa Israeli wakati huo alikuwa kama mkuu wa nchi na Kiongozi wa kidini pia!

Hatutaki kuweka kikomo kile ambacho Mungu anaweza kufanya ndani ya watoto wetu kwa kuwashikilia sisi wenyewe na kujaribu kuwalea peke yetu, kwamba wasiende kokote, kwamba tunakaa na kiota tukikiangalia saa yote

mtoto asitoke. Hakika ikiwa hatuna uhakika kwamba Mwenyezi Mungu anatawala maisha ya watoto wetu, basi tutatawaliwa na hofu. Na njia pekee ya kuwa na uhakika kwamba Mungu *anatawala* ni kusalimisha makucha ya kumiliki kwetu na kumruhusu Mungu ayafikie kikamilifu maisha yao. Njia ya kufanya hivyo ni kuishi kulingana na Neno Lake na njia Zake na kumwomba juu ya kila kitu. Tunaweza kumwamini Mungu kuwatunza watoto wetu vizuri zaidi kuliko sisi tunavyoweza. Tunapowaachilia watoto wetu mikononi mwa Baba yetu wa mbinguni na kukiri kwamba Yeye Ndiye anayetawala maisha *yao* na *yetu,* sisi na watoto wetu tutakuwa na amani kubwa zaidi.

Hatuwezi kuwa kila mahali, Lakini Mungu anaweza hilo. Hatuwezi kuona kila kitu, Lakini Mungu anaweza. Hatuwezi kujua kila kitu, Lakini Mungu anajua yote. Haijalishi watoto wetu wana umri gani, Kuwadondosha au kuwaacha mikononi mwa Mungu ni ishara ya imani na imani yetu Kwake Yeye, ndiyo, hatua ya kwanza kuelekea kuleta mabadiliko katika maisha yao. Maombi kwa ajili ya watoto wetu yanaanzia hapo.

*Maombi*

*Bwana,* ninakuja Kwako kwa Jina la Yesu na kumleta (jina la mtoto wangu ------------------- Kwako). Nina hakika kwamba Wewe peke yako Ndiye unajua ni nini kilicho bora kwa mwanangu huyu.

Wewe peke yako ndiyo unajua anachohitaji. Ninamwachilia Kwako ili

umtunze na umlinde, na ninajitoa kuomba kila kitu kinachomhusu (mwanangu au mtoto huyu) ninachoweza kufikiria au ambacho Unaweka juu ya moyo wangu. Nifundishe jinsi ya kuomba na kuniongoza katika kile cha kuomba kuhusu mtoto huyu/watoto hawa. Nisaidie nisilazimishe mapenzi yangu ninapomuombea/ninapowaombea, lakini badala yake niwezeshe kuomba kwamba mapenzi Yako yatimizwe katika maisha yake.

Asante kwamba naweza kushirikiana na Wewe katika kumlea yeye na kwamba si lazima nifanye peke yangu. Ninashukuru kwamba sihitaji kutegemea mbinu za ulimwengu zisizotegemeka na zinazobadilika kila wakati katika kulea watoto, lakini kwamba ninaweza kuwa na maelekezo yaliyo wazi kutoka kwa Neno Lako na hekima ninapoomba.

Asante Bwana, kwa zawadi ya thamani ya mtoto huyu. Kuna wengine ambao wangependa kuwa na watoto, ila mimi Bwana umenipa mtoto huyu kwa kuzaa au kwa kuasili, au kwa kumjali kama jirani au mshiriki katika nyumba ya ibada. Kwa sababu Neno Lako linasema kwamba kila zawadi njema hutoka Kwako, najua kwamba umemleta mtoto huyu kwangu ili nimtunze, nimwombee, nimpende na kumlea. Nisaidie kufanya hivyo. Nionyeshe pale ninapoendelea kumshikilia kuliko ninavyopaswa na uniwezeshe kumwachilia kwenye ulinzi, mwongozo/uongozi, mashauri na nasaha Zako. Nisaidie nisiishi kwa kuogopa hatari zinazoweza kutokea, bali katika furaha na amani ya kujua kwamba Wewe Ndiye unayetawala sayari zote. Mimi

ninakutegemea Wewe Baba yangu kwa kila kitu, na leo ninamweka kwa imani mtoto/watoto wangu Kwako na kuwaachilia mikononi Mwako. Katika Jina la Yesu ninaomba. Amen

**SILAHA ZA VITA**

Ikiwa basi ninyi, mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, si zaidi sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa mema wale wamwombao!

**MATHAYO 7:11**

Rehema za BWANA ni za milele hata milele kwa wamchao, na haki Yake kwa wana wa wana, kwao walishikao agano Lake, na kwao wazikumbukao amri Zake ili kuzifanya.

**ZABURI 103:17-18**

Hawatajitaabisha bure, wala hawatazaa kwa taabu; kwa maana watakuwa wazao wa hao waliobarikiwa na BWANA, na wazao wao pamoja nao.

**ISAYA 65:23**

Tazama, watoto ni urithi kutoka kwa BWANA, uzao wa tumbo ni thawabu.

**ZABURI 127:3**

Lolote tuombalo, twalipokea kutoka Kwake, kwa kuwa tunazishika amri Zake, na kufanya yale yapendezayo machoni Pake.

**1 YOHANA 3:22**

## Sura ya tatu

## ULINZI DHIDI YA MADHARA

Mara nyingi maombi yetu ya dharura na ya dhati kuhusu watoto wetu ni kwa ajili ya ulinzi wa Mungu kwao. Ni vigumu kufikiria kuhusu vipengele vingine vya maisha yao ikiwa tuna wasiwasi juu ya usalama

wao wa binafsi. Tunawezaje kusali basi kuhusu matukio ya wakati ujao tukiwa na wasiwasi kuhusu matukio ya wakati ujao?

Kuishi katika miji mikuu kama Dar Es Salaam na utekaji wa watoto kama tulivyoishi kwa miaka ishirini, mama yangu aitwaye Upendo alikuwa na hofu mara nyingine hasa ulipokuja ukimwi mwaka wa 1981. Nakumbuka tulikaa kwenye kitongoji kilichoitwa Oysterbay na barabara iitwayo Laiboni, si mbali na daraja kubwa lililoitwa Salender Bridge, japo ni zamani, moyo wa mama alikuwa na sababu nzuri ya kuhofia usalama wetu, hasa sisi watoto wa kike. Nakumbuka mama akiwa kwenye dirisha la sebuleni aliniaga kwa mara ya pili, hapa nilikuwa na miaka 17, wakati tu matokeo yangu ya kidato cha nne yalikuwa yametoka, nikawa naenda Kinondoni ambapo ni maili tatu tu kwenye soko. Alisema akiwa dirishani, kuna ugonjwa umetokea unaoitwa ukimwi, ujihadhari nao, na wakati huu nilikuwa bado sijaelewa gonjwa hili kabisa. Alikuwa tu ndiyo naye ameusikia, na akawa na hofu kuwa nitaupata! Kwa vile maelfu ya watu walikuja nyumbani kwa mwaka, aidha walitaka karamu zao za arusi au zifanyike kwetu, wafanyakazi nyumbani ambao walikuwa watano, mtunza ngombe na kuku, walinzi wawili, mtunza maua, dreva na mfanyakazi wa ndani, siku nyingine alituambia “mjihadhari na ndugu, marafiki na jamaa wanaokuja kututembelea humu wengine wana nia mbaya, ninyi kama wasichana mniambie kinachoendelea”, hapo ni kabla ya enzi za ushoga, siku hizi watu wanalawiti na kubaka hata watoto wa kiume. Uhalifu umezidi kuongezeka polepole katika miaka hiyo, na hata ujirani wetu “mzuri” au

sehemu nzuri tuliyokuwa tunaishi haikuwa ulinzi dhidi ya hilo. Kwa hiyo niliomba ulinzi wa Mungu kila siku. Kwa kweli, nilianza kuwaombea watoto wangu usalama hata kabla hawajazaliwa, nikiombea ulinzi dhidi ya mambo kama vile kifo cha watoto wachanga kitandani (SIDS sudden infant death syndrome) na magonjwa ya watoto wachanga. Walipokuwa wakikua, nilisali ili nipate ulinzi dhidi ya ukatili, unyanyasaji, na ajali. Niliomba peke yangu, nikasali pamoja na mume wangu, na pia wenzangu katika kikundi chetu cha maombi: "Bwana Wafichechini ya kivuli cha mbawa Zako, kutokana na waovu wanaoweza kuwadhulumu, kutoka kwa maadui (wao) wauaji wanaowazunguka." (Zaburi 17:8-9).

Watoto wote wawili walipata sehemu yao ya mikwaruzo midogo ya maisha, michubuko, na majeraha ya kawaida ya utotoni, pamoja na marafiki zetu wengine ambapo wakati fulani ilihitaji kwenda hospitali kwa dharura na kushona mkono uliochanika kidogo. Hata hivyo, hakuna chochote kilichowapata watoto wetu ambacho kilikaribia kuwa kibaya sana au cha kudumu na hata mengine yalipotokea kama ajali nilijipa moyo kwamba hata katika hili Mungu anipe nguvu kuombea mtoto awe salama baada ya kuvunjika paja.

Rafiki mmoja mwanamaombi mpendwa alinisimulia kwamba mapema asubuhi moja, muda mfupi baada ya watoto wangu kufikia umri wa miaka kumi na tano, walienda na basi la shule asubuhi na ndipo nilipokea simu ambayo kila mzazi anaogopa kuipata.

"Mama Sulemani, mwanao Sulemani yuko sawa, pamoja na dadaye Sara, lakini wamepata ajali mbaya ya gari na wako katika chumba cha hospitali cha tiba ya dharura yaani Emergency Room. Basi lilikuwa karibu kugongana uso kwa uso na basi jingine na katika watoto wote hakuna mtoto aliyekuwa amefunga mikanda ya usalama-seat belts."

Tukiwa njiani kuelekea hospitalini, mimi na mume wangu tulisali kwa ajili ya wale watoto watatu waliojeruhiwa katika ajali hii na ambao walikuwa hospitali. Tulipokuwa tukifanya hivyo, nilikumbuka nyakati ambazo tulikuwa tumemwekea mikono Sulemani na Sara na kumwomba Mungu walindwe dhidi ya ajali za gari. Nilikumbuka Maandiko tuliyokuwa tumenukuu mara nyingi juu yake: "Kwa maana atakuagizia malaika Zake, wakulinde katika njia zako zote. Mikononi mwao watakuchukua, usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe" (Zaburi 91:11-12). Mungu hujibu maombi na ahadi Zake ni kweli. Nilijua hilo. Ikiwa Sulemani alikuwa katika ajali ya gari, ni lazima Mungu na malaika Zake wangekuwa hapo wakimlinda. Kisha, nilipokumbuka pia yale ambayo Biblia husema kuhusu mtu mwadilifu anayemcha Mungu—"Hataogopa habari mbaya; moyo wake u thabiti, unamtumaini BWANA " ( Zaburi 112:7 )—Nilianza kuhisi amani ya Mungu ipitayo akili na ufahamu wote.

Tulipofika hospitalini, tulipata habari kwamba Sulemani alikuwa ameketi kwenye kiti cha nyuma cha gari huku akiwa amebeba begi kubwa la sare/jezi za mpira mapajani mwake. Hii ilipunguza athari yake kwa nyuma ya kiti cha mbele na, kwa sababu hiyo, alipatwa na mbamizo wa goti

mdogo na mgongo ulipata mchubuko. Yule mvulana katika kiti cha mbele cha abiria alikuwa ametupwa nje ya basi kupitia kwenye dirisha la mbele ya basi na kujeruhiwa. Dereva aligonga usukani na alikuwa na majeraha usoni. Gari liliharibiwa kabisa-written off.

Sisi pamoja na wazazi wa watoto wengine hatukuamini kwamba baada ya mausia yote mazito tuliyokuwa nayo kwa wana wetu kuhusu umuhimu wa kufunga mikanda ya usalama, bado walikuwa hawajaifunga. Ikiwa wangetii sheria, huenda wasingeumia hata kidogo. Lakini habari njema ilikuwa kwamba ikiwa hatungesali, wangeweza kuuawa au kupata majeraha mabaya na ya kudumu. *Sote* tulijua wana wetu walikuwa wameokolewa kwa sababu ya maombi yetu katika Jina la Yesu kwa niaba yao, na tulimshukuru Mungu. Ni kweli katika kila jambo twapasa kumwendea Mwenyezi Mungu atuliwaze, atuponye, hata mambo yakiwa ni mabaya au mazito kiasi gani.

Kuwa mzazi anayeomba haimaanishi kwamba hakuna chochote kibaya kitakachotokea kwa watoto au kwamba watoto wako hawatawahi kupata maumivu au kifo, la! Wanaweza kupatwa na hayo*, kama Ayubu anavyosema, duniani tunayo dhiki na Shetani hana mema kwa mwanadamu, naye ni simba angurumaye kutafuta mtu ammeze 24/7. Hivyo* maumivu ni sehemu ya maisha katika ulimwengu huu ulioanguka dhambini. Soma zaidi kitabu cha Pambano kuu kwenye tovuti na Daniel 2 kuona pale ufalme wa Mungu wa milele utakapokuja na uovu, kifo, huzuni na machozi yote vitakapotokomea (MaarifaMtandaoni.Com). Hata hivyo, Biblia

inatuhakikishia kwamba sala zetu hutimiza sehemu muhimu katika kuepuka matatizo. Na linapotokea jambo chungu tutalindwa katikati yake hivyo itakuwa ni kwa manufaa ya watoto wetu na si maangamizi yao.

Hapa ndipo Neno la Mungu linachukua sehemu muhimu tena katika maombi yako na ndio msingi wa amani yako. Siwezi hata kukadiria idadi au hesabu pale nilipoomba kwa ajili ya ulinzi wa ajili ya familia yangu na mimi mwenyewe nilipokuwa nikiishi Nairobi, Kila mara nilipomwomba Mungu atulinde kutokana na jeuri ya majambazi, ambayo ilionekana kuwa kila mahali, nilinukuu Maandiko haya: “Yeye hunikomboa kutoka kwa adui zangu. Nawe unaniinua juu ya wale wanaonishambulia; Umeniokoa na mtu jeuri” (Zaburi 18:48). "Na ahimidiwe BWANA, kwa maana amenionyesha fadhili Zake za ajabu katika mji wenye nguvu." (Zaburi 31:21).

Matetemeko ya ardhi yalikuwa jambo la kuleta wasiwasi mwingine mkubwa nilipokuwa naishi California, pale San Francisco, mara zingine yalitokea usiku wa manane nasi tukatimua mbio, na wengine walitoka majumbani mwao bila nguo. Jambo hili lilimtokea pia mtoto wa rafiki yangu Anita na mumewe wakiwa katika ghorofa ya 30 huko Ufilipino mwezi uliopita, na nilisali juu yao na matemeko yetu wakati wote, lakini hasa usiku kabla sijalala. Kila tetemeko baya la ardhi ambalo nimewahi kupata lilinishtua kutoka katika usingizi mzito. Hilo linapotokea unajikuta umeamka ghafla katika giza totoro huku kila kitu karibu nawe kikitetemeka na kelele kubwa ya kutisha kuliko ngurumo inayosikika kwa sauti kubwa zaidi masikioni mwako na majirani unaona wanapiga mayowe na kutimua

mbio. Jambo hili linapaswa kutokea mara moja tu ili kupandikizwa kwenye kumbukumbu yako milele kuhusu tukio hili. Sikuwahi kwenda kulala bila kufikiria matetemeko ya ardhi na kusali juu ya familia yetu yote, na sikuzote nilinukuu: “Mungu ni kimbilio letu na nguvu, msaada utakaoonekana tele wakati wa taabu. Kwa hiyo hatutaogopa, ijapokuwa nchi itatikisika, na milima ijapoondolewa katikati ya bahari; maji yake yajapovuma na kutikiswa, ijapotetemeka milima kwa kiburi chake” (Zaburi 46:1-3). Soma pia Zaburi 91.

Ingawa Maandiko hayo yanaahidi usalama katikati *ya* tatizo hilo, bado mimi nilimwomba zaidi ya hayo: “Bwana, naomba kwamba kusiwe na tetemeko la ardhi. Lakini ikiwa kuna moja litatokea, basi, naomba kwamba tusiwe hapa. Hata hivyo, Bwana, ikiwa ni mapenzi Yako sisi kuwa hapa, naomba ya kwamba utatulinda ndani yake na kututayarisha na kutuondolea hofu hata pale tutakapolala usingizi wa mauti, basi tuwe tayari kukulaki mawinguni.”

Ninaamini kwamba Mungu alijibu sala hiyo tulipohama kutoka eneo hilo la matetemeko ya ardhi. Miezi michache baadaye wakati mimi na watoto wangu tuliporudi kuuona mji huu, tuliona magofu, nasi tuliogopa sana uharibifu uliokuwa umefanywa. Na nyumba iliyokuwa nyumba yetu iliharibiwa. Lakini tuliogopa sana jinsi Mungu alivyotuokoa na kwamba mkono Wake ulikuwa juu yetu kwa kujibu maombi.

Ikiwa tungekuwa katika tetemeko la ardhi, ninatumaini kwamba Mungu angetulinda humo, kama vile alivyofanya kimuujiza kwa wengine wengi.

Maafa yanaweza kutokea popote. Jambo kuu ni kuomba na kumwamini Mungu kujibu.

Mambo mengi hutokea tunapoomba, ambayo hayatatokea kama hatuombi. Ni sehemu ya mpango wa Mungu kutujalia, kwa kujibu maombi ya imani, kile ambacho Yeye asingetupatia kama hatukuomba. Je, nini kinaweza kutokea, au hakiwezi kutokea, kwa watoto wetu ikiwa hatuombi leo? Tusisubiri kujua. Hebu tupige magoti sasa.

***Maombi***

*Bwana,* ninamwinua ---------------(taja jina la mtoto) Kwako na kuuliza kwamba uweke wigo wa ulinzi kumzunguka yeye. Linda roho, mwili, akili, na hisia zake kutokana na aina yoyote ya uovu au madhara. Ninasali kwa kusema wazi jambo hili, yaani kubainisha ili apate ulinzi dhidi ya ajali, magonjwa, majeraha, kutawala nafsi au unyanyasaji wowote wa kimwili, kiakili, au kihisia. Ninaomba kwamba yeye akufanye Wewe kuwa kimbilio na ngome yake na akae "katika uvuli wa mbawa Zako" hadi "maafa yapite" (zaburi 91:1) Mfiche yeye kutokana na aina yoyote ya ushawishi mbaya ambao ungekuja dhidi yake. Mlinde mwanangu au mtoto huyu kutokana na hatari yoyote iliyofichika na usiruhusu silaha yoyote itakayoundwa dhidi yake yeye iweze kufanikiwa. Asante, Bwana, kwa ahadi Zako nyingi zinazohusu ulinzi. Msaidie mwana huyu atembee katika njia Zako na kwa utiifu kwa mapenzi Yako ili asitoke kamwe nje ya mwavuli wa ulinzi Wako. Mhifadhi huyu mtoto katika yote anayofanya na popote aendako. Awe

na tabia kama Yako, ajisalimishe Kwako na Kujazwa Roho Wako.

Katika Jina la Yesu ninaomba. Amen

## SILAHA ZA VITA

Yeye aketiye mahali pa siri Pake Aliye juu atakaa chini ya uvuli Wake Mwenyezi. Nitasema juu ya BWANA, “Yeye Ndiye kimbilio langu na ngome yangu; Mungu wangu, nitamtumaini Yeye.”

**ZABURI 91:1-2**

Upitapo katika maji mengi nitakuwa pamoja nawe; na katika mito, haitakugharikisha. Upitapo katika moto, hutateketea, wala mwali wa moto hautakuunguza.

**ISAYA 43:2**

“Kila silaha itakayofanyika juu yako haitafanikiwa, na kila ulimi utakaoinuka juu yako katika hukumu utauhukumu kuwa mkosa.

Huu ndio urithi wa watumishi wa BWANA, na haki yao inayotoka Kwangu, asema BWANA.

**ISAYA 54:17**

Kwa sababu umemfanya Bwana, aliye kimbilio langu,Yeye Aliye juu, kuwa makao yako, mabaya hayatakupata wewe, wala tauni haitakaribia maskani yako.

**ZABURI 91:9-10**

Nitalala kwa amani na kupata usingizi mara; kwa maana Wewe, BWANA, pekee Yako, Ndiwe unijaliaye kukaa salama.

**ZABURI 4:8**

**Sura ya nne**

## KUHISI KUPENDWA NA KUKUBALIKA

Moja ya mambo magumu ambayo watoto wanapaswa kukabiliana nayo ni uongo ambao unaweza kuja akilini mwao, kisha wakaufanya kwamba ndiyo ukweli: “mimi Sipendwi,” “mimi Sikubaliwi,” “mimi Sithaminiwi,” “mimi Sina mvuto,” “mimi Sifai kwa jinsi ya kutosha;” “Mimi ni mnene sana,” “mimi mwembamba sana,” “mimi mrefu sana,” “mimi ni mfupi sana,” “mimi ni mjinga hakika sina akili,” “mimi ni mwenye akili sana,” “mimi ni kila kitu, wengine hawafui dafu kwangu.” Uongo huu huongezeka watoto wanapoingia katika miaka yao ya ujana, yaani miaka ya balehe/utineja na mara nyingi huendelea hadi wanapokuwa watu wazima. Ndiyo maana ninasadiki kwamba hatutakuwa tumefanya mapema zaidi au haraka sana kuanza kusali ili mtoto ahisi kupendwa na kukubalika— kwanza na Mungu, kisha familia, kisha na marika na wengine. Tunaweza kuanza wakiwa watoto wachanga, au katika umri wowote alionao mtoto wako kwa wakati huu, na kusali kuhusu wasiwasi huu katika maisha yao yote.

Kinyume cha kupendwa na kukubaliwa ni kukataliwa—jambo ambalo sote tumepitia wakati mmoja au mwingine maishani mwetu. Ni nani kati yetu ambaye hajawahi kuona aibu, fedheha, kushindwa, kukosa, au kutokubaliwa na mtu fulani juu ya jambo fulani ambalo tumefanya? Iwe ni kwa mshiriki wa familia, rafiki, au mtu tusiyemfahamu kabisa, kukataliwa hutupata sisi sote. Zaidi ya yote, kulimpata Mwokozi!

Wengine, hata hivyo, wanaweza kubeba majeraha makubwa ya kihisia kutokana na tukio lililofuata tukio la kukataliwa, hivyo ukosefu wowote wa kukubalika unaofikiriwa unaweza kubadilisha haiba yao kuwa kitu kibaya.

Ndio maana kukataliwa ndio chanzo cha maovu mengi tunayosoma kwenye magazeti kila siku. Mfanyakazi aliyekataliwa anarudi kwenye sehemu yake ya kazi ya zamani na kumpiga risasi bosi wake na wafanyakazi wenzake kwa ajili tu ya kukataliwa. Mume aliyekataliwa humpiga au kumuua mke wake. Mama ambaye amekataliwa na wengine anamnyanyasa mtoto wake au hata paka wake. Kukataliwa huleta hali mbaya kwa watu. Upendo na kukubalika na watu huleta yaliyo bora zaidi. Mtu ambaye tayari anahisi kukataliwa hufasiri kila kitu kuwa ni kukataliwa—mwonekano tu, hata kwa neno lisilo na madhara, na tendo lisilo na madhara na maana—wakati mtu anayehisi kupendwa na kukubaliwa, huwa hafikirii chochote kuhusu mwonekano wa nje au sura, neno, au tendo lile lile ambayo yule asiyekubalika analishuku au kujishuku, hata kama hana sura ya kuvutia sana. Mtu anaweza asikataliwe kihalisi, lakini ikiwa (yeye) *anaamini kwamba* ndicho kilichotokea kwake, matokeo yake ni yenye kudhuru kana kwamba ni kweli ilikuwa hivyo.

Upendo wa Mungu, hata hivyo, unaweza kubadilisha haya yote. Kujua kwamba Mungu anatupenda na anatukubali, hubadilisha maisha yetu.

Yeye Anasema, "Nimekuchagua wala sikukutupa" (Isaya 41:9). "Nimekupenda kwa upendo wa milele" (Yeremia 31:3). Na anathibitisha upendo Wake kwa sababu "Mungu aonyesha pendo Lake Yeye Mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi" (Warumi 5:8). Zaidi ya hayo, Biblia inatuhakikishia kwamba "wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka,

wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu" (Warumi 8:38-39).

Ni lazima tuombe kwamba watoto wetu waelewe Kweli hizi; ambazo ndiyo msingi imara ambapo upendo na kukubalika husimikwa katika tabia zao.

Ingawa ni upendo wa Mungu ambao hatimaye ni wa muhimu zaidi katika maisha ya mtu yeyote, upendo wa mzazi (au ukosefu wake) hutambuliwa na kuhisiwa kwanza. Upendo wa mzazi ni upendo wa kwanza ambao mtoto hupata na upendo wa kwanza ndio anaouelewa zaidi na kuuhusisha na upendo wa mwingine anapoanza safari yake. Kwa kweli, mara nyingi upendo wa wazazi ndio njia ambayo watoto hujifunua wenyewe kwa upendo wa Mungu na kuuelewa mapema maishani. Ndiyo maana tangu watoto wetu wanapozaliwa, tunapaswa kusali hivi: "Mungu, nisaidie kumpenda mtoto wangu kiukweli jinsi unavyotaka, nifundishe jinsi ya kumwonyesha kwa njia ambayo yeye anaweza kuelewa." Ikiwa, hata hivyo, mtoto wako sasa ni mkubwa na unatambua kwa sababu moja au nyingine kwamba yeye hahisi kupendwa, unaweza kuanza sasa hivi, kumwomba Mungu apenye moyo wake kwa upendo *Wake* na kuufungua ili kupokea. upendo wako na upendo wa wengine na kuutoa pia.

Mwombe Mungu akuonyeshe unachoweza kufanya ili kuwasilisha upendo kwa mtoto wako—na usimsikilize Shetani akikulemea *na* hatia kuhusu kushindwa huko nyuma. Unajua mbinu zake: Wakati mwingine Shetani atakuambia "Mtoto wako haoni kupendwa kwa sababu wewe ni mzazi

mbaya." au Ikiwa haungekuwa na shida sana ungeweza kuwasiliana na mtoto wako kwa upendo."

"Hakuna mtu aliyewahi kukupenda, kwa hivyo unawezaje kumpenda mtu mwingine yeyote? Huwezi kutoa kile usichokuwa nacho" Huu ni uwongo kutoka kwenye shimo la kuzimu na sehemu ya mpango wa Shetani kwa maisha ya mtoto wako.

Ikiwa unateswa na hatia au hisia za kushindwa katika eneo hili, ungama mawazo yako kwa Mungu, omba juu yake, yaweke mikononi mwa Mungu, na kisha simama na utangaze Ukweli. Sema, "Mungu anampenda mtoto wangu. Mimi nampenda mtoto wangu. Watu wengine wanampenda mtoto wangu. Ikiwa mtoto wangu hajisikii kupendwa ni kwa sababu yeye ameamini uwongo wa adui. Tunakataa kuishi kulingana na uwongo wa Shetani." Ingawa unaweza kulazimika kudumu kwa muda juu ya hili, usikate tamaa kuupinga uwongo wa Shetani kwa kuusema Ukweli wa Mungu. Kisha omba upendo wa Mungu uguse moyo wa mtoto wako, pia omba ili upendo wako utambuliwe na kupokelewa.

Pamoja na sala, watoto wanahitaji kuona upendo ukionyeshwa kwao kwa kuwatazama kwa macho, mguso wa kimwili (kupapasa, kukumbatia, busu), na kwa matendo, mwenendo na maneno yenye upendo. Niligundua kwamba nilipojitahidi kwa kukusudia kuwatazama watoto wangu machoni huku mikono yangu ikiwagusa kwa upole na kusema kwa tabasamu, "Ninakupenda na ninafikiri wewe ni mwana au binti mzuri," niliweza kuona *mara moja* jambo fulani. Mabadiliko katika sura na tabia zao. Jaribu

na utaona ninachomaanisha. Unaweza kujisikia uzito moyoni na kusitata sita mwanzoni ikiwa hujawahi kuonyesha mapenzi yako kwa mtoto kwa njia hii hapo awali, au ikiwa mtoto wako ni mzee au hata mtu mzima, lakini hata hivyo endelea kufanya hivyo. Ikiwa unasitasita, omba kwamba Mungu akuwezeshe kufanya hivyo na kwamba joto-joto hilo la kuonyesha upendo litapokelewa vyema na mwanao.

Ikiwa unahisi huna upendo unaohitaji kumpa mtoto wako, mwombe Roho Mtakatifu. Biblia inasema, "Pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi" (Warumi 5:5). Kusudi moja kuu la Mungu kwa maisha yako ni kukujaza wewe na upendo Wake mwingi ambao unafurika kwa wengine. Huwezi kutoa kile usichonacho.

Kumwombea mtoto wako hakutakuwa tu ishara ya upendo huo moyoni mwako, inaweza pia kuwa njia ambayo upendo huo unazidishwa hadi kufurika.

### *Maombi*

*Bwana,* ninaomba--------- (weka jina la mtoto) ajisikie kupendwa na kukubalika. Penyeza katika moyo wake upendo Wako hivi sasa na umsaidie yeye kuelewa kikamilifu jinsi ulivyo karibu naye kikamilifu. Neno Lako linasema ulitupenda sana hata ukamtuma Mwanao afe kwa ajili yetu (Yohana 3:16). Mwokoe mtoto huyu kutokana na uongo wowote wa adui unaoweza kuwa umepandikizwa akilini mwake hata

kumsababishia kutilia Ukweli huo mashaka. Yesu alisema, “Kama vile Baba alivyonipenda Mimi, Mimi Nami nimewapenda ninyi; kaeni katika pendo Langu” (Yohana 15:9-10). Bwana, naomba msaada kwa ------------------- (jina la mtoto) kukaa katika upendo Wako. Hebu aseme kama Daudi, “Unifanye kusikia fadhili zako asubuhi, maana nimekutumaini Wewe” (Zaburi 143:8). Onyesha upendo Wako kwa mtoto huyu kwa njia halisi leo na umsaidie yeye) kuupokea.

Ninaomba pia kwamba ungenisaidia kumpenda mtoto huyu bila masharti jinsi Wewe unavyofanya kwangu, na uniwezeshe kuonyesha kwa namna anavyoweza kuona. Nifunulie jinsi ninavyoweza kuonyesha na kuiga upendo Wako kwake yeye ----------ili ieleweke wazi. Ninaomba kwamba wanafamilia wangu wote watampenda na kumkubali yeye ----------, na yeye - apate kibali machoni pa watu wengine pia. Kwa kila siku ambayo yeye hukua katika ujasiri wa kupendwa na kukubalika, basi kutolewa ndani yake uwezo wa *kuwasiliana* kwa urahisi na kwa upendo kwa wengine. Mwezeshe (yeye) kufikia katika upendo kwa njia inayofaa. Anapokuja kuelewa kikamilifu kina cha upendo wako kwake na kuupokea ndani ya nafsi yake, mfanye kuwa chombo ambamo upendo Wako hutiririka kwa wengine. Katika jina la Yesu ninaomba.

Amen.

**SILAHA ZA VITA**

Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu

amemtuma Mwanawe pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa Yeye. Hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba Yeye alitupenda sisi hata akamtuma Mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu.

Wapenzi, ikiwa Mungu alitupenda sisi hivi, imetupasa na sisi kupendana sisi kwa sisi.

**1 YOHANA 4:9-11**

Kwa kuwa wewe u taifa takatifu kwa Bwana, Mungu wako; BWANA, Mungu wako, amekuchagua wewe kuwa taifa Lake, tunu kuu kuliko mataifa yote juu ya uso wa nchi.

**KUMBUKUMBU LA TORATI 7:6**

Tumelifahamu na kuliamini pendo alilo nalo Mungu kwetu sisi. Mungu ni upendo, Naye akaaye katika pendo hukaa ndani ya Mungu, na Mungu ndani yake.

**1 YOHANA 4:16**

Imetupasa kumshukuru Mungu sikuzote kwa ajili yenu, ndugu mnaopendwa na Bwana, kwa maana Mungu aliwateua tangu mwanzo mpate wokovu kwa kutakaswa na Roho na kuiamini Kweli.

**2 WATHESALONIKE 2:13**

Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo, kama alivyotuchagua katika Yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili

tuwe watakatifu, watu wasio na lawama mbele Zake. Kwa upendo, akitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi Yake, ili kusifiwa utukufu wa neema Yake, ambayo kwa hiyo ametukirimia katika Mpendwa Wake.

**WAEFESO 1:3-6**

## Sura ya tano

## KUANZISHA WAKATI UJAO WA MILELE

Zaidi ya yote, tunataka watoto wetu wapate maarifa. Wamjue Mungu ni nani na kumjua Yesu kama Mwokozi wao. Hilo linapotokea, tunajua mustakabali wao wa milele ni salama; tunajua kwamba watakapokufa, tutawaona tena mbinguni. Hilo ni tumaini zuri kama nini!

Eliza na mume wake, Salim, ambao walishiriki katika baadhi ya vikundi vyetu vya maombi vya "Kuombea Maisha ya Mtoto Wako", waliniomba mimi na mume wangu tuandike wimbo kwa ajili ya mojawapo ya albamu za Eliza ambazo angeweza kuwaimbia watoto kama wimbo wa moyoni. Niliandika maneno yafuatayo kwa wimbo unaoitwa "Juu ya Vyote Vingine," ambao mume wangu aliuweka kwenye muziki na Eliza akarekodi kwenye albamu yake Maneno haya, naamini, yanaunda kile kilicho ndani ya moyo wa kila mzazi anayeamini.

*"Mwambie mtoto una mengi ya kusema na maisha yamebaki kwa neema ya Mungu kushuhudia hili. Jinsi muda unavyopita.*

*Ikiwa ningepata njia yangu, ningekuweka salama mikononi mwangu.*

*Wakati dhoruba ya maisha inagonga.*

*Sitakuwa na wewe kila wakati, mtoto wangu, lakini maneno naweza kutoa.*

*Wakati pepo za matumaini zinapungua, maneno haya ya Mwenyezi*

*Mungu yataishi.*

*Zaidi ya yote, ujue kwamba Mungu Ndiye ambaye hataondoka kamwe kando yako*

*Wewe Mtazame Yeye kuliko yote.*

*Yeye ni upendo unaoweza kutegemeka, moyo Wake daima wa Hujali.*

*Ikiwa uko katika usiku wa giza kabisa ambao ungepaswa kupotea, Yeye atakuwa huko.*

*Yeye ni Baba wa Milele, Mikononi Mwake wewe hutaanguka au kudondoka kamwe.*

*Yeye Ndiye anayeshikilia yote, Zaidi ya yote.*

*Yeye Ndiye Mwanzilishi wa kicheko chako, Ndiye Mlinzi wa machozi yako, Ndiye*

*ambaye unapaswa kumwogopa zaidi ya yote.*

*Yeye Ndiye Mpaji wa ufalme*

*Aliyechinjwa kwa ajili yako tangu mwanzo,*

*Naye atakutuliza moyo wako zaidi ya yote.*

*Nina mengi sana ya kusema Na muda hautoshi kuyasema.*

*Mpende tu Bwana Zaidi ya yote.*

Mwanangu na binti yangu wote walifanya uamuzi wa kumpokea Yesu maishani mwao walipokaribia umri wa miaka mitano. Tulikuwa tumewafundisha kuhusu mambo ya Mungu, tukiwasomea visa vya Biblia, tulisali nao kila siku, na kuendelea kuwapeleka kanisani, ambako walifundishwa njia za Mungu. Walikuwa na ufahamu mwingi wa wazo la kumpokea Yesu, lakini hatukuwahi kuwalazimisha au kuwauliza kufanya uamuzi. Badala yake, tulisali kwamba mambo waliyojifunza yaingie mioyoni mwao na kuwapa tamaa ya kuwa na uhusiano wa karibu pamoja na Mungu. Tulitaka uamuzi huo utoke mioyoni mwao na uwe wao peke yao. Wakati huo ulipofika, kila mtoto alianza mazungumzo nasi kwa kuuliza maswali kuhusu Yesu, na akaishia kututaka tusali pamoja nao ili kumpokea kama Mwokozi. Mume wangu na mimi tuna amani kuu tukijua mustakabali wa milele wa mwana na binti yetu umejaa furaha na usalama.

Haijalishi watoto wako wana umri gani, wakati huu sio mapema sana au uliochelewa sana kuanza kuombea wokovu wao. Yesu alisema, "Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu" (Yohana 3:3). Pia alisema, "Tazama, nasimama mlangoni nabisha. Mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, Nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami" (Ufunuo 3:20). Tunataka watoto wetu wafungue mlango wa mioyo yao kwa Yesu na kupata uzoefu wa ufalme wa Mungu, katika maisha haya na hata milele baadaye. Kumbuka, *usipoomba* kwa ajili ya maisha ya baadaye ya watoto wako, wanaweza wasiwe na aina ya maisha

unayotaka wawe nayo.

Mara tu watoto wetu wanapokuwa wamempokea Bwana lazima tuendelee kuombea uhusiano wao na Bwana. Ni mara ngapi tumesikia kuhusu watoto wanaotembea na Mungu wakiwa wachanga, lakini wanamwacha katika ujana wao au utu uzima? Tunataka watoto wetu sikuzote "wajazwe ujuzi wa mapenzi Yake Bwana katika hekima yote na ufahamu wa rohoni" na "kuenenda kama inavyomstahili Bwana, wakimpendeza kabisa nao wakizaa matunda katika kila kazi njema na kuzidi katika maarifa ya Mungu'' Wakolosai 1:9-10) Paulo na Timotheo waliomba haya kwa ajili ya watoto wa Mungu huko Kolosai, na sisi tunapaswa kuwaombea watoto wetu. Kuomba kwa ajili ya Bwana kumwaga Roho Wake juu ya watoto wetu lazima iwe kauli mbiu yetu endelevu.

### *Maombi*

*Bwana,* ninamleta------------- (jina la mtoto) mbele Yako na kuomba kwamba utamsaidia yeye kukua katika ufahamu wa kina, na kujua kuwa Wewe ni nani. Fungua moyo wake na umlete kwenye ujuzi kamili wa Ukweli kukuhusu Wewe. Bwana, umesema katika Neno lako, "Ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka" (Warumi 10:9). Ninaomba kwa ajili ya imani ya aina hiyo kwa ajili ya mtoto wangu. Mtoto huyu akuite Wewe uliye Mwokozi wake, na kujazwa na Roho Wako Mtakatifu, akutambue katika kila eneo la maisha yake, akutii, na kukaa ndani Yako na

achague kukufuata Wewe na njia zako ili umsaidie yeye kuamini kikamilifu kwamba Yesu alitoa uhai Wake kwa ajili yake yeye ili yeye apate uzima wa milele tena awe nao tele. Msaidie yeye kufahamu utimilifu wa msamaha Wako ili asiishi katika hatia na hukumu.

Ninaomba kwamba---------- ataishi maisha yenye kuzaa matunda, akizidi kuongezeka katika kukujua Wewe. Daima yeye ajue mapenzi Yako, awe na ufahamu wa kiroho, na atembee katika njia inayopendeza machoni pako. Umesema katika Neno lako kwamba utamimina Roho Yako juu ya wazao wangu (Isaya 44:3). Ninaomba kwamba ungemimina Roho Wako juu ya---------------- (jina la mtoto) siku hii. Asante, Bwana, kwamba unajali kuhusu wakati wake ujao wa milele hata zaidi kuliko mimi na kwamba yuko salama mikononi mwako. Katika Jina la Yesu ninaomba kwamba mtoto huyu asiwe na shaka au kupotea kutoka kwako. Wewe una njia siku zote za maisha yake. Katika Jina la Yesu ninaomba. AMINA

## SILAHA ZA VITA

Mapenzi Yake aliyenituma ni haya, ya kwamba kila amwonaye Mwana na kumwamini yeye anao uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho.

**YOHANA 6:40**

Kwa maana hili ni jema na lakubalika mbele za Mungu Mwokozi wetu ambaye hutaka watu wote waokolewe na kupata ujuzi wa kweli.

**1 TIMOTHEO 2:3-4**

Tunajua kwamba Mwana wa Mungu amekuja na ametupa akili ili

tumjue Yeye aliye wa Kweli; nasi tumo ndani Yake Yeye aliye wa Kweli, ndani ya Mwanawe Yesu Kristo. Huyu Ndiye Mungu wa Kweli na uzima wa milele.

**1 YOHANA 5:20**

Huu ndio ushuhuda: kwamba Mungu alitupa uzima wa milele, na uzima huu umo ndani ya Mwanawe.

**1 YOHANA 5:11**

Nami nitamwomba Baba, Naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele; Ndiye Roho wa Kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni, wala haumtambui; bali ninyi mnamjua, maana anakaa kwenu ..…YOHANA 14:16-17

## Sura ya sita

## KUWAHESHIMU WAZAZI NA KUPINGA UASI

Inaonekana siyo jambo la kawaida *kuhitaji* mtu atuheshimu, sivyo? Ikiwa ni heshima kweli, Je, hawapaswi kuifanya hiyo kwetu bila kuambiwa? Kweli, hii inaweza kuwa kweli kuhusu watu wengine katika maisha yetu, lakini sio watoto wetu. Lazima wafundishwe. Biblia inasema, "Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, kwa maana hii ndiyo haki. 'Waheshimu baba yako na mama yako,' ambayo ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi: 'Upate heri, ukae siku nyingi duniani'" (Waefeso 6:1-3). Ikiwa watoto wetu wataiasi amri hii ya Bwana, wasingeweza tu kukatiliwa mbali na yote ambayo Mungu amewawekea, bali maisha yao yangeweza pia kufupishwa. Biblia pia inasema, "Anayemlaani baba yake au mama yake, taa yake itazimwa katika giza nene." (Mithali 20:20). Ukweli kwamba tunaweza kuathiri urefu na ubora wa maisha ya watoto wetu ni sababu tosha ya kusali, kuwafundisha, na kuwanidhamisha. Pamoja na hayo, ni lazima tutambue na kupinga uasi wowote unaotishia kuingia katika akili zao na kuwafanya wafanye mambo mengine isipokuwa yale ambayo Mungu anaamuru.

Uasi kwa hakika ni kiburi kinachowekwa katika matendo. Muasi husema moyoni, "Nitafanya ninachotaka, haidhuru Mungu au mtu mwingine yeyote anasema nini." Biblia inasema, "Kuasi ni kama dhambi ya uchawi" (1 Samweli 15:23) kwa sababu mwisho wake ni upinzani kamili kwa

Mungu. Mstari huohuo unasema pia kwamba “ukaidi ni kama uovu na ibada ya sanamu.” Kiburi hutuingiza katika uasi, lakini ukaidi ndio unaotuweka hapo. Yeyote anayetembea katika uasi ana sanamu ya ukaidi katika maisha yake. Watoto wasipomheshimu baba au mama yao, mara nyingi huwa ni ishara ya kwanza kwamba sanamu zilizo ndani ya moyo wa mtoto—mtoto wa umri wowote—ni kiburi na ubinafsi. Ndiyo maana watoto ambao hawajafundishwa kuwatii wazazi wao wanakuwa waasi. Wanasema, "Nataka ninachotaka wakati ninapotaka."

‘Ole wao watoto waasi,’ asema BWANA, ‘wanaofanya mashauri, wala si Yangu, watungao mawazo, wala si ya Roho Yangu, ili kuongeza dhambi juu ya dhambi” (Isaya 30:1).

*Kutambua na kuharibu sanamu za kiburi na ubinafsi kupitia sala mara nyingi kunaweza kuwa ufunguo wa kuvunja uasi wa mtoto.*

Kinyume cha uasi ni utii, au kutembea katika mapenzi ya Mungu. Utii huleta usalama mkubwa na ujasiri wa kujua uko pale unapotakiwa kuwa, kufanya kile unachopaswa kufanya. Biblia inaahidi kwamba ikiwa tutakuwa watiifu tutabarikiwa, lakini tusipokuwa watiifu tutakaa gizani na kuangamia.

Hatutaki hiyo kwa watoto wetu. Tunataka watoto wetu watembee kwa utii ili wawe na ujasiri, usalama, maisha marefu, na amani. Moja ya hatua za kwanza za utii kwa watoto ni kuwatii na kuwaheshimu wazazi wao. Hili ni jambo ambalo mtoto lazima afundishwe, lakini kufundisha kunakuwa rahisi wakati maombi yanapofungua njia.

Mwanangu alipokuwa na umri wa miaka kumi na minne, alifunika kuta zake za chumba cha kulala na mabango ya wanamuziki aliowapenda zaidi wanaitwa hapa kwetu celebrities. Tatizo ni kwamba katika baadhi ya picha za mavazi na muziki uliokuwa unawakilishwa ulikuwa wa kuudhi kwa baba yake na mimi na haukumtukuza Mungu. Tulipomwomba Yusufu ashushe mabango hayo na kueleza ni kwa nini, alisitasita, kisha kwa roho ya unyenyekevu akafanya tulichoomba.

Isipokuwa muda mfupi baadaye, hata hivyo, alizibadilisha na kuweka mpya ambazo zilikuwa mbaya vile vile. Tulikabiliana naye tena, tukachukua hatua zinazofaa za kinidhamu, na safari hii tukazitwaa picha zake zote.

Yusufu hakufurahi, nasi tukatambua kwamba tulikuwa tukishughulika na udhihirisho wa mapema wa roho ya uasi. Kwa hiyo tuliamua kufanya kama Biblia inavyosema na "vaeni silaha zote za Mungu mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani" (Waefeso 6:11). Tuliomba, tulitumia Neno la Mungu, na tukakiri imani yetu katika uwezo wa Mungu wa kutufanya washindi. Tulifanya vita katika Roho na kushuhudia amani ya Mungu ikitawala hali hiyo.

Mtazamo wa mwana wetu ulibadilika, na wakati mwingine baadaye alipoweka mabango tena yalitimiza vigezo ambavyo sisi, tukiwa wazazi wake, tulikuwa tumeviweka. Hii ilikuwa ni nguvu ya Mungu katika utendaji, iliyotumiwa na wazazi wanaoomba.

Mabango ya ukutani yanaonekana kama suala dogo sana sasa, lakini wakati

huo tulikuwa tukishughulika na dhamira kali ambayo ilikuwa ikijiinua juu ya wazazi na Mungu. Na kwa kupinga onyesho hilo la uasi, tuliweza kukomesha, kabla halijawa jambo kubwa. Tuliazimia kushinda pambano hilo kwa sababu tulijua kwamba tuna Mungu na Neno Lake upande wetu na kwa sababu, kwa mwana wetu, hatima ya milele ilikuwa hatarini.

Ikiwa mtoto wako ni mzee, kijana au hata mtu mzima, na uasi tayari umeonyeshwa wazi katika tabia yake, sehemu ya nidhamu na mafundisho itakuwa ngumu, lakini bado una nguvu ya maombi. Kumbuka, vita vyako sio vyako pamoja na mwana wako au binti yako. "Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho" (Waefeso 6:12). Vita yako ni pamoja na adui. Habari njema ni kwamba Yesu amekupa mamlaka "juu ya nguvu zote za yule adui" (Luka 10:19). Usiogope kuchukua fursa hiyo.

Uasi utatokea kwa mtoto wako wakati mmoja au mwingine. Kuwa tayari kukabiliana na changamoto kwa maombi na Neno la Mungu, pamoja na kusahihisha, kushugulikia nidhamu, na mafundisho. Usiogopeshwe na roho ya uasi. Yesu ni Bwana juu ya hilo, pia.

### *Maombi*

*Bwana,* ninaomba kwamba ungempa---------- (jina la mtoto) moyo ambao unatamani kukutii Wewe. Weka ndani yake shauku ya kukaa na Wewe, katika Neno Lako na katika maombi, wakati akiisikiliza sauti Yako. Angazia

nuru Yako juu ya uasi wowote wa siri au ukaidi unaokita mizizi ndani ya moyo wake, ili uweze kutambulika na kuangamizwa. Bwana, naomba kwamba ajiondoe (mwenyewe) kwenye kiburi, ubinafsi, na uasi, kwamba ataokolewa kutoka kwenye uasi. Kwa mamlaka Uliyonipa katika Jina la Yesu, "ninasimama dhidi ya hila za Shetani" na ninapinga ibada ya sanamu, uasi, ukaidi, na kutoheshimu watu; havitakuwa na sehemu katika maisha ya mwanangu (binti), wala mtoto wangu, kwani hatatembea kwa njia ya uharibifu na mauti.

Neno Lako linaagiza, "Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika mambo yote, kwa maana hilo lapendeza katika Bwana" (Wakolosai 3:20). Nakuomba Uuelekeze moyo wa mtoto huyu kwa wazazi wake na umwezeshe mwana huyu kuwaheshimu na kuwatii baba na mama ili maisha yake yawe marefu na mazuri. Uelekeze moyo wake Kwako ili yote anayoyafanya yawe ya kupendeza mbele Zako. Hebu na ajifunze kutambua na kukabiliana na kiburi na uasi ndani yake (mwenyewe) na awe tayari kukiri na kutubia. Mfanye asistarehe na dhambi bali ataabike. Msaidie kujua uzuri na urahisi wa kutembea na roho tamu na ya unyenyekevu katika utii na unyenyekevu Kwako.

Katika Jina la Yesu ninaomba. AMINA

**SILAHA ZA VITA**

"Kama mkikubali na kutii mtakula mema ya nchi; bali kama mkikataa na kuasi mtaangamizwa kwa upanga"; kwa maana kinywa cha BWANA kimesema.

**ISAYA 1:19-20**

Wale walioketi katika giza na uvuli wa mauti, wamefungwa katika dhiki na chuma—kwa sababu waliasi Maneno ya Mungu, na kulidharau shauri la Aliye Juu, kwa hiyo alishusha mioyo yao kwa taabu; wakaanguka chini, wala hapakuwa na wa kuwasaidia.

**ZABURI 107:10-12**

Jicho linalomdhihaki baba yake, na kudharau kumtii mama yake, kunguru wa bondeni wataling'oa, na wana tai watalila.

**MITHALI 30:17**

Mwanangu, yasikie mafundisho ya baba yako, wala usiiache sheria ya mama yako; kwa kuwa zitakuwa ni pambo zuri juu ya kichwa chako, na mikufu shingoni mwako.

**MITHALI 1:8-9**

Walakini hawakutii na kukuasi Wewe, ukawatia mikononi mwako maadui, waliowadhulumu.

**NEHEMIA 9:26-27**

## Sura ya saba

## KUDUMISHA UHUSIANO WA FAMILIA BORA MAHUSIANO

Dada yangu na mimi tulipata kuwa na mpasuko wa mahusiano kati yetu miaka kadhaa iliyopita na tukaishia kutowasiliana kwa miaka miwili. Haya yote yalitokana na kutokuelewana. Maumivu yetu binafsi yalikuwa yameficha uwezo wetu wa kuona wazi kile kinachotokea katika hulka na maisha ya kila mmoja wetu. Tulikuwa katika sayari mbili tofauti, ingawa tulilelewa katika nyumba moja, ndani ya familia moja. Kipindi hiki kizima kilinikasirisha sana, nami sikuacha kusali juu yake hadi mimi na dada yangu tulipopatana na uhusiano wetu ukarudishwa. Hata hivyo, ninaamini kama tungekuwa na wazazi wanaosali, jambo hilo halingetokea.

Mojawapo ya mambo ambayo adui wa nafsi zetu hupenda kufanya ni kuingia katikati ya mahusiano yaliyowekwa na Mungu na kutufanya tuongee vibaya, tusiwasiliane, tupoteze muda, tuvunjike au kutengana. Kadiri familia inavyogawanyika, ndivyo inavyozidi kuwa dhaifu na kutofanya kazi kwa ufanisi na ndivyo adui anavyodhibiti maisha yao. Njia ya kuepuka hili ni kupitia maombi. Unaposhughulikia mahusiano ya familia yako kwa sala, iwe ni pamoja na watoto, wazazi, wazazi wa kambo, kaka, dada, babu na nyanya, shangazi, wajomba, binamu, mume, au mke, kutakuwa na matukio machache sana ya mahusiano yenye matatizo au kukatika-katika.

Binti yangu alipozaliwa, kaka yake alikuwa na umri wa miaka minne na nusu. Nilisali tangu mwanzo kwamba Yusufu na mdogo wake Haika wawe na uhusiano wa karibu kati yao, na nilifanya yote niwezayo kuona hilo likitukia. Urafiki wao ulikuwa wa ukaribu na upendo mzito kiasi kwamba watu wengine waligundua na kurejelea juu yake. Kisha siku moja Yusufu akiwa na umri wa miaka kumi na kitu, kila kitu kilibadilika. Ghafla alikuwa na sehemu za kwenda na watu wa kuona na hakuwa tena na wakati na dada yake mdogo. Mateso ya ucheshi aliyoyafurahia akiwa na marafiki zake hayakupokelewa vyema na mdogo wake wa kike. Akihisi kukataliwa na kuumizwa, alilipiza kisasi. Nikawa mwamuzi na moyo wangu uliumia sana kuona kinachoendelea.

Kisha siku moja nilitambua jambo fulani muhimu: Kwa sababu kila kitu kilikuwa kinaendelea vizuri kati ya Haika na Yusufu, nilikuwa nimeacha kusali kuhusu uhusiano wao. Kwa hiyo, nikaanza kusali kuhusu jambo hilo tena, nikitamani nisingekuwa nimeacha kuombea hili kamwe.

Ilichukua muda, lakini hatua kwa hatua niliona jinsi mtazamo wao kuelekeana wao kwa wao, jinsi unavyobadilika. Ninajua kwamba kama sikufanya lolote kungekuwa na mpasuko wa kudumu kati yao kama vile ambavyo kumekuwa na mahusiano mengi sana yenye mpasuko katika siku za nyuma kwenye familia yangu. Sasa kwa kuwa wako katika miaka ya thelathini na kitu, kila mmoja ameolewa na kuoa na mtu mwema, na wote wanne wako karibu, na hutumia wakati mwingi pamoja na kama mzazi, ninapenda kuona hivyo.

Je, ni mahusiano mangapi ya kifamilia yameachwa yawe ya kubahatisha au patapotea kwa sababu hakuna anayeyaombea? Ni mengi sana, ninavyoshuku. Inasikitisha kuona familia zikitengana na watu wawili hawana mahusiano yoyote na mtu mwingine wakati wao ni watu wazima. Inahuzunisha sana kufikiria hilo likifanyika na watoto wetu wenyewe. Hata hivyo si lazima iwe hivyo.

Katika Isaya 58, Mungu anaeleza mambo yote ya ajabu yatakayotokea tunapofunga na kuomba. Anasema, “Utaisimamisha misingi ya vizazi vingi; nawe utaitwa, Mwenye kutengeneza mahali palipobomoka” (Isaya 58:12). Mungu anataka turudishe umoja, kudumisha vifungo vya familia katika Bwana, na kuacha urithi wa kiroho wa mshikamano ambao unaweza kudumu kwa vizazi.

Biblia pia inasema, “Iweni na nia moja ninyi kwa ninyi. Msiweke nia zenu katika mambo ya kujiinua, bali mshirikiane kwa unyenyekevu. Usiwe na hekima machoni yako mwenyewe” (Warumi 12:16). Tunapaswa kuomba kwa ajili ya unyenyekevu na umoja.

Yesu alisema, “Heri wapatanishi, maana hao wataitwa wana wa Mungu” (Mathayo 5:9). Ninasema, tuwe wapenda amani. Ni wazi hatutosheki duniani. “Na tufuatilie mambo ya kuleta amani na mambo ambayo mtu anaweza kujengana kwayo” (Warumi 14:19). Hebu tuanze kwa kuwaombea wale walio karibu nasi—watoto wetu —na tutoke hapo.

***Maombi***

*Bwana,* ninamwombea ------------ (jina la mtoto) na uhusiano wake na wanafamilia wote. Mlinde na mhifadhi dhidi ya ukiukaji wowote ambao haujatatuliwa au wa kudumu. Jaza moyo wake na upendo Wako na ummwagie yeye wingi wa huruma na msamaha ambao utafurika kwa kila mwanafamilia. Hasa, ninaomba kwa ajili ya mahusiano ya karibu, furaha, upendo, na kutimiza haja za mioyo kati ya --------- (jina la mtoto) na (jina la mwanafamilia) katika siku zote za maisha yao. Daima kuwe na mawasiliano mazuri kati yao na kutosamehe kusiwe na mizizi ndani ya mioyo yao. Wasaidie kupendana, kuthaminiana, kuona mwingine ni bora, na kuheshimiana ili uhusiano uliowekwa na Mungu kati yao usivunjwe. Ninaomba kulingana na Neno Lako, kwamba "wapendane na kuwa na fadhili wao kwa wao, kwa upendo wa udugu, kwa heshima, kila mmoja akimkitanguliza mwenzake" (Warumi 12:10).

Mfundishe mtoto wangu kutatua kutoelewana kulingana na Neno Lako. Na kama mafarakano yoyote tayari yamekwisha kuanza au, kama uhusiano wowote umevurugika au kukatika, Bwana, ninaomba ya kwamba utaondoa huo mgawanyiko na kuleta uponyaji. Ninaomba kwamba kusiwe na ushupavu, uvunjaji wa maagizo, kutokuelewana, mabishano, kupigana, au kutenganisha mahusiano. Mpe ---------- moyo wa msamaha na upatanisho. Neno lako linatuagiza "kuwa na nia moja, wenye kuhurumiana; wapendane kama ndugu, wawe na moyo wa huruma, wastaarabu" (1 Petro 3:8). Msaidie --------kuishi ipasavyo, 'mkijitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani' (Waefeso 4:3). Ninaomba kwamba ungetia upendo na huruma nyororo

ndani yake -----

**SILAHA ZA VITA**

Heri wapatanishi maana hao wataitwa wana wa Mungu.

**MATHAYO 5:9**

Tazama, jinsi ilivyo vema, na kupendeza, ndugu wakae pamoja, kwa umoja!

**ZABURI 133:1**

Basi, Mungu wa saburi na faraja na awajalieni kuwa na nia moja ninyi kwa ninyi, kama Kristo Yesu, ili kwa nia moja na kwa kinywa kimoja mtukuze Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo.

**WARUMI 15:5-6**

Ikiwezekana, kwa kadiri inavyowategemea ninyi, kaeni kwa amani na watu wote.

**WARUMI 12:18**

Basi, ndugu zangu, nawasihi kwa Jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja, wala pasiwe na mafarakano kati yenu, bali mshikamane kikamilifu katika nia moja na katika fikira moja.

**1 WAKORINTHO 1:10**

## Sura ya nane

## KUVUTIA MARAFIKI WACHA MUNGU NA MIFANO YA KUIGWA

Siku zote nimetoa sala kwa ajili ya marafiki wa watoto wangu na, kwa sehemu kubwa, wamekuwa na marafiki wazuri. Mara kwa mara wamepata marafiki ambao, kama mzazi, nilikuwa na kutoridhishwa nao. Si kwa sababu sikuwapenda; kwa kweli, katika kila tukio, niliwapenda sana. Nisichokipenda ni aina ya ushawishi waliokuwa nao kwa mtoto wangu, na kuchanganyika kwa mtoto huyo na wangu kulivyozaa mambo yasiyo msaada kwa ukuaji wa kiroho. Njia ambayo siku zote nilichukua ni kwamba niliomba kwamba mtoto huyo abadilishwe la sivyo asihusike katika maisha ya mtoto wangu. Hakika sala hiyo ilijibiwa. Katika visa kadhaa, muda ulivyoenda kulionyesha usahihi wa wasiwasi wangu. Watoto niliokuwa na wasiwasi nao kuhusu tabia na mazoea yao, waliishi maisha yenye matatizo.

Wazazi mara nyingi huwa na hisia za kiwango cha kuumwa matumbo kuhusu marafiki wa watoto wao. Hilo linapotokea, mwombe Mungu akupe utambuzi uliovuviwa na Roho Mtakatifu na uombe ipasavyo (gut feeling).

Moja ya nyakati zangu za bidii za maombezi kuhusu marafiki wa watoto wangu ilikuja tulipohama kutoka Masaka na kwenda Jinja Uganda. Tulihama mara tu mwanangu alipokuwa anaanza mwaka wake wa

mwisho katika shule ya sekondari na binti yangu alikuwa anaanza darasa la saba— hizi ni nyakati mbili mbaya zaidi kwa watoto kubadili shule. Kwa kawaida nisingetaka watoto wangu wabadili shule wakati huo, lakini katika kisa hiki mimi na mume wangu tulihisi uongozi wa Bwana katika kuhama. Kwa sababu nilijua jinsi wakati huu ungeweza kuwa mgumu kwa watoto wangu, kila siku katika miezi kadhaa kabla na baada ya kuhama nilisali, “Bwana, wasaidie watoto wangu wapate marafiki wacha Mungu. Ninajua kwamba *Umetuleta* hapa na hutawaacha watoto wangu wakiwa wameachwa. Nina wasiwasi kwamba katika hitaji lao la kukubalika watapata marafiki ambao viwango vyao vya maadili si vya juu kama vyako. “Leta vielelezo vya uchaji Mungu katika maisha yao.”

Miezi sita ya kwanza ilikuwa nyakati za upweke sana kwa Yusufu na Haika, na mara nyingi nilikesha usiku nikisali kwa niaba yao. Hakuna kitu kingine ambacho ningeweza kufanya. Sikuweza kuingilia kati na kuwaunganisha na marafiki wazuri kama ambavyo ningeweza kufanya walipokuwa wadogo. Lakini hata kama ningeweza kufanya hivyo, nisingefanya kazi nzuri kama vile Mungu anavyojibu sala zangu.

Hatimaye watu walikuja katika maisha yao ambao wamekuwa moja ya marafiki wao wakubwa ambao wamewahi kuwa nao. Hii sio tu bahati njema au mwisho wa kisa hiki.

Haya ni matokeo ya maombi ya maombezi -intercessory prayer. Haya ni matokeo ya kumlilia Mungu, kusema Kwake, “Mungu, wasaidie watoto

wangu wavutie marafiki wacha Mungu na vielelezo vya kuigwa."

Neno la Mungu hutuagiza hivi waziwazi: "Msifungwe nira pamoja na wasioamini kwa jinsi isivyo sawasawa. Kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi? Tena pana ushirika gani kati ya nuru na giza? Tena kuna mapatano gani kati ya Kristo na Beliari? Au anayeamini ana sehemu gani pamoja na asiyeamini?" (2 Wakorintho 6:14-15). Hiyo haimaanishi kwamba watoto wetu hawawezi kamwe kuwa na rafiki asiye mwamini. Lakini kuna maana ya wazi kwamba marafiki zao wa karibu, wale ambao wana uhusiano mkubwa nao, wanapaswa kuwa waumini. "Je, watu wawili wanaweza kutembea pamoja wasipokuwa wamepatana?" (Amosi 3:3). Hapana, hawawezi. Hiyo ina maana kama rafiki mbaya akikubaliwa, lazima abadilike. Na ndiyo maana "Mwenye haki anapaswa kuchagua rafiki zake kwa uangalifu, kwa maana njia ya waovu huwapotosha" (Mithali 12:26).

Ikiwa mtoto wako hana marafiki wa karibu wanaoamini, anza kuomba sasa hivi kuelekea jambo hilo. Ombea marafiki wasioamini wampokee Bwana na marafiki wenye nguvu na waamini waje maishani mwao. Mara nyingi wazazi hujihisi kutokuwa na uwezo wa kufanya lolote kuhusu ushawishi mbaya wa watu fulani katika maisha ya watoto wao. Lakini sisi si wanyonge. Tuna nguvu za Mungu na Ukweli wa Neno Lake nyuma yetu. Usisimame na kubung'aa tu wakati kuna mtu anayempotosha mtoto wako. Kuna mengi sana yaliyoandikwa katika Maandiko kuhusu umuhimu wa makundi au marafiki tunaochangamana nao, na kuchukua mtazamo makini

kuhusu suala hili.

Moja ya ushawishi mkubwa zaidi katika maisha ya watoto wetu itakuwa marafiki zao wa karibu. Je, sisi tunaweza kukaa na kupumzika tu na kuacha *kusali* juu yao?

### ***Maombi***

*Bwana,* ninamwinua--------- (jina la mtoto) kwako na kukuomba kwamba ulete marafiki wacha Mungu wa mfano wa kuigwa katika maisha yake. Mpe hekima anayohitaji ili kuchagua marafiki ambao ni wacha Mungu na kumsaidia asiwahi kuacha safari yake na wewe ili apate furaha na kibali machoni Pako. Ninaomba uongozi wa Roho Mtakatifu– utambuzi uliovuviwa katika jinsi nitakavyomwongoza au kumshawishi katika uchaguzi wa marafiki. Ninaomba kwamba utamweka mbali mtu yeyote ambaye hana mvuto wa Bwana kutoka katika maisha yake au vinginevyo umgeuze mtu huyo kuwa mfano Wako.

Neno Lako linasema, "Anayetembea na wenye hekima atakuwa na hekima, bali rafiki wa wapumbavu ataumia" (Mithali 13:20). Usimruhusu mtoto wangu kuwa rafiki wa wajinga. Mwezeshe atembee na marafiki wenye hekima na asipate uzoefu wa uharibifu unaoweza kutokea kwa kutembea na watu wapumbavu. Mwokoe kutoka kwa mtu yeyote mwenye tabia mbaya ili yeye asijifunze njia za mtu huyo na kuweka mtego kwa ajili ya nafsi yake. Wakati wowote kunapokuwa na huzuni juu ya urafiki uliopotea, mfariji na

umtumie marafiki wapya ambao yeye anaweza kuungana nao, kushiriki nao, kuhuduma nao na kuwa mtu Uliyemuumba kuwa. Ondoa upweke wowote au hali ya kutokuwa na uungwana na kujistahi, ambayo ingemfanya yeye kutafuta uhusiano usio wa kumtukuza Mungu.

Katika Jina la Yesu ninaomba kwamba umfundishe maana ya urafiki wa kweli. Mfundishe jinsi ya kuwa rafiki mzuri na kufanya uhusiano wenye nguvu, wa karibu na wa kudumu. Katika jina la Yesu ninaomba. AMINA

**SILAHA ZA VITA**

Usiingie katika njia ya waovu, wala usitembee katika njia ya uovu.

**MITHALI 4:14**

Nimewaandikia kwamba msichangamane na mtu aitwaye ndugu, akiwa ni mzinzi, au mwenye kutamani, au mwabudu sanamu, au mtukanaji, au mlevi, au mnyang'anyi, hata msile pamoja na mtu kama huyo.

**1 WAKORINTHO 5:11**

Mwanangu, mche BWANA na mfalme; usishirikiane na wale wenye kigeugeu; kwa maana msiba wao utatokea ghafula, na ni nani ajuaye uharibifu unaoweza kuwapata?

**MITHALI 24:21-22**

Usifanye urafiki na mtu mwenye hasira kali, wala usiende na mtu mwenye hasira kali, usije ukajifunza njia zake na kujiwekea mtego nafsi yako.

**MITHALI 22:24-25**

Heri mtu yule asiyekwenda Katika shauri la wasio haki, wala hakusimama katika njia ya wakosaji, wala hakuketi barazani pa wenye mizaha.

**ZABURI 1**

## Sura ya tisa

## KUKUZA NJAA KWA AJILI YA MAMBO YA MUNGU

Tunaposoma katika gazeti kuhusu vijana na tabia kama vile kuiba, kuua, kuharibu mali, au kuwa na uasherati, tunaweza kuwa na hakika kwamba watu hao hawana hofu ya Mungu ifaayo, wala ufahamu mzuri wa njia Zake, wala njaa na kiu ya haki au kumtafuta Mungu. Baadhi ya vijana hawa wanaweza hata kutoka katika familia za Kikristo na wanaweza kuwa wamempokea Yesu, lakini kwa sababu hawajafundishwa kumcha Mungu na kutamani uwepo Wake wanatawaliwa na miili yao, yaani tamaa za macho, tamaa za mwili na kiburi cha maisha haya.

Kumcha Mungu kunamaanisha kuwa na kicho kwa kujitoa wakfu kwa kina, upendo, na heshima kwa mamlaka na nguvu za Mungu. Inamaanisha kuogopa jinsi maisha yangekuwa bila Yeye na kushukuru kwamba kwa sababu ya upendo Wake hatutawahi kuwa na hali ya kukata tamaa kama kwa namna ya kusahau upendo na kujali Kwake. Inamaanisha kuwa na njaa ya yote aliyonayo Mungu na Alivyo, kwa ajili yetu. Kuna mambo mengi sana duniani ya kugeuza mawazo ya watoto wetu mbali na mambo ya

Mungu, mambo yanavutia akili zao, na Shetani atakuja kwa kila mtoto na ajenda yake na mipango yake ili kuona ikiwa watanunua sera zake ndani yao. Lakini tunapofanya sehemu yetu kulea, kuadilisha, kufundisha, kuadabisha, na kuzoeza watoto wetu katika njia za Mungu… tunapovisoma visa kutoka katika Neno la Mungu,

- Tunapowafundisha jinsi ya kuomba na kuwa na imani kwamba Mungu Atafanya kile anachosema atafanya,
- Tunapowasaidia kuunganishwa na marafiki wanaomcha Mungu,
- Wakati tunawaonyesha kwamba, kutembea na Mungu huleta furaha na utimilifu, na sio vikwazo vya kuchoka.
- Tunapoomba pamoja na kwa ajili yao kila siku, …ndipo watoto wetu watakuwa na njaa ya mambo ya Mungu. Watajua kwamba mambo ya Mungu ndiyo ya kwanza kabisa. Wataongozwa na Mungu na sio watu wa matendo ya kuridhisha mwili tu kama chuki, kiburi, mawazo machafu, kushuku watu, usengenyaji, kutosamehe, uasi nk. Watatamani njia Zake, Neno Lake, na uwepo Wake. Watamcha Mungu na kuishi maisha marefu na bora. Kwa maana "kumcha BWANA kwaongeza siku za mtu, bali miaka ya waovu itapunguzwa" (Mithali 10:27).

Wakati mimi na mume wangu tulijua kwamba tutahama kutoka Nakuru na kwenda Mombasa, jambo la kwanza tulilosali lilikuwa kupata kanisa lenye kundi bora la vijana. Sala hiyo ilijibiwa, na ndiyo sababu kuu ambayo watoto wetu waliweza kufanya marekebisho hayo makubwa

kwa mafanikio; kwa kuwa ni katika kanisa lao jipya na kundi la vijana walipata marafiki wacha Mungu na kuendelea kukua katika uhusiano wao na Bwana. Kupata kanisa linalofundisha Neno la Mungu kwa dhati na bidii, kuonyesha upendo wa Mungu, na kushiriki furaha ya Mungu pamoja na watoto Wake na vijana Wake kutafanya tofauti kubwa katika kuwasaidia watoto wako kusitawisha njaa na kiu ya mambo ya Mungu.

Anza sasa hivi kwa kuombea mtoto wako amche Mungu, na awe na imani Kwake na Neno Lake, na asitawishe aina ya moyo unaomtafuta Bwana. Hii inaweza kuwa sababu itakayopelekea mtoto wako kuwa na mapambano ya kudumu katika mwili au kukamilishwa na kubarikiwa kuishi katika Roho. Kumbuka, "Wamchao Bwana hawatapungukiwa na kitu" (Zaburi 34:9). Sio mapema sana kuanza kuomba kuhusu hili. Usisubiri dakika hata moja kufanya hivi.

### *Maombi*

*Bwana,* ninaomba kwa ajili ya--------- (jina la mtoto) kuwa na njaa na kiu inayoongezeka kwa ajili yako zaidi. Na mwanangu atamani uwepo Wako—atamani sana kutumia wakati na Wewe katika sala, sifa, na ibada. Mpe hamu ya Ukweli wa Neno Lako na upendo kwa sheria Zako na njia Zako. Mfundishe kuishi kwa imani na kuongozwa na Roho Mtakatifu, akiwa na matamanio ya kufanya kile unachomwambia afanye. Na awe na ufahamu wa utimilifu wa Roho Wako Mtakatifu ndani yake kiasi kwamba wakati yeye amepungukiwa kwa njia yoyote na Roho Wako, mara moja atakimbilia Kwako ili kufanywa upya na kuburudishwa. Ninaomba kwamba

moyo wake usiwe na kiapo chochote au vizuizi vyovyote mbali na Wewe, bali achukizwe na upotovu na kila kinachopingana Nawe. Heshima na upendo wa kina Kwako na njia Zako zitie rangi nzuri kwa kila kitu anachofanya na kila chaguo analofanya. Msaidie kuelewa matokeo ya matendo yake na kujua kwamba maisha yanayotawaliwa na mwili yatavuna kifo tu. Hebu asiwe na hekima machoni pake mwenyewe, bali "amche BWANA na ajiepushe na uovu" (Mithali 3:7).

Ninaomba kwamba awe mtu wa kutegemeka, kutegemewa, kuwajibika, huruma, hisia, upendo, na kutoa na kuhudumia wengine. Mwokoe kutoka kwa kiburi chochote, uvivu, ugoigoi, ubinafsi, au tamaa ya mwili. Ninaomba awe na roho inayofundishika na ya kunyenyekea ambayo inasema "ndiyo" kwa mambo ya Mungu na "hapana" kwa mambo ya mwili. Mtie nguvu ili asimame imara katika imani yake.

Ninaomba awe daima akitamani kuwa mshiriki hai wa kanisa la Kikristo ambalo liko hai kwa Ukweli wa Neno Lako na nguvu za ibada inayoongozwa na Roho Mtakatifu, maombi, na mafundisho. Anapojifunza kusoma Neno Lako, andika sheria Yako katika akili yake na juu ya moyo wake ili atembee daima na uhakikisho wa haki ya amri Zako. Pale anapojifunza kuomba, basi yeye ajifunze pia kusikiliza sauti Yako. Ninaomba kwamba uhusiano wake na Wewe kamwe hautakuwa vuguvugu, kutojali, au kutokuwa na kina. Daima kuwe na moto wa Roho Mtakatifu ndani ya moyo wake na matamanio yasiyomangamanga katika mambo ya Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo nimeomba. AMEN

## SILAHA ZA VITA

Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watashibishwa.

**MATHAYO 5:6**

Kumcha BWANA ni chemchemi ya uzima, Ili kuepusha mtu na mitego ya mauti.

**MITHALI 14:27**

Nimesulubiwa pamoja na Kristo; si mimi tena ninayeishi, bali Kristo Yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika

imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda na kujitoa nafsi Yake kwa ajili yangu.

**WAGALATIA 2:20**

Heri wazishikao shuhuda Zake, wamtafutao kwa moyo wote!

**ZABURI 119:2**

Unifundishe njia Yako, Ee BWANA; nitakwenda katika Kweli Yako; uunganishe moyo wangu kulicha Jina Lako. Nitakusifu, Ee Bwana, Mungu wangu, kwa moyo wangu wote, na nitalitukuza Jina Lako milele.

**ZABURI 86:11-12**

## Sura ya kumi

## AWE MTU MUNGU ALIYEMUUMBA

Namjua mwanamume aliyeacha kazi yake ya uhandisi yenye mshahara mnono katika kampuni kubwa ili kuwa fundi magari. Alifanya hivyo kwa sababu alipenda kufanya ukarabati wa magari kuliko kitu kingine chochote. Hakuwa fundi bora tu mjini, bali pia mtu mwenye furaha na aliyeridhika. Namjua mtu mwingine ambaye alikataa kufuata wito wa Mungu wa kuwa mchungaji kwa sababu alitaka kuwa mfanyabiashara aliyefanikiwa badala yake. Hatimaye alipoteza familia yake kwa talaka, alipatwa na kifo cha mwanawe mdogo, na aliona maisha yake yakizidi kuwa ya huzuni na hasara. Huenda mambo yangekuwa tofauti kwa kiasi kikubwa kama angekuwa na mzazi anayesali au mtu anayemsaidia kuelewa Mungu alimfanya yeye kuwa nani.

Kutokujua Mungu alituumba kwa sababu gani, ni kujaribu kuwa kile tusichopaswa kuwa, au hata *kutamani* tu kuwa mtu mwingine, hii inaweza tu kusababisha maisha ya taabu, kufadhaika, na kutoridhika.

Tunaona mifano ya hili kwa watu wazima wanaofanya kazi wanazochukia, wanaoishi maisha duni ambayo daima hayafikii matarajio yao. Unaweza kuwa na uhakika kwamba wakati fulani watu kama hao walikubali uwongo unaosema, "Mimi nilivyo haitoshi. Nahitaji kuwa mtu mwingin, najitafuta, na bado sijui niwe nani." Labda hawajawahi kutiwa moyo kutambua uwezo na talanta walizopewa na Mungu. Hakika hawajatambua Mungu aliwaumba kuwa nani.

Tunaweza kuishi kulingana na kusudi Mungu alituumba kuwa tunapomwomba Mungu mwongozo na kisha kufanya kile anachotuambia tufanye.

Nabii Yeremia aliendelea kuwaambia watu wa Israeli kile ambacho Mungu alitaka wasikie, lakini walikataa kusikiliza. Hatimaye, Bwana akasema, "Tazama, nitaleta juu ya Yuda, na juu ya wenyeji wote wa Yerusalemu maangamizi yote niliyoyatamka juu yao; kwa sababu nimesema nao lakini hawakusikia, Nami nimewaita lakini hawakuitika" (Yeremia 35:17). Mambo ya uharibifu hutokea kwetu wakati hatuitikii sauti ya Mungu. Tunaweza kuomba kwamba watoto wetu wawe na masikio ya kusikia sauti ya Mungu ili taabu kama hiyo isiwapate. Moja ya mipango ya Shetani kwa vijana ni kuwafanya wajilinganishe na wengine, wajihukumu kuwa ni wapungufu, kisha watafute kuwa mtu ambaye hawakuumbwa kuwa. Wasichana wachanga hujilinganisha na wasichana wengine na kuwaona kuwa na nywele nzuri zaidi, nguo nzuri zaidi, nyumba bora, umaarufu mkubwa, ufaulu wa juu wa masomo, au talanta na urembo zaidi. Wavulana

wachanga hutazama wavulana wengine na kuwaona kuwa warefu zaidi, wenye sura nzuri zaidi, wanariadha wakubwa zaidi, wenye marafiki wengi, na ndevu nzuri zaidi, mali zaidi, au ujuzi na uwezo zaidi. Siku baada ya siku kujilinganisha na kupungukiwa kunaweza kushambulia utambulisho wa kweli wa mtoto. Nimewajua vijana wengi sana ambao, wanapofikia utineja wao, hutamani kuwa mtu mwingine badala ya jinsi walivyo. Badala ya kuthamini kile Mungu aliwaumba kuwa na kutumia nguvu zao kujaribu kuwa bora zaidi katika hilo, wanajitahidi na kujikaza kuwa kitu ambacho hawawezi kuwa, wanaishi maisha feki, wakifanya kitu ambacho hawatakitimiza kamwe. Maombi yetu wazazi yanaweza kuzuia mpango huu wa adui na kuwapa watoto wetu maono wazi ya wao wenyewe na maisha yao ya baadaye.

Tangu watoto wangu walipokuwa wadogo nilimwomba Mungu kutufunulia karama na talanta zao ni zipi. Pamoja na hayo niliomba hekima ya jinsi ya kuwatia moyo vyema, kuwalea, kuwakuza na kuwazoeza wawe kile chote ambacho Mungu aliwaumba wawe. Kuwasaidia kuthamini uwezo wao na kutozingatia udhaifu wao ilikuwa sehemu ya hayo; na kwa kuwa hii haikuwa rahisi wakati wa miaka yao ya ujana, ilikuwa lengo la mara kwa mara la maombi yangu.

Sehemu kubwa ya kumsaidia mwanangu na binti kuelewa Mungu aliwaumba kuwa nani, ilikuwa ni kuhimiza uhusiano wao na Bwana. Najua hawatawahi kuelewa kabisa *wao* ni nani hadi waelewe *Mungu* ni nani.

Katika Biblia ambapo Mungu anaahidi kumwaga Roho Wake juu ya watoto wetu, Anatamka juu yao, “Watameta kati ya majani kama mierebi kando ya mifereji ya maji.' Mmoja atasema, Mimi ni wa BWANA… na mwingine ataandika kwa mkono wake, ni wa Bwana” (Isaya 44:4-5). Watoto hawa watajua wao ni nani. Watajazwa na Roho Wake na kuwa na ujasiri huo wa ndani wa kujua wao ni Wake. Utagundua usoni mtoto yeyote mwenye ujasiri na mwenye kung’aa anayeweza kusema kwa usadikisho, “Mimi ni wa Bwana.” Je! unataka hiyo kwa ajili ya mtoto wako? Je, nini kitakuchosha ushindwe kuliombea jambo hilo?

### *Maombi*

*Bwana,* ninaomba kwamba ungemimina Roho Wako juu ya -------------- (jina la mtoto) siku hii na kumtia mafuta kwa yote ambayo umemuita kuwa na kufanya. Bwana, umesema, “Kila mtu na abaki na Mungu katika hali ile aliyoitwa nayo” (1 Wakorintho 7:24). Na iwe kwa mtoto huyu kulingana na Neno Lako, kwamba kamwe asipotee kutoka kwa kile Ulichomwita yeye kuwa na kufanya, ama kujaribu kuwa kitu ambacho sio makusudi yako.

Mwokoe kutoka kwa mpango wowote mbaya wa Shetani wa kumnyang'anya maisha, kumwibia upekee wake, utambulisho wake na vipawa, na kisha kuhatarisha njia ambayo umemwita atembee kwayo, au kumharibu mtu uliyemuumba kwa makusudi fulani. Na asiwe mfuasi wa yeyote ila awe mfuasi wako Wewe na kiongozi wa watu katika ufalme wako. Msaidie kukua na kufikia ufahamu kamili wa mamlaka katika Yesu

Kristo, huku akibaki na roho ya utii na unyenyekevu.

Tunda la Roho Wako, ambalo ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, na kiasi, lipate kukua ndani yake kila siku (Wagalatia 5:22-23). Na apate utambulisho wake Kwako, ajione mwenyewe kama chombo Chako, na ajue kwamba yeye amekamilika ndani Yako.

Mpe maono ya maisha yake wakati wa kuweka malengo ya siku zijazo na hisia ya kusudi la juu ya kile Umemwitia yeye kufanya. Msaidie ajione kuwa ameumbwa kwa mfano Wako. Na yeye awe na hakika kwamba mawazo yako kwake ni mawazo ya amani, wala si ya mabaya, kumpa tumaini la siku zijazo (Yeremia 29:11). Mfundishe kukutazama Wewe Bwana, kama tumaini lake la wakati ujao. Aelewe kuwa ni Wewe "uliyetuokoa na kutuita kwa mwito mtakatifu, si kwa kadiri ya matendo yetu, bali kwa kadiri ya makusudi Yako Wewe na neema Yako tuliyopewa katika Kristo Yesu kabla ya nyakati" 2 Timotheo 1:9. Muwezeshe kujitoa Kwako, aliishi kusudi Lako na azidi kukua kila siku katika ujasiri na uimara wa Roho Mtakatifu. Katika Jina la Yesu ninaomba. AMEN

## SILAHA ZA VITA

Ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili Zake, Yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru Yake ya ajabu.

**1 PETRO 2:9**

Jicho halijaona, wala sikio halijasikia, wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao.

**1 WAKORINTHO 2:9**

Fanyeni bidii zaidi kuhakikisha mwito wenu na uteule wenu, maana mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe.

**2 PETRO 1:10**

Nasi twajua kwamba mambo yote hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani wale walioitwa kwa kusudi Lake. Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwanawe, ili Yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi. Tena wale aliowachagua tangu asili, hao pia aliwaita; wale aliowaita, hao pia aliwahesabia haki; na wale aliowahesabia haki, hao pia akawatukuza.

**WARUMI 8:28-30**

Ondoka, uangaze; kwa maana nuru yako imekuja! Na utukufu wa BWANA amekuzukia.

**ISAYA 60:1**

## Sura ya kumi na moja

## KUFUATA UKWELI, KUKATAA UONGO

Katika nyumba yetu, watoto wetu walijua kwamba ingawa ingewezekana kufanya mkataba kuhusu kuondoa adhabu kwa makosa fulani, lakini ikiwa uongo ulikuwa sehemu ya kosa, basi adhabu ingetekelezwa kwa haraka, papo hapo, na ingekuwa isiyopendeza, na isiyoweza kujadiliwa. Tunachukulia kusema uongo kuwa kosa baya zaidi kwa sababu ni msingi wa matendo mengine yote maovu. Kila dhambi au uhalifu huanza na mtu kuamini au kusema uwongo. Hata kama uwongo ni rahisi kama "Ninaweza kupata ninachotaka nikisema uwongo," unafungua njia ya uovu.

Mapema, binti yangu alijaribu kukanyaga ardhi ya "uongo mdogo wa wazi." Lakini haikumchukua muda kuona kwamba adhabu ya kusema

uwongo ilifunika kwa kiasi kikubwa faida yoyote ambayo alifikiri angeweza kuipata kutokana na kusema uwongo. Mwanangu wa kiume, kwa upande mwingine, hakucheza na uongo tu, bali pale aliposema uongo mdogo, aliendelea kusema uongo mkubwa zaidi.

Zakaria alipokuwa na umri wa miaka saba, alikuwa akicheza mpira na rafiki yake Stefano mbele ya nyumba ya wakina Stefano. Mpira uligonga dirisha kubwa la mbele na kuleta mpasuko mkubwa, ambao mara moja ulimleta mama Stefano kwenye mlango wa mbele. “Nani alifanya hivi?” Aliuliza. “Sikupasua dirisha,” alisema Stefano. “Sio mimi,” Zakaria naye alisema. "Stefano, unataka kuniambia kuwa hukugonga dirisha na mpira huu?" alisema. “Hapana, sikufanya hivyo,” alijibu Stefano kwa msisitizo. "Je, Zakaria, wewe *uligonga* dirisha na mpira?" Aliuliza.

"Kama uliniona nimevunja, basi ni mimi nimevunja. Ikiwa hukuniona nikifanya hivyo basi sijafanya hivyo,” Zakaria alijibu kwa sauti yake yenye Ukweli wenye utata. "Sikuona ukifanya hivyo," alisema. “Basi sikufanya hivyo,” akajibu.

Mama yake Stefano alipotuambia kilichotokea, tulijua kwamba tulihitaji kushughulikia jambo hili mara moja ili Zakaria asifikirie kwamba angeweza kuepuka adhabu ya uwongo. “Zakaria, kuna mtu aliona kila kitu kilichotokea. Je, ungependa kutuambia kuhusu hilo?” Nilisema, nikitaka kukiri kwake kamili na moyo wa toba. Aliinamisha kichwa chake na kusema, "Sawa, nilifanya hivyo."

Tulikuwa na mazungumzo marefu kuhusu kile ambacho Neno la Mungu linasema kuhusu uwongo. “Shetani ni mwongo,” nilimwambia. “Maovu yote anayofanya yanaanza na uongo. Watu wanaosema uwongo wanaamini kwamba kusema uongo kutawafanyia mambo kuwa mazuri zaidi. Lakini kwa kweli, inafanya kinyume. Hiyo ni kwa sababu kusema uongo inamaanisha kuwa umejiweka sawa na Shetani. Kila unaposema uongo unampa Shetani kipande cha moyo.

Kadiri usemavyo uwongo mwingi, ndivyo unavyoipa nafasi moyoni mwako roho ya uongo ya Shetani, hadi mwishowe huwezi kujizuia kudanganya. Biblia inasema, ‘Kupata hazina kwa ulimi wa uwongo ni ndoto ya kitambo ya wale wanaotafuta kifo’ (Mithali 21:6). Kwa maneno mengine, unaweza *kufikiri kwamba* unapata kitu cha maana pale unaposema uongo, lakini unachofanya ni kuleta kifo katika maisha yako. Matokeo ya kusema Ukweli lazima yawe bora kuliko kifo. Hata adhabu unayopata kutoka kwake.

Wazazi kwa kusema uongo, itakuwa hali ya kusaidia watoto hawa kwa ubaya kuliko matokeo ya uwongo. Kwa maana Biblia inaahidi kwamba ‘shahidi wa uongo hatakosa kuadhibiwa, naye asemaye uongo hataokoka’ (Mithali 19:5).”

Ilikuwa muda mrefu sana baada ya tukio hilo kabla Zakaria kuniuliza ni nani aliyemwona siku hiyo.

“Ilikuwa Mungu,” nilieleza. “Alikuona. Daima nimemwomba anifunulie chochote ninachohitaji kujua kuhusu wewe au dada yako. Yeye ni Roho wa

Kweli, je, unaelewa."

"Mama, hiyo si haki," ndiyo yote aliyosema. Hata hivyo, baada ya hapo, katika vipindi chache aliposema uwongo, sikuzote alinijia mara moja kuungama. "Niliona afadhali nikuambie kabla hujaisikia kutoka kwa Mungu," angeeleza. Watoto watasema uongo wakati mmoja au mwingine. Swali sio *kama* watafanya hivyo, lakini kama kusema uwongo kutakuwa na jambo wanaloamini kuwa wanaweza kujiepusha nalo. Jinsi tunavyoshughulikia uongo wao ndio huamua matokeo. Tusipowafundisha watoto wetu kile ambacho Mungu anasema kuhusu uwongo, hawatajua kwa nini ni kosa. Tusipowaadhibu wanaposema uongo, watafikiri kusema uongo hakuna athari yoyote. Tusipoomba kuhusu suala hili sasa, kutakuwa na masuala makubwa zaidi ya kushughulikia baadaye.

Biblia inasema hivi kuhusu Ibilisi, "Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo, wala hasimami katika Kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo, husema yaliyo yake mwenyewe, kwa maana yeye ni mwongo na baba wa huo" (Yohana 8:44). Unapofikiria chanzo, hakuna njia unaweza kukaa karibu na kuruhusu mbegu ya uongo kuota mizizi ndani ya moyo wa mtoto wako.

Omba sasa kwamba roho yoyote ya uongo ing'olewe - si tu kwa watoto wako, lakini ndani *yako mzazi* pia.  Usiwe wazazi wale wanaosema "mwambie sipo nyumbani wakati mtoto anapoulizwa, nawe upo". Wakati mwingine wazazi huwa wapole katika suala hili na watoto wao kwa sababu wanasema uongo wenyewe. Tunahitaji kukataa njia ya uwongo na

kufuata Ukweli. Tunahitaji kuwa mfano kwa watoto wetu. *Tunataka* kuweza kusema kama Yohana alivyosema, “Sina furaha iliyo kuu kuliko kusikia ya kwamba watoto wangu wanaenenda katika Kweli” (3 Yohana 1:4). Hatutaki watoto wetu waendane na baba wa uongo. Tunataka wapate kuunganishwa na Baba wa Nuru (Yakobo 1:17).

***Maombi***

*Bwana,* ninaomba umjaze------- (jina la mtoto) na Roho wako wa Ukweli. Mpe yeye moyo unaopenda haki na kuifuata, akikataa uwongo wote kuwa ni dhihirisho la adui. Toa chochote ndani yake ambacho kinaweza kuburudisha pepo wa uwongo na kumtakasa yeye kutokana na kifo chochote ambacho kimeingia kwa sababu ya uwongo ambao yeye alizungumza au kufikiria. Msaidie kuelewa kwamba kila uwongo humpa Shetani kipande cha moyo wake, na ndani ya shimo lililosalia huja machafuko, kifo, na kutengwa na uwepo Wako. Mwokoe kutoka kwa roho yoyote ya uwongo. Ninaomba kwamba asipofushwe au kudanganywa, lakini daima aweze kuelewa Ukweli Wako waziwazi.

Ninaomba kwamba hataweza kamwe kufuga uwongo—kwamba uwongo wote udhihirike na kufichuliwa. Iwapo atasema uwongo, na awe na huzuni kiasi kwamba kukiri na matokeo yake kutaonekana kama kitulizo pekee. Nisaidie kumfundisha yeye maana ya kusema uwongo, na kumwadhibu ipasavyo anapojaribu tabia hiyo. Neno lako linasema kwamba “Yeye atakapokuja, huyo Roho wa Kweli, atawaongoza awatie kwenye Kweli yote”

(Yohana 16:13). Ninaomba kwamba Roho Wako wa Ukweli atamwongoza yeye kwenye Kweli yote. Na kamwe asiwe mtu wa kutoa nafasi kwa uwongo, bali awe mtu mwadilifu anayefuata kwa bidii Roho wa Ukweli. Katika Jina la Yesu ninaomba. Amen

**SILAHA ZA VITA**

Midomo ya uongo ni chukizo kwa BWANA, bali watendao Kweli ndio furaha Yake.

**MITHALI 12:22**

Nafsi yangu inayeyuka kutokana na huzuni; unitie nguvu sawasawa na Neno Lako. Uniondolee njia ya uongo, na unipe sheria Yako kwa neema.

**ZABURI 119:28-29**

Rehema na Kweli zisikuache; zifunge shingoni mwako, ziandike katika kibao cha moyo wako, ukapate kibali na kustahi mbele za Mungu na wanadamu.

**MITHALI 3:3-4**

Kuja Kwake yule mwasi ni kwa jinsi ya kutenda Kwake Shetani, kwa uwezo wote, na ishara, na ajabu za uongo, na madanganyo yote ya udhalimu kati yao wanaopotea, kwa sababu hawakukubali kuipenda ile Kweli, wapate kuokolewa.

**2 WATHESALONIKE 2:9-10**

Mkinipenda, mtazishika amri Zangu. Nami nitamwomba Baba, Naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele; Ndiye Roho wa Kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni, wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua kwa maana anakaa kwenu, Naye atakuwa ndani yenu.

**YOHANA 14:15-17**

## Sura ya kumi na mbili

## KUFURAHIA MAISHA YA AFYA NA UPONYAJI

Binti yangu alipokuwa na umri wa miaka minne aligundulika kuwa na tatizo la macho ambalo daktari alisema lingehitaji kufanyiwa upasuaji na kuvaa miwani minene maisha yake yote.

"Bwana, Je, hivi ndivyo unavyotaka iwe kwa binti yangu?" Niliomba. "Nionyeshe, kwa sababu sina amani juu yake."

Mume wangu alihisi nilivyohisi, kwa hiyo tukasali ili macho ya Anna yapone. Pia tulisali kwamba, ikibidi, tutafute daktari mwingine ambaye angeweza kumsaidia. Siku iliyofuata, kwa njia ya ajabu, nilipokea simu kutoka kwa mtu ambaye hakujua kuhusu hali ya Anna, lakini alikuwa na taarifa kuhusu mtaalamu bora katika kliniki ya macho katika Hospitali ya Watoto huko mjini kwetu. Nilimpeleka Anna kwa daktari

huyu, na baada ya kumpima vizuri, alinipa habari za kutia moyo. Aliamini kwamba aina fulani za miwani, zingerekebisha tatizo hilo na hangehitaji kufanyiwa upasuaji. Tulihisi amani ya haraka kuhusu uchunguzi wake na tukamweka Anna katika uangalizi wa daktari huyu, ingawa hatukuacha kamwe kusali ili apone.

Kwa miaka minane alivaa lenzi za miwani hizi chini ya uangalizi mkali wa daktari. Tulitaabika katika kuitunza miwani yake kila Siku na tulipowapeleka nje kila usiku katika miaka ya mapema nilichoka kuitwa kwenda shule kila mara alipopoteza miwani yake kwenye uwanja wa michezo.

Lakini tulivumilia. Kisha siku moja alipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili, alienda kwa uchunguzi wake wa kawaida wa macho na daktari akasema, “Huhitaji tena mawani hii maalumu au hata upasuaji.

Macho yako ni mazuri.” Tulifurahi na kumshukuru Mungu kwa mwongozo W ake na jibu la maombi.

Tumewaombea watoto wetu katika kila homa, mafua, magonjwa ya mafua, na majeraha, na Bwana amejibu kila mara. Hatusiti kamwe kuwapeleka kwa daktari inapohitajika kufanya hivi, kwa sababu tunajua Mungu anaweza kuponya kupitia madaktari, pia. Lakini Biblia inasema, “Je, kuna yeyote kati yenu aliye mgonjwa? Na awaite wazee wa kanisa, nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa Jina la Bwana. Na kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa huyo, na Bwana atamwinua” (Yakobo 5:14-

15).

Jambo kuu ni kuomba kwanza na kuona daktari kila inapobidi. Na kisha, tunapoponywa, hatupaswi kuhoji au kutilia shaka.

Baada ya hapo, mtoto wetu alipata ajali ya gari. Mgongo na magoti yake yalikuwa yanauma sana. Sisi, tuliomba mara moja, bila kuwa na mashaka, kwa ajili ya uponyaji wake na tukahakikisha kwamba alipigwa Xray (eksirei au picha) na kuchunguzwa vizuri hospitalini. Tuliendelea kusali ili apone kabisa, hata hivyo, kwa sababu hatukutaka awe na udhaifu mgongoni na magotini ambayo ingeweza kuwa tatizo kwa maisha yake yote.

Nilihisi kuvutiwa *sana* na Maandiko, "Kwa maana nitakurudishia afya, na kukuponya jeraha zako; asema BWANA" (Yeremia 30:17). Nilikuwa na hakika kwamba mwanangu alikuwa mzima

"Nataka uponyaji, Bwana, na asante," nilimwambia Bwana bila kusita. Hata watu walipotaka kutukatia bima ya matibabu tulikataa. Sisemi kwamba ni ukosefu wa imani kuwa na bima. Siamini hivyo hata kidogo. Lakini katika tukio hili kukataa fidia lilikuwa jambo sahihi kwetu kufanya. Tunapoomba kwa ajili ya uponyaji na Mungu anatuponya, hatupaswi kutenda kana kwamba halikutokea.

Biblia imejaa ahadi za uponyaji. Daudi alisema, "Ee nafsi yangu, umhimidi BWANA, **Wala usizisahau fadhili Zake zote; Akusamehe maovu yako yote,** Akuponya magonjwa yako yote" (Zaburi 103:2-3). Moja ya mambo makuu ambayo Yesu anataka yatendeke kwetu ni Msamaha wa dhambi

zetu na mponyaji wa miili yetu. Hebu tuishike afya na uponyaji alionao kwa watoto wetu kwa kuuombea hata *kabla* hitaji halijatokea.

***Maombi***

Bwana, kwa sababu umetuagiza katika Neno Lako kwamba tunapaswa kuombeana ili tupate kuponywa, naomba uponyaji na utimilifu kwa---------- (jina la mtoto). Ninaomba kwamba magonjwa na udhaifu visiwe na nafasi au nguvu katika maisha yake.

Ninaomba ulinzi dhidi ya ugonjwa wowote unaokuja kwenye mwili wake (Neno Lako linasema, "Alituma Neno Lake na kuwaponya, na kuwaokoa kutoka kwa uharibifu wao" (Zaburi 107:20).

Popote palipo na ugonjwa, kuugua, au udhaifu katika mwili wake, ninaomba kwamba Wewe, Bwana, umguse yeye kwa nguvu Zako za uponyaji na umrudishe katika afya kamili.

Mwokoe mkewe kutokana na uharibifu au madhara yoyote yanayoweza kumpata. Hasa ninakuomba apone--------- (taja shida yoyote maalum). Kama tunapaswa kumwona daktari, naomba ya kwamba Wewe, Bwana, utuonyeshe huyo Daktari anapaswa kuwa nani. Mpe daktari huyo hekima na ujuzi kamili wa njia bora ya kuendelea kumtibu ………………..

Asante, Bwana, kwa kuwa uliteseka na kufa kwa ajili yetu ili tupate kuponywa. Ninadai ahadi hiyo ya uponyaji ambao umeahidi katika Neno Lako na kuwapa wale wanaoamini. Ninakutegemea Wewe kwa ajili ya

maisha ya afya, uponyaji, na ukamilifu kwa mtoto wangu.

Katika Jina la Yesu ninaomba, AMINA.

## SILAHA ZA VITA

Alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona.

**ISAYA 53:5**

Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, ili mpate kuponywa. Maombi yake mwenye haki yafaa sana akiomba kwa bidii.

**YAKOBO 5:16**

Lakini kwenu ninyi mnaolicha Jina Langu, Jua la Haki litawazukia lenye kuponya katika mbawa Zake.

**Malaki 4:2**

Maana ninyi mliitwa kwa ajili hiyo, maana Kristo Naye aliteswa kwa ajili yetu, akawaachia kielelezo, mfuate nyayo Zake; Yeye Mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili Wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa ajili ya haki ambayo kwa kupigwa Kwake mliponywa.

**1 PETRO 2:21,24**

Nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na uponyaji wako utatokea mara, na haki yako itakutangulia; utukufu wa BWANA utakuwa nyuma ukulinde.

**ISAYA 58:8**

## Sura ya kumi na tatu

## KUWA NA MOTISHA WA KUTUNZA FAMILIA

Wakiachwa peke yao katika ulimwengu huu wa vyakula visivyofaa, watoto watavutiwa na vyakula vyote vibaya. Chakula kingi tunachokula kimepitia mchakato usiofaa, kimetolewa maganda kwa kukobolewa au kusindikwa, kubadilishwa, kuongezwa visivyofaa, na kuondolewa, hivi kwamba kina thamani ndogo kulinganisha na jinsi Mungu alivyoumba kwa asili. Lakini watoto hawajali kuhusu hilo. Wanataka tu chakula chenye kupendeza macho yao au cha maigizo ambacho wengine wanakula pale wanapoendelea kukua au kipo katika fasheni, chenye harufu nzuri, na baadaye wanajenga uzoefu wa kukipenda na kisha wanasema ni kizuri— na ikiwa wamekiona kikitangazwa kwenye

televisheni wao wanaona hicho ni bora zaidi kwao. Na ikiwa una mwenzi, ambaye anapenda chakula kisicho na afya na huleta ndani ya nyumba kwa ajili yake na watoto, una hali ngumu zaidi.

Nilijua nilikuwa na matatizo siku niliyorudi nyumbani, baada ya kumwacha mtoto wetu wa miezi kumi na baba yake mchana, akapewa cocacola kwenye chupa yake ya mtoto. Niligundua basi kwamba maombi ndiyo tumaini langu pekee.

Nilijitahidi sana kufanya milo yenye afya iwe yenye kupendeza, na nilijaribu kuwafundisha watoto wangu mazoea ya kula vizuri. Nilikuwa tayari hata kuvumilia kukosolewa kutoka kwao, alimradi wale kile kilicho na manufaa katika afya zao.

"Nachukia sana chakula cha hapa nyumbani kwetu, ni sisi pekee duniani ambao tuna chakula kibaya jikoni mwetu," alisema mwanangu kwa kuchukizwa sana.

"Hivi vyakula vya afya sana vinanifanya niwe mgonjwa," binti yangu alisema huku machozi yakimtoka.

Kwa sababu ninaamini kwamba "bora mkate mkavu pamoja na utulivu ni bora kuliko nyumba iliyojaa karamu pamoja na ugomvi" (Mithali 17:1), sijaliwezea suala hili kama ambavyo ningependa. Najua siwezi kuwalazimisha watoto wangu kuchagua chakula chenye afya wakati sipo karibu kuwakumbusha. Ni nguvu za Mungu tu kupitia maombi, ndizo zinaweza kuleta mabadiliko katika maisha yao.

Karibu kila mtu anajitahidi kwa kiasi fulani katika eneo la utunzaji mwili kwa usahihi. Lakini kwa sababu ya vitabu vya afya ambavyo nimeandika, semina za afya ambazo nimetoa na kuhimiza mazoezi, nimekutana na watu wengi ambao wanapambana vikali na suala hili—hata kufikia uchungu na kushindwa. Tunawakosea watoto wetu ikiwa hatutawaunga mkono katika maombi, pamoja na kuwaongoza na kuwaelekeza katika mambo ya afya, ili wasije wakaingia kwenye masaibu ya namna hii. Chakula kinarithiwa, wengi hula kile walichoanza kula kutoka udogo wao. Kama mzazi omba na kutoa mfano.

Ikiwa watoto wako ni wachanga, anza kusali ili wavutwe na chakula chenye afya na kutamani kufanya mazoezi na kutunza miili yao vizuri.

Usipofanya hivyo, kufikia wakati wa ujana wao, wanaweza kuwa tayari wamesitawisha mazoea mabaya na hali hiyo inaweza kutoka nje ya udhibiti haraka. Tunaona hili katika matatizo ya ulaji ambayo ni janga miongoni mwa wasichana wa matineja na wale wa umri wa chuo kikuu na ambayo sasa yanaonekana zaidi na zaidi kwa wavulana. Watoto wanakuwa wanene kupindukia, na kupata magonjwa, kumbuka Bustani ya Edeni ilipotea kwa ajili ya chakula! Kuwa na kiasi na kushinda ulafi ni muhimu. Kitabu cha DSM cha kuonyesha magonjwa (diagnosis), kimeongeza kutotawala nafsi kama mojawapo wa maradhi ya akili.

**Anza kuomba kabla ya dalili kama hizo kuonekana.**

Ikiwa watoto wako ni wakubwa, anza sasa hivi kuwaombea kwa niaba yao.

Wanawake wengi wachanga wanaougua ugonjwa wa anorexia na bulimia hupambana na zaidi ya tamaa za mwili; wanakabiliwa na vita vya kiroho pia. Wanalazimika kufuata mazoea ya kula ambayo ni hatarishi na huwa yanapingana kabisa na jinsi Mungu alivyowaumba waishi. Nimejua wanawake wengi sana vijana ambao wanateseka katika suala hili hasa huku magharibi. Wale ambao wana wazazi wanaojifunza kuwaombea kwa niaba yao baadaye wana visa vya mafanikio ya kusimulia. Wengine wasiojaliwa hawana. Mabinti hawa wakiwa wajawazito hujifungua watoto wenye utindio wa ubongo na afya mbaya, kwa vile mwili hauna lishe ya kufaa kwao wenyewe na watoto matumboni mwao.

Mtoto wako anahitaji mwongozo na nguvu ya Roho Mtakatifu ili kufanya kile kinachofaa kwa ajili ya mwili wake. Maombi yako yanaweza kuwaepusha kushindwa sana, kufadhaika, na kuvunjika moyo. Je, hutamani ungekuwa na mtu anayekuombea kuhusu hili? Najua unafanya hivyo.

### *Maombi*

*Bwana, ninamwinua* --------- (jina la mtoto) kwako na kuomba kwamba ungeweka ndani yake hamu ya kula chakula cha afya. Na kumwepusha na ulafi wa chakula.

Ninajua kwamba katika maisha yake, yeye atajaribiwa kufanya uchaguzi mbaya wa chakula na kula kile kinacholeta kifo badala ya afya, Naomba Msaidie yeye kuelewa ni nini chema kwake na kisichofaa, na mpe hamu ya chakula chenye afya. Hebu yeye achukizwe au kutoridhishwa na chakula

ambacho ni hatari.

Ninaomba aepushwe na matatizo yote ya ulaji kwa namna yoyote ile. Kwa mamlaka niliyopewa katika Yesu Kristo (Luka 10:19), kwa niaba ya binti yangu/kijana wangu ninasema, “Hakuna magonjwa ya lishe mbaya hapa kwangu,” “Hakuna anorexia au bulimia,” “Hakutakuwa na uraibu wa chakula,” “Hakuna kula kupita kiasi au ulafi, ” "Hakuna aina yoyote ya mazoea ya ulaji yasiyo na msawaziko kwangu."

Bwana, Neno Lako linasema, “Mtaifahamu Kweli, nayo hiyo Kweli itawaweka huru” (Yohana 8:32). Msaidie aone Ukweli kuhusu jinsi yeye anavyopaswa kuishi, ili aweze kuwekwa huru kutokana na mazoea yasiyofaa. Ninaomba kwamba pamoja na hamu ya kula vizuri, Umpe yeye motisha ya kufanya mazoezi mara kwa mara, kunywa maji mengi safi, na kudhibiti msongo au sonona katika maisha yake kwa kuishi kulingana na Neno Lako. Wakati wowote anapohangaika katika mojawapo ya maeneo hayo na akugeukie Wewe na kusema, “Ee BWANA, unifundishe njia Yako” (Zaburi 27:11). Mpe kuuona mwili wake kama hekalu la Roho Wako Mtakatifu.

Ninaomba kwamba athamini mwili uliompa yeye na kutamani kuutunza ipasavyo. Na asiwe mkosoaji, wala asijichunguze mwenyewe kupitia darubini ya maoni ya umma na kukubalika. Ninaomba asifungwe na mvuto wa magazeti ya mitindo (fasheni), televisheni, au sinema zinazojaribu kumshawishi (yeye) kwa taswira ya kile wanachosema anapaswa kuonekana. Mwezeshe kusema, “Uyageuze macho yangu

yasitazame mambo yasiyofaa" (Zaburi 119:37). Msaidie kuona kwamba kinachomfanya mtu avutie kweli ni Roho Wako Mtakatifu anayeishi ndani yake na kung'aa kwa nje. Na yeye aelewe kwamba mvuto wa Kweli huanzia moyoni mwa mtu anayempenda Mungu. Anzisha maono Yako ya afya na kufanya yavutie ndani yake siku hii ya leo, na uimarishe ndani yake hamu ya kuutunza mwili wake ipasavyo kwa sababu ni hekalu la Roho Wako Mtakatifu. Katika Jina la Yesu ninaomba.

## SILAHA ZA VITA

Je! Hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu, na si mali yenu wenyewe? Kwa maana mlinunuliwa kwa bei; basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu na roho zenu ambazo ni za Mungu.

**1 WAKORINTHO 6:19-20**

Mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi.

**1 WAKORINTHO 3:17**

Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma Zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana.

**WARUMI 12:1**

Mvaeni Bwana Yesu Kristo, wala msiuangalie mwili hata kuwasha tamaa zake.

**WARUMI 13:14**

Basi, mlapo au mnywapo, au mtendapo neno lolote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu.

**1 WAKORINTHO 10:9,10**

## Sura ya kumi na nne

## KUWEKA HAMU YA KUJIFUNZA

Mama mmoja aliandika kwamba Shule ilikuwa kwake rahisi alipokuwa mdogo, ila kukutana na watu wengi wa jamii, ulikuwa uzoefu wa kutisha, lakini kupata A ilikuwa rahisi. Ndiyo maana hakuwahi kufikiria kusali kuhusu watoto wake kuwa na uwezo au motisha ya kujifunza masomo ya darasani.

Mpaka alipogundua kuwa mmoja wa watoto wake alikuwa na aina ya shida ya kujifunza iitwayo dyslexia. Kwa sababu mtoto huyu alikuwa

mchangamfu, mwenye akili, na mwenye vipawa vya kipekee, uwezekano wa ugumu wa kujifunza haukuingia akilini mwake. Hata hivyo, masomo yalikuwa na ugumu kwake tangia mwanzo, na hawakuelewa na mumewe kilichokuwa kikitendeka hadi ugumu wa kusoma wa mtoto wao ulipotambuliwa kitaaluma akiwa katika darasa la tatu. Ingawa walikuwa na nyakati nyingi za kuhuzunisha kwa sababu ya tatizo hili, maombi yaliwategemeza katika njia yote. Mumewe na yeye, na wenzao katika maombi waliendelea kuomba kwamba mtoto huyu apone kabisa au awe na amani kabisa juu yake. Kama hali ilivyotokea, alimfundisha mwenyewe mtoto huyu nyumbani kwa miaka miwili ya sekondari na mtoto aliweza kusitawisha furaha ya kujifunza ambayo ilikuwa imepotea (homeschooling). Leo, mtoto huyu amefanikiwa sana katika taaluma ambayo inaendana na talanta maalum ya mtoto, aliyopewa na Mungu. Mtoto huyu akawa na ushindi wa juu kwenye darasa lake chuoni katika taaluma yake. Miaka hiyo ya mapambano. Kwa njia moja au nyingine, bila shaka, sote tuna mapungufu.

Kwa kushukuru, Mungu hutatua mapungufu yetu kwa nguvu Zake. Neno Lake linasema, “Si kwamba twatosha sisi wenyewe kufikiri neno lolote kuwa latoka kwetu wenyewe, bali utoshelevu wetu watoka kwa Mungu” (2 Wakorintho 3:5). Maarifa ya Kweli na ufahamu huanza na kutoka kwa Bwana.

Biblia inatufundisha kwamba ujuzi huanza kwa kumcha Mungu na njia zake. Tukipokea maneno Yake na kuziweka kuwa hazina amri Zake

mioyoni mwetu, tukifanya kazi ya kujaribu kuelewa na kumwomba Mungu atusaidie kufanya hivyo, ikiwa tunatafuta ufahamu kwa bidii kama vile tungetafuta hazina iliyofichwa, basi tutapata ujuzi wa Mungu (Mithali 2:1-12). Na ni elimu kubwa iliyoje basi. Kwa kweli, ni ngao ambayo hutuokoa na kutulinda kutokana na maovu.

Uwezo na hamu ya mtoto ya kujifunza haiwezi kuchukuliwa kuwa ni jambo la kawaida tu. Hata wakati mtoto wetu angali tumboni tunaweza kusali, "Bwana, acha mtoto huyu aungwe kikamilifu na awe na akili na mwili mzuri, wenye nguvu, wenye afya na kufundishwa na Wewe milele.

Tuanze kuomba mapema ila, hata hivyo kama hukuweza kuomba mapema, anza sasa, haijalishi mtoto wako ana umri gani, maombi yako yatafanya tofauti nzuri, na ya kudumu.

***Maombi***

*Bwana,* ninaomba kwamba-------- (jina la mtoto) awe na heshima kubwa kwa ajili yako na njia zako. Na afiche Neno Lako moyoni mwake kama hazina, na atafute ufahamu kama fedha au dhahabu. Mpe akili nzuri, roho inayofundishika, na uwezo wa kujifunza. Ingiza ndani yake hamu ya kupata elimu na ujuzi, na awe na furaha katika mchakato huo. Zaidi ya yote, naomba kwamba afundishwe na Wewe, kwa maana Neno Lako linasema kwamba watoto wetu wanapofundishwa na Wewe wanahakikishiwa amani. Pia umesema, "Kumcha BWANA ni chanzo cha maarifa, bali wapumbavu hudharau hekima na adabu" (Mithali 1:7). Hebu kamwe asiwe mjinga na

akajiepusha na elimu, bali arejee Kwako kwa elimu anayohitaji.

Ninaomba aheshimu hekima ya wazazi wake na awe tayari kufundishwa nao. Na yeye pia awe na hamu ya kufundishwa na walimu Unaowaleta katika maisha yake. Mchague kila mmoja wa walimu hao, na Bwana, wajalie watu hawa wawe wacha Mungu, ambao yeye anaweza kujifunza kwa urahisi kutoka kwao. Mwondoe katika maisha mwalimu yeyote ambaye angekuwa na mvuto wa kutomcha Mungu au kuunda uzoefu mbaya wa kujifunza. Hebu na apate kibali kwa waalimu wake na awe na mawasiliano mazuri nao. Bwana msaidie mtoto huyu kufaulu shuleni na kufanya vyema katika madarasa yote. Fanya njia za kujifunza kuwa nyororo na sio kitu ambacho yeye lazima ahenyeke sana na kuhangaika. Unganisha kila kitu katika ubongo wake (jinsi inavyopaswa Kuwa, ili awe na uwazi wa mawazo, mpangilio, kumbukumbu nzuri, na uwezo mkubwa wa kujifunza.

Ninamwombea yeye kulingana na Neno Lako, "Elekeza moyo wako kwa mafundisho, na masikio yako kwenye Maneno ya maarifa" (Mithali 23:12). “Bwana akupe akili katika mambo yote” (2 Timotheo 2:7). Bwana, amwezeshe kupata furaha ya kujifunza zaidi kuhusu Mwenyezi Mungu na ulimwengu Wako. Katika Jina la Yesu ninaomba. Amen.

**SILAHA ZA VITA**

Watoto wako wote watafundishwa na BWANA, na amani ya watoto wako itakuwa nyingi.

**ISAYA 54:13**

Mwenye hekima atasikia na kuongeza elimu, na mwenye ufahamu atapata shauri la hekima.

**MITHALI 1:5**

Watu Wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa. Kwa kuwa umeyakataa maarifa, Mimi Nami nitakukataa wewe usiwe kuhani Kwangu; kwa kuwa umeisahau sheria ya Mungu wako, Mimi Nami nitawasahau watoto wako.

**HOSEA 4:6**

Mshike sana elimu, usimwache aende zake; mshike, maana yeye ni uzima wako.

**MITHALI 4:13**

Mwanangu, ukiyapokea Maneno Yangu, na kuyaweka akiba maagizo Yangu ndani yako, hata kutega sikio lako kusikia hekima, na kuelekeza moyo wako upate kufahamu; naam, ukiomba ufahamu, na kupaza sauti yako upate ufahamu, ukiutafuta kama fedha, na kuutafuta kama hazina iliyositirika; ndipo utakapofahamu kumcha Bwana, na kupata maarifa ya Mungu.

**MITHALI 2:1-5**

## Sura ya kumi na tano

## KUTAMBUA VIPAWA NA VIPAJI VILIVYOTOLEWA NA MUNGU

Tangu watoto wangu walipozaliwa, nilimwomba Mungu atufunulie vipawa, talanta, na uwezo alioweka ndani yao na kutuonyesha jinsi ya kuwalea na kuwakuza vyema kwa utukufu Wake. Katika umri mdogo sana watoto wetu wote wawili walionyesha dalili za talanta ya muziki, kwa hiyo nilimuuliza Mungu la kufanya kuhusu hilo na nikangojea jibu.

Isaka alipokuwa na umri wa miaka minne, tulihisi kuelekezwa kumpa masomo ya piano. Alionyesha uwezo wa ajabu, lakini baada ya miaka michache hakutaka kufanya mazoezi ya kinanda. Hata hivyo, Mungu alinionyesha wazi kwamba nisingekuwa msimamizi-au wakili mzuri wa talanta Alizompa mwanangu ikiwa ningemwacha aache wakati huo au kujifanyia anavyotaka tu. Kwa hivyo nilibuni motisha ifaayo kwa mtoto wangu wa miaka sita: Ningemlipa senti ishirini na tano kila wakati alipokuwa akifanya mazoezi. Mpango huu wa malipo lazima ulikuwa umeongozwa na Roho Mtakatifu, kwa sababu sikuwahi kusikia malalamiko mengine kuhusu kufanya mazoezi hadi Isaka alipokuwa na umri wa miaka kumi na mbili. Wakati huo nilihisi aache kusoma piano na kuanza kuchukua masomo ya gitaa. Na sijawahi kumwomba afanye mazoezi ya gitaa. Ana motisha mwenyewe na alianza kushika gitaa na kujifunza kiurahisi sana!

Leo Isaka anaimba na vinanda vya umeme, na kucheza besi, na gitaa, lakini anaandika nyimbo na mipango yake yote kwenye piano. Wakufunzi wake wa muziki walisema kwamba anafanya haya vizuri kwa sababu ujuzi wake wa piano ulimpa ufahamu mzuri wa msingi wa muziki, jambo ambalo

linathibitisha tu uongozi wa Mungu katika miaka hiyo yote iliyopita.

Kwa sababu adui anataka kutumia vipawa vya watoto wetu kwa utukufu *wake,* au angalau kuwazuia wasitumike kwa makusudi ya Mungu, tunapaswa kuwafunika katika maombi. Kuombea maendeleo ya karama na vipaji vya watoto wetu walivyopewa na Mungu ni mchakato endelevu.

Kulikuwa na wakati katika maisha ya watoto wangu wote wawili katika umri wa miaka kumi na miwili na kumi na minne, walipovutiwa na muziki wa ulimwengu na mwonekano na tabia zisizokubalika za wasanii fulani maarufu. Walipenda kufuga nywele na kusuka rasta, na kubandika picha za wanamuziki hawa kwenye vyumba vyao. Mume wangu na mimi tulijua kwamba vita vyetu ni dhidi ya adui, na sio watoto wetu, lakini pia tulijua kwamba tulipaswa kukabiliana nao kuhusu jambo hilo na Tulipaswa kuweka sheria kuhusu muziki ambao wangeweza kusikiliza na ni nini kisichokubalika. (Hii haimaanishi kwamba tunadhani watoto wetu hawapaswi kamwe kuwa na uhusiano wowote na muziki wa kilimwengu, maana kuna nyimbo za kitaifa, na mambo mengine kuhusu asili nk. Hebu chochote wanachofanya, "wafanye yote kwa utukufu wa Mungu" [1 Wakorintho 10:31] kwa sababu Mungu amewaita. Tuliomba macho ya watoto wetu yageuzwe mbali na ulimwengu na kuzingatia kile ambacho Mungu alikuwa amewaita kufanya. Nyimbo kama zile za taifa au za kuonyesha mapenzi ya nchi zetu, au kujifunza zipo sawa, Mungu atatuonyesha zipi ni za kumtukuza Shetani, na kuamsha tamaa za mwili na zipi zipo sawa. Uimbaji ulianzia mbinguni, kwa ajili ya kumtukuza Mungu.

Adui amebuni mengi baada ya hapo.

Tuliomba kwamba Mungu *afungue milango* ambayo walipaswa kupitia na *kufunga milango yote* ambayo hawakupaswa kuingia. Tumemwona Bwana akijibu maombi hayo mara nyingi. Kwa mfano, Isaka aliombwa kuwa sehemu ya vikundi mbalimbali vya muziki na kusafiri nao hapa na pale. Hatukuwahi kuhisi kukosa amani kuhusu kuwa na yeyote kati yao na tukaona ni wakati unaofaa kwake. Kisha, alipokuwa na umri wa miaka kumi na minane, alipewa fursa ya kutengeneza, kuandika, kupanga na kucheza piano, besi, na gitaa wakati wa ibada kwa ajili ya rekodi maarufu ya Kikristo. Tulijua hili kwa wazi kuwa lilitoka kwa Bwana na lilikuwa jibu la maombi yetu kuhusu talanta zake kutumika kwa utukufu wa Mungu. Hii haikutufanya tuache maombi yetu katika suala hili. Mimi na mume wangu tunafahamu vizuri biashara ya muziki ilivyo na vishawishi vya maisha ya safarini kuelekea kwenye sehemu ambayo wanaimba, hata kwa wasanii wa Kikristo, kwa hiyo japo ni mtu mzima sasa, sisi tunaendelea kumuombea Isaka kwa uaminifu ili atumie kipaji na maisha yake kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

Je, ni karama na vipaji vipi ambavyo Mungu amewekeza ndani ya mtoto wako? Kila mtoto anavyo vipaji na karama. Japo unaweza kuona au la. Biblia inasema, "Kila mmoja ana karama yake mwenyewe kutoka kwa Mungu, mmoja karama hii na mwingine nyingine" (1 Wakorintho 7:7). Wakati mwingine inahitaji maombi ili kuzifichua hizi karama. Mungu anapokupa mwanga wa uwezo wa mtoto wako kwa utukufu Wake,

wewe mpende na umwombee mtoto huyu awe hivyo. Biblia inasema, “Atasimama mbele ya wafalme; hatasimama mbele ya watu wasiojulikana” (Mithali 22:29). Omba mtoto wako akue na kufanikiwa katika karama na talanta ambazo Mungu amempa yeye, na umjulishe kwamba Bwana ana kusudi muhimu na la kipekee kwa ajili yake katika ulimwengu huu.

Kila mtoto ana karama maalum na vipaji. Nasi tunahitaji kuwaombea wazitambue karama hizi na wafunuliwe, waendelezwe, watunzwe, na watumike kwa utukufu wa Mungu.

### *MAOMBI*

*Bwana,* nakushukuru kwa vipaji na talanta ulizoweka ndani---------- (jina la mtoto). Ninaomba kwamba utazikuza ndani yake na uzitumie kwa utukufu Wako. Zifanye ziwe dhahiri kwangu na kwake, na unionyeshe kabisa, ikiwa kuna malezi yoyote maalum, mafunzo, uzoefu wa kujifunza, au fursa ambazo ninapaswa kumpa yeye. Hebu vipawa na talanta zake ziendelezwe kwa njia Yako na kwa wakati Wako.

Neno Lako linasema, “Basi kwa kuwa tuna karama zilizo mbalimbali, kwa kadiri ya neema tuliyopewa, na tuzitumie” (Warumi 12:6).

Anapotambua hizi talanta na uwezo Ulizompa, ninaomba kwamba hatakuwa na hisia za kutostahili, woga, au kutokuwa na uhakika, hebu asizuiwe kuzitumia kulingana na mapenzi Yako. Naomba asikie wito Ulionao Wewe juu ya maisha yake, ili asitumie maisha yake yote kujaribu kujua ni nini au akose kabisa. Hebu talanta yake isipotee kamwe, isiingiwe

na unyonge, au itumike kutukuza chochote au kumtukuza mtu yeyote isipokuwa Wewe, Bwana.

Ninaomba kwamba umdhihirishie kazi yake ya maisha, tasnia au taaluma yake ni ipi na afanikiwe katika hiyo. Ibariki kazi ya mikono yake, naye aweze kupata riziki nzuri kwa kufanya kazi anayoipenda na kuifanya vizuri, na hivyo kubariki wengine kwa kipato na karama zake pia.

Neno lako linasema kwamba, "Zawadi ya mtu humpatia nafasi, humleta mbele ya wakuu" (Mithali 18:16). Naomba chochote anachofanya kipate kibali kwa wengine na kipokelewe vyema na kuheshimiwa. Lakini zaidi ya yote, naomba vipaji, zawadi na talanta Ulizoweka ndani yake ziachiliwe ili kupata udhihirisho wake kamili katika kukutukuza Wewe.

Katika Jina la Yesu ninaomba. Amen.

**SILAHA ZA VITA**

Kwa maana karama na mwito wa Mungu haubadiliki.

**WARUMI 11:29**

Kila mmoja wetu alipewa neema kwa kadiri ya kipimo cha kipawa Chake Kristo.

**WAEFESO 4:7**

Kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu.

**1 PETRO 4:10**

Kila kutoa kuliko kwema, na kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kwa Baba wa mianga; kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeuka-geuka.

**YAKOBO 1:17**

Namshukuru Mungu wangu sikuzote kwa ajili yenu kwa ajili ya neema ya Mungu mliyopewa kwa njia ya Kristo Yesu, kwa kuwa mmetajirishwa katika kila kitu kwa Maneno yote na ujuzi wote, kama vile ushuhuda wa Kristo ulithibitika kwenu, hata hamkupungukiwa na karama yoyote, mkikutazamia sana kufunuliwa Kwake Bwana wetu Yesu Kristo.

**1 WAKORINTHO 1:4-7**

## Sura ya kumi na sita

## KUJIFUNZA MANENO SAHIHI YA KUZUNGUMZA

Baada ya shule alasiri moja nilimsikia mwanangu akisema maneno kadhaa ya matusi.

“Lugha ya namna hiyo haikubaliki,” nilimwambia. “Kwa nini unatumia maneno hayo, wakati unajua hupaswi kufanya hivyo?” “Watoto shuleni huzungumza hivyo,” akajieleza. "Watu wengine hufanya hivyo, kwa hivyo wewe unafikiri ni sawa kwako pia kutamka matusi haya?" nilimwuliza.

Kisha katika sentensi yangu iliyofuata nilitamka maneno manne ya matusi niliyokuwa nikisema kabla sijakutana na Bwana na kusafishwa na Roho Wake. Kwa sura ya kutisha na mshtuko akasema, “Mama! Mbona unaongea hivyo?”

Nikasema “Kwa sababu watu wengine huzungumza hivyo,” “Je, wewe unajisikiaje ninapozungumza hivyo?” "Inanifanya nijisikie vibaya." “Je, unajua, naweza kuongea matusi hayo muda wowote ninaotaka. Lakini nachagua *kutofanya* hivyo. Kama unasema kuwa maneno hayo yanakufanya ujisikie vibaya maana yanaumiza roho yako. Basi ujue kuwa ukiongea hivyo *unaniumiza roho nami pia.*

Hebu fikiria kile maneno machafu yanavyofanya kwa Roho wa Mungu. Wewe una chaguo la kumhuzunisha Roho wa Mungu kwa maneno unayosema au kumtukuza. Mwenyezi Mungu anakupenda kwa vyovyote vile na mimi pia nitakupenda. Lakini njia moja itakubariki na njia moja itakuumiza.”

Sikumsikia Isaka akitamka maneno kama hayo tena hadi alipokuwa kijana. Kisha tukafanya mazungumzo haya tena. Ninamwomba Mungu kuwa, hata leo ayakumbuke.

Najua njia yangu ya kufundisha inaweza kuonekana ya kushtua. Ilinishtua hata mimi pia, na nikamuomba Mungu anitakase kutokana na uchafu niliokuwa nao kwa kutamka maneno hayo. Lakini maneno hayo hayakutoka moyoni mwangu. Niliyasema tu kama njia ya kuonyesha

uharibifu wa hayo maneno. Sipendekezi utumie mbinu zangu za kufundisha, lakini ukubali uzoefu wangu kama mfano sahihi wa uwezo wa kile tunachozungumza.

Tunajitengenezea ulimwengu kwa kile tunachozungumza. Maneno yana nguvu, na tunaweza kutamka uzima au kifo katika hali fulani. Biblia inasema kwamba mambo tunayosema yanaweza kutuingiza kwenye matatizo au kutuweka *mbali* na matatizo. Yanaweza hata kuokoa maisha yetu. "Alindaye kinywa chake huihifadhi nafsi yake; Bali afunuaye midomo yake atapata uharibifu" (Mithali 13:3).

Tunahitaji kumwomba Mungu aweke ulinzi juu ya vinywa vyetu wenyewe na pia kinywa cha mtoto wetu.

Hotuba isiyo ya kimbingu au isiyo ya Bwana, kama vile, "Mimi sio mzuri," "Laiti ningalikufa," "Maisha ni ya kutisha," "Watu ni wa kutisha," "Sitawahi kuwa kitu chochote cha pekee katika maisha yangu, mimi nitafeli tu," haiakisi moyo uliojaa Roho Mtakatifu. Inaonyesha kazi ya giza na hilo ndilo litakalojitokeza kwenye jukwaa la maisha ya mtoto wako ikiwa hautamsaidia kufuatilia anachosema.

Biblia inasema katika siku ya hukumu, tutalazimika kutoa hesabu kwa kila neno tulilolinena bila kujali au kwa uzembe. Lakini pia tutalipia mambo mengine hapa hapa duniani. Na tunaweza kulipia gharama kubwa ambayo inaweza kudhibitiwa kwa urahisi na mapenzi yetu wenyewe. Tunaweza kutamka upendo, furaha, na amani katika ulimwengu wetu, au tunaweza

kuzungumza ugomvi, chuki, udanganyifu, na maonyesho mengine ya uovu. Ni chaguo letu.

Tunataka watoto wetu wazungumze maisha. Hii haimaanishi kuwa hawawezi kuwa wakweli kuhusu hisia hasi. Lakini maneno hayo yapasa kusemwa kwa kusudi la kuungama, kuelewa, na kujitiisha kwa Mungu kwa ajili ya uponyaji, na si kama zana za uharibifu.

Maneno ya watoto wetu yanapowahusu wao wenyewe, wengine, hali zao, au ulimwengu unaowazunguka, ni lazima tuwatie moyo kuona katika Neno la Mungu yote yanayoweza kusemwa vizuri zaidi tufanye hivyo. Njia bora ya kuboresha usemi ni kuboresha moyo, "kwa maana kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo" (Mathayo 12:34). Tuombe wawe na moyo uliojaa Roho Mtakatifu, Ukweli wa Neno la Mungu, na upendo wa Mungu. Mungu ataleta usemi Wake Mwenyewe, ambao huleta uhai kwa msemaji na vilevile msikilizaji. Hapa ndipo hatua yetu ya maombi inapaswa kuanza.

### ***MAOMBI***

Bwana, ninaomba kwamba------ (jina la mtoto) atachagua kutumia usemi/maneno yanayokutukuza. Ujaze moyo wake Roho wako na Kweli yako ili yale yatokayo kinywani mwake yawe maneno ya uzima na si mauti. Weka chujio mdomoni mwake (Wafilipi 4: 6-8) ili kwamba kila jaribu la kutumia lugha chafu, hasi, katili, yenye kuumiza, isiyojali, isiyo na upendo, au isiyo na huruma limpige roho yake na kumfanya ahisi kukosa amani. Naomba lugha chafu au matusi yawe mageni kwake kiasi kwamba ikiwa

maneno kama hayo yatapita kwenye midomo yake, yatakuwa kama changarawe kinywani mwake na atachukizwa nayo. Msaidie aweze kuchuja maneno haya mwenyewe kwa msaada wa Roho Mtakatifu, na mdomo wake usafishwe na sabuni ya mbinguni.

Mlinde asinaswe na maneno ya kinywa chake. Wewe umeahidi kwamba “Yule alindaye kinywa chake na ulimi wake, atajilinda nafsi yake na taabu” (Mithali 21:23). Msaidie hata mkewe kuweka mlinzi juu ya kinywa chake na kujiweka mbali na dhiki. Neno lako linasema “mauti na uzima huwa katika uwezo wa ulimi, nao waupendao watakula matunda yake”

(Mithali 18:21). Hebu azungumze uzima na sio kifo. Aweze kuwa mwepesi wa kusikiliza na sio mwepesi wa kusema ili maneno yake yawe na neema siku zote. Mpe kujua jinsi ya kunena, nini cha kunena, na wakati wa kuzungumza na mtu yeyote katika hali yoyote. Mwezeshe daima kunena maneno ya matumaini, afya, faraja, na uzima, na kunuia kwamba kinywa chake hakitafanya dhambi. Katika Jina la Yesu ninaomba. Amen.

**SILAHA ZA VITA**

Maneno ya kinywa changu na mawazo ya moyo wangu yapate kibali mbele Zako, Ee BWANA, Mwamba wangu na mwokozi wangu.

**ZABURI 19:14**

Mtu mwema katika hazina njema ya moyo wake hutoa yaliyo mema, na mtu mwovu katika hazina mbovu ya moyo wake hutoa mabaya.

**MATHAYO 12:35**

Lakini nawaambieni, kwa kila neno lisilo maana watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu. Kwa maana kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa.

**MATHAYO 12:36-37**

Maneno ya kupendeza ni kama sega la asali, utamu wa nafsi na afya mifupani.

**MITHALI 16:24**

Kuna asemaye kama kutoboa kwa upanga, lakini ulimi wa wenye hekima huleta afya.

**MITHALI 12:18**

## Sura ya kumi na saba
## MKAO WA KUVUTIWA NA UTAKATIFU NA USAFI

Watoto wanaofundishwa kuishi katika usafi na utakatifu wana nyuso zinazong'aa kwa uwazi na mvuto wa kuhuisha. Biblia inasema, “Hata mtoto hujulikana kwa matendo yake, kwamba analolitenda ni safi na la haki” (Mithali 20:11). Tunataka watoto wetu wajulikane kwa wema wao. Tunataka watoto wetu wawe wa kuvutia kwa wengine kwa sababu ya usafi wao. Hii haitokei kwa bahati tu. Ni lazima ifundishwe kwa watoto

wetu. Na ingawa tunaweza kufanya mengi kuwafundisha watoto wetu kuhusu kuishi kwa utakatifu katika njia za Bwana na kuiga hili kwa uwezo wetu wote, Mwalimu halisi ni Roho Mtakatifu. Utakatifu huanza na upendo Kwake Bwana. "Jilinde mwenyewe kuwa safi" (1 Timotheo 5:22), Biblia inatuagiza. Huu ni mgawo mgumu kwa mtu yeyote, lakini haswa kwa mtoto. Linaweza tu kutimizwa kwa kujitiisha kikamilifu kwa Mungu na sheria Yake na uwezo wa kuwezesha wa Roho Mtakatifu.

Mwanangu alipoanza mwaka wake wa shule ya sekondari, alikuwa katika shule mpya, katika hali tofauti, na katika utamaduni tofauti—Ulikuwa ni wakati mgumu kwa kijana yeyote, bila kujali msingi wake kabla au kama alikuwa mcha Mungu.

Shule aliyosoma ilikuwa ni shule ndogo ya watu binafsi na ya Kikristo, kwa hiyo ndani ya wiki ya kwanza alikuwa amekutana na wanafunzi wote ambao walikuwa wavulana wakubwa. Hata hivyo, mmoja wa vijana hao alitokea kuwa mwanamichezo bora, alifaulu katika masomo yake, na alikuwa amepokea tuzo baada ya tuzo kwa ufaulu bora. Lakini Amosi alikuwa mwenye kuonekana vyema katika nyanja anuwai na muhimu zaidi pia: Maneno yake na matendo yake yalionyesha staha yake ya kina kwa Mungu na sheria Zake.

Siku moja wakati wa chakula cha mchana muda ambao wavulana wote walikuwa pamoja, mmoja wao alitoa utani wa lugha ambayo haikufaa, na kila kila mtu akacheka. Kila mtu, yaani, isipokuwa Amosi. Mwanangu alikiri kwamba alicheka pia. "Nilikuwa mvulana mpya na sikutaka kila mtu

afikiri kwamba nilitoka sayari nyingine," alieleza kwa unyonge alipotuambia kuhusu tukio hili baadaye.

Jambo ambalo Mika alikuja kutambua upesi ni kwamba Amosi hakucheka kwa matani haya yenye lugha chafu. Wala hakuvuta sigara au kunywa pombe au kutumia lugha chafu. Walakini, cha kushangaza, kila mtu alimpenda na kumheshimu.

Siku moja, muda mfupi baada ya mkutano wa wazazi shuleni, nilifika nyumbani na kumwambia Mika kuhusu kijana mzuri niliyekutana naye huko.

"Anaonekana wazi kuwa ni tofauti na wengine," nilimwambia. "Yeye ni mchangamfu na mwenye upendo sana—mvulana mcha Mungu na mcheshi ajabu. Na alinifanya nijisikie nimekaribishwa sana, kana kwamba nimemfahamu siku zote." Nilipoendelea kumuelezea, alitaja jina lake. "Huyo mama, anaitwa Amosi," alisema. "Bila shaka," nilijibu. "lazima Amosi anao wazazi wenye nguvu na mvuto, watu wa kipekee, wanaoamini na wanaosali. Hakuna mtoto anayetokea kuwa hivyo kwa bahati mbaya."

Katika mwaka mzima tulipata nafasi ya kukutana na familia nzima na kuona jinsi kila mwanafamilia hiyo alivyo wa kipekee; na tuliona kwamba watu hawa wema wao haukuzimika.

Kwa nini? Kwa sababu maisha yao hayakuwa jaribio la kisheria kuwa mkamilifu au tu, kule kutaka watu wengine wavutiwe; mambo yao yalifanywa kutoka mioyoni ambamo mlikuwa na heshima kubwa kwa

Mungu na hamu ya kuishi kwa njia Yake— katika utakatifu na usafi.

Hatuonani tena na Amosi au familia yake kwa sababu maisha yetu yamechukua njia tofauti. Lakini hatutawasahau kamwe. Waliinua viwango binafsi vya kwetu, walitupa kulenga kitu cha juu zaidi, na kuturuhusu kuona jinsi utakatifu unavyovutia kwa namna ya ajabu.

Wacha tuwaombee watoto wetu wavutwe kwa utakatifu na usafi kama sumaku, ili kitu chochote ambacho siyo kitakatifu au safi kitakapowavutia, watambue mvuto huo mara moja na kukosa starehe na raha vya kutosha, kiasi kwamba wakatae kabisa. “Kwa maana Mungu hakutuitia uchafu, bali katika utakatifu” (1 Wathesalonike 4:7). Kuishi ndani kabisa ya mipaka ya sheria ya Mungu ni kupata utimilifu ndani ya mtu kamili. Ukamilifu huo ndio maana ya utakatifu. Watoto ambao hawana matamanio ya utakatifu, na kujaribu kutafuta uwezo wa Mungu wa kuwawezesha ili kuwasaidia kuufikia huo utakatifu, hawawezi kamwe kubarikiwa na kukamilishwa.

Amosi alikuwa kielelezo cha Maandiko yasemayo, “Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo, na imani, na usafi” (1 Timotheo 4:12). Hakuna kitu cha kuvutia na kutia moyo zaidi, kuliko watoto wanaotembea katika utakatifu na usafi. Tuwaombee watoto wetu wawe miongoni mwa wanadamu wanaofanya hivyo.

### *MAOMBI*

*Bwana,* ninaomba kwamba ungemjaza----------- (jina la mtoto) na upendo

Kwako, upendo unaozidi kupenda kwake kitu kingine chochote au mtu mwingine yeyote. Msaidie kukuheshimu Wewe na kuheshimu sheria Zako na kuelewa kwamba ziko kwa ajili ya manufaa yake. Hebu na aone waziwazi kwamba sheria Zako zinapokiukwa, maisha hayana mwendelezo mzuri. Ficha Neno Lako ndani ya moyo wake, ili pasiwe na mvuto wa kutenda dhambi. Ninaomba akimbie kutoka kwenye uovu, kutoka kwenye uchafu, kutoka kwa mawazo machafu, maneno, na matendo, na kwamba atavutwa kuelekea vile vilivyo safi na vitakatifu tu. Hebu Kristo aumbwe ndani yake yeye na kubidiishwa kutafuta nguvu za Roho Wako Mtakatifu ili kumwezesha kufanya yaliyo sawa.

Umesema, “Heri wenye moyo safi, maana hao watamwona Mungu” (Mathayo 5:8). Matamanio ya utakatifu yatokayo katika moyo safi yaonekane katika yote anayofanya. Na idhihirike hivyo katika sura yake pia. Ninaomba kwamba mavazi anayovaa na njia anayochagua kuupamba mwili wake itaonyesha heshima na hamu ya kukutukuza Wewe, Bwana.

Pale ambapo yeye anapotoka kutoka kwenye njia ya utakatifu, hebu mlete kwenye toba na ufanye kazi kwa uwezo wako wa kutakasa ndani ya moyo na maisha yake. Mpe kuelewa kwamba kuishi katika usafi huleta ukamilifu na baraka, na kwamba malipo makubwa zaidi kwa hilo ni kuwa karibu na Wewe. Katika Jina la Yesu ninaomba. Amen.

## SILAHA ZA VITA

Ni nani awezaye kupanda katika mlima wa BWANA? Au ni nani awezaye kusimama katika Patakatifu Pake? Yeye aliye na mikono safi na moyo safi, ambaye hakuinua nafsi yake kwa sanamu, wala hakuapa kwa hila. Atapokea baraka kwa Bwana, na haki kwa Mungu wa wokovu wake.

**ZABURI 24:3-5**

Katika nyumba kubwa hakuna vyombo vya dhahabu na fedha tu, bali pia vya mti na udongo, vingine kwa ajili ya heshima na vingine havina heshima. Kwa hiyo ikiwa mtu atajitakasa kutokana na hivyo vya mwisho, atakuwa chombo cha heshima, kilichotakaswa na cha kumfaa Bwana, kilichotayarishwa kwa kila kazi njema.

**2 TIMOTHEO 2:20-21**

Kila tawi ndani yangu lisilozaa huliondoa; na kila tawi lizaalo hulisafisha, ili lizidi kuzaa.

**YOHANA 15:2**

Hapo patakuwa na njia kuu, na njia, nayo itaitwa Barabara kuu ya Utakatifu. Aliye Najisi hatapita juu yake, lakini itakuwa kwa ajili ya wengine. Mtu yeyote aendaye katika njia hii, ajapokuwa mpumbavu, hatapotea; hao waliokombolewa watakwenda huko, na waliokombolewa na Bwana watarejea, watafika Sayuni pamoja. kuimba, na furaha ya milele itakuwa juu ya vichwa vyao.

Watapata furaha na shangwe, huzuni na kuugua vitakimbia.

**ISAYA 35:8-10**

Kuna kizazi kilicho safi machoni pao wenyewe, lakini hakijaoshwa na uchafu wake.

**MITHALI 30:12**

## Sura ya kumi na nane

## KUOMBA KUPITIA CHUMBA CHA MTOTO

Mwanangu alipokuwa na umri wa miaka kumi na moja hivi, ghafla alianza kuota ndoto mbaya bila sababu za msingi. Hakuwa ameona jambo lolote la kuogofya katika sinema au kwenye televisheni, na hakutupa dalili zozote kwamba jambo lolote lisilo la kawaida lilikuwa limempata. Tulisali pamoja naye mara kadhaa, lakini usiku baada ya usiku, ndoto hizo mbaya ziliendelea.

Nilipokuwa nikiomba peke yangu kuhusu jambo hili asubuhi moja, nilimwomba Mungu anionyeshe ni nini kilikuwa kinasababisha ndoto hizi mbaya. Nilipofanya hivyo, nilihisi kuongozwa kwa nguvu kwenda kwenye chumba cha mwanangu.

“Bwana, ikiwa kuna kitu chochote katika chumba cha Isaya ambacho hakipaswi kuwa hapa, nionyeshe,” nilisali. Mara moja, nilihisi kusukumwa kwenda kwenye kompyuta yake na kutazama michezo yake. Mchezo wa kwanza niliochukua ni ule aliokuwa ameazima kwa rafiki yake kanisani. Nje ya sanduku mchezo huo ulionekana usio na madhara kabisa; ulikuwa ni mchezo wa udadisi na furaha tu kwa mvulana (adventure game). Nilifungua sanduku na kuchomoa kijitabu kidogo cha maelekezo. Kurasa chache za

kwanza hazikuonyesha kitu kisicho cha kawaida, lakini katika kurasa za nyuma nilipata aina mbaya zaidi ya takataka za kishetani. Nilishtuka, lakini nikasema, “Asante, Yesu,” kisha nikautoa mchezo huo chumbani mwake.

Ikiwa mchezo ungekuwa mali ya mwanangu, ningeuharibu mara moja. Lakini kwa vile ulikuwa wa mtu mwingine, hivyo, niliwapigia simu wazazi wa mvulana huyo na kuwaambia nilichopata.

Walishangaa, kwani hawakujua kama sisi. Isaya aliporudi nyumbani kutoka shuleni, nilimwonyesha nilichokuwa nimegundua. Alisema bado hajafika mbali kwenye mchezo huo, yaani pale penye kurasa hizi ambazo niliziona, na hivyo hatambui kile kilichomo ndani yake. Hakusita Kurudisha mchezo huu kule alikouazima. Hakika michezo mingi siku hizi ni ya kuiangalia vizuri.

Mume wangu aliporudi nyumbani, tulipaka mafuta chumba cha mwana wetu na kusali kikamilifu. Tulijua Biblia ilisema, “Nira itaharibiwa kwa sababu ya mafuta yaliyotiwa humo” (Isaya 10:27). Na ingawa mifano mingi ya kibiblia ya kuhusu fungu hili ni ya watu kupakwa mafuta, bado kuna mifano ya majengo au vyumba vilivyotiwa mafuta ili kutakaswa. “Nawe twaa mafuta ya kutiwa, na kuipaka hiyo maskani, na vitu vyote vilivyomo; nawe utaitakasa pamoja na vyombo vyake vyote, nalo litakuwa takatifu” (Kutoka 40:9). Kwa sababu tulitaka kuvunja nira yoyote ya adui na kutakasa chumba cha mtoto wetu kutoka kwa kitu chochote kisicho kitakatifu, tulitia mafuta miimo ya mlango na kusali juu ya chumba chake, tukimkaribisha Roho Mtakatifu kukaa humo na

kufungia nje chochote ambacho si cha Mungu.

Uthibitisho kwetu kwamba tulifanya jambo lililo sawa ni kwamba ndoto mbaya za Isaya zilikoma mara moja— ghafla kama zilivyotokezea ghafla.

Nyumba ya kila mtu inahitaji usafishaji wa kiroho mara kwa mara, hasa katika vyumba ambavyo watoto wetu hulala na kucheza. Biblia inasema tukileta kitu cha kuchukiza katika nyumba zetu, tunaleta uharibifu pamoja nacho. Usafishaji mtakatifu wa nyumba unapaswa kufanywa mara kwa mara kama suala la kanuni, lakini kwa hakika wakati wowote unapohisi shida na kitu katika mtoto wako. Ikiwa anakuwa na hofu, uasi, hasira, huzuni, akili kutanga, mshangao, tatizo la kinidhamu, au kuwa na ndoto mbaya za jinamizi au mazimwi, wakati mwingine. Kuomba tu chumbani mwake kunaweza kubadilisha mambo haraka. Kuimba nyimbo za Kikristo, tenzi, na kwaya za kuabudu katika chumba pia kunasaidia sana, na nimeona badiliko la roho kwa watoto wangu baada ya kufanya hivyo.

Namjua mama na baba mmoja ambao walipigana na ngome kubwa ya adui wa vileo, dawa za kulevya, uasi, na ushirikina- uchawi ndani ya mtoto wao wa miaka kumi na sita kwa kutumia nyimbo za ibada za Kikristo na Neno la Mungu, chumbani mwake alipokuwa shuleni. Waliomba kwa nguvu kila siku pia. Uasi wake ulivunjwa hatimaye, na akawa mtu wa amani na mcha Mungu.

Unaposali kupitia chumba cha mtoto wako, ondoa chochote kisichomtukuza Mungu: mabango, vitabu, magazeti, wanasesere/toys,

sanamu, picha, michezo, au makala za nguo zinazoonyesha matumizi ya dawa za kulevya au kileo, maisha yasiyo ya mbingu, au aina yoyote ya kufuru. Bila shaka Neno la Mungu juu ya hili lapaswa kufafanuliwa kwa upendo kwa mtoto na, ikiwezekana, apaswa kutiwa moyo aondoe makala zenye kuudhi yeye mwenyewe. Eleza kwamba kwa ajili ya amani na baraka zake ni lazima asafishe kitu chochote ambacho si cha Bwana. Kisha omba juu ya chumba vizuri. Nimeona mabadiliko ya kimiujiza kama matokeo ya kufanya hivyo.

Hii sio ibada ndogo ya ushirikina. Haya ni madai yenye nguvu ya nyumba yako, mtoto wako, na nyanja zote za maisha yake kwa Mungu. Simama na kutangaza, “Mimi na nyumba yangu tutamtumikia BWANA” (Yoshua 24:15). Ahadi hii inasema, "Nyumba yangu imetakaswa na kutengwa kwa utukufu wa Mungu."

Hebu tuanze kusafisha nyumba zetu za kiroho kwa kusali kupitia vyumba vya watoto wetu hata *kabla* haja haijatokea.

### *MAOMBI*

*Bwana,* ninamwalika Roho Wako Mtakatifu akae katika chumba hiki, ambacho ni cha ------------(jina la mtoto). Wewe ni Bwana juu ya mbingu na dunia, na ninatangaza kwamba Wewe ni Bwana juu ya chumba hiki pia. Hebu kifurike kwa nuru na uzima Wako. Ondoa giza lolote linalotaka kujiweka hapa, na usiruhusu roho za woga, huzuni, hasira, shaka, wasiwasi, uasi, au chuki zisipate mahali pa kupandikiza miguu yake

popote (taja chochote ambacho umeona kikidhihirishwa katika tabia ya mtoto wako). Ninaomba kwamba hakuna kitakachoingia kwenye chumba hiki ambacho hakijaidhinishwa na Wewe, Bwana. Kitu chochote hapa ambacho hakipaswi kuwepo hapa, naomba unionyeshe ili kitupwe nje.

Weka ulinzi wako kamili juu ya chumba hiki ili uovu usiingie hapa kwa njia yoyote. Jaza chumba hiki kwa upendo Wako, amani, na furaha. Ninaomba kwamba mtoto wangu aseme kama Daudi, "Nitatembea ndani ya nyumba yangu kwa moyo mkamilifu. Sitaweka mbele ya macho yangu neno baya" (Zaburi 101:2-3). Ninaomba ya kwamba Wewe, Bwana, utapafanya mahali hapa kuwa Patakatifu, palipotakaswa kwa ajili ya utukufu Wako. Katika Jina la Yesu ninaomba. **Amen**

## SILAHA ZA VITA

Wala usilete chukizo ndani ya nyumba yako, usije ukaangamizwa kama hilo.

**KUMBUKUMBU LA TORATI 7:26**

Jiosheni, jitakaseni; ondoeni uovu wa matendo yenu usiwe mbele ya macho Yangu. Acha kutenda maovu.

**ISAYA 1:16**

Basi, wapenzi wangu, kwa kuwa tuna ahadi hizo, na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu.

**2 WAKORINTHO 7:1**

Ee Mungu, unirehemu, sawasawa na fadhili Zako; sawasawa na wingi wa rehema Zako, uyafute makosa yangu. Unioshe kabisa na uovu wangu, na unitakase na dhambi yangu.

**ZABURI 51:1-2**

Laana ya BWANA i juu ya nyumba ya waovu, bali huibariki nyumba ya mwenye haki.

**MITHALI 3:33**

## Sura ya kumi na tisa

## KUFURAHIA UHURU KUTOKA KWA HOFU

Hofu ilikuwa mtindo wa maisha yangu nilipokuwa mtoto kwa sababu niliishi na mama ambaye alikuwa mgonjwa sana wa akili. Tabia yake ya ajabu, isiyo ya kawaida, na ya matusi ilikuwa chanzo cha hofu kila wakati. Wakati, nikiwa mtu mzima, nilipomjua Bwana, nilijifunza kutambua chanzo cha kweli cha hofu na vita dhidi yake. Nimetumia mbinu sawa kwa niaba ya watoto wangu.

Tuliishi katika mji ambao kulikuwa na mioto inayotokea mara kwa mara, ujangili, mafuriko, ghasia, na uhalifu mwingine mwingi. Hofu ingeweza kudhibiti maisha yetu ikiwa tungeiruhusu. Kwa hakika, tulijikuta tukiomba juu ya woga na ulinzi mara kwa mara kiasi kwamba ombi hili likawa sehemu ya kila sala. Kila nilipoona woga ukianza kumnyemelea mmoja wa

watoto wangu, tulikuwa tukisali, kusoma Biblia, kuimba nyimbo na pambio za ibada, na kuweka muziki wa Kikristo. Tangu tulipohama mbali na eneo hilo hatuhitaji kushughulika na aina hiyo ya woga kila siku tena, lakini masomo tuliyojifunza kuhusu upendo mkamilifu wa Mungu, unaotoa woga wote, yamewekwa ndani ya moyo wa kila mmoja wetu milele.

Hofu inaweza kuja juu yetu wakati hatuamini kwamba Mungu anaweza kutuweka salama, au kushugulikia yote ambayo sisi binafsi tunajali. Hofu huwapata watoto kwa urahisi kwa sababu hawawezi kutambua kila wakati ni nini kile kilicho halisi na nini sio halisi. Faraja, uhakikisho, na upendo wetu unaweza *kuwasaidia* wao; lakini kuomba, kunena Neno la Mungu kwa imani, na kumsifu Mungu kwa ajili ya upendo na nguvu Zake, kutawaweka *huru.*

Yesu alipokuwa baharini pamoja na wanafunzi Wake na dhoruba ikatokea, alijibu hofu yao kwa kusema, “Mbona mmekuwa waoga, enyi wa imani haba? (Mathayo 8:26). Yeye anatutaka sisi, kama wao, tuamini kwamba mashua yetu haitazama ikiwa Yeye Yuko pamoja nasi.

Hata hivyo, kuna nyakati ambapo hofu inakuwa zaidi ya hisia za mpito au kupitiliza, hasa pale inapoweza kushika moyo wa mtoto kwa nguvu kiasi kwamba hakuna matendo au maneno yanayoweza kuondoa mambo hayo. Jambo hilo linapotokea, mtoto huwa anasumbuliwa na roho ya woga.

Na Biblia inatuambia waziwazi roho ya woga haitoki kwa Mungu. Inatoka kwa adui wa roho zetu.

Wazazi wana mamlaka na uwezo kupitia Yesu Kristo kupinga roho hiyo ya woga kwa niaba ya mtoto wao. *Hofu* haina nguvu juu *yao. Sisi wanadamu tuna* uwezo juu *ya hofu na woga.* Yesu alitupa mamlaka juu ya nguvu *zote* za adui (Luka 10:19).

Usidanganywe kufikiria vinginevyo. Ikiwa hofu itaendelea baada ya kusali, waombe waumini wawili au zaidi wasali pamoja nawe. Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina la Bwana, Yeye Yuko katikati yao (Mathayo 18:20). Hofu na uwepo wa Bwana haviwezi kukaa mahali pamoja.

Kwa sababu tuna Yesu, sisi na watoto wetu kamwe hatuhitaji kuishi na/au kukubali woga kama njia au mtindo wa maisha yetu.

### ***MAOMBI***

*Bwana,* Neno Lako linasema, "Nalimtafuta BWANA, akanijibu, akaniokoa na hofu zangu zote" (Zaburi 34:4). Ninakutafuta Wewe leo, nikiamini kwamba unanisikia, na ninakuomba umwokoe----------- (jina la mtoto) kutoka kwa hofu yoyote ambayo inatishia kumpata. Ulisema "hujatupa roho

ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi" (2 Timotheo 1:7). Mfurikie mtoto huyu kwa upendo Wako na umwondolee hofu na shaka zote. Mpe hisia ya uwepo wa upendo Wako ambayo hupita kwa mbali, hofu yoyote ambayo ingetishia kumpata yeye. Msaidie yeye, kutegemea nguvu Zako kwa namna ambayo itaweka imani yenye nguvu na imani Kwako Wewe Bwana. Mpe akili timamu kiasi kwamba, ataweza kutambua

ushahidi wowote wa uongo Shetani anaoutoa kwake yeye na kuubainisha kuwa hauna msingi wowote katika ile Kweli.

Popote palipo na hatari ya kweli au sababu nzuri ya kuogopa, mpe hekima, umlinde, na umsogeze karibu na Wewe. Msaidie asizikane hofu zake na azilete Kwako kwa maombi, Nawe umtafutie ufumbuzi. Ninaomba kwamba pale ambapo yeye anakaribia karibu na Wewe, upendo Wako utapenya maisha yake na kuzima hofu yote. Panda Neno Lako ndani ya moyo wake. Hebu imani ipeleke ndani mizizi yake katika akili na roho anapokua katika Neno Lako. Asante, Bwana, kwa ahadi Yako ya kutuokoa kutoka kwa hofu zetu zote. Ninaomba uhuru kutoka kwa hofu zote isipokuwa hofu ya Mungu, kwa niaba ya mtoto wangu siku hii. Katika Jina la Yesu ninaomba. Amen.

## SILAHA ZA VITA

Ee Bwana, jinsi wema Wako ulivyo mkuu, uliowawekea wakuchao, Uliowaandalia wakutumainio mbele ya wana wa wanadamu!

**ZABURI 31:19**

Usiogope, kwa maana Mimi Nipo pamoja nawe; usifadhaike, kwa maana Mimi ni Mungu wako. Nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki Yangu.

**ISAYA 41:10**

Bwana Atakufunika kwa manyoya yake, na chini ya mbawa zake utakimbilia; Ukweli Wake utakuwa ngao na kigao chako. Hutaogopa hofu ya usiku,

wala mshale urukao mchana, wala tauni ipitayo gizani, wala uele uharibuo adhuhuri.

**ZABURI 91:4-6**

BWANA ni nuru yangu na wokovu wangu; nitamwogopa nani? BWANA ni ngome ya uzima wangu; nitamhofu nani?

**ZABURI 27:1**

Uchungu wa mauti ulinizunguka, mafuriko ya uovu yalinitia hofu. Kamba za kuzimu zilinizunguka; mitego ya mauti ilinikabili. Katika shida yangu nilimwita BWANA, nikamlilia Mungu wangu; Aliisikia sauti yangu kutoka hekaluni Mwake, na kilio changu kikafika mbele Zake, hata masikioni Mwake.

**ZABURI 18:4-6**

Hakuna hofu katika upendo; lakini upendo kamili huitupa nje hofu, kwa sababu hofu ina mateso. Lakini mwenye hofu hajakamilishwa katika upendo.

**1 YOHANA 4:18**

## Sura ya ishirini

## KUPOKEA AKILI TIMAMU

Ulimwengu na Shetani kwa pamoja hufanya kila juhudi kudhibiti akili ya mtoto wako. Habari njema ni kwamba wewe una mamlaka ya kupinga

jitihada hizo. Ikiwa mtoto wako ni mdogo, una mamlaka juu ya mambo anayotia akilini mwake—televisheni, sinema, simu, na video anazotazama, programu za redio na kanda anazosikiliza, vitabu na magazeti anayosoma, na vifaa vyote vya kielektroniki vilivyo katika milki yake. Unaweza pia kufanya mengi kumsaidia mtoto wako ajaze akili yake muziki, maneno, na picha za mbingu. Lakini muhimu zaidi, ni kuwa, wewe una nguvu kupitia sala. Kwa hiyo, hata ikiwa mtoto wako havutiwi na mambo haya kila siku, wewe unaweza kusali ili akili yake iwe timamu, ilindwe, na iwe huru.

Mojawapo ya mambo mengi ya ajabu kuhusu kumpokea Yesu na kujazwa na Roho Mtakatifu ni kwamba pamoja na kila baraka nyingine, sisi wanadamu tunapata uthabiti na utimamu wa akili ambao hauwezi kupatikana kwa njia nyingine yoyote. Hiyo ni kwa sababu tumepewa nia ya Kristo. Biblia inasema, "Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu" (Wafilipi 2:5). Tunaweza kupinga mawazo ya kidunia na kuruhusu akili Mapenzi na nia ya Bwana itawale maisha yetu, na tunaweza kuendelea kufanya upya nia zetu kwa kuteka kila wazo.

Mama yangu aliugua ugonjwa wa akili kuanzia miaka yake ya ishirini hadi alipofariki akiwa na umri wa miaka sitini na saba. Nilijionea mwenyewe jinsi ilivyokuwa kwa mtu kuishi katika ulimwengu wa kufikirika/fantasia na hivyo kutoweza kudhibiti mawazo yaliyomjia akilini. Ilikuwa ni uzoefu wa kutisha. Mara nilipokuja kumjua Bwana, niliomba mara kwa mara kwamba watoto wangu, wala mimi tusirithi hali hiyo ya kuyumba kiakili. Kila

nilipohisi wasiwasi nilisema, “Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi” (2 Timotheo 1:7).

“Mungu amenipa akili timamu,” niliyatamka na kuyarudia moyoni maneno haya, mara nyingi.

"Pia amempa mwanangu akili timamu na binti yangu kuwa na akili timamu. Sitakubali chochote pungufu ya hapo.”

Ugonjwa wa akili sio lazima uenezwe kutoka kizazi kimoja hadi kingine, na ukosefu wa msawaziko wa akili sio mapenzi ya Mungu kwa watoto wetu. Wala hatuapaswi kuwa na mawazo ya kuchanganyikiwa yasiyo na utulivu.

Sehemu kubwa ya kuwa na *akili timamu* inahusiana na kile kinachoingia ndani yake, tukiingiza uchafu mawazoni, uchafu utatoka nje (garbage in, garbage out). Kujaza akili zetu na kile kilicho huko nje ulimwenguni, huleta mkanganyiko. Kujaza akili zetu na mambo ya Mungu—hasa Neno Lake—huleta uwazi wa mawazo na amani ya akili. Biblia inasema, “Mungu si mwanzilishi wa machafuko, bali wa amani” (1 Wakorintho 14:33). Ni lazima tufanye kila tuwezavyo ili kuhakikisha watoto wetu wana Neno la Mungu akilini mwao ili kuzuia kuchanganyikiwa na kuhakikisha wana akili timamu.

Mungu ametupa *akili timamu.* Kwa nini basi sisi tukubali pungufu ya hapo kwa watoto wetu? Mwombe Mungu kwa ajili ya mtoto.

## *MAOMBI*

*Bwana,* asante kwa kutuahidi kuwa na akili timamu. Ninadai ahadi hiyo kwa ------------ (jina la mtoto). Ninaomba kwamba akili yake iwe safi, macho, angavu, akili, utulivu, amani, na isiyo na vitu vingi. Ninaomba kusiwe na kuchanganyikiwa, kusiwe na ubutu, na kutokuwa na msawaziko wa mawazo, akili kutokuwa na mpangilio, au kufikiri mambo hasi. Ninaomba kwamba akili yake isijazwe na mawazo tata au ya kutatanisha. Bali, mpe uwazi wa akili ili awe na uwezo wa kufikiri sawasawa wakati wote. Mpe uwezo wa kufanya maamuzi wazi, kuelewa yote anayohitaji kujua, na kuwa na uwezo wa kuzingatia kile anachohitaji kufanya. Pale ambapo sasa kuna kuyumba kwa akili, kuharibikiwa, au kutofanya kazi vizuri, ninazungumza uponyaji katika Jina la Yesu. Na afanywe upya katika roho na nia yake (Waefeso 4:23) na kuwa na nia ya Kristo (1 Wakorintho 2:16).

Ninaomba kwamba atampenda sana Bwana kwa moyo wake wote, nafsi yake, na akili zake zote hivi kwamba kutakuwa hakuna nafasi ndani yake kwa ajili ya uwongo wa adui au kelele za ulimwengu. Neno la Mungu na litie mizizi ndani ya moyo wake na kuijaza akili yake mambo ya Kweli, ya adhama, ya haki, safi, ya kupendeza, ya adili na yenye sifa njema. (Wafilipi 4:8). Mpe ufahamu kwamba kinachoingia katika akili yake kinakuwa sehemu yake, ili apime kwa uangalifu kile anachokiona na kusikia.

Umesema katika ahadi yako kuwa, "Wewe, utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea katika amani kamilifu, kwa sababu anakutumaini Wewe" (Isaya 26:3).

Ninaomba kwamba imani yake Kwako na Neno Lako ikue kila siku ili yeye aishi milele kwa amani na utimamu wa akili. Katika Jina tukufu la Yesu ninaomba. Amen.

**SILAHA ZA VITA**

Wala msiifuatishe namna ya dunia hii, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.

**WARUMI 12:2**

Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu; na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu.

**WAFILIPI 4:6-7**

Maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome, tukiangusha mabishano na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu, tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo.

**2 WAKORINTHO 10:4-5**

Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti, bali nia ya roho ni uzima na amani.

**WARUMI 8:6**

Basi, nasema haya, tena nashuhudia katika Bwana, msienende tena kama watu wa mataifa mengine waenendavyo, katika ubatili wa nia zao, akili zao

zimetiwa giza, wametengwa na uzima wa Mungu, kwa sababu ya ujinga uliomo ndani yao, kwa sababu ya upofu wa mioyo yao.

**WAEFESO 4:17-18**

## Sura ya ishirini na moja
## KUALIKA FURAHA YA BWANA

Msichana mdogo alinijia akiwa na macho ya huzuni sana, uso uliokunjamana, na wenye huzuni na msongo. Saa moja iliyofuata, alinishirikisha uchungu wa maisha yake, akilia huku akiongea. Alikuwa akihisi karibu kila hisia hasi inayoweza kuwaziwa na mwanadamu, ikiwemo mawazo ya kujiua. Nilisali pamoja naye kuhusu kila jambo lililonihangaisha kisha nikamwomba Mungu ampe “uzuri badala ya majivu, mafuta ya furaha badala ya maombolezo, vazi la sifa badala ya roho nzito” (Isaya 61:3)

Tulipomaliza nilishangazwa na tofauti ya uso wake. Usemi usio na furaha na wa kuteswa ulikuwa umebadilishwa na uzuri wa mng'ao na utulivu. Roho ya furaha ilikuwa tayari imeanza kuota mizizi, na alionekana kuwa mtu tofauti. Tangu wakati huo nimeona msichana huyu akichanua katika kujiamini na uzuri kiasi kwamba anavutia kila mtu karibu naye. Kwa kusikitisha, vijana wengi leo wanavunjika moyo. Na mbaya zaidi ni kwamba wanaibeba hadi utu uzima. Huja na kupita, kuathiri maisha yao, kuathiri kazi yao, kuvuruga uhusiano wao,

kuharibu afya zao, na hata kuathiri jinsi wanavyomwona Mungu.

Hii si lazima kutokea. Haijalishi ni aina gani ya uzoefu ambao mtu amekuwa nao, hakuna haja ya kuishi na unyogovu au hisia nyingine yoyote mbaya. Usiruhusu mtoto wako abaki na utu wa huzuni, mfadhaiko, hasira, mhemko, au utu mgumu. Omba kuondokana na hali hiyo.

Ni rahisi kujua ni watu gani wamebeba hisia hasi ndani na ni nani walio na roho ya furaha. Ni dhahiri hasa kwa watoto, kwa sababu hawana uwezo wa kuficha hisia zao kama watu wazima. Mtazame mtoto wako kwa muda mrefu. Je, usemi wa kawaida kwenye uso wake ni wa amani, furaha, na shangwe? Au ni dhiki, kufadhaika, kutoridhika, hasira, kuvunjika moyo, au huzuni? Je! mtoto wako huwa na mtazamo mbaya kwa kile kinachoonekana kuwa hakuna sababu yoyote? Je, mtoto wako amewahi kuonekana amevunjika moyo au mwenye hasira na bado hawezi kueleza kwa nini?

Jihadharini na hali hiyo kabla haijawa mazoea. Hisia hasi hujenga mazoea ikiwa hatutazizuia kwa kuwaombea watoto wetu wapitiwe na roho ya furaha.

Usifikiri hata kidogo kwamba kwa kuomba furaha ya Bwana ili kumjaza mtoto wako unatengeneza mtu duni asiye na huruma kwa mateso ya wengine. Hii haitatokea kamwe. Furaha ya Bwana ni tajiri na ya kina na husababisha mtu yeyote atembeaye ndani yake kuwa vivyo hivyo. Hiyo ni kwa sababu furaha haina uhusiano wowote na hali ya msisimko; inahusiana na kutazama uso wa Mungu na kujua Yeye Ndiye yote tunayoweza kuhitaji.

Sisemi kwamba mtoto wako hapaswi kamwe kuwa na hisia hasi au kuonyesha maumivu ya kihisia. Ninasema kwamba hisia hasi hazipaswi kuwa mtindo wa maisha. Ninasema kwamba tunapaswa kumwangalia Bwana kwa sababu "Alitoa watu Wake kwa furaha (Zaburi 105:43). Atawalea watoto wetu vivyo hivyo tukimwomba.

### ***MAOMBI***

*Bwana,* naomba kwamba …………………… (jina la mtoto) apewe zawadi ya furaha na shangwe. Hebu roho ya furaha iinuke moyoni mwake siku hii na yeye ajue utimilifu wa furaha ambayo hupatikana tu mbele yako. Msaidie ………………. kuelewa kwamba furaha ya kweli hupatikana kwako tu.

Kila anapopitiwa na hisia hasi, mzunguke ………. kwa upendo Wako. Mfundishe kusema, "Hii ndiyo siku ambayo BWANA ameifanya; tutashangilia na kuifurahia" (Zaburi 118:24). Mwokoe ………… kutokana na kukata tamaa, mfadhaiko, upweke, kuvunjika moyo, hasira, au kukataliwa. Mtazamo huu mbaya usiwe na nafasi katika maisha ya ……….. (jina la mtoto), wala usiwe sehemu ya kudumu ya maisha yake. Na aamue moyoni mwake, "Nafsi yangu itashangilia katika BWANA; itaufurahia wokovu Wake" (Zaburi 35:9).

Ninajua, Bwana, kwamba hisia zozote mbaya anazohisi mtoto huyu ni uongo, kinyume na ukweli wa Neno Lako. Panda Neno lako kwa uthabiti ndani ya moyo wake na umzidishie imani kila siku. Mwezeshe

kukaa katika upendo wako na kupata nguvu kutoka kwa furaha ya Bwana leo na hata milele. Katika Jina la Yesu ninaomba. Amen.

**SILAHA ZA VITA**

Mkizishika amri Zangu, mtakaa katika pendo Langu, kama Mimi nilivyozishika amri za Baba Yangu na kukaa katika pendo Lake. Hayo nimewaambia, ili furaha Yangu ikae ndani yenu, na furaha yenu ikamilike.

**YOHANA 15:10-11**

Utanionyesha njia ya uzima; mbele za uso Wako ziko furaha tele; mkono Wako wa kuume ziko raha za milele.

**ZABURI 16:11**

Basi Mungu wa tumaini na awajaze ninyi furaha yote na amani katika kuamini, mpate kuzidi sana kuwa na tumaini katika nguvu za Roho Mtakatifu.

**WARUMI 15:13**

Hasira Yake ni ya kitambo tu, Neema Yake ni ya uzima; Huenda machozi yakadumu kwa usiku mmoja, lakini asubuhi huja furaha.

**ZABURI 30:5**

Nitafurahi sana katika BWANA, nafsi yangu itashangilia katika Mungu wangu; kwa maana amenivika mavazi ya wokovu, amenifunika vazi la haki, kama bwana arusi ajipambavyo kwa mapambo, na kama bibi arusi

ajipambavyo kwa vyombo vyake.

**ISAYA 61:10**

## URITHI

Sote tunajua tunaweza kurithi macho ya mama yetu, pua ya baba yetu, au rangi ya nywele za bibi yetu. Lakini je, unajua kwamba tunaweza pia kuchukua sifa za tabia kutoka kwa wazazi wetu, kama vile hasira mbaya, tabia ya kusema uwongo, kuvunjika moyo, kujisikitikia, kijicho, kutosamehe, kutaka ukamilifu, na kiburi? Tabia hizi na nyinginezo ambazo zina mzizi wa kiroho zinaweza kupitishwa kutoka kwa wazazi wetu hadi kwetu, na kutoka kwetu hadi kwa watoto wetu. Katika familia fulani huenda kukawa na mwelekeo kuelekea mambo kama vile talaka, ukosefu wa uaminifu, ulevi, uraibu, kujiua, au kuvunjika moyo nayote ambayo yanakubaliwa kimakosa kuwa "jinsi nilivyo."

Biblia inazungumza kuhusu mvuto ambao wazazi wetu wanaweza kuwa nao juu yetu. Inasema Mungu atawapatiliza wana maovu ya baba zao hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao" (Kutoka 20:5). Maandiko haya yanarejelea watu ambao hawatembei katika uhusiano wa upendo na Mungu. Hata hivyo, mzazi ambaye ni mwamini na anayempenda Mungu bado anaweza kuchagua kutenda dhambi. Na

dhambi yake itaathiri sana watoto wake.

Biblia inasema, “Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; mambo ya kale yamepita; tazama, yote yamekuwa mpya” (2 Wakorintho 5:17).

Hiyo haimaanishi kwamba tunapompokea Yesu tunakuwa wakamilifu ghafla na hatuna uwezo wa kutenda dhambi. Inamaanisha kuwa tumewekwa huru kutokana na matokeo ya dhambi, ambayo ni kifo, na tumepewa uwezo wa kuipinga. Lakini ni lazima tufanye maamuzi kila siku kuhusu kama tutaishi katika uhuru na uwezo huo au la.

Biblia pia inasema, “Kwa hiyo simameni imara katika uhuru ambao Kristo alitupatia, wala msinaswe tena katika nira ya utumwa” (Wagalatia 5:1). Ikiwa haiwezekani kama muumini kunaswa tena na kongwa la utumwa, kwa nini Biblia inatuonya kuhusu hilo? Jibu ni kwamba, ingawa Yesu alituweka huru kutokana na dhambi bado tunaweza kufanya maamuzi ambayo yanaturudisha katika utumwa wake.

Jambo ni kwamba, wakati mwingine tunakubali mielekeo fulani, kuifuatilia dhambi ndani yetu, na sio lazima. Wakati mwingine tunaendeleza mila ya familia ambayo hatupaswi kufanya na inaathiri watoto wetu. Tofauti na tabia za kimwili, mielekeo kuelekea dhambi ni jambo ambalo hatuhitaji kupokea kama urithi kutoka kwa wazazi wetu. Hiyo ni kwa sababu mielekeo hii si chochote zaidi ya kukubali bila shaka uwongo uliokita mizizi wa adui. Bwana Anatutaka tuamini kwamba sisi si kiumbe kipya

katika Kristo na kwamba hatujawekwa huru kutoka kwa asili yetu ya kale.

Yeye Anataka tufikiri kwamba kwa sababu Baba au Babu alikunywa pombe kupita kiasi, au alikuwa mlalamikaji, au alidanganya mke wake, au alinyanyasa familia yake kwa hasira yake, au waliachana, au hakuwa mwaminifu katika shughuli zake za biashara, hivyo ndivyo mambo yanavyofanyika katika familia yetu. Lakini tunaweza kuchagua kuachana na tabia hizi za zamani za kifamilia kupitia maombi na nguvu za Roho Mtakatifu. Na tunapoona mambo tusiyoyapenda katika tabia zetu yakijionyesha kwa watoto wetu, tunaweza kuwaombea waachwe huru na mwelekeo huo pia. Yeye anaweza kuondoa kabisa laana za mababu/ukoo.

"Ikiwa Mungu kwa rehema Zake ametuokoa, na Roho Mtakatifu ametuosha na kutufanya upya, na tunahesabiwa haki kwa neema, basi kwa nini bado ninapambana na dhambi?" Nilimuuliza mshauri wangu wa Kikristo miaka mingi iliyopita.

"Ni kwa sababu dhambi hiyo aidha haijaungamwa, au unachagua kuendelea kuifanya," alijibu.

"Lakini bado nina kutosamehe kwa wanafamilia mbalimbali kwa mambo ambayo yametokea huko nyuma," nilisema. “Nimekiri tena. Sitaki kuifanya. Kwa nini siwezi kupita hapa?”

"Mama yako alikuwa mtu asiyesamehe, sivyo?" alisema. “Sana sana. Alikuwa na kutosamehe kwa karibu kila mwanafamilia. Ndio maana alijitenga na wengi wao. Alikuwa na marafiki wachache kwa sababu

hiyo hiyo—aliwasukuma mbali watu na kutosamehe kwa makosa madogo sana.”

“Je, umewahi kufikiria uwezekano kwamba ungeweza kupata mwelekeo huo wa kutosamehe katika utu wako? Watoto huchukua kile wazazi wao walivyo,” alipendekeza.

Sikuwahi kufikiria juu ya uwezekano wa kuwa na kitu chochote nje ya akili yangu ambacho kilikuwa kikinisukuma kukaa katika hali ya kutosamehe, lakini kadiri nilivyofikiria juu yake, ndivyo nilivyokumbuka kuona tabia hiyo ikidhihirika kwa uzito katika wanafamilia wengine pia. Karibu kila familia inapaswa kukabiliana na hilo wakati fulani, lakini wengi huvuka bila kuruhusu kusababisha uvunjaji mkubwa katika mahusiano ya familia.

"Ninajua hii hainiondolei jukumu langu la kusamehe, lakini naona mwendelezo wa tabia hii katika familia yangu," nilisema. "Na kinachonitisha zaidi ni kwamba watoto ninawaona sasa wanashikilia kutosameheana kwa mambo ambayo yametokea. Ingevunja moyo wangu kufikiria kwamba baada ya wao kukua na kuondoka nyumbani kwetu, au baada ya mimi na mume wangu kulala mauti, hawangekuwa na uhusiano wowote na mtu mwingine. Ninaona kwamba lazima nijiondoe kwa mada hii kwanza mimi mwenyewe.

Mimi na mshauri tuliomba siku hiyo kwamba dhambi ya kutosamehe katika familia yangu isipitishwe kutoka kizazi hadi kizazi, bali ikomeshwe kwa

uwezo wa Roho Mtakatifu. Nilitangaza Ukweli wa Neno la Mungu, linalosema mimi ni kiumbe kipya katika Kristo na si lazima niishi kulingana na tabia na dhambi za zamani. Kupitia ufunuo huo, niliazimia kukiri kutosamehe mara ilipoonekana—hata kama hiyo ilimaanisha kufanya hivyo kwa msingi wa saa baada ya saa.

Kadiri ninavyozidi kuachilia kutosamehe kwa njia ya kuungama, toba, na maombi mbele za Mungu, ndivyo nilivyoona watoto wangu wakiachiliwa pia. Na uhusiano wao kati yao umeboreka. Bila shaka, uwezo wa watoto wangu wa kusamehe hautegemei mimi. Ni uamuzi wao. Lakini kwa matumaini wataona msamaha ukiigwa kwa njia ya wazi ya kutosha kufanya uamuzi wao wa kusamehe kuwa rahisi.

Njia nzuri ya kuona tabia mbaya ikivunjwa kwa mtoto wako ni kuiona ikivunjwa ndani yako kwanza. Mahali pazuri pa kuanzia ni kutambua dhambi yoyote katika maisha yako. Popote palipo na dhambi, unahitaji kuiungama. Dhambi hiyo ikirudiwa mara kwa mara, itazidi kukita mizizi. Kwa mfano, uwongo ni dhambi. Kwa kusema uwongo mara kwa mara, nafasi inatengenezwa kwa sifa hii kujikita, na hivi karibuni kusema uwongo hutoka nje ya udhibiti. Mfano mwingine ni kutaka kufa. Hii ni dhambi. Watu wanaposema, “Nataka kufa” mara za kutosha, wanaweza kufika mahali wanasumbuliwa na mawazo ya kujiua.

Ukiona mahali fulani maishani mwako umetenda dhambi au hukuishi katika njia ya Mungu, tubu mara moja kwa kwenda mbele za Bwana na kuungama. Omba msamaha wa Mungu na useme, “Mungu, Wewe uwe

na udhibiti na unisaidie nisiishi hivyo tena."

Kisha tambua dhambi yoyote ndani ya wazazi wako au babu na nyanya zako ambayo unahisi inaweza kukuathiri wewe au watoto wako na uombe kuhusu hilo pia. Biblia inasema, "Roho Mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu; na kama watoto, basi, tu warithi; warithi wa Mungu, warithi pamoja na Kristo (Warumi 8:16-17).

*Tunataka kuwa warithi wa Mungu, si wa dhambi za familia yetu.*

Katika Jina la Yesu tunaweza kuwekwa huru kutokana na mfumo wowote wa dhambi wa familia, na kwa uwezo wa Roho Mtakatifu tunaweza kukataa kuiruhusu nafasi yoyote katika maisha ya watoto wetu. Ikiwa unaweza kufikiria tabia zozote za familia ambazo hutaki watoto wako warithi, anza kuomba sasa.

## ***MAOMBI***

*Bwana,* umesema katika Neno lako kwamba mtu mwema huwaachia wana wa watoto wake urithi (Mithali 13:22). Ninaomba kwamba urithi ninaowaachia watoto wangu uwe thawabu za maisha ya kumcha Mungu na moyo safi mbele zako. Ili kuhakikisha hilo linafanyika, ninaomba kwamba popote pale ambapo kuna tabia ya dhambi ndani yangu ambayo nimepata kutoka **kwa familia yangu**, niokoe kutoka kwayo sasa kwa Jina la Yesu. Ninaungama dhambi zangu Kwako.

Ninaomba msamaha na urejesho, nikijua Neno Lako linasema, "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote" (1 Yohana 1: 9). Ninajua kwamba kusafishwa kutoka kwa dhambi kwa njia ya kuungama kunapunguza uwezekano wa kupitisha tabia ya dhambi kwa mtoto

Yesu alisema, "Nimewapa ninyi mamlaka… juu ya nguvu zote za yule adui" (Luka 10:19). Ikiwa kuna kazi yoyote ya adui katika maisha yangu ya zamani inayotaka kuingilia maisha ya mtoto wangu,_____ (jina la mtoto), ninaivunja sasa kwa nguvu na mamlaka niliyopewa katika Yesu Kristo. Ninaomba hasa kuhusu (taja kitu ambacho unaona ndani yako au familia yako ambacho hutaki kupitishwa kwa mtoto wako).

Chochote ambacho si mapenzi Yako kwa maisha yetu ikiwemo dhambi ninakataa. Asante, Yesu, kwamba ulikuja kutuweka huru kutoka kwa wakati uliopita. Tunakataa kuishi kwa kufungwa na dhambi. Asante, Baba, kwamba "umetustahilisha kuwa washiriki wa urithi wa watakatifu katika nuru" (Wakolosai 1:12). Ninaomba kwamba mwanangu binti yangu asirithi tabia yoyote ya dhambi kutoka kwangu au kwa familia, lakini "atarithi ufalme uliotayarishwa kwa ajili yake yeye tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu" (Mathayo 25:34). Asante Yesu kwa kuwa ndani yako yale ya kale yamepita na yote yamekuwa mapya. Katika jina la Yesu ninaomba.

## SILAHA ZA VITA

Kwa hiyo simameni imara katika uhuru ambao Kristo alituweka huru nao,

wala msinaswe tena na nira ya utumwa.

**WAGALATIA 5:1**

Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa rehema Zake nyingi alituzaa mara ya pili ili tuwe na tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu Kristo katika wafu, tupate urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliohifadhiwa mbinguni kwa ajili yenu, ninyi mnaolindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mpate wokovu ulio tayari kufunuliwa wakati wa mwisho.

**1 PETRO 1:3-5**

Roho ya Bwana MUNGU i juu Yangu, kwa sababu Bwana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema; Amenituma ili kuwaponya waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka kufunguliwa kwao, na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao.

**ISAYA 61:1**

Kwa hiyo, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; mambo ya kale yamepita; tazama, yote yamekuwa mapya.

**2 WAKORINTHO 5:17**

Maana sisi nasi hapo kwanza tulikuwa wapumbavu, wakaidi, tumedanganywa, tukitumikia tamaa na anasa za namna nyingi, tukiishi katika uovu na husuda, tukichukia na kuchukiana. Lakini wema na upendo wa Mungu Mwokozi wetu kwa wanadamu ulipodhihirika, si kwa matendo ya haki tuliyoyatenda sisi, bali kwa rehema Yake, kwa kuoshwa kwa

kuzaliwa mara ya pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu, ambaye alimimina kwa wingi katika Yesu Kristo Mwokozi wetu, ili tukiisha kuhesabiwa haki kwa neema Yake, tupate kuwa warithi, sawasawa na tumaini la uzima wa milele.

**TITO 3:3-7**

## Sura ya ishirini na tatu

# KUEPUKA POMBE, MADAWA YA KULEVYA NA MADAWA MENGINE

Shetani anataka watoto wetu, na atawachukua anavyoweza. Pombe, dawa za kulevya, na uraibu mwingine ni baadhi ya vivutio vyake vilivyofanikiwa zaidi. Kwa kweli, shambulio dhidi ya watoto wetu ni kubwa sana kiasi kwamba hawawezi kusimama dhidi yake bila msaada wetu.

Habari njema ni kwamba *kwa* msaada wetu kupitia kifuniko cha maombi, na mafundisho, wanaweza kusimama imara.

Sio haraka sana kuanza kuwaombea watoto wetu waepuke pombe na dawa za kulevya, kwa sababu uwezekano wa uraibu wa vitu hivi unaweza kutokea katika umri mdogo sana. Pia haijachelewa sana kuomba juu yake pia, kwa sababu majaribu yanaweza kutokea kwa mtu yeyote wakati

wowote katika maisha yake. Ninamfahamu mtu ambaye hakuwa mlevi wa pombe hadi alipokuwa na umri wa miaka hamsini. Alisema alijua alikuwa na udhaifu kwa hilo, lakini hakukubali hadi alipokuwa kwenye tafrija ndogo ya chakula cha jioni ambapo pombe ilikuwa ikitolewa. Alijaribu kidogo, na aliporudi nyumbani hakuacha kunywa. Labda kama angekuwa na mzazi anayeomba au kikundi cha maombi cha kumwombea hili lisingetokea kamwe.

Nimeona huduma nyingi za muziki wa Kikristo zikipungua kwa sababu ya pombe na madawa ya kulevya. Watu hawa wako mstari wa mbele wa vita na hata hawatambui mpaka waangushwe. Wao ni shabaha kuu za mashambulizi ya adui 'target', na wanaanguka moja kwa moja katika mitego yake kwa sababu hawajafunikwa katika maombi. Ni kweli kwamba baadhi yao hushindwa kimakusudi na vishawishi, lakini ninaamini kwamba wengi wao wanataka kufanya yaliyo sawa. Jambo ni kwamba, mvutano wa mwili na mipango ya Shetani vina nguvu zaidi kuliko vile tungependa kufikiria. Katika wakati wa udhaifu, kama inavyowezekana kwa sisi sote, tunaweza kuishia kufanya kitu ambacho hatujawahi kufikiria tutafanya. Nguvu ya Mungu pekee, kupitia maombi, ndiyo inaweza kuleta mabadiliko.

Ikiwa mtoto wako *tayari* ana shida katika eneo hili na Shetani ameshinda uwanja fulani katika vita, simama kwa ujasiri wa kujua wewe ni nani katika Bwana na upate tena kuwaombea. Watoto wako ni *wako* na *si wa S*hetani, na unaweza kuwatetea mbele ya kiti cha enzi cha Mungu. Una uwezo na mamlaka. Shetani hafanyi hivyo. Anachopaswa kufanya kazi nacho ni

uongo na udanganyifu. Kemea uongo wake kwa uwezo uliowekwa ndani yako kupitia Yesu Kristo Mwokozi wako, ambaye ni Bwana juu ya kila kitu maishani mwako, pamoja na mtoto wako. Biblia inasema, “Lolote mfanyalo, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu” (1 Wakorintho 10:31). Tuombe kwamba kila kitu watoto wetu wanachofanya kwa miili yao, kifanyike kwa heshima na utukufu wa Mungu.

### ***MAOMBI***

*Bwana,* ninaomba kwamba ---------(jina la mtoto) aishi bila uraibu wowote hasa pombe au dawa za kulevya. Mtie nguvu ndani Yako, msogeze karibu nawe na umwezeshe kukuweka Wewe katika udhibiti wa maisha yake. Sema na moyo wake, muonyeshe njia anayopaswa kuifuata, na umsaidie aone kwamba kuulinda mwili kutokana na vitu vinavyouharibu ni sehemu ya huduma yake. Kwako Ninaomba kwamba Wewe, Bwana, ungezuia mpango wowote ambao Shetani anao wa kuharibu maisha yake kupitia pombe na dawa za kulevya, na kuchukua chochote katika utu wake ambacho kingevutwa kwa vitu hivyo. Neno Lako linasema, “Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti” (Mithali 16:25). Mpe utambuzi na nguvu ya kuweza kusema “hapana” kwa mambo yanayoleta kifo na “ndiyo” kwa mambo ya Mungu yanayoleta uzima. Na yeye aone Ukweli wazi kila anapojaribiwa na kukombolewa kutoka kwa yule mwovu kila anaponaswa. Mwezeshe kuchagua maisha katika chochote anachofanya, na uraibu wake pekee uwe kwa mambo ya Mungu. Ninaomba kwamba

kila kitu anachofanya yeye na mwili wake kifanyike kwa utukufu Wako. Katika Jina la Yesu ninaomba. Amen.

## SILAHA ZA VITA

Mkiishi kufuatana na mwili, mtakufa; lakini mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi.

**WARUMI 8:13**

Kwa hiyo ondoa huzuni moyoni mwako, na uondoe uovu katika mwili wako.

**MHUBIRI 11:10**

Nimekuwekea mbele yako uzima na mauti, baraka na laana; basi chagua uzima, ili uwe hai wewe na uzao wako.

**KUMBUKUMBU LA TORATI 30:19**

Haki ya wanyofu itawaokoa, lakini wasio waaminifu watakamatwa na tamaa zao.

**MITHALI 11:6**

Kwa hiyo Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli.

**YOHANA 8:36**

## Sura ya ishirini na nne

## KUKATAA UASHERATI NA NGONO CHAFU

Karibu na jeraha la janga, kifo, na kuzimu ya milele, ngono au uasherati ni uharibifu wa kutisha zaidi kwa maisha ya watoto wetu. Hiyo ni kwa sababu matokeo ya dhambi ya zinaa hudumu maisha yote— mara nyingi kwa wazazi na pia mtoto. Maneno kama vile "kutoa mimba," "kuzaa nje ya ndoa," "kutokuwa mwaminifu," "upotovu wa kingono," "ugonjwa wa zinaa," na "UKIMWI" yote humfanya mzazi ashtuke. Na leo, zaidi ya hapo awali, hili ni suala la uhai na kifo.

Sote tunafahamu vyema kwamba hakuna njia ya kutoka katika uasherati bila madhara. Lakini sio tu kile kinachotokea kwa miili ya watoto wetu kinachotuhusu. Biblia inasema, "Jiepusheni na tamaa za mwili zipiganazo na roho" (1 Petro 2:11). Matokeo ya dhambi ya zinaa huvamia nafsi pia.

Hili ni jambo ambalo nililiombea kwa bidii tangu watoto wangu walipokuwa wadogo hadi walipokuwa watu wazima. Hakika sikutaka wafe kutokana na UKIMWI, wala sikutaka wajukuu waje kabla ya watoto wangu kuolewa/kuoa. Kando na mambo hayo makuu, pia sikutaka wamwasi Mungu na kukosa yote aliyo nayo kwa ajili yao. Ninajua kwamba pamoja na dhambi ya zinaa utimilifu wa uwepo wa Mungu, amani, baraka, na furaha hutolewa dhabihu ya juu sana.

Sikutaka watoto waendekeze uovu wa siri au tabia iliyofichwa, kujifurahisha-kibinafsi, au tamaa ya kipekee ambayo mtu huiweka faraghani, iwe ni dhambi, upumbavu, aibu, au kupoteza muda bila tija kwa viwango vya kijamii. Uovu huu

wa siri nilijumuisha na mambo ambayo yamekuja kwetu hivi karibuni, yaani shughuli ya ngono inayohusisha mtu mmoja tu. Matumizi ya mwili na akili ya mtu mwenyewe kujichochea kingono ambayo yanaweza kujumuisha ponografia, roboti za ngono n.k. Uraibu wa simu ya mkononi, kutazama televisheni na vipindi kwa kupitiliza kiasi, kula chakula kisicho na virutubisho faraghani kwa vile unaogopa watu wasikuseme kuhusu mwili wako, au burudani ya ajabu ambayo mtu huhisi vibaya kuikubali kwa wenzake kwamba anajihusisha nayo

Hatuwezi kungoja hadi watoto wetu wawe vijana ili kusali kuhusu jambo hili, kama vile hatuwezi kungoja hadi wakati huo ili kuwaelekeza kwamba maisha hufanya kazi vizuri zaidi tunapoishi njia ya Mungu. Leo ni siku ya kuomba. Majaribu ya ngono ni kila mahali. Iko mbele ya macho ya watoto wetu kila upande. Iko kwenye mabango, TV, na redio; vipo katika sinema, muziki maarufu, vitabu, na magazeti—hata machapisho yasiyo na hatia kama yale yanayohusu habari, michezo, afya, na mambo ya kupendeza.

Watoto wetu wanashambuliwa nayo, na tunaishi kwa kukataa hili na kujidanganya na ni kana kwamba tunafikiri wanaweza kuwa na nguvu ya kushinda peke yao. Wanahitaji tuombe kwa ajili yao. Hata kama mtoto wako tayari ameshindwa katika eneo hili, haijachelewa sana kwake kuungama na kutubu, na kusamehewa, kuponywa, na kufanywa upya.

Biblia inasema, “Anayeutumainia moyo wake ni mpumbavu, bali yeye aendaye kwa hekima ataokolewa” (Mithali 28:26).

Ni lazima tuwaombee watoto wetu wamwamini Mungu na si hisia zao zisizotegemewa, ili watembee kwa hekima na kuepuka mtego huu hatari.

Ni lazima tuwaombee ili waishi kwa njia ya Mungu.

Njia mojawapo ya Mungu kwa maisha yetu ni usafi wa kijinsia, na msingi wake umewekwa katika umri mdogo sana. Haijalishi mtoto wako ana umri gani—mtoto mdogo, kijana mdogo, au wa miaka thelathini na kitu—na kama ni bikira au anafanya ngono anza kumuombea aishi maisha ya usafi wa kingono kuanzia siku hii na kuendelea.

***MAOMBI***

*Bwana,* ninaomba kwamba utamweka …………………… (jina la mtoto) safi kingono maisha yake yote. Mpe moyo unaotaka kufanya yaliyo sawa katika eneo hili, na acha usafi ukite mizizi katika utu wake na uongoze matendo yake. Msaidie kila wakati kuweka sheria za Kiungu/mbingu kwa uhusiano na kupinga chochote ambacho sio bora kwako. Fungua macho yake kwa Ukweli wa Neno Lako, na umsaidie kuona kwamba ngono nje ya ndoa haitakuwa kamwe upendo wa kujitolea, wa kudumu, usio na masharti ambao yeye anahitaji. Utu wake usiwe na kovu wala hisia zake zisiharibiwe na mgawanyiko wa nafsi unaotokea kwa sababu ya zinaa. Ninaomba kwamba yeye hatashiriki ngono kabla ya ndoa na asifanye ngono na mtu yeyote isipokuwa mwenzi wake wa ndoa.

Ninaomba kwamba upotovu wa kijinsia wa aina yoyote kamwe usiweke mizizi ndani yake au hata kupata fursa ya kujiinua kwake.

Muweke mbali na mtu yeyote mwenye nia mbaya, au mtoe mtu huyo katika

maisha yake. Mlinde dhidi ya unyanyasaji wowote wa kingono au ubakaji. Geuza macho yake kutoka kwenye uasherati unaoujaza ulimwengu na kumwezesha kuelewa kwamba yeyote “atakaye kuwa rafiki wa ulimwengu anajifanya kuwa adui wa Mungu” (Yakobo 4:4). Na atamani kupata kibali chako, Bwana, na asiruhusu uzinzi katika maisha yake wakati wowote. Mwokoe kutoka kwa roho yoyote ya tamaa inayoleta majaribu ya kushindwa katika eneo hili. Weka kengele ya Roho Mtakatifu ndani yake inayolia kama king'ora kikubwa kinachomulika kila anapokanyaga mstari wa yale yasiyo sawa mbele Yako.

Neno Lako linasema, “Heri mtu astahimiliye majaribu; kwa maana akiisha kukubaliwa ataipokea taji ya uzima, Bwana aliyowaahidia wampendao” (Yakobo 1:12). Zungumza naye kwa sauti kubwa wakati wowote kunapokuwa na jaribu la kufanya jambo ambalo hapaswi kufanya, na umfanye kuwa na nguvu za kutosha ndani Yako ili asimamie lililo sawa na kusema “hapana” kwa uasherati. Neema Yako na imwezeshe kujitoa kukaa safi ili apate taji Yako ya uzima.

Katika jina la Yesu ninaomba. Amina

**SILAHA ZA VITA**

Haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu: mjiepushe na uasherati; ili kila mmoja wenu ajue kuuweza mwili wake mwenyewe katika utakatifu na heshima, si katika hali ya tamaa mbaya, kama watu wa Mataifa wasiomjua Mungu.

**1 WATHESALONIKE 4:3-5**

Ikimbieni zinaa. Kila dhambi aitendayo mwanadamu ni nje ya mwili wake; lakini yeye afanyaye zinaa hutenda dhambi juu ya mwili wake mwenyewe.

**1 WAKORINTHO 6:18**

Mwili si wa zinaa, bali ni wa Bwana, na Bwana ni kwa mwili.

**1 WAKORINTHO 6:13**

Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; lakini Mungu ni mwaminifu ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo, lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili.

**1 WAKORINTHO 10:13**

Lakini kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa. Kisha tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi; na dhambi, ikiisha kukomaa, huzaa mauti.

**YAKOBO 1:14-15**

## Sura ya ishirini na tano

## KUPATA MWENZI MWEMA

Muda mfupi baada ya mwanangu na binti yangu kuzaliwa, nilianza kusali kwa mke na mume husika, yaani wale ambao watakuwa wenzi wao. Pamoja na hayo, nilisali kwamba roho ya talaka isipate nafasi yoyote katika maisha yao. Wengine wanaweza kudhani maombi haya ni ya mapema, lakini sivyo. Pamoja na uamuzi wao wa kumpokea Yesu,

uamuzi kama Mwokozi, uchaguzi unaofuata kwa umuhimu ni nani ambaye wanachagua kuoa au kuolewa naye. Huu ni uamuzi muhimu Zaidi ambao watoto wetu watafanya. Utaathiri maisha yao yote, bila kutaja maisha ya wanafamilia wengine.

Uamuzi mbaya unaweza kuleta taabu na maumivu kwa kila mtu anayehusika. Na kwa kuwa ni Mungu pekee Ndiye anayejua ni nani atakuwa mwenzi bora wa ndoa kwa yeyote, Anapaswa kushirikishwa kwanza na Anapaswa kutoa jibu la mwisho.

Ninapofikiria watu ninaowajua ambao wamepitia ndoa zenye taabu, wenzi wanaodhulumiwa au kuteswa kwa kutokuwa waaminifu katika ndoa, au ndoa nyingi, kuchelewa kuolewa, kuwa na watoto kabla ya ndoa, au ambao hawana furaha waseja, jambo moja hutokeza akilini mwangu: Hakuna hata mmoja wao aliyekuwa na wazazi ambao waliwaombea wenzi wao na uhusiano wao wa ndoa.

Kwa upande mwingine, ninajua wanandoa ambao wanalingana kikamilifu katika kifungo cha ndoa na ambao hawajapatwa na matatizo yoyote yaliyotajwa hapo juu. Haishangazi, yote haya watu binafsi walikuwa na wazazi ambao waliwaombea kuhusiana na jambo hili au watu binafsi waliomba na kungoja hadi wahakikishe kuwa wamepata mwenzi ambaye Mungu alikuwa amewachagulia. Pia, watu hao hawakuhama kutoka kwa uhusiano mmoja hadi mwingine au kupuuza sheria za Mungu za usafi wa kingono. Walijiweka safi kwa ajili ya mwenzi ambaye Mungu alikuwa nao kwa ajili yao, na wamefurahishwa sana. Kama matokeo ya uchunguzi

huu wote na uzoefu wangu mwenyewe, sasa ninaamini kwamba ndoa zinaweza kufanywa mbinguni wakati tunaomba kwa Mungu aliye mpangaji/mmachishaji mkuu wa ndoa.

Leo mwana wetu ameoana na msichana mzuri sana, mcha Mungu ambaye tunampenda kama binti. Na binti yetu ameolewa na kijana mzuri ajabu, mcha Mungu ambaye tunampenda kama mwana. Tunajua kwamba nyongeza hizi mbili zilizokaribishwa kwa familia yetu ni majibu ya maombi tuliyoomba kwa ajili ya watoto wetu tangu walipozaliwa. Sasa tunaomba kwa ajili ya miaka iliyo mbele yao.

Harusi za kupendeza hazifanyi ndoa kamilifu. Ni Mungu pekee awezaye kufanya hivyo. Biblia inasema, "Mna mipango mingi moyoni mwa mtu, lakini shauri la BWANA ndilo litakalosimama"

(Mithali 19:21). Sio washauri wa harusi na wahudumu ambao huwaweka bibi na bwana harusi kwenye njia sahihi. Kufuata mashauri ya Mungu na kufuata mwongozo Wake hufanya hivyo. Na maombi pekee huwafanya watoto wetu kuendelea kutafuta mapenzi ya Mungu badala ya kufuata hisia zao wenyewe kwa sasa.

*Roho wa Mungu huweka ndoa pamoja; roho ya talaka huiharibu.*

*Omba sasa kwamba Roho Mtakatifu, sio roho ya talaka, atawale maisha ya baadaye ya mtoto wako.*

Ikiwa mtoto wako tayari ameolewa na mtu fulani, sali kwamba yeye na

mwenzi wake “waunganishwe pamoja kikamilifu katika nia ileile” (1 Wakorintho 1:10), kwa sababu kila “nyumba iliyogawanyika juu ya nafsi yake haitasimama” (1 Wakorintho 1:10) Mathayo 12:25). Waombee waokolewe kutoka kwa roho yoyote ya talaka ambayo ingejaribu kuweka kabari kati yao. Ikiwa mtoto wako tayari ameachwa, omba ili uharibifu wote upone na kwamba hakutakuwa na talaka tena katika maisha yake ya baadaye.

Haijalishi mtoto wako ana umri gani, omba kuhusu hili leo. Talaka ni sehemu ya roho ya wakati huu, na inatishia karibu kila mtu wakati mmoja au mwingine. Tusimame pamoja kulipinga sisi wenyewe na watoto wetu kwa uwezo wa Roho Mtakatifu ndani yetu kupitia Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.

***MAOMBI***

*Bwana,* isipokuwa mpango Wako ni kwa--------- (jina la mtoto) kubaki mseja, ninaomba kwamba Utampatia mwenzi mkamilifu wa ndoa kwa ajili yake. Mpeleke mume/mke wa haki kwa wakati muafaka, na mpe uwongofu ulio wazi kutoka Kwako juu ya mwenzi huyo. Ninaomba kwamba binti yangu /kijana wangu awe mtiifu vya kutosha kusikia sauti Yako inapofika wakati wa kufanya uamuzi wa ndoa, na kwamba yeye atafanya uamuzi huo kulingana na kile Unasema na si tu tamaa ya kimwili.

Nakuomba… akutegemee Wewe kwa moyo wake wote na asitegemee akili zake mwenyewe; kwamba atakukubali Wewe katika njia zake zote ili

kwamba Wewe umwongoze njia yake (Mithali 3:5-6).

Andaa mtu huyo ambaye atakuwa mume /mke kamili kwa ajili yake yeye. Msaidie binti yangu/ mwanangu kuelewa tofauti kati ya kupenda tu na kujua kwa hakika huyu ndiye mtu ambaye Mungu anamtaka yeye atumie maisha yake yote naye. Ikiwa yeye anavutiwa na mtu ambaye hapaswi kuoana naye, ninaomba kwamba Wewe, Bwana, ungeukata uhusiano huo. Msaidie kutambua kwamba isipokuwa Wewe uko katikati ya ndoa, haitasimama kamwe. Wewe Usipoibariki, haitabarikiwa. Maana Neno Lako linasema, "BWANA asipoijenga nyumba, waijengao wafanya kazi bure" (Zaburi 127:1). Ninaomba kwamba ungejenga ndoa ambayo nyumba yao inaanzishwa. Wakati yeye anapopata mtu sahihi wa kuoana naye, naomba huyo mtu atakuwa mtumishi Wako mcha Mungu na aliyejitoa, ambaye anakupenda Wewe na kuiishi njia Yako, na atakuwa kama mwana (binti) kwetu na baraka kwa wanafamilia wengine wote. Mara baada ya yeye kuoa/kuolewa, basi kusiwe na talaka katika maisha yake ya baadaye. Kamwe kusiwe na unyanyasaji wa kiakili, kihisia, au kimwili wa aina yoyote, bali umoja wa kiakili, kihisia, na kimwili ambao hauguswi kamwe na mgawanyiko. Ninawaombea ukombozi kutoka kwa roho yoyote ya talaka, utengano, au mafarakano ambayo yangejaribu kuleta ugomvi katika uhusiano wao. Wape kila mmoja hamu kubwa ya kuishi katika uaminifu, na uondoe majaribu yoyote ya ukafiri.

Na awe na mwenzi mmoja wa maisha, ambaye pia ni rafiki yake wa

karibu zaidi. Na wawe waaminifu kwa pande zote mbili, wenye kuhurumiana, wanaojaliana, wenye kuheshimiana, wenye upendo, wenye kusamehe na kusameheana, wenye kusaidiana, wenye kujaliana, na wenye kupendana siku zote za maisha yao na kupenda watu. Katika Jina la Yesu ninaomba. Amen.

## SILAHA ZA VITA

Tangu mwanzo wa uumbaji, Mungu aliwaumba mume na mke. Kwa sababu hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe, na hao wawili watakuwa mwili mmoja; kwa hiyo, wao si wawili tena, bali mwili mmoja. Kwa hiyo aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe.

**MARKO 10:6-9**

Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi; bali waasherati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu.

**WAEBRANIA 13:4**

Yeyote anayemwacha mke wake na kuoa mwingine anazini dhidi yake.

**MARKO 10:11**

Apataye mke apata kitu chema, naye ajipatia kibali kwa BWANA.

**MITHALI 18:22**

Mnaifunika madhabahu ya BWANA kwa machozi, kwa kulia na kulia;

kwa hivyo haizingatii sadaka tena, wala haipokei kwa radhi kutoka kwa mikono yako. Lakini unasema, "Kwa sababu gani?" Kwa sababu BWANA amekuwa shahidi kati yako na mke wa ujana wako, ambaye umemtendea kwa hiana; lakini yeye ni mwenzako na mkeo kwa agano. Lakini je, kuna mtu mmoja atafutaye uzao wenye kumcha Mungu? Kwa hiyo jihadharini roho zenu, mtu awaye yote asimtende kwa hiana mke wa ujana wake. Kwa maana BWANA, Mungu wa Israeli, asema kwamba anachukia talaka.

**Malaki 2:13-16**

## Sura ya ishirini na sita

## KUISHI BILA KUTOSAMEHE

Wakati wowote ninapolazimika kuomba msamaha kwa watoto wangu kwa jambo fulani, mimi huwaambia ninahitaji kuwasikia wakisema, "Nimekusamehe." Sifanyi hivyo kwa sababu tu ninahitaji *kuisikia;* Ninafanya hivyo kwa sababu *wanahitaji kusema na* kuachilia kabisa. Vivyo

hivyo, watoto wangu wakigombana, mimi huwapa agizo kwao kwamba waseme "samahani" na "nimekusamehe" wao kwa wao. Hata kama hawahisi mambo hayo kwa moyo wote kwa wakati huo, najua kwamba wanachosema hatimaye kitatenda kazi katika nafsi zao. Kwa kweli ni bora ikiwa watoto watasema mambo haya na kuyamaanisha bila kuambiwa, lakini hadi hilo liwe Ukweli, hii ni bora zaidi kuliko kutofanya chochote na kungoja tu msamaha kutokea. "Msamaha ni *chaguo* mnalofanya," nimewaagiza.

"Usiposamehe, inaleta kifo katika maisha yako kwa namna moja au nyingine. Njia bora ya kusamehe ni kusali kwa ajili ya mtu unayehitaji kumsamehe. Ingawa inaweza kuonekana kuwa ngumu mwanzoni, mara tu unapoingia ndani na kutafuta mambo mengi zaidi ya kusali, utaona moyo wako ukiwa laini kumwelekea mtu huyo." Nimejionea moja kwa moja, kama vile nina uhakika na hili pia, familia zinazosubiri msamaha kutokea. Hawasamehi mpaka wajisikie *kusamehe.* Matokeo yake, kuna mpasuko mkubwa ambao hutokea mara nyingi kati ya wanafamilia. Wao huwa na mazoea ya kusema mambo yasiyofaa au *kuhusu wao* kwa wao, au labda hata hawajazungumza kwa miaka mingi. Ukosefu wa kipekee wa neema na kuthaminiana huweka msingi wa kila neno na tendo kwa sababu roho ya kutosamehe imepewa makao huko. Familia nzima huteseka wakati mmoja au zaidi pale wanafamilia wanapotembea katika hali ya kutosameheana.

Kama sehemu ya kuheshimu baba na mama na kupokea ahadi ya maisha marefu na baraka inayoambatana na amri hiyo, kila mtoto anahitaji

kuwasamehe wazazi wote wawili kwa kutokamilika kwao, na jambo lolote ambalo huenda walifanya, ambalo lilikuwa la kuumiza. Pamoja na hayo wanahitaji pia kusamehe akina dada, kaka, shangazi, wajomba, binamu, babu na nyanya, marafiki, maadui, na wakati mwingine hata wao wenyewe—na tunahitaji kuwatia moyo kufanya hivyo. Ikiwa hatutawafundisha watoto wetu kusamehe, tunafanya upotovu ambao unaweza kuwa na madhara makubwa.

Mojawapo ya mambo bora tunayoweza kufanya ili kuwasaidia watoto wetu kukaa bila kutosamehe. Kando na kuwafundisha kusamehe na kuomba ili watembee katika msamaha, ni kujiweka huru na kutosamehe sisi wenyewe. Kutokusamehe kunaweza kuwa sehemu ya maisha yetu kwa urahisi kiasi kwamba tunabeba jambo hilo pamoja nasi popote tunapoenda bila hata kutambua kuwa tumebeba mzigo huo. Hatimaye nilipojifunza kuwa msamaha haumfanyi *mtu mwingine kuwa sawa, bali* unakufanya wewe *uwe huru,* nilipata mafanikio makubwa katika eneo hilo. Sikuzote nilihisi kwamba kusamehe mtu kulimaanisha nilikuwa nikisema, “Ulichofanya ni sawa.” Lakini sivyo ilivyo hata kidogo. Msamaha ni kuamini kwamba Mungu ni Mungu wa haki, kwani anasema Yeye na kusema, "Baba, sitamshikilia mtu huyo kwangu tena kwa kutosamehe." Ni kukiri kwamba Mungu anajua ukweli na kumruhusu kuwa mwamuzi, kwa sababu Yeye peke yake Ndiye anayejua kisa kizima.

Biblia inasema, “BWANA ni Mungu wa haki; heri wote wamngojeao” (Isaya 30:18). Tutabarikiwa ikiwa tutaungama kutosamehe kwetu, kuomba

tukombolewe kutoka kwayo, na kisha kuketi na kumngojea Mungu afanye lililo sawa huku tukifurahia baraka zake. Je, hiyo haionekani kuwa ya kufurahisha zaidi kuliko kuishi katika gereza la kutosamehe na kuteseka ugonjwa unaoletwa katika nafsi zetu, miili, mahusiano, na maisha yetu? Kwanini watu waishi vichwani mwetu bila kulipa kodi, kana kwamba tunaamini tukinywa sumu sisi wao watakufa.

Mwana anamsamehe vipi baba aliyempiga? Mama anamsamehe vipi dereva mlevi aliyemuua bintiye? Msichana mdogo anamsamehe vipi mjomba aliyemnyanyasa? Mtu yeyote anawezaje kuonyesha rehema kwa mtu ambaye hakuwa na rehema? Hawawezi kuonyesha rehema au kusamehe kikamilifu, isipokuwa waje katika uwepo wa Bwana na kuelewa msamaha wake *kamili.* Hakuna kitu kama machozi ya furaha na kuachiliwa tunayohisi tunapofika mahali pale pa msamaha kamili mbele za Bwana. Inaleta uzima kwa sababu inafanya upya utu wetu wote. Biblia inasema, "Natenda neno moja tu, nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu" (Wafilipi 3:13-13). 14).

Hatuwezi kuendelea na maisha yetu na yote ambayo Mungu anayo kwa ajili yetu ikiwa bado tumefungwa kwa yaliyopita. Wala watoto wetu hawawezi. Yesu alisema, "Heri wenye rehema, maana hao watapata rehema" (Mathayo 5:7). Tuwaombee watoto wetu wapate rehema na hakuna kitakachozuia huruma ya Mungu kwao. Hebu tuwaombee wawe watu wanaosema, "Nimekusamehe" kila hitaji la kufanya hivyo

linapojitokeza. Tuombe ili uchungu na kutosamehe usifanye ukuta kati yetu na Mungu na kuzuia maombi yetu. Hatuna wakati wa hilo. Kuna maombi mengi sana ya kufanywa.

### *MAOMBI*

*Bwana,* ninaomba kwamba ungemwezesha-------- (jina la mtoto) kuishi katika msamaha unaoendelea. Mfundishe kina cha msamaha Wako kwake ili naye aweze kuwa msamehevu kwa wengine. Msaidie kufanya uamuzi wa kusamehe kulingana na yale ambayo Umetuomba tufanye na si kwa yale anayojisikia vizuri kwa sasa. Na aelewe kwamba msamaha hauhalalishi matendo ya mtu mwingine; badala yake, humfanya kuwa huru. Msaidie yeye kuelewa kwamba Wewe pekee Ndiye unayejua kisa kizima kuhusu yeyote kati yetu, na ndiyo sababu yeye hana haki ya kuhukumu.

Bwana, Neno Lako linasema, "Yeye ampendaye ndugu yake, akaa katika nuru, wala ndani yake hamna sababu ya kujikwaa. Bali yeye amchukiaye ndugu yake yu katika giza, tena anatembea gizani, wala hajui aendako, kwa sababu giza limempofusha macho" (1 Yohana 2:10-11). Nionyeshe mahali ninapotembea katika giza la kutosamehe. Bwana, mimi sitaki giza hilo maishani mwangu. Ninataka kuona kwa uwazi na kujua ninakoenda. Na ninaomba hivyo kwa ajili ya mtoto wangu pia. Hebu daima atembee katika nuru ya upendo na msamaha. Mwezeshe yeye kusamehe wanafamilia, marafiki, na wengine wote pia. Umfundishe yeye kuachilia yaliyopita kwenye mikono yako ili aweze kuingia katika yale yote uliyo nayo kwa ajili yake. Usimruhusu kuweka vinyongo, visasi, uchungu, na hasira, lakini

badala yake umsaidie kukabidhi hisia hizi Kwako mara moja wakati zinapoingia moyoni.

Ninaomba kwamba yeye ataweza kujisamehe mwenyewe katika nyakati za kushindwa, na asije akakulaumu Wewe Bwana, kwa mambo yanayotokea duniani na katika maisha yake Kulingana na Neno Lako naomba kwamba yeye atawapenda adui zake, na kuwabariki wale wanaomlaani, awafanyie wema wale wanaomchukia, na awaombee wale wanaomuudhi na kumtesa kwa chuki, ili yeye aweze kufurahia baraka zako zote (Mathayo 5:44-45). Ninaomba kwamba ataishi katika utimilifu wa msamaha Wako kwa ajili yake na atembee katika uhuru wa msamaha katika moyo wake mwenyewe. Katika Jina la Yesu ninaomba. Amen.

## SILAHA ZA VITA

Uchungu wote na ghadhabu na hasira na kelele na matukano yaondoke kwenu pamoja na ubaya wote. Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.

**WAEFESO 4:31-32**

Mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. Lakini msipowasamehe watu makossa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu.

**MATHAYO 6:14-15**

Bwana wake akakasirika, akamtia mikononi mwa watesaji, hata atakapolipa deni lake lote. Ndivyo na Baba Yangu wa mbinguni atawatenda ninyi ikiwa kila mmoja wenu hatamsamehe ndugu yake kwa moyo wake wote.

**MATHAYO 18:34-35**

Busara ya mtu humpunguzia hasira, na utukufu wake ni kusahau kosa.

**MITHALI 19:11**

Kila msimamapo na kusali, sameheni, mkiwa na neno juu ya mtu, ili na Baba yenu aliye mbinguni awasamehe na ninyi makosa yenu.

**MARKO 11:25**

## Sura ya Ishirini na Saba

## KUTEMBEA KATIKA TOBA

Umewahi kuona watoto wanaoishi katika hatia na hukumu kwa sababu hawajaadhibiwa, hawajaungama, hawajatubu, na kusamehewa dhambi zao? Hawana nyuso zenye amani na macho yao yanaangalia chini na wanakosa ujasiri ambao watoto wasio na lawama wanao. Biblia inasema, "Walimtazama na kung'aa, na nyuso zao hazikuona haya" (Zaburi 34:5). Watoto wanaokubali makosa yao na wanajuta kiasi cha kutaka kubadili njia zao wana sura tofauti kabisa na wale wanaoficha dhambi zao na hawana nia ya kuungama.

Kuungama na kutubu ni kanuni mbili za maisha tunazopaswa kusisitiza kwa watoto wetu, kwa sababu dhambi isiyoungamwa itaweka ukuta kati yao na Mungu. Toba, ambayo kihalisi humaanisha "kugeuka na kuamua kutorudia tena," hudhihirishwa mtoto anaposema, kwa kweli, "nilifanya hivi, sasa nasikitika, na sitafanya tena." Ikiwa dhambi haitaungamwa na kutubiwa kwa njia hiyo, mtoto hawezi kuwa huru kutoka kwa utumwa unaoendana na dhambi ambayo haijaungamwa, na hilo litaonekana kwenye uso wake na katika utu wake, hayo ndiyo mambo ambayo Mungu aliwaambia Waisraeli ambao hawakumtii na hawakutubu, "Nanyi mtazikumbuka njia zenu na njia zenu zote. Matendo ambayo ulitiwa unajisi nayo; nanyi mtajichukia nafsi zenu kwa ajili ya maovu yote mliyoyatenda" (Ezekieli 20:43). Kujichukia huko kwa dhambi

ambayo haijaungamwa na ambayo haijatubiwa ni sehemu *yetu* pia, na moja ya maonyesho yake ni taswira binafsi mbaya. Hisia hizo za kushindwa na hatia zitaleta uharibifu katika maisha ya watoto wetu ikiwa hawatafundishwa kuungama na kutubu.

Nakumbuka kwamba niligundua dhambi kwenye nyuso za watoto wangu kabla sijaigundua katika matendo yao. Walikuwa wakiniambia jinsi ilivyokuwa inakera, kwamba hawakuweza kamwe kujiepusha na jambo lolote kwa muda mrefu.

"Hiyo ni kwa sababu nilimwomba Mungu anifunulie chochote ninachohitaji kujua," nikawaambia Watoto wangu kuwa, "na Roho Mtakatifu huniambia kila mara ikiwa umefanya jambo baya."

Wakati wowote nilipoona nyuso zao haziko wazi, kwamba walijificha, na macho yakawa kana kwamba yamemefunikwa na tabia isiyo ya uaminifu, nilimwomba Mungu anionyeshe dhambi yoyote iliyofichwa. Baada ya kuungama na kutubu na kupokea adhabu ifaayo, nyuso zao zilionekana tofauti kabisa—kana kwamba uzito au kivuli kilikuwa kimeondolewa kutoka kwao. Dhambi ina athari ya sumu. Dhambi isiyoungamwa inatulemea; inapotosha na kutia giza taswira yetu. Dhambi iliyoungamwa na moyo uliotubu huleta nuru, uzima, ujasiri, na uhuru.

Kwa sababu hakuna mtoto mkamilifu, tunahitaji kumwomba Mungu afunue, afichue, au aanike wazi dhambi yoyote iliyofichwa ambayo

imekita mizizi ndani ya mioyo ya watoto wetu ili iweze kushughulikiwa sasa badala ya baadaye, wakati matokeo yake huwa makubwa zaidi. Mungu atafanya hivyo, “kwa maana Yeye anazijua siri za moyo” (Zaburi 44:21). Sote tumesikia kisa cha mwanamume mzuri, anayependeza kwenye taarifa ya habari" ambaye anampiga mke wake, anawadhulumu watoto wake, au anafanya mauaji. Unaweza kuwa na hakika kwamba alikuwa mtu ambaye alikuwaameficha dhambi moyoni mwake kwa muda mrefu—labda tangu utotoni. Tunaweza kuwa na hakika kwamba dhambi yoyote iliyofichika kwa watoto wetu hatimaye itajionyesha kwa njia isiyohitajika. Wakati wa kuidaka na kuiondoa kabisa ni sasa. “Tupilieni mbali nanyi makosa yote mliyoyatenda, mkajipatie moyo mpya na roho mpya. Kwa nini ufe?” (Ezekieli 18:31). Mwombe Mungu akutolee nje dhambi iliyofichwa ndani yako au watoto wako ili kusiwe na gharama ya kimwili na ya kihisia ya kulipia.

Dhambi inaongoza kwenye kifo. Toba inaongoza kwenye uzima. Hatumwungamii Mungu ili apate kujua jambo. Tayari Yeye anajua. Kukiri ni nafasi kwetu kufuta kibao kichafu, na kuwa na ubao mpya. Toba ni fursa kwetu kuanza upya. Watoto wetu, kama sisi, wanahitaji hiyo fursa.

### *MAOMBI*

*Bwana,* ninaomba kwamba ungempa------- (jina la mtoto) moyo ambao ni mwepesi wa kukiri makosa yake Na awe na toba ya kweli kwa haya makosa, ili aweze kusamehewa na kutakaswa. Msaidie kuelewa kwamba

sheria Zako ni kwa manufaa yake na kwamba maungamo na toba anayohitaji lazima iwe njia ya maisha. Mpe hamu ya kuishi katika Ukweli mbele Zako, na aseme kama Daudi alivyosema, “Unioshe kabisa na uovu wangu, na unitakase na dhambi yangu…Uniumbie moyo safi, Ee Mungu; uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu. Usinitupe mbali na uwepo Wako, wala usiniondolee Roho Wako Mtakatifu. Unirudishie furaha ya wokovu Wako” (Zaburi 51:2,10-12

Bwana, onyesha dhambi zozote zilizofichwa ili ziweze kuungamwa, kutubu na kusamehewa. Neno Lako linasema, “Heri aliyesamehewa dhambi, ambaye dhambi yake imesitiriwa” (Zaburi 32:1). Ninaomba binti yangu/mwana wangu asiweze kuficha dhambi ndani yake lakini badala yake awe na hamu ya kukiri kikamilifu na kusema, "Uone kama iko njia yoyote ya uovu ndani yangu, ukaniongoze katika njia ya milele” (Zaburi 139:24). Asiishi katika hatia na hukumu, bali akae na dhamiri safi katika ufahamu kamili wa msamaha wake katika Kristo. Ninaomba yeye akutazame kwa uso unaomeremeta. Katika Jina la Yesu ninaomba. Amen.

## SILAHA ZA VITA

Wapenzi, ikiwa mioyo yetu haituhukumu, tuna ujasiri kwa Mungu. Na lolote tuombalo, twalipokea Kwake, kwa kuwa twazishika amri Zake, na kuyatenda yapendezayo machoni Pake.

## 1 YOHANA 3:21-22

Mtu mbaya na aache njia yake, na mtu asiye haki aache mawazo yake; na amrudie BWANA, Naye atamrehemu; na kwa Mungu wetu, Naye atamsamehe kabisa.

**ISAYA 55:7**

“Kwa hiyo nitawahukumu ninyi, enyi nyumba ya Israeli, kila mmoja kwa kadiri ya njia zake, asema Bwana MUNGU. "Tubuni, mkaghairi, na kuacha makosa yenu yote, ili uovu usiwe uharibifu wenu."

**EZEKIELI 18:30**

Afichaye dhambi zake hatafanikiwa, bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema.

**MITHALI 28:13**

Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako Kwake Bwana.

**MATENDO 3:19**

## Sura ya ishirini na nane

# KUVUNJA MAHUSIANO NA WASIOMCHA MUNGU

Je, umewahi kuona kitu kwa mtoto wako ambacho kinakusumbua lakini huwezi kutambua ni nini? Hilo likitokea, usipuuze hisia yako uliyopewa na Mungu. Mwambie Mungu akufunulie kile unachokihisi. Tumeunganishwa na Muumba wa ulimwengu, ambaye anaelewa kikamilifu kile kinachoendelea, na tunahitaji kumwomba hekima na ufunuo.

Je, umewahi kugundua usoni mwa mtoto wako kunaonyesha hatia, lakini wewe hukujua sababu yake?

Kwa maneno mengine, ulishuku kosa linalostahili aina fulani ya nidhamu lakini hukuwa na ushahidi wa kutosha au wenye uhakika. Wakati wowote jambo hilo lilipotokea kwa mmoja wa watoto wangu, niliomba, "Bwana, Wewe wajua upumbavu wetu na dhambi zetu, hizi hazijafichwa kwako (Zaburi 69:5). Nifunulie ninachokihisi kwa mtoto huyu, Kila wakati, Naye Bwana alifunua ngome isiyomcha Mungu iliyojisimamisha yenyewe katika mwili. Kwa mfano, wakati mmoja mtoto alikuwa akisafirisha vyakula vilivyokatazwa hadi chumbani kwake na kutumia kwa siri. Wakati mwingine, uwongo ulikuwa ukianzishwa ili kupata matokeo yaliyotarajiwa. Katika kila hali dhambi zilifunuliwa *baada ya* kuomba.

Sikuzote niliwaambia watoto wangu haitakuwa faida kwao kutomtii mama yao kwa sababu Mungu angetufunulia sisi kila mara-hautafaidika

kutotii. Baada ya muda waliniamini.

Mfano mmoja hujitokeza akilini mwangu. Wakati fulani binti yangu Miriam alipokuwa na umri wa miaka saba hivi, huwa nilikuwa nampa vitamini fulani kila asubuhi, ili ameze. Hizi vitamini zilikuwa zimeagizwa na daktari wetu, na sikuzote nilihakikisha kuwa nimeziweka kwenye sahani ndogo karibu na sahani yake kwenye meza wakati wa kifungua kinywa. Hapo mwanzo alikataa kila mara kuzimeza. Baada ya muda akawa mchangamfu zaidi, na mwishowe akaacha kulalamika kabisa. Wakati huohuo, nilihisi kitu kuhusu Miriam ambacho kilinisumbua, lakini sikuweza kubainisha shida iliyokuwepo.

“Nionyeshe, Bwana. Je, kuna kitu ambacho ninapaswa kuona kwa Miriam?" Niliomba.

Hakuna kilichotokea kwa siku kadhaa zilizofuata, na sikufikiria sana kuhusu hilo kwa sababu nilikuwa na shughuli nyingi mpaka wakati nikipakia mizigo yetu nyumbani ili kuhamia eneo lingine. Siku ambayo kampuni ya Kusaida kuhamisha watu ilikuja kufunga mizigo mikubwa, tulianza kutoa mito midogo ambayo ilikuwa imefungwa kwenye viti vya jikoni. Huko, chini ya mto wa kiti cha Miriam, nilikuta vitamini ishirini na sita zimeenea kuzunguka kiti. Sikuamini macho yangu. Nilimwita mume wangu ili kumwonyesha nilichopata, na sote tulicheka, ingawa tulijua kwamba tungemkabili na jambo hili atakapofika nyumbani kutoka shuleni.

Tuliendelea kufungua mito mingine mitano na, kwa mshangao wetu, chini ya yote isipokuwa mto mmoja tuligundua vitamini ishirini hadi thelathini. Kiti pekee kilicho mbali zaidi na chake ndicho kilikuwa tupu, yaani bila dawa. Safari hii tulianguka kwa kicheko.

Miriamu alipofika nyumbani kutoka shuleni, tulifuta tabasamu usoni mwetu na kumpa zawadi zaidi ya mia moja

Za vitamini na kikombe kikubwa cha maji. Tulimwambia kwamba kama hataki kunywa vitamini hizi zote basi ni vyema aelezee kile kilichotokea.

Tukio hili linaonekana kuwa la ucheshi na dogo, lakini kama udanganyifu wa Miriam haungetambuliwa na kamwe haungeshughulikiwa, ungeweza kusababisha udanganyifu mkubwa zaidi na udanganyifu huu ungepata nafasi katika maisha yake. Ninamshukuru Mungu kwamba Yeye anatufunulia mambo kama haya *kabla* hayajawa na madhara au hatari.

Si lazima dhambi za mtoto zihusike. Inaweza kuwa kuumizwa au kuogopa juu ya kitu ambacho amefikiria, ameona, au uzoefu aliopata. Inaweza kuwa kukosa tumaini, kuchanganyikiwa, wivu, ubinafsi, au kiburi. Haiwezekani kukisia, kwa hiyo ni vyema kumwomba Mungu akufunulie hilo. Hata kama hutapata mwongozo wazi mara moja, bado unaweza kusali kuhusu jambo hilo. Yesu alituagiza tuombe kwa uhakika jambo hili, "Utuokoe na yule mwovu" (Mathayo 6:13). Wakati fulani hatuhitaji kuwa mahususi zaidi ya kuomba ili Mungu apenye maisha ya watoto wetu kwa uwezo wa Roho Wake na kuwakomboa kutoka kwa uovu.

Jambo ni kwamba, usipuuze maonyo haya. Hata kama huhisi chochote kwa mtoto wako kwa sasa, bado ni hatua nzuri ya kuzuia mambo haya kwa kutoa dua na sala kama ifuatayo. Sio kwamba lazima uwe na mashaka na watoto wako milele, lakini ni lazima uwe na mashaka na adui anayejificha akingojea kuweka ngome katika maisha yao. “Iweni na kiasi na kukesha; kwa sababu mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze” (1 Petro 5:8). Mstari unaofuata huo unatupa miongozo ya jinsi ya kukabiliana na hili: *“Mpingeni,”* inasema. Je, sisi tubweteke tu, na kukaa bila kuomba?

### *MAOMBI*

*Bwana,* asante kwa kuwa umeahidi katika Neno Lako kutukomboa tunapokulilia. Ninakuja Kwako kwa niaba ya ----------- (jina la mtoto) na ninakuomba umwokoe mtoto huyu kutokana na upotovu wowote ambao unaweza kutishia kuwa ngome ya maisha yake. Ingawa mimi sijui yeye anahitaji nini ili kuwekwa huru ila Wewe unajua. Ninaomba katika Jina la Yesu kwamba ufanye kazi ya ukombozi katika maisha yake popote inapohitajika. Ninajua kwamba ingawa “tunaenenda katika mwili, sisi hatufanyi vita kwa jinsi ya mwili. Maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome, tukiangusha mabishano na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu” (2 Wakorintho 5:10)

Nipe hekima na ufunuo juu yake. Najua kuna maeneo ya operesheni za adui ambayo siwezi kuona kwa haya macho ya mwili, kwa hiyo mimi

nakutegemea Wewe Bwana, kunifunulia haya kama ninavyohitaji kuyajua. Sema na moyo wangu. Nionyeshe jinsi ya kuomba wakati kuna kitu ndani ya roho yangu, ambacho hakijatulia, kimevurugwa, au kinasumbua juu ya mtoto huyu, Baba Nionyeshe chochote nisichokiona, na kifichuke na kukaa wazi, naam yale ote yaliyofichika.

Ikiwa kuna hatua yoyote ninayohitaji kuchukua, mimi ninakutegemea Wewe unionyeshe. Asante kwa kunisaidia mimi kama mzazi wa mtoto huyu.

Bwana, ninamweka ………… (jina la mtoto) mikononi mwako leo. Mwongoze, mlinde, na uisumbue dhamiri yake wakati dhambi inapojaribu kuota mizizi. Mtie nguvu katika vita, wakati Shetani anapojaribu kupata nafasi katika moyo wake. Mfanye yeye awe makini na uvamizi wa adui, hebu na akukimbilie Wewe ili uwe ngome yake na kimbilio lake wakati wa shida. Kilio cha moyo wake kiwe, "Unisafishe na dhambi ya siri" (Zaburi 19:12). Kulingana na Neno Lako, nasema kwamba Bwana atamkomboa kutoka kwa kila kazi mbaya na kumhifadhi kwa ufalme Wake wa mbinguni (2 Timotheo 4:18). Katika Jina la Yesu ninaomba. Amen.

## SILAHA ZA VITA

Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni, na lolote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni, na lolote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni.

**MATHAYO 16:19**

Hakuna kitu kilichofunikwa ambacho hakitafunuliwa, na kilichofichwa

ambacho hakitajulikana.

**MATHAYO 10:26**

Ingawa wataungana, waovu hawatakosa kuadhibiwa; lakini wazao wa wenye haki wataokolewa.

**MITHALI 11:21**

Bwana atakuwa msaada kwa walioonewa, Na kimbilio wakati wa taabu.

**ZABURI 9:9**

Niite, Nami nitakuitikia, na nitakuonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua.

**YEREMIA 33:3**

## Sura ya ishirini na tisa

## KUTAFUTA HEKIMA NA UTAMBUZI

Je! mtoto wangu anajua kwamba kuingia kwenye gari na mtu asiyemjua ni hatari? Je, ataona dawa au msaada katika jambo fulani mahsusi? Je, atakumbuka kuangalia pande zote mbili kabla ya kuvuka barabara? Je, atamposa msichana asiyefaa na kumwambia amuoe? Je, ataweza kuhisi hatari inapokaribia? Je, atazungumza tu yale anayopaswa kuzungumza na watu ambao anapaswa kusema machache tu kwao? Kwa hivyo usalama na ustawi wa watoto wetu hutegemea maamuzi ambayo wao pekee watafanya. Matokeo ya uwezekano wa maamuzi hayo yanaweza kuonekana kuwa ya kutisha kwa mzazi.

Hatuwezi kuwa na hakika kuwa watafanya uamuzi sahihi isipokuwa wawe na karama za hekima, ufunuo, na utambuzi, pamoja na sikio lililowekwa wazi, ili kusikia sauti ya Mungu. Njia pekee ya kupata chochote kati ya mambo hayo ni kumtafuta Mungu kwa ajili yao. Biblia inasema, "Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu, wala hakemei, naye atapewa" (Yakobo 1:5).

Je, umewahi kuwa na nyakati maishani mwako ulipojua hekima ya Mungu inatawala na ukafanya uamuzi sahihi licha ya wewe mwenyewe kufikiri vinginevyo? Labda uliamua kupinda kulia katika taa za trafiki, maana hakukuwa na mtu wa kukuona, na baadaye mtu alikuja akiendesha

gari na kukungoja, wewe huwezi kuchukua sifa kwamba ndiye uliyeepusha ajali. Hekima ya Mungu inatuepusha na ajali mara nyingi. Na mara nyingi zaidi kuliko tunavyojua, inaokoa maisha yetu. Tunataka hekima na utambuzi huo huo utiririke katika maisha ya watoto wetu, hasa wanapokuwa wakubwa na kufanya maamuzi mengi muhimu bila sisi. Maamuzi fulani ambayo mwanangu alipaswa kufanya baada ya kuhitimu kutoka shule ya sekondari, yalinifanya nikae pembeni nikishusha pumzi na kuomba, "Bwana Mpe hekima, Mushi. Na awe na uongozi ulio wazi kutoka Kwako." Mungu alijibu sala hizo, na tunaona sasa jinsi maamuzi ya mwana wetu yalivyokuwa sahihi—kwa sababu ni Mungu pekee Ndiye ambaye angeweza kujua.

Mithali ya kale isemayo, "Mwana mwenye hekima humfurahisha babaye, bali mwana mpumbavu ni mzigo wa mamaye" (Mithali 10:1), hilo ni sahihi kabisa. Hakuna mtu anayeweza kuwa na kujivunia mtoto, kama Baba wakati mtoto wake anafanya uamuzi wa busara. Lakini wakati mtoto anatenda bila hekima, hakuna mtu anayehuzunika zaidi kuliko mama. Mithali pia inasema tulilie ufahamu na kuutafuta kama hazina iliyofichwa tutapata maarifa yote ya Mungu (Mithali 2:3-5).

Ninaamini hayo ndiyo maarifa yote, hekima, na utambuzi tunayoweza kuhitaji. Hebu tumlilie Mungu na tujiokoe kutoka katika baadhi ya huzuni basi, ili tusije tukawa tunapigwa kofi na kila tukio.

### *MAOMBI*

*Bwana,* ninaomba kwamba ungetoa zawadi za hekima, utambuzi, na ufunuo kwa--------- (jina la mtoto). Msaidie yeye kukutegemea Wewe kwa moyo wake wote, bila kutegemea ufahamu wake mwenyewe, bali akukubali Wewe katika njia zake zote ili apate kusikia mwongozo Wako wazi kuhusu njia ya kuchukua (Mithali 3:5-6). Msaidie yeye kupambanua mema na mabaya na kuwa mwangalifu kwa sauti ya Roho Mtakatifu akisema, "Njia ni hii, ifuate" basi hebu na aifuate (Isaya 30:21).

Ninajua kwamba furaha yake nyingi maishani inategemea kupata hekima na utambuzi, ambao Neno Lako linasema huleta, ikiwa ni pamoja na maisha marefu, utajiri, kutambuliwa, ulinzi, furaha, kutosheka, na amani ya moyoni. Nataka vitu hivyo vyote kwa ajili yake yeye, lakini nataka vije kama baraka kutoka Kwako.

Neno Lako linasema, "Kumcha BWANA ni mwanzo wa hekima, na kumjua Mtakatifu ni ufahamu"

(Mithali 9:10). Hofu yenye afya ya akili na ujuzi juu Yako iwe ndio msingi ambao juu yake yeye amesimikwa ndani yake hekima na utambuzi. Hebu na akugeukie Wewe kwa maamuzi yote ili asifanye maamuzi mabaya. Msaidie yeye kuona kwamba hazina zote za hekima na elimu zimefichwa Kwako na kwamba Wewe unatoa kwake bila malipo tunapoziomba.

Anapotafuta hekima na utambuzi kutoka Kwako, Mola, mmiminie mema kwa wingi ili njia zake zote ziwe za amani na uzima. Katika Jina la Yesu ninaomba. Amina.

## SILAHA ZA VITA

Baba yake mwenye haki atafurahi sana, naye amzaaye mtoto mwenye hekima atamfurahia na wafurahi baba yako na mama yako, na afurahi aliyekuzaa.

**MITHALI 23:24-25**

Hekima ndio jambo kuu; basi pata hekima. Na katika kupata kwako yote, pata ufahamu. Mtukuze, naye atakukweza; atakuletea heshima, unapomkumbatia.

**MITHALI 4:7-8**

Sheria ya BWANA ni kamilifu, huiburudisha nafsi; ushuhuda wa BWANA ni amini, humtia mjinga hekima.

**ZABURI 19:7**

Hekima ikiuingia moyo wako, na maarifa yatakupendeza nafsi yako, busara itakuhifadhi; ufahamu utakulinda, ili kukuokoa na njia ya uovu, na mtu anenaye mapotovu.

**MITHALI 2:10-12**

Heri mtu yule aonaye hekima, na mtu yule apataye ufahamu; maana mapato yake ni bora kuliko faida ya fedha, na faida yake ni bora kuliko dhahabu safi. Yeye ni wa thamani kuliko marijani, na vitu vyote unavyotamani haviwezi kulinganishwa naye.

Urefu wa siku u katika mkono wake wa kuume, katika mkono wake wa

kushoto utajiri na heshima. Njia zake ni njia za kupendeza, na mapito yake yote ni Amani, yeye ni mti wa uzima kwa wale wanaomshika, na wenye furaha ni wote wanaomshika.

**MITHALI 3:13-18**

## Sura ya thelathini
## KUKUA KATIKA IMANI

Ni mara ngapi nimesikia wazazi wa vijana au matineja au vijana wakisema, “Mwanangu hana hamasa ya kufanya lolote, yaani ni vigumu kumshawishi yeye kufanya lolote.” "Binti yangu huzunguka nyumbani kama vile moyo wake umenyong’onyea, kila wakati." "Mwanangu anaacha shule na haonekani kujali." "Binti yangu anaonekana kutojitambua, ni kana kwamba amepotea kwani anaishi maisha yake kama vile hayana kusudi."

Katika kila tukio, watoto hawa wanapambana na ukosefu wa maono ya maisha yao kwa sababu hawana imani katika Mungu na Neno Lake.

Watoto wasio na imani wana wakati mgumu maishani. Watoto wasio na imani hawana motisha chanya, hawana maana na kusudi, na hawana matumaini ya kuwa tofauti na hilo. Watoto wasio na imani huketi muda hata muda na siku baada ya siku, mwezi baada ya mwezi. Watoto wasio na imani huzurura mitaani wakitafuta matatizo na kwa kawaida huyapata. Watoto wasio na imani huzunguka-zunguka na watoto wengine wasio na imani, na hilo ndilo tatizo kuu la watoto ambao wako katika changamoto na shida leo.

Hawajui kwamba Yesu alikufa kwa ajili yao, hata wanapokuwa wangali bado dhambini (Warumi 5:8) na kwamba wao ni watoto wa Mungu (Yohana 1:12), ambao wanapendwa, na wana kusudi maalum na wito maalum (1 Wakorintho 7:22), na wakati ujao mzuri na nyeti (1 Wakorintho 2:9), na kwa sababu hiyo wao ni washindi hakika (Warumi 8:37). Hawajui kwamba "yote yanawezekana kwake yule aamiye (Marko 9:23), na hivyo hawaamini kuwa kuna uwezekano wowote wa maisha yao ya baadaye. Yote wanayoyaona ni mapungufu yao wenyewe na kushindwa kwao na mapambano ya watu wazima walio karibu nao, na hivyo huacha kumtegemea Bwana na kupigana mieleka na Bwana.

Lakini ni zaidi ya hayo, kwa sababu kuhisi mapungufu yetu haimaanishi kuwa hatuna imani. Ni kuhisi kwamba Mungu ana mipaka inayoonyesha ukosefu wa imani.

Na ikiwa watoto hawana imani katika kitu pekee ambacho ni salama, kisichobadilika, na chenye uwezo wote, wanawezaje basi kujiamini wenyewe na maisha yao ya baadaye, ambayo wanajua siyo salama, siyo imara, na yasiyo na nguvu?

Baada ya kulea watoto wawili tangu kuzaliwa hadi utu uzima, nimetambua kwamba jambo kuu ambalo watoto wetu watachukua wanapoondoka katika eneo letu la mvuto/ushawishi ni imani kwa Mungu.

Ikiwa tunaweza kuwa na uhakika kwamba wana imani yenye nguvu

katika Mungu na Neno Lake, na upendo wa Mungu mioyoni mwao, basi tunaweza kujua wamewekewa umilele. Maombi yetu yanaweza kuwa na sehemu kubwa katika kuwasaidia kufikia hilo.

Mitume, waliokuwa pamoja na Yesu kila siku, wale ambao walimsikia akifundisha na kutazama kile alichofanya, bado iliwabidi kumwomba, "Tuongezee imani" au hata "Tufundishe jinsi ya kuomba" (Luka 17:5 na Mathayo 6). Hakika *sisi* tunaweza kuomba vivyo hivyo kwa watoto wetu. "Bwana, waongezee Watoto wetu imani."

Waisraeli, ambao walijionea miujiza mingi kuliko tutakavyowahi kuona, hawakuruhusiwa kuingia katika Nchi ya Ahadi kwa sababu ya kutoamini kwao (Waebrania 3:19). Katu sisi hatutaki ukosefu wa imani kuwazuia watoto wetu wasiingie katika yote ambayo Mungu ameahidi kwa ajili yao. Tunaweza kuwafundisha Neno la Mungu, ambalo hupanda imani ndani yao, na tunaweza kusali ili imani yao ikue.

Watoto walio na imani wana tabia tofauti kabisa na wale wasio na imani. Wanajiamini zaidi, wanahamasishwa zaidi, wanafurahi zaidi, wanaishi kwa mtazamo chanya zaidi juu ya siku zijazo, na kujitolea zaidi. Kwa kweli, mojawapo ya maonyesho makuu ya mtu mwenye nguvu katika imani ni uwezo wa kutoa—si kwa pesa au mali tu, bali pia wakati, upendo, kitia-moyo, ushauri na msaada. Mtu wa imani amejazwa na upendo wa Mungu na anatafuta fursa za kushiriki upendo huo na wengine.

Biblia inasema, "Basi inadumu imani, tumaini, upendo, haya matatu;

lakini lililo kuu katika hayo ni upendo" (1 Wakorintho13:13). **Mbinguni, imani haitakuwa muhimu kwa sababu tutakiona kila kitu uso kwa uso. Tumaini halitahitajika kwa sababu tunaweza kutumaini nini zaidi?**

**Upendo pekee ndio utakaodumu** milele, kwa sababu Mungu ni upendo na *Yeye* ni wa milele. Ndiyo maana haijalishi ni kitu gani kikubwa tunachofanya au tunatoa kiasi gani; ikiwa vitu hivi havijafanywa kwa upendo, haina maana. "Nikitoa mali yangu yote kuwalisha maskini, tena nijapoutoa mwili wangu uchomwe moto, kama sina upendo, haunifai kitu" (1 Wakorintho 13:3). Kila kitu tunachofanya kwa upendo kitadumu milele na thawabu ni za milele.

Upendo ndio fadhila kuu. Ni kuu hata kuliko imani. Lakini katika imani, ndipo unapoanzia huo upendo. Ndiyo maana tunapaswa kuomba kwamba imani inapoongezeka kwa watoto wetu, wawe vyombo vya Mungu vya utoaji. Sababu mojawapo ambayo watu hawatoi ni kwamba wanaamini kuwa vitu au fedha hazitawatosha au kukidhi mahitaji yao wakifanya vile; lingine ni kwamba hawana upendo wa Mungu mioyoni mwao kwa wengine. Omba kwamba kanuni ya **kutoa**—kutokana na upendo, kama kwa Bwana, kwa imani, *kwa hekima* na uongozi wa Roho Mtakatifu— kutiwe ndani ya mioyo na akili za watoto wako, kwa sababu wanapoishi ipasavyo, wanahakikishiwa kubarikiwa sana na kuwa na raha na kuridhika moyoni kwamba mambo muhimu na makuu yametimizwa katika maisha yao.

Katika eneo lolote la wasiwasi au tashwishwi, tunapoanza kuomba kwa kina kwa ajili ya mtoto wetu, mara nyingi tunakutana uso kwa uso na hitaji

letu la maombi, ukombozi, na urejesho. Je, tunawezaje kuomba kwa ufanisi kwa watoto wetu kuwa watu wa kusamehe ikiwa tunahifadhi kutosamehe katika mioyo yetu wenyewe? Je, tunawezaje kuwaombea wawe na uwezo wa kutubu ikiwa tuna dhambi amba*yo* haijaungamwa? Je, tunawezaje kumwomba Mungu awafanye watoto wetu wajazwe Imani, wakati sisi wenyewe tunapambana na mashaka? Je, tunawezaje kuwaombea wawe watoaji wakati sisi tuna wakati mgumu kutoa? Mimi hutiwa hatiani kwa mambo hayo pia. Lakini siruhusu hilo linizuie kuomba. Ninaenda mbele za Bwana kwa moyo mnyenyekevu, nikikiri kile ninachokiona ndani yangu na kumwomba msaada tu, kwani sina mahali pengine.

Ikiwa, kwa mfano, unahisi kuwa huna imani ya kutosha, ungama kwa Mungu na usali sala iliyo mwisho wa sura hii na weka jina *lako* ndani yake kabla ya kuomba kwa ajili ya mtoto wako hiyo imani. Biblia inasema kwamba "Lolote lisilotokana na imani ni dhambi" (Warumi 14:23). Ikiwa tuna shaka, hatumtii Mungu. Ikiwa tuna imani, tunakuwa watiifu. Shaka huja kwa kuamini kwamba Mungu si mweza wa yote. Usiruhusu ukosefu wako wa imani kuweka ukuta kati yako na Mungu. Hebu huo ukosefu wako, uwe mwaliko wa kumkimbilia Mungu kwa maombi, ukimwomba akuongezee imani *yako* na ya *mtoto wako.*

Kumbuka kwamba nguvu uliyo nayo kama mzazi anayeomba ni nguvu za Mungu. Maombi yako yanaachilia nguvu hiyo ya kufanya mapenzi ya Mungu. Nguvu na uwezo huu, unapatikana kila wakati, nao haupungui kamwe, na kizuizi pekee ni ukosefu wa imani kwamba, Mungu atajibu.

Na hata hivyo, neema ya Mungu ipo, kwamba pale ambapo hatujisikii tuna imani nyingi, na imani tuliyo nayo ni kama punje ya haradali tu— basi imani hiyo inatosha kitu kukua na kuwa kitu kikubwa sana. Hebu tuungane na wazazi wengine wanaoomba na kusema, “Mbegu za imani yetu, zilizopandwa katika maombi, zizae uhai na kukua kwa watoto wetu mpaka wawe majitu (giants) wanaofuata moyo wa Mungu.”

***MAOMBI***

Bwana, umesema katika Neno Lako kwamba “umemgawia kila mtu kiasi cha imani” (Warumi 12:3). Ninaomba kwamba uchukue imani uliyoipanda kwa ----------(jina la mtoto) na kuizidisha. Kweli ya Neno Lako isimamishwe kwa uthabiti ndani ya moyo wake, ili Imani hiyo ikue kila siku na kuendesha maisha yake. Msaidie yeye akuamini Wewe, wakati wote anapokutazama Wewe, afundishwe Ukweli, apate mwongozo, na apate mabadiliko na kuakisi sura yako. Ninakutumaini Wewe kumwezesha yeye kufanya chaguo hilo. Ninaomba kwamba yeye atakutazama kwa kila kitu, akijua kwamba yeye hana tumaini kamwe, isipokuwa kutoka Kwako tu. Imani yake na iwe “na hakika ya mambo yatarajiwayo, bayana ya mambo yasiyoonekana” (Waebrania 11:1). Ninaomba kwamba atakuwa na imani yenye nguvu za kutosha ya kumwinua yeye juu ya hali yake na mipaka yake na kutia ndani yake ujasiri wa kujua kwamba kila kitu kitafanya kazi pamoja kwa wema (Warumi 8:28).

Ninaomba kwamba yeye atakuwa na nguvu sana katika imani kiasi kwamba uhusiano wake na Wewe utashinda yote mengine katika maisha

yake—na hata ushawishi wangu kama mzazi. Kwa maneno mengine, na awe na uhusiano na Wewe, Bwana, huo aumiliki kama ni wake kweli—na sio mwendelezo wa Imani kutoka kwangu au kwa mtu mwingine yeyote. Nataka faraja ya kujua kwamba nitakapokuwa sipo tena katika dunia hii, imani yake itakuwa na nguvu vya kutosha kumweka yeye "imara, asiyetikisika, akizidi sana daima katika kazi ya Bwana" na hata kuwasaidia wengine pia kukuza Imani yao (1 Wakorintho 15). :58).

Anapotembea katika imani, hebu na awe na moyo wako wa upendo unaofurika kwa wengine, moyo ambao uko tayari kujitolea kwa hali na mali kulingana na uongozi Wako. Hebu na aone kwamba kutoa kwa upendo ni hakika na kweli kuwa ni kurudisha Kwako kwa imani na kwamba yeye hatapoteza chochote kwa kufanya hivyo. Ninaomba achukue "ngao ya imani" ili "kuzima mishale yote yenye moto ya yule mwovu" (Waefeso 6:16), na hivyo aweze kusimama imara katika imani na kusema, "Mimi namshukuru Kristo Yesu Bwana wetu aliyenitia nguvu, kwa maana alinihesabu kuwa mwaminifu" (1 Timotheo 1:12). Katika Jina la Yesu ninaomba. Amina

**SILAHA ZA VITA**

Pasipo imani haiwezekani kumpendeza, kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba Yeye Yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wanaomtafuta kwa bidii.

**WAEBRANIA 11:6**

Kwa hiyo nawaambia, Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.

**MARKO 11:24**

Mkiwa na imani kiasi cha punje ya haradali mtauambia mlima huu, Ondoka hapa uende kule; na hakuna ambalo halitawezekana kwenu.

**MATHAYO 17:20**

Lakini na aombe kwa imani, pasipo shaka yoyote; maana mwenye shaka ni kama wimbi la bahari lililochukuliwa na upepo, na kupeperushwa huku na huku. Mtu kama huyo asidhani ya kuwa atapokea kitu kwa Bwana; ni mtu wa nia mbili, asiye na msimamo katika njia zake zote.

**YAKOBO 1:6-8**

Wala tusichoke katika kutenda mema, maana tutavuna kwa wakati wake tusipozimia moyo. Kwa hiyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema, hasa jamaa ya waaminio.

**WAGALATIA 6:9-10**

## Sura ya thelathini na moja

## KUPITIA MAISHA YA UJANA KWA MAFANIKIO

Hii ni sura mpya kabisa ninayoongeza kwenye toleo hili la *mazungumzo haya ya nguvu ya mzazi anayeomba au kuombea Watoto wake kama mwendawazimu.* Ulimwegu wetu wa utandawazi umefanya mambo kubadilika sana katika utamaduni na wakati wetu—hasa linapokuja suala la watoto. Watoto wetu wanakabiliwa na uovu mwingi na makosa ya kiroho kuliko sisi wazazi tulivyowahi kukabiliwa, wakati wa umri wetu mdogo kwani adui ameongeza hasira na moto wa vita, akijua muda wake ni mfupi. Kile ambacho tunaweza kuwa tumekabiliwa nacho katika ujana wetu tukiwa na miaka ishirini na kitu, watoto leo wanakabiliana navyo wakiwa na miaka tisa au kumi Kwa sababu miaka ya utineja ya kila mtu ni mikali na maisha hufinyangwa hapa, ni vyema wawe imara mara zote kwa kadri inavyowezekana, kwani huathiriwa na kile wanachojifunza na kile kinachotokea kwao katika msimu huu wa maisha yao. Kama wazazi, lazima tuwe tunawaombea watoto wetu miaka ya ujana *kabla ya* kufika huko. Inatubidi tuwafunge mshipi wa maombi kabla ya wakati wanapopitia

mlango huo wa shule ya msingi na sekondari, kwa sababu mapigo yatokayo kwa roho ya mpinga-Kristo, ambayo imekita mizizi katika ulimwengu yatawajia kwa kasi ya radi na yatapiga popote pale penye udhaifu.

Watoto wako wana adui—adui wa kiroho—vivyo hivyo nawe fanya kama unajua kabisa kwamba una maadui wa kiroho. Huwezi kupuuza ukweli huo, na lazima watoto wako wasiruhusiwe, kupuuza pia. Watoto wako wachanga wanapaswa kufahamishwa juu ya kile kilicho nje - ikiwa sio kwa undani au uwazi kabisa, basi angalau katika roho. Uovu wa ulimwengu utawalenga vijana wako kwa vishawishi vya kilimwengu na uvutano usio wa Kiungu, na kuwavuta kuamini uwongo juu yao wenyewe. Hawawezi kupinga hayo yote peke yao bila kutiwa moyo, hekima, mwongozo, upendo, na usaidizi wa maombi.

Watoto wetu wapo vitani, makombora yanaanguka kushoto na kulia kwao. Vita ya muda mfupi kupita zote ilipiganwa kwetu hapa Zanzibar Mwaka 1896 kwa dakika 38 tu, kati ya Oman na Uingereza. Sultani wa Oman alijisalimisha na Waingereza wakakichukua kisiwa hicho. Vita kubwa na ya muda mrefu kupita zote ilianzia mbinguni ambapo Shetani alitaka kumpindua Mungu na achukue uongozi (Ufunuo 12). Alishindwa vita hivyo na akatupwa chini hapa, na yupo kibaruani zaidi ya miaka 6000 na bado hajajisalimisha mpaka leo. Nia yake ni kumfanya mwanadamu awe upande wake katika vita ili apate adhabu naye, karamu ya adhabu yake ya mwisho aliandaliwa mwenyewe tu, hivyo hatuna haja kwenda kwenye karamu tusiyoalikwa (gatecrash). Silaha Saba za Waefeso sita ni lazima zivaliwe na kila anayetaka kushinda, na hili wana wetu wanapaswa kulitambua. Muhtasari wa Maandiko ni

maneno matatu tu-(Uumbaji, Maanguko, Ukombozi)-Uumbaji katika Mwanzo moja na mbili, Maanguko katika Mwanzo tatu na Ukombozi, ni kuanzia Mwanzo Nne Mpaka Ufunuo ishirini na mbili. Mungu alileta manabii nao wakapigwa vita mwishowe anamleta Mwanawe, Naye anazaliwa na kuishi na Kufa, na kupaa, na sasa anafanya kazi ya upatanishi kwetu sisi na watoto wetu. Anatuombea kutokana na kitabu cha Waebrania 8-10, na hivi karibuni atatokea Mawinguni. Tunaona viashiria vingi vya Yeye kutokea hivi punde. Kitabu hiki ni cha kila binadamu kukisoma, hasa kwa wakati huu tunaoishi. Tuombeane. Tunakaribia nyumbani! MASIHI Anakuja upesi! Ukiwa na mashaka na Historia yoyote ya Biblia mfano Danieli, tafuta vitabu vya historia halisi kama vile vya mitaala ya shule au google mtandaoni ili uthibithishe mwenyewe! Biblia inaendana na historia ya mwanadamu na ndicho kitabu cha dini pekee ambacho kinaendana na historia ya kweli ya mwanadamu. Historia hii ni pungufu ya miaka 6000. Maana katika kila nchi watu huanza kusoma kuhusu Mesopotamia kama historia iliyothibithishwa, miaka 5000+ iliyopita, hawataji mwaka wa milioni moja nini kilitokea au 3,000,000 KK! Biblia ndiyo kitabu pekee cha Maandishi ya Kale chenye kukubalika na kuaminiwa zaidi, cheye Ukweli, naam chenye ithibati kupita maandiko mengine yoyote ya kale (the most authentic document in ancient writings-Luka na Matendo vilichukuliwa kuthibithisa jambo hili)

Ikiwa tuna muda wa kuomba na kuombea watoto wetu, Mungu atatujibu. Maombi haya matatu yanakuja na baraka zote:

1. Roho Mtakatifu
2. Kujisalimisha kwa MUNGU na
3. Kuwa ndani Yake Mungu.

Basi mambo muhimu kwa Kila Mwanadamu ni haya saba tukimsubiri Masihi

1. Kumkiri Mungu na kutubu dhambi zetu
2. Kusali daima
3. Kusoma Neno Lake Mungu Kila siku
4. Kuishi mtindo wa maisha kutokana na Maandiko
5. Kuwaambia wengine habari Njema yaani Ukweli
6. Kuhudhuria ushirika unaofuata Maandiko
7. Huduma za Jamii

Kutokuwa na tumaini kunakowapata vijana wenye huzuni au waliovunjika moyo ambao hawana mwelekeo na wanaamini kwamba hawana wakati ujao ni janga.

Na ni vivyo hivyo kwa vijana waasi, wanaojiweka wenyewe kama kipaumbele cha ulimwengu wao, na sio Mungu kuwa kitovu cha ulimwengu wao. Kinachohitajika tu, ni ushawishi *mmoja* mbaya, na huu hupanda *mara* Moja mbegu *moja* mbaya katika nafsi ya mtoto, na hii inaweza kukua bila kutambuliwa mpaka siku *moja* unashangaa nini kilichotokea kwa mtoto huyo wa ajabu uliyemlea. Habari njema, hata hivyo, ni kwamba unaweza kuwa shujaa wa maombi na kwenda vitani dhidi ya nguvu za uovu kwa niaba ya mtoto wako. Kama mzazi, uko kwenye vita kwa ajili ya maisha ya mtoto wako, na maombi *ndiyo* vita.

Jambo moja muhimu sana la kuzingatia ni kama watoto wako wana furaha na wanastawi katika kanisa ambalo wewe na wao huhudhuria. Kuwa na furaha katika kundi la vijana kanisani ni jambo muhimu kwao.

Uamuzi kuhusu ni kanisa gani la kuhudhuria lazima utegemee mahali ambapo watoto wako wanatamani kwenda na watafanikiwa. Mahali ambapo wanapata mafunzo, wana marafiki na wanaona hakuna usumbufu kwao au mahali wanapopata faraja.

Na hilo litaamuliwa ikiwa wanahisi kuwa wanakubalika, wanathaminiwa, na wanahamasishwa huko, na ikiwa wanatiwa nguvu na kuongozwa na Neno la Mungu. Iwapo hawahisi upendo wa Mungu hapo, basi tafuta kanisa wanakohisi haya mambo mema. Mapema unapopata mahali hapo ni bora zaidi.

Katika kuchagua kanisa, hakikisha watoto wako wanalipenda—kwamba programu kwa ajili ya watoto na hasa vijana wa kabla ya utineja na matineja ni nzuri, na inayosimamiwa na watu wema, wacha Mungu waliojitolea kusaidia. Vijana wanamjua na kumpenda Bwana, wanaamini Neno Lake, na kuelewa kwamba ana mpango mzuri kwa maisha yao. Bila kufahamu kusudi la Mungu kwao, wanaweza kutanga-tanga bila kusudi, kuvunjika moyo, kuathiriwa na mvuto mbaya, na kumwacha Mungu. Je! unajua ni watoto wangapi wanaishia kwenye madhehebu fulani au magenge kwa sababu ni mahali pekee ambapo walipata upendo na kukubalika? Jibu ni, *wengi mno!*

Kadiri watoto wako wanavyokuwa wamejirekebisha vizuri zaidi kanisani *kabla ya* kufikia miaka yao ya utineja, ndivyo watakavyokuwa bora zaidi. Ikiwa hawataki kushiriki ibada wakiwa watoto au vijana, hii haitawaletea ishara nzuri wanapokuwa nje ya udhibiti wako baada ya kuhitimu na

kwenda chuo kikuu au kufanya kazi. Wanaweza kuacha kanisa kabisa na wasirudi kwa miaka mingi—au wasirudi kabisa. Haya yanatokea sasa kwa kasi ya kutisha.

Mahali ambapo watoto wako huenda shuleni ni muhimu pia, wazungu wanasema location, location na location yaani mahali- mahali- mahali.

Rafiki yangu wa karibu aliona jinsi binti yake mdogo—ambaye alikuwa amekaribia miaka yake ya utineja—alikuwa ameanza kupata maksi mbaya ghafla, hakutaka kwenda shuleni, na alionekana mwenye huzuni, kuvunjika moyo, na woga wakati wote. Pia mara nyingi hakwenda shule kwa sababu ya ugonjwa. Mama yake aliitwa mara kwa mara kwenye ofisi ya shule na kugundua kuwa binti yake amepata shida.

Hakuna hata moja ya mambo haya yalikuwa yametokea katika miaka iliyopita. Kwa hiyo mama na mimi tuliomba pamoja kwa ajili ya binti yake, na kama tulivyofanya nilihisi Roho Mtakatifu akifunua kwamba binti yake alikuwa akionewa (bullied). Nilimwambia mama, "Unahitaji kumwondoa binti yako katika shule hiyo. Muulize Mungu kuhusu kuhamia shule nyingine katika mfumo wa elimu wa wilaya tofauti."

Ninampongeza mama huyo kwa kufanya hivyo haraka iwezekanavyo. Baada ya hatua hiyo bintiye alifichua kuwa kweli kulikuwa na wasichana kadhaa wakorofi katika shule ya awali ambao walikuwa wakimnyanyasa kila siku. Alianza kuogopa na alihisi kukata tamaa kuhusu hilo kwa sababu hangeweza kumwambia mama yake, au mtu yeyote katika

uongozi wa shule, kwa kuhofia wasichana wangekaripiwa na kulipiza kisasi kwake jambo ambalo lingekuwa la hatari zaidi.

Mara tu binti yake alipoanza kuhudhuria shule mpya, kila kitu kilibadilika mara moja. Alipata maksi nzuri tena darasani. Hakuwa tena na huzuni na woga. Akawa na afya nzuri ya kimwili. Alifurahia kwenda shule na hata akaanza kupanga mipango ya maisha yake ya baadaye baada ya shule ya sekondari. Leo macho yake yameelekezwa kwenye kazi maalum na sasa anasoma chuo ambacho kinaweza kumsaidia kufikia malengo hayo. Yeye ni mtu tofauti na alivyokuwa katika shule yake ya zamani. Na kizuri zaidi, yeye na mama yake walipata kanisa kubwa katika eneo jipya wanalolipenda wote wawili. Hii ilihitaji kujitoa sana kwa mama huyo kwa sababu sasa ilibidi aendeshe mwendo safari ndefu kwenda kazini. Lakini ulikuwa uamuzi sahihi kabisa, na wote wawili walikuwa na furaha walipofuata uongozi wa Roho.

Hautakuwa umeharakisha kuanza kuomba kwa ajili ya miaka ya ujana ya mtoto wako, kwa sababu ukifika miaka hiyo utasikia sauti kubwa ya kuogofya, na itakuwa adui wa nafsi zao kujaribu kuwanyang'anya na kuwatisha watoto wako. Usiruhusu hilo litokee. Una zana za kuizuia kwa kuwa shujaa wa maombi kwa watoto wako. Hata kama watoto tayari ni vijana, hujachelewa kuanza kusali. Wewe una Mungu na Neno Lake upande wako. Ikiwa umempokea Yesu, basi una uwezo wa Roho Mtakatifu ndani yako akikupa hekima, utambuzi, nguvu, upendo, na nguvu zaidi yako mwenyewe—na kila kitu unachohitaji ili kushinda

vita hivi. Dai ahadi za Mungu kwa mtoto wako kwa ufalme wa Mungu. Dai ahadi za Mungu kwako na kwa watoto wako katika Neno Lake. Anza na, "Nitamimina Roho Wangu juu ya uzao wako, na baraka Yangu juu uzao wako" (Isaya 44:3). Nguvu zote za kuzimu haziwezi kuja karibu na kumpinga Roho Mtakatifu aliyemiminwa juu ya maisha ya watoto wako kwa kujibu maombi yako.

## *MAOMBI*

*Bwana,* ninaomba----------- (jina la mtoto) awe na moyo wa kukufuata Wewe. Fanya kazi ndani yake ili avutwe daima kuelekea Kwako. Mnyamazishe adui akijaribu kumvuta katika mawazo ya kidunia, mitazamo, na matendo ambayo hupingana na mapenzi Yako na njia Zako. Msaidie asikie sauti Yako katika nafsi yake. Mweke mbali na machafuko ya dunia ili aweze kufanya maamuzi sahihi na maamuzi ya wazi yanayokupendeza Wewe. Zuia kila uvamizi wa adui kupata mapokezi yoyote ndani ya moyo wake.

Mtie nguvu ili apinge shinikizo la rika ambalo lingemvuta yeye katika jambo lolote ambalo halikuheshimu Wewe. Nisaidie mimi na wanafamilia wengine kumpenda yeye kwa njia ambayo inawakilisha wazi upendo Wako kwake yeye. Kuza ndani yake yeye hiyo hisia ya uwepo Wako na upendo wako ili kwamba kamwe asitake kujitoa kutoka kwako.

Nifunulie kama yeye yumo katika shule sahihi na kanisa linalofaa. Nionyeshe ni wapi yeye atastawi na atapenda kuhudhuria kila wakati.

Nionyeshe ikiwa tunapaswa kufanya mabadiliko ya aina yoyote. Ninaomba usiwepo mpango wa adui utakaofaulu kumvuta yeye mbali na Wewe. Ikiwa adui tayari amepata msingi wowote ndani yake kupitia Runinga, Mtandao, muziki, au watu wengine, naomba ungekatilia mbali kishawishi hicho na kuvunja mvuto wowote wa ulimwengu. Mlinde dhidi ya wanyanyasaji au waonevu wa aina yoyote. Mfiche yeye katika kivuli chako kutokana na hatari hizo. Onyesha ushawishi wowote mbaya. Ninadai ahadi kwa --------- (jina la mtoto) kwa Mipango na makusudi Y*ako* pekee. Katika Jina la Yesu ninaomba. Amen.

**SILAHA ZA VITA**

Nitamimina maji juu yake aliye na kiu, na mito juu ya nchi kavu; Nitamimina Roho Yangu juu ya uzao wako, na baraka yangu juu ya uzao wako; watamea kati ya majani kama mierebi kando ya mifereji ya maji.

**ISAYA 44:3-4**

Nitashindana naye anayeshindana nawe, Nami nitawaokoa watoto wako.

**ISAYA 49:25**

Tokeni kati yao na mjitenge, asema Bwana. Msiguse kitu kichafu, Nami nitawapokea. Nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa Kwangu Wanangu wa kiume na wa kike, asema BWANA Mwenye Nguvu Zote.

**2 WAKORINTHO 6:17-18**

Basi angalieni jinsi mnavyoenenda; si kama wapumbavu, bali kama

watu wenye hekima, mkiukomboa wakati kwa maana zamani hizi ni za uovu.

**WAEFESO 5:15-16**

Anayejidhania kuwa amesimama na aangalie asianguke.

**1 WAKORINTHO 10:12**

# 10 Morning Prayers FOR KIDS EACH DAY

**1. Simple Morning Prayer**
Father God, thank you for this new day. Help me to use it wisely and to do things that will please you. I pray for your thoughts, not my own, and that I will be a blessing to others. In Jesus' name, Amen. Isaiah 55:9

**2. Prayer For A New Day**
Father God, thank you for this new day. Each day you give us is a blessing and another opportunity to glorify you. Help me honor you today. In Jesus' name, Amen. Lamentations 3:22

**3. Morning Prayer For Thankfulness**
Father God, thank you for who you are and for this day. Remind me to give thanks in every situation, and know that you are good always. Thank you. Amen. Thes 5:17-18

**4. Prayer For Family**
Father God, thank you so much for my family. Help me to bless them today. I pray that you will help me humble myself and put others before me. Amen. Phil 2:3

**5. Prayer For Friends**
Father God, help me to choose my friends wisely. Surround me with friends who will encourage me with your Word. Also, help me to be a blessing to my friends. In Jesus' name, Amen.

**6. Prayer For Attitude**
Father God, help me to act like Jesus today. Help me to respond to people like you would. Help me follow Jesus' example. In your name I pray, Amen. 1 Cor 11:1

**7. Affirming Morning Prayer**
Father God, thank you for making me a new creation. Remind me that I don't have to live like I used to. Because of Jesus, you have forgiven me and made me new. Amen. 1 Cor 5:17

**8. Prayer For God To Guide Me**
Father God, thank you for who you are and for this day. Remind me to give thanks in every situation, and know that you are good always. Thank you. Amen. Thes 5:17-18

**9. Rhyming Morning Prayer**
Teach me now my heart to raise In a morning hymn of praise; And for Jesus' sake I pray, Bless and keep me through the day. Psalm 136:1

**10. Lord's Prayer**
Read Matthew 6:9-13 in your Bible or with a parent!

www.mindyjonesblog.com

# SEHEMU YA PILI

# JINSI YA KUOMBEA WATOTO WAKUBWA

## Sura ya thelathini na mbili

# KUWAOMBEA WATOTO WAKO WAKUBWA

Haijalishi watoto wapo katika umri mkubwa kiasi gani, daima wataendelea kuwa watoto wako. Hawakosi kamwe kuhitaji upendo wako na kibali chako, ushawishi wako na heshima yako, au tegemeo lako kwa hisia zao za kina kihisia na kiroho. Nawe utaendelea kutamani mema ya Mungu katika maisha yao. Daima utataka walindwe na kuhudumiwa, wakue katika kumjua Bwana, watimize kusudi la Mungu wao, na kuwa kama Mungu alivyowaumba wawe. Watoto wako wanapokuwa sehemu ya maisha yako, sehemu ya moyo wako itakuwa nao kila wakati, haijalishi wanaenda wapi au wanafanya nini.

Niliandika kitabu hiki, wakati watoto wangu wakiwa wameondoka nyumbani kwenda chuo kikuu, sasa wamerudi, na kuondoka nyumbani tena mpaka wakawaweza kujitegemea kimaisha. Nimewaona wakikua na kuwajibika katika maisha yao ya kikazi na kibinafsi. Wamejifunza baadhi ya masomo magumu, na wamepata hekima kutokana na makosa yao, na wameelewa ni nini kinachofaa na kisichozaa matunda. Wamekaa kanisani na kukua katika Neno la Mungu. Wanaelewa nguvu ya maombi na wamekuwa watu wenye nguvu ya kuomba peke yao. Wamejifunza kufanya maamuzi mazuri—na Mungu amewasaidia Kuhusu watu waliowachagua kuoana nao. Sala zetu hazijapata kujibiwa kwa kina zaidi katika nyanja hii, na tunamshukuru Mungu kila siku kwa hilo.

Katika kipindi cha miaka thelathini na mitano iliyopita, mimi na mume wangu tumeunda vikundi vingi vya maombi nyumbani mwetu ili kuwaombea hasa watoto wa wazazi hao waliokuwa kwenye kikundi, nasi hatujapoteza hata mtoto mmoja. Sisemi kwamba hakuna hata mmoja wa watoto hawa aliyewahi kuwa na matatizo. La! Hilo hata lisingekuwa la kiafya au hata Kimaandiko. Ikiwa mtoto hatapatwa na matatizo yoyote au kukatishwa tamaa, ataelewaje basi, uhitaji wake kwa Mungu? Angekuwa katika hatari ya kuharibiwa, kulindwa kupita kiasi, kutojali, kutowajibika, au kutumbukia mahali. Tunataka watoto wetu wajifunze kuwajibika, kuwa na upendo mwanana, kujali, huruma, ukarimu, rehema na uelewa. Tunataka wapate ujuzi unaohitajika kushughulikia kile ambacho maisha yanawatupia. Je, watamjuaje Mungu kama msaidizi wao, mlinzi, mpaji, au mwokozi

ikiwa hawamhitaji Yeye kamwe kuwasaidia, kuwalinda, kuwapa, au kuwaokoa? Watoto hawa wote walipitia mambo, lakini waliibuka kupitia hayo wakiwa na nguvu, busara, na huruma zaidi kuelekea mapambano ya wengine. Maombi yanafanya kazi! Hata utafiti wa kisayansi umehakikisha!

## Jinsi Ya Kuombea Watoto Wako Wanapoondoka Nyumbani

Watoto wako wanapoenda ulimwenguni peke yao, maombi Yako hayatakoma. Kwa kweli, yanaweza hata kuongezeka kwa sababu huna tena jukumu la kila siku ulilokuwa nalo kwao. Maombi yanaweza kuwa njia yako pekee yenye nguvu. Lakini usipunguze umuhimu wa hilo. Kwa sababu watoto wako bado ni watoto wako, maombi yako daima yatakuwa na matokeo makubwa katika maisha yao. Huenda usiweze tena kuwaambia la kufanya, lakini kwa hakika unaweza kutangaza kile ambacho adui hawezi kufanya jambo linapokuja kwao. Unaweza pia kumwambia Mungu kila kitu kilicho moyoni mwako kuhusu watoto wako.

Unaweza kumwambia Mungu jinsi gani ungependa kumuona Yeye akitembea katika maisha yao. Katika maombi utaunganishwa kwa nguvu na watoto wako watu wazima, na watapata matokeo ya maombi yako. Huo ni ushawishi mkubwa na wa ajabu! Kama vile ambavyo hatujui umeme unavyofanya kazi, lakini bado tunaweza kupata faida yake, maombezi kwa watoto wetu au watu, huleta tofauti, kwamba inakuwaje-kuwaje, sisi hatujui ila Mwenyezi Mungu ametuagiza kuomba kwa ajili ya wengine, na kwa kufanya hivi Yeye atafanya yale ambayo pengine asingeweza kufanya katika ulimwengu wa pambano kati ya milki ya Bwana na ya uovu na

mapepo.

Ikiwa una mtoto ambaye amekua na kuondoka nyumbani kwenda chuoni au kutafuta njia ya ulimwengu, ongeza sala fupi zifuatazo kwenye sala mwishoni mwa kila sura iliyotangulia. .

Hivi ndivyo ninavyowaombea watoto wangu walio watu wazima, na inanipa amani kujua kwamba Mungu anasikia maombi yangu. Wazazi wote wa watoto wakubwa wanahitaji aina hiyo ya amani.

## Omba Maombi Yafuatayo kwa WATOTO WAKO WAKUBWA

### 1: Kujiombea kama Mzazi

*Bwana,* nionyeshe jinsi ya kuomba hasa kwa ajili ya mtoto wangu sasa kwa kuwa siko naye mara kwa mara. Nakutegemea Wewe unipe maarifa na moyo wa upendo. Nionyeshe mambo ninayohitaji kuona na jinsi ninavyopaswa kuomba. Nisaidie niwasilishe upendo wangu mwanana kwake na kujitolea kwangu kumuombea daima kwa njia ya kutia moyo. Mpe shauku ya kuwasiliana na mimi na kuhitaji maombi yangu na ushauri akijua na nikijua kwamba ninaweza kuaminiwa kumsaidia mambo yote kwa heshima na usiri. Mpe shauku ya kupokea simu yangu napomwita!

### 2: Kumwachilia Mtoto Wangu Mikononi mwa Mungu

*Bwana,* kadiri mtoto wangu anavyoimarisha maisha yake ya kujitegemea,

ndivyo sina chaguo ila kumwachilia mikononi mwako kabisa. Njia pekee ninayoweza kujisikia salama juu yake, ni kujua kwamba yeye anaendelea kuishi chini ya udhibiti Wako. Nimefanya yote niwezayo kumfanyia, kwa hivyo ninamwachilia----------- (jina la mtoto mzima) mikononi Mwako na kukutegemea Wewe kuwa msimamizi wa maisha yake. Hata kama simwoni kila siku, najua kuwa Wewe unamwona. Ninakuamini kwamba utamhifadhi katika njia Zako kwa ajili yake.

**3: Kujikinga dhidi ya hatari**

*Bwana,* ingawa siku zote sijui mtoto wangu yuko wapi, Wewe wajua. Asante kwa kuwa unaweka macho yako kila wakati kwake, ili kumlinda dhidi ya hatari. Asante kwa kuwa hakuna silaha itakayorushwa dhidi yake itakayofanikiwa.

Popote atakapokuwa, atakapoenda, atakaporuka, au anapotembea, mzuie, mzunguke na Malaika Wako. Mwongoze mbali na hatari na mbali na mipango yoyote miovu ya ushawishi mbaya.

**4: Kujisikia Kupendwa na Kukubaliwa**

*Bwana,* najua ya kuwa unawafadhili wale wakupendao. Ninaomba kwamba--------(jina la mtoto mkubwa) ajifunze kukupenda Wewe zaidi kila siku na kufurahia kibali Chako katika maisha yake. Na apate upendo na kukubalika popote aendako. Mwezeshe kufurahia kibali na watu wote, kuanzia wanafamilia, marafiki, na wafanyakazi wenzake hadi marafiki wa kawaida na wageni. Hebu na azidishe upendo na kukubalika kwa wengine

kwa njia inayokupendeza Wewe.

**5: Kuanzisha Wakati Ujao wa Milele**

*Bwana,* ninaendelea kuomba kwa ajili ya uhusiano----------- (jina la mtoto mkubwa) alio na Wewe. Daima uhusiano wake na Wewe uwe na nguvu na usioyumbayumba. Daima uhusiano uwe thabiti na bila kuporomoka. Naomba kisiwepo chochote katika dunia kitakachopofusha macho yake asikuone Wewe ni nani, na kufanya kazi Yako ndani yake. Ninaomba kwamba asitange mbali na uso wako au kujazwa na shaka juu ya wokovu wake ndani yako, Yesu. Maisha yake ya baadaye na Wewe, hebu na yawe salama daima.

**6: Kuwaheshimu Wazazi na Kupinga Uasi**

*Bwana,* naomba kwamba---------- (jina la mtoto mtu mzima) hatakataa mambo mazuri aliyofundishwa kwa kufanya chochote kitakachokuvunjia heshima Wewe au mama yake na baba yake. Mpe nguvu na hekima ya kupinga vishawishi vya kuwa muasi katika matendo yake yoyote. Hebu na awe mtiifu kwa mambo anayojua ni sawa machoni pako. Mpe mtazamo unaonyenyekea kwa hiari mamlaka yote katika maisha yake, na umsaidie kutii sheria daima.

**7: Kudumisha Uhusiano Mzuri wa Kifamilia**

*Bwana,* ninaomba kwamba-------- (jina la mtoto mkubwa) abaki karibu na wanafamilia wake, ingawa yeye anaishi mbali nao. Ninaomba kwamba atatenga muda kudumisha uhusiano thabiti wa kifamilia. Pia

ninaomba kwamba apate kibali kwa wakwe zake wote, wa sasa au hata wa siku zijazo, na kwamba mahusiano yao yawe sawa, yenye upendo, na chanya. Popote ambapo kuna uhusiano wowote wa kifamilia uliovunjika, ninaomba kwamba yeye atakuwa wa kwanza kunyosha mkono kutafuta upatanisho.

**8: Kuvutia Marafiki Wacha Mungu, na mifano ya kuigwa**

*Bwana,* ninaomba---------- (jina la mtoto mkubwa) awe makini kuona tabia ya kweli katika watu. Mpe ufahamu ili atambue mtu yeyote ambaye ni mfamo mbaya ili aepuke kuanzisha uhusiano wa karibu pamoja na mtu huyo. Hebu asipotoshwe na mtu anayezungumza maneno laini lakini yasiyo na nia zisizo safi. Mpe shauku ya kutafuta kaka na dada katika Bwana ili kutumia wakati nao wakati wowote inapowezekana. Walete watu katika maisha yake ili wamshauri kubakia kwenye njia iliyonyooka daima.

**9: Kukuza Njaa ya Mambo ya Mungu**

*Bwana,* usimruhusu----------- (jina la mtoto mkubwa) kuanguka mbali na njia zako. Maisha yake yanapozidi kuwa na shughuli nyingi na majukumu zaidi na zaidi, hebu na atamani uhusiano wa kina na matembezi ya karibu na Wewe. Usimruhusu kuwa asiyejali katika kujitoa kwake kukutumikia Wewe na kuishi kwa njia Yako. Daima awe na hamu ya uwepo Wako na hamu ya kukujua Wewe zaidi.

**10: Awe Mtu ambaye Mungu Alimuumba**

*Bwana,* ninamwinua-------- (jina la mtoto mkubwa) kwako na kuomba kwamba umpe ufahamu mpya juu ya wewe uliyemuumba kuwa. Usimruhusu ajaribiwe na kuhatarisha maisha uliyonayo kwa ajili yake kwa njia yoyote ile kwani yeye anatafuta nafasi za kazi na kupata marafiki wapya.

Kama hali mpya zinatokea, mzuie kutokana na vitisho vinavyoweza kumfanya atupilie mbali yale anayojua yeye kuwa ya kweli ili kuwavutia wengine. Mwongoze katika aina ya kazi na shughuli ambayo itatimiza hatima uliyonayo kwake.

**11: Kufuata Ukweli, Kukataa Uongo**

*Bwana,* ninaomba kwamba--------- (jina la mtoto mkubwa) asianguke kwenye mawindo ya kuamini uwongo. Hebu na yeye awe na Roho Wako wa Ukweli ndani yake kama kipimo ili kile kisicho cha Kweli kiwe dhahiri. Pia ninaomba kwamba asijaribiwe kusema uwongo kwa manufaa binafsi. Hebu asifikiri hata kidogo kwamba yeye anaweza kusema uongo kwa sababu tu watu wengine wanaonekana kusema uongo. Roho Wako wa Ukweli, awe ndani yake ili awe akimkumbusha kila wakati wa kile ambacho ni Kweli na sahihi.

**12: Kufurahia Maisha ya Afya na Uponyaji**

*Bwana,* msaidie-------- (jina la mtoto mkubwa) kukumbuka daima kwamba Wewe ni mponyaji wake. Yeye kamwe asikubali aina yoyote ya udhaifu bila kutafuta mguso Wako wa uponyaji pamoja na msaada

ufaao wa tiba. Mpe imani ya kuamini miujiza ya uponyaji katika maisha yake. Hebu na awe mwepesi kuombea wengine uponyaji na kuweza kusimama imara katika imani anapokungojea Wewe, Bwana, kwa majibu.

**13: Kuwa na Motisha ya Utunzaji Sahihi wa Mwili**

*Bwana,* naomba kwamba--------- (jina la mtoto mkubwa) atakuwa na hamu ya kutunza mwili wake kwa usahihi. Mkumbushe kwamba ingawa wewe uko juu yake, yeye bado ni hekalu la Roho Wako Mtakatifu. Kwa sababu hiyo, yeye anapaswa kuwa na bidii ya kujitunza yeye mwenyewe, mpatie hofu anaposhawishiwa kufanya mambo mabaya yanayohatarisha afya yake na usalama wake. Mfundishe kile anachopaswa kujua kuhusiana na kutunza mwili wake.

**14: Kuweka Tamaa ya Kujifunza**

*Haijalishi Bwana* kwamba----------- (jina la mtoto mkubwa) atakuwa na umri gani, yeye daima awe na hamu kubwa ya kujifunza na kuongezeka katika ujuzi. Ninajua kwamba ili yeye aendelee katika ulimwengu wa ushindani, lazima azidi kuongezeka katika ujuzi wake. Ninaomba kwamba atajifunza kukuza uwezo na maarifa yake zaidi, na katika kila msimu wa maisha. Nawe mzidishie elimu yake katika Wewe, na njia Zako.

**15: Kutambua Talanta Na Vipawa Vilivyotolewa Na Mungu**

*Bwana,* naomba kwamba-------- (jina la mtoto mtu mkubwa) ataendelea kufahamu zaidi na zaidi karama na talanta ulizoweka ndani yake, Zisafishe

karama hizi kwa matumizi makubwa zaidi katika kutumikia makusudi Yako hapa duniani. Mwachilie katika matumizi kamili ya vipawa na uwezo wake sasa, na usiruhusu chochote kimzuie asitumie mada ulizomuumba afanye.

**16: Kujifunza Kuhusu Maisha**

*Bwana,* najua kwamba-------- (jina la mtoto mtu mkubwa) anapotoka ulimwenguni kila siku, hebu asisikie lugha mbaya ambayo haitamjenga au kukutukuza. Weka kipimo/kiwango ndani yake ambacho kinatambua, kinapima, na kuchukizwa na kitu chochote kisichoheshimu uwepo Wako. Mpe nguvu za kuchukua hatua zinazohitajika, wakati wowote inapowezekana, ili kujitenga na watu wanaozungumza kwa jeuri au bila heshima. Weka shauku ndani ya moyo wake kusema maneno yenye kuleta uzima. Maneno ya kinywa chake na mawazo ya moyo wake yapate kibali mbele zako daima, Ee Bwana, nguvu yetu na Mkombozi wetu (Zaburi 19:14).

**17: Kukaa Kuvutiwa na Utakatifu na Usafi**

*Bwana,* ninaomba ---------- (jina la mtoto mkubwa) daima awe na moyo safi. Ninaomba kwamba yeye atajitakasa kutokana na chochote kitakachomzuia asiwe chombo cha heshima Yako na chenye manufaa kwa makusudi Yako. Ondoa chochote katika maisha yake kinachomzuia asizae matunda mazuri. Wacha yeye alenge sio tu kuwa safi machoni pake au kwa maoni ya wengine, lakini muhimu zaidi, machoni Pako.

## 18: Kuomba Kupitia Chumba cha Mtoto

*(Unapoomba sala iliyo mwishoni mwa ombi hili kwa ajili ya mtoto wako mtu mzima, badilisha maneno "nyumbani" kwa maneno "chumba hiki," kisha uendelee na sala hii.*

*Bwana,* ninaomba kwamba nyumba ambayo-----------(jina la mtoto mkubwa) anaishi itakuwa makao ya uwepo wako. Mjulishe chochote huko kisichokutukuza. Usimruhusu alete kitu chochote ambacho ni chukizo Kwako kwenye makazi yake. Ninaomba kwamba hakuna kitakachoendelea katika nyumba hiyo ambacho hakipendezi machoni Pako. Linda nyumba yake dhidi ya wavamizi au majanga ya aina yoyote.

## 19: Kufurahia Uhuru kutoka kwa Hofu

*Bwana,* naomba kwamba---------- (jina la mtoto mkubwa) atakumbuka daima kwamba Wewe uko pamoja naye popote aendako, na kwamba utaendelea kumshikilia na kumtia nguvu. Mkumbushe kwamba haijalishi ni mambo mangapi ya kutisha yanayoendelea kumzunguka, Wewe ndiyo mlinzi wake. Endelea kumkamilisha katika upendo Wako ili asiishi kwa hofu. Msaidie kujua kwamba yeye anaweza daima kukimbilia Kwako.

## 20: Kuwa Na Akili Nzuri

*Bwana,* ninaomba --------- (jina la mtoto mkubwa) kadri anavyozidi kukua, Utamlinda dhidi ya mawazo mabaya ya dunia

yaliyochanganyikiwa. Mpe yeye uwazi wa mawazo na kinga dhidi ya sauti za kuchanganyikiwa ambazo zingetaka yeye aendane na njia zake. Akili yake na izidi kutawaliwa na Roho Wako. Hebu asiifuatishe namna ya dunia hii, bali abadilishwe kwa kufanywa upya nia yake (Warumi 12:2). Msaidie kila siku kulivuta kila wazo kuwa mateka katika utiifu Kwako.

**21: Kualika Furaha ya Bwana**

*Bwana,* najua kwamba kwa sababu ya jinsi maisha yalivyo, kadiri---------- (jina la mtoto mkubwa) anavyoishi, ndivyo maumivu, mateso, na hasara zinaweza kuja katika maisha yake au ataona katika maisha ya wengine, hilo likitokea, hebu mzuie asipoteze imani na amani moyoni.

Wakati wowote roho yake inapohuzunika kwa sababu ya hasara fulani, naomba umpe mafuta ya furaha kwa maombolezo na vazi la sifa badala ya roho nzito (Isaya 61:3). Msaidie akimbilie Kwako, akijua kwamba katika uwepo wako ndipo furaha inapatikana (Warumi 15:13).

**22: Kuharibu Urithi wa Utumwa wa Familia**

*Bwana,* ninamwinua----------- (jina la mtoto mkubwa) kwako na kuomba kwamba chochote kibaya kutoka kwa maisha yangu ya zamani au mzazi wake haitakuwa kitu ambacho atalazimika kuhangaika nacho au mzigo ambao atalazimika kuubeba. Ninajua kwamba mambo ya zamani yanaweza kujaribu kuinua vichwa vyao vibaya katika maisha yake kadiri anavyozeeka, lakini naomba agundue kuwa mambo haya

yamevunjwa kwa uwezo wa Roho Wako. Yeye awe na nguvu za kutosha ndani Yako ili ashike urithi wa uhuru ambao ulinunuliwa kwa ajili yake msalabani. Asante, Bwana Yesu, kwamba ulilipa gharama hiyo ili sisi na watoto wetu tuishi maisha ya furaha.

**23: Kuepuka Pombe, Madawa ya Kulevya, na Uraibu Mwingine**

*Bwana,* najua kwamba inawezekana katika umri wowote kuwa mlevi, mraibu wa dawa za kulevya, au kukuza uraibu wa aina nyingine. Tafadhali weka ulinzi kwa ----------- (jina la mtoto mkubwa) dhidi ya mambo hayo yote. Iwapo adui atapata nafasi katika eneo hilo, mwachilie huru. Wakati wowote kitu kama hiki kinapokuwa kishawishi, mwokoe kutoka humo. Msaidie kuona wazi kifo kinacholetwa na mambo haya yote, na umwezeshe kuchagua uzima.

**24: Kukataa Uasherati**

Bwana, najua kwamba majaribu ya ngono yapo kila mahali na inaonekana kana kwamba hayawezekani kuepukwa, na kisha dhambi ya ngono inazidi kukubalika katika jamii kama mtindo wa maisha ya kawaida. Pia najua ni mojawapo ya njia ambazo adui anataka kumharibu-------- (jina la mtoto mtu mzima). Hebu na ajifunge roho yake nawe, na nafsi yake, na akili yake, isaidiwe Nawe, ili asimame kwa nguvu. Wakati wowote anapohisi kuvutwa kutoka kwenye yale yaliyo sawa machoni Pako, naomba msaidie kusimama imara na kupinga ushawishi huo ili aweze kuhifadhi maisha yake kwenye njia Yako.

**25: Kutafuta Mpenzi Mwaminifu**

*Bwana,* ninaomba kwamba--------- (jina la mtoto mkubwa) atakuwa na mume/mke ambaye wataishi pamoja daima wakisaidiana. Usimruhusu afanye makosa kuhusiana na hilo. Pale ambapo makosa tayari yamefanywa, ninaomba kwamba Ukomboe hali hiyo. Wakati wa kuvunjika moyo katika eneo hilo, mweke akiwa amedhamiria kutokubali jaribu la kutoka nje ya mapenzi Yako kwa ajili ya maisha yake. Ninaomba kwamba ndoa yake iwe ya mpango Wako wa mbinguni na ipate "uzao wa kumcha Mungu" kama vile Wewe unavyotaka.

**26: Kuishi Bila kinyongo na kusamehe**

*Bwana,* naomba kwamba bila kujalisha ana umri gani---------- (jina la mtoto mkubwa) au nini kinatokea katika maisha, yeye atakataa kuwa na uchungu, kisasi, na kinyongo kwa wengine. Na awe tayari kusamehe makosa ya mwingine dhidi yake kama vile Ulivyomsamehe makosa yake yeye dhidi Yako. Hebu awe si mwepesi wa hasira na aweze kusahau kosa (Mithali 19:11). Mpe uwezo wa daima kuwa na upendo na roho ya ukarimu kwa wengine, hata kwa wale ambao hawako hivyo kwake.

**27: Kutembea katika Toba**

*Bwana,* ninaomba kwamba ungempa----------- (jina la mtoto mkubwa) moyo unaoendelea kuzaliwa upya. Na kamwe asifikie mahali ambapo yeye hataelewa thamani ya maungamo na toba katika maisha yake. Hebu asifikirie kamwe kwa sababu hakuna mtu anayetazama, basi hata Wewe, huoni yote anayofanya. Msaidie awe na uharaka kutubia udhalimu wowote katika mawazo na matendo yake. Daima aweze kufunua dhambi zake)

mbele zako, akiziungama na kuziacha, ili aweze kufurahia rehema na uongozi wako (Mithali 28:13).

### 28: Kuvunja Ngome Zisizomcha Mungu

Bwana, najua adui anapenda kuweka ngome katika maisha yetu katika shughuli zetu na uhitaji na shinikizo la maisha, na sisi wala hata hatutambui. Ninaomba kwamba Utafichua jambo kama hilo katika maisha ya --------- (jina la mtoto mkubwa) na kuvunja kila ngome mbaya katika maisha yake. Mwonyeshe mambo ambayo hajaona, na usiruhusu neno lolote lifichwe, ambalo linapaswa kufunuliwa (Mathayo 10:26).

### 29: Kutafuta Hekima na Utambuzi

*Bwana,* ninaomba kwamba ungempa-------- (jina la mtoto mkubwa) zawadi ya hekima. Mwezeshe kuona vitu ambavyo hajaweza kuona hapo awali. Mpe hekima kwa maamuzi yote, hasa maamuzi ya dharura au haraka pale ambapo hakuna muda wa kuomba kwa kina. Msaidie afurahie maisha marefu, utajiri, heshima, raha, furaha, na amani uliyo nayo Wewe kwa ajili yake kwa sababu ya hekima Uliyopanda ndani yake (Mithali 3:13-18).

### 30: Kukua katika Imani

*Bwana,* najua kuwa kutakuwa na matukio katika maisha ya----------- (jina la mtoto mkubwa) ambayo yatajaribu imani yake, lakini ninaomba kwamba yeye atapitia kila nyakati hizi kwa imani kubwa kuliko hapo awali. Imani yake iendelee kukua kupitia chochote kinachotokea katika maisha ili iwe na nguvu inayoendelea kukua mwaka hadi mwaka.

Mpe imani ya kuamini kwamba yeye anaweza kuingia katika yote uliyo nayo kwa ajili yake. Mafanikio yake maishani yasiwahi kuathiriwa na imani dhaifu katika uwezo wako wa kufanya yale yasiyowezekana.

**31: Kuvuka Miaka ya Ujana kwa Mafanikio**

Bwana, naomba umkomboe kutoka uzoefu wake wowote mbaya, ambao umempata mtoto wangu mtu mzima katika miaka yake ya utineja, msaidie kujenga tabia ndani yake. Toa mema kutoka kwa hali hiyo, na uyatumie kwa utukufu Wako. Ninajua miaka hiyo ina athari kubwa kwa kila mtu, kwa hivyo ninaomba kwamba athari yoyote mbaya juu ya --------- (jina la mtoto wako mtu mzima) itageuzwa kuwa na matokeo chanya.

## Nyongeza

## KUOMBA PAMOJA NA WAZAZI WENGINE

Baada ya kujaribu njia kadhaa za kuandaa muda wa maombezi (intercessory prayer) kwa watoto, nilipata maombezi yanayofanya kazi vizuri. Kwanza kabisa, kila kusanyiko la maombi linapaswa kuwa na muda rasmi wa kuombea watoto wao wasiozidi kumi na wawili kwa wakati mmoja, kwa sababu inachukua dakika ishirini hadi thelathini kwa kila mtoto kushiriki mahangaiko na maombi na kuwaombea vya kutosha. Hata tukiwa na watoto kumi na wawili tu, hiyo inamaanisha saa sita za kuomba. Hii ni kafara au dhabihu ya wakati na kujitoa kwa mzazi, bila kusema ni kwa kiasi gani inasukuma mipaka ya uvumilivu kwa watoto.

Ndiyo maana tunafanya mara moja au mbili tu kwa mwaka—kawaida Jumamosi au wakati wa likizo. Ikiwa unataka ichukue muda mfupi, basi waalike watoto wachache.

Jinsi tunavyopanga ni kuanza kusali saa mbili asubuhi, na kuchukua mapumziko ya chakula cha jioni kutoka saa 11:00 jioni hadi 11:30 jioni na kisha kuomba kutoka 11:30 jioni hadi 2:30 usiku. Wakati mwingine kila mtu huleta chakula ili kushiriki; wakati mwingine tunaagiza tuletewe chakula hapo.

Tunaajiri vijana ili kuwapa burudani na kuwatunza watoto wachanga katika chumba tofauti huku watu wazima wakisali faraghani. Tumeona haifanyi kazi vizuri kuwaombea watoto wote wa familia moja baada ya nyingine, kwa sababu mara nyingi familia hiyo huhisi kuwa wamemaliza wakati huo na wanaweza pia kwenda nyumbani. Pia sio vyema watu waingie ndani kuombewa kisha kuondoka—au mbaya zaidi kumwacha mtoto ili aombewe, kisha warudi baadaye kumchukua. Wakati pekee tuliofurahia kufanya hivyo ni katika kisa cha mzazi asiye na mwenzi aliyefanya kazi na hangeweza kuipanga ratiba vinginevyo. Kwa sehemu kubwa, wakati huu wa maombi lazima uwe miadi ya wazazi wote kwa watoto wote kwa muda wote unaohitajika. Wajulishe watu mapema kile kinachotarajiwa kutoka kwao katika suala hili, ili waweze kuamua kama wanaweza kutunza ahadi hiyo.

Tunapoanza, tunachora majina ya kila familia ili kuona ni kwa mpangilio gani tutaendelea nao. Kisha tunaomba kwa utaratibu huo, mmoja baada ya

mwingine, kwa ajili ya mzaliwa wa kwanza wa kila familia. Tunapomalizana nao, tunawaombea wale wazaliwa wa pili, kisha wa tatu, na kadhalika.

Kila mara tunaanza wakati wa maombi bila mtoto kuwepo ili wazazi waweze kutoa maombi na mahangaiko yao na tunaweza kuombea masuala yoyote nyeti ambayo hawataki mtoto asikie. Kisha tunamwalika mtoto ndani ya chumba ili kushiriki maombi yake maalum. Tunapoomba kwa ajili ya mahitaji hayo, pia tunasali kwa ajili ya afya ya mtoto, usalama, ulinzi, mwongozo, ukuzaji wa talanta na vipaji, na ikiwezekana kubainisha kwa busara tashwishwi/wasiwasi uliotajwa hapo awali wa mzazi.

Kwa mfano, mzazi mmoja alionyesha hangaiko lake juu ya ushawishi mbaya wa marafiki fulani katika maisha ya mtoto. Tulipoomba bila mtoto, tuliomba kwa undani sana kuhusu marafiki maalum.

Tuliposali pamoja na mtoto huyo, tulisali ili mtoto huyo awe na utambuzi wa kutafuta marafiki wanaomcha Mungu na kuwapinga marafiki wasiomwogopa Mungu.

Busara ni muhimu hapa ili mtoto asihisi kusalitiwa au kuhukumiwa, lakini kupendwa tu. Familia ambazo tumeomba nazo kwa miaka mingi bado zinazungumza kuhusu athari kubwa ya nyakati zetu, pamoja na majibu mengi ya maombi ambayo yalikuja kama matokeo. Watoto pia walifurahia vipindi hivi vya maombi kwa sababu viliwafanya wahisi kutunzwa, kujaliwa na kuwa wa pekee.

Kulikuwa na hata matukio ambapo wazazi walikuja kufanya kundi liombee mtoto mtu mzima anayeishi mbali na nyumbani, na pia baadaye walishuhudia matokeo chanya ya maombi hayo.

Ni nani ajuaye ni maisha mangapi yameweza kuokolewa kwa njia moja au nyingine kwa sababu tu ya wazazi wanaosali kwa kujiunga pamoja? Usisite kuweka mikakati ya kikundi cha wazazi kinachoomba katika eneo lako. Hitaji ni kubwa. Wewe ukipanga tu, watu watakuja.

## NGUVU YA KUMWOMBEA MTOTO WAKO

Kuna mambo saba kila mzazi wa mtoto mzima anahitaji kujua, na mara nyingi hakuna mtu anayekuambia jambo lolote kati ya hayo. Nadhani ingekuwa nzuri ikiwa mtu angefanya angalau nimetaja machache kati ya mambo haya kabla watoto wangu hawajazeeka vya kutosha kuingia katika utu uzima. Basi ningeweza kujitayarisha. Unapokuwa mzazi mdogo/kijana, wazazi wakubwa na wenye uzoefu zaidi kwa hamu hukupongeza kwa kutarajia mtoto. Na kisha wanafanya tena wakati mtoto wako amezaliwa, lakini wakati huu pia wanakupa ushauri juu ya malezi ya watoto wachanga.

Hata hivyo, kuhusu miaka ya baadaye ya mtoto, kila mtu yuko kimya. Wao hutabasamu kwa kuwa wana fununu na hawasemi chochote juu ya kile kilicho mbele. Nina hakika wanafikiria, kwanini waseme chochote sasa? Wazazi watajua tu kwa wakati. Ama sivyo wanaamini wao ndio wale tu ambao wanapitia changamoto zozote na watoto wao watu wazima, hivyo kwa nini wamtishe mtu yeyote? Kwa sababu yoyote ile isiyoeleweka vyema, hakuna mtu anayezungumza juu ya jambo hilo. Angalau mimi kamwe

sikusikia chochote.

Nilidhani kwamba wakati watoto wako wanatimiza miaka 18 wanahitimu kutoka shule ya sekondari na kwenda chuo kikuu, na kisha kukabili maisha ya utu uzima kwa ajili ya majukumu ya uzazi. Wana maisha yao wenyewe na wewe una yako, na wanakumbuka kila kitu wewe ulichowafundisha, na hivyo wanaendelea kutafuta kazi zenye mshahara mkubwa na kuolewa na kuja kukutembelea mara chache kwa mwaka na wajukuu. Sawa! Msimu wa Uzazi umekamilika! Sasa unaweza kufanya mambo ambayo umekuwa ukiota/ukiwazia kila wakati kufanya, lakini ulikuwa na shughuli nyingi kulea watoto.

**SAHAU! HILO HALITATOKEA!**

Mtoto wako anafikisha miaka 18 na—unatumaini—atahitimu kutoka shule ya Sekondari, na kisha unagundua siku zako za malezi mazito ndio zimeanza. Unaomba yeye aingie katika chuo kizuri au shule ya biashara ambayo maprofesa hawafundishi kwamba Mungu amekufa na ukomunisti ndiyo nadharia ya maana, au kwamba maadili yana mipaka na upotovu ni jambo la kutamanika. Athari kwa mtoto wako mtu mzima sasa ni nyingi Zaidi na mbaya kuliko vile ulivyowahi kufikiria miaka iliyopita wakati yeye akiwa mdogo-na kwa uhakika mambo ni ya kutisha zaidi kuliko wakati wewe mwenyewe ulikuwa unahitimu kutoka shule ya sekondari-na huwezi kuacha kufikiria juu ya uwezekano wote wa kutisha.

Na ingawa kuna mengi ya kuwa na wasiwasi, wewe una udhibiti mdogo juu

ya chochote kinachohusiana na maisha yao kuliko hapo awali. Baada ya watoto wako kuhitimu - ikiwa watahitimu - unatumaini watapata kufanya kazi ya aina fulani ya usalama na faida.

Wewe huwa na wasiwasi kila wakati kwamba watakutana na mtu binti au kujana wa kiume wa kuoana naye, na baada ya kuoana unatumaini wao watabaki kwenye ndoa. Una wasiwasi kuhusu jinsi walivyo makini au kutojali afya zao na kama wanaweza kulipa kodi za nyumba zao au kulipa mikopo ya nyumba. Wewe sasa wahangaika kufikiria kuhusu wajukuu zako—ambao siku moja utapata na namna watavyokuwa na afya njema na kuinuliwa kuwa watu wema, na wacha Mungu. Vema, niko hapa kukuambia kile ambacho unaweza kuwa tayari unashuku—au kwa hili, wakati bado una uhakika nalo. Na sio tu kuwafichulia ukweli huu—ambao mtu alipaswa kukuambia zamani—pia kupata njia ya kushughulikia hilo.

Lakini kwanza nahitaji kukushirikisha kwa haya.

## MAMBO SABA AMBAYO KILA MZAZI WA MTOTO MKUBWA ANATAKIWA KUJUA.

### 1. Uzazi Hauna Mwisho

Sehemu ambayo hakuna mtu anayekuambia kuhusu kuwa mzazi ni kwamba uzazi haukomi. Nilikuwa nafanya mzaha na wazazi wapya waliochoka na waliolemewa na wasiwasi juu ya jukumu la ghafla la "saa 24-kwa-siku-

siku-7-kwa-wiki" na "Orodha isiyoisha ya mambo ya kufanya na kutokuwa na wakati wa kutosha kwa siku kufanya yote" nakuwaambia, “Msijali. Hii itadumu miaka 18 tu.” Nilijua kuwa huo ulikuwa mzaha usio na huruma, lakini nilitaka wajue ukweli.

Na zaidi ya hayo, nilipenda kusikia miguno yao ya uchovu ikifuatiwa na kicheko cha kusita-sita. Walakini, sasa naona kwamba utani ulikuwa juu yangu. Na ni mkatili zaidi kuliko nilivyowaza. Hiyo ni kwa sababu ya ukweli kwamba malezi hayana mwisho! Ingawa watoto wapo hatua tofauti na misimu ya majukumu ya uzazi tofauti, moyo wako na akili daima utakuwa na kila mmoja wa watoto wako, kwa maisha yako yote. Na hii sio kazi rahisi, kwani haijalishi wapi wanaenda au wanafanya nini, sehemu yako huenda pamoja nao. Wakati wanafurahi, unafurahi. Wanapoteseka, unateseka.

Hata baada ya kukua nawe usiwe nao kimwili bado unajali kila siku—na usiku mwingi, naweza kuongeza—kuhusu usalama wao na mapambano, hofu na udhaifu wao, mafanikio yao na kushindwa, uchaguzi wao na makosa. Sio tu kwamba moyo wako bado uko kwa watoto wako baada ya kuwa watu wazima, wao mara nyingi wako kimwili bado na wewe, pia. Ninakumbuka siku ambayo mume wangu, Michael, na mimi tulimpeleka mwana wetu, Christopher chuoni na kumpeleka katika chumba chake cha kulala. Nililia njia nzima tulipokuwa tunarudi nyumbani—chuo kilikuwa kilikuwa ni kama dakika 15 tu kutoka nyumbani kwetu Na sio kwamba sitamwona tena, lakini nilijua siku za kuishi naye ziliisha na huu ulikuwa

mwisho wa zama.

Nilikuwa na huzuni siku iliyofuata pia, lakini nilijishughulisha na mradi wa kuandika vitabu ambao ulipaswa kuendelea na nilihitaji kusaidia kwenye kampuni ya baba yangu mwenye umri wa miaka 85, ambaye alikuwa akiishi nasi katika nyumba hiyo; dada yangu, ambaye alifanya kazi katika ofisi yetu ya nyumbani; na mume wangu, ambaye alikuwa akifanya kazi, kutoka studio ya nyumbani. Saa tatu mchana nilisikia mtu akiingia ndani ya nyumba kupitia mlango wa nyuma, na nikamsikia baba yangu akizungumza na mtu huyo. Huyo anaweza kuwa nani? Nilijiuliza. Kila mtu anayeishi au kufanya kazi ndani ya nyumba alikuwepo nyumbani na hatukuwa tumetarajia mgeni yeyote.

Niliingia jikoni, na kwa mshangao mkubwa nilimuona mwanangu. “Haya, Christopher. Unafanya nini nyumbani? Umesahau kitu?" “Hapana, nilitaka tu kusema, ‘Halo kwa Babu,’” alisema kwa furaha, kisha akaketi kitini jikoni na kuzungumza na baba yangu kwa karibu saa mbili. Saa 11 jioni ilipofika, yeye alituaga na kuondoka kurudi chuo kikuu kula chakula cha jioni na marafiki zake chuoni kisha kuendelea na masomo.

Alifanya hivyo karibu kila siku kwa muda mrefu, kisha mara kadhaa kwa wiki, na hatimaye mara moja au mbili kwa wiki katika umri wake mdogo. Jambo hili lilinifanya nitabasamu kufikiria kwamba, katika sehemu zote ambazo angeweza kwenda katika hizo saa mbili alasiri, alitaka kuwa na familia yake, kuzungumza na babu yake ambaye alikuwa mpweke ndani ya nyumba iliyojaa watu waliopenda kazi ambao hawakuwa na wakati kukaa

chini kila siku kwa saa mbili na kuzungumza naye kuhusu siku za zamani. Baba yangu aliishi hadi miaka 93, na hadi siku aliyokufa hakuacha kuzungumza kwamba Christopher alikuja nyumbani kutoka chuoni kila siku ili tu kuzungumza naye.

Ukweli ni kwamba, hutaacha kuwa mzazi anayejali sana ustawi wa mtoto maisha yako yote, haijalishi ana umri gani, au wewe una umri gani, au mko karibu kiasi gani au mko mbali sana. Milele! Na si hivyo tu, inaonekana kwamba mambo ambayo yanawakabili watoto wetu watu wazima, yanabeba matokeo makubwa zaidi kuliko walipokuwa vijana. Tunapofikiria mahali ulimwengu ulipo, na jinsi maovu yalivyoenea na kuenea, na jinsi sisi wanyonge hujisikia kutoweza kufanya chochote kuhusu mambo hayo, tunaweza kujipatia wenyewe wazimu na wasiwasi kwa kuwa ulimwengu una mambo ya kutisha.

Ingawa watoto wadogo wanaweza kukabili mambo magumu sana pia—hata maisha na hali za kutisha au kubadilisha maisha—ukweli kwamba bado wako pamoja nasi katika nyumba zetu na chini ya uangalizi na ulinzi wetu hutufanya tujisikie kuwa hatuna udhibiti zaidi juu ya hali hizo, au hakuna tunaloweza kufanya kwa sehemu kubwa. Lakini wakati watoto wetu ni watu wazima na hufanya maamuzi mengi juu yao wenyewe bila mchango kutoka kwetu, tunaona madhara yote makubwa yanayoweza kutokea na kutengeneza matokeo yasiyo sahihi. Na pia tunaona jinsi tutakavyokuwa tunaumia pamoja nao pale wanapokosea katika maamuzi.

Tunapoona maisha yakiendelea kwa watoto wetu wakubwa kwa njia yenye

changamoto, Je, tunajikuta tunataka kuwasaidia? Mungu pekee Ndiye anayejua jibu la swali hilo. Sisi wazazi wa watoto ambao wamekwisha kuwa watu wazima, tunaweza kuwa na wasiwasi mwingi, lakini sio lazima lazima kwetu kutafuta ufumbuzi kila mara kwao, au hata fursa ya kutoa mawazo yetu yote, mapendekezo, na maoni. Angalau tusifanye hivi kwa watoto wetu watu wazima. Lakini tuna fursa kubwa ya kuweza kueleza mahangaiko hayo kwa Mungu na kumwalika afanye kitu kwa ajili yao. Na jambo kuu juu ya hilo ni kwamba, tunapopeleka mahangaiko yetu kwa Bwana, tuaamini kwamba Yeye husikia maombi yetu na kuyajibu kwa niaba ya watoto wetu watu wazima----hii inamaanisha maombi yetu yana nguvu ya kuathiri mabadiliko katika maisha yao. Na hiyo inatupa amani ambayo hatuwezi kupata ufumbuzi kwa njia nyingine, nje ya Bwana.

**2. Kuna changamoto Huwezi Kuzirekebisha**

Nilikuwa tu nimetambulishwa kwa mwanamke kijana mwenye kuvutia katika miaka yake ya mapema ya arobaini. (Unapokuwa na umri wangu, 40 ni mchanga, 30 ni mchanga sana, na mtu yeyote mdogo kuliko 30 ni mtoto tu.) (Kwa jambo hilo, kwa njia nyingine, miaka ya arobaini na hamsini ni vijana kwangu, miaka ya sitini na sabini ni watu wa makamo, na themanini na kuendelea mtu anakaribia uzee. Labda katika miaka kumi nitarekebisha jinsi navyoona haya yote!) Mwanamke huyu mchanga, akiwa pamoja nami, tulizungumza kwa ufupi kuhusu hali ya hewa—jinsi ilivyokuwa joto siku hiyo na wakati mvua ingeweza kunyesha tena—na kisha ghafla akasema, “Mimi nataka kukushukuru kwa kuandika kitabu…” Hakuweza kumaliza sentensi hiyo kwa sababu midomo yake ilitetemeka sana hivi kwamba

ilimbidi afunge mdomo wake kwa nguvu na kumeza mate kwa nguvu akijaribu kupambana na machozi yaliyokuwa yanataka kutoka. Lakini machozi yalikataa kuzuiliwa na kumtiririka mashavuni. Katika muda ulioonekana kuwa mrefu, kati ya wakati alipokaa kimya, na pale hatimaye alipoweza kuongea tena, nilijiuliza kama alikuwa anaumia katika hisia zake au pengine katika ndoa yake. Nilimgusa mkononi ili kumfariji na kukaa kimya mpaka akamaliza sentensi yake. "…kitabu chako nguvu ya mzazi aombaye," alisema kwa sauti ya kutetemeka.

Aliposema neno "mzazi," nilijua mara moja chanzo chake cha mateso au huzuni. Ilikuwa ni aina ya maumivu ya kina ambayo ni mzazi tu anaweza kuhisi, wakati kitu fulani kinaenda vibaya kwa mtoto wake. Mara nyingi nilikuwa nimesikia kutoka kwa wazazi wengine, na kisha nilikumbuka kwa watoto wangu pia. Huzuni yao juu ya kuvunjika moyo kwa kutotii kwa mtoto, uasi, magonjwa, misiba au majeraha, au huzuni kubwa ya kuwaona hawaishi kulingana na uwezo wao, yote yalikuja akilini mwangu kama mafuriko.

Ilikuwa, ni mtoto wake mtu mzima ambaye alikuwa akimzungumzia. Yeye aliniambia kuhusu baadhi ya matatizo makubwa ambayo yeye na mume wake walikuwa nayo na mtoto wao wa miaka 28. Alisema kuwa hata miaka ya mapema pamoja naye ilikuwa mibaya na yenye changamoto sana, lakini kwamba kitabu changu kilimsaidia kupitia kila mwaka na kila shida. Hata hivyo, alipokuwa mtu mzima wazazi hawa walilazimika kukabiliana na uzembe wake, ulegevu, uvivu, uchaguzi mbaya, tabia mbaya, na majanga

mengi ya kibinafsi. "Je, mwanangu huyu atasimama lini?" Mzazi alilia na kulowesha uso machozi akisema. “Hivi sisi tuna muda gani, wa kuendelea kuumia na kuteseka na kumwombea mtoto wetu na kulipia makosa yake—hasa ya kifedha?” “Natamani ningeweza kukuambia tarehe kamili ambayo haya yatakoma,” nilijibu, “lakini sidhani kama iko siku maalum ambayo haya yataisha. Hauko peke yako katika hili. Nimevisikia visa vya aina hii kuhusu watoto watu wazima kila mahali ninapoenda. Wazazi wanaona ni vigumu sana kujua wapi wachore mstari kati ya kuruhusu mtoto mtu mzima kujifunza somo gumu, na kuwasaidia kusimama kwa miguu yao.

Tunajua hatuwezi kuwaacha tu waendelee kuumia, lakini wakati mwingine tunaweza na inabidi tuwaache waanguke na kujifunza. Hata hivyo tunahitaji kuwa na hekima kuhusu hilo. Hatuwezi kukaa kimya na kuwaacha wajiangamize wenyewe. Tunataka wajifunze masomo, lakini hatutaki masomo hayo yaharibu maisha yao katika mchakato huo. Inatubidi kuwa na kiasi kati ya kuwasukuma wenyewe na kuwashauri, ikiwa hawajawa tayari, na kuwafanya iwe rahisi sana kwao kukaa kwenye shimo, wakati wanahitaji kukua na kujifunza kuruka.

"Njia pekee ninajua, ya jinsi ya kutambua mstari huo mzuri kati ya kusaidia mtoto wako mtu mzima na kumwezesha kuishi maisha ambayo ni pungufu kuliko yale ambayo Mungu anayo kwa ajili yake ni kumwomba Bwana akupe hekima,” nilimwambia. “Sote lazima tuombe Mungu atuonyeshe sisi tufanye nini na tusifanye nini kwa watoto wetu watu wazima. Tunapaswa kumtafuta Mungu kama jinsi ya kuwaombea.

Tunahitaji kumwomba Bwana kwa uwazi na utambuzi, ili kujua wakati wa kuomba tu na kumwacha afanye kazi katika maisha yao bila msaada mwingine wowote kutoka kwetu. Mungu pekee Ndiye anayejua jambo sahihi la kufanya, na wakati sahihi. Na wakati mwingine unapaswa kumwachilia mtoto wako mtu mzima mikononi mwa Mungu kabisa na kumweka Bwana katika mamlaka ya maisha yake na unaweza kuwa na amani ya kweli. Huwezi kumbadilisha mwanao, lakini Mungu anaweza. Mwanao anahitaji wewe umpende, umwamini, na umuunge mkono katika sala. Basi wewe fanya chochote ambacho Bwana anakuambia ufanye, au usifanye, ili kumsaidia mtoto kupata njia sahihi."

Nilisali pamoja naye na mume wake, ambaye, kama ilivyokuwa, alikuwa akimngojea umbali mfupi tu kutoka kwetu, na baadaye alionekana kuwa na nguvu zaidi na amani katika nafsi yake. Nilimtia moyo kuelewa kwamba Mungu Ndiye mzazi mkuu, na Hangewapa tu hekima kuhusu jinsi ya kushughulikia kijana wao na matatizo yake, lakini pia angefanya kazi katika maisha ya mtoto wao aweze kubadili hali yake na kumleta katika upatanifu na njia za Mungu. Na Mungu pia angeondoa hatia ambayo walikuwa wakihisi juu ya kile kilichokuwa kinatokea kwa mtoto wao. Sote tunahitaji kuelewa kwamba hatuwezi "kurekebisha" au "kubadilisha" watoto wetu wazima.

Ni Mungu pekee anayeweza kufanya mabadiliko ambayo yatadumu kwa mtu yeyote. Kazi yetu ni kuwaachilia watoto wetu watu wazima mikononi mwa Mungu na kisha kuomba kwa Bwana kufanya mabadiliko ndani yao

na maisha yao kulingana na mapenzi Yake.

**3. Mungu Anaweza Kubadilisha Kila Kitu**

Si rahisi kuwa mzazi wa mtoto mtu mzima. Hiyo ni kwa sababu ni vigumu kujua nini cha kufanya na nini usifanye kwa ajili yao. Unahitaji kuingilia wakati gani? Je, umefanya mengi kupita inavyotakiwa? Ni wakati gani matarajio yako ni ya juu sana au chini sana? Ni wakati gani upendo wako mgumu ni mgumu sana au sio mgumu vya kutosha? Wakati mwingine unafikiri unafanya jambo sahihi na sivyo. Au labda ilikuwa sawa kwa mtoto mmoja lakini si kwa mwingine. Nimegundua kuwa Mungu pekee Ndiye anayeweza kukupa hekima unayohitaji kuhusu mambo hayo. Na atawapeni hekima mnapomuomba. Lakini kwanza unapaswa kuelewa na kuamini kwamba unapoomba kuhusu mtoto wako mtu mzima, Mungu atakusikia na kujibu. Lakini lazima tujue kuwa maombi sio kumwambia Mungu cha kufanya au kumfundisha Yeye.

Maombi ni kushirikiana na Mungu, kuona kwamba mapenzi Yake yanatimizwa. Si lazima kuelewa mapenzi ya Mungu kikamilifu, kwamba ni nini tuombe ili mapenzi Yake yatimizwe. Pia unapaswa kuamini kwamba wakati huwezi kubadilisha chochote kwa maisha ya mtoto wako mtu mzima, Mungu anaweza kubadilisha kila kitu. Ingawa ni kweli kwamba Mungu hatakiuka mapenzi yenye nguvu, au upinzani ya mtu, Atapenya moyo wa mtu ambaye ni mdogo zaidi na muwazi Kwake. Na hatujui kwa hakika ni nani aliyefungiwa kabisa mambo ya Bwana na ambaye hajafungiwa. Mungu pekee Ndiye anayejua hilo. Kwa hivyo tunahitaji kuomba na

kumuachia Mungu afanye kazi. Bila maombi yetu kuchukua nguvu za Mungu, maisha yetu yameachwa kuwa bahati nasibu, na patapotea na wakati mwingine huleta matokeo mabaya. Ngoja nikupe mifano mwiwili mikali au migumu ya kile ninachozungumza.

Ninajua familia moja—hebu tuwaite akina Solinka—ambao kijana wao alikuwa akiendelea kupata matatizo. Hatimaye alikamatwa, na badala ya kumtoa nje kwa dhamana, Bwana na Bi Solinka waliamua kumruhusu ajifunze somo gumu kwa kukaa gerezani kwa muda. Kwa bahati mbaya, alishambuliwa gerezani na kupigwa na mmoja wa wafungwa mpaka akafa kutokana na majeraha yake. Wazazi walipigiwa simu na mamlaka kuwajulisha nini kilitokea na wapi wanaweza kuchukua mwili wake. Walihuzunika na kugubikwa na hatia kwa sababu wangeweza kuzuia jambo hili. Walikuwa wazazi wazuri ambao walikuwa wakijaribu kufanya yaliyo sawa, lakini hali iligeuka kuwa mbaya sana. Sijui wako wapi leo, lakini mimi nina hakika bado wanateseka kutokana na tukio hili la kusikitisha.

Ninajua familia nyingine—hebu tuwaite akina Maina—ambao mtoto wao pia alikuwa akiwapa wazazi wake huzuni kwa muda. Alipokamatwa na kuhukumiwa kwenda jela, pia hawakujaribu kumtoa. Walijua kwamba alikuwa na hatia, na walitaka aelewe athari/matokeo ya tabia yake. Alimaliza kutumikia muda mfupi wa jela, lakini iligeuza maisha yake. Wakati wake wa jela ulikuwa tukio lisilosahaulika na la kutisha ambalo hakutaka kulirudia. Sisi wote tulimwomba Mungu amfungue macho ili apate ukweli kuhusu njia aliyoipitia, aliyokuwa anaiendea na alikokuwa

anaelekea. Tuliomba kwamba Mungu amfunulie kuwa aliumbwa kwa kusudi gani. Mungu akawajibu hayo maombi, kwa sababu alitoka nje ya jela, akiwa mtu aliyebadilika. Alienda chuo kikuu, na mara moja alihitimu, alikuwa na taalumu nzuri katika maisha yake na hakupoteza muda kwa shughuli za kijinga tena.

Wote akina Solinka na Maina walikuwa wakijaribu kufanya jambo sahihi—wakitumaini kwamba matendo yao yangechochea mabadiliko kamili kwa mtoto wao mtu mzima. Na seti zote mbili za wazazi walifanya uamuzi sawa. Lakini kulikuwa na aina mbili za matokeo yaliyotofautiana sana. Kwa familia moja uamuzi ulileta maafa, na kwa nyingine ulileta ukombozi. Tofauti ilikuwa nini? Tofauti, naamini, ilikuwa uwepo wa Mkombozi.

Ninajua kwa hakika kwamba Yesu alialikwa katika hali ya pili ya familia yaani familia ya Maina. Walikuwa waumini na Bwana alitawala mioyoni mwao. Roho Mtakatifu alialikwa kuhamia katika hali hii pamoja na mtoto wao, na wao na marafiki zao waliomba kwa bidii kwamba Bwana azungumze na moyo wa huyo kijana. Katika maombi walimwomba Mungu awamiminie Roho Wake wa Kweli juu ya mwana wao na kumwonyesha kile ambacho kilikuwa kikitendeka katika maisha yake kutoka kwa mtazamo wa Mungu.

Katika jela hiyo, Mungu alizungumza na moyo wake, na ikawa wazi kwake kwamba ingawa yeye alikuwa amefanya jambo la kipumbavu, hakuhitaji kuendelea kuishi kama mpumbavu. Alikuwa na chaguo. Kwa ufahamu wangu, wazazi wa mwana wa kwanza—wakina Solinka—hawakuwa

waumini na hawakuwa watu wanaosali. Mtoto wao hakuwa amejitoa kwa Bwana au kufundishwa njia za Mungu au kuombewa.

Hakuwa na faida ya maombi ya wazazi wake, familia, au marafiki kumlinda na kumsaidia kusikia kutoka kwa Mungu katika maisha yake. Sisemi kwamba watoto wazima wa wazazi wanaosali kamwe hawawezi kuwa na matatizo yoyote. Hakika wanakuwa nayo. Lakini mzazi akianza kuomba kwa ajili ya mtoto wao mzima, hata mambo mabaya yanapotokea yatatokea kwa wema.

Huenda tusiweze kuona kwa wakati huo, lakini Mungu atatumia hali zao na kuigeuza kuwa kitu chanya kwa namna fulani. Mungu hutumia kile tunachokiona kama matatizo kupata umakini wa vijana wetu na kuwafundisha kwamba hawawezi kuishi bila Yeye. Wakati mwingine mambo magumu yanayowapata ni kwa sababu ya huruma na upendo wa Mungu, unaofanya kazi katika maisha yao na kuwaokoa, kuwarekebisha, au kuwalinda kutokana na jambo baya zaidi (Mithali 3:11-12).

Ikiwa haujawahi kumwombea mtoto wako mtu mzima hapo awali, au ikiwa kuna mambo mabaya yamemtokea kabla hujajifunza kuomba, usifadhaike. Mungu ni Mkombozi. Ukombozi ni somo alilobobea, ni taaluma Yake. Na sio tu Yeye anakomboa maisha yetu na kifo na kuzimu na kutuokoa milele, bali pia anatukomboa kutoka kuzimu duniani. Mungu atatukomboa na hali ya kusumbua maishani mwetu anapoalikwa kufanya hivyo. Unapoomba kwa ajili ya mtoto wako mtu mzima, kuna baadhi ya mambo kuhusu Mungu ambayo ni muhimu wewe kuyaamini bila shaka:

1. Ni lazima uamini kwamba Mungu anakupenda wewe na watoto wako watu wazima na Atasikia maombi yako kwa ajili yao. Unahitaji kujua kwamba “vitu vyote hufanya kazi pamoja kwa ajili ya kuwapatia mema wale wanaompenda Mungu, kwa wale walioitwa kwa kusudi Lake” (Warumi 8:28). Ikiwa unampenda Mungu na unataka kuishi kwa njia Yake, basi ndivyo ulivyo; mmoja wa wale walioitwa kwa kusudi Lake. Mistari kabla tu ya huo inazungumza kuhusu maombi. Je, inaweza kumaanisha kwamba mambo yote hufanya kazi pamoja kwa manufaa katika maisha yetu tunapoomba?

2. Ni lazima uamini kwamba Mungu anaweza kukukomboa kutoka kwa woga wowote unaowahusu watoto wako wakubwa. Kilichokuwa kweli kwa Daudi ni kweli kwako pia. Daudi akasema,"Nalimtafuta BWANA akanijibu, akaniponya na hofu zangu zote" (Zaburi 34:4). Unaweza kumtafuta Bwana kuhusu watoto wako watu wazima, Naye atasikia na kukuokoa na hofu zako zote pia.

3. Ni lazima uamini kwamba Mungu anaweza kukupa wewe na watoto wako watu wazima kile unachohitaji unapoomba. Unahitaji kuwa na imani katika uwezo wa Mungu wa kusikia na kujibu. “Na aombe kwa imani, pasipo shaka yo yote; maana mwenye shaka ni kama wimbi la bahari linavyosukumwa na kupeperushwa huku na huku na upepo. Kwa maana mtu huyo asidhani kuwa yeye atapata chochote kutoka kwa Bwana; yeye ni mtu wa nia mbili, asiye na msimamo katika njia zake zote” (Yakobo 1:6-8). Hatuwezi kutarajia majibu ya maombi yetu bila kuwa na imani kwa Mungu

wetu tunayemwomba.

4. Ni lazima uamini kwamba, hata matatizo ya mtoto wako mtu mzima yawe makubwa kiasi gani, Mungu ni mkuu zaidi. Yesu alisema, “Yasiyowezekana kwa wanadamu yanawezekana kwa Mungu” (Luka 18:27 ) na “kwa Mungu mambo yote yanawezekana” ( Mathayo 19:26 ). Pia alisema kwa baba mmoja ambaye alikuwa akitafuta ukombozi kwa ajili ya Mwanae, “Ukiweza kuamini, mambo yote yanawezekana kwake yeye aaminiye” (Mk 9:23). Yeye ni Mungu wa yasiyowezekana, na hiyo ina maana Kwake Yeye mambo yote yanawezekana. Mungu anaweza kubadilisha chochote au mtu yeyote—hata wewe na mtoto wako mtu mzima— lakini ni lazima kwanza aalikwe katika hali hiyo. Hiyo hutokea tu unapoomba.

5. Ni lazima uamini kwamba kwa sababu upendo na nguvu za Mungu zimemiminwa ndani yako, maombi yako kwa ajili ya watoto wako watu wazima yatakuwa na nguvu daima. Kwa sababu maombi yana nguvu, wewe utakuwa na matumaini daima. "Matumaini hayakatishi tamaa, kwa sababu pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu ambaye tulipewa sisi” (Warumi 5:5). Roho Mtakatifu ni nguvu ya Mungu. Nguvu ya Mungu inapofanya kazi katika maisha yako, una matumaini kwa lolote. Orodha ya ahadi za Mungu kwako ni ndefu zaidi kuliko orodha yako ya mambo yanayohusu mtoto. Kila mtoto mtu mzima anahusika na matatizo. Hata watoto bora wanaweza bado wakapitia mambo magumu wanapokuwa watu wazima. Mtoto wako anaweza kuwa aliwekwa

wakfu kwa Mungu au kubatizwa, alimpokea Bwana, amekuwa katika shule ya Biblia na ibada kwa miaka 18, na amefundishwa nyumbani yote hayo, na bado wakati yeye yuko nje ya udhibiti wako anaweza kuingia katika baadhi ya changamoto kubwa, au kuanguka katika tabia mbaya, au kuchagua marafiki wasiohitajika, au kupata matokeo ya uchaguzi mbaya. Lakini habari njema ni kwamba Mungu anaweza kubadilisha hayo yote, wakati wowote wewe omba tu, usikate tamaa, maadamu una pumzi bado.

**4. Unatakiwa Kujua Lazima Uache Kulaumu**

Hebu wote tukabiliane na hali hii. Watoto ni safari ya hatia tangu wakati wanazaliwa. Tunakaa tukifikiri, Je, ninamlisha sana? Je, sikumlisha vya kutosha? Je! minafanya mambo kupita kiasi? Je, sifanyi vya kutosha? Je, nimetoa sana? Je, nini hajapewa vya kutosha? Na inafanywa kuwa ngumu zaidi na ukweli kwamba kila mtoto ni tofauti. Kwa hivyo kile kilichoonekana kufanya kazi kwa mtoto wa kwanza kinaweza kisifanyie kazi kwa mtoto wa pili. Mtoto wetu wa kwanza Daudi, tangu wakati alipoweza kusimama katika kitanda chake alikuwa na mawazo yake juu ya alichotaka kufanya na ni lini alipotaka kufanya hivyo, bila kujali wazazi wake walitaka nini. Ilichukua nidhamu kali na thabiti ili kumfanya aone hekima ya kutii mama na baba yake. Mtoto wetu wa pili Farida, alikuwa tofauti kabisa. Ilichukua tu mtupo mkali wa jicho wa kutokubaliana ikiwa alikuwa anafanya kitu kibaya. Nidhamu kali kwake ingekuwa mbaya kama tu nidhamu dhaifu kwake. Kila mara tulipambana na hatia, katika kujaribu kujua kama tulikuwa tukimshukia kwa nguvu sana au nguvu tuliyotumia ilikuwa haitoshi kwake. Hiyo si kusema hatukufanya makosa katika pande

zote mbili. Nyakati nwingine zilikuwa ngumu sana au rahisi sana kwa kila mmoja wao. Na tuliona matokeo ya hali zote mbili. Ilitubidi kumwomba Mungu hekima kila siku. Na nilipambana na hatia yote—mambo ambayo nilipaswa kufanya au kusema, lakini sikufanya, na mambo ambayo sikupaswa lakini nikafanya au kusema. Hatia ni muuaji wa moyo. Sisi wazazi tunajipiga fimbo kwa hatia kila wakati jambo baya linapotokea kwa mmoja wa watoto wetu kwa sababu tunaona jinsi labda sisi tungeweza kufanya mambo kwa njia tofauti na ikiwezekana kuizuia. Kwa mfano, ikiwa mtoto hapati maksi nzuri shuleni, tunajilaumu wenyewe. Ikiwa ana tatizo la kutopatana na rafiki, ni lazima kwa namna fulani tunafikiri lilikuwa kosa letu. Ikiwa anaumwa au kuumia, tunahangaika juu ya kile ambacho tungefanya kwa njia tofauti. Na tunafanya hivi hata zaidi wanapokua. Wakati sisi tunaona kitu kwa mtoto wetu mtu mzima ambacho tunahisi si sawa, au kinachokiuka nini tuliamini katika misingi yetu ya malezi, inatufanya tujiulize, Je, ni wapi tulikosea? Tunapoona kitu ndani yake ambacho ni udhaifu, tunaogopa na kujilaumu. Hata kama umefanya jambo ambalo unajua limeathiri mtoto wako vibaya, bado unapaswa kuacha kulaumu au kujilaumu. Labda unajuta kwa kutokuwepo karibu vya kutosha katika utoto wake. Au kulikuwa na matukio ambayo umekosekana katika maisha ya mtoto ambapo unajua unapaswa kuwa huko. Au unahisi ulikuwa labda mkali sana au mpole sana. Au umesema kitu ambacho unatamani usingesema, au kuna mambo ulipaswa kufanya ambayo hukufanya. Hakuna kitu kinawezekana kufanyika sasa ili kufuta au kufanya hali ionekane kana kwamba haijawahi kutokea. Lazima upate uombe msamaha tu na kusonga

mbele kwa kuomba hekima ya Mungu, na hilo linaweza tu kufanywa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.

Kazi yako ya kwanza katika kitabu hiki ni kuondoa hatia hiyo yote! Ili kuwa na ufanisi katika kumwombea mtoto wako mtu mzima, lazima uache kujilaumu kwa kila jambo linaloenda vibaya. Mpe Mungu sifa kidogo hapa. Kama umefanya makosa, yakiri mbele za Bwana na mbele ya mtoto wako pia, ikiwa hiyo italeta uponyaji ili uweze kufurahia uhuru wa msamaha wa Mungu kwa ajili yako. Jiulize, "Je, ninaweza kufanya lolote kuhusu hilo sasa?" Kama ndivyo, fanya. Ikiwa sivyo, mpe Mungu nafasi na umwombe akukomboe kutokana na hali hiyo na kukuponya katika mchakato huo. Hii ni kuchukulia, bila shaka, kwamba unamjua Bwana. Kama hujawahi kumpokea Mwenyezi Mungu kuwa Mfalme na kiongozi maishani mwako, mwambie aingie moyoni mwako sasa na akusamehe dhambi zako zote na kushindwa kwako na kukujaza na Roho Wake Mtakatifu. Mshukuru kwamba alikufa msalabani kwa ajili yako ili upate ondoleo la dhambi na uzima wa milele pamoja naye. Kisha mwombe akutakase kutokana na madhara ya kushindwa na kuumizwa hapo awali, na akusaidie kuishi kwa njia Yake sasa. Mwambie akuweke huru kutoka kwa hatia.

Kuna njia mbili tu za kuzuia hatia kama mzazi. Ya kwanza ni kukubali kuendelea kubeba hatia ambayo itasababisha kifo chako mapema. Pili ni kutembea na Mungu kila siku na kumwomba hekima kwa kila jambo. Ninasema kwamba kutembea na Mungu ndilo suluhisho bora zaidi katika hayo mawili. Unapotembea na Mungu, huwezi kumwendea tu kupata

mwongozo, unaweza pia kumwomba akuweke huru kutokana na hatia yoyote unayohisi kama mzazi. Bila shaka, kuna baadhi ya wazazi ambao hawajilaumu kamwe kwa lolote.

Badala yake, wanalaumu kila mtu mwingine. Wanasema mambo kama vile, "Binti yangu amepata matatizo kwa sababu ya wasichana wengine aliokuwa nao." Au, "Mwanangu ni mvivu kwa sababu baba yake hakuwahi kumlazimisha kufanya lolote nyumbani." Lakini kuwatupia lawama wengine badala ya kuipeleka kwa Mungu hairuhusu mzazi au mtoto kupata uzoefu mzuri wa namna Mungu anaweza kuwatoa katika hali ngumu. Kuna ukuaji mkubwa wa tabia wakati mtoto anahimizwa kuona matokeo ya kushiriki katika jambo lolote baya walilofanya.

**5. Jua Kwamba Unatakiwa Kusamehe**

Sote lazima tukumbushwe kwamba kutosamehe kunaweza kuingia na kuvizia pembe za siri za mioyo yetu, na tunaweza kuipa hali hii nafasi bila hata kutambua ni nini. Ndiyo maana ni lazima mara kwa mara tumwombe Mungu afunue hali yoyote ya kutokusamehe ndani yetu—hasa kwa wanafamilia wetu. Msamaha unapaswa kutiririka ndani yetu kabla ya nguvu za Roho Mtakatifu kutiririka kupitia sisi tunapoomba. Biblia inasema, "Nikiutafakari uovu moyoni mwangu Bwana hatasikia" (Zaburi 66:18). Mojawapo ya maovu makubwa ambayo mara nyingi tunashikilia ndani ya mioyo yetu, ni kutosamehe. Hiyo ni kwa sababu ni rahisi sana kufanya hivyo. Tunaweza hata kujidanganya na kujifanya kuwa hakuna jambo ambalo hatujalisamehe. Na ni rahisi sana kujificha kutoka kwa wengine,

kwa sababu ingawa watu wengi wanaweza kuiona hali hii kwenye nyuso zetu au katika mtazamo wetu, hawawezi kutambua ni nini.

Lakini Mungu huiona daima, na haipendi. Yeye Anataka tuondoe hali za kutosamehe, na wakati mwingine Atasubiri kujibu maombi yetu hadi tutakaposamehe. Kwa kweli tunahitaji kusamehe kila mtu, lakini kwa kuwa ninazungumza juu ya watoto wetu wakubwa hapa, nimekuwekea orodha fupi lakini muhimu ya kufanya kwa ajili yenu, katika kuangalia mbali. Nataka tu uwe huru ili maombi yako yaweze kuwa na nguvu. Jikumbushe kuwasamehe watu wafuatao. Ikibidi, andika haya kama kumbukumbu kwako mwenyewe.

## UJUMBE WA KWANZA KWAKE MWENYEWE:

Nawasamehe watoto wangu wakubwa kwa chochote ambacho wanaweza kuwa wamefanya ili kuniumiza, kunikatisha tamaa, kupuuza, au kunikasirisha. Mwambie Mungu akuonyeshe ikiwa una kitu chochote ndani yako ambacho ni kidogo na kinachohitaji kumsamehe yeyote kati ya watoto wako walio watu wazima na hiyo inajumuisha wakwe zako pia wa kike na wa kiume. Ruhusu hewa safi kati yenu. Ikiwa wameonyesha kutowajibika, kupuuza, ufidhuli, kutokuwa na mawazo, au kutojali, au walifanya jambo ambalo lilikuumiza, kiri hisia zako kuhusu hilo kwa Bwana. Hili ni jambo la muhimu sana, kwa sababu sisi wazazi huwa tunajifikiria sisi kuwa hatuwezi kushikilia chochote dhidi yetu, au watoto wetu watu wazima. Hatupendi tunapoona aina hiyo ya kitu kwa wengine.

Lakini wakati mwingine mambo haya hupata makao katika mioyo yetu. Kukatishwa tamaa ni jambo lingine la hila ambalo tunaweza kushikilia dhidi ya watoto wetu wakubwa wakati wowote ambao hawakuishi kulingana na matarajio yetu kwao, iwe ilithibitishwa au la. Kwa hivyo ninamaanisha matarajio yetu yanaweza kuwa pia kutokuwa na busara kwa mtoto huyo, lakini bado tunaweza kuwa na matarajio na tukakata tamaa. Tunapaswa kuleta kila hali ya kukatishwa tamaa mbele za Bwana na kuitoa Kwake ili tumsamehe kabisa huyo mtoto mkubwa kwa kutuangusha. Ikiwa hutawasamehe watoto wako wakubwa kwa chochote walichofanya zamani, unaweza kujikuta unawaletea shida au kuruhusu chuki yako toka nje kwa muda mrefi usio na ulinzi. Unaweza pia kuhitaji kusema kitu kwa mtoto wako mkubwa juu ya ukweli kwamba umewasamehe kwa jambo fulani maalum, lakini muombe Mungu akupe hekima juu ya hilo. Wanaweza kuwa hata hawajui unashikilia hilo dhidi yao, kwa hivyo kuna faida kidogo kuwajulisha sasa, isipokuwa pale itakapowafafanulia kitu ambacho wamehisi, au kitaponya mahusiano yenu.

Usiseme maneno kama, "Nimekusamehe kwa kuwa mjinga na kuharibu sifa ya familia yetu." Sema badala yake, “Ninatambua kuwa nimeshikilia baadhi ya mambo dhidi yako wewe, na ikiwa nimetenda kwa njia isiyo na msamaha kwako, ninasikitika sana hiyo. Nataka ujue kuwa ninakusamehe kwa makosa yako yote ya zamani, na mimi nakuomba unisamehe makosa yangu yote pia.”

Mwombe Mungu akuonyeshe kile unachohitaji kusema, ikiwa kuna

chochote. Yeye atajua muda kamili na Anaweza kukupa maneno sahihi. Na ukimuomba, Yeye pia atatayarisha moyo wa mtoto wako mkubwa kuyapokea haya. Ikiwa una kutosamehe kwa mkwe binti au kijana, ushauri wangu ni kupeleka kwa Mungu kwanza kabla hujaipeleka kwao. Tengeneza moyo kuweka mambo sawa na Bwana. Huu ni uhusiano nyeti sana na wa juu sana wenye thamani. Kuna mengi sana hatarini na nafasi kubwa sana kwa mtu kutokuelewana ambayo inaweza kuwa mbaya. Ushauri wangu ni kwenda kwa mkwe tu kwa kukiri kwa upande wako. Kwa mfano sema, “Ninahitaji kukuomba msamaha kwa jambo nililosema.”

Usimwambie mkwerima au mkamwana au mzazi wake kwamba utamsamehe ikiwa ataomba msamaha kwako. Kwa mfano, usimwambie mkwerima wako, "Nimesamehe kwa kumchukua binti yangu na kuharibu maisha yake.” Na usiseme kwa mkamwana, "Nimekusamehe kwa kutumia pesa zote za mwanangu sasa lazima uangaike na kutafuta riziki.” Kumbuka kwamba unataka kuona wajukuu zako siku moja.

Kusamehe watoto wako wakubwa ni muhimu sana kwa kila mtu anayehusika. Omba Mungu akusaidie. Mwambie afichue kitu chochote ambacho unaweza kuwa hukioni. Ikiwa unaona kuwa watoto wako watu wazima wanapaswa kukuomba msamaha, omba kwamba wataweza kufanya hivyo. Walakini, usisubiri tu. Anza kusonga mbele na kujua la kufanya na kuomba ili litokee mioyoni mwao pia.

**UJUMBE WA PILI KWAKE MWENYEWE:**

Msamehe mzazi mwingine wa mtoto aliye mtu mzima. Kuna uwezekano

mkubwa kwamba wengi wetu tumeona kitu kwa mzazi mwingine wa mtoto mtu mzima ambaye tungependa kuona akibadilishwa. Hii inaweza kuwa jambo ambalo limeathiri mtoto wako kwa njia mbaya. Ukiona baadhi ya udhaifu au kasoro ya tabia katika mtoto wako mtu mzima ambayo unamlaumu mwenzi wako, muombe Mungu akusaidie umsamehe mume wako au mke wako na uachane na hayo kwa wema.

Omba Mungu ausafishe moyo wako ili uwe huru kuendelea mbele. Kilichofanyika kimefanywa, na unahitaji kuwa huru kuanza kumwombea mtoto wako mtu mzima kwa moyo safi sasa. Daima nimesema, na nimeiandika katika vitabu vyangu vyote, kwamba kusamehe mtu hakumfanyi mkosaji kuwa sawa; bali hukufanya wewe uwe huru. Lazima uwe huru. Ikiwa unaomwombea mtoto wa mtu mwingine aliye mtu mzima, mwombe Mungu akusaidie kupata moyo wa kusamehe kwa mzazi-mwenza mwingine. Ombea chochote unachokiona kibaya katika mtoto huyo.

Mtoto mtu mzima anaweza kulaumiwa kwa urahisi na mzazi huyo, na chuki inaweza kusitawi ndani ya moyo wako juu yake. Haijalishi ni nini kimeendelea huko nyuma, ni wakati wa kuruhusu yote kufagiliwa mbali. Madhara ya kutosamehe ni makubwa sana kuweza kuruhusu kuendelea. Tena, aina hii ya kutosamehe inaweza kuwa ngumu kugundua. Ikiwa hisia za kutosamehe zimekuwa za muda mrefu, zinaweza kuwa sehemu yako sana kiasi kwamba huna hamu hata kuwaona. Ndio maana unapaswa kumwomba Mungu akuonyeshe. Sema, “Bwana, nionyeshe mimi ikiwa nina kutokusamehe au chuki yoyote ndani yangu kwa mzazi mwingine wa

mtoto wangu mtu mzima." Utashangaa jinsi Mungu atakavyojibu ombi hilo haraka- Baba au mama wa mtoto, hasa kama mmeachana.

## UJUMBE WA TATU KWAKE MWENYEWE:

Msamehe mtu yeyote ambaye alimkosea mtoto wangu katika siku za nyuma au alimfanyia ubaya kwa njia yoyote. Nakumbuka kocha mmoja mtu mzima ambaye alimdhalilisha mmoja wa watoto wangu wadogo wakati fulani na kumbukumbu yake iliniumiza mimi na mtoto wangu. Ilikuwa nje ya utaratibu kabisa na ilifanyika mbele ya wachezaji wenzao na wazazi wao. Ilikuwa jambo la kikatili kufanya, na ninaamini lilifanywa kwa roho ya wivu ndani ya kocha huyo. Lakini ilinibidi kulileta mbele za Bwana mara kadhaa ili kulitoa katika moyo na akili yangu.

Miaka mingi baadaye mtoto wangu alipokuwa mtu mzima, ilinibidi kuombea kuhusu jambo hilo tena kwa sababu niliona mambo kwa mtoto huyo ambayo nilifikiri ni matokeo ya moja kwa moja ya tukio hilo. Niliomba, "Bwana, ninainua kumbukumbu ya tukio hilo la kuumiza Kwako na kukiri kwamba bado linanikera. Lakini muhimu zaidi, nahisi imesababisha maumivu ndani mtoto wangu ambaye ameyabeba maumivu kwa miaka mingi, na labda athari zake bado zinaonekana.

Sitaki kuibeba ndani yangu tena, na hakika sitaki mtoto wangu kuyabeba haya pia. Nimemsamehe kocha huyo kwa maneno hayo ya kuumiza. Badili mtazamo wangu kwa mtu huyo. Zaidi ya yote, ponya moyo wa mtoto

wangu mtu mzima na uujaze kwa msamaha kamili kwa mtu huyo na tukio hilo."

Mwombe Mungu akuonyeshe ikiwa kuna jambo lolote kutoka zamani lililotokea kwa mtoto ambaye bado anakusumbua na kukufanya uhisi chochote hasi. Unahitaji kuliondoa kwa sababu linachanganya akili yako na linaweza kuingilia kati uwezo wako wa kuomba kwa ufanisi.

## UJUMBE WA NNE KWAKE MWENYEWE:

Nisamehe Bwana kwa lolote hapo awali ambapo nilihisi ningeweza kufanya vizuri zaidi kama mzazi. Muombe Mungu akuonyeshe ni wapi una majuto yoyote kuhusiana na kulea watoto wako. Ikiwa kuna mambo bado unajipiga teke, au ikiwa wewe unashtuka unapofikiri juu ya kile ambacho unatamani ungesema au kufanya—au laiti usingesema au kufanya—basi ulete mambo hayo mbele za Bwana. Omba Bwana akusamehe na kukusaidia kujisamehe mwenyewe. Mwambie unataka kuwa na moyo safi ili uweze kuanza upya kama mzazi wa mtoto aliye mtu mzima anayesali. Ikiwa hautaachiliwa kwa hili, adui wa roho yako atakuwa akilitumia kila wakati dhidi yako.

Ikiwa umefanya makosa—na hebu tuchukulie kwamba sote tuna makosa na —tuombe Mungu alete ukombozi. Hata kama umetembea na Mungu na kujaribu kuishi kwa njia yake, lakini kuna hofu kwamba umefanya makosa katika kulea mtoto wako, mlete mbele za Mungu sasa. Usipoteze wakati mwingine wa maisha yako na hatia na hukumu mabegani mwako. Sema, "Bwana, ninakiri ninahisi majuto na hatia kuhusu baadhi ya mambo ambayo

mimi nilifanya au sikufanya kama mzazi. (Ungama maelezo yoyote mahususi yaliyo moyoni mwako.) Nisaidie niachane na yaliyopita na nisiangalie nyuma, bali nisonge mbele na Wewe." Omba Mungu akupe uwezo pia wa kuomba msamaha kwa watoto wako wakati umethibitishwa.

Watoto wako wakubwa wanahitaji kusikia maneno "Nisamehe" kama vile wewe unavyohitaji. Hii itawaweka huru pia. Ikiwa wanahitaji kukusamehe kwa chochote, wao watakwama pale walipo na kushindwa kusonga mbele katika maisha yao hadi wao wamesamehe pia. Ukishaungama hayo yote na moyo wako uwe safi mbele za Bwana, fahamu kwamba hukumu yoyote au hatia unayojisikia sasa itakuwa inatoka kwa adui wa nafsi yako. Na hapo ndipo lawama zinapaswa kuwekwa. Jumbe hizi fupi ambazo umesoma hivi punde ni muhimu sana. Usipuuze lolote katika maeneo haya manne ya msamaha, kwa sababu kila moja linaweza kuzuia majibu ya maombi yako.

## 6. Unatakiwa Kujua Kuna Mzazi Mmoja Tu Mkamilifu Naye Ni Mungu Wa Mbinguni

Hebu tuwekane wazi. Hakuna wazazi wakamilifu. Hiyo ni kwa sababu hapana mtu duniani aliye mkamilifu. Kumewahi kuwa na mzazi mmoja tu mkamilifu, na huyo Ndiye Mungu Baba yetu. Wewe na mimi ni watoto Wake watu wazima. Na unajua ni shida ya kiasi gani Amekuwa nayo katika safari ya kutulea. Lakini Yeye kila wakati, Yupo akitungojea sisi kuja Kwake na hisia zetu na kufanya mambo kwa njia yake. Kwa sababu Yeye Ndiye mzazi bora, Yeye ndiye pekee ambaye anaweza kutusaidia sana

kuwa mzazi bora kwa watoto wetu watu wazima. Inatubidi tujifunze kutoka Kwake. Biblia inasema “mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataicha hata atakapokuwa mzee” (Mithali 22:6). Hiyo ni habari njema kwa wale ambao waliwazoesha watoto wao katika njia za Mungu tangu utotoni. Lakini vipi kuhusu wazazi wote ambao hawakumjua Bwana na njia Zake wakati wao walikuwa wakiwalea watoto wao, na hivyo watoto wao watu wazima na hawatembei katika mambo ya Mungu sasa? Je, wamechelewa mno na hawawezi kufanya lolote?

Je, vipi kuhusu sisi ambao tulimjua Bwana tulipokuwa tukilea watoto wetu, na tulikuwa tukitembea katika njia za Bwana jinsi tulivyojua, lakini bado tulikuwa chini ya viwango vya wazazi wasio wakamilifu? Je, sisi tunapotazama nyuma tunaweza hatutamani kufanya mambo kadhaa tena, tunapojua tunachokijua sasa, kuwa na nafasi ya kufidia muda uliopotea? Siamini kuwa tumechelewa sana, leo tunaposikia sauti ya Mungu, naam yeyote kati yetu ambaye anamjua Bwana, tunatii sauti Yake, na kusahau yaliyopita, kuandamana Naye. Hiyo ni kwa sababu Mungu ni Mkombozi, na hatujachelewa sana kumwona akifanya kazi ya ajabu ya ukombozi katika kujibu maombi yetu—hasa maombi kwa ajili ya watoto wetu watu wazima.

Ikiwa hujatembea na Mungu katika miaka yako ya awali ya uzazi na mtoto wako ni mtu mzima sasa, nenda mbele za Mungu na uungame Kwake. Sema, “Bwana, mimi nakiri kwamba sikukujua, wala sikuishi njia Yako, wala sikukutafuta nilipokuwa nikilea mtoto wangu. Nisamehe kwa makosa yoyote niliyofanya. Nisaidie nitengeneze yote, kwa kuishi katika njia Yako

sasa. Nionyeshe jinsi ya kumwombea mtoto wangu mtu mzima jinsi ambavyo Wewe ungetaka nifanye."

Nina hakika kwamba kupitia maombi yetu, na upendo Wake na rehema, Mungu anaweza kufundisha watoto wetu vitu ambavyo hatukufanya. Ndiyo maana nilichagua kuandika kitabu kinachozungumzia hili. Katika kifungu hiki Mungu anazungumza na watu Wake— kupitia nabii Isaya—Maneno ya tumaini na ahadi za urejesho. Anasema kwa hakika kama ahadi aliyoitoa "kwamba maji ya Nuhu hayatakuwapo tena kuifunika dunia," Pia anaahidi kwamba "milima itaondoka na vilima vitaondolewa, lakini fadhili Zangu hazitaondoka kwako" (Isaya 54:9-10). Yeye inasema juu ya ahadi hizi kwamba huu ni "urithi wa watumishi wa BWANA" (Kifungu cha 17). Katikati ya ahadi hizi nyingi, kuna ahadi ambayo kila mzazi anapaswa kuiweka karibu na moyo wake: "Watoto wako wote watafundishwa na BWANA, na amani ya watoto wako itakuwa nyingi" (mstari 13).

Ni ahadi kubwa kama nini kwa watu wote wa Mungu! Bado tunanufaika na ahadi kuhusu gharika ya Nuhu, kwamba hayatawahi tena kufufuka duniani kama yalivyofanya katika siku za Nuhu. Na Mungu anatoa ahadi kwamba Yeye atawafundisha watoto wetu, hivi ni hakika atafanya hivyo. Ndio maana tunaweza kudai ahadi hii kwa watoto wetu watu wazima. Walakini, kwa sababu tu tunaelewa kitu katika Neno la Mungu kuwa ahadi kwetu haimaanishi inatokea tu moja kwa moja. Ni lazima tusali juu yake. Omba kwamba ufahamu wako wa ahadi katika Neno la Mungu utaongeza imani ya kuomba na kuamini kwa ajili yao kupata utambuzi katika maisha yao.

Pale tulipodhani kuwa wewe na mimi tungefanya vizuri zaidi, tulijua hakika jinsi wakati huo tulipolea watoto wetu, na tuna uhakika kwamba hatukuwa wazazi wakamilifu, tunaweza kutumaini kwamba watoto wetu bado wanaweza kufundishwa na Bwana leo na kwa maisha yao yaliyosalia. Wanaweza kujifunza mambo ambayo hatukuwafundisha au ambayo hatukuwafundisha vizuri kama tunavyopaswa.

Je, tuliwafundisha jinsi ya kupigana na wenzi wao kwa sababu sisi tulipigana na wenzi wetu? Je, tuliwafundisha kuwa watu wazima wenye shughuli nyingi sana kiasi cha kukosa muda na watoto wao, hivyo basi watakuwa na shughuli sana kiasi cha kukosa muda na familia zao? Je, tuliwafundisha kuwa hawahitaji kufanya kazi kwa bidii kwa sababu tulifanya maisha yawe rahisi sana kwao kupata kila kitu walichotaka? Je, tuliwafundisha kwamba hawahitaji kwenda kanisani kwani ndivyo tulivyowaonesha mfano? Chochote ambacho hakikuwa kamili kuhusu jinsi tulivyowafundisha watoto wetu, Mungu anaweza kuwakomboa nacho na kuwafundisha yale ambayo wana haja ya kuyafuta sasa. Lakini tunahitaji kuomba ili hilo litokee.

## 7. Unahitaji Kujua Na Unaweza Kusema Kwa Moyo Wako Wote,

“Nilimuombea Mtoto Huyu Mzima” Maneno matano kati ya hayo sita katika nukuu hapo juu yalisemwa na Hana katika Biblia, ambaye alikuwa ameomba na kuomba kwa ajili ya kupata mtoto. Hana “alikuwa na uchungu rohoni, na akamwomba BWANA akalia kwa uchungu” (1 Samweli 1:10)

kwa kukosa mtoto. Kisha akaweka nadhiri kwa Bwana kwamba kama angempa mwana, atampatia Bwana kwa maisha yake yote. Bwana alisikia maombi yake, Naye akaruhusu kuzaliwa kwa mtoto wa kiume mwaka uliofuata.

Mtoto alipokuwa na umri wa miaka mitatu hivi, Hana alimpeleka hekaluni na akamkabidhi kwa Bwana kama alivyoahidi. Akamwambia kuhani, "Niliomba mtoto huyu kwa Bwana, na BWANA akanipa dua yangu niliyomwomba. Kwa hiyo mimi nami nimemkabidhi Bwana; muda wote atakaokuwa hai atakopeshwa BWANA" (1 Samweli 1:27-28). Na kisha akamwabudu Mungu. Angalia Maneno katika italiki. "*Naliomba kwa ajili ya mtoto huyu; BWANA amenijalia dua… nami nimemkopesha BWANA"*. Kumbuka Maneno hayo unaposoma kitabu hiki.

Kisa cha Hana ni moja wapo ya mifano mikuu ya maombi ya bidii ya mzazi na yasiyo na kikomo. Imekuwa uchunguzi wangu katika Neno, na katika maisha, kwamba kadiri bidi inavyoongezeka katika maombi, ndivyo ambavyo Mungu atafanya mambo makuu kupitia wao. Ndio maana sitaki ukate tamaa unapoomba kwa ajili ya mtoto wako mtu mzima. Nataka uwe na bidii. Matokeo ya maombi ya Hana ya bidii, ya muda mrefu yalikuwa kwamba amzae mtoto wa kiume na akamzaa Samweli, ambaye alikuja kuwa mmoja wa viongozi wakuu na wenye ushawishi mkubwa na wenye nguvu katika Israeli yote, kiserikali na kidini. Huwezi kujua ni mambo gani ya ajabu na makuu utazaa ndani ya maombi yako ya dhati kwa mtoto wako mtu mzima. Lakini kwanza ni lazima ufanye kile ambacho Hana alifanya na

umkabidhi mtoto wako mtu mzima kwa Bwana. Unapaswa kumwachilia mtoto wako mikononi mwa Mungu. Yote katika Agano la Kale na ndani ya Agano Jipya ni mifano ya wazazi kuwatoa watoto wao kwa Bwana. Ni muhimu kufanya hivyo mapema iwezekanavyo. Ni lazima iwe wazi kwa wote hasa adui kwamba huyu mtoto ni wa Bwana. Ikiwa haujawahi kufanya hivyo, unaweza kuifanya sasa. Sema, "Bwana, mimi sasa namkabidhi ……. (jina la mtoto mzima) Kwako. Ninamweka wakfu Kwako kwa ajili ya utukufu Wako. Ingawa ninaona kutoka kwa Neno Lako kwamba ni vizuri kufanya hivi tangu utoto, Pia ninajua kutoka kwa Neno Lako kwamba sijachelewa sana kufanya jambo sahihi. Namwachilia mikononi Mwako sasa."

Ikiwa tayari umemweka wakfu mtoto wako kwa Mungu, sema, "Bwana, ninamweka wakfu tena …….. (jina la mtoto mzima) mikononi Mwako. Ninaomba akutumikie Wewe siku zote za maisha yake na kwamba yeye atakututukuza kwa kila njia. Kwa muda mrefu kadiri atakavyoishi ninaomba kwamba atakuwa chini ya macho Yako. Ninamwachilia tena mikononi Mwako. Katika Jina la Yesu ninaomba."

Basi mwabudu Mungu kama Hana alivyofanya, na umtukuze Yeye Aliye mkuu kuliko lolote ambacho wewe au mtoto wako mtu mzima mtakabiliana nacho sasa au mtakachowahi kukutana nacho katika siku zijazo. Asante Mungu kwa zawadi zote kuu ambazo Mungu Umeweka ndani yake. Msifuni Mungu kwa ajili ya mambo ya ajabu ambayo anaenda kufanya katika maisha yake kupitia maombi yako. Njia pekee ya kuwa na amani

kuhusu mtoto wako mtu mzima ni kujua kwamba unayo nafasi ya kumfunika mtoto wako katika sala. Wakati unaweza kusema kama Hana, “Kwa ajili ya mtoto huyu mimi nimeomba,” ndipo utajua kwamba umefanya jambo kuu zaidi unaloweza kumfanyia. Unapoweza kusema, “Bwana amejibu maombi yangu,” utaweza kuwa na furaha katika nafsi yako. Na wakati umewaacha watoto wako watu wazima kwa Bwana, utakuwa na amani, ukijua umewaweka mbinguni kwenye Mikono ya BABA, ambaye Ndiye mzazi mkuu kuliko wote. Elewa kuwa kazi yako kama mzazi haina mwisho, na sio lazima iwe mzigo mzito. Inaweza kuwa changamoto yenye kuthawabisha. Mungu amekupa nafasi kwa kila mmoja wa watoto wako watu wazima kuwafunika katika sala, na kuwapenda na kuwaunga mkono kwa njia yoyote ambayo wewe na Bwana mwaona inafaa kufanya. Ni upendeleo kumtumikia Bwana kwa njia hii, ukijua unafanya kazi pamoja Naye kuona kwamba hawa watoto Wake wa thamani hawapotei, hawaharibiwi, au kuvutiwa na kuondoka kwenye njia Yake kutokana na baraka alizo nazo kwao. Na hii ni kweli bila kujali umri wao. Najua watu wa miaka ya themanini na tisini wanaowaombea watoto wao walio na umri wa miaka sitini na sabini. Rafiki yangu Idela, kila anaponiita, anawaombea watoto wake wa miaka 74 na zaidi ambao waliacha imani, na hawasomi Maandiko au kwenda kwenye Ibada. Kumbuka kwamba sikusema kamwe kuna mwisho wa kuwaombea watoto wako. Hata kama una mtoto mtu mzima ambaye amepotea njia ambayo Mungu amemwekea au ambaye hajawahi kuwa kwenye njia sahihi kuanzia azaliwe, jua kwamba maombi yanaweza kumsaidia kusikia kutoka kwa Mungu na kuweza

kufanya maamuzi ya busara na kuishia pale anapotakiwa kuwa. Wakati Mungu hatakiuka mapenzi ya mtoto wako mtu mzima, maombi yako bado yana ushawishi mkubwa katika maisha yake. Maombi yanaweza kufungua milango inayohitaji kufunguliwa na kufunga milango inayohitaji kufungwa. Ikiwa unaanza tu kuombea MTOTO WAKO MKUBWA, inaweza kuchukua muda kubadili chombo hicho kuzunguka na kuelekeza katika mwelekeo mpya. Endelea kuomba hata chochote kinapotokea, na usikate tamaa. Wakati hakuna dhamana kwa matokeo ya matendo yaliyozaliwa na hekima ya kianadamu, kuna dhamana inakuja kwa maombi na moyo wa Mungu. Ikiwa unaomba kwa Mungu kwa yasiyowezekana kwa ajili ya mtoto mtu mzima ambaye yeye mwenyewe ameshindikana au anayeonekana kuwa katika hali isiyowezekana, hii inamaanisha utakuwa na fursa ya kushuhudia muujiza.

Hatuna tena udhibiti wa watoto wetu watu wazima. Hatuwezi kuwafanya wafanye tunachotaka. Lakini kwa kusali, tunaweza kuwasaidia wasikie kutoka kwa Mungu ili YeyeAweze kuwaongoza kufanya Anachotaka. Kwa maombi yetu tunaweza kuwasaidia kuepuka mitego ya maisha na mitego ya adui iliyoundwa ili kuwaharibu. Sio kwamba tunajaribu kusali kila tatizo liende mbali nao na hata kama ndivyo inavyowezekana, hapo hawatakua kamwe na kujifunza masomo wanayohitaji kujifunza. Lakini tunaweza kuwasaidia kukaa kwenye njia sahihi ili waweze kuinuka na kuishi ile mipango Mungu aliwaumbia waiishi au kuwa.

Hatujui kila mara maelezo mahususi ya kile tunachohitaji kuombea watoto

wetu watu wazima, kwa sababu mara nyingi hutujulisha tu kile wanachotaka sisi tujue. Lakini tunapojua mambo maalum ya kuombea kuhusu maisha yao, kwa vyovyote vile tunapaswa kusali kuhusu mambo hayo. Hata hivyo, kuna njia ya kuwaombea kila siku watoto wako watu wazima, bila kujua hitaji lao maalum, maombi ambayo yatashughulikia maisha yao na kuwaweka katika njia ambayo Mungu amewawekea.

Sura 15 zinazofuata zina njia 15 za kuwaombea watoto wako watu wazima, na haijalishi kinachoendelea katika maisha yao. Iwe maisha yao ni kamili, au kila kitu kinaenda mrama, au mahali fulani katikati kuna mambo yamegeuka, basi omba juu ya mambo hayo na hii itawalinda, na kuwafanya wasogee katika mwelekeo sahihi, na kukupa amani ndani ya mchakato. Sura nne za kwanza ni  msingi muhimu kwa zingine, kwa hivyo soma haya kwa mpangilio ili uweze kuweka msingi. Basi unaweza kusonga kupitia sura nyingine 11 kwa mpangilio wowote unaotaka, kulingana na wasiwasi wako mkubwa.

Kwa sababu hakuna mtu aliye na mzigo wa moyo kwa WATOTO WAKO WAKUBWA kama ulionao wewe, maombi yako kwa ajili yao yatakuwa na bidii ambayo hakuna mtu mwingine atakuwa nayo. Haya, na tuendelee kuanza?

## NGUVU YA MAOMBI

Bwana, naomba unifundishe jinsi ya kuwaombea watoto wangu watu wazima. Asante kwa kuwa unanipenda mimi na watoto wangu na utasikia maombi yangu kwa ajili yao. Niweke huru kutokana na wasiwasi wote

nilionao juu yao ili nipate amani. Najua Wewe ni mkuu kuliko chochote wanachokabiliana nacho. Asante kwa sababu Upendo Wako na nguvu Zako zimemiminwa ndani yangu, maombi yangu kwa ajili yao yatakuwa na nguvu. Nisaidie nisijilaumu kwa mambo yanayoenda mrama katika maisha yao. Pale ambapo mimi nimefanya makosa, ninayakiri hayo Kwako na na kuomba uwakomboe wote na kunifungua kutoka katika hatia. Nisaidie kuwasamehe watoto wangu watu wazima kwa lolote walilofanya kuniumiza au kunikatisha tamaa. Nisaidie kuwasamehe watoto wangu kwa lolote ambalo nahisi nilikosea kuwalea. Nisaidie kumsamehe mtu yeyote ambaye amewaumiza watoto wangu watu wazima kwa njia yoyote. Nisaidie kujisamehe mwenyewe kwa wakati wowote nahisi kuwa sijawa mzazi bora.

Bwana, najua Wewe Ndiye mzazi pekee mkamilifu. Asante kwa kumpenda mtoto wangu mtu mzima kama mimi. Asante kwa kusikia maombi yangu kwa ajili yao. Nipe imani ya kuamini na subira ya kusubiri majibu. Leo nasema, "Kwa huyu mtoto nimeomba, na ninakushukuru kwamba Wewe, Bwana, umesikia maombi yangu nami naomba unipe dua yangu" (1 Samweli 1:27). Ninakupa sifa na utukufu wote. Katika Jina la Yesu ninaomba. AMINA

Kwa ujumbe maalum kutoka kwa Stormie, ambaye ametupa mengi ya kuombea watu wazima tafadhali tembelea tovuti http://bit.ly/PrayForAdultChildrenIntro

**NGUVU YA NENO**

Huu ndio ujasiri tulio nao Kwake, ya kwamba, tukiomba kitu sawasawa na

Mapenzi Yake, anatusikia. Na kama tukijua ya kuwa anatusikia, tumwombalo lolote, tujue kwamba tunayo maombi tuliyomwomba.

**1 YOHANA 5:14-15**

Nafsi yangu, umngojee Mungu peke yake, kwa maana matarajio yangu yanatoka Kwake.

**ZABURI 62:5**

Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtapata; bisheni nanyi mtafunguliwa. Kwa maana kila aombaye hupokea, naye atafutaye huona, na kila anayebisha atafunguliwa.

**MATHAYO 7:7-8**

Kwake Yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo; kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu, Kwake Yeye uwe utukufu katika kanisa na katika KristoYesu kwa vizazi vyote, milele na milele.

**WAEFESO 3:20-21**

Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba pamoja na kushukuru.

**WAKOLOSAI 4:2**

## OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE KUMTAZAMA MUNGU AKIMIMINA ROHO WAKE JUU YAO.

Mara tu unapowaachilia watoto wako watu wazima mikononi mwa Mungu na kujiweka wakfu au waliojitoa upya Kwake (kama nilivyoeleza kwenye ukurasa wa 28), ndipo njia ya kwanza na muhimu sana ya kuanza kuomba ni kumwomba Bwana amimine Roho Wake juu yake yao. Haijalishi ni kitu gani kingine unachohitaji kuomba hasa; utakuwa unaelekea juu dhidi ya mkondo mkali ikiwa wewe na wao hamsogei mbali na mtiririko wa Roho wa Mungu. Kila siku tunataka Roho wa Mungu aje juu yetu na atubebe pale tunapotaka kwenda. Tunamtaka afungue macho yetu kwa ile Kweli na kufungua masikio yetu ili kusikia Sauti Yake. Tunamtaka atujaze upya na Roho Wake ili maisha yetu tuishi kwa ajili Yake na tunaweza kuingia katika yote aliyo nayo kwa ajili yetu. Na hivyo ndivyo hasa tunataka kwa watoto wetu watu wazima pia. Kwa kweli, watoto wetu watu wazima wataomba kumiminiwa Roho Mtakatifu wenyewe. Lakini kwa kweli, vijana wengi hata hawafikirii kupokea na Roho Mtakatifu, au kuelewa maana yake au kwa nini wanapaswa kujazwa na Roho Mtakatifu. Itakuwa ajabu kama watoto wetu watu wazima kama wangeomba kwa ajili ya mambo yote yaliyopendekezwa katika kitabu hiki juu ya maisha yao wenyewe, lakini wawe wanafanya hilo au la, bado wanahitaji usaidizi wetu wa maombi.

Omba Ili Wakukaribishe Kumiminwa kwa Roho Mtakatifu; Ahadi tukufu ambayo Mungu alitangaza kwa watu Wake ilisikika kwa mara ya kwanza katika Agano La Kale kupitia nabii Yoeli (Yoeli 2:28) na kisha kunukuliwa baadaye katika Agano Jipya. Inasema: “Itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu, nitamimina Roho Wangu juu ya wote wenye mwili; wana wenu na binti zenu watatabiri, vijana wenu wataona maono, na wazee wenu wataota ndoto” (Matendo 2:17. Maneno haya yakazie haswa).

Tunaishi katika siku za mwisho Mungu anazungumza juu yake. Ikiwa huna uhakika kuhusu hilo, soma Biblia yako kisha uwashe TV na kuitazama kwa wiki moja. Wewe tazama dalili zake kila mahali-dalili za siku za mwisho. Ahadi kwa watoto wetu wazima katika maneno "wana wenu na binti zenu watatabiri" ni kwamba wakati Roho Mtakatifu Anamiminwa juu yao, wataweza kusikia kutoka kwa Mungu. Watakuwa na neno kutoka kwa Mungu mioyoni mwao, na litakuwa sababu ya kuwatia moyo katika maisha yao yote. Na Mungu atatukuzwa katika mchakato huo. Kwani ndiyo zawadi kubwa kupita zote hapa duniani, Roho Mtakatifu huja na mibaraka yote!

Wakati watoto wetu watu wazima wanaweza kusikia kutoka kwa Mungu, basi watajua mahali Yeye anawaongoza, na wataelewa jinsi anavyotaka wamtumikie. Huenda wasijue moja kwa moja, lakini watakuwa na mwelekeo. Mara nyingi sana vijana watu wazima hawawezi kujua mwelekeo wa maisha yao kwa sababu katika mioyo yao hawajasikia neno kutoka kwa Mungu kuhusu mwelekeo wanaopaswa kuchukua. Hii inaweza kuendelea kwa miaka hadi upate kuona kwamba watoto wazima ambao

wana malengo na wana hisia ya kusudi au wito.

Lakini Bwana, umesema kwamba siku za mwisho utamimina Roho Wako juu ya wote mwili. Ninakulilia kutoka kwenye kina cha moyo wangu na nakuomba umimine Roho Wako Mtakatifu juu ya watoto wangu wazima. Mimina Roho wako juu yangu na wanafamilia yangu wengine pia. Mimina Roho wako juu ya wakwe zao wote. Mimina Roho Wako juu ya lolote gumu ambalo kila mmoja wa watoto wangu wakubwa anakabiliana nalo. Uwe Bwana juu ya kila sehemu ya maisha yao na kila nyanja ya maisha yao. Ongea na moyo wa mtoto wangu mtu mzima na umsaidie kusikia kutoka Kwako. Muwezeshe yeye kuelewa uongozi wako na mwelekeo wa maisha yake. Fungua masikio yake kusikia Ukweli Wako ili apate kukataa uwongo wote. Msaidie kutembea kwa uwezo wa Roho Wako. Mwezeshe kuinuka juu ya shambulio hilo la uovu katika utamaduni wetu. Ambapo yeye amekwenda mbali na Wewe kwa njia yoyote. Baba nyosha mkono Wako na kumrudisha nyuma. Usimruhusu ………….. atembee na chochote ambacho sio cha kupendeza machoni Pako. Ubadili moyo wake na umrudishe mahali ambapo yeye anapaswa kuwa. Roho Mtakatifu akamwagike juu yake kabisa na kupunguza nguvu ya adui anayejaribu kumwaga uovu katika maisha yake.

Najua Unaweza kufanya mengi zaidi katika maisha ya mtoto wangu mtu mzima kuliko niwezavyo kufanya, na mimi nakualika kufanya hivyo. Lakini ikiwa kuna jambo lolote ninalopaswa kufanya—au nisifanye—niweke wazi ili nifanye lililo sawa. Roho Mtakatifu wa Kweli, funua

Ukweli unaohitaji kuonekana kwao na kwangu. Niongoze katika majibu yangu kwao daima. Ninaomba mtoto wangu mtu mzima asiwahi kumhuzunisha Roho Wako Mtakatifu (Waefeso 4:30) ila ampokee kama zawadi kutoka kwako (Luka 11:13). Mjaze kwa Roho Wako na kumwaga ndani yake amani yako, imani, tumaini, imani, Ukweli, na nguvu. Wacha sifa zitoke moyoni mwake na umfundishe kukuabudu katika Roho na Kweli.

Katika Jina la Yesu ninaomba. Amina

## NGUVU YA NENO

Ikiwa basi ninyi, mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, si zaidi sana Baba yenu wa mbinguni atawapa Roho Mtakatifu wale wamwombao!

**LUKA 11:13**

Mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu.

**MATENDO 1:8**

Mtu yeyote atakayenena neno juu ya Mwana wa Adamu, atasamehewa; lakini mtu ye yote atakayenena maneno mabaya juu ya Roho Mtakatifu, hatasamehewa katika ulimwengu huu wa sasa wala katika ulimwengu ujao.

**MATHAYO 12:32**

Unabii haukuja kamwe kwa mapenzi ya mwanadamu, bali watu watakatifu wa Mungu walinena wakiongozwa na Roho Mtakatifu.

**2 PETRO 1:21**

Tubuni, na kila mmoja wenu abatizwe kwa jina la Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi; nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.

**MATENDO 2:38**

## OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE KUSITAWISHA MOYO WA MUNGU, NENO LAKE, NA NJIA ZAKE MIOYONI MWAO

Watu ambao wana moyo kwa ajili ya Mungu wanataka kumjua Yeye vizuri. Watu wanaomtafuta Mungu wanataka kile anachotaka. Na Mungu anataka nini? Mungu anataka kwamba tunakuwa zaidi kama Yeye. Kwa sababu sisi sote tunapungukiwa na utukufu wa Mungu kwa jinsi tunavyofikiri, kutenda, na kuishi maisha yetu, sote tunahitaji kubadilika. Lakini Mungu pekee Ndiye anayeweza kufanya mabadiliko ya kudumu ndani yetu. Na kama tunavyomtafuta kwa ajili ya hayo mabadiliko. Haijalishi tumemjua Mungu kwa muda gani au tumetembea Naye muda gani, tunaweza siku zote kuomba tumjue zaidi na tutembee Naye karibu zaidi. Jinsi tunavyojiombea wenyewe, tunaweza pia kuwaombea watoto wetu watu wazima. Wakati sisi tunaomba uhusiano na Mungu uwepo kwa ajili yao, tunaweza kuomba kwamba mioyo yao itaelekezwa kwa Bwana na kufunguliwa kupokea kutoka Kwake. Tunaweza kuomba kwamba wawe na hamu ya kumjua Mungu zaidi na kuwa kama Yeye zaidi. Tunaweza kuomba kwamba mioyo yao ifungwe kwa uwongo wa adui na kufunguliwa kwa Kweli ya Mungu.

**Zifuatazo ni baadhi ya njia mahususi za kuomba Ili mtoto wako mtoto wako mtu mzima atembee na Mungu.**

## OMBA ILI WATAMANI KUMJUA MUNGU

Tamaa ndani ya moyo wa mtu yeyote ya kutaka kumjua Mungu ndiyo itakayomwokoa maisha. Hiyo ni kwa sababu mtu yeyote ambaye kwa kweli anataka kumjua Mungu ataenda hatimaye kuongozwa kwa miguu ya Yesu, Mwokozi. Kunaweza kuwa na wengine ulimwenguni ambao kudai wanaweza kukuokoa, lakini Yesu pekee Ndiye aliyekufa na kufufuka jambo ambalo linathibitisha kwamba Yeye Ndiye anayeweza kweli. Sote tunahitaji kuokolewa kwa sababu tumepotea bila Kristo. Mtume Petro alisema hivi kumhusu Yesu, "Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hakuna jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu ambalo kwayo imetupasa kuokolewa" (Matendo 4:12). Bila Yesu tutatangatanga tukijaribu kujitafutia nafasi katika hii dunia na bila kufanikiwa kamwe. Daima tutahisi kuna kitu kinachokosekana kwa sababu hatutakuwa na muunganisho thabiti kwa Mungu na nguvu Zake tunazohitaji ili kuishi ndani Yake. Na wakati wetu ujao wa milele hautakuwa mzuri. Sote tunahitaji kuokolewa kwa sababu hiyo ndiyo njia pekee tunaweza kuwa wapya. "Kama mtu yeyote yu ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya; mambo ya kale yamepita; tazama, yote yamekuwa mapya" (2 Wakorintho 5:17). Sote tunahitaji kuwa na mwanzo mpya. Baadhi yetu huhisi kwamba tunahitaji moja kila siku. Kuna njia moja tu ya uzoefu wa Kweli kuwa mpya,

na hiyo ni kwa njia ya Kristo kuishi ndani yetu na kutufanya upya. Hakuna mtoto mtu mzima ambaye ni mzuri kiasi kwamba hana haja ya kuokolewa. Na hakuna mtoto mtu mzima ambaye ni mbaya kiasi kwamba hawezi kuokolewa. Biblia inasema kwamba Mungu hakuwaacha Waisraeli hata "nchi yao ilipojaa dhambi juu yake Mtakatifu wa Israeli" (Yeremia 51:5). Ikiwa Mungu hakuwaacha watu Wake baada ya hapo, japokuwa kulikuwa na mambo yote ya kutisha waliyofanya, Yeye hatamuacha mtoto wako mtu mzima. Haijalishi amefanya nini pia. Na hasa, sio wakati mama au baba kama wewe mkiomba kwa bidii na Yesu wenyewe akibisha mlango wa mbinguni kila siku katika maombezi. Maombi yako yanaweza kumsaidia mtoto wako mtu mzima kuufungua moyo wake Kwake Mungu.

Mtoto wako mtu mzima anaweza kuwa amemjua Bwana tangu umri mdogo, na ikiwa ndivyo, endelea kuomba kwamba yeye kamwe asianguke kutoka Kwake. Na usifikirie kwamba haiwezi kukutokea, kwa sababu kila muumini ni shabaha ya Shetani, na yeye hataacha kujaribu kutuondoa njiani. Kuna ushawishi duniani leo, ulioundwa mahsusi kwa ajili hiyo. Mtoto wako mtu mzima anahitaji maombi yako ili kuwa imara katika vita. Ikiwa mtoto wako mtu mzima hamjui Bwana, omba kwamba aweze kukutana na Mungu aliye hai. Ingawa ni vigumu kufikiria, Mungu anajali hata zaidi juu ya wokovu wake kuliko wewe. "Bwana hakawii kutimiza ahadi Yake, kama wengine wanavyohesabu kukawia, lakini ni mvumilivu kwetu, wala hataki yeyote apotee bali wote wafikilie toba" (2 Petro 3:9).

Katika Biblia Mungu alimwonyesha nabii Yeremia vikapu viwili vya tini.

Moja ya vikapu vilikuwa na tini nzuri tayari kwa kuliwa; nyingine ilikuwa na tini mbaya zilizokuwa hazifai kuliwa. Mungu alisema kama vile tini mbaya hazingeweza kuliwa kwa sababu zilikuwa mbovu; watu wabaya hawakuwa na maana "Angewaweka kwenye shida" na maisha yao yangelaaniwa kwa shida moja baada ya nyingine (Yeremia 24:8-10). Watu wabaya anaowazungumzia hapa ni watu ambao mioyo yao ni migumu dhidi Yake Mungu na kila kitu anachosimamia. Kwa upande mwingine, Mungu alisema tini nzuri ni kama watu wema waliokuwa wamechukuliwa mateka wakati huo. Mungu alisema amewaruhusu wawe mateka lakini angewakazia macho na kuwarudisha na kuwajenga tena. Angewapanda ili waweze kuzaa matunda, na sio kuwang'oa, hivyo wasingeangamizwa (Yeremia 24:1-6). Hii ituaambia nini kuhusu asili ya Mungu kuhusu watoto wetu watu wazima ni kwamba mtu anapouzwa kwa moyo mgumu ili kumpinga Mungu kila njia, Mungu atamtia kwenye matatizo. Lakini na mtu ambaye ana moyo wa kumjua Mungu, atawaangalia na kuwajenga ili waweze kuzaa matunda. Na ijapokuwa wanaweza kutoka kwenye njia na Mungu akaruhusu baadhi ya mambo magumu kutokea kwao, itakuwa kwa manufaa yao wenyewe. Jambo linalofuata Mungu anasema kuhusu watu wema ambao wanawakilishwa na tini nzuri ni, “Ndipo nitawapa moyo wa kunijua Mimi, ya kuwa Mimi Ndimi BWANA; na watakuwa watu Wangu, Nami nitakuwa Mungu wao, kwa maana watanirudia kwa mioyo yao yote” (Yeremia 24:7).

Asante Mungu kwa ahadi hiyo nzuri kwetu na hasa kwa watoto wetu watu wazima! Ingawa wanaweza kuwa wamekwenda mbali na Mungu, Yeye atawapa moyo wa kumjua Yeye. Na ikiwa wameishia mbali kutoka hapo

walivyopaswa kuwa, Mungu atawavuta kwa wema na kuwafanya kurudi Kwake kwa moyo wote. Ahadi hii pekee, bila hata ya kuongeza zingine, inapaswa kumpa mzazi yeyote matumaini. Jambo kuhusu ahadi za Mungu, hata hivyo, ni kwamba lazima wafunikwe katika maombi yetu. Lazima tuseme, "Bwana, naomba ya kwamba utampa ……………(jina la mtoto mzima) moyo wa kukujua Wewe kama Bwana, na kwamba yeye ataendelea daima kurejea Kwako kwa moyo wake wote." Omba Ili Watamani Kuishi Njia ya Mungu. Moja ya sababu nyingi za kuomba kwamba Mungu amimine Roho Wake juu ya watoto wetu walio watu wazima ni kwamba, kuwa na Roho Mtakatifu katika maisha yetu ndiyo njia pekee tunayoweza kuishi njia ya Mungu kwa mafanikio. Sote tunahitaji msaada kwa hilo. Hakuna anayeweza kutii maagizo ya Mungu yaani sheria kikamilifu bila msaada wa Mungu. Hatuwezi kujifanya wazuri vya kutosha kuwa na uhusiano na Mungu. Tunapotoa mioyo yetu na maisha yetu kwa Mungu, Yeye hutusaidia kuwa watiifu na wema. Chaguo ni letu, lakini Yeye hufanya hilo liwezekana baada ya kumpa chaguzi zetu.

Yesu alisema ilimbidi aondoke ili atume Roho Mtakatifu kwetu. "Nawaambia Ni kwa faida yenu mimi niondoke; kwa maana nisipoondoka, basi Msaidizi hatakuja kwenu; lakini nikienda Zangu, nitampeleka kwenu. Naye atakapokuja, atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na juu ya hukumu" (Yohana 16:7-8. Maneno mepesi kukazia). Roho Mtakatifu ni msafi sana, hivyo hawezi kukaa katika watu ambao hawajatakaswa. Tumetakaswa kwa damu ya Yesu, Mwana-Kondoo wa dhabihu wa Mungu. Tunapompokea Yesu, tunatakaswa kwa damu

aliyomwaga kwa ajili yetu alipolipa adhabu ya dhambi zetu. Roho Mtakatifu Ndiye pekee anaweza kutusaidia kufanya jambo sahihi. Yeye Anatufundisha nini cha kufanya kwa kuzungumza na mioyo yetu na kuweka uhai katika Neno la Mungu tunapojifunza kwalo.

Pia anafanya kazi katika mioyo yetu na kutupatia tabia ya kufanya jambo sahihi. Yeye huunda ndani yetu kipimo kitakatifu ambacho hutuambia kwa silika, ni nini sahihi au kisicho sahihi. Biblia inasema kwamba tunapoishi kulingana na Roho, tunaweka mawazo yetu juu ya mambo ya Roho. Inasema kwamba tuko katika Roho ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yetu (Warumi 8:6-10). Lakini Mungu halazimishi kuingia mlango wa mioyo yetu. Yeye  Anasubiri kualikwa. Ingawa hatuwezi kuomba Roho Mtakatifu ndani yao watoto watu wazima, tunaweza kuomba kwa ajili ya mioyo yao kulainika na fursa ya kusikia sauti ya Bwana ikisema nao. Tunaweza kuomba kwa ajili ya kunyamazishwa kwa uongo wa adui karibu nao, ili waweze kusikia sauti ya Roho wa Kweli. Hakuna anayeweza kujua njia za Mungu ni zipi ikiwa hasomi Neno Lake Bwana. Ombea mtoto wako mtu mzima kuwa na moyo wa kupenda kusoma na kutafakari Neno la Mungu. Biblia inasema kwamba “sheria za Mungu ni kamilifu, humtia mjinga hekima”…“sawa, na hufurahisha moyo”, hutia macho nuru”…“ya kutamanika kuliko dhahabu”…na “Ni tamu kuliko asali na sega la asali” (Zaburi 19:7-10).

Kitabu cha Mithali kinasema, “Anayedharau Neno ataangamizwa, bali yeye anayeogopa amri atalipwa” (Mithali 13:13).

Kitu tusichotaka kamwe ni watoto wetu watu wazima kuangamizwa kwa kukosa ujuzi wa Neno la Mungu na njia Zake. Sisi sote lazima tuwe na ujuzi wa Kweli ambao ni Neno la Mungu, ili tusiishie kuamini uwongo. "Msisikilize maneno ya manabii ambao hutabiri uongo. Wanazungumza maono ya mioyo yao wenyewe, si kutoka katika kinywa cha BWANA… na kwa kila mtu aendaye sawasawa kwa maamuzi ya moyo wake wenyewe, husema, 'Ubaya hautawapata'" (Yeremia 23:16-17). Ni watu wangapi wameongozwa kwenye njia ya uharibifu kwa sababu waliamini uwongo na sio ukweli?

Omba kwamba watoto wako wakubwa wawe na maarifa makubwa ya Ukweli kwamba watauona uwongo wa adui ukiwa maili moja. Omba kwamba wasiwasikilize watu wanaozungumza maono ya mioyo yao wenyewe. Yeyote anayewafuata watu wanaomdharau Mwenyezi-Mungu naye atapotea na kuharibiwa. Ikiwa hukulea watoto wako katika njia za Mungu wamjue Bwana na njia Zake, mwombe Mungu akomboe hiyo hali sasa. Mshukuru kwa njia zote ulizowafundisha watoto wako zilizo sawa na nzuri. Kumbuka kwamba alisema, "Watoto wako wote watafundishwa na Bwana," kwa hiyo mwombe akufundishie watoto wako watu wazima njia Zake kila siku. Ikiwa ninyi mliwalea watoto wenu katika njia za Mwenyezi Mungu na wakapotea wakiwa watu wazima, waombee ili wasimpe kisogo tena. Mungu anasema juu ya watu wasiosikiliza maagizo Yake, "Wamenigeuzia mgongo, na si uso; ingawa niliwafundisha, nikiamka mapema na kuwafundisha, bado hawakusikiliza ili kupokea mafundisho" (Yeremia 32:33).

Omba ili watoto wako walio watu wazima wasikilize sauti ya Mungu na kamwe wasigeuze migongo Kwake. Ikiwa wewe ni mmoja wa wazazi waliobarikiwa ambao watoto wao wazima walilelewa katika njia za Mungu, na hawajawahi kupotea kutoka Kwake, omba kwamba hawataweza kamwe kupotea. Mungu alisema, "Watakuwa watu Wangu, Nami nitakuwa Mungu wao; basi nitawapa moyo mmoja na njia moja, ili waniche Mimi milele, kwa mema yao na ya watoto wao baada yao. Nami nitafanya nao agano la milele ili nisiache kuwatendea mema; lakini nitatia hofu Yangu ndani ya mioyo yao ili wasiniache" (Yeremia 32:38-40).

Ombea watoto wako watu wazima wawe na hofu ya Mungu kila wakati mioyoni mwao. Mshukuru kwamba kumcha Mungu moyoni mwako kutakuwa urithi tajiri kwako na wao pia.

## OMBA ILI WATAMANI KUWA NA MOYO WA TOBA

Kuwa na moyo wa toba ni moja ya funguo za mafanikio. Moyo wa toba unasema, "Nionyeshe dhambi zangu, Bwana, nami nitazitubu. Niongoze katika njia zako. Sitashikilia kwa uasi njia yangu ya kufanya mambo yaliyo kinyume na njia Zako." Kuwa na moyo wa toba haimaanishi kuwa lazima tumefanya jambo fulani baya, ingawa inaweza kumaanisha hivyo. Maana yake ni kwamba tuko tayari kuruhusu Mungu atuonyeshe ikiwa hatujafanya mambo kikamilifu. Ina maana tuko wazi kuona makosa yetu wenyewe badala ya kujiona kuwa waadilifu na kujiona kuwa sisi ni wazuri kiasi kwamba sisi kamwe hatuna haja ya kutubu chochote.

Ndoa nyingi nilizoziona zimevunjika na kuishia katika talaka, daima

kulikuwa na angalau mtu mmoja ambaye hakuwa na moyo wa toba. Kulikuwa na mtu mmoja ambaye hangesema, “Naona sehemu yangu katika matatizo haya na mimi nitafanya kile kinachohitajika kurekebisha mambo." Kwa kweli, watu wote wawili wanapaswa kusema hivyo na sio mmoja tu. Mara nyingi, mwanamke alikuwa akiomba aina fulani ya mabadiliko ndani yake mume, naye akakataa kusikiliza. Alikataa kuona kile alichohitaji kufanya kukidhi matakwa yake. Alikataa kuwa na moyo wa toba. Mwenye kutubu kwa unyenyekevu. Moyo wa toba ndio ufunguo. Na Mungu atampa mtu yeyote anayetafuta kuwa nao. Moyo uliotubu ni ule ambao hauna maasi ndani yake.

Uasi unasema, “Mimi nataka ninachotaka ninapotaka, na ninastahili kuwa nacho bila kujali jinsi nitakavyokipata au niliyemuumiza. Sina budi kuishi kwa sheria. Sina budi kuishi kwa sheria za wazazi, si lazima niishi kulingana na sheria za Mungu, na si lazima niishi kulingana na sheria za mwenzi. Nina sheria zangu mwenyewe na watu wengine wanaishi kulingana na zangu." Uasi ni kuishi kimakusudi nje ya njia za Bwana.

Yeremia alizungumza na Mungu kuhusu Israeli kutotii njia za Bwana na akipokea hukumu, alisema, “Ee BWANA, macho Yako hayaangalii uaminifu? Umewapiga, lakini hawakuhuzunika; Umewakomesha lakini, wamekataa kupokea kurudiwa. Wamezifanya nyuso zao kuwa ngumu kuliko mwamba; wamekataa kurudi” (Yeremia 5:3). Kuwa na uso ambao ni "mgumu kuliko mwamba" inamaanisha mtu anakataa kupokea maonyo ya Bwana. Hakuna huzuni mioyoni mwao kwa mambo wanayofanya vibaya.

Kwa kweli, mara nyingi hakuna utambuzi mioyoni mwao kwamba wamefanya jambo lolote baya. Huu ni moyo wa kuasi.

Mtu mwenye moyo wa toba huhuzunika kwa lolote alilofanya kinyume na njia za Mungu. Yeremia aliendelea kuzungumzia matokeo ya watu wanaoishi ndani ya uasi dhidi ya njia za Mungu, ingawa wanajua Ukweli. Kama matokeo ya uasi na kutokutubu, watu hawa walipoteza ulinzi wa Mungu Katika maisha yao.

Bila kutubu, dhambi zetu zinatutawala. "Kuasi ni kama dhambi ya uchawi, na ukaidi ni kama uovu na kuabudu sanamu" (1 Samweli 15:23). Toba pekee ndiyo itavunja nguvu ya dhambi kwenye maisha ya mtu yeyote. Bila hivyo, kifo ndicho kitakuja na kutuangamiza pamoja na dhambi ambayo hatujatubu inayoendelea kukua yenyewe kwenye maisha yetu. Bila toba tunalipa gharama kila mara kwa kutoishi katika njia ya Mungu.

Mungu hatasikiliza maombi yetu tunapoishi katika uasi. Mungu hasikii maombi yetu tunapokuwa na dhambi, bila kutubu maishani mwetu. "Maovu yenu wamewatenga ninyi na Mungu wenu; na dhambi zenu zimeuficha uso wake, hata hataki kusikia" (Isaya 59:2).

**Maneno mepesi kukazia**

"Kama natafakari maovu moyoni mwangu, Bwana asingesikia" (Zaburi 66:18). imeongezwa). Mtunga-zaburi aliyeandika hivyo pia alisema kwamba alipomlilia Mungu, Yeye alimkomboa (mstari wa 19), lakini haingetokea kama angaliweka dhambi ndani ya moyo wake. Tunapotaka

majibu ya maombi yetu, lazima tuwe na mioyo safi hapo kwanza, mbele za Mungu, na hilo huhitaji moyo wa toba. Moyo uliotubu ni moyo mnyenyekevu. Kiburi kinatuangamiza. Unyenyekevu hutuletea heshima. “Kiburi cha mtu kitamshusha, lakini mwenye roho ya unyenyekevu atabaki na heshima” (Mithali 29:23). Kiburi ni anguko letu kwa sababu ndicho kitu kitakachotufanya siku zote tuishi bila kutubu. Lakini mtu mwenye moyo mnyenyekevu anaweza kutambua udhaifu au dhambi yake mwenyewe. Kinyume cha unyenyekevu ni kiburi. Jeuri inatuzuia kuona Ukweli kuhusu sisi wenyewe.

Watoto wetu walipokuwa wachanga, mojawapo ya njia ambazo mimi na Mume wangu tulihakikisha kwamba nidhamu yenye ufanisi ilitungwa/iliwekwa walipofanya jambo baya ilikuwa ni kuona ikiwa Amani au Neema walikuwa na moyo wa toba au la. Kwa maneno mengine, walikuwa na huzuni sana kwa walichokifanya au waliomba samahani tu kwasababu walikamatwa? Ikiwa ilionekana kama adhabu hata haikufisha kiburi na kuleta toba, basi tungekuwa hatujaifanya ipasavyo. Sisi tuliamini kuwa haikuwa haki kutomruhusu mtoto kujifunza kuwa kuna matokeo ya kufanya mabaya. Watoto wasipojifunza hilo, watakua na kuona ni rahisi kufanya mabaya kwa sababu wanaamini hakuna kitakachotokea kwao. Wakati hawana nidhamu, hawajifunzi kujinidhamisha. hawajifunzi kujidhibiti. Ni mara ngapi tumeona muuaji mbaya mahakamani aliyetangazwa kuwa na hatia na bado hana majuto yoyote? Tunaona kiburi ndani yake badala ya unyenyekevu. Hakika mtu huyo hakuwahi kuwa makini na matokeo ya kutisha kwa ajili ya matendo yake wakati yeye

alikuwa akikua ili kuunda ndani yake moyo wa toba. Nafikiri kutafuta ule moyo wa toba katika kila mtoto wetu kuliwafanya wawe na usikivu wa kukabiliwa na kusahihishwa akiwa mtu mzima wakati wanapokengeuka kutoka kwenye njia njema. Haikuwazuia kufanya chochote kibaya, lakini Mungu aliwafanya wawe wepesi kutubu. Sote tumeona matokeo mabaya wakati kijana mdogo alikataa kupokea marekebisho kutoka kwa mzazi au mtu mwenye mamlaka na kuendelea kufanya kwa uasi alichotaka kufanya. Ni mara ngapi tumeona vijana wakiripotiwa kwenye televisheni kufanya jambo fulani la kuogofya, nasi tunashangaa, Je! wanaweza kuwa wajinga hivyo? Hawajui wanatupa pipani maisha yao? Kwa nini wanafikiri wanaweza kuondokana na hatia ya matendo yao? Nini kiliwafanya wawe na jeuri na kuamini kwamba hakutakuwa na matokeo?

Stefano, mmoja wa wanaume mashemasi waliochaguliwa kuwasaidia wanafunzi baada ya Yesu kuwa aliyesulubiwa, alikuwa amejaa imani na nguvu za Roho Mtakatifu (Matendo 6:5). Aliita watu waliokuwa wakimhoji kuwa “wenye shingo ngumu na wasiotahiriwa moyo na masikio.” Alisema, “Sikuzote mnampinga Roho Mtakatifu” (Matendo 7:51). "Shingo ngumu" maana yake ni ukaidi. “Moyo usiotahiriwa” unamaanisha kutotubu. Kwa kitendo cha kuwa mkaidi na asiyetubu, mtu anampinga Roho Mtakatifu.

Mungu atambariki kila wakati mtu mwenye moyo ulio haraka kusikia na anayetubu anapofanya makosa. Omba kwamba watoto wako watu wazima wapate mioyo kwa ajili ya Mungu inayokubali maonyo na kutubu Kwake. Hiyo ina maana wao daima wako wazi kwa kusahihishwa na Roho

Mtakatifu. Tunapaswa pia kuomba kwa ajili ya mioyo iliyotubu kwa ajili yetu wenyewe. Ndicho ambacho Mungu anataka kwa ajili yetu, na itatusaidia vizuri siku zote za maisha yetu.

## OMBA ILI WATAMANI KUJUA KILE MUNGU AMEFANYA

Mungu anatupa njia ya kuwaachia watoto wetu urithi ambao ni wa kiroho. Na urithi huu wa kiroho ni muhimu zaidi kuliko urithi wa fedha. Urithi huu wa kiroho watoto wako watu wazima wanaweza kuanza kuupokea mara moja. Hivyo kama huwezi kuwaacha watoto wako watu wazima katika njia ya urithi ambao unaweza kuwekwa benki, usijali kwa sababu unaweza kuwaachia urithi wa kiroho ambao utadumu maisha yao yote duniani. Urithi wa kiroho ni urithi wa tabia njema, uadilifu, upendo, jina zuri, uhuru kutoka kwa utumwa, na baraka kutoka kwa Mungu. Kwa maneno mengine, watoto wako wakubwa watakuwa na uwezekano mkubwa wa kurithi ndani yao yale ambayo wameona na kuiga kwako.

Mojawapo ya njia unazoweza kushiriki urithi wa kiroho ni kuwaambia watoto wako nini Mungu amefanya katika maisha yako. Asafu, mtunga-Zaburi akiandika katika Agano la Kale, alisema juu ya mambo ambayo Mungu alikuwa amefanya, “Nitafungua kinywa changu kwa mfano; Nitasema maneno ya kale, tuliyoyasikia na kuyajua, ambayo baba zetu walituambia. Hatutawaficha watoto wetu, tutakiambia kizazi kijacho sifa za BWANA, na nguvu Zake, na kazi Zake za ajabu alizozifanya” (Zaburi 78:2-4). Aliendelea kusema kwamba Mungu aliwaamuru kufanya mambo haya yajulikane kwa watoto wao ili vizazi vijavyo vijue na visisahau mambo yale

Bwana aliyofanya. Na hiyo ingesaidia watoto wao watu wazima kuweka tumaini lao kwa Mungu, na ingewazuia kuwa watu wakaidi na waasi ambao hawatakuwa na mioyo sahihi au roho za uaminifu kwa Mungu na unyenyekevu (Zaburi 78:5-8).

Kuna maneno yale yale tena: "wakaidi na waasi." Nini Mtunga-zaburi anasema ni kwamba Mungu anataka wazazi kushiriki na watoto wao kile Yeye amewamefanyia katika maisha yao ili watoto wao wasiwe waasi. Sisi, pia, tunahitaji kuwajulisha watoto wetu kile ambacho Mungu amefanya katika maisha yetu, ili wasiishi katika uasi, na hivyo wanaweza kuwafundisha watoto wao wenyewe mambo haya. Sisi tunataka watoto wetu watu wazima wasisahau kamwe wema wa Mungu kwetu, ili wao waweke tumaini lao kwa Bwana na kuchagua kuishi njia Yake.

Inasema baadaye katika Zaburi hiyo kwamba watu ambao hawakukumbuka ni mambo gani Mungu alikuwa amefanya “humjaribu Mungu, na kumwekea kikomo Mtakatifu wa Israeli. Anasema: zikumbukeni nguvu Zake, siku ile alipowakomboa na adui zenu.” (Zaburi 78:41-42, Hatimaye waliishia kumwasi Mungu na kugeukia miungu ya uwongo (Zaburi 78:56-58). Ndio maana tunapaswa kushiriki na watoto wetu nyakati zote kuhusu namna Mungu ametukomboa kutoka katika mikono ya adui. Sisi tunapaswa kukumbuka nguvu Zake alizotuonyesha zamani ili tuweze kukumbuka nguvu Zake kwa sasa tunapozihitaji sana. Na hiyo itatupa amani kuhusu siku zijazo.

Ni muhimu kuwaambia watoto wako wadogo na wale ambao

wameshakuwa watu wazima kwamba Mungu anamaanisha nini kwako, jinsi ambavyo amejibu maombi yako, na mambo makuu yote Aliyokufanyia huko nyuma, pamoja na yale unayotarajia Atafanya kwa ajili yako katika siku zijazo. Waambie jinsi ulivyokutana na Bwana, jinsi alivyokubadilisha na akakuruzuku, na jinsi anavyokuongozeni hata hivi leo. Hii itaimarisha imani yao, na yako pia, kwa sababu wataikumbuka, hata miaka mingi baadaye.

Usifanye hivyo kana kwamba unatoa mahubiri. Tafuta tu wakati mzuri wa kusimulia kisa kuhusu mambo ambayo Mungu amekutendea au kukufundisha. Unaposhiriki hii sehemu muhimu ya maisha yako pamoja nao, wataona ni kiasi gani ina maana kwako na na italeta matokea chanya katika maisha yao.

Ikiwa umeanza kuishi kwa njia ya Mungu hivi majuzi tu au umeweza kumjua Bwana baada ya watoto wako kukua, usijisikie kuwa umechelewa kuwaachia watoto wako wakubwa, urithi wa kiroho. Mungu atakutendea mambo makuu sasa-hata leo. Mwambie akufundishe jambo kubwa kutoka katika Neno Lake. Mwombe Roho Mtakatifu afanye jambo la ajabu katika maisha yako sasa hivi. Na anapofanya hivyo, liandike na ukumbuke kuwaambia watoto wako watu wazima wakati ufaao. Unaweza kuwa na utajiri wa vitu vya kushiriki juu ya kile ambacho Mungu amefanya ndani ya muda mfupi sana.

Hungekuwa unasoma kitabu hiki ikiwa hutaki mema kwa watoto wako wakubwa na amani ya akili yako mwenyewe. Ikiwa unataka kuwasaidia

kwa njia yoyote unaweza, lakini hutaki kuchukua nafasi ya Mungu kama chanzo kikuu kwa uhitaji n amahitaji yao yote. Unataka kuwa na uwezo wa kuwashawishi na kuwaathiri kwa njia ya Kiungu/kimbingu zaidi, lakini pia unataka wawe na uhusiano wenye nguvu na Mungu ili watamani kuishi njia Yake. Unataka wampende Mungu jinsi unavyofanya na zaidi. Njia bora ya kuwasaidia wajifunze kumpenda Mungu ni kuwaonyesha jinsi Mungu alivyo na anavyowapenda. Na unafanya hivyo kwa kuwaonyesha jinsi unavyowapenda. Sema juu ya mambo mazuri unayoyaona kwao na mustakabali mkuu unaoutarajia kwao. Waambie Neno la Mungu linasema nini kuhusu wao. Wakati watoto wako wakubwa watakapoona upendo ndani yako kwa ajili yao, wao watafungua mlango na kukuruhusu wewe katika maisha yao, na watashiriki mahangaiko na mahitaji yao ya ndani kabisa. Wanaposikia habari za Upendo wa Mungu kwao, watamfungulia Yeye njia mpya na ya kina pia.

## NGUVU YA MAOMBI

Bwana, ninaomba kwa ajili ya ………….. (jina la mtoto mzima) na kusihi kwamba ungempa moyo wa kukujua Wewe. Ninaomba kwamba kama tu ilivyosemwa juu ya wema Wako na mtumishi mwaminifu Danieli kwamba "Roho bora ilikuwa ndani yake" (Danieli 6:3), na iwe hivyo pia alisema juu ya nwana wangu/binti yangu kwamba roho bora iwe ndani yake. Mvute karibu Kwako na umwezeshe kuwa zaidi kama Wewe.

Umesema katika Neno Lako kwamba Wewe Ndiwe mlango ambao mtu yeyote anaweza kuingia na kuokolewa (Yohana 10:9). Mzuie ….. asipitie

mlango mwingine wowote isipokuwa njia ya umilele uliyo nayo kwa ajili yake. Ikiwa binti yangu au mwanangu amekwenda mbali na Wewe kwa njia yoyote, mfanye arejee Kwako kwa moyo wake wote (Yeremia 24:7). Mwezeshe kuwa kiumbe kipya ndani ya Kristo kama ulivyosema katika Neno Lako (2 Wakorintho 5:17). Mpe moyo wa toba—aina ya moyo ambao ni mnyenyekevu na akageuke kuelekea Kwako. Popote panapokuwa na uasi wowote ndani yake, nakuomba Wewe ungeumba ndani yake moyo safi na kufanya upya roho iliyo tulia ndani yake. Ondoa kiburi chochote kinachomruhusu kufikiria kuwa anaweza kuishi bila Wewe. Mpe hamu ya kutaka unachotaka.

Ninaomba kwamba yeye atapenda Neno Lako na atailisha nafsi yake Neno Lako kila siku. Sema na moyo wake na mpatie uhai katika kila Neno Lako Takatifu. Mfundishe njia Zako na sheria Zako na umwezeshe Yeye kufanya jambo sahihi. Ninaomba Bwana unyamazishe sauti ya adui kwake ili yeye aweze kumsikia Roho Wako Mtakatifu akisema na moyo wake. Mpe hamu ya kuishi kwa njia Yako. Umesema katika Neno Lako kwamba mtu anapogeuka sikio lake lisisikie sheria kwamba hata maombi yake ni chukizo (Mithali 28:9). Ninaomba kwamba yeye hataziba sikio kwa sheria Zako. Mungu Baba, msaidie mwanangu/binti yangu kuwa na shauku kwa uwepo wako na Neno Lako. Msaidie kuhisi uwepo wa Roho wako Mtakatifu anayemwongoza. Ninaomba kwamba yeye atakuinua, akupende vya kutosha kukuweka Wewe kwanza, na kukutumikia Wewe. Mwaga Roho Mtakatifu ndani yake na kumpa nguvu ya kujitoa Kwako. Ninaomba kwamba yeye apate nguvu kutoka kwa uhusiano wake Nawe. Sawazisha

mapenzi yake na mapenzi Yako. Mshikilie kwenye njia Yako na siku zote mweke mahali Unakotaka Wewe awe, akifanya vile Unavyomtaka afanye. Nisaidie kushiriki na mtoto wangu mtu mzima mambo yote mazuri uliyofanya kwa ajili yangu na maisha yangu. Nifanye kuwa kama Wewe zaidi ili niweze kumwachia urithi mwingi wa kiroho. Niwezeshe kuhamasisha ndani yake upendo mkubwa Zaidi kwa ajili Yako kwa sababu yeye anaona upendo Wako ndani yangu. Katika Jina la Yesu ninaomba, Amen.

**NGUVU YA NENO**

Ninyi mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote; nanyi mtatendewa. Kwa hili hutukuzwa Baba Yangu, kwa vile ninyi mnazaa matunda sana; nanyi mtakuwa wanafunzi Wangu.

**YOHANA 15:7-8**

Katika njia ya haki kuna uhai, na katika mapito yake hakuna kifo.

**MITHALI 12:28**

Kwa maana macho ya BWANA hukimbia-kimbia duniani mwote, ili kuonyesha Mwenye nguvu ambao moyo wao ni mwaminifu Kwake.

**2 NYAKATI 16:9**

Tunajua kwamba Mungu hawasikii wenye dhambi; lakini ikiwa mtu yeyote ni mcha Mungu na anafanya mapenzi Yake, humsikia.

**YOHANA 9:31**

Mkaribieni Mungu Naye atawakaribia ninyi. Osha mikono yako, wewe wenye dhambi; na kuisafisha mioyo yenu, enyi wenye nia mbili.

**YAKOBO 4:8**

## OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUE KATIKA HEKIMA, UTAMBUZI, NA UFUNUO

Ili kuwa na amani kama wazazi, tunapaswa kusali ili mambo fulani yawe halisi katika maisha ya watoto wetu watu wazima. Na kisha tunapaswa kumwamini Mungu kujibu hayo maombi. Hatuwezi kuwa na wasiwasi juu ya kila kitu kinachotokea katika maisha yao, kwa sababu hiyo haitatutia wazimu tu, bali itamtia wazimu kila mtu anayetuzunguka pia. Na hiyo sio njia nzuri zaidi ya kuwaombea hata hivyo. Siyo kazi yetu kutambua kila kinagaubaga au jambo dogo katika maisha yao; hiyo ni kazi ya Mungu. Inabidi tuwaombee kwa mtazamo mpana, omba kwa ajili ya maswala muhimu zaidi, omba ili kubadilisha mipango ya adui, sali kuhusu mambo anuwai ikiwa unayajua, na usali ili mapenzi ya Mungu yatimizwe katika kila jambo la maisha ya watoto wetu. Mojawapo ya mambo muhimu tunayohitaji kuombea watoto wetu watu wazima waweze kufanya kazi kwa hekima ya Kiungu, utambuzi, na ufunuo wa kimbingu. Karama hizi tatu kutoka kwa Mungu pekee zinaweza kuwafikisha mbali kimaisha na kuwawezesha kuepuka hali zinazoweza kuwa mbaya.

Ni wangapi kati yetu—na wangapi kati yao— tungeepushwa na baadhi ya shida ambazo tumekuwa nazo, kama tungekuwa na karama zinazofanya kazi kikamilifu katika maisha yetu?

Hakuna hata mmoja wetu anayeweza kuishi maisha kwa mafanikio bila hekima, utambuzi, na ufunuo kutoka kwa Mungu—hasa watoto wetu wakubwa. Kwa ufahamu wa Neno la Mungu—pamoja na shauri lililotolewa na Roho wa hekima—wanaweza kuzunguka kwenye mitego iliyotegwa kama ili waanguke. Kwa kuwa tuna utambuzi na ufunuo kutoka kwa Mungu wanaweza kutembea kwa mafanikio na kupita salama katika kuchanganyikiwa na udanganyifu ulio karibu nao.

Kuwa na hekima ya Kiungu, utambuzi, na ufunuo kunaweza kudumisha ujana wa watoto wetu kutoka mahali pasipofaa kwa wakati unaofaa. Huweza kuwazuia kutokana na kufanya maamuzi mabaya. Huweza kuwazuia wasiwaamini watu wabaya au kushindwa kumwamini mtu asiye sahihi kwa wakati sahihi. Inaweza kuwasaidia kuchagua kitu kizuri juu ya kitu ambacho sio kizuri sana, haswa wakati ambapo sio rahisi kutofautisha Ukweli kutoka kwenye uongo. Inaweza kuwawezesha kuona mambo wanayotarajia ambayo bila neno wasingeweza. Inaweza kuwapa hisia ya hatari au ya kutatanisha wakati kwa faida yao. Inaweza kuwazuia kutoka kwa shida na mbali na madhara.

Kila mmoja wetu anahitaji karama hizi zote tatu kutoka kwa Mungu, zifanye kazi ndani yetu na kuziishi kila siku. Ni lazima tumwombe Mungu atufanye wenye hekima na utambuzi, na ni lazima tumuombe atupe ufunuo

kuhusu kile tunachopaswa kufanya, wapi tunapaswa kwenda, na jinsi tunavyopaswa kufikiri. Sio tu kwamba tunaweza kuomba kwa ajili ya mambo haya kwa ajili yetu wenyewe, lakini tunaweza kuwaombea watoto wetu watu wazima wayapate pia. Ombea Mtoto Wako mtu mzima Apate Hekima kutoka kwa Mungu. Mengi yanasemwa kuhusu hekima katika Biblia kiasi kwamba ni dhahiri hatutakuwa Salama kuishi bila hiyo.

Lakini hekima ya kweli hutoka kwa Mungu pekee. Tuna habari zaidi kuliko wengi wetu tunazohitaji na zaidi ya ilivyo salama katika ulimwengu wetu. Tunachohitaji ni hekima zaidi ya kushughulikia habari tulizonazo. Hekima inayomiminwa na Roho wa hekima hupita mbali Zaidi ya elimu na maarifa. Ni hisia ya kina ya Ukweli.

Hatutaki watoto wetu watu wazima wawe aina ya watu ambao "wanajifunza siku zote na kamwe hawawezi kuja kwenye ujuzi wa Kweli" (2 Timotheo 3:7). Tunataka wawe nayo hekima ya Kiuingu, ambayo ni ujuzi unaofanya kazi kwa Ukweli. Wakati wana hekima ya Mwenyezi Mungu, wanaweza kufanya maamuzi haraka inapobidi na yale maamuzi yatakuwa sahihi. Wataweza kuchukua taarifa walizonazo na wazitumie kwa wema ili zizae matunda.

Watoto wetu wazima wako busy na maisha yao, wakijaribu kujua ni nini kinachofaa na nini hakifai, ni nani anayefaa kwa maisha yao na ni nani asiyefaa. Wanajaribu kutambua wanachohitaji kufanya ili kufanikiwa na ni kwa bidii kiasi gani wanapaswa kufanya kazi au kusoma ili kufanikisha hilo. Wanafikiria juu ya kuanzisha mahusiano mazuri, kutafuta mwenzi sahihi

wa ndoa, au kufanya ndoa yao iwe bora. Wanajaribu kuanzisha nyumba imara na kulea familia yenye mafanikio. Wao wanajitahidi kupata nafasi zao duniani, kwa hiyo wako bize kupima mipaka yao na karama zao. Wangeweza kujua haya yote vizuri zaidi ikiwa wangekuwa na hekima kutoka kwa Mungu. Kuwa na hekima ya Bwana kutafanya maisha yao yaendelee kuwa rahisi zaidi na laini zaidi.

Biblia inasema kwamba tunachopaswa kufanya ni kumwomba Mungu hekima, Naye atatupa. "Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote kwa ukarimu wala hakemei, naye atapewa" (Yakobo 1:5). Tunaweza kuomba kumwagwa kwa Roho wa hekima kwa niaba ya watoto wetu wazima. Ni lazima tumwombe Mungu awape hekima kuhusu jinsi ya kufikiri, kutenda, na kuishi. Tunapokuwa na hekima, tunaweza kuona matokeo ya matendo yetu kabla ya kutenda, jambo ambalo hutuwezesha kufanya uamuzi sahihi kuhusu hatua gani ya kuchukua. Hekima hutupatia ufahamu wa kina kuhusu masuala ya maisha yetu, na matokeo yake inatusaidia kuwa na uwezo wa kufikiri. Inatupa ufahamu, akili nzuri, na maamuzi sahihi. Tunaweza kuhisi Roho wa hekima akifanya kazi katika maisha yetu. Je, umewahi kufanya uamuzi kuhusu jambo ambalo umeona ni sahihi kufanya na baadaye ukagundua kwamba lilikuwa jambo sahihi kufanya kwa wakati huo? Huyo Ndiye Roho wa hekima atendaye kazi ndani yako, akikuwezesha wewe kufanya maamuzi mazuri zaidi ya uwezo wako wa asili kufanya hivyo.

## NJIA SABA ZA KUFAA ZA KUOMBEA HEKIMA

a) Omba kwamba mtoto wako mtu mzima awe na hekima ya kumcha Mungu. “Kumcha BWANA ni mwanzo wa hekima” (Mithali 9:10). Hekima yote huanza kwa kumcha Mungu na njia za Mungu. Kuwa na heshima/hekima ya namna hiyo humfanyia nafasi Roho wa hekima apate makao ndani yako na ndani ya moyo wa mtoto wako mtu mzima.

b) Omba ili mtoto wako mtu mzima apate hekima ya kuzungumza maneno sahihi. “Unamuona mtu mwenye pupa katika maneno yake? Kuna matumaini zaidi kwa mpumbavu kuliko yeye” (Mithali 29:20). Kuzungumza maneno yasiyo sahihi kwenye wakati mbaya kumewaingiza watu wengi kwenye matatizo makubwa. Kujua jinsi gani kuongea maneno yaliyo sahihi na kwa wakati muafaka kunaweza kufungua milango ya baraka na neema kwao.

c) Omba ili mtoto wako mtu mzima apate hekima ya kutolikufuru Jina la Mungu. “Ee Bwana Kumbuka hili, adui ameshutumu, na watu wapumbavu wamelitukana Jina Lako” (Zaburi 74:18). Maneno ambayo si ya kumtukuza Mungu ni uharibifu mkubwa kwa mtu anayeyatumia. Hii inaonekana katika amri ya tatu ya zile Amri Kumi inayosema mtu yeyote akilitaja Jina la BWANA bure hatahesabiwa na Mungu kuwa hana hatia (Kutoka 20:7). Kama kuna kukufuru, maneno hayo kuna matokeo ambayo ni njia ya hatari pia.

d) Omba ili mtoto wako mtu mzima awe mnyenyekevu na asiwe na kiburi. "Wakati wa kiburi kinakuja, ndipo inakuja aibu; bali kwa wanyenyekevu iko heshima” (Mithali 11:2). Kuwa na unyenyekevu daima ni busara, lakini

hii ina maana kwamba si tu ni busara tuwe wanyenyekevu, lakini tunapokuwa wanyenyekevu tunakuwa katika hekima na hatutaanguka.

e) Omba ili mtoto wako aliye mtu mzima apate hekima ya kutovutwa kuelekea hekima ya dunia. “Je, Mungu hakuifanya hekima ya dunia hii kuwa upumbavu?” (1 Wakorintho 1:2). “Kwa maana hekima ya ulimwengu huu ni upumbavu” (1 Wakorintho 3:19). Kile ambacho ulimwengu huona kuwa cha hekima ni upumbavu machoni pa Mungu, na kila kitu ulimwengu unaona kuwa ni upumbavu ni busara machoni pa Mungu ni hekima. Kwa mfano, ulimwengu unaona kuwa na imani katika Yesu ni upumbavu, lakini Mungu anaona ni jambo la hekima zaidi tuwezalo kufanya.

f) Omba ili mtoto wako mtu mzima apate hekima ya kupenda Neno la Mungu. “Mwanangu, ukiyapokea Maneno Yangu, na kuyaweka akiba maagizo yangu ndani yako; na kutega sikio lako kusikia hekima...ndipo utafahamu kumcha BWANA, na kupata kumjua Mungu” (Mithali 2:1-2,5). Kuwa wazi kwa Neno la Mungu na kuthamini sheria na njia za Mungu kunamaanisha umeelekea kwa Roho wa hekima, ambaye hukuwezesha kugundua na kuelewa mambo ambayo huwezi kuanza kuelewa bila uwezeshaji wa Mungu.

g) Omba ili mtoto wako mtu mzima apate hekima ya kutafuta ushauri kila mara kwa watu wacha Mungu na wenye hekima. “Tega sikio lako, uyasikie maneno ya wenye hekima, na kuuelekeza moyo wako katika maarifa yangu” (Mithali 22:17). “Amebarikiwa mtu asiyekwenda katika shauri la wasio haki, wala hakusimama katika njia ya wakosaji, wala hakuketi

barazani pa wenye mizaha" (Zaburi 1:1). Ni muhimu kwamba watu wanaoathiri na kushugulika watoto wako wakubwa ni watu wacha Mungu wanaoeneza hekima katika mwelekeo wao.

Omba kwamba watu pekee walio karibu na mtoto wako mtu mzima wawe ni watu ambao ndani yao hukaa Roho wa hekima. Kifungu kimoja kirefu katika sura ya kwanza ya Mithali kinaeleza hekima kama mwanamke ambaye anatuita. "Hekima huita kwa sauti nje; anapaza sauti yake ndani ya viwanja vilivyo wazi" (Mithali 1:20.). Chini hapo ni mambo muhimu kutoka kifungu hicho: Enyi wajinga, mtapenda ujinga hata lini ?

Geukieni maonyo yangu hakika nitamimina roho Yangu juu yenu; Nitawajulisha Maneno Yangu (mistari 22-23). Kwa sababu ulidharau mashauri Yangu yote, wala hukutaka kukemea kwangu, Mimi Nami nitacheka msiba wenu (mstari 25-26). msisitizo umeongezwa, Wataniita, lakini sitaitika; watanitafuta kwa bidii, lakini hawatanipata. Kwa sababu walichukia maarifa na hawakuchagua kumcha BWANA. (mistari 28-30. Maneno mepesi kukazia hapo ni Kwa hiyo watakula matunda ya njia zao wenyewe... kurudi nyuma kwao wajinga kutawaua, na kufanikiwa kwa wapumbavu kutawaangamiza (mistari 31-32. Maneno mepesi kukazia). Bali yeye anisikilizaye atakaa salama, naye atakuwa salama; bila kuogopa uovu (mstari 33.). Kwa maneno mengine, Roho wa hekima anataka kumwaga hekima juu yetu, lakini ikiwa hatutafuti kuwa nayo na kukataa ushauri wa busara, tutateseka na hatutapata matokeo bora. Walakini, ikiwa tunatafuta hekima, tutaishi maisha salama na salama. Kama vile mstari wa 23 hapo juu

unavyofafanua hekima kama roho iliyomiminwa juu yetu, Biblia pia inasema kwamba hekima ya Bwana huja kupitia Roho Mtakatifu wa Mungu. "Mtu hupewa neno la hekima kwa njia ya Roho, na mwingine neno la maarifa kwa Roho yeye yule, na mwingine imani katika Roho Yeye Yule na mwingine karama za kuponya katika Roho Yeye Yule, na mwingine matendo ya miujiza" (1 Wakorintho 12:8-10).

Katika kuzungumza juu ya kuja kwa Bwana Yesu miaka mingi kabla haijatokea, nabii Isaya alisema, "Roho wa BWANA atakaa juu Yake, Roho wa hekima na ufahamu, Roho wa shauri na uweza, Roho wa maarifa na kumcha BWANA" (Isaya 11:2. Maneno mepesi kukazia). Biblia inasema kwamba Yoshua "alijaa roho ya hekima, kwa maana Musa alikuwa Nayo akaweka mikono yake juu yake" (Kumbukumbu la Torati 34:9).

Tunaweza kuweka mikono juu ya watoto wetu watu wazima na kuwaombea wajazwe na Roho wa hekima vilevile. Kiini cha Maandiko hapo juu ni kwamba Mungu Yuko tayari kumwaga Roho ya hekima kwa yeyote anayetaka kuwa nayo. Wale ambao hawana uzoefu huu, wako katika maafa na uharibifu. Wale wanaoitaka wataipata, na matokeo yake watapata kukaa kwa usalama na bila hofu. Roho ya hekima ikimiminwa juu ya watoto wako watu wazima atafanya maisha yao kufanya kazi vizuri zaidi. Elimu tu ya maarifa ya kidunia haitoshi. Hekima itokayo kwa Mungu itawasaidia kuchukua taarifa wanazopata na kuzitumia kuzaa matunda katika maisha yao. Roho ya hekima Itawalinda. Omba kwa ajili ya kumiminiwa kwa Roho wa hekima kwa watoto wako watu wazima ili wajue

jinsi ya kufikiri, kutenda, na kuishi.

Ombea watoto wako wakubwa wawe wacha Mungu na wapate Utambuzi. Watoto wako watu wazima wanapokuwa na utambuzi, wataweza kuelewa kile ambacho kwa kawaida hakijafahamika kwao. Watakuwa na ufahamu katika hali kuwawezesha kuona kile ambacho watu wengi hawawezi kuona. Kwa mfano, wataweza kutambua tabia ya kweli ya mtu, ambayo inaweza kuwaokoa na huzuni kubwa na shida. Ni watu wangapi wangeepushwa na mambo mabaya kama wangekuwa na utambuzi tu? Ni wasichana wangapi wadogo wasingeuawa au kubakwa kama wangeweza kutambua tabia halisi ya mtu huyo waliyemruhusu maishani mwao na aliyewanyanyasa?

Sababu Tano Kwa nini Watoto Wako watu wazima wanahitaji kuwa Wacha Mungu na wenye utambuzi. Wakati watoto wako watu wazima wana utambuzi, daima watafanya jambo sahihi. Bila huo utambuzi, wanaweza kutenda ujinga. “Ujinga ni furaha kwake aliye asiye na ufahamu, bali mtu wa ufahamu hutembea kwa unyofu” (Mithali 15:21). Hatutaki watoto wetu wazima kufanya chochote kijinga. Tunawataka kuwa na ufahamu mkubwa ili watembee katika njia iliyo sawa na kufanya mambo sahihi.

Watoto wako watu wazima wanapokuwa na utambuzi, wataweza kuona vizuri kwamba lipi jema na lipi ni baya. Mungu alipomtokea Sulemani katika ndoto akiuliza kile alichotaka Bwana ampe, Sulemani akajibu, “Nipe hekima na moyo wa adili niwahukumu watu Wako, nipate kupambanua mema na mabaya” (1 Wafalme 3:9). Jibu la Sulemani lilimpendeza Mungu kwa sababu hakuomba maisha marefu au utajiri au maisha ya maadui zake.

Badala yake, alitaka uwezo wa kuona wazi ni nini na nani alikuwa mzuri, na nini na nani alikuwa mbaya. Mungu alijibu ombi lake na kumpa moyo wenye hekima na ufahamu.

Watoto wako watu wazima wanapokuwa na utambuzi, wataweza kuona ni nini kitakatifu na safi na nini sio. “Watawafundisha watu Wangu tofauti kati ya vitu vitakatifu na vitu visivyo vitakatifu, na kuwafanya wapambanue kati ya yaliyo najisi na yaliyo safi” (Ezekieli 44:23). Katika siku hii ya udanganyifu mkubwa wa adui, sote tunahitaji zawadi hii kutoka kwa Mungu ili tuweze kupambanua kilicho kitakatifu, kilicho safi, na kizuri na kisicho kitakatifu; najisi, na kibaya. Sisi na watoto wetu watu wazima hatuwezi kuona Ukweli siku zote bila hiyo.

Watoto wako watu wazima wanapokuwa na utambuzi, wataweza kuona ni nini sahihi na nini si sahihi. Paulo aliwaombea Wafilipi kwamba wangetambua lililo bora na waishi kwa uadilifu. “Hili naomba, ili upendo wenu upate kuzidi sana katika maarifa na ufahamu wote, mpate kuyakubali mambo yaliyo bora, mpate kuwa na moyo safi na bila kosa hata siku ya Kristo, mkiwa mmejazwa matunda ya haki ipatikanayo kwa njia ya Yesu Kristo, kwa utukufu na sifa kwa Mungu” (Wafilipi 1:9-11.). Paulo alitaka watu wawe sawa katika mahusino na Mungu. Na ndivyo tunavyotaka sisi wenyewe na watoto wetu wazima tuwe.

Watoto wako watu wazima wanapokuwa na utambuzi, wataweza kuelewa mambo ya Mungu. Paulo alisema Mungu hutufunulia mambo kwa Roho wake. “Sisi tulipokea, si roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu; ili

tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu" (1Wakorintho 2:12). Pia alisema kwamba "mtu wa asili hapokei mambo ya Roho wa Mungu, kwa maana kwake ni upuzi; wala hawezi kujua kwa maana yatambulikana kwa jinsi ya rohoni" (1 Wakorintho 2:14). Mambo ya rohoni yanaweza tu kutambuliwa kiroho na watu walio na Roho Mtakatifu ndani yao na kwa hiyo wanaongozwa naye. Habari njema ni kwamba utambuzi ni jambo ambalo tunaweza kumwomba Mungu. "Ukiomba ufahamu, na kupaza sauti yako upate ufahamu; ukiutafuta kama fedha, na kuutafuta kama hazina iliyositirika; basi utapata ufahamu, kumcha BWANA, na kupata kumjua Mungu" (Mithali 2:3-3).

Tukiomba kwa bidii kwa Mungu kwa ajili ya utambuzi na ufahamu, Yeye atatupatia sisi, pamoja na roho ya kumcha na kumjua Mungu kwa kina. Ni lazima tuombe hilo kwa watoto wetu watu wazima pia.

## OMBEA MTOTO WAKO MTU MZIMA APATE UFUNUO KUTOKA MUNGU

Kuwa na ufunuo maana yake ni kuwa na maarifa uliyopewa na Mungu. Yeye Anafunua kile ambacho tayari ni kweli lakini kilikuwa imefichwa kwa akili na moyo wako. Kwa maneno mengine, ilikuwa kweli wakati wote, lakini sasa Mungu amekufunulia ili uweze kuiona Kweli hiyo vizuri. Mungu Ndiye anayefichua jambo tunalofanya ili kulibaini. Mungu

hutufunulia mambo katika Neno Lake tunapolisoma, kulisikia, au kulinena. Mtu naweza kusoma au kusikia kifungu au mstari wa Maandiko tena na tena na siku moja ghafla unapata ufunuo mpya juu yake ambao hujawahi kuuona hapo awali. Mungu pia hujidhihirisha kwetu tunapotembea Naye na kuwasiliana Naye katika maombi ili tuweze kumjua vizuri zaidi. Mungu hutufunulia mambo tunapomtafuta Yeye na maarifa yake. “Bwana, nipe ufunuo kuhusu maisha yangu ya baadaye. Je, mimi naweza kuhamia mji huu au mwingine? Je, niende kwenye kanisa hili au lile? Je, mimi naweza kuwa na mtu huyu au mtu mwingine?” Tunapoendelea kumwomba ufunuo, siku moja tutakuwa nao.

## SABABU NNE ZA KUMWOMBA MUNGU UFUNUO

1. Ufunuo kutoka kwa Mungu hadi mioyoni mwetu hutupatia maono ya maisha yetu. Hii haimaanishi kuwa tunajua kila kitu kwa undani, lakini tunajua tuna wakati ujao na kwamba ni mzuri. Biblia inasema,

“Pasipo maono watu huacha kujizuia; bali ana Heri yule aishikaye sheria” (Mithali 29:18). Mtu ambaye hana ufunuo kutoka kwa Mungu huwezi kuona picha kubwa na kwa hivyo hakuna kitu cha kumzuia asifanye chochote anachotaka. Atafanya hivyo asizuiwe kwa sababu hana chochote kinachomuongoza na Wala hajali siku zijazo.

2. Ufunuo kutoka kwa Mungu unamaanisha kwamba Yeye hufungua macho yetu na kutupa kuelewa na kuelimika kuhusu kusudi na wito wetu. Na Yeye Anadhihirisha ukuu wa uweza Wake kwa niaba yetu. Mtume Paulo akizungumza kwa Waefeso aliwaambia aliomba “kwamba Mungu wa

Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awape ninyi roho ya hekima na ufunuo katika kumjua Yeye, macho ya ufahamu kuangazwa” ili waweze kujua “tumaini la mwito Wake ni nini” na "Je! ni nini ukuu wa uweza Wake kwetu sisi tuaminio" (Waefeso 1:17-19). Nani kati yetu hahitaji hiyo? Ndiyo maana ni lazima uombe ili kupata ufunuo kwa ajili yetu wenyewe na kwa ajili ya watoto wetu watu wazima.

3. Ufunuo kutoka kwa Mungu hutusaidia kupata jibu linalofaa. “Mtu anayekengeuka kutoka katika njia ya ufahamu atatulia ndani ya kusanyiko la wafu” (Mithali 21:16). Bila ufunuo tunaweza kufanya maamuzi mabaya. Sio tu kwamba watoto wetu watu wazima hawawezi kufanya uchaguzi mzuri bila ufunuo kutoka kwa Mungu, mara nyingi hawawezi kufanya uchaguzi wowote mzuri. Jambo la kawaida sana katika jamii yetu leo ni kwa vijana kutokuwa na uwezo wa kufanya maamuzi ya maisha-kuhusu chochote! Mara nyingi wana shida ya kuamua wapi pa kufanya kazi, nini cha kufanya, nani wa kuoa, wapi pa kwenda, na mambo mengine muhimu ili kuendeleza maisha yao. Neno moja tu kutoka kwa Mungu kwenye mioyo yao linaweza kuwafanya wasogee wakiwa na uhakika wa aina yoyote. Ufunuo kutoka kwa Mungu hubadilisha kila kitu. Bila ufunuo kutoka kwa Mungu, vijana hawajui wafanye nini na wanaweza kubaki bila kuendelea mbele.

4. Ufunuo kutoka kwa Mungu unamaanisha kwamba anatufunulia Yeye ni nani kwetu. Wakati Yesu anawauliza wanafunzi Wake, Ninyi mwasema Mimi ni nani? Petro akajibu, “Wewe Ndiye Kristo, Mwana wa Mungu aliye

hai." Ambapo Yesu alijibu kwa kusema Petro amebarikiwa kwa sababu "mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye mbinguni" (Mathayo 16:15-17). Petro alimjua Yesu nani ilikuwa kwa sababu Mungu alikuwa amempa ufunuo kuhusu hilo. Mungu atatupa pia ufunuo juu yake Mwenyewe tunapoomba. Tunaweza kuwaombea watoto wetu watu wazima wapate ufunuo kutoka kwa Mungu kuhusu Yeye pia.

Yesu aliwaambia wanafunzi Wake kwamba "hakuna ajuaye Mwana ni nani ila Yeye Baba, na Baba ni nani isipokuwa Mwana, na Yule ambaye Mwana amtaka kumfunua" (Luka 10:22). Ufunuo wowote tunaopata kuhusu Mungu ni nani huja kwa sababu Yesu anataka kumfunua. Watu wengi sana hawamwamini Mungu kwa sababu hawajawahi kuwa na ufunuo wa Yeye ni nani.

Nilipompokea Bwana, nilitoka nje kwa imani na alichukua nafasi kwamba Yeye alikuwa halisi na kwamba kile ambacho Biblia ilisema kilikuwa Kweli. Lakini baada ya Mungu kujifunua kwangu nilipokuwa nikisoma Neno Lake, nilipokuwa nasikia Neno Lake likifundishwa, nilipotumia muda katika kusifu na kuabudu, na wakati mimi nilikuwa nikiomba. Nilimwomba Mungu kwa ajili ya ufunuo kuhusu maisha yangu na kuhusu Yeye, na Yeye alinipa. Kidogo kidogo na hatua kwa hatua, Mungu alinipa ufunuo huo wa mimi ni nani nikapewa maono ya maisha yangu na kusudi la kuwepo kwangu.

Ombea moyo wa kila mmoja wa watoto wako walio watu wazima kutamani hekima ya Bwana, utambuzi, na ufunuo. Mambo haya yanabadilisha maisha

na yatawanufaisha sana kila siku ya maisha yao

## NGUVU YA MAOMBI

Bwana, naomba kwamba ……………… (jina la mtoto mtu mzima) awe na hekima inayoletwa na Roho wako Mtakatifu (1 Wakorintho 12:8). Msaidie kuwa na nguvu, akikataa kuanguka katika njia za wajinga. Msaidie kuwa na hekima na kamwe asilikufuru Jina Lako. Lete usadikisho wenye nguvu ndani ya moyo wake wakati wowote anapokuwa anajaribiwa. Badala yake, ninaomba kwamba yeye "ataruhusu sifa kuu za Mungu" kuwa kinywani mwake na "upanga wenye makali kuwili" mkononi mwake (Zaburi 149:6). Bwana, umesema kwamba ikiwa tunakosa hekima, tunapaswa kuiomba na utatupatia. Kama ulivyoahidi katika (Yakobo 1:5). Ninakuja Kwako nikiomba kwamba umiminie Roho ya hekima juu ya watoto wangu watu wazima. Wape hekima ya kusema neno sahihi kwa wengine kila wakati, kutafuta ushauri wa kimungu na wenye hekima, kuwa wanyenyekevu na sio wenye kiburi, na wasiovutwa kuelekea hekima ya ulimwengu. Wasaidie wawe na aina ya hekima ifaayo inayoleta busara, hivyo kwamba itakuwa uhai kwa nafsi yao (Mithali 3:21-22). Wape hekima ambayo itawasaidia daima kufanya maamuzi mazuri, na kuamini watu sahihi. Wape hekima inayowaongoza mbali na hatari na kuwakinga na maovu. Wape hisia ya kina ya Ukweli, na uwezo wa kuchukua habari na kufanya maamuzi sahihi juu ya taarifa wanazozipata.

Najua ya kuwa Neno Lako ni upanga ukatao kuwili unaoutaka mkononi mwake, kwa hivyo ninaomba kwamba uweke upendo kwa Maandiko ndani

ya moyo wake na hamu ya kusoma Biblia kila siku. Andika Maneno Yako kwenye akili yake na moyoni mwake ili viwe uzima kwake. Mwezeshe kubaki na Neno Lako na kuzishika amri Zako apate kuishi (Mithali 4:4). Bwana, umesema katika Neno Lako kwamba “mwenye hekima atasikia na kuzidi kujifunza, na mtu wa ufahamu atapata shauri la hekima” (Mithali 1:5). Ninaomba kwamba mtoto wangu mtu mzima ajazwe na hekima Yako na aweze kusikia Ukweli na akujue. Msaidie kuelewa kumcha Bwana na kuwa na moyo wa heshima Kwako. Ninaomba kwamba “atapata utambuzi” na kupaza sauti yake kwa ufahamu ili yeye aweze kupata “Ufahamu na kumcha BWANA na kupata kumjua Mungu” (Mithali 2:3,5). Mpe hekima katika mambo yote ili aumbwe na Mkono wako na sio ulimwengu. Ninaomba Bwana umpatie mtoto wangu mtu mzima uwezo wa kupambanua kati ya mema na uovu, kama vile ulivyompa Sulemani uwezo huo. Msaidie kutambua kati ya vitu vitakatifu na visiyo vitakatifu, safi na najisi, mema na mabaya. Mpe ufahamu wa watu na hali, ukimwezesha kuona kile anapaswa kuona na kufanya. Msaidie kutambua tabia ya kweli ya kila mtu. Msaidie kuona mambo ambayo yanaweza tu kutambulika kiroho (1 Wakorintho 2:14).

Bwana, ninaomba kwamba ungewapa watoto wangu watu wazima ufunuo kwa ajili ya maisha yao. Wasaidie kuongozwa na ufunuo huo katika yote wanayofanya. Usiruhusu wawe waliopooza kwa kukosa uamuzi kwa sababu hawana Neno Lako mioyoni mwao. Wape ufunuo unaojaza akili na mioyo yao maono kwa ajili ya maisha yao ambayo hufungua macho yao kwa kusudi na wito Wako. Wape aina ya ufunuo unaowawezesha kufanya

uamuzi sahihi. Zaidi ya yote, naomba ungewafunulia Wewe ni nani kwao kwa namna ambayo wanajua kuwa ni ujumbe kutoka Kwako. Katika Jina la Yesu ninaomba.

**NGUVU YA NENO**

Kumcha BWANA ni chanzo cha maarifa, bali wapumbavu hudharau hekima na maelekezo.

**MITHALI 1:7**

Sheria ya mwenye hekima ni chemchemi ya uzima, ili kuepusha mtu na mitego ya kifo.

**MITHALI 13:14**

Upumbavu wa mtu hupotosha njia yake, na moyo wake huwa na hasira juu ya BWANA.

**MITHALI 19:3**

Yeyote apendaye hekima humfurahisha baba yake.

**MITHALI 29:3**

Mwana mwenye hekima husikiliza maagizo ya baba yake, lakini mwenye dharau hasikilizi maonyo.

**MITHALI 13:14**

## OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE KUTAFUTA UHURU, UREJESHO, NA UKAMILIFU

Mungu anataka sisi sote tuishi katika uhuru, urejesho, na ukamilifu alionao kwa ajili yetu. Haijalishi jinsi tulivyolelewa vizuri au hafifu, au jinsi inavyoonekana wakamilifu au tusio wakamilifu na vile uzoefu wetu wa maisha umekuwa, sote tuna vitu ambayo tunahitaji kuwekwa huru kutoka kwavyo. Watoto wetu wazima sio tofauti. Hata kama wao walilelewa katika nyumba bora zaidi na baba bora, bado watahitaji kwenda katika uhuru katika Kristo na kuwa zaidi kama Bwana. Kila mmoja wa watoto wetu watu wazima anawajibika na makosa kama mtu yeyote kimawazo, hisia hasi, matendo na mitazamo ya dhambi, au mambo ya zamani huwaathiri vibaya leo, na wanahitaji uhuru na uhuru kutoka kwa vikwazo vyote hivyo. Wanaweza kupata dhuluma kutoka kwa adui wa nafsi zao akijaribu kuwaibia na kuwaangamiza, na hivyo ni lazima wapate ukombozi na ni Mungu pekee awezaye kuleta urejeshwaji. Bila kujali kinachotokea katika maisha yao, wanahitaji kugeuzwa kuwa na sura ya Kristo. Bila hivyo, hawawezi kutafuta utimilifu wa Mungu kwa ajili yao. Habari njema ni kwamba Mungu ni mkuu kuliko chochote ambacho watoto wetu wazima wanaweza kufungwa nacho, na mipango Yake kwa kila mmoja wao ni pamoja na uhuru kutoka kwa kila kitu ambacho kinawatenganisha na yote aliyo nayo Mungu kwa ajili ya maisha yao.

Moja ya mistari ninayoipenda sana katika Biblia inasema, “Basi Bwana

Ndiye Roho; na alipo Roho wa Bwana, hapo ndipo penye uhuru (2 Wakorintho 3:17). Haya ni Maandiko ya kina hasa na ya kubadilisha maisha. Inasema kwamba Roho wa Mungu ni Roho wa uhuru. Na tunapokuwa katika uwepo wa Roho Mtakatifu wa Mungu, tunawekwa huru kutokana na mambo hayo ambayo yanatufunga, yanatupofusha, yanatuzuia, na yanatuzuia tusiwe vile tulivyokusudiwa kuwa tangu tulipoumbwa.

Jambo kuu hapa ni uwepo wa Bwana. Simaanishi kuwa uwepo wa Bwana hauna utata, kwani nani anaweza kuelewa kikamilifu yote anayoleta maishani mwetu? Lakini tunapokuwa na swali kuhusu jinsi tunavyoweza kupata uhuru, jibu si tata. Sisi kwa urahisi tunaweza kuwa katika uwepo wake. Uhuru wa kweli hautokei mbali na Bwana. Mabadiliko yanapatikana katika uwepo wa Mungu. Tunapokuwa katika ushirika na Roho wa Mungu, tunapata uhuru. Hiyo ni sababu ya msingi ni kwa nini ni lazima tuwe katika uwepo wake kadri tuwezavyo. Na tunahitaji kuomba ili watoto wetu watu wazima kuwa na ufahamu na hamu ya uwepo wa Roho Mtakatifu ili waweze kupata uhuru na uhuru wote, ukombozi na urejesho, mabadiliko na ukamilifu Mungu alio nao kwa ajili yao.

## UHURU NA KUWA HURU

Katika sura ya 1 ya kitabu hiki, sala ya kwanza kabisa tuliyoomba ilikuwa kumwomba Mungu amimine Roho wake juu ya watoto wetu watu wazima. Roho Mtakatifu anapomiminwa juu yao, Yeye huleta karama nyingi za ajabu na muhimu katika maisha yao. Moja ya mambo hayo matukufu ya Roho Mtakatifu ambayo Yeye huleta pamoja Naye ni Roho Yake ya uhuru.

Unaweza kuwa unafikiri, Ikiwa tayari tumeomba Roho Mtakatifu amiminwe kwa watoto wetu watu wazima, kwa nini tunahitaji kuomba tena kwa Roho wa uhuru ili kuwaweka huru?

Jibu la hilo ni kwamba tunapaswa kuomba hasa wakati kuna hitaji maalum. Hatuombei tu watoto wetu wazima wawe wazi kwa kile Roho Mtakatifu anataka kufanya ndani yao, tunaomba pia Roho Mtakatifu awaweke huru kutoka kwa kitu fulani. Sehemu yenye changamoto ni kwamba Roho Mtakatifu hatafanya yale ambayo mtu anampinga kufanya. Yeye Atamimina Roho Wake juu yetu, lakini hatalazimisha ukombozi Wake juu yetu. Hatatuweka huru ikiwa sisi hatutaki kuwa. Hii ndiyo sababu, kuwaombea watoto wetu watu wazima ni muhimu sana. Hatuwezi kulazimisha kutaka kuwa huru. Na tuseme ukweli, kunaweza kuwa na mambo ambayo sisi kama wazazi tunataka watoto wetu wazima kuwa huru, lakini hawaoni kwa namna iliyo sawa. Wanapenda tabia zao mbaya, ushawishi mbaya, au uchaguzi mbaya. Maombi yetu kwa watoto wetu wakubwa yanaweza kuwasaidia kutambua kwamba wanahitaji kuwa huru na kile wanachohitaji kuwa, na sala zetu zinaweza kufungua mioyo yao kutaka uhuru huo.

Wanapoelewa Ukweli kwamba Roho Mtakatifu ni Roho wa uhuru, basi watatafuta uwepo wa Mungu na mtiririko wa Roho Wake ndani yao. Wanapoona ni kwa uwezo wa uwepo Wake kwamba vifungo vya kuzimu vimevunjwa, basi watajitahidi kuondoa chochote katika maisha yao ambacho kinasimama katika njia ya uweza wake unaopita kati yao. Yesu

alikwenda katika sinagogi na kusoma kutoka katika kitabu cha Isaya akisema, "Roho wa BWANA yu juu Yangu, kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao na vipofu kupata kuona tena na kuwaacha huru waliosetwa." (Luka 4:18). Alisema mambo mengine muhimu kutoka kwa kifungu hicho pia, lakini kwa madhumuni ya sura hii, hebu tuzingatie yale maneno sita niliyoandika kwa italiki— "***kuwatangazia wafungwa uhuru wao***." Baada ya kumaliza kusoma kifungu hiki Yesu alisema, "Leo Maandiko haya yametimia masikioni mwenu" (mstari 21). Hii ina maana Yesu Ndiye utimilifu wa Maandiko hayo.

Mungu amemtia mafuta Yesu kutangaza uhuru kwa wafungwa. Aina ya uhuru ambao Yesu anaongelea hapa inamaanisha hakuna kuachiliwa kutoka kwa kitu kingine chochote isipokuwa uwezo wa Mungu juu yetu. Hatuna tena kikwazo na chochote ambacho Mungu anataka kufanya katika maisha yetu. Tunapompokea Bwana, tunawekwa huru mara moja kutoka katika utumwa wa dhambi. Tunakuwa watumwa wa haki badala yake (Warumi 6:18). Na tunaweza kukombolewa kutoka chochote kinachojaribu kutuzuia kufanya hivyo.

Mtoto wako mtu mzima anaweza kumjua Bwana na sheria Zake na bado akachukuliwa mateka kwa namna fulani na mtu au ushawishi fulani. Kama unafahamu jambo lolote ambalo mtoto wako mtu mzima anahitaji kuachiliwa—mtazamo usiofaa, tabia mbaya, kutomcha Mungu, uvutano usiofaa—mwombee kupata uhuru ambao Mungu anao kwa ajili yake. Kama

huna uhakika ni nini yeye anahitaji kuwa huru, mwombe Mungu akufunulie chochote kionekane ili uweze kuomba ipasavyo. Mara nyingi wazazi ndio wa mwisho kujua kuhusu mambo ambayo watoto wao watu wazima wanahitaji kuwekwa huru kwayo, kwa sababu wazazi ndio ambao watoto wao wakubwa hujaribu kuficha mambo haya kutoka kwao. Hatuwezi kamwe kudhani kwamba tunajua kila kitu tunachopaswa kujua kuhusu watoto wetu watu wazima. Mungu pekee Ndiye anayejua hilo. Lakini atatupa ufunuo tunapomuomba. Naye atatuonyesha jinsi ya kuomba.

Moja ya mambo makuu tunayoweza kuwafanyia watoto wetu watu wazima ni sisi wenyewe kuwa huru. Hii ni sehemu ya urithi huo wa kiroho tunaowaachia. Nimeishi muda wa kutosha kuwaona wana wa mwenye haki na watoto wa Mungu pia wasio waadilifu wakikua tangu utotoni na kuwa watu wazima. Nimeona tofauti ya baraka kwa watoto wa waumini walioishi njia ya Mungu ambayo mimi sijaiona katika watoto wa makafiri. Kuna kitu kuhusu tabia, ulinzi, utajiri wa roho, utimilifu, na hali ya maisha inayofanya kazi hutokea kwa watoto wa wenye haki. Angalia sijasema kuwa watoto wa wenye haki ni wakamilifu. Au watoto wa wazazi ambao hawakuwahi kufanya makosa, au watoto wa wazazi ambao walikuwa na yote yaliyofikiriwa tangu mwanzo.

Haki yako inakuja kwa sababu ya Masihi ndani yako. "Yesu Anapoalikwa moyoni mwako—au wakati wowote unaporudi Kwake baada ya kuanguka. Baraka za maisha ya haki—maisha ya walioishi kwa njia ya Mungu—zinaweza kumiminika kwako na kwa watoto wako wakubwa leo. Na hata

zaidi unaporuhusu maisha yasiyofaa, unazuia mtiririko wa Roho Mtakatifu ndani yako. Chochote unachofanya kinaweza kuathiri maisha ya watoto wako wakubwa, hata wasiweze kuachiliwa huru, wakati huo huo. Uhuru wako utafanya iwe rahisi kwao kupata uhuru wenyewe kwa sababu wanaona inawezekana kufanyika na hiyo inawapa imani ya kuamini kwamba inawezekana.

Pia, wakati wowote unapowekwa huru kwa chochote, kuna kitu kinavunjika katika ulimwengu wa roho, na hiyo inaweza kuendelea na kudhihirika kwa nguvu katika ulimwengu wa kimwili. Kwa mfano, mzazi akiwekwa huru kutokana na ulevi kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, itakuwa na athari kubwa katika uwezo wa mtoto mkubwa anayejitahidi kujiweka huru kutoka kwa kitu fulani.

Amri ya kwanza kati ya zile Kumi inasema, "Usiwe na miungu mingine ila Mimi." Amri ya pili inasema, "Usijifanyie sanamu ya kuchonga…usivisujudie wala kuvitumikia. Kwa maana Mimi, BWANA Mungu wako, ni Mungu Mwenye wivu, nawapatiliza watoto maovu ya baba zao hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, Nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao na kuzishika amri Zangu" (Kutoka 20:3-6).

Unaweza kuwa unawaza kama nilivyofikiria niliposoma amri hiyo mara ya kwanza, Hii sivyo kuhusu mimi-mimi siko hivi! Sijawahi kuchonga ndama wa dhahabu na sisujudu kwa sanamu yoyote iliyoundwa na mwanadamu. Lakini ukweli ni kwamba kuna njia nyingi tunaweza kuwa na picha ndani akili zetu juu ya kile tunachotaka ambacho tunainamia ndani ya mioyo yetu.

Tunachonga mawazo ya dhahabu kuhusu kile tunachofikiri tunahitaji kuwa nacho, au tunapaswa kuwa, au tunachotaka kutimiza—au kile ambacho watoto wetu wanahitaji kuwa nacho au kuwa au kutimiza—na sisi tunainua picha hizo zilizo juu katika mioyo yetu kila siku, hata juu ya mapenzi ya Mungu. Ni mara ngapi kile tunachotaka kinakuwa muhimu zaidi kuliko kile ambacho Mungu anataka, ni sanamu ndani ya mioyo yetu. Yeyote kati yetu, anaweza kuanguka kwa urahisi katika aina hiyo ya dhambi iliyofichwa. Miungu ya leo ni fedha, ngono, mahusiano, watu mashuhuri, kazi, uzuri, elimu, kutambuliwa, usingizi, taaluma, mali na vitu, michezo, simu, mazoezi mengi, hobby, uraibu, kamari, kununua vitu, utalii, starehe, chakula, muziki, maoni binafsi au maoni ya kufikirika, kukaa kwenye filamu, afya, marafiki, mifugo, pets, mume, mke, watoto, uhuru na haki zako, mahitaji na faraja yangu, siasa, kudhibiti wengine, cheo, wadhifa katika jamii, teknolojia, nafsi, social media likes, vita au silaha nk.

Mungu anasema katika amri hii ya pili kwamba matokeo ya dhambi za wazazi zitapatilizwa juu ya watoto, wajukuu, na vitukuu wa wale wasiompenda Bwana na kuishi katika njia Yake. Bila shaka, itahitaji mtu katika mojawapo ya vizazi hivyo kusema, "Mimi na nyumba yangu, tutamtumikia Bwana, na hivyo naomba katika Jina la Yesu kwamba dhambi hii na matokeo yake yaishie hapa na sasa," na laana hiyo ya kizazi itakuwa imevunjwa.

Muombe Mungu akuonyeshe sehemu yoyote katika maisha yako pale ulipo, siku zote unapaswa kulipa matokeo ya kitu kinachohitaji kuvunjwa.

Mwambie Mungu afungue macho yako kwa chochote unachoishi nacho ambacho hupaswi kuwa. Muulize Mungu akufunulie hatia yoyote ambayo huendi katika utiifu wa mapenzi Yake na sheria Zake. Muombe adhihirishe chochote unachokiabudu kisichokuwa Yeye.

Tunapotakaswa kutoka kwa mabaki ya dhambi zote, hatutapitisha tabia yoyote mbaya kwenda kwa watoto wetu. Ninakuuliza, kwa kuzingatia Maandiko hayo hapo juu kuhusu Mungu kuwalipiza maovu ya baba juu ya vizazi vyao, si ni sawa pia kuamini kwamba Yeye atatoa au kulipiza baraka zinazokuja kama matokeo ya haki ya mzazi katika uzao wao? Kwa maneno mengine, ikiwa tunapitisha matokeo kwa vitu tulivyofanya vibaya, Je, haingii akilini kwamba tutapata thawabu kwa ajili ya mambo tunayofanya sawa? Hiyo ndiyo maana ya maneno katika sehemu ya mwisho ya amri inayozungumza kuhusu Mungu "akiwaonyesha rehema maelfu elfu, wale wampendao na kuzishika amri Zake."

Habari njema ni kwamba hujachelewa kuanza kumpenda Mungu na kuishi kwa njia Yake ili upate faida za rehema Zake. Haijalishi nini kimetokea, au kwamba kinafanywa na mtoto wako mtu mzima, haujachelewa sana kwa ukombozi, uponyaji, na wokovu wa Bwana, kubadili mambo kwa njia ya muujiza. Na uzuri ni kwamba, hili linaweza kuanza na wewe.

Hutaki kuwapitishia watoto wako watu wazima kumbukumbu za mtu asiye na upendo, hali ya kiroho isiyo na uhai, isiyo na nguvu, na isiyo na shauku. Unataka kuwaonyesha upendo mwanana, nguvu, uchangamfu, kujazwa, tunda la roho na matumaini, kulazimisha, kuishi katika uhusiano na Bwana.

Unataka watoto wako watu wazima wamjue Bwana kama Mungu Mwenyezi ambaye Kwake hakuna lisilowezekana. Inastahili kuomba kwamba Mungu atafanya kukufunulia wewe—na pia mtoto wako mkubwa—chochote unachohitaji kuwekwa huru nacho, na kisha mwombe Roho Mtakatifu afurike kwenu ninyi nyote kwa ukombozi na uwepo Wake.

## UKOMBOZI NA UREJESHO

Kujua Ukweli hutuweka huru. Yesu alisema, "Ninyi mkikaa katika Neno Langu, ninyi hakika ni wanafunzi Wangu. Nanyi mtaifahamu Kweli, nayo Kweli itawaweka ninyi huru" (Yohana 8:31-32). Alikuwa anazungumza juu ya Ukweli wa Mungu hapa. Tunaweza kuwekwa huru kutokana na jambo fulani kila wakati tunaposoma Biblia na Roho Mtakatifu hulifanya Neno liwe hai katika mioyo yetu.

Omba kwamba watoto wako wakubwa wajue Ukweli unaowaweka huru. Wakati mwingine, hata hivyo, sisi tumefungwa na tunahitaji Mkombozi—Yesu—ili atukomboe kutoka katika makucha ya mwovu. Ukombozi unamaanisha kuishi bila kitu chochote kinachotuweka mateka dhidi ya Mungu. Inamaanisha kuokolewa kutoka kwa mtu au kitu kinachotutenganisha na Bwana. Yesu alitukomboa kutoka katika dhambi, mauti, na kuzimu, kwa hiyo sisi tunapompokea, tunapopokea ukombozi huo. Lakini kupitia mawazo yetu ya dhambi na kutojali tunaweza kufanya kazi wenyewe katika utumwa wa dhambi tena na kuhitaji kukombolewa kutoka kwa hali hiyo tena.

Mojawapo ya mambo ambayo Yesu alisema pia alipozungumza kuhusu

jinsi Roho wa Mungu wa Bwana alikuwa juu Yake ni kwamba Mungu alikuwa amemtia mafuta “kuwaweka huru wale ambao wanaoonewa” (Luka 4:18).

Inavyoonekana, ni jambo moja kuwa mateka na jingine kudhulumiwa. Yeye Alitangaza uhuru kwa wafungwa, lakini pia Aliwaweka huru wale walioonewa. Wakati mwingine tunakombolewa kwa haki kwa sababu Yeye Alisema hivyo; nyakati zingine tunaipa nafasi dhambi maishani mwetu na kuonewa na adui, hivyo tunamhitaji Mkombozi ili atuweke huru.

Yesu aliendelea kusema kwamba “yeyote atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi,” lakini “Ikiwa Mwana atawaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli” (Yohana 8:34-36). Yakobo, ndugu Yake Yesu alisema, “Hamna kitu kwa sababu hamwombi” (Yakobo 4:2). Tunahitaji kuomba ukombozi, kwa ajili yetu na watoto wetu wakubwa, ili Yesu aweze kutuweka huru kabisa. Tunapomwomba Mungu ukombozi, Yeye hatatukomboa tu, bali atatuokoa na pia kuwaweka huru watoto wetu kutoka kwa chochote kinachowafunga au kuwafanya kuwa kile ambacho Mungu aliwaumba kuwa. Lakini wanapaswa kutaka kuwekwa huru. Wanapaswa kutaka kuondolewa dhambi zote, na kuwa bainishi katika kuchagua hili. Ikiwa una mtoto mtu mzima ambaye haoni hitaji la kuwa huru kutokana na jambo ambalo ungependa yeye awe huru nalo, omba kwamba macho yake yanafumbuliwe, na kisha aone hitaji la ukombozi kutoka kwa chochote kilichofungwa katika maisha yake. Omba kwamba yeye mwenyewe atake uhuru kutoka kwa utumwa huo. Wakati fulani tunahitaji ukombozi, ingawa hatujafanya kosa lolote. Baada

ya Yesu kusulubiwa na kufufuka kutoka kwa wafu, Mfalme Herode alitesa waumini yaani kanisa. Alimuua Yakobo, mtume wa kwanza kati ya wale 12. Kisha akamkamata Petro kwa nia ya kumuua pia, mara tu Pasaka ilipoisha. Gerezani, Petro alifungwa minyororo kati ya askari wawili na akawa amezungukwa na wanajeshi 16 kwa jumla. Lakini waumini walikuwa na maombi ya kudumu kwa ajili ya Petro wakati huo-Mdo 12.

Alipokuwa amelala, malaika wa Bwana akasimama karibu naye na mwanga mkali ukaangaza ndani ya gereza. Malaika alimwambia Petro aamke na alipofanya hivyo, ile minyororo ikaanguka mikononi mwake. Kisha malaika akaamuru kuvaa nguo na viatu vyake na kumfuata (Matendo 12:1-8). Petro na malaika walipokuwa wakipita mbele ya walinzi, hakuna mtu aliyewaona. Na walipofika kwenye lango kubwa la chuma lililowafungia ndani, lilifunguka lenyewe (Kifungu cha 10). Mara tu Petro alipokuwa huru, malaika alitoweka na Petro akatambua kwamba Mungu alikuwa amemkomboa kabisa kutoka mikono ya adui.

Herode anamwakilisha Shetani na mashambulio yake yasiyoisha kwa waumini. Petro ni muumini ambaye alikuwa amefungwa minyororo, ingawa hakufanya chochote kibaya. Mpango wa Shetani ulikuwa kumwangamiza Petro, hivyo Petro alihitaji muujiza wa ukombozi. Na Mungu alimtoa katika hali isiyowezekana katika kujibu maombi ya bidii ya wengine. Mara baada ya kukombolewa, Petro alienda mahali watu walikuwa wakiendelea kusali na kuwaambia jinsi Mungu alivyomwokoa kutoka mikononi mwa adui. Maombi yasiyokoma ya waumini yalileta ukombozi na uhuru kwa Petro.

Ninahudhuria kanisa ambalo linapenda uinjilisti sana. Tunapanda makanisa katika Union na Majimbo ulimwenguni kote - haswa katika maeneo ambayo ni ya hatari kwa Mkristo kuwepo, maeneo ya JoshuaProject.Org au dirisha ya 1040, katika nchi 163 za dunia, ambapo bado kufikika kwa injili. Siwezi kutaja majina ya watu au hata nchi ninazozungumzia kwa sababu ya hatari itakayowapata wamishenari na familia zao. Mchungaji mmoja, ambaye nitamwita William, alianzishaa Kanisa la Kikristo katika moja ya nchi hatari sana kwa Mkristo. Hilo kanisa lilikua na kustawi kwa siri, lakini hatimaye William alikamatwa kwa kosa la kuzungumza na mtu kuhusu Masihi. Adhabu ya kitu kama hicho katika nchi hiyo huwa ni kifo. Alienda mahakamani bila uwakilishi wowote wa kisheria, wala baraza la majaji ikabakia kwa hakimu pekee yake kuamua hatima yake. Bila shaka, alitangazwa kuwa na hatia na kuhukumiwa kifo.

Kanisa letu lilisali kwa bidii kwa ajili ya William na familia yake, na makanisa yaliomba duniani kote. Tuliomba kwa vikundi, katika mikutano maalum ya maombi, na pia peke yetu katika vyumba vyetu vya maombi. Tuliposikia William amehukumiwa kifo, tuliendelea kuomba kwa bidii ili aachiliwe, huku tukijiandaa sisi wenyewe kwa mabaya zaidi ambayo yangeweza kutokea. Lakini siku moja habari zilitujia kwamba uamuzi wa hakimu ambaye alikuwa amesikiliza kesi ya William na kutangaza hukumu ya kifo nafasi yake ilitwaliwa ghafla na hakimu mwingine. Hakimu huyu wa pili, kwa sababu zisizojulikana kwetu, alibatilisha uamuzi wa jaji aliyepita na kumwacha William huru. Sote tulishangazwa na kile ambacho Mungu alifanya. Hali ilikuwa haiwezekaniki kabisa, lakini Mungu wa

yasiyowezekana alifanya muujiza kabisa. Ikiwa Mungu anaweza kufanya aina ya miujiza aliyofanya kwa Petro na William kwa kujibu maombi ya waumini, Je, ingekuwa vigumu kwake kumweka mtoto wako mtu mzima huru kutokana na kifungo chochote au hukumu ambayo imetamkwa juu yake au maisha yake? Nakuambia hakuna lisilowezekana kwa Mungu linapokuja suala la mtoto wako mtu mzima.

Ikiwa mtoto wako mtu mzima amefungwa na adui, au adui anajaribu kuingilia maisha ya mtoto wako mtu mzima, unahitaji kuimarishwa katika sala. Usisite kualika wengine kuomba pamoja nawe. Mara kwa mara, bila kukoma, maombi ni ufunguo wa uhuru na ukombozi kwako na kwa watoto wako watu wazima. Mungu anaweza kugeuza vita kwa njia yoyote anayotaka kupitia maombi, hasa wawili au zaidi wanaposali pamoja.

Hakuna watu wawili ambao wangeweza kufungwa zaidi bila matumaini, au karibu zaidi kunyongwa bila uwezekano wa kuachiliwa, kuliko Petro au William. Hata hivyo walikuwa wote wawili wamewekwa huru kwa uwezo wa Roho Mtakatifu kwa kuitikia maombi yasiyokoma ya waumini. Wakati ule watu walipokuwa wakimuombea Petro, Mungu aliangaza nuru Yake ndani ya gereza ili aweze kuona. Omba ili Mungu aangazie nuru kwa lolote lililomfunga mtoto wako mtu mzima amefungwa ili aweze kuona vizuri na kumfuata Roho Mtakatifu hadi kuwa huru.

Pamoja na ukombozi, Mungu ataleta urejesho wa yote yaliyokosekana kutoka kwa maisha yetu kwa sababu tulikuwa katika utumwa wa kitu fulani. Hiyo ina maana Yeye atarejesha miaka iliyoliwa na nzige na  tunutu. Na hii

ni habari njema kwa mtu yeyote ambaye maisha yake kwa namna fulani yamemezwa na adui. Chochote ulichonacho, kinachoonekana kuchukuliwa mbali na maisha yako au maisha ya watoto wako watu wazima-waliopoteza miaka au fursa, mahusiano yaliyopotea, kupoteza afya, kupoteza uwezo, kupoteza uhuru; unaweza kumwomba Baba wa mbinguni kuleta urejesho na Yeye atafanya.

Urejesho haimaanishi kwamba ikiwa mtoto wako mkubwa amekuwa na shida ya miaka kumi tangu alipokuwa na umri wa miaka 20, kwamba sasa Mungu atamrudisha tena kuwa na miaka 20 ghafula. La! Lakini inamaanisha kwamba Mungu aliyemkomboa kutoka katika taabu ataleta fursa mpya, afya mpya, mahusiano mapya, uwezo mpya wa wakati ujao na pia uhuru katika Kristo.

Biblia inasema kwamba "wazao wa wenye haki wataokolewa" (Mithali 11:21). Hiyo ina maana kwamba watoto wetu watu wazima watawekwa huru. Lakini wanapaswa kurudi kwa Bwana. "Ee BWANA, uturudishe Kwako, nasi tutarudishwa; ufanye upya siku zetu kama zamani" (Maombolezo 5:21). Ombea watoto wako watu wazima daima kumwelekea Bwana ili waweze kupata urejesho. Ujasiri tulio nao katika kumkaribia Mungu ni "kwamba tukiomba neno lolote sawasawa na mapenzi Yake, anatusikia. Na kama tukijua kwamba Yeye hutusikia"— chochote kile tuombacho tunajua kwamba tunayo ile haja tuliyomwomba (1 Yohana 5:14-15). Jambo kuu ni kuomba kulingana na mapenzi Yake. Tunahitaji ufunuo kutoka kwa Mungu na Neno Lake kujua mapenzi Yake tunapoomba.

Tunaweza kuomba hilo pia.

## MABADILIKO NA UKAMILIFU

Maisha yanaonekana kudorora na kukosa tija wakati mambo hayaendi vizuri. Ndio maana Mungu anachukua uharibifu wa mioyo iliyovunjika, akili iliyovunjika, roho iliyovunjika na kuwafanya watu kuwa wakamilifu. Anachukua vipande vilivyovunjika vya maisha yetu na sio tu anaviunganisha pamoja tena, lakini Yeye pia hufanya kitu kizuri kutokana na vipande hivyo. Ili aina hiyo ya utimilifu itendeke, lazima tukombolewe kutoka kwa chochote kinachopunguza mabadiliko ambayo Mungu anataka kufanya katika maisha yetu.

Ukamilifu kwa watoto wetu watu wazima humaanisha, miongoni mwa mambo mengine, kuwa na hisia zenye afya za wao ni nani, katika Bwana, Mungu aliwaumba wawe nani, na ni karama gani Mungu aliweka ndani yao. Inajumuisha kupata uhuru wa chochote kinachozuia ufunuo huo. Inamaanisha kujitenga na chochote kinachotutenganisha na Mungu. Inamaanisha kutumia muda katika uwepo wa Mungu ambapo utimilifu unapatikana. Hata wanapokua katika nyumba bora zaidi za Kikristo, ni vigumu kwa watoto kupitia utoto wao na miaka ya ujana bila aina fulani ya mvunjiko.

Kitu ambacho mtu alisema au kufanya, au hakufanya au kusema, au kitu alichoona au uzoefu fulani aliopitia, vinaweza kusumbua akili zao changa na kuvunja mioyo yao. Mahusiano yaliyovunjika bila uponyaji na urejesho yanaweza kuathiri mahusiano yao yote, na hasa uhusiano wao na Mungu.

Ikiwa yeyote miongoni mwa watoto wako wakubwa anapitia mambo ya kuvunja moyo katika maisha yao, unaweza kuwaombea wawekwe huru kutoka kwenye kumbukumbu zote mbaya.

Nimewajua watoto wengi watu wazima ambao walikuwa watu waliovunjika moyo na maisha yao yalikuwa yamevunjika, lakini kwa maombi ya wazazi wao waliachiliwa na maisha yao yalirudishwa pamoja. Mungu alitenda kwa nguvu katika kujibu maombi.

Hiyo haimaanishi kwamba mtu ambaye hana mzazi anayemwombea hawezi kupata uhuru. Kama hiyo ingekuwa kweli, nisingekuwa hapa leo. Nilikulia katika nyumba ambayo mama alikuwa mgonjwa sana wa akili na alikuwa akitupiga, akitunyanyasa na kututukana. Nilijaribu kila kitu ili kuondokana na maumivu ya utoto wangu, lakini ilinifanya tu kuwa mpweke na mnyonge, mwenye hasira, hofu, na kukata tamaa. Kila siku niliweza kuhisi maisha yangu yakizama ndani ya shimo lenye giza nene ambalo nilihofia kuwa nisingeweza kamwe kutoka humo.

Ilikuwa ni maombi ya wengine ambayo yaliokoa maisha yangu na kunileta kwa Bwana. Na kupitia maombi ya wengine, Bwana Aliniinua kutoka kwenye shimo lile; akaniweka huru kutoka kwa unyogovu, hofu, na wasiwasi; alibadilisha kabisa maisha yangu; nami nikafanywa kuwa mzima. Nilipoteza miaka mingi sana nikiishi kwa njia mbaya, lakini Mungu amenirudishia miaka hiyo zaidi ya nilivyowahi kufikiri kwamba inawezekana. Ikiwa anaweza kunifanyia hivyo mimi, fikiria ni kiasi gani Anachoweza kumfanyia mtu ambaye ana maombi ya dhati ya mzazi nyuma

yake.

Kila hatua tunayopiga kuelekea kufanya upya akili na nafsi zetu katika Bwana hutubadilisha zaidi na zaidi katika sura ya Kristo. Ni kweli, sote tuna safari ndefu, lakini kila wakati wa mabadiliko hutuleta karibu na ukamilifu Mungu alionao kwa ajili yetu. Je! Umepata sasa picha ya jinsi haya yote yanavyomaanisha maishani mwako na kwa watoto wako watu wazima?

Ina maana kwamba haijalishi ni nini watoto w=etu wakubwa wanahitaji ili kuwekwa huru kutoka kwacho, maombi yako yanaweza kuwa muhimu katika hilo kutokea. Bila shaka, kuna mambo watoto wako watu wazima wanapaswa kufanya kwao wenyewe. Kama vile Petro alivyopaswa kuvaa kabla ya kuruhusiwa kutoka gerezani, watoto wako watu wazima watalazimika kuvaa wenyewe pia. Omba kwamba watoto wako watavaa mavazi ya haki, sifa, upendo, unyenyekevu, na imani. Na jua kwamba Mungu ataheshimu sala yako, mpaka sifa, unyenyekevu, na imani vitakapoingia ndani yao.

## NGUVU YA MAOMBI

Bwana, ninaomba kwamba watoto wangu watu wazima watapata uhuru wote na uhuru uliotoka kwako. Waweke huru kutokana na chochote kinachowatenganisha na Wewe. Ninaomba kwa ajili ya kumiminiwa kwa Roho Wako Mtakatifu wa uhuru juu yao kila wakati. Kama wamefungwa kwa dhambi zao wenyewe, au uongo na mipango ya adui imewateka,

naomba uwakomboe. Ikiwa wanahitaji kuwekwa huru kutokana na mtazamo mbaya au imani isiyo ya Kiungu, wasaidie kurudi kwa Kristo.

Sijui njia zote ambazo watoto wangu watu wazima wanahitaji kuwekwa huru, lakini Wewe unazijua, Bwana. Angazia nuru Yako juu ya chochote kinachopaswa kuangazwa. Fichua chochote kilichowazuia. Nionyeshe jinsi ya kuomba ili waweze kukombolewa kutoka lwa kila kitu ambacho kinawazuia kutoka kwa yote Uliyonayo kwa ajili yao.

Bwana, najua Wewe ni mkuu kuliko chochote kinachoweza kuwafunga watoto wangu watu wazima. Mipango Yako kwa maisha yao ni ya uhuru kamili. Roho Mtakatifu, wasaidie kuelewa kwamba Wewe ulipo, kuna uhuru (2Wakorintho 3:17). Wasaidie kupata mabadiliko ambayo yanaweza kupatikana tu katika uwepo Wako. Mfundishe watoto wangu kutafuta uwepo wako katika Neno, katika maombi, shukrani, utii na ndani ya sifa na ibada. Msaidie kujua Ukweli katika Neno Lako unaomweka huru. Msaidie kuona Ukweli kuhusu dhambi yoyote katika maisha yake. Aone wapi adui anamdhulumu, ondoa upofu machoni mwake aweze kutambua Ukweli kuhusu hilo pia. Ambapo hukumu ya kikatili imekabili uhai wake, lete muujiza wa nafuu na mpe uwezo wa kutambua kwamba ni Wewe Ndiye uliyemkomboa.

Bwana Yesu, Neno Lako linasema kwamba ulikuja "kuwatangazia wafungwa uhuru wao" na "kuwaweka huru wale wanaoonewa" (Luka 4:18). Ninaomba hivyo popote mtoto wangu mtu mzima ametekwa na kitu chochote, Wewe Ungemweka huru. Pale ambapo yeye anakandamizwa na

adui, ninaomba ya kwamba umuokoe kutokana na adhabu hiyo. Vunja ngome yoyote ambayo adui ameiweka dhidi yake.

Bwana, najua kwamba moja ya mambo makuu ninayoweza kuwafanyia watoto wangu watu wazima ni kujiweka huru. Nionyeshe mahali ambapo nimejiruhusu kufungwa kwa njia yoyote—ama kwa mawazo na matendo yangu mwenyewe au kwa adui wa nafsi yangu. Nionyeshe ikiwa ninatumbuiza chochote katika akili yangu, moyo wangu, au maisha yangu ambacho si Chako ili niwe huru kutoka katika vifungo vyote. Niokoe kutoka kwa kila kitu kinachozuia mtiririko wa Roho Wako ndani yangu. Ninaomba kwamba uhuru wangu uwe wazi kwa watoto wangu watu wazima na kwamba itahamasisha hamu ya uhuru ndani yao. Nisaidie kuwa na aina ya uhusiano wenye nguvu, na uliojaa tumaini na uliofungwa Kwako Wewe ambao unatia ndani msawaziko wa akili na roho. Uniwezeshe daima kuishi njia Yako ili watoto wangu wote wapate kuvuna faida za rehema Zako (Kutoka 20:6). Ninaomba kwamba baraka za maisha yangu, nilizoishi kulingana na sheria Zako japo kidogo, zimiminike kwao. Ninaomba Ungemaliza chochote katika maisha ya watoto wangu watu mzima kinachohitaji kuvunjwa. Rejesha yale yote ambayo yamepotea. Rejesha wakati uliopotea, tunda la roho lililopotea, fursa, afya iliyopotea, mahusiano yaliyopotea, au chochote kile ambacho kimechukuliwa kutoka kwake na adui kama ulivyoahidi katika (Yoeli 2:25). Lete mabadiliko yanayohitajika ili yeye aweze kupokea utimilifu ulio nao kwa ajili yake.

Mara baada ya yeye kuwekwa huru, msaidie kukaa huru. Mshike

asiyumbishwe tena na mwovu na tamaa za dunia. Nitawaambia wanangu kwa uwezo wako wasimame imara katika Roho. “Simameni basi katika uhuru ambao Kristo alituweka huru nao wala msinaswe tena na nira ya utumwa” (Wagalatia 5:1). Ninasema Wewe, Bwana, “Utukuzwe, Ee Mungu, juu ya mbingu, na utukufu wako juu ya mbingu zote na ardhi; ili wapendwa wako waokolewe” (Zaburi 108:5-6). Katika Jina la Yesu ninaomba. Amina.

**NGUVU YA NENO**

Kwa sababu ameweka upendo wake juu yangu, kwa hiyo nitamtoa... Ataniita Mimi, Nami nitamjibu; nitakuwa pamoja naye katika taabu; nitamkomboa na kumheshimu. Kwa maisha marefu nitamridhisha.

**ZABURI 91:14-16**

BWANA huwapa wafungwa uhuru.

**ZABURI 146:7**

Malaika wa BWANA hufanya kituo kuwazunguka pande zote wanaomcha na kuwaokoa.

**ZABURI 34:7**

Farasi huwekwa tayari kwa siku ya vita, lakini wokovu unatoka kwa BWANA.

**MITHALI 21:31**

Anayeutumainia moyo wake ni mpumbavu, lakini aendaye kwa hekima

atakuwa salama mikononi mwa Mungu.

**MITHALI 28:26**

## OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE KUELEWA KUSUDI LA MUNGU KWA MAISHA YAO

Ugonjwa mmoja unaoenea kwa kasi ninaona leo kati ya watoto wengi wazima ni kuchanganyikiwa kuhusu kusudi lao ni nini maishani. Moja ya mambo yanayochangia mkanganyiko huo ni kwamba wanapata maoni mengi kutoka kwa ulimwengu kuliko maoni yanayotoka kwa Mungu. Njia za ulimwengu mara nyingi zinachanganya, wakati njia za Mungu zina uwazi. Na unapoishi maisha kwa njia Yake Bwana, huleta uwazi moyoni zaidi.

Kusoma tu Neno la Mungu, kwa mfano, kunaweza kumaliza mkanganyiko. Lakini watoto wengi wazima hutumia muda wao mwingi wa ziada kutazama televisheni, kuangalia kompyuta zao, michezo, simu au kushiriki katika aina nyingine za burudani, na hutumia muda mchache sana, kama upo, katika kusoma Biblia. Na mtu yeyote anayepokea maoni zaidi kutoka vyombo vya habari kuliko kutoka kwa Mungu, anaweza kuishia kutangatanga bila kufahamu kusudi. Wakati sauti ya Mungu imenyamazishwa, hakuna mwongozo wa Kweli wanaoupata na wanaweza

kwa urahisi kuongozwa katika mwelekeo mbaya.

Kuwa na kusudi maishani haimaanishi kuwa watoto wako wakubwa watajua kila undani kuhusu kile wanachopaswa kufanya na wapi wanapaswa kwenda, lakini watakuwa na mwanga katika baadhi ya mambo. Huenda wasijue kile hasa wanachotaka kufanya maishani, lakini watajua, kwa mfano, kwamba wao wanataka kwenda chuo kikuu au shule ya ufundi ili kuelimishwa na kupata ujuzi katika taaluma. Watoto wengine watu wazima wasio na nuru ya kusudi la Mungu hawana hata wazo mioyoni mwao kuhusu mipango ya Mungu maishani mwao. Bila uongozi wowote kutoka kwa Mungu, wanaweza kuwa wasio na malengo, au wanaweza kufuata kitu ambacho hatimaye kitakuwa kibaya kwao na kuishia kupoteza miaka ya thamani ya maisha yao kabla ya kubaini njia sahihi.

Bila mwongozo kutoka kwa Mungu juu ya nini cha kufanya, wanaweza kuogopa kutoka na kufanya chochote kwa sababu wanaogopa kwamba wanaweza kushindwa. Lakini wanapokuwa na uongozi wa Mungu ingawa wanaweza kuwa na mawazo ya uwezekano wa kushindwa, haiwazuii kusonga mbele na kile ambacho Mungu anawaita kufanya.

Uzoefu wa shule ya msingi na shule ya upili waweza kuleta madhara makubwa kihisia na kwa kusudi la kijana. Ikiwa watadhihakiwa au kudhalilishwa kwa sababu yoyote (bullied), jambo hili linaharibu hisia zao kuhusu wao ni nani. Ikiwa wanahisi kuwa hawakubaliki nyumbani kulinganisha na wengine, wanaweza kuwa na wakati mgumu kugundua na kujifunza kuthamini vipaji na vipawa vyao vya kipekee. Wakati kila siku ni

mtihani wa uvumilivu na wanajaribu tu kuishi, wanaweza kushindwa kuanzisha maana ya kusudi.

Binti yangu, Nuru, alitumia muda mwingi katika shule ya upili akijilaumu kwa sababu alikuwa na dyslexia. Nasema ni kwa sababu ameshinda hali hiyo sasa kimiujiza. Lakini ilichukua hatua kali na maombi mengi ya dhati. Kwa miaka mingi alikuwa ameniomba nimfundishe kusoma nyumbani, na nilisitasita kwa sababu mimi nilijua alikuwa na akili na kipawa maalumu na niliamini alihitaji ushirikiano na watoto wengine kwa kuhudhuria shule. Lakini nilikosea. Shule ilikuwa inakaribia kumwangamiza. Mwishoni mwa mwaka wake wa pili katika shule ya upili, alinisihi tena kumsaidia asomee nyumbani. Niliweza kuona maumivu makubwa ambayo yalikuwa yamejaa katika moyo kwa miaka mingi ya kile alichohisi ni kutofaulu na fedheha. Nilijua angefanya kazi kwa bidii kwa sababu alikuwa amefanya kazi kwa bidii zaidi shuleni, kuliko wenzake wengi na kwa matokeo kidogo sana. Pia nilitambua kuwa yeye alikuwa amepoteza kabisa furaha ya kujifunza aliyokuwa nayo kwa wingi, akiwa mtoto.

Niliamua kuchukua wajibu huo wa kumwanzishia shule ya nyumbani, ingawa nilitilia shaka uwezo wangu wa kuifanya vizuri kazi hiyo. Nilijua kwamba ningeweza kufundisha madarasa yake kama historia, jiolojia, jiografia, sayansi, Kiingereza fasihi, Kuandika, na Biblia, kwa sababu hayo ndiyo madarasa niliyopenda.

Lakini nilipata wasiwasi kuhusu hisabati. Sikuzote nilikuwa nimefanya vizuri katika hesabu shuleni, lakini hiyo ilikuwa wakati huo. Hesabu mpya

za siku huzi, zilikuwa nje ya uwezo wangu kupata maarifa sahihi ndani ya muda mfupi kiasi hicho. Hivyo mume wangu na binti yangu na mimi tuliomba, na Mungu alijibu maombi yetu kwa kutupatia mwalimu mzuri wa hesabu na mcha Mungu. Shule ya nyumbani ilikuwa jambo bora kwa Nuru, na tulifurahia sana kuifanya. Uzoefu wa somo la historia ulikuwa mzuri na wenye kuleta uhai wa mahusiano kwa sisi sote, na tuliendelea na safari nzuri za kwenda kwenye makumbuso na kuona maeneo ya kihistoria. Kiingereza kilikuwa cha furaha aliposoma kwa kujifurahisha na kuandika machapisho ya ajabu ya utafiti na insha. Tulijifunza Biblia pamoja kila siku na kusali kuhusu kusudi lake na wakati ujao. Nilianza kuona furaha yake ya kujifunza, ikianza kuchanua tena.

Baada ya shule ya upili alienda chuo kikuu cha muziki na burudani, lakini hakupenda watu walipotoa maoni kila mara kuhuzu sura na urembo wake, Mbali na maneno hayo ambayo hayakukoma ya kujihukumu mwenyewe bila kikomo. Alikuwa mwimbaji mzuri tangu alipokuwa mdogo. Alishinda shindano la talanta la shule zote kwenye jimbo, alikuwa moja ya viongozi katika tamthilia ya muziki jijini, aliimba kitaalamu kwa muda akifanya sauti za nyuma kwa wasanii wengine (background voices), na kurekodi albamu na waimbaji wengine wawili. Fadhili na mimi tulikuwa tukimtia moyo katika mwelekeo huo kwa sababu sisi tulifikiri kwamba talanta hii ni wazi aliumbwa kuzifanyia kazi. Lakini hakufanya hivyo kwa shinikizo na ushindani, wala uchunguzi wa mara kwa mara na uamuzi ambao kazi katika muziki ilihitaji. Alitaka maisha rahisi na ya amani, na tasnia muziki kawaida, hata tasnia ya muziki wa Kikristo haikuwa rahisi. Yeye hakuwa na

moyo kwa hilo. Jambo la msingi ni kwamba hakuwa na maana na kusudi kuhusiana na muziki.

Nuru alikuwa na kazi nyingi tofauti za vipindi vifupi, kutoka kuwa karani wa duka hadi kuhudumu, na katika kila kazi alikuwa akipata uzoefu mzuri kwa sababu alijifunza kuheshimu sana watu wanaofanya kazi kwa bidii katika aina hizo za kazi kwa muda wote, ili kusaidia familia zao.

Bado, hakuwa na maono wazi ya maisha yake, isipokuwa kwamba alikuja kupata ukakika kwamba kazi hizo zilikuwa njia ya kufikia tu lakini sio mwisho wa kusudi la maisha yake. Kwa hiyo tulikuwa tunaendelea hivyo hadi siku moja mimi na Nuru tukiwa tunaomba pamoja haswa ili Mungu afungue macho yake aone kusudi lake lilikuwa nini kwa ajili yake, ghafla kikamjia kile alichopaswa kufanya katika maisha yake. Alijua kwamba alikusudiwa kuwasaidia watu kiafya, yaani tiba ya mwili. Nilikuwa nimemweleza hayo hapo awali nilipokuwa nikimwambia kuhusu karama nilizoziona ndani yake. Daima alikuwa na mikono ya uponyaji ya ajabu.

Kulelewa karibu na wataalamu wa tiba ya mwili—kwa sababu sikuzote nimekuwa nikihitaji sana tiba kwa sababu ya majeraha ambayo nimekuwa nayo-ilimpa hisia ya asili ya jinsi ya kusaidia mtu mwenye maumivu. Na aliamini katika nguvu za matibabu na uponyaji. Mara moja akajua ndivyo alivyopaswa kufanya.

Nuru alijiandikisha katika shule ya taaluma hiyo na akagundua ni mahali pake hasa. Aliwapenda waalimu, alipata maelewano makubwa na

wanafunzi wengine, na yuko sasa hivi kujitolea kufanya mazoezi ya aina tofauti za tiba ya mwili ambayo inaweza kuhimiza uponyaji katika mwili (massage, tiba mbadala, sanitarium nk). Kila kitu kilianguka mahali pake na milango ikafunguka kwa ajili yake mmoja baada ya mwingine. Anasema mstari wake mpya wa maisha ni: "Usifanye lolote kwa ubinafsi au majivuno, bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko yeye mwenyewe. Kila mmoja wenu asiangalie masilahi yake tu, bali pia mambo ya wengine" (Wafilipi 2:3-4). Amanda anahisi kwa asilimia 100 yuko katika mahali anapopaswa kuwa na anafanya kile ambacho Mungu alimuumba kufanya—yaani kuwapa afya na uhai watu wanaoumia. Kilichobadilika ni hisia zake na kusudi.

## IKIWA MTOTO WAKO WAKUBWA HANA MAANA YA KUSUDI

Mtoto wako mtu mzima anaweza kuwa na maana ya kusudi tangu wakati anapoanza kusimama kwenye kitanda chake. Au unaweza kuwa na umri wa miaka 30, akiwa amelala karibu yako nyumbani kwa sababu amehama tena kwa mara ya tano baada ya kupata kazi nyingine na sasa ameamua kubaki nyumbani tu. Au labda yeye hakuwahi kuhama hata mara moja maana hajajua bado kusudi la Mungu katika maisha yake, ambapo Ningependekeza ujipatie sponji za magoti, kwa sababu unaenda utahitaji kujihusisha kupiga magoti katika maombezi fulani ya dhati, ili mtoto apate kufanya maamuzi na apate kusikia sauti ya Bwana.

Kwa kweli, ningesema chukua siku kila mwezi kufunga na kumuombea mtoto huyo mtu mzima. Omba Mungu avunje na kupunguza vizuizi vyovyote vinavyomzuia kupata maono ya maisha yake na hisia ya kusudi na wito wa Mungu. Niruhusu nipendekeze kwamba mtoto wako mtu mzima ambaye anaendelea bila hisia yoyote ya kusudi ni jambo la hatari. Nina uhakika kwamba watoto wanaojiua, wanaotumia madawa ya kulevya, wanywaji pombe kwa mazoea, wafanya uhalifu, au vurugu za mauaji kwa kawaida hawana maana au kusudi la maisha. Ikiwa wangefanya hivyo, hawangefanya chochote kinachokukiuka kusudi hilo. Wasingetaka kuacha njia ambayo Mungu amewawekea. Ikiwa mtoto wako mkubwa haonekani kuwa na maana ya kusudi hivi sasa, usioneshe kuwa na wasiwasi na hilo. Badala yake, mwamini Mungu na kumkabidhi tatizo hilo kwa sababu wewe ndiye unayepaswa kuliombea. Lakini ikiwa halikutokea mara moja, usiache kuomba. Najua wazazi wema ajabu na wacha Mungu ambao mwana wao hakuonekana kuwa na kusudi lolote. Alikuwa muumini, aliyelelewa katika kanisa la Kikristo lenye nguvu, na alikuwa mcha Mungu na marafiki wote wanaomzunguka pia. Nimeijua familia hii tangu enzi mtoto wao akiwa na miaka sita, na hangeweza kuwa na nyumba nzuri zaidi ya kupata malezi bora kuliko hapo alipokuwa. Baada ya shule ya upili hakutaka kwenda chuo kikuu au kufanya kitu kingine chochote. Wazazi wake waliomba na kumuombea apate ufahamu wa wito wa Mungu juu ya maisha yake. Miaka michache nje ya shule ya upili bado hakufanya kazi au kupata elimu yoyote zaidi, kisha akaenda safari ya misheni na kanisa lake na Roho Mtakatifu alipenya.

Alirudi nyumbani kutoka kwa safari hiyo akiwa na maono ya maisha yake kuwasaidia wengine. Alienda hadi chuo kikuu, akapata shahada ya kwanza, shahada ya uzamili, na udaktari. Kisha yeye alikutana na msichana mzuri na akamwoa. Haya yote yalitokea kwa sababu alipata maono kwa maisha yake na hisia kali ya kusudi la maisha yake kutoka kwa Mungu.

Watoto wengine huchukua muda mrefu zaidi kuliko wengine kupata maono ya makusudi yao toka kwa Mungu. Kila mtu ana njia yake wenyewe na ratiba yao wenyewe. Usijitie mwenyewe kufanya kazi hiyo ikiwa unaona mtoto wako mtu mzima anajitahidi kupata nafasi yake ulimwenguni. Na usimkaripie kwa maneno, kwa sababu itamtenga tu kutoka kwako na haitatimiza chochote. Unaweza kuomba, kumtia moyo sana, na kumfanya azungumze yeye mwenyewe kuhusu ndoto, matumaini, mawazo yake, na mambo anayopenda na asiyopenda. Mwambie ni kiasi gani unampenda na kuvutiwa naye. Mwambie kuhusu sifa nzuri na vipaji unavyoviona ndani yake. Mwombe Mungu akufunulie kile unachohitaji kuona kuhusu mtoto wako mtu mzima asiye na motisha. Jaribu kuwaelekeza waache kukaa katika vyumba vyao siku nzima ili kusikiliza muziki au kuvinjari katika mtandao. Hii haitawasaidia kugundua kusudi lao. Badala yake tabia hizi zitaweka ukungu kwenye ubongo. Ikiwa wataishi katika nyumba yako, wafanye kuwa sehemu ya kaya yako. Wape kazi za kufanya na kuwa na matarajio ya kile wanachopaswa kuchangia, kama vile wewe au mwenzi wako au yeyote mwingine anayeishi huko anavyotarajiwa kufanya. Wahitaji waishi kwa sheria zako.

Kuwa na matarajio ya chini kwa watoto wako watu wazima haifanyi chochote kizuri, kama vile kuwa na matarajio ambayo ni makubwa sana pia. Mume wangu na mimi tuliwaruhusu watoto wetu watu wazima kuishi katika nyumba yetu hadi walipokuwa tayari kifedha kuhamia katika maeneo mazuri na salama katika umri wa miaka ishirini+. Walikuwa wakiishi mbali na nyumbani chuoni katika vyumba nje ya chuo pamoja na wenzao. Mara walipokuwa nje ya chuo, kila mmoja alifanya kazi kwa muda wote na walitunza pesa za mishahara yao ya kwenye pochi zao wenyewe, na kila mmoja wao alisaidiwa na kiasi fulani alipokuwa tayari kifedha kuchukua jukumu hilo.

Ninaweza kuona kwa nini wazazi huwaruhusu watoto wao watu wazima kuishi nao kwa muda mrefu sana wakati hawafanyi kazi. Ni nafuu kukaa nao, na angalau unajua wako salama. Lakini inafika wakati ambapo mstari lazima uchorwe. Kwa mfano, kusema, "Ndiyo, wewe unaweza kukaa hapa, lakini lazima uwe unafanya kazi au uende shule au yote mawili. Ikiwa mtoto wako hawezi kufanya chochote. Hatapata kusudi lake akiwa ndani mbele ya TV, simu au mchezo wa video. Yeye hatapata kusudi akiwa amelala siku nzima na kukaa nje usiku kucha na marafiki zake. Yeye anaweza kuwa anafanya kazi katika mgahawa wa chakula (mama nitilie), lakini angalau wakati yeye anafanya kazi huko yeye anaweza kutambua kusudi lake ni nini. Na hiyo itasaidia katika kuratibu vyema huo mchakato.

Hata hivyo, watoto wako wakubwa hawawezi kuishi nawe milele, kwani hapo hawataweza kugundua kile alichonacho Mungu kwa ajili yao.

Isipokuwa Wao ni walemavu na wanahitaji utunzaji wako wa wakati wote, wakati fulani lazima waanze kuishi maisha ambayo Mungu amewaitia. Wewe na wao hamtafurahi mpaka wao watakapotimiza kusudi la Mungu maishani mwao. Ombea watoto wako watu wazima wapate hisia ya kusudi kutoka kwa Mungu, kwa sababu itawasukuma kufanya chochote wanachohitaji kufanya ili kutimiza hilo. Mtu mzima asiye na maana ya kusudi hatafanya chochote, lakini mtoto mtu mzima mwenye hisia ya kusudi atafanya kile kinachohitajika ili kufika pale anapohitaji kuwa.

## IKIWA MTOTO WAKO MKUBWA ANAHITAJI MWELEKEO

Kila mtoto mzima anahitaji hisia ya mwelekeo. Je, waende shule au kukaa karibu na nyumbani? Je, watapata kazi katika mji mwingine au katika mji wao yaani pale kabila lao lilipo au walipozaliwa? Je, wafanye kazi na kampuni hii au ile? Hata kama hawajaweza kujua madhumuni yao, wanahitaji kuchukua hatua katika mwelekeo fulani. Nawe unataka wawe na njia moja sahihi.

Baada ya kuanguka kwa Yerusalemu, watu walioachwa huko walimwomba Yeremia awaombee wapate mwongozo kutoka kwa Bwana ili wajue la kufanya. Kama ni kukaa pale Yerusalemu walipokuwa au kwenda Misri.

Yeremia aliomba, lakini jibu halikuja mara moja. "Ikawa baada ya siku kumi Neno la BWANA likamjia Yeremia" (Yeremia 42:7). Yeremia alikuwa na mawasiliano moja kwa moja kutoka kwa Mungu na alikuwa na

kibali cha Mungu, lakini bado alilazimika kungojea jibu. Daima kumbuka kwamba wewe, pia, una mstari wa mawasiliano ya moja kwa moja na Mungu. Line au  mstari Jina Lake ni Yesu. Na una kibali kwa Mungu kwa sababu Yesu anaishi ndani yako. Na unaweza kuomba mwongozo kwa mtoto wako mtu mzima kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Lakini usikate tamaa ikiwa jibu halijatokea mara moja. Linaweza kuja ghafla, kama swichi ya taa inavyowashwa. Au kinaweza kuja hatua kwa hatua, kama jua. Hakuna njia maalum ya jinsi jibu linavyokuja, litaendana sawa na lengo kwa sababu limetoka kwa Bwana.

Tatizo la Waisraeli lilikuwa ni kwamba walikuwa wameshatengeneza matokeo na majibu yao kabla hawajamwomba Yeremia awaombee kwa Mungu. Pamoja na hayo Mungu akawaagiza wakae Yerusalemu; hata hivyo walikuwa wameazimia kwenda Misri. Kwa sababu hawakusikiliza mwongozo wa Mungu, waliangamizwa. Omba kwa ajili ya watoto wako watu wazima sio tu wasikie mwongozo wa Mungu, lakini kufanya kile anachosema Yeye. Inasemekana juu ya Yerusalemu kwamba mji ulianguka kwa sababu haukufikiria hatima yake; kwa hiyo anguko lake lilikuwa la kutisha; haukuwa na “mfariji” (Maombolezo 1:9). Hili halikuwa hivyo kwa sababu Mungu hakuwahurumia watu; bali ni kwa sababu walikuwa wamekengeuka kutoka kwa Mungu na kufuata masanamu na hawakutubu kabisa. Watu hawakuzingatia kwamba dhambi yao ingewaongoza kwenye uharibifu. Walifanya wakifikiri hakutakuwa na matokeo. Hii hutokea hasa wakati watu wanajaribu kuishi bila mwelekeo waliopewa na Mungu juu ya hatima yao. Omba kwamba watoto wako watu wazima wawe na hekima ya

kutosha kuzingatia hatima yao. Ili kufanya hivyo, watahitaji kushauriana na Mungu ili aweze awaweke sawa katika mwelekeo sahihi.

Watoto wetu watu wazima wanaweza kuwa na mwelekeo na bado wanakuwa shida kufanya maamuzi. Wakati hawawezi kufanya maamuzi na uchaguzi kuhusu mambo muhimu, tunahitaji kuomba kwa ajili ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu juu yao ili kuwasaidia kutambua mambo. Na inatubidi tuendelee kuomba hadi wapate majibu yao

## IKIWA MTOTO WAKO MKUBWA TAYARI ANA HISIA YA KUSUDI

Jione kuwa umebarikiwa ikiwa mtoto wako mtu mzima tayari ana maana ya kusudi. Unachotakiwa kufanya ni kuomba kwamba asipoteze kusudi, na kwamba Mungu ataendelea kuwasaidia kufafanua na kuwawezesha kuchukua hatua zinazofaa ili kuona kusudi hilo likitimia katika maisha yao. Kumbuka, hata hivyo, kwamba kila mara inawezekana kwa mtu yeyote kupoteza hisia ya kusudi kwa kufanya kazi kupita kiasi, kuzidiwa, kufadhaika, kuugua, tamaa, mashaka, au kwa kufanya uamuzi mbaya, kushindwa kunakojirudia, kusikiliza ushawishi mbaya, au kuchanganywa na adui. Daima kama unaona hilo likitokea kwa watoto wako watu wazima, waombee wasikie upya sauti ya Roho Mtakatifu na warudi kwenye njia.

Mtume Paulo aliwaambia Waefeso akiomba kwamba macho yao na ufahamu ungetiwa nuru, ili waweze kujua nini tumaini la Wito Wake (Waefeso 1:18). Unaweza kuomba vivyo hivyo kwa watoto wako watu

wazima.

Omba ili macho yao yafumbuliwe kuona mwito wa Mungu ulio juu ya maisha yao. Omba ili waelewe kwamba kusudi na wito wao utakua na kutambulika kadiri uhusiano wao na Bwana unavyozidi kuongezeka.

## NGUVU YA MAOMBI

Bwana, ninaomba--------- (weka jina la mtoto mzima) apate maana na kusudi kwa ajili yake. Mpatie maisha na uwezo wa kuelewa kusudi hilo kwa uwazi. Mpe yeye Roho ya hekima na ufunuo ili macho ya ufahamu wake yapate kuangaziwa. Msaidie kujua ni nini tumaini la mwito Wako na ni nini ukuu usio wa kawaida wa uweza Wako kwa ajili yake (Waefeso 1:17-19). Ninaomba kwamba mipango Yako ya kutimiza hatima na kusudi Ulinalo nalo kwake ikafanikiwe, na sio mipango ya adui.

Bwana mwezeshe yeye kujitenga mbali na vikengeushi vyote vya huu ulimwengu na kukugeukia Wewe ili kusikia sauti Yako. Mzuie asipoteze muda wa maisha yake akifuata kitu chochote kinachomtoa kwenye njia uliyo nayo kwake. Ninaomba kwamba kila tukio limpeleke karibu na Wewe na mweke mbali zaidi kutoka kwa chochote kinachodhoofisha mipango Yako kwa ajili yake. Naomba kwamba wakati wote yeye ataunga mkono kusudi hilo na sio kuahirisha utekelezaji wake. Mwezeshe yeye daima kukua katika uhusiano wake na Wewe. Bwana, nionyeshe jinsi ya kuombea kusudi la mtoto wangu mtu mzima, mwelekeo na wito.

Nipe utambuzi na ufunuo. Nisaidie kumtia moyo na kumpa maoni ya

kusaidia bila kuhukumu au kudhulumu. Nioneshe wapi mipaka inahitaji kuchorwa, nionyeshe waziwazi inavyopaswa kuwa na unisaidie ili kuiweka. Pale ambapo jibu linaonekana kuwa linachukua muda mrefu kuja, nisaidie ili nisikate tamaa. Niweke nguvu katika maombi hadi kusudi Lako litimie kwa maisha yake.

Wasaidie watoto wangu watu wazima kusikia sauti yako ili wawe na neno kutoka Kwako mioyoni mwao, nalo liwe chachu inayowasukuma katika mwelekeo sahihi. Wape hisia kali ya mwelekeo na kusudi ambalo linapita hofu yote, ondoa kusitasita, uvivu, na kushindwa.

Wakati watoto wangu watu wazima wanapokuwa na kusudi, ninasali kwamba wasiweze kulipoteza. Wape hekima na hamasa ya kuchukua hatua sahihi kila siku. Bwana wawezeshe kuelewa ni nini muhimu zaidi katika maisha, ili waweze kufanya maamuzi na chaguzi kwa urahisi. Naomba kamwe wasikose kuzingatia hatima yao katika kila chaguo wanalofanya na katika kila wanalofanya. Wasaidie wasiwe na akili zinazotenda lolote bila kushauriana na Wewe. Wazuie kusisitiza juu ya yale wanayoyataka badala ya kutaka unachotaka Wewe.

Ingiza ndani ya watoto wangu watu wazima hamu ya kuwa daima katika mapenzi Yako. Nawaombea, “Mungu awape haja za mioyo yenu, zilizo katika mapenzi Yake; na kutimiza makusudi Yako yote” (Zaburi 20:4). Katika Jina la Yesu ninaomba. Amina.

## NGUVU YA NENO

Tunajua kwamba mambo yote hufanya kazi pamoja kwa ajili ya kuwapatia mema kwa wale wanaompenda Mungu, wale ambao wameitwa kwa kusudi Lake hasa.

**WARUMI 8:28**

Akupe kwa kadiri ya haja ya moyo wako, na kutimiza kusudi Lako lote.

**ZABURI 20:4**

Ninawataja katika sala zangu kwamba Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awape ninyi roho ya hekima na ya ufunuo katika Kristo kumjua Yeye, macho ya akili yenu yatiwe nuru; kwamba ninyi mpate kujua ni nini tumaini la mwito Wake.

**WAEFESO 1:16-18**

Karama na mwito wa Mungu havibadiliki.

**WARUMI 11:29**

Kwa kila jambo kuna majira yake, na wakati kwa kila kusudi chini ya mbingu.

**MHUBIRI 3:**

## OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE KUFANYA KAZI KWA MAFANIKIO NA WAWE NA UTULIVU

**WA KIFEDHA**

Moja ya mambo muhimu sana ambayo watoto wetu watu wazima, ni kwamba wanahitaji kusikia kutoka kwa Mungu kuhusu mwelekeo kuhusu kazi yao ya maisha. Bila ya uongozi utokao Kwake, wao wanaweza kuhangaika, kuteleza, na kutangatanga kwa miaka mingi, wakitoka kazi hadi kazi na kutoka kuchanganyikiwa hadi kukatishwa tamaa kwa mashaka ya kufa moyo. Tunataka pia wapate kusudi katika kila kazi wanayofanya, hata ikiwa kusudi hilo ni kuwafanya waseme kwa uhakika, “Nitarudi shuleni na kupata mafunzo zaidi au mafunzo mapya ya shahada kwa sababu sitaki kuishia kufanya vibarua ya aina hii katika muda wa maisha yangu yote." Au kusema, “Nitachukua yale niliyojifunza katika kazi hii na kuyatumia kwa kazi inayofuata." Suala ni kupata uwiano huo kati ya kupata uzoefu na sio kupoteza muda wao kwa kitu ambacho Mungu habariki.

Sura tano za kwanza za kitabu hiki zinazungumza juu ya kumwomba Mungu amimine Roho Wake juu ya watoto wetu watu wazima; ili kuwasaidia kukuza moyo kwa ajili Yake, njia Zake, na Neno Lake; na kuwapa hekima, utambuzi, na ufunuo; kuwaweka huru ili wawe vile alivyowaumba; na kuwawezesha kuendeleza maana wazi ya kusudi. Kuomba kwa njia hizi tano kutaweka msingi ndani ya maisha ya watoto wako wakubwa ambayo haitawasaidia tu kuelewa jinsi Mungu alivyowaita kumtumikia, lakini pia itawafunulia kujua kazi ya maisha yao. Mara nyingi watoto wetu watu wazima hawawezi kupata mwelekeo wa Mungu kwa maisha yao kuhusu kazi yao kwa sababu hawasikii kutoka Kwake. Bila

maono waliyopewa na Mungu, watasonga bila malengo. Maombi yako yanaweza kuwasaidia kupata maono yote hayo.

Isaya alizungumza kuhusu jinsi Mungu atakavyoumba mbingu mpya na nchi mpya, na nchi ya kwanza haitakumbukwa (Isaya 65:17). Na katika hiyo siku maisha ya watu wema yasingekatika kabla ya wakati wake. Na unachokifanyia kazi utakihifadhi na usiibiwe. "Watajenga nyumba na kukaa ndani yake; watapanda mizabibu na kula matunda yake… na wateule Wangu wataifurahia kazi ya mikono yao muda mrefu. Hawatajitaabisha bure…Na itakuwa ya kwamba kabla hawajaomba, nitajibu; na wakiwa bado kunena, nitasikia" (Isaya 65:21-24).

Mungu anataka tufurahie kazi yetu na si kujitaabisha bure. Na ndivyo sisi sote hutaka pia. Ndiyo maana tunapaswa kuomba, "Bwana, umesema matamanio yako kwa wale wanaokupenda na kuishi kwa njia Yako ni kwamba tutafurahia kwa muda mrefu kazi ya mikono yetu na kwamba tusifanye kazi bure. Ninawaombea watoto wangu watu wazima kwamba watakupenda Wewe, na wataishi katika njia Yako, na wataelewa wanachopaswa kufanya na maisha yao. Ninawaombea wafurahie kazi ya mikono yao kila wakati na sio kutumia wakati wa thamani katika kazi isiyozaa matunda."

## OMBA ILI WAWE NA BIDII NA KUFANYA KAZI KWA BIDII

Nimesikia ikisemwa na watu wanaomiliki biashara kuwa vijana wengi leo

wanataka kulipwa, lakini hawataki kufanya kazi kwa bidii na kuwa na jitihada kuhusu kazi zao. Najua hilo si kweli kwa wengi, lakini kuna watu wazima ambao ni vijana, wasioelewa jinsi kazi ngumu ilivyo muhimu. Nilipokuwa kijana, sikuwa na subira ya kungoja kuingia kazini na nilitaka kufanya kazi kwa bidii. Na tangu nilipokuwa na umri wa miaka 14 nimefanya kazi kwa bidii kila mwaka katika maisha yangu yote. Nadhani sababu ya kujitolea kwangu ni kwa sababu nimelelewa kama mtoto maskini na ikiwa sikuifanya kazi, sikuwa na pesa ya kujisaidia.

Ukweli kwamba baadhi ya watu hawana nia ya kufanya kazi kwa bidii sio siri. Kuna mengi ya kufaidisha katika kufanya kazi—na sio tu kwa pesa. Kuna pia hali ya kuridhika kwa nafsi na hisia ya kufanikiwa ambayo huja kama thawabu kwa nafsi. Na ile dhana kwamba umehudumu akumsaidia mtu. Lakini sisi wazazi mara zingine tumekuwa tukiwapa watoto wetu watu wazima kila kitu kiasi kwamba wao hufikiria, Kwa nini tufanye kazi kwa bidii wakati tunaweza kupata tunachotaka bila kugharimia kitu? Au wana roho ya uvivu, ambayo hufunika mawazo yao. Au wametumia madawa ya kulevya, ambayo yanawaficha wasione uhalisia wa maisha yao.

## MAMBO MATANO AMBAYO BIBLIA INASEMA KUHUSU WATU WENYE KUFANYA KAZI KWA BIDII

A. Wale wanaofanya kazi kwa mkono mlegevu watapata daima umaskini wa kutosha. Bali mkono wa mwenye bidii hutajirisha.” (Methali 10:4).

A. Wale wanaofanya kazi kwa bidii watakuwa na hazina kubwa ya ndani. “Mtu mvivu hapiki mawindo yake, mwenye bidii anazo mali za thamani nyingi” (Mithali 12:27).

B. "Nafsi ya mtu mvivu hutamani, asipate kitu; bali nafsi ya mwenye bidii itatajirika” (Mithali 13:4).

C. Wanaofanya kazi kwa bidii watakuwa viongozi. “Mkono wa mwenye bidii utatawala, bali mtu mvivu - atalipishwa kodi-atatumikishwa kazi na kulazimishwa” (Mithali 12:24).

D. Wale wanaofanya kazi kwa bidii daima watazidishwa. "Utajiri uliopatikana kwa udhalimu utapungua, bali yeye akusanyaye kwa jasho ataongezeka” (Mithali 13:11).

Sababu hizi tano pekee, zinatupa msukumo wa kutosha wa kuwaombea watoto wetu watu wazima kufanya kazi kwa bidii. Wakikataa, watapata mwisho usio na mafanikio yoyote.

## IKIWA UNA MTOTO AMBAYE HAWEZI KUTUNZA KAZI YAKE ANAACHA HAPA ANAENDA KULE.

Watoto wetu watu wazima ambao hawawezi kuendelea na kazi au hawapati kazi, kwa kawaida hawana mawasiliano ya kutosha na Mungu kupitia maombi binafsi. Mimi ninao uhakika kwamba kama mtu humwomba Mungu mwongozo kwa ajili ya maisha yao, hasa kuhusiana na kazi yao, Yeye atawapa. Ni lazima waweze kusikia kutoka kwa Mungu kuhusu hili,

kwa sababu Yeye anaweza kupata mwelekeo wao wa kitaaluma na usalama wa kifedha kwa njia ambazo hawawezi kuanza kufanya wao wenyewe. Ni lazima wajue waliumbwa kufanya nini na wapate mwongozo kutoka kwa Bwana kuhusu jinsi ya kufanya hivyo.

Hii haimaanishi kwamba watu walio na uongozi wa Bwana daima watafanya kazi katika kutimiza makusudi. Sisi sote tuna wakati tunafanya kazi katika ofisi fulani ili kulipa tu bili, na hakuna ubaya kwa hilo. Kwa kweli, mradi tu tunatambua kusudi ndani yetu na kumshukuru kwa Mungu kwa ajili ya hilo. Haijalishi jinsi kazi tuliyo nayo inaonekana kuwa haina maana, tunaweza bado kufanya kazi kuelekea malengo fulani. Tunaweza kufanya kazi ya kuchosha ikiwa inahudumia kusudi, kama vile inatupa uwezo wa kumweka mtoto katika shule bora, inatusaidia kulipa deni, kwaajili ya kuishi katika eneo salama, kuwa na pesa kwa elimu zaidi, au chochote kile chenye maana kwa maisha yetu. Tunaweza kuweka wakfu kazi yoyote kwa utukufu wa Mungu, bila kujali jinsi gani inavyoonekana kuwa mbali kutoka kwa kazi tunayotazamia kuwa nayo. Wakati watoto wetu watu wazima wanajitolea chochote wanachofanya kwa utukufu wa Mungu, Mungu ataibariki na kuleta mema yake mengi. Atahakikisha kwamba kila kazi inaongeza kitu kingine juu ya kingine na kujenga kuelekea kitu fulani chenye mantiki.

Itakuwa msaada sana ikiwa watoto wako watu wazima wanaelewa kwamba "katika kazi yote kuna faida," hata wakati hawajalipwa kama vile ambavyo wangependa, na kwamba ni kuzungumza tu kuhusu kufanya kazi bila

kufanya kazi yenyewe ndiyo husababisha umaskini (Mithali 14:23). Wakati hawaoni faida yoyote katika kazi wanayofanya, mioyo yao haitakuwa ndani yake na hawatakuwa na nia ya kufanya kazi zao pia. Kazi itawamaliza badala ya kuwatia nguvu. Lakini ikiwa wanamtumikia Mungu, hata katika kazi ikiwa duni, watakuwa na kusudi kwamba kazi hii inawafikisha kwenye kazi bora na ya mafanikio makubwa. Ikiwa una watoto watu wazima ambao hawatafanya kazi, wako kwenye njia ambayo hatimaye italeta uharibifu. Usiwaruhusu waende kwenye njia hiyo. Bibilia inasema, "Tamaa ya mtu mvivu humwua, kwa maana mikono yake hukataa kufanya kazi" (Mithali 21:25).

Omba ili wapate furaha inayotokana na kuiweka wakfu kazi yao kwa Bwana na kupata utimilifu wa kufanya kazi ili kuwasaidia wengine. Kuna tofauti kati ya mtoto mtu mzima ambaye hajapata kazi na anataka kucheza zaidi na kazi na kwa sababu hiyo hawezi kulipa kodi yake, na mtoto mzima ambaye anafanya kazi kwa bidii lakini biashara inaleta faida polepole sana au ameachishwa kazi kwa sababu mwajiri wake anapunguza wafanyakazi na sasa hawezi kufanya kazi huko alikoachishwa bila kupewa malipo. Katika hali ya kwanza mtoto anaweza kulazimika kuanguka ili aweze kupata ufahamu sahihi juu ya umuhimu wa kujishughulisha. Katika hali ya pili, unaweza kumzuia mtoto huyo mtu mzima kuharibiwa au kukatishwa tamaa kwa kumsaidia. Mwombe Mungu akuonyeshe ukweli.

Ikiwa mtoto wako mtu mzima anapata usaidizi wa kifedha kutoka kwako, au kutoka kwa mtu mwingine yeyote, wewe una haki ya kuzungumza naye

kuhusu kile anachofanya na maisha yake. Omba kwanza ili yeye apate moyo wa kupokea mashauri, na uwe tayari kusikiliza maoni yake. Basi omba kwamba awe mnyenyekevu kiasi cha kukuheshimu kama mzazi kwa kusikiliza ushauri wako. Je, wewe unakumbuka amri inayosema watoto lazima waheshimu wazazi wao na ikiwa wanawaheshimu, Je! unatarajia mambo yaende vizuri kwao? (Kutoka 20:12). Huwezi kujua kama mambo si mazuri katika kazi ya mtoto wako mtu mzima kwa sababu yeye hajakuambia na anakuheshimu kama mzazi.

Mwombe Mungu akuonyeshe ikiwa unampa mtoto wako mtu mzima msaada mwingi sana kiasi kwamba yeye halazimiki kujitegemeza. Kuna wakati ambapo kusaidia kunakuwa kuwezesha uvivu, na tunahitaji Mungu atuonyeshe ni wapi pa kuweka mpaka kwa misaada ya watoto wetu wakubwa.

## OMBEA WAWEZE KUWA NA HALI NJEMA KIUCHUMI

Pamoja na kusali kuhusu kazi ya watoto wetu watu wazima, tunahitaji pia kuomba kuhusu fedha zao. Omba ili wawe na kipato kinachokidhi mahitaji yao. Kwa mtoto mtu mzima mwenye mke na watoto wanne, anahitaji mapato zaidi kuliko mtoto mmoja kwani agawa mshahara wake na watuwatano. Kadiri mahitaji yao yanavyoongezeka, ndivyo tunavyopaswa daima kuomba kwamba mapato yao pia yainuke. Hakika wanataka kufanikiwa, na hilo litaonekana katika jinsi mapato yao yanavyoongezeka. Omba kwamba wao watapata msawaziko wa mawazo ili wasiwe na "mkono

mlegevu" na kuwa maskini (Mithali 10:4) au “kufanya kazi kupita kiasi ili kuwa tajiri” (Mithali 23:4). Omba kwamba wafanye kazi kwa bidii ya kutosha, na kuwa na fursa ya kutosha, kuleta mapato wanayohitaji.

Bila shaka, ni bora kuomba kabla ya kitu chochote kutokea, kama kuzuia ni bora kuliko kuponya. Kwa mfano, mwombee ili apate kibali kwa watu ambao anafanya kazi nao. Muombee awe sawa na mshahara unaoendana na kazi anayofanya. Omba kwamba kazi yake itathaminiwa na kutambuliwa, kumwezesha kusonga mbele. Omba kwamba yeye anafanya kile anachopaswa kufanya kila wakati katika majukumu yake ya kazi. Ikiwa watoto wako watu wazima wanataka kazi mbaya—nje ya mapenzi ya Mungu, kama vile kufungua baa, kutengeneza pombe, umalaya, wizi, ukatili, kutoa video chafu kama ponografia, kufuatilia madeni ya watu, na kunyanyasa watu (debt collector), matangazo ya bidhaa kinyume na Maandiko, matumbuizo ya aina fulani au michezo kama ndondi nk—ndipo wataendelea kuhangaika. Hiyo si kusema hawatafanya jitihada katika kazi yao ikiwa wako katika mapenzi ya Mungu, lakini pambano hilo litapelekea kitu kikubwa. Wanapokuwa nje ya mapenzi ya Mungu, mapambano yataongoza popote pale. Afadhali kuhangaika ukiwa katika mapenzi ya Mungu na hatimaye kuzaa matunda kuliko kuhangaika nje ya mapenzi ya Mungu na kutokuwa na kitu cha kudumu cha kuonyesha kwa ajili Yake.

Watoto watu wazima walio na wazazi wanaoomba kwa nguvu, mara nyingi hupata kazi ya maisha yao mapema, lakini kwa hakika sio hivyo kila wakati. Kuna wazazi wengi wacha Mungu, waliojitoa na wanaoomba ambao

wamechanganyikiwa na ukosefu wa motisha wa watoto wao wakubwa, hasa wakati watoto wao wengine watu wazima hawana shida hiyo. Jambo la kufanya katika hilo ni kuendelea kuomba kwa bidii na kutokata tamaa. Mtoto huyo ana kusudi kuu, na mara nyingi inachukua maombi makubwa kuona kusudi kuu likitokea. Kumbuka kwamba adui daima atakuja kuzuia na kupinga mipango ya Mungu katika mtoto wako mkubwa na kujaribu kulazimisha mipango yake mwenyewe. Achilia maombi yako kuwa nguvu ambayo ni hatua ya kupambana na adui. Salimisha ndoto na mipango yoyote unayoweza kuwa nayo kwa ajili ya maisha ya mtoto wako mtu mzima na kuomba kwa ajili ya mpango wa Mungu kutawala juu ya yote.

Mipango ya Mungu na ndoto zako zinaweza kuwa moja na sawa, lakini unahitaji kuwa na uhakika. Na unapaswa kuruhusu mipango yako ivunjike ikiwa hailingani na mipango ya Mungu. Mungu atatuhitaji tuweke ndoto zetu kwa ajili ya watoto wetu watu wazima Kwake kwa sababu Yeye anataka sisi na watoto wetu watu wazima kumtegemea Yeye kutengeneza maisha yao, ili yatokee kwa uzuri.

Mungu alimwomba Ibrahimu amchukue mwanawe wa pekee, Isaka, mahali maalum ili amtoe dhabihu. Isaka alikuwa mtoto wa ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu na Sara, ambaye hakuwa na mtoto hadi uzee. Mungu alikuwa anamwomba Ibrahimu aweke chini ndoto yake ya kuwa na mwana wa ndoto yake na kusudi la mwanawe na kumpa Mungu ndoto hiyo kikamilifu. Kama ilivyotokea, hii ilikuwa mahali pale pale ambapo Mungu hatimaye angemtoa Mwanawe wa pekee, Yesu katika Mlima Moria. Na kwa kuwa

tayari kutoa dhabihu hiyo, Ibrahimu alionyesha heshima yake, upendo usiobadilika, na kumtumaini Mungu kwa sababu aliamini Mungu angemwinua Isaka kutoka kwa wafu. Mungu aliingilia kati kwa wakati ufaao kwa kutoa kondoo dume kwa ajili ya sadaka badala ya Isaka (Mwanzo 22:1-13). Kisha "Abrahamu akaita Jina la mahali pale, BWANA-Atatoa; kama inavyosemwa hadi leo, 'Katika Mlima wa BWANA atajipatia" (Mwanzo 22:14).

Maana yake kwetu ni kwamba Mungu ni mwaminifu kuturuzuku kwa wakati, kuhusu yale tunayohitaji, ikiwa sisi ni waaminifu kumtii na kufuata mwongozo Wake. Inamaanisha pia kwamba Mungu anatuhitaji tuweke ndoto yetu Kwake na anataka tujue maono yetu yanapaswa kutoka Kwake—kwa sababu anataka tujue kwamba Yeye Ndiye ataifanikisha njozi hiyo. Tunapoacha ndoto kufa ambayo ni mapenzi ya Mungu, Yeye atafanya ifufuke. Kisha tutajua kwa hakika kwamba Mungu aliiweka kwetu na tukifanya hivyo tusiifanye kwa nguvu zetu wenyewe.

Omba ili mtoto wako mtu mzima aweze kusalimisha ndoto yake kwa Bwana. Na hiyo ndoto unapojisikia kuwa imekufa, omba Mungu aifufue. Ombea mtoto wako mtu mzima aone mkono wa Mungu ndani yake. Kujielekeza katika mwelekeo wa Njia za Mungu kutakusaidia usikate tamaa na kuwa na wasiwasi unapoona mapambano ya kifedha yakitokea kwa mtoto wako mtu mzima. Itakusaidia kumtia moyo, hata anapokata tamaa, maana utakuwa unaona picha kubwa zaidi.

## NJIA NANE ZA KUOMBEA USALAMA WA KIFEDHA

1. Omba kwamba mtoto wako mtu mzima afanye kazi kila wakati fursa inapotokea. “Alalaye wakati wa mavuno ni mwana asababishaye aibu” (Mithali 10:5).

2. Omba ili mtoto wako mtu mzima awe na hekima ya kuokoa pesa kwa ajili ya nyakati za kupungukiwa.

“Akusanyaye wakati wa kiangazi ni mwana mwenye hekima” (Mithali 10:5).

3. Omba kwamba mtoto wako mtu mzima ajifunze kumpa Bwana kile anachohitaji “Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba Yangu, mkanijaribu kwa njia hii, asema BWANA wa majeshi, muone kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni na kuwamwagieni Baraka hata isiwepo nafasi ya kutosha au la’” (Malaki 3:10).

4. Omba kwamba mtoto wako mtu mzima atatoa kwa ukarimu kwa maskini na wahitaji daima. “Amebarikiwa yeye anayewaangalia maskini; BWANA atamwokoa wakati wa taabu. BWANA atamlinda na kumweka hai, naye atabarikiwa duniani; hatamtia katika matakwa ya adui zake” (Zaburi 41:1-14).

2). “Azibaye masikio yake asisikie kilio cha maskini naye atalia na Bwana asisikie” (Mithali 21:13). “Awapaye maskini hatakosa, bali afichaye macho yake atakuwa na laana nyingi” (Mithali 28:27).

5. Omba kwamba mtoto wako mtu mzima atamtafuta Bwana kuhusu kila

kitu, ikiwa ni pamoja na kumtolea Mungu. “Wana-simba hukosa na kuona njaa; lakini wale wamtafutao BWANA hawatapungukiwa na kitu chochote chema” (Zaburi 34:10).

6. Omba kwamba mtoto wako mtu mzima apate mali kulingana na mapenzi ya Mungu, ili asipoteze uwezo wa kufurahi. “Baraka ya BWANA hutajirisha; wala hachanganyi huzuni pamoja nayo” (Mithali 10:22).

7. Omba ili mtoto wako mtu mzima ajue kwamba hazina ya Kweli inapatikana katika Bwana. “ilipo hazina yako, ndipo utakapokuwa na moyo wako pia” (Mathayo 6:21).

8. Omba kwamba mtoto wako mtu mzima daima atakuwa na hisia ya kile ambacho ni sawa na cha kimaadili. “Kama kware akusanyaye makinda asiyoyazaa, ndivyo alivyo yeye apataye utajiri, lakini si kwa haki; utamwacha katikati ya siku zake, na saa zake za mwisho atakuwa mpumbavu” (Yeremia 17:11).

Uchumi wa dunia umeyumba sana. Hakuna dhamana, isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu. Mungu anasema ukitoa, utapokea; ukitafuta mapenzi Yake, utapata yote unayohitaji; ukifanya kazi kwa bidii, utapata thawabu; kama unaishi katika njia ya Mungu, hutapata njaa. Watoto wetu watu wazima wanahitaji maombi yetu ili kuwasaidia kuelewa na kuamini kanuni hii ya utoaji.

Kumbuka kila wakati unapoomba kwamba, wakati fulani Mungu hutumia fedha—au ukosefu wa fedha ili kupata usikivu wa mtoto wako mtu mzima.

Ukiomba na kusali na mambo hayabadiliki, mwombe Mungu akuonyeshe wewe na mtoto wako mtu mzima ikiwa kuna masomo muhimu ambayo anahitaji kujifunza kupitia hili. Au labda Mungu ana mipango mingine kwa ajili yake ambayo inahitaji aina fulani ya mabadiliko katika kazi, mtindo wa maisha, umakini, mtazamo, malengo, au maono. Unapoomba kuhusu hili, utapata ujasiri wa kujua kwamba mtoto wako mtu mzima yuko mikononi mwa Mungu. Labda Mungu anamtaka tu kuelewa ilipo hazina yake ya kweli kabla ya kumbariki na tuzo za fedha.

Sisi sote tuna nyakati nzuri na mbaya linapokuja suala la kazi na fedha. Ikiwa tunatembea na Mungu, basi hata vikwazo havitakuwa tena vya kuhuzunisha tukijua Mungu Yuko nasi katika hayo. Tunachotaka kuepuka ni majanga makubwa, kama vile kupoteza nyumba, kuingia kwenye deni, au kufilisika. Maombi yetu hayahakikishi kuwa watoto wetu watu wazima wataweza kuepuka matatizo yote ya kifedha, lakini unaweza kuamini kuwa Mungu atawasaidia katika hali kama hizo na kuwafundisha masomo muhimu katika hali kama hizo. Kuna watoto wetu wengine watakuwa na fedha nyingi na hata mamilionea, hata wanahitaji pia kuombewa ili waelewe kwamba daima mwanadamu ni wakili, kama hawajaoa au kuolewa, tafuta ukubali wao katika kujadili na kusaidiana, Mungu hatoi mali ili itufujwe tu au kutumia kwa kujionyesha.

## JINSI YA KUOMBEA MTOTO MTU MZIMA ALIYE NA MATATIZO YA KIFEDHA

Hakuna anayetaka kuona watoto wake watu wazima wakipitia matatizo ya kifedha. Lakini pia hatuyataki kwa ajili yetu wenyewe pia, kwa kuwa ni jambo linalogharimu sana. Mara nyingi Mungu atatumia matatizo ya kifedha kupata umakini wa mtu. Na hakuna kinachofanya hivyo kwa haraka, isipokuwa kwa ugonjwa. Shida ya kifedha ni moja ya nyakati ngumu katika maisha yetu, na ni kama dhiki kwetu tunapoiona ikitokea kwa watoto wetu watu wazima.

Sote tumeona majanga ya kifedha yakitokea kwa sababu ya shida za kiafya, talaka, watoto kupata matatizo, au ukosefu wa ajira. Na Mungu huyatumia haya matatizo ili kupata umakini wetu. Huenda ubaradhifu wa kifedha, kufungwa, au kufilisika ndiyo njia pekee ya kuwafikisha watoto wako kwenye njia sahihi. Wanaweza kuwa na maanguko na kuweza kumwona Mungu Ndiye chanzo chao cha yote mema.

Omba na umwombe Mungu akuonyeshe wewe ukweli kuhusu hilo. Yeye Atafanya hivyo. Hakuna mtu anayetaka kupata shida ya kifedha, lakini shida inaweza kusababisha mabadiliko makubwa kwa mtoto wako mkubwa. Ikiwa watoto wako wakubwa tayari wamekumbwa na msiba wa kifedha – iwe kutokana na matumizi ya hovyo au wameangukia kwenye nyakati ngumu, iwe wameingia hatua ya kuhangaika au wamepoteza nyumba yao kwa kufilisika jua kwamba Mungu anaweza kuwarudisha, kuwaweka kwenye mahali salama, na kuwapa fedha kwa utulivu tena. Omba ili hali yao iwaelekeze kwa Bwana na njia Zake zaidi ya hapo awali katika maisha yao.

Ikiwa maafa ya kifedha au shida husababishwa kwa sababu mtoto mtu mzima hawezi kazi-iwe ni kwa sababu ya ukosefu mkubwa wa kujiamini, hofu ya kushindwa, unyogovu, ubinafsi, au uvivu—yeye anahitaji usaidizi wa kitaalamu wa mshauri wa kifedha na labda mshauri wa Kiroho. Hili ni tatizo ambalo halitapita bila kuingilia kati, hasa ikiwa kuna tatizo la kitabia.

Kama mtoto mkubwa ni mchapakazi hadi kufikia hatua ya hii katika maisha ya kazi na mambo yanatokea kama vile afya kudidimia, ndoa kusambaratika, watoto na anakosa wakati wa kuwa pamoja na Bwana, basi omba kwa ajili ya uamsho ndani yake ili aweze kuelewa haja ya usawa na hisia ya vipaumbele vilivyowekwa na Mungu.

Moja ya faida ya kupoteza kila kitu ni kwamba inakulazimisha kutambua kwamba Mungu ni kila kitu. Naye atatoa kila kitu. Na ndani Yake kila kitu kupatikana. Na kila ulicho nacho kinatoka Kwake. "Mungu wangu atawajazeni nyote haja kwa kadiri ya utajiri wake katika utukufu ndani ya Kristo Yesu" (Wafilipi 4:19).

Kumtegemea Mungu kabisa kutawasaidia watoto wako waliokomaa kutatua hali hiyo na kuanza upya bila kukata tamaa. Itawaongoza kupata kazi inayofaa. Itawapa hekima ya kutumia na kuweka akiba na kuishi kulingana na uwezo wao. Kwa kutoa sala—na sifa kwa Mungu kwamba anafanya mambo makuu katikati ya hali hii, yaweza kuwa jambo bora zaidi kuwahi kutokea kwao. Inaweza kuwa kichocheo kinachowasukuma kwenye njia sahihi.

Jambo bora la kufanya ni kuanza kuomba juu ya utulivu wa kifedha kabla chochote kibaya hakijatokea. Walakini, ikiwa umechelewa sana kuomba ili kuzuia hali mbaya, omba sasa maombi ya ukombozi badala yake. Kumbuka kwamba Mungu anaweza kukomboa kila kitu—hata watoto wetu wazima kutoka katika shida zao za kifedha.

## NGUVU YA MAOMBI

Bwana, ninaomba baraka zako juu ya-------- (jina la mtoto mzima). Ibariki kazi ya mikono yake kwa kila njia. Mpe hisia kali ya kusudi ili yeye aongozwe kwenye kazi inayofaa na daima awe katika kazi au nafasi ambayo ni ya mapenzi Yako kwa ajili ya maisha yake. Mwambie kuhusu yale aliyoumbwa kuyafanya ili kamwe asitange-tange kutoka kazi hadi kazi bila kusudi. Msaidie kupata kusudi kubwa katika kila kazi anayofanya. Na Kumsaidia kuwa na bidii katika kila kitu na kamwe asishindwe na uvivu au tabia ya kutojali. Ambapo kuna aina yoyote ya uvivu au woga unaomshikilia na kumvuta nyuma, naomba kwa ajili ya kuvunjwa kwa ngome hiyo. Mimina Roho Wako Mtakatifu juu yake yake na umpe hekima ya kuinuka kutoka katika udanganyifu huo na kuwa na nguvu ya kutembea bila minyororo hiyo ya kupooza. Msaidie na bidii sawasawa na agizo Lako "msilegee katika bidii, mwe na bidii katika roho mkimtumikia Bwana" (Warumi 12:11).

Ninaomba kwamba yeye daima atafanya kazi yake kwa utukufu Wako sawasawa na (Wakolosai 3:23). Uchunguze moyo wake ikiwa kuna kishawishi chochote cha kufanya chochote kisicho cha maadili, iwe kwa

makusudi au kwa kutojua. Mwongoze mbali na vitendo vya kutiliwa shaka au haramu. Msaidie kujua kila wakati kuwa chochote kinachotokea ni kwa faida yake na kwa vitendo vya kinyume cha sheria au kinyume cha maadili visiruhusiwe kamwe maana itamharibia sifa yake mwishowe. Ninaomba kwamba yeye atajua kwamba sifa nzuri ni ya thamani zaidi kuliko utajiri (Yeremia 17:11).

Wape watoto wangu watu wazima hekima kuhusu mambo yote ya pesa. Wasaidie kuona hatari kabla ya jambo lolote kubwa kutokea. Wape ufahamu kuhusu kutumia, kuweka akiba na kuwekeza kwa busara. Wasaidie wasifanye makosa ya ujinga au uzembe. Walinde ili fedha zao zisipotee, zisiibiwe au kupotezwa. Naomba kwamba adui hataruhusiwa kuiba, kuua, au kuharibu kitu chochote ndani ya maisha yao. Ninawaombea watoto wangu watu wazima kwamba "watende mema, wawe matajiri katika kazi njema wawe tayari kutoa, tayari kushiriki, wakijiwekea msingi mwema kwa wakati ujao, ili wapate uzima wa milele" (1 Timotheo 6:18-19).

Bwana, wasaidie watoto wangu watu wazima kuweka fedha zao Kwako ili kwamba Wewe uwe msimamizi wao. Wasaidie kupata uhuru dhidi ya madeni na kuwa makini na matumizi ili maisha yao ya baadaye yawe salama. Wawezeshe kuwa mawakili wazuri wa yote uliyowapa. Wasaidie wajifunze kukupa kwa njia ya kupendeza machoni pako.

Ambapo mtoto wangu mtu mzima ana matatizo ya kifedha hivi sasa, ninaomba mambo yageuke. Msaidie kujifunza kutokana na marekebisho na maelekezo kwa walimu wenye hekima na watu waenye uzoefu na, hekima

na wakomavu, ili yeye aepuke umaskini na aibu na kupata heshima na ufanisi (Mithali 13:18). Kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, ninazungumza baraka za Mungu za utoaji juu ya….. (jina la mtoto mzima). Mpe hekima kuhusu kazi, biashara, na taaluma. Ninaombea mafanikio katika kazi uliyomwita yeye kuifanya. Fungua milango ya fursa na umsaidie kupata kibali mahali pake  pa kazi na biashara. Msaidie kulipwa mshahara ipasavyo kwa kazi aliyoifanya.

Bwana, umesema “utafuteni ufalme wa Mungu, na haki Yake na hayo yote mtazidishiwa” (Luka 12:31). Wasaidie watoto wangu watu wazima kukutafuta Wewe, na wewe Uwe kipaumbele chao cha kwanza ili waweze kupata utulivu wa kifedha. Wasaidie kujisalimisha Kwako katika mwili, akili, nafsi, na roho ili waweze kuingia katika wingi na mafanikio uliyonayo kwa ajili yao. Naomba uzuri wa Bwana uwe juu yao na kuithibitisha kazi ya mikono yao (Zaburi 90:17). Ninaomba kwamba “wafurahie kazi ya mikono yao muda mrefu” na kwamba “hawatajitaabisha bure” sawa na ahadi yako katika (Isaya 65:22-23 ). Katika Jina la Yesu ninaomba. Amina

**NGUVU YA NENO**

Lo lote mfanyalo, lifanyeni kwa moyo, kama kwa Bwana na si kwa wanadamu.

**WAKOLOSAI 3:23**

Kila mtu anapaswa kula na kunywa na kufurahia mema ya kazi yake yote—ndiyo zawadi ya Mungu.

**MHUBIRI 3:13**

Mkabidhi BWANA kazi zako, na mawazo yako yatathibitika.

**MITHALI 16:3**

Nalikuwa kijana, na sasa ni mzee; lakini sijamwona mwenye haki ameachwa; Wala watoto wake wakiomba mkate.

**ZABURI 37:25**

Msisumbukie kile mtakachokula au kile mtakachokunywa, wala msiwe na wasiwasi Kwa maana hayo yote mataifa ya ulimwengu huyatafuta, lakini Baba yenu anajua kwamba unahitaji vitu hivi. Bali utafuteni ufalme wa Mungu na haki Yake, na hayo yote mtazidishiwa.

**LUKA 12:29-31**

## OMBA ILI WATOTO WAKO WATU WAZIMA WAWE NA AKILI TIMAMU ZENYE HEKIMA NA MTAZAMO MWEMA WA MAMBO.

Hakuna hata mmoja wetu anayejua nini mtu mwingine anafikiria. Pia ni watu wachache sana, akiwapo yoyote, hushiriki kila mawazo yao na mtu mwingine. Hata mume na mke; basi ndiyo ilivyo hata katika uhusiano wa karibu kati ya wazazi na watoto watu wazima. Ukweli ni kwamba, Mungu pekee Ndiye anayejua mawazo yetu yote, hata Shetani hana uwezo huo wa kujua mawazo yetu. Ndio maana Mwenyezi Mungu ndiye wa kumhusisha na kila kinachoendelea katika akili na hisia za mtoto wako mtu mzima.

Baadhi ya mapambano makubwa ambayo wengi wa watoto wetu watu wazima wanapaswa kukabiliana nayo ni yale yanayotokea katika akili zao. adui daima hujaribu kuwapata waamini uongo wake na kukataa Ukweli wa Mungu. Anajua ili mradi tu wataamini uongo wake, atakuwa ameshinda. Sote tunaweza kuwa na mawazo ambayo yanatusumbua na yanakcheza juu ya vichwa vyetu, hata kusababisha maonyesho katika miili yetu, kama vile maumivu, kichefuchefu, magonjwa, au kutoweza kwa miili yetu kufanya kile inachopaswa kufanya.

Mawazo yetu hayawezi tu kutufanya wagonjwa katika mwili wetu, lakini katika akili zetu na hisia pia. Wazo moja tu baya linaweza kutufanya tushindwe na kuanguka kimaisha. Ikiwa tunaamini uongo juu yetu wenyewe badala ya kile Neno la Mungu linasema juu yetu; Kwa mfano, ikiwa tunasema mara kwa mara, “Siku zote mimi huwaga nashindwa katika kila jambo nalojaribu kufanya” badala ya “Naweza kufanya mambo yote kwa njia ya Kristo anitiaye nguvu,” kuna uwezekano mkubwa wa kupata kushindwa.

Tatizo ni kwamba mara nyingi tunaamini uwongo ni Ukweli kwa sababu sisi hatujui kwa wazi juu ya Ukweli wa Mungu ni nini. Na tunasikia sauti ya mayowe ya adui katika akili zetu, ambazo ni kubwa zaidi kuliko sauti tulivu, ndogo ya Mungu kwetu. Biblia inasema juu ya adui kwamba "hakuna Ukweli ndani yake… kwa maana yeye ni mwongo na baba wa uongo" (Yohana 8:44). Kila mtu anahusika na aina hiyo ya mateso ya kiakili, lakini watoto wetu wazima wanapatwa na hali hiyo zaidi. Kwa sababu haikujalisha ni kelele ngapi  za hovyo za kidunia tumezipata wakati wa kukua, ila watoto wetu wana kila aina ya kifaa  elektroniki kinachochukua umakini wao. Baadhi ya vijana wakubwa masikio yao, macho, na akili zao kwa muda mrefu zimeunganishwa katika kitu kingine ambacho hakipatani na Bwana au hakimpi Bwana nafasi. Hata masikio yao daima yana bluetooth.

Chochote kinachovutia macho na masikio yao pia kitateka akili na mioyo yao. Kujiua au ghasia za mauaji ya vijana wote huanza kama mbegu ya uongo iliyopandwa katika akili zao kupitia macho yao au masikio yao, na inaota na kukua kimya kimya katika sehemu za giza la roho zao. Hisia mbaya kama vile hasira, kuumizwa, kukataliwa, woga, wasiwasi, na upweke zote huchochea na kuwalisha uongo ili uweze kukua hadi hali itakapokuwa nje ya udhibiti wao. Mtu anayeamini kuwa amekataliwa atakuwa na maumivu, wasiwasi, hofu, kuudhika na kisha upweke na kutengwa, na hatimaye hasira. Mambo yote haya mabaya ya utu wake yatasababisha watu kumkataa hata zaidi. Na kwa hivyo uwongo unakua hadi unakuwa sio tu wa kujiangamiza mwenyewe bali uharibifu kwa watu

wengine pia.

Watoto wetu watu wazima wanaweza kuwa na uwongo unaocheza akilini mwao ambao unapunguza uwezo wao wa kufikiri kwa uwazi na kwa usahihi kuhusu wao wenyewe na hali zao. Wao wanaweza kuishia kuamini uwongo kama vile:

1. Hakuna anayenipenda.

2. Nimekataliwa na watu ninaotaka wanikubali.

3. Siwezi kufanya chochote sawasawa.

4. Mimi sio mzuri kwa chochote kile.

5. Mimi ni wa kushindwa.

6. Hakuna anayenijali.

7. Haijalishi ninafanya nini.

8. Hakuna ninachoweza kufanya kubadili mambo.

9. Mungu hasikii maombi yangu.

10. Sijui mimi ni nani, wacha niende nikajitafute

11. Sura yangu mbaya, natamani ningekuwa kama fulani

10. Mungu hajali kuhusu mimi.

Wakati watoto wako watu wazima wana mawazo hasi na kuamini uongo

kama ulio hapo juu, mawazo haya yanaweza kuwasukuma kuelekea kwenye kile walichoogopa yaani kushindwa na kukataliwa. Ni lazima tuombe ili macho ya watoto wetu watu wazima yafunguliwe na wapate kuona kwamba mawazo haya hayatoki kwa Mungu bali ni adui anayesemasema uongo kwa nafsi zao na wao wanakubali.

Mawazo haya yanaonekana kutokuwa na madhara mwanzoni, lakini nuru ya kweli ya Mungu katika Neno Lake hufichua uongo jinsi ulivyo. Moja ya mbinu za adui ni kujaribu kuiba ile Kweli wa Mungu kutoka kwa watoto wako watu wazima kwa kuwafanya waihoji Biblia (skepticism). Ataleta migongano katika akili zao kuhusu kutegemeka kwa Neno la Mungu. “Je, kweli Biblia iliongozwa na roho ya Mungu au ni akili za watu tuu. “Je, kweli Mungu anamaanisha hivyo?” Hawatambui kwamba huo ni mvuto wa adui unaowaita kuwa na mashaka na Neno la Mungu. "Kuna njia ambayo inaonekana sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti” (Mithali 14:12). Wanafikiri ndivyo walivyo na wana haki ya kutilia shaka Neno la Mungu. Swali la wazi ni kwamba: Je, wana makusudi gani? Na kwa nani? Mara nyingi mtoto mtumzima huwa wazi kwa adui kuingia akilini mwake badala ya kumruhusu Mungu ndani ya nafsi yake.

## MAMBO AMBAYO NI KWELI KUHUSU AKILI YA MUUMINI

Dhambi zote huanza kama wazo katika akili. “Kutoka ndani, ya moyo wa mtu hutoka mawazo mabaya, uzinzi, uasherati, uuaji, wivi, kutamani, uovu, hila, ufisadi, kijicho, matukano, kiburi; upumbavu” (Marko 7:21-22). Ikiwa

hatutadhibiti akili zetu, Shetani ataziteka na kuziweka chini ya mapenzi yake. Kizazi chetu kitalazimika kufuata dhambi ikiwa tulikuwa na mwelekeo wa kufanya hivyo. Watoto wetu wakubwa wanaitazama dhambi kila siku, na itawalazimu tu kufanya yote wawezayo kuinuka washindi juu ya dhambi. Wanahitaji msaada na uwezeshaji wa Bwana kupitia maombi yetu. Kuombea watoto wako wakubwa kunaweza kutuliza sauti za adui wa nafsi zao na kuwasaidia kutambua vyema na kudhibiti mawazo yao ili kuruhusu katika akili zao mambo yaliyo mema kupata nafasi.

Mambo Matatu Ambayo Ni Kweli Kuhusu Akili ya Muumini

1. Mungu humpa kila mmoja wetu akili timamu.

2. Adui anataka kuharibu akili zetu timamu kwa uongo wake.

3. Tuna chaguo kuhusu kile tunachoruhusu katika akili zetu. Tunaweza kudhibiti tunachofikiri.

## MAMBO MATATU YA MAOMBI KWA AKILI ZA WATOTO WETU WAZIMA

1. Omba kwamba watoto wako watu wazima wasiwe na akili pungufu wa ile anayotoa, maana Yeye Mungu Ndiye Mwenye hekima yote kwa kila mmoja wao.

2. Omba ili adui wa nafsi zao asiweze kujaza akili zao na uongo huo wa kuwakandamiza kiakili na kihisia.

3. Omba kwamba watoto wako watu wazima wafanye maamuzi sahihi kuhusu kile wanachoruhusu katika akili zao.

Hatujaribu kufanya mazoezi ya aina fulani ya udhibiti wa akili hapa. Sisi tunapaswa kupata uzoefu wa kumruhusu Mungu kutawala kila kitu tunachofanya. Kupitia maombi yetu tunataka kuweka kizuizi dhidi ya chochote kinachopinga akili timamu tulizopewa na Mungu.

Ninawajua watoto watu wazima wengi ambao waliamini uwongo mwingi kuwahusu wao. Waliamini kuwa hawakuwa na akili za masomo darasani, hawakuwa na vipaji, au hawakuwa wenye kuvutia. Mabinti wengine walihisi kwamba hakuna mwanamume ambaye angevutiwa nao na kwa sababu hiyo Ikiwa ungekutana naye na kuzungumza naye, ungejua kwamba hakuna chochote kati ya hayo ambacho kilikuwa ni kweli na ungeshangaa hata kusikia kwamba aliamini mambo kama hayo kumhusu yeye mwenyewe.

Hata hivyo, imani hizo zilimfanya asisonge mbele katika maisha yake kwa muda mrefu na kumwondolea tumaini, na kwa hivyo alivunjika moyo, akajitenga, na kutengwa. Alitarajia kushindwa na kukataliwa kwa sababu ilionekana kwake kuwa kila kitu alichofanya kiliishia katika kushindwa. Mama yake alipomwalika katika kikundi cha maombi ya kila juma, walianza kusali kwa ajili yake mara kwa mara juu ya kuvunja udhibiti wa mawazo mabaya ya kushindwa. Waliomba kwamba macho yake yafumbuliwe na aone Ukweli na kujua kwamba uwongo wa adui kwa akili na moyo wake ungefichuliwa na nguvu za adui zingevunjika. Walisali

kwamba awe huru kusikia Ukweli kuhusu yeye mwenyewe kutoka kwa Roho Mtakatifu.

Majibu ya maombi haya hayakutokea mara moja, lakini hatimaye mawazo yote hayo  hasi na kukubali uongo juu yake vilivunjwa na yeye alianza kubadilika. Alikuwa wazi zaidi, mwenye urafiki, na mwenye furaha. Alianza kufikiria kidogo juu yake mwenyewe na zaidi juu ya wengine. Mambo mazuri yalianza kutokea kwake, na milango ilifunguliwa kwa kazi mpya na bora zaidi. Leo ana matumaini kuhusu maisha yake na mustakabali wake, na kufurahi na vile Mungu alimfanya kuwa. Watoto wengi watu wazima ndivyo wanavyokuwa. Na bila msaada wa maombi na kuwa na uwezo wa kutambua uongo, wataendelea kuamini kwamba uongo kutoka adui ni kweli na Ukweli wa Neno la Mungu ni uongo.

Watoto watu wazima ambao wanalelewa kuwa wenye fikra thabiti na wanyoofu bado wanaweza kukandamizwa katika akili na hisia zao na adui. Namjua kijana mwanamume aliyelelewa katika familia yenye nguvu ya Kikristo ambaye alifikiria kujiua kwa sababu msichana ambaye alikuwa akifikiria kwa dhati kufunga naye ndoa alivunja uhusiano wao. Kukataliwa ni jambo gumu kwa mtu yeyote kulipokea hasa kutoka kwa mtu muhimu sana katika maisha yako, lakini adui anaweza kuingiza aina hiyo ya hali na kuingiza mawazo ya kujiangamiza kwa watoto wetu.

Kwa asili hatutaki kujiangamiza wenyewe. Tumejengwa kwa ajili ya kujihifadhi na kupenda kuishi, na wala sio kujiangamiza. Mungu alituumba tukiwa na hamu ya kuendelea kuwa hai. Ni adui anayekuja kupofusha

macho yetu ili tufikiri kwamba hakuna njia nyingine ya kutoka ila kujiua ni njia pekee iliyosalia. Bila shaka, huu ni mfano uliokithiri lakini sio uliokithiri zaidi. Hali mbaya zaidi ni pale watu wanapowaza na kuchukua hatua ya kuua wengine na kisha kujiua. Sisemi kwamba mtoto wako mtu mzima atawahi kuingia katika kundi la wanaoweza kufikiria kujiua kwa sababu yoyote, lakini ninasema kwamba adui wa nafsi ya mtoto wako mkubwa atakuwa kila mara akijaribu kumfikisha katika hatua hiyo. Na ndio maana lazima tuombe kwa ajili ya watoto wetu wazima kuwa huru na ukandamizaji wote wa adui.

## OMBA ILI WAFANYE MAAMUZI SAHIHI KUHUSU NINI WANARUHUSU KINGIE AKILINI MWAO

Sisi sote tuna chaguo kuhusu kile tunachoruhusu katika akili zetu. Omba kwamba mtoto wako mtu mzima ataelewa hilo na kufanya maamuzi sahihi. Tena, sura tano za kwanza za kitabu hiki zitaathiri hili. Mungu akijibu maombi hayo kwa mtoto wako mkubwa na kumwaga Roho Wake juu yao, huwavuta karibu na Yeye na Njia Zake, hufanya Neno Lake kuwa hai mioyoni mwao, huwapa hekima na utambuzi, huwaweka huru kutokana na chochote kinachowazuia kuwa vile Yeye Mungu aliwafanya kuwa, na kuwapa hisia ya kusudi Lake kwa maisha yao, basi wao watakuwa na uwezekano mkubwa wa kufanya maamuzi mazuri kuhusu kile wanachoruhusu katika akili zao. Kwa sababu ya shambulio baya kwenye

akili zao, watoto wetu watu wazima wanahitaji sala zetu ili ziweze kuwatia nguvu. Mtoto mtu mzima ambaye ana akili timamu na asiye na hisia anaweza kukamilisha mambo makubwa katika maisha yake.

## KUONDOA MTAZAMO MBAYA

Mtazamo mbaya ni kitu ambacho watu wanaweza kuwa nacho bila hata kujua. Mtu anaweza kudhani ana mawazo binafsi ya ndani tu, lakini watu wanakasirishwa na mtazamo wao, hata kama hawajui ni nini hasa.

Mtoto mmoja mtu mzima aliniambia kwamba alijitahidi kuwa na mtazamo wa kuchambua mambo kuhusu wengine. Alisema kuwa kutafuta makosa kwa wengine kulimfanya ahisi vizuri zaidi kuhusu mwenyewe. Ilikuwa ni njia ya ulinzi ambayo alijijengea huku akiwahukumu wengine akilini mwake. Ingawa hakuwahi kusema ukosoaji wake, tabia hii ilipenyeza utu wake na kusababisha mgawanyiko kati yake na wengine, ikipunguza marafiki zake. Nilimwambia aombe kila siku na kumuomba Mungu amfungue katika tabia hii na amsaidie ajisikie vizuri zaidi na kuwathamini wengine zaidi. Alipokuwa akiomba, Roho Mtakatifu alimwonyesha jinsi alivyokuwa na kiburi na roho mbaya. Aliona jinsi mtazamo wake haukumpendeza Mungu, na kwamba Yeye Mungu asingebariki roho ya kukosoa. Hatimaye alikombolewa kabisa kutokana na hali hiyo mbaya ya tabia ya kuchambua wengine iliyokuwa ikimuharibu—na tabia yake iliyopita. Watu sasa wanajisikia vizuri wakiwa naye, naye ana aina ya urafiki wa karibu aliotaka kuwa nao siku zote na hakuweza kuudumisha hapo awali.

Mojawapo ya mambo tunayoweza kufanya ili kuwasaidia watoto wetu watu wazima ni kuomba waondokane na mitazamo hasi ili kujiweka huru wao wenyewe. (Kumbuka, nilizungumza juu ya wazazi kupata uhuru katika sura ya 4?) Ikiwa tunaweza kuondoa hasira yetu, wasiwasi, woga, kiburi, au roho ya kuchambua yote hayo huchangia mtazamo mbaya na tunatayarisha njia kwa watoto wetu watu wazima kutambua tabia zao mbaya na kujikomboa nazo pia.

Ikiwa tuko katika utumwa wa aina yoyote wa hisia hasi, watoto wetu wazima wanaweza kuchagua hiyo pia. Tukiachana na mitazamo mibaya, mawazo mabaya, au hisia zisizofaa leo, wanaweza kuwa wafuasi wa hizo hisia mbaya pia. Ukweli kwamba Yesu alikufa na kufufuka tena unatuhakikishia urithi pamoja naye wa yote aliyo nayo Baba Mungu kwa watoto Wake wanaomwamini na kumpokea Yesu kama Mwokozi. Urithi wa milele tunaopokea kutoka kwa Baba wa mbinguni hatimaye ni maisha ya utukufu pamoja Naye milele.

Lakini Yeye pia huturithisha sisi wema Wake, neema, upendo, amani, furaha, na uwezo Wake sasa hivi. Tunarithi Akili yake timamu na uhuru kutoka kwa hisia hasi sisi pamoja na watoto wetu wakubwa ikiwa watafungua mioyo yao na kupokea yote hayo na ikiwa mioyo yao iko wazi kwa mambo ya Mungu na wanatambua yote aliyo nayo kwa ajili yao. Ndiyo maana ni lazima tuwaombee ili wasikie kutoka kwa Mungu na kuwa wazi kwa Roho Wake Mtakatifu kufanya kazi katika maisha yao.

Namjua mama mmoja ambaye alikuwa anaogopa sana kila kitu alipokuwa

analea watoto wake. Binti yake sasa anaogopa kila kitu wakati wa kulea familia yake. Ni jambo moja kuwa na hofu kuhusu jambo baya linalomtokea mtoto wako maana kila mzazi ana hofu hiyo kwa kiwango fulani, lakini hofu inapokudumaza na kudhibiti maisha yako, hukufanya wewe na wengine wanaokuzunguka kuwa duni, mnakuwa na "roho ya hofu." Mama na binti wote ni waumini, lakini hawajawahi kujua uhuru katika Kristo katika eneo hili. Hawaelewi kuwa hofu ni roho ambayo huleta mateso. Hofu inayotawala maisha yako kamwe haitoki kwa Mungu. Kama huyu mama angemuomba Mungu kumweka huru kutoka kwa hofu yote, Angeweza kufanya hivyo. Na hii ingekuwa msaada kwa upande wake kumsaidia binti yake kuamini juu ya uwezo wa ukombozi wa Mungu kumweka huru kutokana na hofu pia.

Ni lazima tumwombe Mungu atuweke sisi na watoto wetu watu wazima kutoka kwa uovu wowote mitazamo hasi, na atusaidie kuona maisha yetu kwa mtazamo Wake.

## HISIA TANO HASI NA MITAZAMO MBAYA YA KUEPUKA

i. Omba kwamba mtoto wako mtu mzima asiwe na kiburi. "Kiburi cha mtu kitamshusha, lakini mwenye roho ya unyenyekevu atabaki na heshima" (Mithali 29:23). Kiburi kila mtu anacho, ila inabidi tumwombe Mungu akitokea kwani kina matokeo yaliyojengeka na kitamshusha mtoto wako mtu mzima haraka kuliko kitu chochote kingine. Shetani alishushwa na kiburi, na ndivyo atakavyokuwa kila mtu mwingine aliyenacho. Hiyo ni

kwa sababu Mungu anachukia kiburi. Yeye huwapinga wenye kiburi na huwapa neema wanyenyekevu (Yakobo 4:6). Omba kwamba kiburi kisiwatawale watoto wako wakubwa na kuharibu maisha yao.

ii. Omba ili mtoto wako mtu mzima asiwe na woga.

## SIFA HUPONYA AKILI, HISIA, NA MITAZAMO

Moja ya mambo yenye nguvu zaidi tunaweza kufanya katika maisha yetu ili kuondokana na hisia hasi, misukosuko katika akili zetu, na mitazamo mibaya ni kumuabudu na kumsifu Mungu. Haijalishi nini kinatokea katika maisha yetu, au katika maisha ya watoto wetu wakubwa, Mungu anastahili sifa zetu daima. Kumsifu kunakaribisha uwepo wake kutawala katikati yetu. Na mabadiliko hupatikana katika uwepo wa Mungu.

Ni muhimu kukumbuka mambo mazuri ambayo Mungu amefanya katika maisha yetu na tuwakumbushe watoto wetu wakubwa mambo hayo pia. Hiyo itawasaidia kuunganishwa na wema wa Mungu na huo ukae juu yake. Katika kitabu cha Esta imeandikwa kwamba Wayahudi waliamua kwamba wangekumbuka mara kwa mara na kusherehekea jinsi wao walivyowashinda adui zao, "ili sikukuu hizi zikumbukwe na kushikwa katika kila kizazi, kila familia ... na kwamba kumbukumbu yao inapaswa iwasaidie wasiangamie miongoni mwa adui zao" (Esta 9:28).

Sisi wazazi wenye watoto ambao wameshakuwa watu wazima tunahitaji kufanya vivyo hivyo. Ni lazima tutoe shukrani na sifa kwa Mungu kwa uwazi kwa ajili ya mambo makuu aliyofanya katika maisha yetu. "Kizazi

kimoja kitasifu Matendo Yako kwa mwingine, na kuyatangaza matendo Yako makuu” (Zaburi 145:4). Tuna haja ya kuwaambia jinsi Mungu alivyotuweka huru kutoka kwa adui wa roho na akili zetu, na jinsi anavyoweza kuwafanyia vivyo hivyo.

Zaidi ya hayo, ni vizuri kuwaambia watoto wako kuhusu matokeo ya dhambi katika maisha ya watu unapoiona ikitokea duniani. Kama vile Mungu alivyosema kupitia Yoeli akisema, “Waambie watoto wako kuhusu hilo, watoto nao watawaambia watoto wao, na watoto wao watawaambia kizazi kingine” (Yoeli 1:3).

Wanahitaji kujua kwamba dhambi hufungua mlango kwa mashambulizi ya adui. Lakini wakumbushe juu ya ahadi za Mungu katika Neno Lake ili liturudishe kutoka katika dhambi ili tuweze kupata uponyaji na urejesho. Zungumza Neno la Mungu kwa watoto wako wakubwa wakati wowote unaoweza. Ikiwa wana wasiwasi, waambie kwamba hakuna silaha itakayoundwa dhidi yao itakayofanikiwa wanapoishi njia ya Mungu (Isaya 54:17).

Huenda huna tena mamlaka juu ya watoto wako, lakini unayo mamlaka juu ya nguvu zote za adui. Mawazo hasi, hisia, na mitazamo inaweza kuwa hila ya adui kumwangamiza mtu kwa kusababisha mateso ya kiakili na nafsi. Na mtu anaweza kumkaribisha adui kwa makusudi katika uasi wake wenyewe na uasi wao huanza kama tabia mbaya ambayo hairekebishwi. Dhambi inapokuwa na mazoea zaidi na zaidi, huweka mizizi na njia ya kuondoa ni kuomba kwa bidii. Biblia inasema kwamba uasi ni kama "dhambi ya

uchawi" (1 Samweli 15:23). Uasi ni njia binafsi ya kuelekea kwenye uharibifu. Mtazamo sahihi hauna uasi wowote unaohusishwa nayo. Hivyo omba mtoto wako mtu mzima apinge tabia ya uasi na badala yake kuwa na roho ya sifa na ibada.

Kumbuka kwamba Mungu ndani yetu ni mkuu sana kuliko adui na mipango yake. “Ninyi, watoto wadogo, mwatokana na Mungu nanyi mmemshinda, kwa sababu Yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia” (1 Yohana 4:4). Sisi ni lazima daima kuwakumbusha watoto wetu watu wazima kuhusu hilo, na kuomba kwamba Ukweli huu upate mizizi ndani ya mioyo yao. Wakumbushe kwamba kwa sababu sisi ni waamini, “tuna nia/akili ya Kristo” (1 Wakorintho 2:16). Omba kwamba watatulia Zaidi kwa Kristo.

## NGUVU YA MAOMBI

Bwana, ninaomba kwamba umchukue……. (jina la mtoto mzima) kudhibiti akili na hisia zake. Mwezeshe (yeye) kuleta kila wazo lake katika mapenzi Yako (2 Wakorintho 10:5). Msaidie asiburudishe wazo lolote linalokuja kichwani mwake, lakini awe na utambuzi wa kutambua sauti ya adui ikisema uongo. Ondoa udanganyifu wote ili yeye asikubali uongo kwa kuukataa Ukweli. Msaidie kumtambua wazi adui wa udanganyifu anayekuja kwa lengo la kumwangamiza. Mpe uwezo wa kukataa kujaza akili yake na chochote kile kisichokutukuza Wewe. Msaidie achukizwe na uovu usiojenga ikiwemo vitabu, majarida, muziki, filamu, na picha za mtandao na televisheni ili aweze daima kujiepusha na mambo hayo. Msaidie badala

yake kujaza akili yake na mawazo yanayokupendeza. Msaidie kufikiria juu ya mambo ambayo ni Kweli, matakatifu, yenye haki, safi, mwenye kupendeza, mema, yenye sifa njema (Wafilipi 4:8). Msaidie aijaze akili yake na "yale yaliyo bora zaidi, na sio mabaya zaidi; mazuri na sio mabaya; mambo ya kusifiwa, si ya kulaaniwa" (Wafilipi 4:8). Ninamuombea mtoto wangu aweze kupinga jaribio lolote la adui kujaribu kutesa akili yake kwa mawazo na hisia hasi. Msaidie kuchagua upendo, nguvu, na akili timamu uliyompa. Futa giza la hisia hasi ambazo linaelea juu yake. Mweke Mwanangu huru kutoka kwa machafuko yote na kuleta uwazi wa akili. Nia ya Kristo iwe ndani yake (Wafilipi 2:5). Msaidie kufanywa upya katika roho na akili (Waefeso 4:23). Ondoa kiburi chote na ulete unyenyekevu ndani yake. Ondoa uasi na kuleta toba. Ondoa wasiwasi wote na kuleta amani. Mpe Imani na uondoe mashaka yote. Mpatie furaha Yako pale ambapo kuna huzuni. Bwana ruhusu amani, subira, na msamaha kuchukua nafasi ya hasira yote. Mpe Upendo wako wa kufuta hofu yote. Naomba uwepo wako umwondolee upweke wote.

Ninaomba kwamba umpatie hekima kuhusu kile anachoruhusu kuingia katika akili yake. Mpatie utambuzi mkubwa ili aweke mpaka kati ya mema na mabaya yanaonekane wazi. Mfanye ajisikie kuwa na hatia wakati wowote anapovuka mstari, na ihuzunishe roho yake jinsi anavyomhuzunisha Roho Wako. Ninaombea akili yake itekwe na Wewe. Popote ambapo akili na hisia zake zimetekwa na chochote kisichokuwa Chako, naomba umwezeshe kunyamazisha sauti ya adui kwa kusema Ukweli Wako. Mfundishe kuinua sifa na kukuabudu mpaka aisikie sauti

yako ikizungumza na nafsi yake waziwazi.

Iwapo mtoto wangu mtu mzima amedhihakiwa, amedhalilishwa, au amefanywa ajisikie mdhaifu kuliko vile ulivyomfanya kuwa, ninaomba kwamba uponye majeraha hayo na kufuta makovu. Mzuie asifungwe au kuzuiwa na kumbukumbu mbaya. Ikiwa nimesema au nimefanya chochote ili kumfanya mtoto wangu mtu mzima ajisikie mnyonge kuliko ulivyomfanya kuwa, na hili limemzuia asiendelee mbele katika maisha, ninaomba msamaha wako. Nisaidie nijisamehe na kuwawezesha watoto wangu wanisamehe pia.

Ikiwa nimekuwa na hisia hasi ambazo zimesababisha mwanangu aweze kuathiriwa na kitu chochote, naomba sote tuwe huru kutokana na hilo. Najua kwamba "mauti na uzima huwa katika uwezo wa ulimi" kama unavyosema katika (Mithali 18:21). Kwa hivyo ninaomba kwamba ungenisaidia daima kuzungumza maneno ya uzima kwa mtoto wangu mtu mzima ili akili na moyo wa mtoto viwe na usikivu kila ninapozungumza naye. Niwezeshe kumjenga juu na kuonyesha upendo kwa njia ambayo anaweza kutambua. Nisaidie kumkumbusha mema yote ambayo Mungu amefanya katika maisha yake.

Bwana, mvute mtoto wangu mtu mzima kwa Neno lako ili liwe "Uwe kiongozi wa mawazo na makusudi ya moyo wake" kila mara anapoisoma (Waebrania 4:12) mwoneshe mawazo au imani yoyote mbaya na ufanye mawazo Yako yawe yake. Msaidie kuwa na "nia ya Kristo" kila wakati (1Wakorintho 2:16).

Pale ambapo watoto wangu watu wazima bado wanapambana na hawajashinda katika akili au hisia zao, ninaomba uwaweke amani kama maji ya mto (Isaya 66:12). Kwa mtoto wangu mtu mzima ninaomba kwamba "amani ya Mungu, ipitayo akili zote, ilinde mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu" (Wafilipi 4:7). "Wacha amani yako itawale mioyoni mwao…… na wawe ni watu wa shukrani" (Wakolosai 3:15). Katika Jina la Yesu ninaomba. Amen.

**NGUVU YA NENO**

Wala msiifuatishe namna ya dunia hii, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nafsi zenu Na nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.

**WARUMI 12:2**

Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu.

**WAFILIPI 2:5**

Basi nasema haya, tena nashuhudia katika Bwana, kwamba msienende tena kama vile watu wa mataifa mengine wanavyoenenda katika ubatili wa nia zao, wakiwa na mawazo yao ufahamu umetiwa giza, na kutengwa na uzima wa Mungu, kwa sababu ya ujinga uliomo ndani yao, kwa sababu ya upofu wa mioyo yao.

**WAEFESO 4:17-18**

Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekaa katika amani kamilifu, kwa sababu yeye anakutumaini Wewe.

**ISAYA 26:3**

Msijisumbue kwa neno lolote, bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu; na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu.

**WAFILIPI 4:6-7**

## OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE KUZUIA USHAWISHI MWOVU NA TABIA ZENYE KUHARIBU.

Yeyote anayepitia utamaduni huu nyakati hizi atapambana ushawishi mbaya. Isipokuwa wao ni watu waliotengwa kabisa, haiwezekani kuishi bila majaribu. Ikiwa watoto wetu watu wazima si waangalifu kwa makusudi na huku wanafahamu, akili na mioyo yao inaweza kupakua virusi vya kijamii

na kiroho ambavyo vinaweza kuharibu maisha yao kabla hata ya wao kujua kinachoendelea.

Ushawishi mbaya unapowashinda watoto wetu watu wazima, wanaweza kunaswa na tabia mbaya kutoka kwa vitu kama vile pombe, dawa za kulevya, ulaji, machafuko, uasherati, ponografia, na mengine mengi yanayoweza kuharibu maisha yao. Ukweli ni kwamba watoto wabaya kutoka kwa familia zisizo na malezi mema wamefanya mambo mabaya na kuingia kwenye shida nzito. Vilevile kuna watoto wazuri kutoka kwa familia nzuri ambao wanashawishiwa kufanya mambo ya kutisha na ya uharibifu.

Haijalishi umekuwa mzazi mzuri kiasi gani, watoto wako watu wazima bado wanaweza kuathiriwa na upande wa giza wa tamaduni za leo. Ni lazima kukumbuka kwamba mchoro wenye sumaku na wa nguvu mbaya za ulimwengu huu unaonyesha mara kwa mara kuna vita kwa ajili ya watoto wetu. Inabidi tuendelee kuomba ili wawe na nguvu za kutosha kupinga uvamizi huu usiokoma wa adui katika maisha yao.

Mapema katika kitabu hiki nilizungumza juu ya mstari wa Maandiko wenye nguvu unaosema watoto wetu wote watafundishwa na Bwana (Isaya 54:13). Aya chache baadaye zinasema kuhusu sisi tunaoamini kwamba "silaha itakayofanyika juu yako haitafanikiwa…Huu ndio urithi wa watumishi wa BWANA, na haki yao hutoka Kwangu, asema BWANA" (Isaya 54:17). Hii ni ahadi ya thamani sana kurudia ili tusisahau. Tunarithi haki yetu kutoka kwa Bwana. Yeye Ndiye haki yetu. Na kwamba uadilifu hupambana na

mvuto mbaya daima.

Walakini, haki haiwezi kutokea tu bila maombi. Inatubidi kwanza tuombe ili kumpokea Yesu na haki Yake. Kisha tunapaswa kuomba ili kupokea yote Mungu aliyonayo kwa ajili yetu. Sisi hatuombi ili kupata kitu; bali tunaomba kupokea kitu. Bila maombi ambayo ni kuwasiliana na Mungu, mambo haya hayatokei tu. Hatuwezi kufikiri kwamba hakuna silaha itakayoundwa dhidi yetu itakayofanikiwa bila kuamini kwamba itakuwa. Ahadi za Mungu hazitokei moja kwa moja bila sisi kufanya sehemu yetu. Kama hatuombi, adui anasubiri kutushambulia na kutuharibu.

Yesu alijua kwamba Shetani alikuwa akimshambulia Simoni Petro, na hivyo alimwombea Petro kuwa na imani ya kustahimili. “Simoni, Simoni! Hakika Shetani amewataka ninyi, ili awapepete kama ngano. Lakini nimekuombea, ili imani yako isitindike” (Luka 22:31-32). Yesu angeweza kusema, “Shetani, potea,” na Yeye alitambua jambo hilo kuwa na imani na kuwa na uwezo wa kupinga ilikuwa sehemu ya jukumu la Petro. Iwapo Yesu ilimbidi kuomba kwamba walio Wake wasitindikiwe na Imani hata kushindwa katikati ya shambulio la Shetani, ni kiasi gani zaidi sisi tunahitaji kuomba kwamba imani ya watoto wetu wazima isishindwe wanapokuwa wanajaribiwa? Adui anapokuja kuwajaribu mbali na kile ambacho Mungu anataka wao, tunaweza kuomba kwamba wawe na imani yenye nguvu katika Mungu na nguvu Zake juu yao kwa niaba yao.

Yesu aliwaagiza wanafunzi Wake “Kesheni mwombe ili msiingie katika majaribu” (Luka 22:40). Ni lazima tuwafundishe watoto wetu watu watu

wazima vivyo hivyo. Tunapaswa kumkemea adui kwa niaba yao kwa Jina la Yesu, lakini lazima pia kuwa na imani thabiti ya kuomba na kupinga majaribu na chochote kile ambacho adui huwarushia watoto wetu.

Ushawishi mbaya unaweza kumkabili hata muumini aliyejitoa kabisa kwa Yesu. Yesu aliomba ili wanafunzi Wake walindwe dhidi ya adui. Akamwambia Baba Yake wa mbinguni, “Siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu, bali uwalinde na yule mwovu” (Yohana 17:15). Wanafunzi walikuwa wametembea pamoja na Yesu kwa muda wa miaka mitatu na kuona miujiza Yake na kusikia mahubiri Yake na mafundisho Yake kutoka kwa Neno la Mungu kuhusu ufalme wa Baba, na bado walihitaji kuombewa ili kulindwa na adui.

"Ingawa Yesu alikuwa amewatayarisha wanafunzi Wake, Yeye bado aliomba, “Uwalinde na yule mwovu.” Sisi wazazi hatupaswi kufanya kidogo. Sisi lazima tuwaombee wana wetu, “Bwana, walinde watoto wangu na yule mwovu.”

## WAKATI SIO KOSA LAO

Wakati uovu unapenya maisha ya mtoto wako mtu mzima na mambo mabaya kutokea lakini hakuna makosa katika njia zao, kwa sababu wamekuwa wakiishi njia ya Bwana, unaweza kutumaini kwamba Mungu atawabariki katika hilo. Kisa cha Yusufu ni mfano kamili wa mazingira hayo. Kisa chake chaonyesha maovu yanayokutokea ni mabaya kama inavyokuwa, lakini Mungu Yupo kukomboa hali yake. Kwa sababu ya wivu na uovu katika mioyo ya ndugu zake, walimuuza Yusufu utumwani na

akapelekwa Misri. Lakini pamoja na kwamba Yusufu alikuwa mcha Mungu na mwaminifu, Mungu aliruhusu mabaya yote yaliyomjia. Jambo muhimu zaidi ya hilo ni ukweli kwamba Bwana alikuwa pamoja na Yusufu. Wengine waliona hivyo na kumtuza. "BWANA alikuwa pamoja na Yusufu… na bwana wake akaona ya kuwa BWANA alikuwa pamoja naye na kwamba BWANA alifanikisha yote aliyoyafanya mkononi mwake. Hivyo Yusufu akapata kibali machoni pake, akamtumikia. Kisha akamweka kuwa msimamizi wa yumba yake, na vyote alivyokuwa navyo akaviweka chini ya mamlaka yake" (Mwanzo 39:2-4). Tangu wakati huo na kuendelea, "BWANA akaibariki nyumba ya yule Mmisri kwa ajili ya Yusufu; na baraka za BWANA zikawa juu ya vyote alivyokuwa navyo nyumbani na shambani" (Mwanzo 39:5).

Lakini tena, Yusufu aliteswa kwa sababu ya uovu na dhambi ya mtu mwingine. Mke wa bwana wa Yusufu alijaribu kumtongoza, lakini alishinda jambo kwa kuepuka dhambi na kukataa kufanya jambo kutenda lolote baya machoni pa Mungu. Kisha yule mwanamke alidanganya na kumshtaki akijaribu kumdhalilisha, naye akatupwa gerezani (Mwanzo 39:11-20). Bado ndani ya gereza "BWANA alikuwa pamoja na Yusufu, akamrehemu, naye akampa kibali machoni pa mkuu wa gereza…kwa sababu BWANA alikuwa pamoja naye; na kila alilofanya, BWANA alilifanikisha" (Mwanzo 39:21, 23).

Kila uovu ulipomjia Yusufu, alikataa kuasi sheria za Mungu, na hivyo Bwana alikuwa pamoja naye katika kila jambo alilofanya. Mungu

hakugeuza tu mambo bali alimzunguka Yusufu, na hatimaye alimpandisha cheo hadi kuwa kiongozi wa pili katika utawala wa Misri yote. Aliishia kuwasamehe kabisa ndugu zake na kuwahifadhi familia yake kutokana na maafa. Aliwaambia akina ndugu ambao walikuwa wametubu sana kwa ajili ya dhambi waliyofanya "Mlikusudia mabaya juu yangu; lakini Mungu alikusudia kwa wema" (Mwanzo 50:20). Haikuwa mapenzi ya Mungu kuona Yusufu akiwekwa utumwani, kushtakiwa kwa uwongo, na kufungwa, lakini Mungu alitenda kazi kupitia hali hiyo ili kumfanikisha na hatimaye kumweka katika nafasi ya kufanya jambo ambalo kwa ajili yake aliumbwa.

Ikiwa mtoto wako mkubwa anavumilia adhabu isiyostahiliwa au ugumu wa aina fulani kwa sababu ya uovu au dhambi ya wengine, omba kwamba yeye asigeukena  kumuacha Bwana lakini badala yake atamkaribia zaidi Mungu na kumsifu katika kila hali. Omba ili asimame imara katika njia za Bwana, ili Mungu amfanikishe na kumbariki. Mungu anafanya kazi kwa nguvu katikati ya moyo mtiifu na wenye shukrani kugeuza mambo na kufanya muujiza. Mwombe Mungu ashughulikie hali ngumu ya mtoto wako mtu mzima na atumie uovu unaofanywa dhidi yake kwa wema- Mwanzo 50:20.

Zaidi ya yote, mwombee mtoto wako mtu mzima afanye yaliyo sawa kila wakati bila kujali jinsi maisha yanaonekana kuwa yasiyo ya haki. Ikiwa mtoto wako mkubwa analipa gharama ya juu sana sasa kwa kosa la mtu mwingine au dhambi na uovu wa mtu mwingine, fahamu kwamba katika Biblia watu wa Mungu "walipata neema nyikani" (Yeremia 31:2). Omba kwamba mtoto wako mtu mzima hataishi tu kutokana na matokeo ya

ukosefu wa haki, lakini wakati anapitia hayo yeye pia atapata neema ya Mungu hata katika hali mbaya ya maisha ambayo inaonekana kuwa tasa.

Yesu hakuwa na hatia, na aliomba ili asipitie mazito yaliyo mbele Yake. Lakini pia alisali kwamba mapenzi ya Mungu yatimizwe wala si Yake Mwenyewe (Luka 22:42). Alipokabidhi mapenzi Yake kwa Baba Yake wa mbinguni, "ndipo malaika kutoka mbinguni akamtokea, akamtia nguvu" (Luka 22:43). Nguvu ilikuja kutoka mbinguni ili kumpitisha katika yale Aliyokabiliana nayo. Mwambie Mungu atume nguvu kutoka mbinguni ili kumsaidia mtoto wako mtu mzima kushinda kile anachokabiliana nacho.

## WAKATI NI KOSA LAO

Ikiwa mtoto wako mtu mzima atalazimika kukabiliana na matokeo magumu ya kutokupinga ushawishi mbaya na tabia ya uharibifu, omba kwamba yeye ajifunze somo kupitia uzoefu huo bila kuharibiwa. Omba kwamba bila kujali ni nini atakabiliana nacho kama matokeo ya matendo yake, kwamba Mungu atamtia nguvu ili apitie hali hii huku akijifunza na kuimarishwa. Omba kwamba yeye atubu na kujisalimisha kwa mapenzi ya Mungu kabisa. Mungu huwapa thawabu wenye moyo mnyenyekevu, uliotubu, mtiifu, tegemezi. Haijalishi nini kitatokea, mtoto wako mtu mzima ana wakati ujao wenye kusudi ambao unastahili kuuombea kwa bidii sasa.

Mtoto wa kwanza wa Adamu na Hawa alikuwa Kaini na wa pili alikuwa Habili. Mungu hakufurahishwa na kile Kaini alimtolea kama dhabihu kwa sababu ilikuwa ni tendo la wazi la kutotii. Kaini alikasirika kwa ajili ya jambo hilo, lakini Mungu akamwambia, "Kwa nini una hasira? Ukifanya

lililo sawa, utapata kibali Kwangu. Lakini ikiwa hutafanya jambo sahihi, dhambi inakuotea mlangoni ikuangamize. Lakini unapaswa kuishinda." (Mwanzo 4:6-7).

Mungu alimpa Kaini chaguo. Angeweza kuchagua kufanya jambo lililo sawa na kutawala dhambi, na hivyo kumpendeza Mungu. Au angeweza kuchagua kutofanya jambo sahihi na kuruhusu wivu wake mwenyewe (dhambi), hasira (dhambi), na kisasi (dhambi) kutawala juu yake. Yeye akamchagua yule wa pili, naye akamuua Abeli ndugu yake kwa hasira ya wivu. Wakati Mungu aliuliza Kaini nini kilimpata kaka yake, Kaini alidanganya na kusema hajui. Kumdanganya Mungu sio wazo zuri, ni dhambi. Hasa kwa vile Yeye anajua ukweli tayari.

Kitu pekee ambacho Mungu anataka kujua anapouliza swali ni jinsi unavyochagua kujibu. Inasikitisha sana kwamba Kaini hakujua hilo. Baada ya Kaini kusema uwongo, Mungu alimwambia tangu wakati huo na kuendelea atalaaniwa kama na kuwa mkimbizi. Lakini hata hivyo Mungu kwa rehema Zake asingeruhusu mtu yeyote kumuangamiza Kaini. Badala yake, Mungu alimruhusu Kaini, mtoto mtu mzima aliyemuua ndugu yake mwenyewe, bado aendelee kuwa na familia yenye watoto na wajukuu na vitukuu. Mungu alimwadhibu, lakini hakumkataa Kaini kabisa.

Bado kulikuwa na baraka nyingi katika maisha yake, hata baada ya dhambi yake mbaya. Hatuwezi kuwaacha watoto wetu watu wazima pia, bila kujali wamefanya nini. Hakika si lazima kusamehe au kutoa udhuru kwa matendo yao, bila shaka kwa kufanya hivyo itawawezesha wadumu katika dhambi

zao, au itawafunika macho wasione kama dhambi yao ina madhara yoyote. Lakini tusikate tamaa kuwaombea. Lazima tuendelee kuamini katika uwezo ambao Mungu ameweka ndani yao, hata kama hatuwezi kuuona kwa sasa.

Omba kwa ajili ya roho ya unyenyekevu, toba, na inayofundishika katika mtoto wako mtu mzima. Mfalme Daudi alifanya makosa mengi sana. Alifanya uzinzi na kuua. Alidanganya na kufanya makosa mabaya sana katika maamuzi. Na hakuweza kusimamia nyumba yake mwenyewe na watoto. Hata hivyo, Mungu alisema kumhusu Daudi kwamba alikuwa “mtu aliyeufurahisha moyo wangu, atakayefanya mapenzi yangu yote” (Matendo 13:22). Kwa wazi, “BWANA huutazama moyo” (1 Samweli 16:7).

Haikuwa kweli kwamba Daudi hakuwahi kufanya jambo lolote baya au hakuwahi kukosea. Ni kwamba alikuwa mwepesi kujinyenyekeza mbele za Mungu na kutubu. Na kwa sababu yeye alikuwa na roho ya kufundishika, alijifunza kutokana na makosa yake yote na uamuzi mbaya, naye akabadili njia zake. Alilipa gharama kwa kila dhambi, na bado hakukataa marekebisho ya Bwana. “Mwanangu, usidharau kuadhibiwa na BWANA; wala usichukie kurudiwa Kwake; kwa maana BWANA ampendaye humrudi kama baba mwana ambaye amependezwa Naye” (Mithali 3:11-12).

Visa hivi vinathibitisha kwamba upendo na neema ya Mungu iko kwa watoto wetu watu wazima bila kujali wamefanya nini, ili kuleta ukombozi na urejesho. Na hivyo ndivyo tunavyopaswa kuomba kwa ajili ya moyo uliotubu na mabadiliko katika maisha ya watoto wetu wakubwa. Na tunapaswa kumshukuru Mungu kwa neema Yake, ambayo hutupatia sisi

zaidi ya tunavyostahili na hatuadhibu kadri ya tunavyostahili.

## NJIA SABA ZA KUMWOMBEA MTOTO WAKO MKUBWA ILI KUPINGA ATHARI ZA UOVU

1. Omba kwamba Mungu afungue macho ya mtoto wako mtu mzima kuona Ukweli na sio kupofushwa na adui. "Hata kama injili yetu imefunikwa kwa wale wanaoangamia, ambao mungu wa dunia hii amezipofusha akili zao, wasioamini, isije nuru ya Injili ya utukufu wa Kristo, ambaye ni mfano wa Mungu, basi kwa watoto wetu wakubwa utukufu wa Mungu uangaze juu yao" (2 Wakorintho 4:3-4).

2. Omba ili mtoto wako mtu mzima aweze kusikia sauti ya Mungu ikimuongoza. "Masikio yako yatasikia neno nyuma yenu, likisema, Njia ni hii, ifuateni; wakati wowote ugeukapo kwenda mkono wa kuume au unapogeuka kwenda mkono wa kushoto" (Isaya 30:21).

3. Omba kwamba moyo wa mtoto wako mkubwa ujazwe na hekima na maarifa. "Hekima inapoingia moyoni mwako, na ujuzi utapendeza kwa nafsi yako, busara itakuhifadhi; ufahamu utakuweka, ili kukuokoa na njia ya uovu" (Mithali 2:10-12).

4. Omba ili mtoto wako mtu mzima aache maovu. "Huenda ikawa kwamba nyumba ya Yuda itasikia mabaya yote ninayokusudia kuleta juu yao, ili kila mtu aghairi njia yake mbaya, ili nipate kuwasamehe wao uovu na dhambi yao" (Yeremia 36:3).

5. Omba ili mtoto wako mtu mzima aelewe kwamba yeye yuko katika vita ya

kiroho. “Kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama, bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili enzi, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho” (Waefeso 6:12).

6. Omba kwamba majaribu ya mtoto wako mtu mzima yatamgeuza amwelekee Mungu. “Nimechoka kwa kuugua kwangu; usiku kucha nakiogelea kitanda changu; Ninalowesha kitanda changu kwa machozi yangu. Jicho langu linachoka kwa huzuni; ninazeeka kwa sababu ya adui zangu wote. Ondokeni kwangu, ninyi nyote watenda maovu; kwa maana BWANA ameisikia sauti ya kilio changu. BWANA amesikia dua yangu; BWANA atayapokea maombi yangu” (Zaburi 6:6-9).

7. Omba ili mtoto wako mtu mzima ajifunze kumsifu Mungu kwa uponyaji na ukombozi alionao kwa ajili yake. “Alituma Neno Lake akawaponya, na kuwaokoa na maangamizo yao. Loo, kwamba wanadamu wangetoa shukrani kwa BWANA kwa ajili ya fadhili Zake, na kwa ajili ya matendo yake ya ajabu kwa ajili ya watoto wao! Na watoe dhabihu za shukrani, na yahubirini matendo Yake kwa furaha” (Zaburi 107:20-22).

## IKIWA UNAHISI KUWA UNASHINDWA VITA

Ikiwa una watoto watu wazima ambao wamekamatwa na ushawishi mbaya na tabia ya uharibifu, na wanaendelea kurudia tena ndani yake mara tu wanapowekwa huru, usikate tamaa na kuacha kuomba. Mara kwa mara Biblia inazungumza kuhusu jinsi Mungu aliwaokoa watu Wake kutoka kwa adui. Mungu anaweza kutukomboa na anaahidi kuendelea kutufungua, na hiyo inajumuisha watoto wako watu wazima. Mtume Paulo alisema,

“Tulikuwa na hukumu ya kifo ndani yetu wenyewe, ili tusijitumainie nafsi zetu sisi wenyewe bali katika Mungu ambaye huwafufua wafu, ambaye alituokoa kutoka kwa mauti kuu namna hii tena atatuokoa, ambaye tunamtumaini, ninyi mkisaidiana pia katika maombi kwa ajili yetu” (2 Wakorintho 1:9-11).

Mungu hatasimamisha mchakato wa ukombozi na urejesho mradi sisi na watoto wetu watu wazima tuko tayari kuendelea kuomba. Wakati mwingine inaweza kuonekana kuwa unapoomba zaidi, ndivyo hali inavyozidi kuwa mbaya. Lakini wewe usirudi nyuma. Ikiwa adui ameinua kiwango, wewe unahitaji kuongeza bidii. Mara nyingi vita huwa vikali kadiri unavyokaribia ushindi. Kama vile mama anavyosahau kuhusu uchungu wa kuzaa mara tu anapomwona mtoto mchanga, unapokaribia kuzaa ushindi lazima upitie maumivu zaidi na endelea kuomba hadi uone kuzaliwa kwa maombi yaliyojibiwa. “Kilio kinaweza kukaa usiku kucha, lakini asubuhi furaha inakuja” (Zaburi 30:5). Fikiria juu ya furaha ya mafanikio ambayo iko mbele.

Mungu hataki ukate tamaa, bali uwe mfungwa wa matumaini. Badala ya kufungwa na huzuni, woga, kukosa tumaini, au hofu, weka tumaini katika Bwana lisha imani yako. Amua kutembea kwa imani na si kwa kuona. Chukua maono uliyonayo moyoni mwako kwa ajili ya mtoto wako mtu mzima na kutangaza kwamba ushindi unaouona kwake, umekwisha patikana kwa Jina la Yesu.

Omba ili Mungu ajidhihirishe kwa watoto wako watu wazima. Ingawa Yeye

hatakiuka mapenzi yao, unapowaombea nguvu ya Mungu inaalikwa kupenya maisha yao. Mungu ana njia zisizohesabika ambazo kwazo anaweza kupenya mioyo ili wawe wazi zaidi kwa ushawishi Wake. Zaidi ya yote, usiruhusu adui akufanye uhisi kuwa hustahili kufanya maombezi yenye nguvu kwa watoto wako watu wazima kwa sababu ya makosa waliyofanya huko nyuma.

Chochote ulichopuuza kufanya au haukuweza kufanya kwa ajili yake, udhaifu wa kibinadamu, kutoweza, mapungufu, au mizigo nzito wakati wa kulea watoto wako kuna ahadi kwamba Mungu atafidia zaidi udhaifu huo kwa mtiririko wa Roho Wake wa neema na nguvu vikiingia katika maisha yao. Unayo mamlaka ya kumwita Mkombozi kwa niaba ya watoto wako watu wazima ili waweze kupata ukombozi wanaohitaji.

Kumbuka kwamba “mambo yote hufanya kazi pamoja kwa wema kwa wale wanaompenda Mungu, ili kuwapatia mema wale walioitwa kwa kusudi lake” (Warumi 8:28). Kumbuka pia kwamba aya za kabla ya hii zinazungumzia kuhusu maombi. Mambo hufanya kazi pamoja kwa wema ikiwa tunaomba. Usisahau kwamba “katika mambo haya yote sisi ni zaidi ya washindi katika Yeye aliyetupenda” (Warumi 8:37). Mungu anatafuta watu wanaompenda ili aweze kuwaokoa. “Macho ya BWANA hukimbia-kimbia duniani mwote, ili ajionyeshe Mwenye nguvu kwa ajili ya wale waliokamilika moyo kuelekea Kwake.” (2 Mambo ya Nyakati 16:9). Mwambie Bwana ajionyeshe mwenye nguvu kwa niaba yako na mtoto wako mkubwa leo.

## OMBA ILI MUNGU AANGAMIZE ROHO YOYOTE YA UASI

Watoto wengi watu wazima wanateseka kwa sababu wazazi wao walishindwa kuwafundisha na kuwaonyesha kwamba kuna madhara makubwa kwa matendo mabaya. Sisi tunapaswa kuwarekebisha watoto wetu, kama vile Mungu anavyotusahihisha kwa sababu Yeye anatupenda. Ikiwa hatujasahihisha jinsi tunavyopaswa kufanya ikiwa masahihisho yetu yamekuwa matusi badala ya kuwarekebisha sisi pia tutalipa matokeo tutakapoona matokeo. “Fimbo na kemeo hutoa hekima, lakini mtoto aliyeachiliwa humwaibisha mama yake.” (Methali 29:15).

Mungu anaelewa maumivu, huzuni, mapambano, maudhi, kukatishwa tamaa, na kuchanganyikiwa tunavyopitia kama wazazi. Mwenyezi Mungu ni Mfalme wa ulimwengu na Muumba wa vitu vyote, lakini bado ni Baba yetu wa mbinguni. Hakika anapata huzuni wakati sisi, watoto Wake, tulipokuwa waasi na wasio na shukrani na tunapoamua kufanya mambo kwa njia yetu bila uongozi Wake. Kama wazazi, tunahuzunika juu ya watoto wetu wanapofanya makosa au chaguzi mbaya. Tunaumia wakati mambo yenye kuumiza yanapotokea kwao. Sisi tunakasirishwa na uasi wao kwa njia za Mungu. Sisi sote tunafanya makosa kama wazazi, kwa hivyo wacha tuondoe kumbukumbu hizo kutoka kwenye mioyo na akili zetu kwa kwenda mbele za Bwana na kumwomba afunue chochote ambacho kinahitaji kuwekwa chini ya msalaba na kuwasilishwa kwa uwezo wa utoaji wa Roho takatifu.

Sema, “Bwana, nionyeshe kama nimeshindwa kuwaadhibu watoto wangu wakati gani walipokuwa wadogo na hii imehimiza uasi au kuwafanya wasielewe matokeo ya dhambi sasa.”

Ikiwa unaona maeneo ambayo mtoto wako ameshindwa kuwa na nidhamu wakati anapaswa kuwa nayo, usiruhusu adui kushinda hii. Ungama mbele za Mungu. Mfalme Daudi katika Biblia, yule ambaye Mungu alisema alikuwa mtu aliyeufuata moyo wa Mungu, moyo huo huo ulishindwa kama mzazi. Alifanya mambo ya kutisha yaliyoenda kinyume na Mungu. Inasemwa juu ya Adoniya, mwana mwasi wa Daudi, kwamba “baba yake hakuwa akimkemea wakati wowote” (1 Wafalme 1:5-6). Daudi hakumwadhibu Adonia popote, jambo ambalo lingefanya kazi kubwa ya kumtengeneza kuwa binadamu mwenye heshima na hekima badala ya upuuzi wa kujitakia mwenyewe. Aliasi dhidi ya baba yake na alifikia mwisho mbaya. Watoto wasio na nidhamu hujifikiria wenyewe, hujitumikia, na hatimaye kujiangamiza. Daudi hakufanya alichopaswa kufanya kumtengeneza mwanawe awe mtu wa Mungu ambaye angepaswa kuwa, na hivyo Adonia alifanya alichotaka kwa sababu hakujua matokeo. Kisa cha Adoniya kinatuonyesha kwamba matokeo ni makali wakati watoto hawakulelewa katika njia ya Bwana. Lakini Mungu hataki mtu yeyote awe wa kuharibiwa kama Adonia badala yake Anawataka watu wote watubu (2 Petro 3:9).

Watoto wadogo ambao wana nidhamu kwa upendo na kujifunza sheria na mipaka, hukua na kuwa watu wazima salama zaidi. Sizungumzii kupiga;

Ninazungumza kuhusu kumuumba mtoto ipasavyo. Kumlea mtoto kunahitaji upendo na nidhamu, lakini kuna thawabu kubwa. "Kila adhabu wakati wake haionekani kuwa kitu cha furaha, bali cha huzuni; lakini baadaye huwaletea wao waliozoezwa nayo matunda ya haki yenye amani." (Waebrania 12:11). Biblia inasema, "Usimnyime mapigo maana ukimpiga kwa fimbo hatakufa" (Mithali 23:13). Inasema kwamba hatima ya mtoto wetu ni kubadilishwa na jinsi tunavyomtia adabu. Na kwamba ukimtia adabu, utaiokoa nafsi yake na kuzimu" (Mithali 23:14). Kwa maneno mengine, tusipowaadhibu watoto wetu, Shetani atafanya hivyo na aweza kutumia pia vyombo vya dola kwa kwenda jela nk.

Tunapowaadhibu watoto wetu, inawalinda dhidi ya adui. Na Amani yetu inaongezeka pia. "Mrudi mwanao, naye atakupa raha; ndio, yeye atakufurahisha nafsi yako" (Mithali 29:17). Mtoto anapokosa utii na asiadhibiwe, matokeo yake hufungua mlango wa roho ya uasi. Uasi husababisha mtu kushawishiwa na kuyumbishwa na adui. Biblia inasema hatupaswi "kutoa nafasi kwa Ibilisi" (Waefeso 4:27). Asili ya uasi inaonyesha kuwa mtu amempa adui nafasi katika moyo wake. Uasi hufunika hekima yote na utambuzi na kuruhusu watoto wako watu wazima kufunguka kwa ulimwengu ambao ni giza na uovu (1 Samweli 15:23). Kamwe usifikiri kuwa uasi hauna madhara. Daima uasi huleta shida.

Ombea Bwana avunje uasi wowote kwa watoto wako watu wazima. Maombi yako hayawezi tu kumzuia adui asipate msingi zaidi katika maisha yao sasa, lakini maombi yanaweza kumrudisha nyuma kabisa. Kumbuka tu

kwamba vita yako unapigana na adui wa roho ya mtoto wako na si na watoto wako watu wazima. Ushawishi wa Roho Mtakatifu ndani yao una nguvu zaidi kuliko ushawishi wa adui ndani yao. Hakuna kitu kigumu kwa Mungu. "Aa, Bwana MUNGU! Tazama, Umeziumba mbingu na nchi kwa uwezo wako mkuu kwa mkono wako ulionyoshwa. Hakuna jambo lolote lililo gumu kwako" (Yeremia 32:17).

Haijalishi mtoto wako ameenda mbali kiasi gani na Mungu au ndani yao kuna uasi kiasi gani, Mungu ameahidi kuwaokoa na kuwarudisha kutoka pale walipochukuliwa mateka. "Usifadhaike, Ee Israeli! Kwani tazama, nitakuokoa kutoka mbali, na wazao wako katika nchi ya uhamisho wao" (Yeremia 46:27). Kila siku sema, "Asante, Bwana, kwamba utamleta mtoto wangu mtu mzima kutoka katika nchi ya uhamisho wake."

## USISITE KUPIGA SIMU KWA UIMARISHAJI

Sura hii ni ndefu kuliko nyingine kwa sababu inashughulikia masuala ya maisha na mauti. Ikiwa hatuombi juu ya mambo haya kwa ajili ya watoto wetu watu wazima, matokeo yanaweza kuwa mabaya. Siwezi kuanza kuelezea uharaka ninaohisi juu ya hili. Ndiyo maana ikiwa mmoja au zaidi ya watoto wako watu wazima wako katika mapambano mazito, usiombe peke yako. Jiunge na wengine. Hili ndilo jambo lenye nguvu zaidi na unaweza kufanya zaidi kwa kufunga na kuomba.

Mchungaji Jack  alisema haya katika mojawapo ya mahubiri yake kuhusu nguvu ya kuomba pamoja: "Kuna kanuni ya kibiblia kwamba kuongeza idadi ya wanaoomba kwa ajili ya jambo fulani huzidisha mwelekeo wa

matokeo. kauli hii imechukuliwa kutoka kwa Bwana, ambaye alisema watu watano watafukuza mia, na mia watawakimbiza elfu kumi (Mambo ya Walawi 26:8).

Sio suala la kusema Mungu anajibu kwa sababu ya idadi, lakini kuna nguvu ya kupenya wakati kuna mapatano katika maombi (synergy). Kukubaliana ni kama kuandika maandishi kwa upatanifu. Maneno 'agano moja' yanawasilisha wazo la watu wote kuwa na joto-joto sawa-kiwango sawa cha shauku, kiwango sawa cha kuzingatia (Matendo 2:1, 2:46, 4:24, 5:12). Ukweli huu unatuita sisi kuomba pamoja, tukiamini vivyo hivyo juu ya kile kinachowezekana."

Aliendelea kueleza kwamba inabidi "tufafanue kile ambacho tutaomba" na pia "kuelewa ahadi za kibiblia ambazo kupitia kwazo tunatarajia mambo hayo kutokea." Wapo watu wengi ambao wangependa kuomba pamoja nawe kuhusu mahangaiko yoyote uliyo nayo hasa kuhusu watoto wako watu wazima.

Wanafunzi walipokusanyika pamoja na wengine kuomba pamoja, palikuwa na udhihirisho wa nguvu ya Roho Mtakatifu. "Walipokwisha kuomba, mahali pale pale walipokuwa wamekusanyika palitikisika; wakajazwa wote na Roho Mtakatifu, wakanena Neno la Mungu kwa ujasiri. Wengi wa walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja" (Matendo 4:31-32).

Nguvu ya maombi yao iliongezeka, lakini si kwa sababu tu walikuwapo kwa idadi kubwa zaidi. Ilibidi pia kuwe na imani zaidi pamoja na kuzingatia

kwa pamoja. Hapo ndipo sehemu ya "nia moja" inapoingia. Wakati watu, kama wewe na mimi, wanapoungana pamoja katika kukubaliana kuhusu jambo muhimu katika maombi, mambo yanatokea.

Pia inasema kwamba “neema kuu” ilikuwa juu yao wote (Matendo 4:33). Neema hii ni neema ya Mungu juu yetu. Lakini "neema kuu" inarejelea ambapo uweza wa Roho Mtakatifu unafanya kazi katika maisha yetu na kudhihirisha majibu ya maombi yetu. Tunapowaombea watoto wetu watu wazima hatuhitaji neema pekee bali neema zaidi kutoka kwa Mungu kuliko tunavyostahili. Tunahitaji neema kuu, ambayo ni nguvu ya Roho Mtakatifu inayofanya kazi katika maisha yetu na katika maisha ya watoto wetu watu wazima. Tunahitaji mahali tulipo patikiswe na uwepo wa Roho Mtakatifu. Sio lazima nyumba au chumba, lakini hali ya moyo.

Zerubabeli, gavana wa Agano la Kale wa Yuda, alihusika kulijenga upya hekalu la Mungu, lakini aliagizwa asitegemee nguvu au rasilimali za mwanadamu kuifanya. Bwana alitaka Zerubabeli amtumaini Yeye. Mungu alisema kazi yake haingetimiza “sio kwa uwezo wala kwa nguvu, bali kwa Roho Wangu” (Zekaria 4:6). Mungu aliendelea kusema, “Wewe ni nani, Ee mlima mkubwa? Mbele ya Zerubabeli utakuwa nchi tambarare! Naye atalileta lile jiwe la kifuniko kwa kelele za ‘Neema, neema iwe!” (Zekaria 4:7).

Tunapozungumza neema kwa kizingiti au kizuizi tunachokabiliana nacho au kile kinachowakabili watoto wetu wakubwa ambacho ni kama mlima kwetu, ni tendo la imani kwetu. Tunakubali kwamba hatuna uwezo wa kubadilisha

mambo, lakini Mungu anao uweza na nguvu. Na kwa Roho Wake wa neema, Yeye atafanya jambo hilo.

Unapomwita Mungu katika maombi, piga kelele “neema” kwa mlima wowote wa upinzani unaokupinga wewe au mtoto wako mkubwa. Sema, “Bwana, katika Jina la Yesu mimi natumainia neema kwa ajili ya ….. taja jina la mtoto." Na utaje kikwazo unachotaka kuona kikivunjwa. Sema, kwa mfano:

Bwana, ninatamka neema kwa tabia mbaya za binti yangu.

Bwana, ninatamka neema kwa shida ya mwanangu ya dawa za kulevya.

Bwana, ninatamka neema kwa shida ya kula ya binti yangu.

Bwana, ninatamka neema kwa shida za kifedha za mwanangu.

Tamka neema kwa mlima wowote wa upinzani au kikwazo anachokabili mtoto wako mtu mzima.

## OMBA MTOTO WAKO MKUBWA ARUDI KWA BWANA

Kuna sehemu katika Biblia ambapo Bwana anazungumza kupitia nabii Yeremia na kuzungumza na jiji la watu waliokuwa wakiharibiwa na ufisadi wao wenyewe. Mungu anaahidi kuwarejesha ikiwa watarejea Kwake na kutubu. Hizi zilikuwa ahadi sio tu kwa watu wazima, lakini kwa watoto wao kama watatembea na Mungu katika utii. Biblia inasema fadhili za Bwana ni za milele (Zaburi 89:28). Kwa hivyo ingawa Mungu anazungumza na watu wa Israeli wakati huo, alitoa ahadi kwao kwamba sisi

pia tunaweza kuamini. Inatuhusu sisi tunaoomba na kulia kwa ajili ya watoto wetu watu wazima ambao wamechukuliwa mateka na adui.

Ahadi hii inasema, "Jizuie sauti yako usilie, na macho yako yasiwe na machozi; kwa maana kazi yenu itakuwa na thawabu,' asema BWANA, 'nao watarudi kutoka nchi ya adui. Kuna tumaini katika wakati wako ujao,' asema BWANA, ili watoto wako warudi hadi katika mpaka wao wenyewe" (Yeremia 31:16-17).

Ikiwa una watoto watu wazima ambao wamechukuliwa mateka na ushawishi mbaya, soma tena huo mstari hapo juu na uamini kwamba Mungu anazungumza nawe maneno hayo. Mistari hii inaniambia kwamba kazi yetu ngumu katika maombi kwa ajili ya watoto wetu watu wazima itakuwa na thawabu, kwa sababu watarudi kutoka katika nchi ya adui ambayo kwao wamechukuliwa mateka.

Hii ni ahadi kubwa kwa wazazi wa watoto watu wazima ambao wamepotea kutoka katika njia ya Mungu kwa maisha yao. Huenda hujui ni njia gani hasa Mungu aliyonayo kwa ajili yao, lakini mnajua kama hiyo njia wanayofuata sasa siyo aliyokusudia Bwana. Huu ni ujumbe wa matumaini kwa watoto wako watu wazima pia, na haijalishi ni umbali gani adui amewatoa katika maisha waliyokusudiwa kuishi, hakika watarudi kutoka nchi ya adui hadi mpaka wao wenyewe.

Unakumbuka nilichosema kuhusu ahadi za Mungu? Hizi zio programu ya haki. Huu ni uhakikisho wa Mungu wetu kwetu. Ingawa ni kweli kwamba

sisi tunapaswa kufurahia kile ambacho hatujapata, bado tunapaswa kuomba ili kukipokea. Tunaweza kulia katika maombi kwa ajili ya watoto wetu watu wazima, lakini sio lazima kulia na kukata tamaa. Tunaweza kumsifu Mungu kwa ajili ya ahadi Zake za kuwarejesha watoto wetu kutoka kwenye makosa ya malezi.

Ikiwa mtoto wako mtu mzima amepotoka kutoka kwa familia yako au dini yako, au amevunja uhusiano wako na yeye na amechagua maisha ambayo ni tofauti na jinsi ulivyomlea na kwamba inakuweka katika huzuni kubwa, muombee apate urejesho. Hii haimaanishi kuwa yeye atarudi kwako mara moja hata hivyo usiwe na wasiwasi na ongeza matumaini yako juu ya kile Mungu atakachofanya kupitia maombi. Hii ina maana kwamba unapoomba, Mungu atashusha mgawanyiko huo mkubwa, afungue milango ya mawasiliano tena, na kukusaidia kuwaunganisha tena.

Ikiwa mtoto wako mtu mzima anahitaji kurudi kwenye mpaka wake mwenyewe, kurudi kwenye njia za Bwana na kile anachojua kuwa ni sawa, Mungu anasema kwamba Yeye anaona machozi yako na kusikia maombi yako. Endelea kumuombea mpaka yeye atakaporudi kutoka katika nchi ya adui na kuishi katika milki yako ambayo ni ufalme wa Mungu duniani.

Usikate tamaa na kuacha kuomba juu ya hili. Mpe Mungu nafasi kulifanyia kazi. Kumbuka kwamba Yeye Anashughulika na nia na mapenzi yenye nguvu katika mtoto wako mtu mzima, ambayo mtoto tayari amejiwekea mpango wa kutoukiuka. Ni mara ngapi sisi sote tumelia mbele za Bwana huku tukiomba kwa ajili ya watoto wetu wakubwa? Mioyo yetu inavunjika

tunapoona chochote kilichovunjika ndani yake.

Biblia yasema hivi: "Yeye atokaye sikuzote, akilia, akipanda mbegu; bila shaka atakuja tena kwa furaha, akichukua miganda yake pamoja naye" (Zaburi 126:6). Tunapopanda mbegu katika maombi na kuzimwagilia machozi yetu ya uchungu na huzuni, jambo lenye nguvu hutokea. Unapolia kwa shauku katika maombi, utakuwa na furaha kujua kwamba kitu kikubwa kilikuwa kikikamilika katika ulimwengu wa roho. Na utayaona yanadhihirika katika ufalme wa kimwili pia.

## WAKATI UNACHOHITAJI KUSEMA NI KIGUMU KWAO SIKIA

Kama nilivyosema katika utangulizi wa kitabu hiki, hatuwezi kukaa tu na kuruhusu watoto wetu watu wazima hufanya uharibifu kwa maisha yao tunapoona hali ya hatari kama vile ulevi au kukosa malengo. Tunapaswa kusema kitu. Mimi na mume wangu tumelazimika kufanya hivyo kwa kila mmoja wa watoto wetu watu wazima. Na kila wakati tulifanya kwa upendo, na sio hasira. Kuonyesha upendo wakati huo haikuwa mwitikio wetu wa kawaida wa kwanza, wala sio hekima yetu. Mchungaji alituambia kwamba hii ndiyo njia pekee ya kujibu ikiwa tunataka kuona matokeo mema.

Tulipoenda kwa kila mtoto mtu mzima, kila mmoja kwa nyakati tofauti na kwa sababu tofauti tuliwaambia kwamba walichokuwa wakifanya kilikuwa nje ya njia ambayo Mungu alikuwa nayo kwa ajili yao na ilikuwa

haikubaliki. Tuliwaambia hatutakubali kitu ambacho kingekuwa chini kuliko kile ambacho Mungu anacho kwa ajili yao kuendelea kutokea katika maisha yao wakati tulikuwa na uwezo wa kuingilia.

Tulimhakikishia kila mmoja kwamba tunampenda sana kiasi kwamba hatuwezi kumwacha atembee juu ya mwamba wakati tunaweza kumsaidia kubadili njia. Pia tuliwaambia tumemwomba Bwana atufunulie chochote kinachohitaji kufunuliwa katika mojawapo ya maisha yao, na ilikuwa ni kwa msaada wa Bwana kabisa tulifahamishwa kuhusu mambo fulani yaliyokuwa yakitokea. Tulipokabiliana nao, walitubu mara moja na kufanya marekebisho makubwa katika njia zao za maisha. Katika visa vyote viwili, walikuwa wameruhusu mvuto wa watu wasiomwogopa Mungu uwaongoze wao katika mwelekeo mbaya.

Kabla hatujakabiliana na kila mmoja wao, tulisali kwa bidii. Tulitaka kwenda kukutana nao katika Roho wa Bwana na si katika hasira ya mwili, kwa maana ndivyo ilivyokuwa muhimu tuone badiliko la moyo na kisha kufumbua macho yao kwa Ukweli. Na, tunamshukuru Mungu, tulifanya hivyo. Tulishukuru kuona hili likiwa na matokeo makuu na ya uhakika katika kila maisha yao. Lazima niseme kwamba ilikuwa huzuni kwa sisi sote kwa wakati fulani, lakini mengi mazuri yalitokea ndani yake nami ninajua Bwana alikuwa katika mchakato wote.

Usifikiri kwamba kwa sababu watoto wako ni watu wazima hawahitaji maoni yoyote zaidi kutoka kwako. Wanahitaji! Wawe ni watoto wanaoomba au la. Chagua tu muda mfupi. Usifanye shuguli ya kuwasonda

na kuwahukumu. Toa ushauri kwa uangalifu na pale tu inapoonekana wanaupokea au wako tayari kusikiliza. Lakini ukiona wanakaribia kugonga ukuta, usisite kuingia na kusaidia kugeuza mambo. Utakuwa na mamlaka makubwa katika maisha ya watoto wako watu wazima ikiwa wewe mwenyewe utawakilisha kwa mamlaka ya Baba Mungu katika maisha yako mwenyewe. Kwa mamlaka simaanishi kujaribu kuwafanya watoto wako watu wazima kufanya mambo kwa njia yako. Namaanisha kuwa na uwezo au mchango unaoaminika katika maisha yao wanapouhitaji. Hatutaki kuwazuia watoto wetu watu wazima wasiwe na uwezo wa kufikiri wenyewe na kufanya maamuzi yao wenyewe.

Tunataka kuwa msaada kwao katika maamuzi wanayofanya na bado wanayo nafasi ya kuadhibiwa ikiwa watafanya makosa makubwa sana.

Ikibidi useme jambo ambalo unajua litakuwa gumu kwa mtoto wako mtu mzima kusikia, hauna budi kuingia katika maombi kwanza. Ombea maneno sahihi na wakati sahihi. Ombea moyo ili mtoto wako mtu mzima aweze kupokea mashauri yako. Ikiwa umemwomba Mungu kupata usikivu wa mtoto wako mtu mzima kwamba Mungu aweze kumweka mtoto wako katika njia sahihi, fahamu anapofanya hivyo hasa. Wakati fulani Mungu anaruhusu mambo yatokee au yasitokee, jinsi itakavyokuwa ili kumsababishia kutafakari upya matendo yake. Inaweza kuwa ngumu kutazama, lakini jambo hilo litafaa unapoona mafanikio.

Amini hisia yako inapokuletea jambo fulani juu ya watoto wako wakubwa. Hii sio leseni ya kuwa na mashaka nao wakati wote, lakini unapaswa kuwa

na shaka na adui kila wakati. ikiwa unaona kitu sio sawa kwa watoto wako wakubwa au kitu fulani kimekuwa kikikusumbua katika nafsi yako kuhusu wao, amini sauti au hisia hiyo! Mungu huwapa wazazi antena takatifu maalum ambazo zinaweza kuhisia uovu wa mtoto umbali wa maili moja. Anza kuomba mara moja kwa Mungu aweze kufunua kila kitu na kufichua dhambi yoyote ili toba, ukombozi, na uponyaji uweze kuanza. Una nguvu. Adui ana uongo tu. Omba kwamba Ukweli wote uwekwe wazi.

## NGUVU YA MAOMBI

Bwana, naomba kwamba umpe …. (jina la mtoto mzima) utambuzi maana anahitaji kuelewa uchaguzi wazi kati ya mema na mabaya, na haki na makosa, kati ya kile kinachotoa uhai na kuharibu uhai, na kati ya njia inayoingia kwenye usalama na mustakabali mzuri wa maisha yake. Ninaomba kwamba yeye kamwe asiruhusu dunia kumuunda, lakini badala yake angeumbwa na Wewe. Najua kwamba ushawishi wa adui unaweza kuja kwa hila kiasi cha kukaribia kutogunduliwa hadi kuchelewa sana. Lakini ninaomba kwamba kwa hekima aliyopewa na Roho Mtakatifu apate utambuzi na aweze kuwa tayari kwa ajili ya adui na kutarajia mipango yake. Msaidie "kuokolewa na kizazi hiki kiovu" (Matendo 2:40).

Ninaomba kwamba utamaduni huu wa kidunia usiwe na nguvu juu yake. Bwana vunja namna yoyote ya yeye kushikamana na maovu ya dunia na kumwachilia yeye kushikamana na Wewe tu. Mlinde kutokana na kila shambulio la adui. Msaidie yeye kuweka tumaini Kwako na nguvu Zako na sio "kumpa Ibilisi nafasi" (Waefeso 4:27). Ninaomba kwamba atafute

mwongozo Wako kwa ajili ya maisha yake. Bwana, ninaomba kwa ajili ya mtoto wangu mtu mzima kwamba uwe "maficho yake" ambapo yeye atahifadhiwa kutokana na shida. Mzunguke "kwa nyimbo za ukombozi" na umfundishe yeye katika njia anayopaswa kuiendea (Zaburi 32:7).

Uwe nguvu zake wakati wa taabu na umwokoe kutoka kwa mikono ya mwovu (Zaburi 37:39-40). Asante, Bwana, kwamba unatukomboa kutoka kwa maadui zetu (Zaburi 18:48). Bwana, ninaomba kwamba unipe hekima ya kujua jinsi ya kuombea kila mmoja wa watoto wangu wazima. Nipe ujasiri wa kuwakabili ninapohitaji. Nisaidie kusubiri muda sahihi na kunipa maneno kamili ya kusema. Fungua mioyo yao kusikia kutoka kwangu. Popote walipopotea kutoka kwa njia Zako, nakuomba kwa nguvu Zako Wewe uliye mchungaji mwaminifu uwarudishe zizini.

Ambapo mtoto wangu mzima amechukuliwa mateka na ushawishi mbaya au tabia ya uharibifu, naomba kwamba umfungue awe huru. Asante, Bwana, kwamba umesema kwamba watoto wangu "watarudi kutoka katika uteka wa adui" na kwamba kuna tumaini katika wakati wangu ujao kwa sababu "watoto wangu watakuja kurudi hadi mpaka wao wenyewe" (Yeremia 31:16-17).

Bwana ninagundua kuwa sijui kila kitu kinachoendelea katika akili ya mtoto wangu mtu mzima, hisia, au maisha, lakini Wewe Wajua. Fichua kile kinachohitaji kufunuliwa. Fichua upotovu wowote wa fikra kwa uwazi kiasi kwamba yeye aweze kuletwa kwenye toba mbele Yako. Usimruhusu yeye kujiepusha na chochote. Popote yeye ambapo anaona ni sawa kucheza na

kitu ambacho ni mtego wa adui kwa uharibifu wake, nakuomba Umwokoe kutoka humo.

Mweke mtoto wangu mbali na watu wanaokusudia kufanya uovu au kumhusisha katika matendo maovu. Mzuie asianguke katika majaribu. Mtie nguvu ili kupinga vishawishi vyote viovu na kuepuka tabia yoyote ya uharibifu. Ambapo yeye amekuwa mwathirika wa uovu, ninaomba kwamba ungemponya, ungemrejesha, na umnyanyue juu ya uovu katika ushindi. Toa mema kwake. Kama vile Ulivvyomwinua Yusufu ili kuokoa taifa baada ya njama mbaya juu ya maisha yake kutekelezwa, nakuomba ungemwinua binti yangu au mwanangu kwa mambo makubwa licha ya uovu unaoendelezwa dhidi ya maisha yake. Kwa sasa, mwezeshe wakati huu kupata "neema nyikani" (Yeremia 31:2).

Bwana Fanya kazi katika maisha yake ili kumleta katika upatanisho kamili na mapenzi Yako hivyo hakuna nafasi kwa adui kupenya ukuta wako wa ulinzi. Weka ulinzi kwake na umlinde na yule mwovu. Fungua macho yake kuona Ukweli Wako, hivyo yeye hatakuwa na udanganyifu wowote. Ponda sanamu zozote za uwongo katika akili yake zinazomshawishi atoke kwenye njia uliyonayo kwa ajili yake. Msaidie na mgeuze akili yake iachane na uovu ili yeye asifanane na dunia. Msaidie abadilishwe kwa kufanywa upya nia yake ili yeye awe katika mapenzi Yako kikamilifu (Warumi 12:1-2).

Najua kwamba Hutalazimisha mapenzi Yako kwa mtoto wangu mkubwa maana anapaswa kukuruhusu uingie katika maisha yake, lakini ninakualika upenye maishani mwake kwa uwezo wa Roho wako Mtakatifu na kuufanya

moyo wake kuguswa na uwepo wako. Wakati wowote ninapohisi kukata tamaa, au kuogopa kwamba tunashindwa vita, nitainua sifa kwako, kwani Wewe ni mkuu zaidi kuliko ushawishi wowote mbaya alio nao mtoto wangu mzima kutoka kwa yale yanayowakabili.

Ninaomba kwa uwezo wa Roho Wako Mtakatifu kwamba mtoto wangu mzima atakuwa huru dhidi ya ushawishi mbaya wote na tabia ya uharibifu. Fichua chochote kinachohitajika kufunuliwa kwa nuru Yako inayopenya na kuona kila kitu ili ukombozi na uhuru uweze kuja Katika Jina la Yesu ninaomba. Amen.

**NGUVU YA NENO**

Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote mkiri Yeye, Naye atayanyosha mapito yako.

**MITHALI 3:5-6**

Maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu wa kuangusha chini ya ngome.

**2 WAKORINTHO 10:4**

Ninyi mnaompenda BWANA, chukieni uovu! Huzihifadhi nafsi za watakatifu wake; Yeye huwaokoa na mkono wa waovu. Nuru hupandwa kwa wenye haki, na furaha kwa wanyoofu wa moyo. Furahini katika BWANA, enyi wenye haki, na kutoa shukrani kwa ukumbusho wa Jina

Lake takatifu.

**ZABURI 97:10-12**

BWANA ni jabali langu na ngome yangu na mwokozi wangu; Mungu wangu, nguvu zangu, Ndiye ambaye nitamtumaini.

**ZABURI 18:2**

“Si kwa majeshi wala si kwa silaha, bali ni kwa Roho Yangu,” asema BWANA wa majeshi.

**ZEKARIA 4:6**

## OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE KUEPUKA UCHAFUZI WOTE WA NGONO NA VISHAWISHI

Katika miaka 37-pamoja tangu mtoto wangu wa kwanza kuzaliwa, nimeona mabadiliko makubwa katika ulimwengu ikiwemo televisheni ambazo ni dalili ya kile ambacho kimetokea kwa utamaduni wetu. Wakati wangu watoto wakiwa wachanga, mara chache sana tuliwasha televisheni mchana. Mara chache mume wangu au mimi tuliwasha TV jioni ili kutazama taarifa ya habari, michezo au kitu maalum ambacho tulipendezwa nacho, watoto walikuwa wamelala. Sikuwazuia kutazama TV kwa sababu niliogopa wangefanya hivyo endapo wangezuiliwa kabisa, lakini kwa sababu sikutaka kuwatia ganzi akili zao na kuzuia ubunifu wao. Nilitaka wacheze nje ya nyumba kadri iwezekanavyo, na wakati wakiwa ndani wawe na uwezo wa

kufikiria mambo ya kufanya na wanasesere/toys, vitabu, michezo na mambo mengine ya kushughulisha mawazo yao.

Waliruhusiwa kutazama video fulani ambazo nilikuwa nimeona na kujua zimepita viwango vya kile nilichohisi kilikuwa cha manufaa kwao. Na walitazama Vipindi maalum vya televisheni ambavyo vilivutia na kufurahisha sana. Lakini, kwa sehemu kubwa, walipata tabia ya kuwa bize bila TV na hivyo hawakuitegemea. Nyakati nyingine walikuwa wanakaa kwenye nyumba ya rafiki, bado sikuwa na wasiwasi kuhusu nini wangeona kwenye TV. Hali haikuwa kama ilivyo leo.

Leo hali ni tofauti. Ikiwa ningekuwa ninalea watoto leo, sijui kama ningeendelea kuwa na TV ndani kwa ajili yao. Leo, hata mimi kama mtu mzima siwezi kugeuza chaneli tu kwa sababu kuna mambo mengi ya kukera ambayo huchukuliwa kuwa ya kawaida, na yabidi tuombe zaidi maana Tv ana dada yake aitwaye simu za mkononi, na hivyo TV imeingia chumbani. Hakuna jinsi tutakavyomhuzunisha Roho Mtakatifu ndani yetu na kuruhusu nafsi yetu kunyanyaswa kwa sababu tu  ya kutazama chaneli za kutisha. Mengi yanayokuja kwenye televisheni leo ni yenye kuchafua maisha yetu yote. Hisia zetu zinaweza kuchafuliwa kwa urahisi kwa lugha chafu yenye kuudhi, ukosefu wa adili waziwazi, usiobadilika, kukufuru juu ya kila kitu kinachohusiana na Mungu, na kuinuliwa Kwake;  watuwasiomcha Mungu hupunguza wacha Mungu.

Watoto wetu watu wazima-wako na wangu-wamekabiliwa na aina hii ya ushawishi kwa miaka. Shule zetu zimekuwa na kila chembe ya ushahidi

kwamba Mungu Yupo, au kwamba Ukristo ni muhimu kwa maisha yao.

Hakuna chochote kati ya Amri Kumi kinachoruhusiwa katika mashule mengi. Maombi yamepigwa marufuku katika mashule mengi. Maoni yote ya Mwenyezi Mungu yameondolewa. Bado tumeshambuliwa na nguvu zinazopinga yote ambayo yanamhusu Mungu na yote anayosimamia, na tumekuwa tukihimizwa kukubali mema kuwa mabaya na mabaya kuwa mema. Sauti ya dunia inajaribu kufuta sauti ya maadili. Na watoto wetu watu wazima wana msukumo kwa hayo kila siku kwa namna fulani.

Zaidi ya yote haya, uovu ulioenea wa uasherati na ngono ya kawaida huleta kuchanganyikiwa katika maisha yao. Upotoshaji unakuzwa kuwa sio tu jambo la kawaida tu, bali pia uhitajika-ni hitaji. Uovu umetokea kwa watoto wetu watu wazima na kuwalenga. Uzinzi unamaanisha kufanya ngono sasa, bila vizuizi. Inamaanisha kwamba ikiwa wewe ni bikira, wewe sio wa kawaida, na pengine ni kana kwamba umeachwa na basi. Watoto wetu wanaongozwa kuamini kwamba uasherati, au kufanya ngono kabla ya ndoa, si tu jambo nzuri lakini ni jambo linalotarajiwa, kama ibada. Jambo hili linakuzwa kama kitu cha kutafutwa na ushujaa. Ngono nje ya ndoa hutukuzwa na kuonyeshwa kuwa ni bora kuliko ngono ndani ya ndoa. Mtazamo wa kawaida kuelekea uasherati umekuwa janga linaloambukiza kila mtu. Na sizungumzii chochote zaidi ya kuwasha TV. Hata matangazo ya biashara yenye picha za ngono au chafu yanaweza kuchafua akili zetu.

Ili watoto wetu watu wazima waishi kwa mafanikio katika kila nyanja yao ya maisha, usafi wa kijinsia ni muhimu. Inaathiri namna ya wao kujitambua

kuwa wao ni nani. Inaathiri uhusiano wao muhimu zaidi katika ndoa. Wakati wanaishi katika  ngono chafu au isiyo halali katika maisha yao, huathiri kila Nyanja ya maisha yao. Mahusiano yao yanakuwa dhaifu, na wanapoteza hisia ya kusudi lao la Kweli na utambulisho wao.

Usifikirie kwa muda kwa sababu wewe au Watoto Wako Wakubwa hawajawahi kutazama kitu chochote kinachokaribia ponografia, basi akili zao hazijapata kuchafuliwa kwa namna fulani. Roho iliyo nyuma ya haya yote—roho ya tamaa—ndiyo iko kila mahali, na roho hii Kaini alikuwa nayo kabla ya mtandao au Tv. Watoto wako watu wazima huona picha za ngono kwenye mabango wanapoendesha gari barabarani. Wanaiona kwenye magazeti ya kawaida au yasiyo ya kawaida. Wanaiona ndani ya filamu zinazopendwa na wengi—hata katika filamu inayodhaniwa kuwa ya heshima. Wanaiona ndani video za muziki, na wanaisikia katika maneno ya nyimbo fulani. Ngono imekuwa sanamu ambayo tamaduni zetu huabudu, na watoto wetu watu wazima wanashawishiwa kufikiria kuhusu hilo sana. Mambo ya ushoga yameingia kwa kasi kutoka magharibi, katika miaka hii michache na yanasambaa kama moto kwenye majani makavu. Yote haya ni mambo ya kuombea.

Yale ambayo yeyote kati yetu anayatazama hata kwa bahati mbaya yanatuathiri zaidi kuliko tunavyotambua. Picha zinaweza kucheza mara kwa mara katika akili zetu ambazo hutufanya kuhisi maelfu ya hisia kama vile mshtuko, tamaa, hatia, karaha, au maudhi. Picha hizi zinatulazimisha akili kwenda mahali ambapo hatutaki ziende, hata ikiwa ni kwa muda mfupi tu.

Sisi basi itabidi tusipoteze wakati wa thamani kushughulika na mawazo na hisia hizo. Sisi tunapaswa kumwomba Mungu asafishe akili zetu kuondoa mambo haya ili tufanye uamuzi mzuri. Mungu anatuambia tena na tena katika Neno Lake kwamba tunapaswa kukimbia kutoka kwa mambo mabaya na tusiyaangalie. Hata hivyo, uovu unasukumwa katika nyuso zetu wakati hatutarajii na haswa kwa watoto wetu wazima.

Maana yake yote ni kwamba tunapaswa kuomba kwa bidii na kwa juhudi sana kwa ajili ya watoto wetu watu wazima ili kumuona Mungu akivunja nguvu za giza zinazowazunguka katika maisha.

## NJIA KUMI ZA KUOMBEA WATOTO WAKO WAKUBWA KUPINGA UCHAFUZI WA NGONO

1. Omba kwamba watoto wako watu wazima wapate kumiminiwa upya Roho Mtakatifu juu yao. Hii itawafanya waone kwa mtizamo na macho mapya. Omba kwamba waweze kuona mambo kwa mtazamo wa Mungu na kuwezeshwa na nguvu ya Roho Mtakatifu, waweze kupinga vyema shambulio lolote la uchafuzi wa kingono, ili wapate kuondokana na roho ya tamaa juu yao. “Kwa kuwa na nia ya mwili ni mauti, bali kuwa na nia ya roho ni uzima na amani” (Warumi 8:6).

2. Omba ili watoto wako wakubwa wawe na moyo mpya kwa Mungu, Wapende Neno la Mungu, na njia Zake. Wapate kuvutwa kuelekea mambo

ya Mungu na wawekwe mbali na chochote kinachompinga Mungu. Omba wapate Kuwa na moyo unaozielekea Njia za Mungu na Neno Lake ili wasistarehe na picha au matendo ya ngono ambayo yanakiuka au kuathiri njia za Mungu. "Haki ya wanyofu itawaokoa, lakini wasio waaminifu watakamatwa na tamaa zao" (Mithali 11:6).

3. Omba kwamba Watoto Wako Wakubwa wawe na hekima, utambuzi, na ufunuo. Wanahitaji hekima kubwa kujua jinsi ya kuepuka uchafuzi wa ngono. Wanahitaji utambuzi wa wazi ili kuona wazi mitego katika uchafuzi wa kijinsia. Na wanahitaji ufunuo kutoka kwa Mungu kuhusu jinsi ya kujilinda na kuishi katika usafi. "Hekima inapoingia katika moyo, na maarifa yanapendeza nafsini mwako, busara itakuhifadhi wewe; ufahamu utakulinda, ili kukuokoa na njia ya uovu; kutoka kwa mtu anenaye mapotovu" (Mithali 2:10-12).

4. Omba kwamba Watoto wako wakubwa watapata uhuru, urejesho, na uzima. Omba ili wawe huru kutokana na chochote kinachowavuta kuelekea chochote kinachowachafua kingono. Omba kwamba waokolewe kutoka kwa chochote kinachowashikilia, kama vile picha za ngono ndani ya akili ambayo imekuja kupitia aina yoyote ya vyombo vya habari.

Omba kwamba watapata mrejesho kutoka kwa kuvunjika au kushindwa kwa kijinsia katika siku zao zilizopita ili kwamba wao waweze kuwa na usafi upya na utimilifu ambao Mungu anao kwa ajili yao. "Kwa hiyo nyenyekea kwa Mungu. Mpingeni Shetani naye atawakimbia" (Yakobo 4:7).

5. Omba ili watoto wako watu wazima wasiache macho yao yatazame mambo yasiyo na thamani. Omba kwamba watakataa hata kutazama kitu ambacho ni cha kumchukiza Mungu na ambacho hakiongezi chochote cha thamani kwa maisha yao. “Geuza mbali macho yangu yasitazame mambo yasiyofaa, unihuishe katika njia Yako. Uthibitishe Neno Lako kwa mtumishi Wako, ambaye amejitolea kukucha Wewe” (Zaburi 119:37-38).

6. Omba ili watoto wako walio watu wazima wasipate mwelekeo wao nje ya njia ya Mungu na makusudi ya Mungu kwao. Ni muhimu daima kuelewa kusudi lao ili wakatae kukiuka hilo kwa njia yoyote ile. “Wacha macho yako yatazame mbele, na kope zako zitazame mbele yako sawasawa” (Mithali 4:25).

7. Omba kwamba watoto wako wakubwa watambue nguvu ya tamaa ya kuharibu nafsi zao. Mungu anatarajia zaidi ya hayo. Wanapaswa kumpinga adui katika hii vita kwa ajili ya nafsi zao. “Wapenzi, nawasihi kama wapitaji na wasafiri. Ziepukeni tamaa za mwili zipinganazo na roho” (1 Petro 2:11).

8. Omba ili watoto wako watu wazima wasipate tamaa ya namna yoyote ile iliyo kinyume mapenzi ya Mungu. Kuelewa mapenzi ya Mungu kwa maisha yao kunahitaji kuwa kipaumbele chao. “Ili asiishi tena wakati wake uliobaki katika tamaa za wanadamu, bali kwa mapenzi ya Mungu” (1 Petro 4:2).

9. Omba ili watoto wako wakubwa waishi katika Roho wa Mungu na si katika tamaa za mwili. Wanahitaji kuelewa wazi kile ambacho ni cha Roho

Mtakatifu na kuepukana na tamaa za mwili ambazo hazimtukuzi Mungu. “Basi nasema: Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili” (Wagalatia 5:16).

10. Omba ili watoto wako wakubwa wamkimbilie Bwana na Kweli ya Neno Lake kila wanapojaribiwa kuvutiwa katika aina yoyote ya uchafuzi wa ngono. Matokeo ya kufanya vinginevyo ni makubwa sana. Ni suala la maisha na kifo kwa namna nyingi sana. “Kabla sijateswa mimi, nilipotea, lakini sasa nimelitii Neno Lako” (Zaburi 119:67).

**NGUVU YA MAOMBI**

Bwana, ninaomba …………. (jina la mtoto mzima) asiwe na uchafuzi wowote wa ngono. Popote pale alipoona mambo ambayo yamehatarisha usafi wake wa kijinsia Nakuomba uitakase akili yake na kutoa mawazo hayo nje ya moyo wake. Kama yeye amejihusisha kwa hiari katika jambo lolote linalokiuka viwango vyako vya usafi, naomba kwamba ungetia hatiani dhamiri yake kuhusu hilo na kumleta yeye katika toba mbele Yako. Msaidie kugeuka kwa hiari na kuikimbia kila sanamu na machukizo (Ezekieli 14:6). Vunja nguvu ya roho yoyote ya tamaa inayojaribu kuleta mauti kwa nafsi yake (Ezekieli 18:31-32).

Msaidie yeye aepuke uchafuzi wa kingono ili auepuke, asiuangalie, na kutovutwa ndani yake na kukataa kutiwa unajisi na sanamu za ulimwengu (Ezekieli 23:30). Mpe yeye imani ya kubadilisha chaneli; kuzimisha tovuti; kutupa gazeti, programu ya simu, au kuacha mitandao ya kijamii mibaya; au

kutoka nje ya ukumbi wa michezo iliyo kinyume na Wewe (Mithali 27:12). Mpe mtoto wangu kuelewa kwamba upotofu wowote kutoka kwa njia Yako una madhara kwake na hata ikiwa inatokea tu katika akili itakuwa mtego kwa ajili ya nafsi yake.

Mwezeshe mtoto wangu kusimama juu ya mwamba imara na kwa usafi mbele zako. Msaidie kuona kwamba hata kutotii njia Zako bila kukusudia kutahitaji toba na utakaso. Msaidie yeye kuficha Neno Lako ndani ya moyo wake ili asije akakutenda dhambi (Zaburi 119:9-11). Ninaomba kwamba yeye atalindwa kwa busara na kuvutiwa na maarifa na ufahamu ambao utamwokoa na uovu (Mithali 2:10-12).

Pale ambapo yeye ameruhusu matamanio yoyote yasiyo ya Bwana, naomba Ungemweka huru. Weka ndani ya moyo wake hamu ya kukupendeza Wewe kwa kutembea katika Roho na sio mwili (Warumi 8:8). Msaidie ajue kuwa Wewe ni kimbilio lake, naye anaweza kukugeukia wakati wowote majaribu yanapojitokeza (Zaburi 141:8). Msaidie yeye kuelewa ukuu wa uwezo Wako wa kumweka huru. Geuza macho yake kutoka kwenye mambo yasiyofaa (Zaburi 119:37). Mpatie yeye uwezo wa kutafakari kila kitu anachofanya na kila hatua anayochukua ili asitembee katika njia ya uovu (Mithali 4:26-27).

Popote pale ambapo kumekuwa na kushindwa kwa maadili kwa upande wake, mpatie moyo wa toba ili yeye aweze kuja mbele Zako na kutakaswa kutoka kwa madhara yaliyotokana na uchafuzi na matokeo yake. Ninaomba kwamba asishawishiwe kamwe na njia iendayo kwenye uharibifu. Fungua

macho yake kwa kila uwongo unaowasilishwa kama Ukweli. Mwezeshe yeye kupinga majaribu yote. Mpatie "roho ya hekima na ufunuo" ili yeye aelewe kusudi ulililoweka kwa ajili yake na asiweze kukengeuka (Waefeso 1:17-18).

Bwana, umesema dhambi hutokea kwa kutazama tu kitu kibaya (Mathayo 5:28). Lakini ulitupatia njia ya kuondokana na tabia hiyo (Mathayo 5:29). Ninaomba kwamba mtoto wangu mtu mzima ataondoa chochote ndani ya maisha yake ambayo humsababishia kuhatarisha usafi wa nafsi Unaotaka. Usifanye nuru iliyo katika macho yake ife kwa sababu ya kuona uchafuzi wa ngono. Msaidie kukutazama Wewe na sio uchafu wowote (Zaburi 123:1). Mruhusu aseme kama Daudi alivyosema, "Sitaweka mbele ya macho yangu neno baya" (Zaburi 101:3).

Ninaomba kwamba tamaa ya sanamu za uasherati, ponografia, upotovu, uasherati, na uasherati katika vyombo vya habari, katika ardhi yetu, katika nyumba zetu, na katika maisha yetu iweze kuvunjika. Ninaomba hasa kwamba watoto wangu watu wazima wasijaribiwe, wasinaswe na kuyumbishwa, au kuchafuliwa na chochote katika hayo Katika Jina la Yesu ninaomba. Amina.

## NGUVU YA NENO

Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na tamaa mbaya kiburi cha uzima havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia.

**1 YOHANA 2:16**

Tubuni, ziacheni sanamu zenu, na kugeuza nyuso zenu mbali na machukizo yenu yote.

**EZEKIELI 14:6**

Ni nani awezaye kupanda katika mlima wa BWANA? Au ni nani awezaye kusimama katika Patakatifu Pake? Ni Yeye aliye na mikono safi na moyo safi, ambaye hakuinua nafsi yake kwa sanamu, wala kuapa kwa hila. Atapokea baraka kwa BWANA, na haki kutoka kwa Mungu wa wokovu wake.

**ZABURI 24:3-5**

Mwenye busara huona mabaya na kujificha; Bali wajinga huendelea mbele wakaumia

**MITHALI 27:12**

Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, ili mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana akiomba kwa bidii

**YAKOBO 5:16**

## OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE KUFURAHIA AFYA NJEMA NA UPONYAJI WA MUNGU

Watoto wangu walilelewa na tabia nzuri. Walijua jinsi ya kula vizuri, kufanya mazoezi, na kupata usingizi wa kutosha. Na hawakuwa wagonjwa sana walipokuwa vijana. Kwa kweli, kila mmoja alipokea tuzo kwa

kuhudhuria masomo kikamilifu walipokuwa katika shule (perfect attendance). Lakini baada ya kuwa peke yao, walipata ugonjwa wa kusahau na "Walisahau" mengi ya yale waliyojifunza. Walikula walivyotaka, hawakufanya mazoezi, na walikuwa na tabia mbaya ya kulala saa sita ya usiku na kuendelea badala ya kulala kabla ya saa nne, na walifanya mambo bila kujali matokeo.

Baada ya kuwa wakubwa na kuondoka nyumbani, ningewaona wakifanya vibaya chaguzi za utunzaji wa miili wao. Kando na kula vyakula visivyofaa na kutofanya mazoezi, pia waliendelea na kazi saa nyingi sana na kuishi mara nyingi bila usingizi mzuri wa kutosha. Kwa sababu najua ni uharibifu kiasi gani mambo hayo yanaweza kufanya kwa mwili, nilikuwa na wasiwasi sana. Nilizungumza nao juu ya tabia hizi mara kwa mara, lakini maneno yangu yakaanguka kwenye masikio ya viziwi. Sio kwamba walikuwa wanaasi kwa makusudi nilichokuwa nikisema; walihisi tu walikuwa na wakati mwingi wa kurekebisha njia zao. Baadaye walitetea vitendo hivyo vya uzembe kwa kusema kwamba ni kwa sababu walikuwa na afya njema na kwa vile karibu miaka yao yote ya mapema, walitunza afya zao vizuri walidhani kuwa hiyo afya itakuwa hapo kwa ajili yao kila wakati.

Nikijua kwamba wangelazimika kujifunza masomo magumu, niliomba waamke na kuelewa walichokuwa wakijifanyia kabla ya jambo la kutisha halijatokea. “Bwana, awasaidie kuelewa Ukweli kuhusu miili yao kuwa hekalu Lako na kuwafundisha kuitunza. Wapatie umakini mapema kabla ya kuharibu afya zao." Haikuwa mpaka kila mmoja wao alipokuwa na

kusumbuliwa na dalili zisizowafurahisha ambazo zilibadilisha sana njia zao.

Siku hiyo iliwafikia wote wawili wakiwa katika miaka ya ishirini, na kila mmoja alianza kuwa na matatizo makubwa ya afya yake. (Dalili tofauti na kwa nyakati tofauti kwa kila mmoja wao.) wakati dalili fulani katika kila mnoja wao zilianza kuonekana, nilikuwa na kikundi changu cha maombi tukaanza kuomba pamoja nao ili wao kila mmoja apate mwamko kabla hajachelewa.

Binti yangu alikuwa akiugua zaidi kila siku, akionyesha dalili karibu kila sehemu ya mwili wake, lakini madaktari hawakuweza kupata tatizo lake. Alikuwa anapungua uzito sana, jambo ambalo lilimtia hofu kwa sababu alihisi atakuwa msichana asiyevutia kwa kuwa mwembamba sana. Ilionekana kana kwamba shambulio la pande zote lilikuwa likifanywa juu ya mwili wake, na ilikuwa inazidi kuwa ngumu kustahimili. Ili kufupisha kisa hiki, baada ya kuona wataalamu mbalimbali, Mungu alituongoza kwa daktari ambaye alimjaribu kwa mambo mengi na kugundua kuwa ana mzito wa unga wa ngano [gluteni].

Kitu chochote kilicho na ngano au nafaka nyingine yoyote iliyo na gluten yaani kila nafaka isipokuwa mchele na mahindi kimsingi ilikuwa ikiharibu mwili wake. Daktari wake alimweka binti kwenye lishe kali isiyo na gluteni na akaanza kuimarika. Mtaalamu mwingine alipata vyakula vingine ambavyo alikuwa na mzio navyo pia, ambao tunajua sasa ni wa kawaida zaidi kwa wale walio gluteni allergy.

Baada ya kuacha vyakula hivi na kuchukua virutubisho vya asili chini ya ushauri wa wataalamu hawa, maisha yake yaligeuka kabisa. Yeye sasa alianza kuwa na nguvu na afya na ana maisha mapya ndani yake.

Mungu alijibu maombi yetu, lakini bado tunamwomba awe kamili na kuponywa na allergy hizi zote maana zinafanya maisha yake kuwa magumu sana, haswa wakati inapobidi kusafiri. Mungu ni Mungu wa yasiyowezekana, na tunaomba na kuamini kwamba siku moja Mungu atafanya jambo lisilowezekana kwa binadamu na kumweka huru kutoka kwa mzigo huu. Afanye au asifanye hili, yote yako mikononi Mwake. Kwa sasa, Amanda anajifunza njia mpya ya kula, na yeye ana bidii sana kuona kwamba anafanya njia yoyote kuokoa afya yake.

Dalili za mwanangu zilikuwa mbaya kama za binti yangu na kila kukicha zilizidi kutisha. Charles alianza kuwa na mashambulizi makubwa ya kizunguzungu na ganzi upande mmoja wa mwili wake ambao ulimfanya ajisikie kana kwamba alikuwa na kiharusi au mshtuko wa moyo. Alikuwa katika ofisi ya daktari na chumba cha dharura mara kadhaa-emergency room, na kwa kila tukio walimwambia lazima iwe inahusiana na msongo wa mawazo kwa sababu hawakuweza kuona chochote kibaya kwake kwenye uchunguzi wowote wa kidaktari. Matokeo yake, ilipendekezwa kwamba aende kwa mtaalamu wa magonjwa ya akili, ambaye aliweza kuagiza kitu cha kupunguza dalili hizi za mfadhaiko. Alipoenda kwa daktari wa magonjwa ya akili, daktari alisema haiwezi kuwa dhiki ya akili, kwa sababu dalili za msongo haziwezi kutokea upande mmoja tu wa mwili. Kwa

hiyo daktari wa magonjwa ya akili alimtuma kwa daktari wa neva, ambaye alichukua vipimo zaidi na kumwambia kuwa kutokana na dalili zake na a vipimo, ilionekana kwamba alikuwa na sclerosis au sivyo angekuwa na kiharusi kidogo. Akamwambia arudi hospitali wiki iliyofuata kuchukua vipimo vingine vikubwa, kwa gharama kubwa ambavyo vingefunua kwa hakika kama ni mojawapo ya magonjwa hayo.

Mwanangu na mimi sote tuliangalia ugonjwa wa sclerosis katika tiba yetu na kusoma kwenye google search na tuliogopa kuona kwamba alikuwa na kila dalili yake. Kwa kweli, ilionekana kana kwamba hii ndiyo shida hasa aliyokuwa nayo, na tulikuwa na wasiwasi sana. Haya yote ndiyo niliyokuwa nikiomba kwa miaka mingi yasitokee. Kufikiria kwamba mtoto aliyekuwa na afya njema sasa alikuwa na ugonjwa usio na tiba kwa sababu alikuwa amezembea afya yake iliniumiza moyo. Ni hasara gani isiyo ya lazima. Charles pia alikuwa na wasiwasi sana.

Niliita kikundi changu cha maombi kuomba, na mume wangu na mimi na mwana wetu na binti kila mmoja aliomba kwa bidii kila mchana na usiku kwamba haya yasiwe maisha ya daima kwa ajili yake. Lakini ikiwa ni kile tulichoogopa, tuliomba kwamba Mungu alete uponyaji kwa mwili wake. Mapema asubuhi moja nilipokuwa katika ombi hili, nilimkumbusha Mungu kwamba mimi nilikuwa nimeomba kila siku kwa ajili ya afya ya mwanangu tangu alipozaliwa na hata kabla. Na nilisali kwa bidii kila siku ili akiwa mtu mzima awe na afya njema na asiudhulumu mwili wake.

Ndipo Mungu akaleta Maandiko moyoni mwangu alisema watumishi wa

Bwana hawatazaa watoto kwa taabu na hivyo sisi tunaomtumikia Mungu tungebarikiwa na watoto wetu pia (Isaya 65:23). Mwanangu aliwekwa wakfu kwa Bwana tangu alipozaliwa, na akaombewa kila siku ya maisha yake. Nilihisi Mungu alikuwa akisema kwamba tunapaswa kuamini kwamba yeye hakuzaliwa kwa ajili ya shida.

Nilishiriki hilo na mwanangu na binti yangu na mume, na sote tukaomba, “Asante, Bwana, kwamba Charles hakuletwa kuishi kwa shida." Wakati hatimaye tulipopata matokeo ya MRI siku kadhaa baadaye, tuligundua ilikuwa sio sclerosis baada ya pilikapilika zote, wala haikuwa kiharusi. Hatimaye, tuligundua kuwa yeye ana mzio sana kwa artificial sweetener au sukari bandia-inayopatikana katika vinywaji fulani vya cola na alikuwa akitumia kila siku. Tukampeleka pia kwa mtaalamu aliyemhudumia binti yetu na tukagundua kuwa ana mzio wa mambo mengine pia. Mwili wake ulikuwa na usawa maalum baadda ya kutibiwa na virutubisho, lishe sahihi, na matibabu ya mzio. Yeye ni mtu mpya saa. Yeye anakula vizuri ajabu. Ana stamina, anaonekana mwenye nguvu na ni mzima wa afya.

Na sasa watoto wangu wote wawili ambao ni watu wazima hufanya mazoezi mara kwa mara kila wiki nyumbani kwao katika chumba cha mazoezi na mara nyingi na mkufunzi mtaalamu ambaye anafanya kazi huko-health coach.

Matokeo ya visa hivi viwili ni muujiza kwetu sote, kwa sababu huko kulikuwa na nyakati ambapo kila mmoja wao alikuwa katika mapambano yake na yalionekana kuwa makubwa na kulikuwa hakuna dalili ya

mafanikio. Lakini tulipoanza kuvunjika moyo, tulisali sote zaidi. Tulikuwa tukidumu katika maombi kwa sababu tulikuwa na imani na azimio la kutokata tamaa hadi tuone uponyaji na msaada tuliohitaji. Mwana na binti yangu wameona mabadiliko makubwa katika maisha yao. Wao kila mmoja anahisi kwamba amepewa maisha mapya na anataka kuwasaidia wengine kujisikia vizuri pia. Kama matokeo, mwanangu anafanya kazi katika nyumba ya mtaalam wa lishe huku akifanya kazi binafsi kama mtayarishaji wa rekodi na mtunzi wa nyimbo. Yeye aliona ni mabadiliko gani ya ajabu yanaweza kutokea katika miili yetu tunapoishughulikia. Binti yangu amesoma, na ana ujuzi katika, aina tofauti za tiba ya mwili kwa sababu Anajua nguvu ya uponyaji ya haya yote na anataka kusaidia wengine wasiwe na maumivu na kupata afya bora na uponyaji.

Sikuwahi kufikiri kwamba ningemwona yeyote kati ya watoto wangu wazima akifanya mojawapo ya haya mambo. Na hakika sikuwahi kufikiria ningeona siku watakapokuwa wakinipa ushauri wa kiafya, ambao wote wawili wanafanya sasa mara kwa mara. Ni tofauti gani kutoka miaka michache iliyopita wakati nilikuwa na wasiwasi sana juu ya wote wawili ambapo niliomba mchana na usiku kwa ajili ya afya zao. Mungu hakuwaponya tu, lakini pia aligeuza maisha yao kabisa. Ikiwa umewahi kuangalia tabia za afya za watoto wako wakubwa na kujisikia wasiwasi, jua kwamba maombi yako kwa ajili ya wao kugeuka hayaanguki kwenye masikio ya Mungu aliye kiziwi. Yeye Atakusikia na kukujibu. Usiache tu kuomba, hadi uone matokeo.

## KUJIFUNZA KUDUMISHA AFYA BORA

Ninashughulikia huduma ya afya na uponyaji katika sura hii kama masuala mawili tofauti. Huduma za afya ni kitu tunachofanya ili kulinda miili yetu. Tunaitendea haki na kwa kujali. Uponyaji ni kitu tunachoomba na Bwana hujibu maombi yetu. Mungu anatutazamia tuwe mawakili wazuri juu ya yale anayotupa ndani ya miili yetu. Yeye Anataka tuijali na tusiinyanyase kwa njia yoyote ile. Inasikitisha lakini ni kweli kwamba tuna bidii zaidi juu ya kutunza afya zetu baada ya kuiharibu au kuipoteza. Tunaweza kuwa na uzembe wa kutisha wa miili yetu wakati tunafikiri tunaweza kupata na tuna tabia ya kupuuzia afya zetu kadri tuwezavyo. Sote tunaweza kuwa na visingizio visivyoisha kwa nini hatujitunzi vizuri zaidi. “Mimi pia "Sina motisha." "Ninapata shida sana." "Sijui la kufanya." "Sina thamani." "Sihitaji kabisa." Tunaona ni vigumu kuwa na nidhamu, au sisi tuko wazi kwamba hatutaki kufanya hivyo.

Mwombe Mungu awaonyeshe watoto wako watu wazima kitu cha kufanya ili kudumisha afya njema. Mwambie awafundishe nini cha kula, jinsi ya kufanya mazoezi, na nini cha kufanya au nini usifanye ili kupata usingizi mzuri. Muombe Mungu awape hekima ya kufanya maamuzi sahihi kwa afya njema, utambuzi wa kujua ni nini kinachofaa kwao na kisichofaa, na ufunuo juu ya kile kinachofaa kwa mwili wao.

## KUMJUA YESU KAMA MPONYAJI WAO

Yesu Ndiye Mponyaji wetu, na kuwa na hakika juu ya hilo ni lazima.

Mungu anajua hatuwezi kufanya kila kitu kikamilifu, na ndiyo sababu alimtuma Yesu sio tu kutuokoa, kutusamehe sisi, na kutukomboa kutoka kwa adui, lakini pia kutuponya. Pamoja na kuwaombea watoto wetu watu wazima wawe na tabia njema za kiafya, lazima pia wao wasali ili wamjue Yesu kuwa Mponyaji wao. Kutakuwa na nyakati watakapougua au kujeruhiwa, na lazima wajue jinsi ya kuombea uponyaji katika Jina la Yesu. Utunzaji wa afya zao unaposhindwa, wanahitaji nguvu za Mungu kuwafanya wajisikie vizuri. Anaweza kufanya hivyo kwa msaada wa madaktari, kwa kufichua kwao kitu ambacho wanahitaji kujua na kufanya, au kwa kazi Yake kuu.

Baada ya Yesu kusulubishwa, kufufuka, na kupaa mbinguni, Mungu akamwaga Roho Wake juu ya wanafunzi wa Yesu. Petro, akisha kujazwa na Roho Mtakatifu alikwenda pamoja na Yohana mpaka Hekaluni, akamwona mtu mmoja aliyekuwa kiwete tangu kuzaliwa akiwa ameketi langoni akiomba pesa. Petro akamwambia yule mtu maneno haya maarufu sana, "Fedha na dhahabu sina, lakini nilicho nacho ndicho ninachokupa. Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama, uende" (Matendo 3:6). Ndipo Petro "akamshika mkono wa kuume, akamwinua, na mara miguu yake na vifundo vya miguu yake vikatiwa nguvu" (Matendo 3:7). Akaruka akainuka, akatembea, akamsifu Mungu, na watu waliomwona akitembea "wakajaa kwa mshangao na kustaajabia yaliyompata" (Matendo 3:10).

Petro alipoona mwitikio wa watu, akasema, "Mbona mnatutazama sisi? kana kwamba kwa nguvu zetu wenyewe au kwa utauwa wetu tumemfanya

mtu huyu aende? (Mdo 3:12). Alieleza kwamba ni Mungu, akimtukuza Mwanawe, Yesu, ambaye alikuwa naye akafufuka kutoka kwa wafu. Kisha ikaja sehemu muhimu zaidi ya kisa hiki. Petro alisema, “Na katika Jina Lake kaw Imani, limemtia nguvu mtu huyu ambaye ninyi mnamwona na kumjua. Ndiyo, imani ile iliyo Kwake Yeye imemfanya huyu kuwa mkamilifu na mzima mbele yenu nyote” (Matendo 3:16).

Petro anasema kwamba haikuwa kwa uwezo wake wowote maalum mtu huyu aliponywa, lakini kwa nguvu ya Jina la Yesu. Imani katika Jina la Yesu inaleta nguvu inayoponya, na maombi huelekeza nguvu ya kutuletea uponyaji. Huu ni muujiza wa kwanza kurekodiwa kuwa ulifanywa na mmojawapo wa wanafunzi wa Yesu. Na kwa kusimulia kile kilichotokea, tunaweza kuona jinsi ya kuomba. Petro aliamuru kuponywa kwa yule kiwete, lakini aliomba kwa Jina la Yesu Kristo wa Nazareti. Kwa kunena Jina kamili la Yesu, cheo Chake, na alikotoka, hakukosea alikuwa anazungumza juu ya nani.

Petro alikuwa akisema kwamba uponyaji ulikuja kupitia kwa Yesu Huyu na si kwa njia nyingine. Kama tukio hili la uponyaji lilikuwa muhimu vya kutosha kujumuishwa katika Biblia, ni muhimu vya kutosha kwetu kukumbuka wakati tunawaombea watoto wetu watu wazima, na sisi wenyewe au mtu mwingine yeyote.

Tunapokiri kwamba Yesu Kristo ni Bwana, na ametupa nguvu na mamlaka katika Jina Lake kuamuru magonjwa yaondoke. Kwa hivyo inatubidi kuomba kwa ajili ya imani inayoongezeka kila mara ili kuamini kwamba

kile ambacho Biblia inasema ni Kweli, na anayosema Yesu ni Kweli yote [Absolutel Truth]. Tunapaswa kuomba kwamba kwaajili ya tumaini ndani yetu sisi, kwa sababu ya yale ambayo Yesu ameyakamilisha kwa niaba yetu, sisi hatutashindwa kamwe au kudhoofika.

Yule mtu aliyekuwa kilema tangu kuzaliwa aliponywa kwa sababu ya nguvu za Jina la Yesu.

Je, Jina la Yesu lilikuwa na nguvu tu Petro aliposali katika Jina hilo? Au Jina la Yesu Kristo lina nguvu wakati yeyote anayeamini anapoomba kwa Jina hilo? Ninaamini ya kwamba kama Mungu ni Yeye Yule Yule jana, leo, na hata milele, na kile ambacho Yesu alitimiza msalabani kilitimizwa kwa nyakati zote na kwa watu wote, basi uweza wa Jina Lake ni kwa ajili yetu sisi tunaoamini sasa. Haikuwa kwa ajili tu ya Petro na Yohana wakati huo.

Biblia mara nyingi huwekewa vikwazo na baadhi ya watu wakisema, "Sehemu hii ilikuwa tu kwa wanafunzi, sehemu hiyo ilikuwa kwa ajili ya Wakorintho tu, sehemu hii ni kwa ajili ya Waisraeli tu," na kuendelea hadi Biblia nzima ifafanuliwe na inakuwa kitabu cha historia tu, na ambacho mara nyingi ni kigumu kuelewa.

**Usiruhusu** wanadamu kuondoa kile ambacho Mungu amekupa katika Neno Lake. Usiruhusu wakuambie Mungu Yuko kimya na haongei na watu tena. Au kwamba Yeye haponyi watu tena. Au kwamba hafanyi miujiza tena. Yeye ni Yule Yule jana, leo, na hata milele, ama sivyo. Biblia inatuambia Mungu ni nani. Usiruhusu mtu yeyote aibe uponyaji wako kwa kudhoofisha

imani yako katika Jina la Yesu na uwezo Wake wa kuponya. Yeye Alikuwa Ndiye Mponyaji. Yeye Ndiye Mponyaji, Mkuu, Tabibu Mkuu Mwenye Upendo Mwanana na huruma nyororo. Yeye daima atakuwa Mponyaji.

## NJIA TANO ZA KUOMBEA AFYA NA UPONYAJI KWA WATOTO WAKO WAKUBWA

1. Omba ili watoto wako watu wazima waelewe jinsi mwili wao ni muhimu kwa Bwana. “Je, hamjui kwamba miili yenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu, nanyi si mali yenu wenyewe? Kwa maana mlinunuliwa kwa thamani; basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu” (1 Wakorintho 6:19-20).

2. Omba kwamba watoto wako wakubwa waishi njia ya Mungu. "Kwa kuwa njia ya haki ni uhai, na katika mapito yake hakuna mauti” (Mithali 12:28).

3. Omba ili watoto wako wakubwa wamjue Mungu kama Mponyaji wao. “Mimi Ndiye BWANA nikuponyaye” (Kutoka 15:26).

4. Omba kwamba watoto wako wawe na imani thabiti ya kuomba uponyaji. “Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa, na Bwana atamwinua. Na ikiwa amefanya dhambi, atasamehewa” (Yakobo 5:15).

5. Omba ili watoto wako waponywe na Mungu. “‘Kwa maana nitarudisha

afya kwako na kukuponya/kukuganga jeraha zako, asema BWANA" (Yeremia 30:17).

## OMBA UJASIRI WA KUZUNGUMZA NENO LA MUNGU LA UPONYAJI

Baada ya Petro na Yohana kutoka gerezani na kwenda kwa wenzao ili kuwaeleza yaliyotokea, waliomba pamoja wakisema, "Bwana, Wewe Ndiwe Mungu, uliyezifanya mbingu na nchi na bahari na vyote vilivyomo...Sasa, Bwana, tazama vitisho vyao, na uwajaalie waja Wako wapate kwa ujasiri wote kunena Neno Lako, kwa kunyosha mkono Wako wa kuponya, na hizo ishara na maajabu yanaweza kufanywa kupitia Jina la Mtumishi Wako mtakatifu Yesu.' Na walipokuwa wameomba, mahali pale walipokusanyika pakitikiswa; na wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakanena nao Neno la Mungu kwa ujasiri" (Matendo 4:24,29-31).

Mtikisiko huu wa nguvu ulitokea kwa sababu waliomba pamoja kwa umoja, usadikisho uleule, kwa imani, na nia. Walimwomba Mungu awawezeshe kuzungumza Neno Lake kwa ujasiri. Wakamwomba anyooshe mkono Wake na kuponya na kufanya ishara na maajabu kwa jJina la Yesu. Na Mungu alijibu maombi hayo kwa njia yenye nguvu. Sisi pia tunaweza kumwomba Mungu atusaidie kusema Neno Lake kwa ujasiri, hasa aya za Maandiko zinazohusu uponyaji. Wewe tafuta baadhi ya Maandiko hayo chini ya "Neno Nguvu" katika ukurasa wa mwisho wa hii sura. Mwombe Mungu akuwezeshe kunena Neno la Mungu kwa ujasiri siku ya leo.

Kufanya hivyo huongeza imani yako kuamini kwamba Mungu anaweza na atakuponya kwa Jina la Yesu.

## UNAPOKABILIANA NA VITISHO VIKUBWA VYA AFYA

Ikiwa mtoto wako mkubwa anakabiliwa na tishio kubwa kwa afya yake, sali pamoja na watu wengine wa imani wanaoamini kama unavyoamini kwamba Yesu Ndiye Mponyaji na hivyo maombi katika Jina Lake yana nguvu ya kutosha kuleta uponyaji. Zungumza Neno la Mungu kwa Imani, na kumsifu Mungu kwa uweza Wake mkuu unaotenda kwa niaba yetu. Mwombe Mungu akuonyeshe ikiwa kuna uasi wowote katika njia za mtoto wako mtu mzima. Musa alipowatoa wana wa Israeli kutoka Misri, wakavuka Bahari ya Shamu, na katika jangwa, alimlilia Mungu amsaidie kupata maji ya kunywa. Bwana alimwonyesha jinsi ya kusafisha maji machafu na kisha akamwambia kwamba ikiwa wangeshika amri za Bwana na kufanya alichowaambia kufanya, angewalinda na magonjwa na kuwaponya (Kutoka 15:26).

Mungu aliweka wazi kwamba tunapaswa kuishi kwa njia Yake ikiwa tunatarajia kuwa na afya na uponyaji. Mara nyingi tumeiumiza miili yetu, tumeishi bila amani au furaha. Kuna nguvu katika Jina la Yesu kwa sababu ya kile alichotimiza juu ya msalaba. Sio nguvu ya imani yetu, kana kwamba tunaitimiza. Uponyaji hutokea kwa sababu tunaweka imani yetu katika Jina la Yesu. Nguvu iko katika Jina Lake.

Adui wa nafsi zetu daima anataka kutushawishi kwamba hatuna tumaini katika udhaifu wetu na hakuna njia ambayo Mungu atatuponya sisi au watoto wetu watu wazima. Anajua pia kwamba kukosa tumaini hutudhoofisha kama vile magonjwa. Kwa kweli, mimi nina uhakika kwamba kukata tamaa kupita kiasi kunachangia kudhoofika vibaya, na kutokulala usingizi wa kutosha au kutokufanya mazoezi. Au tukifunga ndani a nfasi  dhambi ambayo inafungua mlango wa udhaifu au ugonjwa. Mwombe Mungu akuonyeshe wewe ukweli kuhusu watoto wako wakubwa.

Kuna nyakati ambapo uponyaji utatokea mbinguni, na hiyo sio jibu tulikuwa tunaomba au tulitaka kusikia. Ikiwa hiyo itatokea kwa mmoja wa watoto wako, ombeni uponyaji wa Mungu mioyoni mwenu na marejesho ya roho zenu. Hapana mtu anapaswa kumzika mtoto wako anapokuwa katika maombi mpaka Mungu atakapoingilia kati. Lakini wakati wa kufa kwa mtu yeyote uko mikononi mwa Bwana kabisa. Tumaini lako ni kwamba utamwona mtoto wako tena mbinguni. Ikiwa unajua mtoto wako aliyekufa alikuwa amempokea Bwana, basi unajua utakutana naye Bwana atakaporudi. Ikiwa hujui kama yeye amempokea Bwana kabla ya kifo, basi hujui kwamba yeye hakujua pia. Huwezi kujua kama katika wakati wa mwisho kabla ya mtu kufa, alipata utambuzi kamili wa Yesu ni nani, na akampokea kama Mwokozi. Mungu pekee Ndiye anayejua kwa hakika.

Uwe na amani kwa kujua kwamba ni mapenzi ya Mungu kwamba hakuna yeyote atakayeangamia. Kwa kujua upendo na wema wa Mungu kama nijuavyo, sina shaka kwamba Yeye ni miongoni mwa waliokombolewa

wengi kabla ya kifo kitu ambacho huwezi hata kujua. Tukiwa pamoja na Bwana, daima kuna tumaini la kuwaona watoto wetu tena hata wangekuwa na umri gani walipoiaga dunia hii.

Ninaamini siku zote ni mapenzi ya Mungu ni kuponya. Kwa nini Yesu aje kama Mponyaji wetu kama hakutaka kutuponya? Kwa nini inasemwa sana basi katika Biblia kuhusu kutuponya, na miujiza Yake mingi aliifanya kwa uponyaji wa kiroho, kimwili na kiakili, na ilisemekana hata hakusalia mmoja aliyekuwa mgonjwa ambaye alimjia, isipokuwa pale watu walikuwa hawaamini uweza Wake. Kwa nini sio kila mtu anayeomba kuponywa anapata uponyaji? Ni Mungu pekee anayejua. Mwambie Mungu akuonyeshe jinsi ya kudai ahadi Zake za uponyaji na kuweka imani katika nguvu ya uponyaji ya Jina la Yesu. Haijalishi ni daktari gani ametoa ripoti, wewe usiache kuomba kwa ajili ya uponyaji kamili. Omba kila siku ili mtoto wako mkubwa aishi maisha marefu na yenye afya.

## NGUVU YA MAOMBI

Bwana, naomba kwamba ……….. (jina la mtoto mzima) atafurahia afya njema na maisha marefu. Mpe yeye hekima na ujuzi unaohitajika kutambua kwamba mwili wake ni hekalu la Roho Mtakatifu na kwamba unapaswa kutunzwa na kulelewa na sio kupuuzwa au kudhulumiwa. Msaidie yeye kuthamini afya njema kama zawadi kutoka Kwako ili kulindwa na sio kuharibiwa kwa upumbavu au kutojali kwa namna wanavyoishi. Ingiza

ndani ya moyo wake ufahamu wa kutokuharibu afya njema uliyompa 3Yohana 1: 2.

Mfundishe yeye jinsi ya kufanya maamuzi ya busara na kukataa chochote kile kinachodhoofisha afya njema. Fichua ukweli wowote unaohitaji kuonekana, na umpe yeye kuelewa. Mfundishe kuwa na nidhamu katika namna ya kula na kufanya mazoezi na kupumzika vizuri. Msaidie kuuleta mwili wake katika utii (1 Wakorintho 9:27). Mpe hekima na utambuzi ajue ni lipi la kufanya na lipi asifanye na kuhusu lililo jema na lililo baya. Msaidie kutambua mahali popote ambapo yeye ametoa nafasi kwa kutojali afya yake na kisha aachane na tabia zinazoharibu maisha yake. Msaidie kuuthamini mwili wake na kuutunza, na kumfundisha njia sahihi ya kuishi hasa katika ulimwengu wa media, mitandao ya kijamii, simu za mkononi, kompyuta na televisheni, hivi vinatakiwa kumilikiwa kwa kutawala nafsi. Mpatie kujifunza zaidi kuhusu akili mnemba na madhara yake na hata akili ya hisia (emotional intelligence), haya yatamsaidia katika kudhibiti mambo mengi na kuishi na watu vyema. Mwombe kwa haya pia.

Ninaomba kwamba yeye ajifunze kuomba kwa nguvu kwa ajili ya uponyaji wake. Mpatie imani kuu katika Jina la Yesu. Mpe ufahamu na maarifa ya kudai uponyaji ambao ulipatikana pale msalabani. Mahali popote katika mwili wake palipo na magonjwa, udhaifu, au jeraha, naomba umguse na kuleta uponyaji kamili. Msaidie asikate tamaa kusali mpaka yeye aone uponyaji kamili ulio nao kwa ajili yake yeye. Kama uponyaji wake ni wa papo hapo au unajidhihirisha katika kupata nafuu taratibu, na kushukuru

kwa muujiza wa uponyaji Utakaofanya katika mwili wake. Mwezeshe kuona kwamba ni Wewe uliyeponya na si nguvu za kibinadamu au marafiki waelewa mlio nao. Waongoze madaktari wote wanaomwona na kumtibu. Wawezeshe kutengeneza utambuzi sahihi na kujua nini cha kufanya. Ambapo uponyaji inaonekana kuwa ni wa muda mrefu ujao, utusaidie tusikate tamaa wala tumaini, bali tuongeze nguvu na bidii katika maombi yetu.

Wakati wowote yeye ni mgonjwa, naomba Uwe Mponyaji wake. Ninaomba uponyaji kwa ………… (jina la mtoto mzima) na ninaomba haswa uponyaji wa ………………………. (eneo la mwili ambalo linahitaji uponyaji). Mrejeshee afya na apone majeraha yote (Yeremia 30:17). Mpe ujuzi na imani ya kusema, "Ee BWANA wangu Mungu, nalikulilia, Ukaniponya" (Zaburi 30:2). Uniponye Ee Bwana nami nitaponyeka uniokoe nami nitaokoka kwa maana wewe ndiwe uliye sifa yangu (Yeremia 17:14). Msaidie yeye awe msimamizi mzuri wa mwili wake na alipe uzito jambo la afya njema. Mfundishe kuelewa kwamba yeye anapaswa kuwasilisha mwili wake kama dhabihu iliyo hai, takatifu na yenye kukubalika Kwako (Warumi 12:1). Mwezeshe kuelewa wazo la kukutukuza katika uangalizi wa mwili wake, kwa sababu ni makao ya Roho Wako. Katika Jina la Yesu ninaomba. Amina.

## NGUVU YA NENO

Ee nafsi yangu, umhimidi BWANA, wala usizisahau fadhili Zake zote; akuponya magonjwa yako yote, aukomboa uhai wako na kaburi; akuvikaye

fadhili na rehema.

**ZABURI 103:2-4**

Uniponye, Ee BWANA, nami nitaponyeka; niokoe, nami nitaokolewa kwa ajili Yako Nami nitakusifu daima.

**YEREMIA 17:14**

Ukiisikiza kwa bidii sauti ya BWANA, Mungu wako, na kufanya yaliyo sawa machoni pake, ukizisikiliza amri Zake, na kuzishika amri Zake zote, sitaweka hata moja magonjwa juu yenu ambayo nimewaletea Wamisri. Kwa maana Mimi Ndimi BWANA nikuponyaye.

**KUTOKA 15:26**

Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona.

**ISAYA 53:5**

Lakini kwenu ninyi mnaolicha Jina Langu, Jua la Haki litawazukia pamoja na kuponya katika mbawa Zake; nanyi mtatoka na kunenepa kama ndama waliolishwa.

**MALAKI 4:2**

## OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE KUFURAHIA NDOA YENYE MAFANIKIO NA KULEA WATOTO WACHA MUNGU

Mojawapo ya mambo muhimu zaidi katika akili zetu kama mzazi na moja ya tamaa kubwa ya mioyo yetu kwa watoto wetu watu wazima ni kuona kwamba watafanya chaguo sahihi linapokuja suala la kuchagua mwenzi wao wa maisha. Jambo la mwisho tunalotaka kuona likitokea ni talaka katika maisha yao ya baadaye. Ingawa sio mwisho wa hatima ya mstakabali wa wanadamu kabisa ikiwa wataachana, au wakaendelea kuishi maisha mazuri. Talaka sio matokeo yanayotarajiwa, tusingependelea waipate. Ndio maana inatubidi tuombe kwa bidii ili watoto wetu wakubwa wapate hekima juu ya uamuzi huu muhimu. Sote tunajua jinsi ilivyo rahisi kufikiria ikiwa watakutana na mtu nyakati nyingine talaka haiepukiki, kama vile mtu anapofunga ndoa na mtu ambaye ni mnyanyasaji, asiyewajibika, asiye na maadili, asiyevumilika, hatarishi, au amefungwa bila tumaini na ushawishi mbaya. Ikiwa mtoto wako mtu mzima tayari amefanya kosa kama hilo na limeishia kwa talaka, unaweza kuomba kwamba kusiwepo talaka katika maisha yake ya baadaye. Unaweza kuomba leo kwamba roho ya talaka isiwe na fungu lolote katika maisha yake kuanzia sasa. Omba kwamba mtoto wako mkubwa aoane na Muumini.

Jambo la kwanza na muhimu zaidi kwa mzazi wakati wa kuomba juu ya

nani ataoana na mtoto wao mtu mzima, ni kwamba awe mtu ambaye ni muumini na mcha Mungu. Kuna mambo fulani unaweza na unapaswa kuwauliza watoto wako watu wazima. Hili ni mmoja wao. Hili sio tu kwamba ni jambo la mzazi kusumbua, au njia ya kufanya hivyo ili kujaribu na kudhibiti maisha yao, lakini unaweza kuweka wazi kwamba nia yako kubwa kwao ni waoe au kuolewa na waumini, kwa sababu ni mapenzi kamili ya Mungu kwao.

Muumini ni mtu ambaye mtoto wako wakubwa anaweza kujenga nae maisha imara juu ya msingi thabiti katika njia za Mungu. Mawazo ya mwanao au binti kuolewa na mtu ambaye si muumini wa Mungu, au mbaya zaidi, ambaye ni kinyume na Mungu jambo ambalo, linasikitisha. Ndoa ni ngumu vya kutosha bila msingi thabiti katika Bwana. Walakini, ikiwa mtoto wako mtu mzima tayari ameoa mtu ambaye sio muumini, pata faraja kwa kujua kwamba ni mapenzi ya Mungu kujibu maombi juu ya wokovu. Unaweza kuomba kwamba Mungu amguse mkwerima wako au binti mkamwana wako kwa upendo Wake na Ukweli na kumleta katika ufalme.

Omba Mungu akutumie wewe na waumini wengine pamoja na mume au mke wa mtoto wako mtu mzima ili kwamba njia za upendo wa Mungu zitakua katika maisha yao. Wanawake wawili ambao wamekuwa karibu sana nami katika maisha yangu wameolewa na waume wasio wa dhehebu letu, na wanaume hao ni watu wawili wema niliopata kuwafahamu maisha yangu yote. Wao ni Wakristo bora kuliko wengi wetu ambao ni tunasema tu Waamini. Wao tayari wana mtindo mzima wa maisha ya Kikristo chini;

sasa ni suala lao wakikiri mioyoni mwao ya kuwa Yesu ni Bwana. Wanajua jinsi ya kuishi kwa njia ya Mungu bila kumjua Mungu. Lakini wanahitaji uhusiano huo na Yesu, na utimilifu wa Roho Mtakatifu ndani yao, ili kuwa na wakati ujao wa milele pamoja na Bwana na baraka nyingi zaidi sasa. Hatuachi kuombea hilo na kuamini Mungu atavunja kutokuamini kwao.

Katika Biblia, Isaka na Rebeka walikasirika sana mwana wao mwenye umri wa miaka 40 Esau, alipooa katika jamii isiyomcha Mungu iliyo nje ya imani na utamaduni wa familia yake, na alikuwa na wake wengi wasioamini (Mwanzo 26:34). Jambo hili lilileta huzuni mioyoni mwa Isaka na Rebeka" (Mwanzo 26:35). Esau alijua kwamba jambo hilo liliwachukiza wazazi wake, lakini hata hivyo aliwaoa. "Esau akaona kwamba binti za Kanaani hawakumpendeza Isaka baba yake" (Mwanzo 28:8). Watoto wa Isaka walitenda mmoja kwa ujinga na kisha mwingine kwa busara. Mmoja aliwatii wazazi wake, na mwingine hakuwatii. Mmoja alitekeleza ahadi katika ukoo wa familia yake, na mwingine hakufanya hivyo. Mmoja alikuwa na akili juu ya maadili ya juu, na mwingine hakufanya hivyo. Mmoja alioa muumini, na yule mwingine hakufanya hivyo. Kabla ya hayo yote kutokea, Esau alikuwa ameuza haki yake ya uzaliwa wa kwanza, urithi wa familia yake. yeye akauza kwa ndugu yake kwa ajili ya chakula alipokuwa na njaa. Esau angerithi sehemu kubwa ya mali ya baba yake na kubeba jina la familia. Hata hivyo, kwa sababu alikuwa daima na tabia ya kutenda bila hekima hakuwa tayari kungoja na kufanya lililo sawa, alipoteza yote.

Tunaona katika kisa kichungu ambacho wazazi wake walipata wakati Esau alipooa asiyeamini. Wazazi wowote wanaoamini watapata uchungu huo kwa sababu wanataka jambo bora kwa watoto wao watu wazima. Ndio maana inabidi uombe kwamba mtoto wako mtu mzima atapata mume au mke kutoka katika familia ya waumini. Omba pia kwamba mtoto wako mtu mzima atakuwa kila kitu anachohitaji kuwa katika Bwana ili aweze kukutana na mtu mcha Mungu na wa ajabu wa kuoana naye. Bila Bwana, ndoa ni kamari kubwa zaidi ambayo mtu anaweza kuicheza. Hakuna njia ya kutabiri matokeo ikiwa wewe hutamkaribisha Mungu na kumwomba amdhihirishe mtu sahihi na kwa wakati sahihi.

Moja ya mambo ambayo tumeomba mara kwa mara katika kila moja ya vikundi vya maombi ambavyo nimekuwa navyo kwa wazazi ni kwamba kila mtoto wetu atakua hadi kuoana na mwanamume au mwanamke wa ajabu, mcha Mungu, anayeamini. Hadi leo, kila mtoto mzima ambaye ameolewa sasa ameolewa, amepata na mtu mzuri, mcha Mungu, muumini pamoja na watoto wangu mwenyewe. Tunapoona ni nani kati ya hawa vijana wamechagua, tunamsifu Mungu, tukijua ni Yeye pekee angeweza kuweka wanandoa pamoja kikamilifu.

Mume wangu na mimi tulisali kwa miaka mingi kuhusu jambo hilo, na nina hakika sala zetu zimesababisha kuacha makosa machache. Kulikuwa na simu za karibu ambapo watoto wetu walioana na mtu ambaye aligeuka kuwa mtu mbaya. Si kwamba watu hao walikuwa watu wabaya. Kwa kweli, walikuwa wacha Mungu kabisa, watu wa ajabu, waaminio, lakini

hawakuwa tu watu sahihi kwa watoto wetu watu wazima. Mwana wetu na binti yetu hawakukutana na wenzi wao hadi walipofikisha miaka ya thelathini. Mkamwana wetu na mkwe wetu ni waumini wenye nguvu katika Yesu na watu wa ajabu. Hatuwezi kuwa na furaha zaidi au kumshukuru Mungu vya kutosha.

Mfano mwingine katika Maandiko wa kujali na maombi ya mzazi juu ya mtu mzima juu ya mwenzi wa baadaye wa mtoto alikuwa Abrahamu. Hakutaka mwanawe, Isaka, aoe mtu asiyeamini pia. Huyu Ndiye Isaka. Kwa hiyo tunaona Abrahamu, baba wa Isaka, alihangaikia sawa na vile Isaka alivyohangaikia maisha ya wanae baadae yaani, Esau na Yakobo. Abrahamu alitaka kuhakikisha kwamba mtoto wake haoi mmoja wa wale wanawake wasioamini wa Wakanaani wasiomcha Mungu, lakini wangeoana na mtu kutoka katika imani yake mwenyewe. Kwa hiyo alimwagiza mtumishi wake aliyemwamini zaidi amtafutie Isaka mke. Akasema, Nitakuapisha kwa BWANA, Mungu wa mbinguni, na Mungu wa nchi, usije ukamtwalia mwanangu mke katika binti za Wakanaani, ambao ninakaa kati yao; lakini utakwenda katika nchi yangu na watu wangu ukamtwalie mwanangu Isaka mke" (Mwanzo 24:3-4).

Mtumishi alikuwa na wasiwasi kwamba mwanamke hangekuwa tayari kuja na arudi pamoja naye na akafikiri kwamba Isaka anapaswa kwenda pamoja naye. Lakini Abrahamu alisema hapana kwa sababu fulani, na akamwambia mtumishi kwamba Mungu amesema naye angemtuma malaika wake atangulie kumtengenezea mtumishi Wake njia ya kumpata mke sahihi kwa

ajili ya Isaka (Mwanzo 24:5-7).

Ibrahimu ni wazi alikuwa akiwasiliana na Mungu kuhusu hili na kuomba hasa kuhusu mke kwa ajili ya mwanawe. Alikuwa na uongozi wa Bwana alipomwagiza mtumishi wake aende katika nchi ya watu wake kumtafuta. Kwa hivyo basi, mtumishi angekuwa akifuata mwongozo wa Bwana anapoenda huko.

Mtumishi aliondoka kama alivyoagizwa na kuomba kwamba Mungu ampe mafanikio (Mwanzo 24:12). Alipofika katika nchi ya ukoo wa Ibrahimu, akakaribia kisima ambako watu wa mjini walikwenda kuteka maji, alimwomba Mungu Amuonyeshe mke wa Isaka angekuwa nani. Aliomba hasa ishara-kwamba msichana kisimani ambaye alimwomba ampe maji ya kunywa asikubali tuu kumpa maji, lakini pia angewanywesha ngamia wake maji. Ikiwa hiyo ingefanyika, angejua kwamba huyo ndiye mwanamke ambaye Mungu alikuwa amemchagua kuwa mke wa Isaka (Mwanzo 24:13-14).

Kwenye kisima alikutana na Rebeka bikira na binti mrembo aliyekuja kuteka maji. Hakumpa mtumishi maji tu, bali yeye mwenyewe pia alijitolea kuteka maji kwa ngamia zake (Mwanzo 24:15-20). Na bado wakati yule mwanamke alikuwa akiteka maji kisimani, mtumishi akaomba tena kimya kimya huku akisubiri kusikia kutoka kwa Mungu ili kuhakikisha kuwa huyu ndiye mwanamke ambaye alikuwa amemchagua. Hakika huu ni muujiza, maana watu wengi hawapendi kuwasaidia wengine kama shuguli yake ni kubwa, ngamia 10 ni wengi, kwani kila mmoja hunywa wastani wa galoni

50, na hivyo galoni 500 za maji! Je, hizi ni lita 1800?

Akiwa amehakikishiwa na Mungu kwamba yeye ndiye, mtumishi huyo, alimpa Rebeka vito vilivyotumwa pamoja naye kama zawadi kwa ajili yake.

Rebeka alimwambia mume wake kwamba hangeweza kuvumilia maisha yake kwa sababu ya kile Esau alifanya yaani, kuoa binti wa Hethi, hivyo na ikiwa mwana wake mwingine, Yakobo, ndugu pacha ya Esau, angefanya jambo hilo hilo, basi alihisi maisha yake hayangestahili kuishi. “Rebeka akamwambia Isaka, ‘Mimi nimechoshwa na maisha yangu kwa ajili ya binti za Hethi; ikiwa Yakobo ataoa mke katika binti za Hethi, kama hawa walio binti za nchi, je! maisha yangu yatakuwa kwangu?” (Mwanzo 27:46).

Kwa hiyo Rebeka akamhimiza Yakobo aende katika nchi ya familia yake na kutafuta mke kwa ajili yake mwenyewe ambaye angekuwa baraka kwake na kwa Isaka. Isaka akamwambia Yakobo, “Usitwae mke katika binti za Kanaani” (Mwanzo 28:1). Kwa maneno mengine, Isaka alimwambia Yakobo asimchukue binti asiyeamini kuwa mke wake, bali aende kwa familia yake katika nchi nyingine na kuchukua mke kutoka huko. Na kwa kuwa Yakobo alikuwa mwana mtiifu, ndivyo alivyofanya. Kwa kufanya hivyo, alipata upendo wake wa kweli na kubwa zaidi, baraka katika maisha ya mkewe Raheli. Hatimaye akawa mama wa Yusufu, ambaye alikuja kuwa mmoja wa viongozi wakuu katika historia yote ya Israeli, kwa sababu aliwaokoa watu wake kutokana na uharibifu wa hakika. Yakobo pia alidanganywa kuchukua mke mwingine Lea dada yake Raheli, lakini hiyo ni hicho ni kisa kingine, kwani Lea naye amekuwa mbari ya Masihi.

Jambo kuu ni kwamba makabila 12 yote ya Israeli yalizaliwa na Yakobo. Hakuna aliyetoka kwa Esau. Hapa walikuwa wana wawili, waliolelewa na wacha Mungu sawa na wote Walikuwa wa familia ambayo ilitokana na Ibrahimu.

Mtumishi aliinama na kumwabudu Bwana, akimshukuru kwa kumwongoza moja kwa moja mpaka mahali hapa na kwa jamaa ya bwana wake (Mwanzo 24:26-27). Mtumishi alisimulia hadithi ya Rebeka kwa familia yake na jinsi Ibrahimu alikuwa amemuahidi kwamba malaika angeenda pamoja naye na kumpa mafanikio ili kumpata mke wa Isaka (Mwanzo 24:28-40).

Kisa hiki kizuri ya mzazi akiomba kwa ajili ya uongozi wa Bwana kupata mwenzi kamili kwa mtoto aliyekomaa inaweza kutumika katika maisha yetu pia. Bila shaka, kulikuwa na sababu kwa nini Isaka hakuweza kwenda huko kumtafuta mke wa Isaka mwenyewe. Na sisi tusifanye, kwa tamaduni zetu, bali Mungu anavyotuongoza kama ni tutoke na kutafuta mke kwa mtoto wetu au mume kwa binti yetu na kupanga ndoa, ombea hilo ingawa hilo ni wazo linaloshawishi wazazi kufanya mara nyingine. Lakini ni bora zaidi kwamba tunaweza kumtafuta Mungu kuhusu hili na kumwomba kupanga mambo. Tunaweza kuomba kwamba mtoto wetu mtu mzima ataongozwa hadi mahali pazuri na wakati sahihi ili kukutana na mtu sahihi. Na tunaweza kuamini kwamba sala zetu zitasikilizwa na kujibiwa na Bwana.

Kwanza kabisa, ni lazima tuombe kile tunachojua ni mapenzi ya Mungu. Ibrahimu hakutafuta mke miongoni mwa makafiri. Alimtafuta kati ya wacha Mungu wa familia ya ndugu zake. Kama mwamini, washiriki wa

familia yetu ni waumini ndugu zetu na dada katika Kristo. Maombi yetu ya kwanza yanapaswa kuwa, “Bwana, mlete mwanamke mcha Mungu, aaminiye katika maisha ya mwanangu kuwa mke wake.” “Bwana, ninaomba kwamba binti yangu atampata mwanamume mcha Mungu na mwamini awe mume wake.” Ikiwa mtoto wako mtu mzima tayari ameolewa, mwombee mwenzi wake awe muumini na mcha Mungu. Omba mtoto wako Mkubwa Aolewe na Mtu msafi wa moyo.

Mtumishi wa Abrahamu alisali kwamba mke wa baadaye wa Yakobo angekuwa bikira mwanamke safi. Mapenzi ya Mungu kwetu ni kuwa safi kingono kabla ya ndoa. Hata hivyo leo kuna watu wengi katika utamaduni wetu wamekuwa na uchafuzi wa mazingira kingono wakiwa na maadili potovu, shinikizo la marika kufanya uasherati, na kuabudu sanamu za tamaa na kuridhika, kuna watu wengi zaidi wema ambao wamejikuta wamefanya makosa ya ngono na hata kupata watoto na wanajiuliza kama sasa mambo yatakuwaje. Ingawa chaguo la mwisho lingekuwa kuwa bikira, na ndivyo unapaswa kuomba kwa sababu ni mapenzi ya Mungu, usipunguze uweza wa Bwana kutakasa na kumkomboa mtu ambaye amefanya makosa. Hayo pia ni mapenzi ya Mungu kukutakasa na kukukomboa. Mungu anaweza kuleta katika maisha ya mwana au binti yako mtu ambaye ametakaswa na kukombolewa ikiwa dhambi zilizopita zimeungamwa na kutubiwa na moyo ni safi na hakuna kushindwa tena kimaadili na amekuwa na maisha mapya na kuishi kama mtu wa usafi. Mungu anapotakasa, hufanya kazi kamili.

## OMBA MTOTO WAKO WAKUBWA AOE AU AOLEWE NA MTU MWENYE TABIA YA KIUNGU

Jambo lingine muhimu ambalo mtumishi wa Abrahamu alisali kuhusu Mke wa Isaka anazungumza na asili ya tabia ya Rebeka. Alitaka kupata mwanamke ambaye angejitolea kusaidia na kumpa mgeni anayehitaji. Rebeka bila kusita alimpa maji. Na haraka akajitolea kumpa maji ngamia wake bila hata wazo la pili. Hakutoa huduma yake kwa kusitasita. Ilikuwa ni tabia yake kusaidia yaani alikuwa mtu mwema.

Yeye sio tu alimpa kile alichoomba, lakini akatoa pia kile alichokuwa hajaomba. Alitoa kile kilichokuwa cha heshima. Kwa asili ya neema, fadhili, na ya ukarimu, Rebeka pia alimpa mahali pa kulala usiku huo (Mwanzo 24:21-25).

Nilikuwa nikiishi kwenye shamba nilipokuwa mdogo. Tulikuza mahindi na ngano, lakini pia tulifuga ng'ombe. Hatukuwa na umeme wala mabomba. Tulikuwa na taa za gesi na choo cha nje. Tulichota maji yetu kwenye kisima. Ikiwa tulitaka maji ya kunywa, ilitubidi kuchukua ndoo safi hadi kisimani na kuteka maji juu kwa mkono na kamba iliyounganishwa kwenye ndoo. Ikiwa tungetaka kuoga, ambayo ilikuwa kamwe si zaidi ya mara moja kwa wiki, tulilazimika kuteka maji na kupasha moto kwenye jiko la kuni. Hii ilifanyika baada ya sisi kusanya kuni, vipande vidogo vya kutosha vya mbao na kuweka kwenye jiko la kuni. Ilikuwa kazi ngumu sana. Maji ni mazito, kwa yeyote kati yenu ambaye hajawahi kuvuta maji kutoka kisimani na kuyapeleka ili kuweka katika jiko lako la kuni. Kuchota maji kutoka kwenye kisima ni kazi kubwa hata ungeweza kufanya hivyo ni jambo moja kumpa kikombe cha maji mgeni mwenye kiu, lakini unaweza

kufikiria mara mbili kabla ya kujitolea kunywesha ngamia na ndoo zake. Lakini ikiwa ungekuwa mwenye huruma, mwenye upendo, mkarimu, na mtu mwenye kufikiria sana kama Rebeka, ungefanya hivyo bila kusita.

Omba kwamba mtoto wako mtu mzima aolewe na mtu mwenye neema, mkarimu, anayetoa, na mwenye asili ya kupenda. Biblia inasema kwamba Rebeka alikuwa mrembo. Nina hakika kuwa sehemu yake kubwa ya uzuri ulikuwa wa ndani, kutokana na tabia yake nzuri. Hata hivyo, sio kosa kumwomba Mungu mke mzuri na mrembo kwa mwanao au mume mzuri kwa binti yako. Simaanishi kuwa wanahitaji kuwa wakamilifu kwa viwango vya ulimwengu, lakini wavutie kila wakati kwa mwana au binti yako. Kumbuka kwamba Bwana anaweza kuchukua mwanamume au mwanamke yeyote na kuipamba sura yake ya ndani yaani roho ya mtu huyo. Nimeona watu wasiovutia wakija kwa Bwana, na Roho mwema na mzuri wa Mungu anapokaa ndani yao, wanabadilika na kuwa watu wazuri na wenye kuvutia ndani na nje.

## OMBEA WATOTO WAKO WATU WAZIMA KUWA NA UHUSIANO MZURI NA WAKWE ZAO.

Labda hakuna uhusiano dhaifu zaidi kuliko wa vijana na wakwe, na uhusiano mbaya wa wakwe huleta usumbufu, huumiza sana, na huleta hali isiyo shwari. Ikiwa watoto wako wakubwa wameolewa na wana wakwe, Sali ili mahusiano yao yawe mazuri na dhabiti. Omba pia uhusiano mzuri na binti-mkwe wako au mkwe wako. Mwombe Mungu akupe vipawa maalum

vya hekima, usikivu, ukarimu wa roho, na upendo usio na masharti ili uwe mama mkwe au baba mkwe bora kadir inawezekana. Mwambie akuonyeshe ni kiasi gani cha mawasiliano ni kikubwa na kipi ni kidogo kiasi kwamba hakitoshi linapokuja suala la mawasiliano na usaidizi. Zaidi ya yote, ombea Upendo wa Mungu kutiririka kupitia kwako kwa njia ambayo ni dhahiri.

Ikiwa mtoto wako mtu mzima tayari ameolewa na mtu mzuri, omba kwa ajili ya mkamwana au mkwerima kubarikiwa kwa kila namna. Walakini, ikiwa mtoto wako mtu mzima ameolewa na mtu una mashaka naye kwa sababu yoyote ile, omba kwamba Mungu amimine Roho Yake juu ya mkwe wako au binti-mkwe wako na wadhihirishe tunda la Roho katika tabia zao, ambazo ni upendo, furaha, Amani uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi (Wagalatia 5:22-23). Muombe Mungu akupe neema ya ukarimu, utu wema, kuvutia, na tabia ya Kiungu/Bwana. Hivi ndivyo Mungu anataka. Ni nani ajuaye kama maombi yako yanaweza kumsaidia kijana au mwanamke kupata utakaso na mabadiliko kwa nguvu za Bwana.

Ikiwa mtoto wako mkubwa ameolewa na mtu ambaye anaonekana kuwa mbali au asiye wa kawaida au mgumu, au mkwe wako ni mtu anayemsumbua mtoto wako mtu mzima na kumfanya asiwe na furaha sana au awe na hofu, basi andaa magoti yako kwa ajili ya maombi mengi kwa sababu utahitaji maombi mengi.

Omba kila kitu ambacho umejifunza kuomba kwa ajili ya watoto wako wakubwa katika hili weka daftari kwaajili ya mkwerima wako au mkamwana wako. Omba kwamba utampenda mkamwana wako au

mkwerima wako kwa moyo wako wote. Ikiwa unahisi huna aina hiyo ya upendo, mwombe Mungu akupe upendo Wake kwa mtu huyo. Yeye Atamimina upendo Wake kikamilifu ndani ya moyo wako ambao utatiririka kutoka kwako kila wakati.

## OMBA KWAMBA KWAMBA AWE NA NGUVU NA KUWA NA UHUSIANO NA BWANA.

Ikiwa kijana wako hajampokea Bwana bado au amempokea, omba ili tabia ya Kristo iundwe ndani yake. Omba ili uwe mama mkwe au baba mkwe bora unayeweza kuwa. Ombea uhusiano wako naye uweze kuwa mzuri. Yanaweza kuwa moja ya mahusiano mazuri zaidi utakayowahi kuwa nayo, au yanaweza kuwa mabaya zaidi utakayowahi kushuhudia. Usikubali chochote kidogo kuliko mema na mazuri. Na usisahau kwamba Mungu anaweza kufanya mambo makubwa kupitia mahusiano yako na wakwe zako.

## NJIA TANO ZA KUOMBEA WATOTO WAKO WAKUBWA WAWE WAZAZI WAZURI

1. Omba kwamba watambue watoto wao kama zawadi kutoka kwa Mungu. “Tazama, watoto ni urithi utokao kwa BWANA, uzao wa tumbo ni thawabu” (Zaburi 127:3).

2. Omba ili wawafundishe watoto wao katika njia za Bwana. "Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha hata atakapokuwa mzee” (Mithali

22:6).

3. Omba ili wawafundishe watoto wao kwa upendo na sio hasira. "Na ninyi, akina baba, msiwachokoze watoto wenu, bali waleeni katika mafundisho na maonyo ya Bwana" (Waefeso 6:4).

4. Omba ili wawe na bidii na hekima ya kuwaadibisha watoto wao. "Yeye asiyetumia fimbo yake anamchukia mwanawe, bali yeye ampendaye humrudi upesi" (Mithali 13:24).

5. Omba kwamba watembee katika utiifu kwa njia za Mungu katika kulea watoto wao ili maombi yao yatajibiwa. "Na chochote tunachoomba sisi tunapokea kutoka Kwake, kwa sababu tunazishika amri Zake na kufanya mambo yapendezayo machoni Pake" (1 Yohana 3:22).

## NJIA KUMI ZA KUWAOMBEA WAJUKUU ZAKO

1. Omba ili wawe na afya njema na wakamilifu katika akili, mwili na roho zao.

2. Omba kwamba waishi bila ajali, majeraha, au magonjwa.

3. Omba kwamba daima wataishi kwa amani, usalama, na upendo.

4. Omba kwamba walindwe dhidi ya yeyote mwenye nia mbaya ya kuwadhuru maisha yao kwa njia yoyote.

5. Omba ili wapate kumjua Bwana mapema maishani mwao, kwa kina, na kwa kujitolea na watajifunza kutembea katika njia Zake.

6. Waombee wawe na nidhamu na kusahihishwa ipasavyo ili wao waweze kuelewa matokeo ya tabia mbaya.

7. Omba ili wawe na moyo mnyenyekevu, wa toba, na wenye kufundishika ili wao waishi bila maasi na matatizo.

8. Omba ili uwe na hekima kutoka kwa Mungu kuhusu jinsi ya kuwa babu/bibi bora zaidi na kuunga mkono kwa uaminifu matakwa ya wazazi wao.

9. Omba kwamba Mungu awape wazazi wa wajukuu wako afya njema, nguvu, hekima ya Mwenyezi Mungu, na subira ya ajabu.

10. Omba ili Mungu akuonyeshe jinsi ya kuombea kila mjukuu hasa.

Huhitaji kuwa na wajukuu ili uanze kuwaombea. Wewe unaweza kuwaombea mapema katika mambo hayo kumi ya maombi. Kama wewe tayari una wajukuu, umebarikiwa na una kusudi kubwa katika maisha yako. Hatujui ni watu wangapi wameokolewa, wamelindwa, wameponywa, kufanikiwa, kukamilika, na zaidi, yote kwa sababu walikuwa na bibi anayeomba au babu.

Nilitazama katika Biblia baadhi ya maombi ya baraka zilizoombwa na wazazi wacha Mungu juu ya watoto wao watu wazima na kuja na muhtasari wao mfupi kwamba sisi wazazi tunaweza kuwaombea watoto wetu watu wazima, pamoja na wajukuu zetu:

Nakuombea Mungu akubariki na akupe matokeo mazuri ya maombi yako.

Naomba kwamba Mungu Azidishe mafanikio kwa watoto wako katika kazi yao, pamoja na kuongezeka kwa fedha zao, na kwa usalama nyumbani. Ninaomba hata wasiwe wazururaji kamwe lakini kwamba wataweka mizizi na kuimiliki nchi wanayoikaa. Ninaomba kwamba watajenga maisha mazuri, madhubuti na salama siku zote kwako na kwa mkwerima/mkamwana na watoto na wajukuu zako. Katika Jina la Yesu ninaomba. Amen.

## NGUVU YA MAOMBI

Bwana, ninamwombea …… (jina la mtoto mzima) na ninaomba kwamba umpe mume/mke mwema anayekupenda. Mletee mwanamke/mwanaume muumini ndani ya maisha yake, ambaye watakuwa pamoja naye kwa maisha yao yote katika utimilifu na furaha ya ndoa. Ninaomba kwamba yeye atakuwa na usafi wa moyo, pamoja na asili na tabia ambayo ni ya neema, fadhili, kutoa, na upendo.

Kwa mtoto wangu mtu mzima ambaye tayari ameolewa, naomba utamsababishia yeye na mwenzi wake waongezeke katika upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, uaminifu, upole, na kiasi (Wagalatia 5:22-23). Naomba ili mioyo yao ikue pamoja na sio kutengana. Fanya mabadiliko yanayohitajika ndani yao. Msaidie kila mmoja wao ajifunze kuomba kwa nguvu kwa ajili ya mwenzake.

Ninaomba kwamba watapendana na kuheshimiana, na kujifunza kunyenyekeana kila mmoja kwa mwingine (1 Petro 5:5). Wasaidie kuwasiliana na kuthaminiana kwa heshima. Ninaomba zaidi ya yote

kwamba “wawe na upendo wa dhati wao kwa wao, kwa maana ‘upendo utafunika wingi wa dhambi’

(1 Petro 4:8). Bwana naomba ukae katika ndoa yao na uifanye vile unavyotaka iwe. Ninaomba kwamba msamaha utatiririka kwa urahisi kati yao na kusiwe na hisia hasi zitakazoharibu hali ya nyumba yao. Ninaomba kwamba mioyo yao iwe na wema, huruma nyororo, na upendo mwanana na kujaliana kwa kila mmoja, na kwamba kila mmoja atamtanguliza mwenzake kila wakati. Fanya ndoa yao kuwa kisa cha mafanikio ili kusiwe na talaka katika mahusiano yao.

Bwana, msaidie mtoto wangu mtu mzima kuwa mume au mke bora iwezekanavyo. Mfundishe mambo yanayohitajiwa ili kufanya ndoa yao ifanikiwe. Mpe uelewa, uvumilivu, na uwezo wa kuwasiliana vizuri. Ondoa katika maisha yake na chochote ambacho kingemzuia yeye kuwa mume/mke Unayemtaka yeye kuwa.

Ninaomba kwamba kila mmoja wa watoto wangu watu wazima wawe na afya njema, watoto wenye akili, vipawa, na wacha Mungu. Wasaidie kupitia kila hatua ya uzazi salama na kuwawezesha kufanikiwa katika kuwalea watoto ambao ni watiifu, angavu, wenye afya njema, wenye furaha, na wenye matokeo.

Kama wazazi, wape wingi wa upendo, subira, ufahamu, na hekima. Waongoze kila hatua katika njia, kupitia kila hatua ya ukuaji wa kila mtoto. Ninaomba kwamba wakutazame Wewe kwa ajili ya uwongofu, wala si

dunia, ili wapate mafunzo ya kuwapa watoto wao katika njia Zako. Wafundishe jinsi ya kunidhamisha, kuadhibu, kusahihisha, kuongoza, na kulea watoto wao ipasavyo. Wasaidie daima kutambua kwamba watoto wao ni zawadi kutoka Kwako. Ninaomba kwamba uhusiano wao na kila mtoto uwe mzuri na wa kudumu.

Linda kila mjukuu wangu kutokana na madhara yote na mipango yoyote ya uovu. Bwana walinde kutokana na majeraha au magonjwa. Naomba mtu yeyote mwenye nia mbaya kamwe asiruhusiwe kuwakaribia. Wasaidie wakujue Wewe na wajifunze kuishi kwa njia yako. Usiwaruhusu kuishi katika kutengwa na Wewe. Wape roho ya unyenyekevu na inayofundishika, na kuwasaidia daima kuwaheshimu na kuwatii wazazi wao na sio kuanguka katika uasi.

Bwana, nisaidie kuwaachia watoto wangu na watoto wao urithi mkubwa wa hekima, utauwa, kuzaa matunda, na utimilifu utakaowabariki kwa maisha yao yote (Mithali 13:22). Wasaidie kuishi maisha ya utauwa/Kiungu yanayokupendeza Wewe, ili kwamba nisijue tu rehema Yako, bali wao pia wataijua (Zaburi 103:17-18). Katika Jina la Yesu ninaomba. Amina.

**NGUVU YA NENO**

Alichounganisha Mungu, mwanadamu asitenganishe.

**MATHAYO 19:6**

Bwana asipoijenga nyumba, waijengao wafanya kazi bure.

**ZABURI 127:1**

Mwenye haki huenenda katika unyofu wake; watoto wake wamebarikiwa baada yake.

**MITHALI 20:7**

Rehema za BWANA ni za milele hata milele kwa wamchao; na haki Yake kwa wana wa wana, kwao walishikao agano Lake, na kwa wale wanaokumbuka amri Zake ili wazifanye.

**ZABURI 103:17-18**

Hawatajitaabisha bure, wala hawatazaa kwa taabu; maana watakuwa wazao wa hao waliobarikiwa na BWANA, na wazao wao pamoja nao.

**ISAYA 65:23**

## OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE KUWA NA MAHUSIANO MAZURI

Dumisha Mahusiano Yenye Nguvu ambayo ni muhimu sana kwa kila mmoja wetu. Sote tunahitaji mema kutoka kwa watu wanaotuzunguka wanaotuimarisha na kuchangia katika ubora wa maisha yetu. Mahusiano mazuri ni muhimu kwa watoto wetu wazima. Sote tumeona ni vipi mvuto mbaya wa marafiki wasiofaa unavyoweza kufanya ikiwa si kwa watoto wetu wenyewe, basi tumeona kwa wengine.

Urafiki usio na afya na mahusiano yasiyo ya busara yanaweza kuharibu

hisia zao za jinsi Mungu alivyowaumba kuwa na waongozwe katika njia ambayo Mungu amewawekea. Kuna mahusiano fulani ambayo ni muhimu kwa mafanikio yao katika maisha. Mbali na hilo mahusiano na mke na mume na wakwe ambayo nilizungumzia katika sura iliyopita, kisha mahusiano mengine muhimu ni pamoja na marafiki, wafanyakazi wenzao, ndugu, majirani, shule na wazazi. Yote huchangia hisia ya ustawi na ni lazima kufunikwa na maombi. Hatuwezi kudharau thamani ya kuwa na mahusiano haya mahususi yenye nguvu na imara katika maisha ya watoto wetu watu wazima.

## OMBEA MAHUSIANO MEMA NA MARAFIKI WACHA MUNGU

Watoto wetu wakubwa wanahitaji marafiki wema, na wacha Mungu. Sio afya kwa mtu yeyote kuwa peke yake sana hasa kwa hisia ya moyo, kiakili, kiroho, au kimwili. Watu ambao wamejitenga sana daima huishia mbali kidogo katika kufikiri kwao. *Hii ni kweli iwe ni waumini au la. Lakini kama waumini tunahitaji watu wanaotuzunguka ambao ni wacha Mungu na wenye upendo wa Mungu, Roho Mtakatifu, na Yesu ndani yao. Watu kama hawa hutujenga na kutusaidia kuweka mambo ndani ya mtazamo sahihi.*

Ndiyo maana ni muhimu ili kuhakikisha mahusiano yetu ya karibu yanakuwa na watu wacha Mungu. Bibilia inasema “msifungiwe nira pamoja na wasioamini kwa jinsi isivyo sawasawa” (2 Wakorintho 6:14).

Ni lazima tuwaombee watoto wetu watu wazima wawe na marafiki wacha

Mungu. Sio kwamba hawawezi kuwa karibu na watu ambao si waumini, lakini watu ambao ni wengi zaidi na wenye ushawishi katika maisha yao wanapaswa kuwa wale wanaomjua Bwana.

Biblia inasema mengi kuhusu umuhimu wa kuchagua marafiki wanaofaa ambayo hatuwezi kuyapuuzia umuhimu wake. Nimeona matatizo isitoshe katika maisha ya watoto watu wazima ambao walitumia wakati na watu wasio sahihi. "Watu wema wanapaswa kuchagua rafiki zake kwa uangalifu, kwa maana njia ya waovu huwapoteza" (Mithali 12:26).

Mimi na mume wangu tulikuwa na suala moja kuu na watoto wetu watu wazima, ni kwamba kuna nyakati waliruhusu watu wasiofaa kuwa na ushawishi katika maisha yao. Na mahusiano hayo yaliwaondoa katika njia ambayo Mungu alikuwa nayo kwa ajili yao. Watoto wangu waliokomaa kwa asili sikuzote walikuwa wenye fadhili, wenye moro wa urafiki, na wenye kukubalika kwa kila mtu, na walidhani wangeweza kushughulika na mtu ambaye alikuwa na udunia moyoni kwa kiasi fulani, hasa wakati mtu huyo alijigeuza kuwa Mkristo.

Hata hivyo, wao walikuwa wachanga sana na wasio na uzoefu wakati huo kuona kupitia watu hawa, na jinsi uhusiano wowote nao ungewapeleka kwenye matatizo. Kupitia maombi ya wazazi na washiriki wa vikundi vya maombi hatimaye macho yao yalifunguliwa kuona Ukweli kuhusu mahusiano hayo na wakayatenga haraka.

Leo, ingawa hakuna marafiki wasumbufu katika maisha yao, bado ninasali

kuhusu hili. Ushawishi mbaya ni sehemu ya mpango wa adui kwa kifo chetu, kwa hivyo ninaendelea kumwomba Mungu awape hekima, utambuzi, na ufunuo kuhusu watu wanaokutana na kutumia muda nao. Marafiki ambao watoto wetu wazima huwa nao huathiri sana maamuzi muhimu watakayofanya.

Omba kwamba watoto wako watu wazima watachagua marafiki wao kwa uangalifu ili wasiweze kuishia kupotoshwa. Katika utamaduni huu ambapo kuna ushawishi mwingi wa uovu, ni vigumu kujua tabia ya kweli ya mtu isipokuwa una hekima ya Bwana na utambuzi. Ombea watoto wako watu wazima wawe na hisia sahihi ya nani ana ushawishi mzuri na nani asiye. Itawasaidia kufanya maamuzi sahihi kuhusu nani wanashirikiana na kuaminiana nao. Ubora wa urafiki wao utaathiri ubora wa maisha yao.

## OMBEA MAHUSIANO MEMA NA WAFANYAKAZI WENZAO

Namjua kijana mmoja ambaye alikuwa akijaribu kutafuta kibali kwa watu ambao alikuwa akifanya kazi nao, ambao walikuwa watu wa kilimwengu, nawanywaji pombe kupita kiasi. Walizishilia pombe zao na hawakuweza kuziacha. Kwa hiyo na yeye alikaribia kuwa mlevi. Kushirikiana nao kuliishia kumgharimu karibu kila kitu, ikiwemo sifa nzuri kupoteza uaminifu kwa watu ambao walikuwa muhimu zaidi kwake, kwani walianza kujitenga naye. Pia alipoteza miaka michache ya maisha na kupata shida katika maisha yake ya kazi.

Alikuwa na wazazi wanaosali ambao walikuja kumuokoa mara tu jambo hili lilipofunuliwa kwao na wakaona ni nini kilikuwa kinatokea. Waliweza kuona kwa jinsi alivyoonekana kuwa kuna makosa, lakini hawakuwa na ushahidi wa wazi. Waliwaita kwanza marafiki wachache wa karibu na wanaoaminika kuwaunga mkono katika sala. Kisha wao na mchungaji wao walimkabili, wakati ambapo maisha yake yalikuwa yanaanza kusambaratika. Ilikuwa jambo chungu sana kwa kila mtu anayehusika, lakini kupitia wakati huu wa upendo, makabiliano na maombi endelevu, maisha ya kijana huyu yaligeuzwa.

Ninatoa mfano huu kwa sababu hakuna mtu ambaye angefikiria kuwa kitu kama hicho kinaweza kutokea kwa kijana huyu. Alikuwa muumini na mcha Mungu ambaye alikuwa amelelewa katika nyumba nzuri, yenye imani. Haya yote yalitokea kwa sababu ya mahusiano yake na marafiki wa kazini. Hawa hawakuwa marafiki aliowachagua, bali wafanyakazi wenzake aliokuwa akijaribu kuwavutia na ambao alihisi alihitaji kuambatana nao na kukubalika kwao.

Omba ili watoto wako watu wazima wapate kibali kwa watu wanaofanya nao kazi bila kulazimishwa kutikisa chochote kile ambacho ni sawa katika macho ya Mungu. Bila shaka, ikiwa hawawezi kupatana na wengine watakuwa na matatizo ya kuendeleza kazi vizuri na kwa mafanikio, lakini kupatana haimaanishi kutupa kile wanachojua ni njia za Mungu. Waombee waheshimiwe na wafanyakazi wenzao kwa sababu ya maisha yao ya kumcha Mungu.

## OMBEA MAHUSIANO MEMA NA NDUGU NA DADA

Ni muhimu kwa kila mtu kuwa na uhusiano mzuri na ndugu zake na dada. (Ikiwa mtoto wako mtu mzima ni mtoto wa pekee, labda kuna binamu au mwanafamilia mwingine, ambaye ni kama kaka au dada kwake.) Mimi nimekuwa hivyo siku zote, nikiwaombea watoto wangu wawe na uhusiano mzuri kati yao, na ndivyo hivyo nashukuru kuona kwamba wako karibu sana na ndugu zao, hadi siku hii. Nina hakika kwamba baada ya mimi na mume wangu kulala mauti, wataendelea kuwa karibu. Nimeona ndugu wengi sana kuwa na nafasi ndogo ya kuonana tena au kutembeleana. Mara wazazi wanapolala mauti, wao kamwe hawawezi kuwa na mawasiliano yoyote. Watu wengi hawatambui umuhimu wa mahusiano ya familia kwa ustawi wao.

Daima ni muhimu sana kutoonyesha upendeleo kwa watoto wako. Inaleta tu chuki na inavunja umoja wa familia. Wakati mwingine mtoto mmoja inakuwa rahisi zaidi kuwa naye au kupatana nae kuliko mwingine, kutokana na asili yake au hata upendo wake kutoka kwa Mungu. Ikiwa una mtoto kipenzi (pet unayemdekesha), mwombe Mungu akupe upendo sawa kwa watoto kama vile Yeye Mungu anavyotupenda sote. Mwombe akusaidie kuonyesha upendo sawa kwa kila mmoja wao kwa njia ambayo wanaweza kuiona wazi.

Mfano kamili wa mzazi kuwa na kipenzi kati ya watoto wake ulikuwa Yakobo, ambaye baadaye aliitwa Israeli. “Israeli alimpenda Yusufu kuliko watoto wake wote, kwa sababu alikuwa mwana wa uzee wake. Pia

alimfanyia kanzu ya rangi nyingi. Lakini ndugu zake walipoona kwamba baba yao alimpenda kuliko wote, wakamchukia, wala hawakuweza kusema naye kwa amani." (Mwanzo 37:3-4).

Kitendo cha Yakobo kumpendelea mwana wake mchanga Yusufu kilisababisha chuki kubwa kati yake na ndugu. Isitoshe, Yusufu aliwaambia ndugu zake kuhusu ndoto aliyoota iliyoashiria kuwa ndugu zake siku moja watamsujudia. Kisha "ndugu zake wakamhusudu" na "wakapanga njama dhidi yake ili wamuue" (Mwanzo 37:11,18). Lakini wafanyabiashara wa watumwa walikuja, na ndugu za Yusufu wakamuuza Yusufu kwao badala ya kumuua (Mwanzo 37:28). Hii ilikuwa hali ya kutisha ambayo Mungu baadaye aliigeuza kuwa kitu kizuri kwa sababu ya utauwa wa Yusufu. Mwishowe, yeye na ndugu zake walipatanishwa, familia ikaunganishwa tena, na Yusufu akawaokoa wote kutokana na njaa kali katika nchi.

Ikiwa una familia iliyochanganywa na watoto kutoka kwa mama au baba tofauti kama Yusufu, maana yeye na ndugu zake walikuwa na baba mmoja, lakini mama tofauti na ikiwa una watoto wa kambo waliochanganyika na watoto wako, omba kwamba kusiwe na wivu kati yao. Mwombe Mungu akusaidie kuepuka kuonyesha upendeleo wowote unaoweza kuuonyesha na kusababisha chuki. Upendeleo daima utasababisha kifo cha aina fulani; kifo cha uhusiano, kifo cha upendo na wema, na kifo cha familia kwa sababu baada ya wewe na mzazi mwingine wa watoto hao kufa, familia itakufa na kusambaratika kabisa.

Nimeona matokeo haya katika familia mara nyingi sana, na ndivyo ilivyo

na inasikitisha sana. Omba ili jambo hili lisitokee kwa familia yako. Ombea mahusiano mema kati ya watoto wako wote ili baada ya wewe kuondoka wasiweze kuachwa wakijihisi kutokuridhika. Kila mtu anahitaji jotojoto hil la kifamilia zaidi kuliko tunavyoweza kutambua.

Omba ili watoto wako wasiishie kuoneana wivu kwa sababu yoyote ile. Ni vyema uhakikishe kuwa kila kitu kimegawanywa kwa usawa hata kama wewe una mali kidogo tu za kuwaachia.

Nimeona ndugu wakipigania urithi mdogo ambao haukuelezwa waziwazi katika wosia, au uliandikwa waziwazi katika hati ya kisheria iliyofichua upendeleo wenye kuumiza. Ndugu hawa na dada waligawanyika na kuharibiwa maisha yao yote. Migogoro na ushindani kati ya ndugu ni uharibifu na yaweza kuwa utumwa wa kila mtu anayehusika - utumwa wa chuki, uchungu, hasira, kijicho, hisia za kukataliwa, na kutoaminiana ambazo hupelekea kuvunjika kwa mahusiano ya familia.

Ikiwa hilo tayari limetokea kwa njia fulani katika familia yako, Sali vunja hiyo roho ya mgawanyiko. Mwambie Mungu aponye mipasuko na kurejesha mahusiano ya ndugu. "Basi ukileta sadaka yako madhabahuni na kukumbuka kwamba ndugu yako ana jambo dhidi yako, acha sadaka yako hapo mbele ya madhabahu, nenda zako. Upatane kwanza na ndugu yako, kisha njoo utoe sadaka yako" (Mathayo 5:23-24).

Ikiwa hakuna kitu kama hicho kimetokea katika familia yako, mwombe Mungu akusaidie kuhakikisha kuwa mpasuko hautokei. Kitu chochote

kinachoharibu mahusiano kati ya watoto wako watu mzima kitasaidia kutimiza mpango wa adui kwa uharibifu wao.

## OMBEA MAHUSIANO MEMA NA WAZAZI

Moja ya baraka kuu zaidi watoto wako watu wazima watakazowahi kupokea ni kuwa na wewe kama rafiki mcha Mungu. Utakuwa mama au baba yao kila wakati, lakini wakati wao wataondoka na kwenda kuanzisha maisha yao wenyewe na wasiwe tegemezi juu yako, unahitaji kumwomba Mungu kukusaidia kupata msawaziko/balansi kamili wa kuwa na upendo, lakini sio kuvuta watu upande au ule; kutia moyo, lakini si kufanya wajiachie; kuchua tahadari, lakini siyo kuwa na wasiwasi; kujali, lakini sivyo kudhibiti; mjenge, lakini msijizuie; kuunga mkono, lakini sio kulemaza.

Ni Mungu pekee ndiye anayeweza kukusaidia kutembea kwenye mstari huo nyeti. Ikiwa uhusiano wako na mtoto wako mtu mzima yameharibiwa au kudonolewa-donolewa na mzazi wake mwingine, jua kwamba Mungu anaweza kuyarejesha na kwamba Yeye Mungu ana hamu ya kufanya hivyo. Mahusiano yote yanaweza kuharibiwa ikiwa Mungu hatawaweka pamoja dhidi ya mashambulizi ya adui. Adui anataka kuharibu mahusiano yetu kwa sababu anajua hilo hutudhoofisha kiroho na kiakili na halimpendezi Mungu. Tamaa ya adui ni kuleta machafuko kwenye mahusiano na ndio sababu huleta tafsiri mbaya ya maneno, vitendo, au nia. Adui anawapofusha wanadamu wasiuone Ukweli na kuwalisha uongo. Anajua jinsi ya

kuwatenganisha watu na Mungu kupitia kuwagombanisha kila mmoja na mwingine. Lakini nguvu za Mungu ni kubwa zaidi kuliko za adui. Adui anashinda tu katika maisha yetu wakati anaweza kutufanya tuamini uwongo juu ya Mungu.

Kila wakati unapowaombea watoto wako watu wazima, kumbuka daima adui anayetaka kuwaona wakipofushwa anayemelea na ni rahisi kudanganywa, kushushwa, na kuharibiwa. Biblia iko wazi kabisa kuhusu uwepo wa Shetani na nia yake katika maisha yetu. Lakini Biblia pia inasema kwamba Yesu alishinda kifo na mauti msalabani. Hiyo maana yake ni kwamba alishinda uwezo wa adui wa kudhibiti maisha yetu.

Unapoomba juu ya jambo ambalo linaonekana kutokuwa na tumaini au jambo fulani umeombea muda mrefu bila kubadilika katika maisha ya watoto wako, kumbuka kwamba huna vita na wao;wewe uko vitani na adui ambaye ni mungu wa zama hizi, au wa ulimwengu huu, anayepofusha macho watu kwa Ukweli (2 Wakorintho 4:3-4). Bwana anaweza kuhuisha uhusiano wowote ambao umekufa. Anaweza kurekebisha uhusiano ambao umevunjika. Anaweza kuunganisha tena uhusiano ambao umepata mpasuko. Maombi yako yanaweza kugeuza mambo na kusaidia hilo kutokea. Maombi yako yanaweza kukuza msamaha, urejesho, na uponyaji pale inapohitajika.

Hata katika ukoo wa Mfalme Daudi ambaye kupitia kwake Masihi angezaliwa baadaye kulikuwa na mahusiano yaliyovunjika na yenye matatizo. Hata hivyo Mungu alileta wema mkuu kutoka katika ukoo huo katika kuzaliwa kwa Mwanawe, Yesu. Mungu atatengeneza uhusiano wako

na watoto wako watu wazima na uhusiano wao na wanafamilia wengine pia.

Mungu Atajibu maombi yako ya upatanisho. Hakuna kitu kisichoweza kufikiwa na neema ya Mungu, ahadi za Neno la Mungu, au mkono wa Mwokozi ulionyooshwa kwako na kwa WATOTO WAKO WAKUBWA. Mungu anaweza kuvunja ukaidi wetu, kiburi, maudhi, kutosamehe, hasira, na maumivu.

Anaweza kuweka uhusiano wowote ambao WATOTO WAKO WAKUBWA wanao na mzazi yeyote pamoja tena na kuzaliwa kitu kipya na kikubwa katika mchakato. Onyesha upendo wa Mungu kwa watoto wako watu wazima kwa maneno unayozungumza nao. “Maneno yenu yawe na neema siku zote, yakikolea munyu, mpate kjua jinsi iwapasavyo kumjibu kila mtu” (Wakolosai 4:6).

Omba Mungu akupe hekima kila unapozungumza nao ili maneno yako yasiwe ya kukosoa, kuudhi na kujeruhi kwa njia yoyote. “Kuna asemaye kama kuchoma kwa upanga, bali ulimi wa mwenye hekima huleta afya” (Mithali 12:18). Mwombe Mungu akuonyeshe jinsi ya kuangaza nuru yake ya upendo usio na masharti kwa kila mmoja wao (Mathayo 5:14-16). Ikiwa unaomba kwa mbali, waambie jinsi unavyowaombea na kuwatia moyo. Ifanye kuwa uthibitisho chanya. Usiseme, “Ninakuombea na huyo mke wako aache kufanya maamuzi ya kijinga kuhusu fedha zako.” Sema badala yake, “Ninaomba kwa ajili ya Mungu kumwaga wingi wa Baraka juu yenu wawili katika njia ya kila mmoja wenu.” Usiseme, "Ninakuombea uamke na uondoe marafiki wako wabaya.” Sema badala yake, “Nakuombea upate

hekima na maarifa kutoka kwake Mungu ili ufanye maamuzi sahihi siku zote juu ya marafiki zako."

Watoto watu wazima daima hufaidika kutokana na baraka zozote unazozungumza juu ya maisha yao, hivyo sema baraka juu yao kila unapokuwa pamoja nao. Sema kitu kama, "Ninaomba Mungu akufungulie milango ambayo hakuna mtu anayeweza kuifunga." Au, “Mimi ninaomba kwamba Mungu atatumia karama na talanta alizoweka ndani yako kwa utukufu wake.” Kwa sababu wao ni wakubwa sasa haimaanishi kwamba watoto wako wakubwa hawahitaji upendo wako na msaada wa kihisia tena.

Wanaweza kutenda kana kwamba hawafanyi kwa sababu wanataka ujue wanaweza kushughulikia maisha yao wenyewe, lakini ukweli ni kwamba wanakuhitaji zaidi kuliko wanavyoweza kusema. Masuala yanayowakabili ni makubwa zaidi na upinzani ni mkali zaidi. Ombea mahusiano yao yote yawe na nguvu, lakini hasa wewe na mzazi wao mwingine au wazazi wa kambo.

Omba ili watoto wako watu wazima wasiathiriwe kamwe na dhambi ya kutokusamehe na uchungu katika mahusiano yao yoyote, bali msamaha utatiririka kama maji ya kisima katika nyoyo zao.

## NGUVU YA MAOMBI

Bwana, ninaomba ….. (jina la mtoto mzima) apate marafiki wacha Mungu katika maisha yake. Ninaomba kwamba wawe na ushawishi chanya kwake. Mwezeshe kuona ukweli kuhusu watu na kuvutwa kuelekea kwa wale walio

wema. Mpe nguvu na hekima ya kujitenga na mtu yeyote asiye na ushawishi mzuri. Ondoa katika maisha yake mtu yeyote ambaye ana ushawishi mbaya na ambaye humvuta mbali na Wewe na njia zako (1 Wakorintho 5:11). Ninaomba kwamba yeye atakuwa na marafiki wanaomwambia Ukweli kwa upendo (Mithali 27:6) na utampa ushauri na mwongozo mzuri (Mithali 27:9). Ninaombea marafiki walio na hekima (Mithali 13:20) na daima watakuwa msaada mkubwa kwa ajili yake (Mhubiri 4:9-10). Ninaomba kwamba kila uhusiano unaoingia katika maisha yake utakuwa wa kukutukuza wewe, Bwana.

Pamoja na marafiki, ninaomba hasa uhusiano mzuri na wazazi, ndugu, na wanafamilia wengine. Bariki mahusiano haya kwa upendo wa kina, huruma kubwa, kuelewana, na mawasiliano mazuri. Ikiwa ipo sehemu yenye uhusiano mbaya katika uhusiano wowote kati ya hayo, ninaomba kwamba Wewe ulete amani, uponyaji, na upatanisho. Ninaomba kwamba adui asiwe na uwezo wa kuvunja uhusiano wowote wa kifamilia au urafiki.

Ninaomba hasa kwa ajili ya uhusiano wake na ………………….. (jina la mtu). Naomba Bwana Ungeponya mpasuko uliopo au matatizo yoyote kati yao na kuleta maelewano kwa nguvu za Roho wako Mtakatifu. Pale ambapo kumekuwa na mawasiliano mabaya, leta uwazi na mawasiliano mazuri. Ambapo kumekuwa na malalamiko ya haki, leta toba na kuomba msamaha. Popote ambapo uhusiano umevunjika, kwa kwa sababu yoyote ile, Bwana leta uponyaji na urejesho. Ninaomba kwamba yeye daima atakuwa na uhusiano mzuri na wafanyakazi wenzake.

Pale ambapo kuna mfanyakazi mwenzake asiyemcha Mungu, naomba mtoto wangu awe na ushawishi wa Kiungu juu ya mtu huyo. Msaidie kusimama imara na asiwe dhaifu kwa vitisho. Ninaomba kwamba atatembea na wenye hekima na hivyo kuwa na hekima zaidi, na asiwe "rafiki wa wapumbavu" na kuangamizwa (Mithali 13:20). Msaidie kujifunza utiifu na msamaha. Mwezeshe aweze kusamehe kwa urahisi na sio kubeba kinyongo, chuki, uchungu, au orodha ya binafsi ya makosa. Msaidie kuachilia kutosamehe haraka kwa wengine, ili iwe hivyo kutokusamehe kamwe kusiingilie uhusiano wake na Wewe na hucheleweshа msamaha na Baraka za maisha yake mwenyewe (Marko 11:25). Katika Jina la Yesu ninaomba. Amen.

**NGUVU YA NENO**

Anayetembea na wenye hekima atakuwa na hekima, bali rafiki wa wapumbavu daima ataharibiwa.

**MITHALI 13:20**

Mimi ni rafiki wa wote wakuchao. na wale wanaozishika amri Zako.

**ZABURI 119:63**

Msifungwe nira pamoja na wasioamini kwa jinsi isivyo sawa. Kwani kuna ushirika gani uadilifu pamoja na uasi-sheria? Tena pana ushirika gani kati ya nuru na giza? Tena pana mapatano gani kati ya Kristo na Beliari? Au muumini ana sehemu gani na asiyeamini?

**2 WAKORINTHO 6:14-15**

Usiingie katika njia ya waovu, wala usitembee katika njia ya uovu.

**MITHALI 4:14**

Lakini tukienenda nuruni kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi na damu ya Yesu Kristo Mwanawe yatusafisha na dhambi yote.

**1 YOHANA 1:7**

## OMBA ILI WATOTO WAKO WALINDWE NA KUOKOLEEWA NA NYAKATI MGUMU

Kabla hata hawajazaliwa, moja ya maombi ya kwanza tunayoomba kwa ajili ya watoto wetu ni juu ya ulinzi wao. Na tunaendelea kuomba kuhusu hilo karibu kila siku kwa uendelevu. Wasiwasi muhimu zaidi wa mzazi yeyote ni kwamba mtoto wao alindwe kutokana na majeraha makubwa na magonjwa. Pia tunataka walindwe dhidi ya watu waovu wanaotaka kufanya vitendo vya uhalifu dhidi yao. Na hakika tunawataka kulindwa kutokana na kifo cha mapema. Tunawaombea waishi zaidi na wafurahie maisha marefu na maisha ya afya. Haijalishi mtoto wako ana umri gani-unaweza kuwa 99 na mtoto wako ana miaka 81 na daima bado utakuwa na wasiwasi. Ndio maana kuomba Ulinzi wa Mungu ndiyo njia pekee ya kuwa na amani juu yao.

Dada yangu, Suzy, na mimi tumekuwa katika kundi la maombi ya kila wiki pamoja na wanawake wengine kwa zaidi ya miaka 20. Kila wiki tunaomba

kwea kubainisha kwa njia mahsusi kwa kila mmoja wa watoto wetu sasa watu wazima. Binti ya Suzy mpwa wangu, Stephanie ana umri sawa na binti yangu, Raheli. Kwa kweli wameachana kwa wiki mbili tu. Moja ya baraka kubwa zaidi imekuwa ni kuwaona wakikua pamoja. Lile jambo ambalo tumewaombea siku zote ni kwamba Mungu awalinde. Wakati Stephanie alikuwa katika miaka yake ya ishirini aliolewa kabla ya mwaka mmoja kuisha tangu kufunga ndoa, mumewe Jeremy, ambaye alikuwa amehitimu kutoka njoro na alikuwa afisa katika jeshi, alipelekwa Congo kwa mwaka wa kazi. (Naomba kuongeza kwamba Jeremy hakika ni jibu la ajabu kwa maombi yetu kwa ajili ya mume mcha Mungu na mkamilifu kwa ajili ya Stephanie.)

Wakati askari waliondoka kwenye jumuiya walimoishi karibu na kambi ya jeshi, ikawa kama mji wa kutisha, karibu wanaume wote walikuwa wamekwenda vitani na wanawake na watoto walirudi nyumbani na wazazi wao. Stephanie alikuwa akiishi peke yake ndani ya nyumba na kuhisi hatari sana kwa sababu hiyo. Alikuwa na amekuwa sehemu ya kikundi changu cha maombi kwa miaka michache, kwa hiyo alituomba kabisa tumfunike katika maombi kwa ajili ya usalama wakati huu.

Katika kila moja ya mikutano yetu ya kikundi cha maombi, kila mara tunasoma Neno kwanza, tunakuwa na wakati wa ibada, na kisha tunajifunika sisi wenyewe na jamaa zetu zote wa karibu na wanachama kwa majina katika maombi ya usalama na ulinzi. Lakini wiki hii tulitaja kwa kubainisha kuhusu Jeremy aliyekuwa akipigana katika eneo hatari la vita na

Stephanie nyumbani peke yake katika mji na watu wachache waliobaki humo.

Jambo unalohitaji kujua kuhusu Stephanie ni kwamba ni mtu mwangalifu sana na aliye na mpangilio wa mambo na anayewajibika ambaye namjua. Lakini alasiri moja yeye alienda sokoni kufanya manunuzi ya vyakula na akaja nyumbani, na kisha akasikia simu ikiita na mbwa wakibweka. Alikuwa na bidii sana kutokosa kupokea simu akitarajia yaweza kuwa ni mumewe anapiga simu kutoka vitani, kwa hivyo alikimbia mlangoni, akaweka mboga zake haraka kwenye meza, na kujibu haraka simu. Baada ya kumaliza na simu, aliweka mboga zake mahali pake na kutengeneza chakula cha jioni kwa ajili yake mwenyewe. Mara baada ya kula, akawapa chakula mbwa, na kusafisha jikoni, ilikuwa ni wakati wa kujiandaa kwa ajili ya kulala. Alihakikisha milango yote ilikuwa imefungwa na taa zote zilikuwa zimezimwa, isipokuwa ukumbi wa mbele aliacha taa ikiwaka, kisha akaingia chumbani kwake na kuingia kitandani.

Lakini hakuweza kulala mara moja. Aliendelea kuhisi wasiwasi zaidi na zaidi juu ya usalama wake. Alihisi kuongozwa sana kuomba haswa kwamba Mungu amlinde yeye na wanawake wengine waliobaki peke yao katika nyumba zao kwenye eneo lao la kambi usiku huo. Pia alisali kwa bidii kwa ajili ya usalama wa mumewe. Alijiuliza ikiwa ni kwa ajili yake kwamba alihisi kuongozwa kuomba hivyo kwa bidii, lakini kadiri alivyozidi kuomba, ndivyo alivyohisi kuwa ni kwa ajili ya usalama wake mwenyewe alihitaji kuomba.

Alipoamka asubuhi iliyofuata, alienda kwenye mlango wake wa mbele kama kawaida kuangalia watu wanaouza vitu. Muda alipofungua mlango, alishtuka kuona funguo za nyumba yake, na funguo za gari zimeegeshwa, bado katika kufuli ya mlango wa mbele. Zilikuwa zimekaa kwenye kitasa cha mlango wa mbele na nyumba ipo futi chache kutoka barabarani na mwanga wa ukumbi wa mbele ukiangazia usiku mrefu wote. Mtu yeyote angeweza tu kutembea ndani ya nyumba na kungekuwa hakuna wa kumzuia. Stephanie alijua kwamba Mungu alikuwa amemwongoza kusali usiku huo kwa ajili ya usalama wake mwenyewe, na alijua ni Mungu ambaye ndiye alikuwa amemlinda. Yeye mara moja aliwaita washiriki wa kikundi cha maombi na kutuambia kilichotokea. Sote tulijua Mungu alikuwa amejibu maombi yetu mengi kwa ajili ya usalama wake.

## NJIA KUMI ZA KUOMBEA ULINZI KWA WATOTO WAKO WAKUBWA

1. Omba ili watoto wako walio watu wazima wawe na hekima na uamuzi mzuri wa kufanya jambo sahihi. Hekima yao itawaepusha na hatari zaidi kuliko tutakavyowahi kujua. “BWANA huwapa hekima; kutoka kinywani Mwake hutoka maarifa na ufahamu; Huweka akiba ya hekima kamili kwa ajili ya watu wema; Yeye ni ngao kwao waendao kwa unyofu; Analinda njia za wenye haki, na kuihifadhi njia ya watakatifu Wake” (Mithali 2:6-8).

2. Omba ili watoto wako wakubwa wajifunze kumcha Mungu na si wanadamu. Wakiwa na hofu ya mwanadamu inawafanya wafanye ujinga, wasiwe wacha Mungu, na mambo mengine ya kusikitisha. “Kuwaogopa wanadamu huleta mtego, bali yeye anayemwamini BWANA atakuwa salama” (Mithali 29:25).

3. Omba ili watoto wako wakubwa wamwamini Mungu na Neno Lake. Kuamini katika njia za Mungu zitawaweka katika njia iliyo sawa. “Kila Neno la Mungu ni safi; Yeye ni ngao yao wanaomtumaini” (Mithali 30:5).

4. Omba ili watoto wako watu wazima waishi katika uwepo wa Mungu mahali ambapo ni usalama. Wanapomwalika Mungu akae mahali pao pa siri moyoni, wataishi katika kivuli Chake cha ulinzi, wakiwa wamefichwa mbali na hatari. “Akaaye mahali pa siri Pake Aliye juu atakaa chini ya uvuli wa Mwenyezi” (Zaburi 91:1).

5. Omba ili watoto wako wakubwa wamfanye Mungu kuwa kimbilio lao na kumgeukia kwa ulinzi. Kisha wanaweza kumwamini Mungu kuwaokoa na hatari na mashambulizi yote ya adui. “Nitasema juu ya BWANA, ‘Yeye Ndiye kimbilio langu na ngome yangu; Mungu wangu, ambaye nitamtegemea.’ Hakika Yeye atakuokoa kutoka katika mtego wa mwindaji na katika tauni hatari.” (Zaburi 91:2-3).

6. Omba kwamba watoto wako wakubwa watafichwa katika Bwana na kutumia Neno Lake kama ngao yao. Ni lazima watambue kwamba Neno la Mungu hufanya kizuizi cha kinga kinachowalinda dhidi ya mashambulizi ya

adui. “Atakufunika wewe kwa manyoya Yake, na chini ya mbawa Zake utakimbilia; Kweli Yake itakuwa ngao na kigao chako” (Zaburi 91:4).

7. Omba ili watoto wako watu wazima wasiishi kwa hofu ya hatari au magonjwa. Wanapokaza macho yao kwa Mungu, hawatalazimika kuishi kwa hofu ya mashambulizi ambayo yanaweza kutokea wakati wowote, mchana au usiku. “Usiogope hofu ya usiku, wala ya mshale urukao mchana, wala tauni iendayo gizani, wala uele uharibuo adhuhuri” (Zaburi 91:5-6).

8. Omba ili watoto wako wakubwa wasiogope, hata wanapoona uharibifu unaotokea karibu nao. Hii si kuishi katika kukataa; ni kwa sababu wanajua kwamba wanatembea na Mungu, Yeye ni mlinzi wao wakati wote. “Elfu wataanguka upande wako, na elfu kumi mkono wako wa kuume; lakini uharibifu hautakukaribia wewe” (Zaburi 91:7).

9. Omba ili watoto wako waelewe matokeo ya kutokuishi katika njia ya Mungu. Watu wengi hawaelewi kuwa kuna gharama lazima ulipe unapoasi, na siku moja uovu utakuja juu yao. “Utatazama kwa macho yako tu, uyaone malipo ya waovu” (Zaburi 91:8).

10. Omba ili watoto wako watu wazima waelewe kwamba thawabu ya kuishi katika Njia ya Mungu ni ulinzi Wake. Wanapoishi katika njia ya Mungu, Yeye atawaongoza kwenye njia iliyo sawa, kutoka katika njia ya madhara, iliyokingwa na uovu, madhara, na ugonjwa. “Kwa sababu umemfanya BWANA, aliye kimbilio lako, naam Aliye juu, kuwa makao yako, hakuna uovu utakaokupata, wala tauni haitakaribia maskani yako”

(Zaburi 91:9-10).

## OMBA MUNGU AMZINGIRE MTOTO WAKO NA MALAIKA

Biblia ina mengi ya kusema kuhusu malaika. Na hasa wale wanaotulinda sisi. Hapa kuna mifano michache mikuu ya kutokea kwa malaika:

Malaika wa Bwana alimtokea mara kadhaa Yusufu, mume wa Mariam, kuhusu wapi wanapaswa kwenda ili kuwa salama. Malaika alimwagiza Mariamu na Yusufu kuondoka Bethlehemu pamoja na Yesu. "Malaika wa Bwana akamtokea Yusufu katika ndoto, akisema, Ondoka, umchukue Mtoto na mama yake, ukimbilie Misri, kaeni huko hata nitakapowaambia; kwa maana Herode atamtafuta kumwangamiza Mtoto" (Mathayo 2:13).

Malaika wa Bwana aliingia ndani ya gereza alimokuwa Petro na kumwokoa. Katika sura ya awali ya kitabu hiki nilieleza jinsi malaika alivyomtoa Petro kwa uhuru kwa njia ambayo kibinadamu isingewezekana. "Basi tazama, malaika wa Bwana akasimama karibu; naye, na mwanga ukaangaza gerezani; akampiga Petro ubavuni, akamwinua, akisema, 'Ondoka upesi!' Minyororo yake ikaanguka mikononi mwake… akatoka akaenda katika njia moja, na mara malaika akaondoka. Na Petro alipopata fahamu, akasema, Sasa najua hakika Bwana amemtuma malaika Wake, na kuniokoa na mkono wa Herode na kwa kutazamia kwa watu wote wa Kiyahudi" (Matendo 12:7-11).

Malaika alimjia mtume Paulo katikati ya dhoruba. Malaika alizungumza na

Paulo kuhusu yale ambayo yangempata na ambayo yasingempata. Paulo aliwekwa salama na kile kilichotabiriwa kilifanyika kama vile malaika alivyosema. "Kwa maana hapo alisimama usiku huu malaika wa Mungu ambaye mimi ninamtumikia, akisema, ‘Usiogope, Paulo; lazima upelekwe mbele ya Kaisari; na kwa hakika Mungu atakupa wote wanaosafiri pamoja nawe” (Matendo 27:23-24).

Yesu alisimulia jinsi malaika walezi wa watoto wetu ni wa maana. Wanafunzi walikuwa wakimuuliza Yesu, ni nani aliyekuwa mkuu katika ufalme wa mbinguni (Mathayo 18:1). Kisha Yesu akamwita mtoto mdogo na kuwaambia, “Yeyote ambaye hujinyenyekeza kama mtoto huyu mdogo ni mkuu katika ufalme wa mbinguni. Yeyote anayempokea mtoto mdogo kama huyu kwa Jina Langu, ananipokea Mimi.” (Mathayo 18:4-5). Yesu akaendelea kusema, “Jihadharini, msimdharau hata mmoja wa walio wadogo hawa, kwa maana nawaambia ya kwamba malaika wao mbinguni siku zote huuona uso wa Baba Yangu Aliye mbinguni” (Mathayo 18:10). Mungu anagawia malaika walinzi kutunza watoto wetu.

Hakuna mahali katika Biblia panaposema kwamba malaika hawa walinzi wanamwambia mtoto mara anapofikisha miaka kumi au kumi na mbili, “Sawa binti au mwana, kazi yangu saa imekamilika. Uko peke yako sasa (you are on your own baby! Take care)." Hapana, Yesu anasema kuhusu watoto kwamba si mapenzi ya Baba yao aliye mbinguni kwamba hata mmoja wao apotee (Mathayo 18:1-14). Hiyo inazungumza wazi kwangu kwamba madhara, uharibifu, kifo, au kupoteza mtoto yeyote kwa namna

yoyote ile ni kazi ya adui na si mapenzi ya Mungu.

Mtoto wako mtu mzima bado ni muhimu kwa Mungu kama vile alipokuwa mtoto mdogo. Lakini wakiwa watu wazima, wako katika umri ambao wanajitengenezea maamuzi yao, kwamba wataishi kwa njia ya Mungu au la, au kama wataishi wenye kutubu au wenye kuasi. Katika Biblia, malaika wanaelezewa kuwa "ni roho watumikao kwenda kuwahudumia wale watakaourithi wokovu" (Waebrania 1:14. Pia inasema, "Kwa maana atakuagizia malaika Zake, wakulinde katika njia yako yote. Mikononi mwao watakuchukua, usije ukajikwaa mguu wako kwenye jiwe" (Zaburi 91:11-12).

Tunaposoma aya hizo mbili hapo juu katika nuru ya sehemu iliyobaki ya Zaburi ya 91, tunaweza kuona kwamba Mungu atawaamuru malaika Wake juu yetu ili kutulinda tunapoishi njia Yake. Ikiwa tunataka ulinzi wa malaika, lazima tuishi ndani ya mipaka na chini ya mwavuli wa ulinzi wa Mungu. Ni lazima tukae na Bwana na kumfanya kimbilio letu. Ndiyo maana ni lazima tuombe kwa ajili ya watoto wetu wakubwa. Waombee Watoto wako wakubwa Wapate maisha marefu na wawe na maisha yenye kuzaa matunda na tija. Sisi tunataka watoto wetu waishi maisha marefu na sio kufa wakiwa vijana.

Mungu huwapa watoto wetu wakubwa njia ya kuwa na maisha marefu na yenye baraka, na hivyo inawezekana katika kumpenda na kumtii, ahadi hii ikatimia. "Kwa kuwa amekaza kunipenda nitamwokoa na kumweka palipo juu; kwa sababu amenijua Jina Langu. Ataniita Nami nitamwitikia;

nitakuwa pamoja naye katika taabu; nitamwokoa na kumtukuza. Kwa maisha marefu nitamshibisha, na kumwonyesha wokovu Wangu" (Zaburi 91:14-16).

Amri ya tano kati ya zile amri kumi ni amri ya kwanza yenye ahadi. Inasema, "Waheshimu baba yako na mama yako, siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako" (Kutoka 20:12)).

Kukuheshimu kama mzazi wao ni njia nyingine kwa watoto kumtii Mungu na kuwa na maisha marefu na yenye matunda. Mtume Paulo alipowaagiza watoto wote watii wazazi wao, alisema wanapaswa kuwaheshimu "ili upate heri na kuishi siku nyingi katika nchi akupayo Bwana." (Waefeso 6:1-3). Mtoto anayewaheshimu baba na mama ataona maisha yake yanaenda vizuri na kudumishwa kwa muda mrefu. Tena, sioni sehemu ya mpaka ambapo Mungu anakata kwa kusema, "Wewe ni mtu mzima sasa, kwa hivyo sio lazima tena uwaheshimu wazazi wako." Ahadi hii ni ya maisha yetu sote. Ikiwa mtoto mkubwa huwadharau wazazi wake katika umri wowote, hataona maisha marefu yenye mafanikio, na maisha ya kuridhisha Mungu aliyonayo kwa ajili yake. Watoto lazima wafundishwe kuheshimu wazazi wao, sio tu kwa upendo na heshima kwao, bali pia kwa kumcha Bwana. Wanahitaji kutambua kwa wazi kile ambacho Mungu anatazamia kutoka kwao na kuwa na matamanio ya kumpendeza. Ikiwa mtoto wako mkubwa hukutendea kwa kutokuheshimu, au anakuona kama mtu wa kuvumiliwa kinyume na kuthaminiwa, omba mara moja kwa ajili ya mabadiliko ya moyo ndani yake. Kama mtoto wako aliondoka nyumbani kwa kukukosea

heshima alipokuwa mchanga, ndivyo ulivyo uwezekano kwamba bado yuko hivyo sasa. Hata hivyo, haijalishi yeye ana umri gani.

Daima wazazi tunakuwa na nguvu wakati mzazi mmoja anasimama kwa ajili ya mwingine. Ninapenda wakati mimi ninapoona baba ya watoto wangu na mume wangu akisema, “Usiongee na mama yako hivyo.” Hii inaweza kufanywa kwa watoto wakubwa pamoja na watoto wadogo. Ukiruhusu mtoto wako mtu mzima akuvunjie heshima au amvunjie heshima mzazi mwingine, unachangia kuanguka kwao. Kumheshimu baba au mama sio juu ya kutoa tu zawadi nzuri ya  Mama au Siku ya Baba [mother’s day or father’s day au hata children’s day ni kila siku! Siyo zawadi bali heshima na upendo]; ni juu yao kukuonyesha heshima, kukuthamini, na upendo.

Nina rafiki yangu ambaye ni muumini lakini mume wake si muumini. Nitamwita Abby na mumewe John. Mke wa kwanza wa John alimwacha yeye na watoto wao wawili wakiwa wachanga sana, watoto ambao aliwalea peke yake. Miaka kadhaa baadaye Abby alikutana na John, watoto wake walikuwa na umri wa miaka minane na kumi. Baada ya Abby na John kuoana, John alilea watoto kama wake. Sasa wamekua na wako kwenye umri wa miaka thelathini.

Ingawa watoto hawa watu wazima wamemheshimu Abby kama mama yao, hasa Siku ya Akina Mama, walikosana na baba yao. John alitoa maelekezo yake kuhusu baadhi ya vipengele vya maisha yao, lakini hayakupokelewa na hivyo wakaacha kusema naye. Vijana wote mwaka jana na huu, hata hawakupiga simu au kumtumia kadi katika Siku ya Baba duniani, siku yake

ya kuzaliwa, au Krismasi. Bila shaka, aliumizwa sana na matendo hayo. John anakaribia umri wa miaka 70, na ni Mungu pekee anayejua ni muda kiasi gani ambao yeyote kati yetu amebakiza hapa duniani. Inahuzunisha moyo kwa Abby kuona jinsi watoto wake wakubwa walivyomvunjia heshima baba yao, ambaye alijitolea maisha yake yote kwao na kuacha kufanya mengi ili kuwainua. Sio tu kwamba wamemfanyia madhara makubwa, bali pia wamefunga baraka katika maisha yao wenyewe.

Kama ningekuwa katika hali ya Abby, ningemwita kila mmoja wa watoto na kuelezea madhara yanayotokana na kutomheshimu baba yao. Lakini kwanza ningeomba hivi: Bwana, inanihuzunisha kuona jinsi mume wangu amevunjiwa heshima na watoto wake mwenyewe. Ninaomba ya kwamba ungesaidia moyo wake kupona kutokana na kuumizwa na kuweza kuwasamehe kabisa. Geuza mioyo ya watoto hawa wakubwa kumwelekea baba yao. Naomba kwamba wao wataongozwa kumuomba msamaha kwa lolote walilokoseana. Naomba hilo likamilike na maridhiano yatokee kati yao. Nionyeshe ninachoweza kufanya au kumwambia mmoja wa watoto wetu au baba yao kusaidia hii hali. Ithibitishie mioyo yao juu ya hili kabla hawajapata matokeo ya kumvunjia heshima baba yao. Ninaomba kuwe na urejesho kamili wa mahusiano haya.

Ikiwa tunataka watoto wetu watu wazima wawe na maisha marefu na yenye matunda/tija, tunapaswa kuomba na kuwahimiza kutuheshimu kama wazazi. Hatutaki maisha yao yafupishwe au kupunguzwa kwa njia yoyote.

Tunapaswa pia kujiombea sisi wenyewe kwamba tutafanya iwe rahisi kwao

kutupenda na kutuheshimu, na sio vigumu. Upendo ndio njia kuu Zaidi ambayo kwa hiyo itahamasisha heshima. Mwambie Bwana, “Nifundishe jinsi ninavyoweza kuonyesha upendo kwa watoto na kuwaonya kwa njia ambayo inawapa heshima." Wakati mwingine kuna hali mbaya sana kiasi kwamba kuheshimu mzazi ni jambo gumu. Lakini bado ni lazima hilli lifanyike.

Namjua mwanamke Mkristo ambaye sasa ni mama mseja kwa sababu mumewe alikuwa na matatizo ya kutisha na ponografia na yeye hakuweza kuruhusu watoto wake kuvutwa na ushawishi huo. Wakati idadi kubwa ya wanaume wamekombolewa kutokana na hilo na kuweza kupata uponyaji, hakuwa mmoja wao. Aliendelea kuwafundisha watoto wake kumheshimu kama baba yao, hata ingawa hawakujua Ukweli kuhusu kwa nini wazazi wao waliachana. Wakati mtoto wao alikaribia umri wa ujana, alikiri kwa mama yake kwamba baba yake alikuwa akimuonyesha ponografia na kumdhulumu kingono. Alikuwa akiishi kwa upweke na akiwa amenyimwa haki zote za mzazi kutoka kwa mume wake wa zamani. Alikuwa mwanamke mcha Mungu, akijaribu kufanya lililo sawa kwa kuwafundisha watoto wake kumheshimu baba yao, na baba alijivunjia heshima kabisa. Wakati mwingine mzazi lazima awe anaheshimiwa kutoka mbali.

Ukweli kwamba unahitaji watoto wako wakubwa wakuheshimu kama mzazi haimaanishi kuwa unasema, "Nipe heshima au sivyo utaona, wakati wewe mwenyewe hujiheshimu kabisa na unawakwazwa hata mbele ya watu wasioamini." Wewe unahitaji kuchora mipaka inapohitajika na

kuwaonyesha watoto wako ni wapi heshima inaisha na kutoheshimu huanza. Tunapaswa pia kumwomba Mungu atusaidie kuwa katika hali ambayo itatustahilisha heshima ambayo hatuhitaji kamwe kuidai. Tunapowalea watoto wetu, mimi na mume wangu tumeona jinsi ya kupanda mbegu moja ndogo inayoweza kukua na kuwa kitu kikubwa ama kwa uzuri au ubaya, kwa kujenga au kubomoa, kumpeleka mtoto katika mwelekeo mmoja au mwingine.

Tunaweza kupanda mbegu kwa watoto wetu. Tunaposema mambo kwa watoto wetu watu wazima ambayo hujenga na kuwainua, huwasaidia kuona sifa zao nzuri na uwezo wao mkubwa na kusudi, na kuwapa hisia ya thamani yao wenyewe, basi hatutakuwa na wasiwasi kuhusu wao kutuheshimu. Watafanya tu kwa upendo na shukrani. Hebu tuombe Mungu atusaidie kupanda mbegu nzuri.

## OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAWEZE KUSTAHIMILI NYAKATI NGUMU

Sisi wazazi tunaumia sana tunapoona watoto wetu wakubwa wanapitia nyakati ngumu. Tunateseka pamoja nao, na hatutaki wapate shida. Lakini Mungu hutumia nyakati ngumu ambazo sote tunapitia kwa wema tunapotembea pamoja Naye kupitia hizo. Hiyo inamaanisha kuwa hatutalindwa kila wakati kutoka kwa nyakati ngumu, lakini ndani ya nyakati ngumu Mungu atakuwa pamoja nasi. Tunahitaji kusali kila siku ili watoto wetu wakubwa watambue kwamba “Jina la BWANA ni ngome imara;

wenye haki huikimbilia na kuwa salama” (Mithali 18:10). Omba kwamba daima watakimbilia kwa jina la Yesu, ambalo kwalo watapata ulinzi, nguvu, na usalama.

Mara nyingi Mungu ataturuhusu kupitia nyakati ngumu ili kupata mawazo yetu au kurekebisha njia yetu. Mungu anaruhusu kuteseka maishani mwetu kama njia ya kutia nidhamu ndani yetu na kututayarisha kwa yale yaliyo mbele. “Yeye ambaye BWANA ampenda humrudi, na humpiga kila mwana ampokeaye” (Waebrania 12:6).

Kusudi kuu la mateso anayoyaruhusu Mungu maishani mwetu ni kuturudisha kwenye uhusiano sahihi Kwake. Hakuna hata mmoja wetu anayeweza kusimama kuona watoto wetu wakiteseka, hata hivyo, zinapotokea nyakati ngumu kwa watoto wetu wakubwa tunataka kukimbilia na kurekebisha kila kitu. Lakini hatuwezi kuigiza nafasi ya Mungu (we can’t play God). Inabidi tumwulize Bwana ili atuonyeshe kile kinachotendeka. Ikiwa umekuwa ukiomba hivyo Mungu atapata usikivu wa mtoto wako mtu mzima na kufanya kile kinachohitajika ili kumfanya aendelee katika njia sahihi, na kisha aina fulani ya taabu hutokea, ambayo inaweza kuwa ni jibu kwa maombi yako.

Bila shaka, hatutaki watoto wetu watu wazima wateseke bila sababu, au wateseke na kujeruhiwa au kuharibiwa. Ni lazima kuwasaidia wakati msaada unahitajika, lakini sisi inabidi tumuombe Mungu hekima na utambuzi kuhusu hilo. Wakati mwingine mtoto mkubwa anapaswa kujifunza somo ngumu. Omba Mungu akupe mwelekeo na ufahamu. Na

haijalishi ni nini kinaendelea, mwombe Mungu amsaidie mtoto wako aliyekomaa kuokota chochote anachotaka au anachohitaji kujifunza kutokana na uzoefu wowote mgumu anaopitia na kumng'ang'ania Mungu.

Tunapokuwa katikati ya hali ngumu, tunatazamia kila wakati siku ambayo hali hiyo itaisha na tunaweza kuendelea na maisha yetu. Lakini Mungu anatutaka kujua kuwa maisha yetu yanaendelea hapo hapo. Anataka tujue kwamba Yeye Yuko pamoja nasi katika nyakati hizo ngumu tunapomwomba aje, na hiyo inamaanisha kuna mambo mazuri yanafanyika iwe tunaweza kuyaona kwa sasa au la. Mungu anatutaka tumwamini Yeye atuongoze kupitia humo na kutoka humo. Ni lazima kuomba kwa ajili ya mtoto wetu mtu mzima kuelewa haya yote. Pengine tunahitaji kujiombea sisi wenyewe kuelewa vizuri pia, kwa sababu wakati mwingine ni vigumu kukumbuka haya mambo tunapokuwa katikati ya majaribu.

Ikiwa kitu kibaya kimetokea kwa mmoja wa Watoto Wako Wakubwa, jua kwamba hakuna shida ngumu sana ambayo nguvu ya Mungu haiwezi kuirekebisha hali na katika kila shida ikiwa wewe utasimama imara kuna maisha ya urejesho na baraka. Unapoomba kwa ajili ya watoto wako watu wazima wanaopitia wakati mgumu, jua kwamba wanaweza kutokea upande mwingine katika hali nzuri zaidi kuliko hapo awali na kwa uhusiano wa ndani zaidi na Mungu.

Wakati mwingine hakuna njia rahisi kutoka kwenye shida, na mtoto wako mkubwa anapaswa kukabiliana nayo ana kwa ana. Kwa sababu, wakati mwingine tunapoibeba shida moja kwa moja badala yake na kujifanya kuwa

wote ni shida yetu, huhafifisha namna ambayo mtoto angejifunza kutokana na hali hiyo ngumu. Kumbuka tu kwamba wakati Mungu analetwa katika hali hiyo kupitia maombi, "Mambo yote hufanya kazi pamoja kwa wema". Ikiwa Mtoto Wako Mkubwa anateseka na kazi ya adui, omba kwamba Mungu amkomboe kutoka katika hali hiyo na kurejesha kile kilichoharibika. Urejesho kamili ndio kuishi maisha ambayo Mungu anayo kwa ajili yetu kupitia Yesu Kristo. Mapenzi Yake ni kurejesha utu wetu wote na maisha yote. Anataka kiwango hicho cha urejesho kwa watoto wetu watu wazima pia.

## OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WAELEWE WEMA WA MUNGU

Moja ya mambo mengi niliyojifunza kutoka kwa mchungaji wangu wa muda mrefu, Sambeke, ilikuwa kuwasimulia watoto wetu kisa kuhusu sisi wenyewe, familia yetu, au wao, ambayo inaweza kuboresha ufahamu wao wa wema wa Bwana na njia Zake. "Nitafungua kinywa changu kwa mfano; Nitatamka maneno ya giza ya zamani, ambayo hatukusikia wala kujua, na baba zetu wametuambia. Hatutawaficha watoto, tutakiambia kizazi kijacho Sifa za BWANA, na nguvu Zake na kazi Zake za ajabu alizozifanya" (Zaburi 78:2-4).

Mojawapo ya visa nilivyovipenda kuwasimulia watoto wangu na sasa watoto wangu watu wazima ni jinsi baba yangu alivyokuwa na mama anayeomba. Alikuwa Mkristo aliyejitolea ambaye aliombea watoto wake

wanane, na sisi binafsi tumeona matunda ya maombi hayo kwa ajili yangu na baba yao. Baba yangu aliepuka kifo mara nyingi sana maishani mwake kiasi kwamba unaweza usiamini visa vya matukio hayo. Mara nyingi nimesikia visa vyake, kutoka kwa familia zingine waumini, na kutoka kwa marafiki wa zamani wa familia, na aliwaambia mara kwa mara watoto. Wakati mmoja nilimuhoji kwa karibia saa mbili kuhusu matukio haya na niliyarekodi mazungumzo yetu kwenye kanda ili niwe na kumbukumbu yake kila wakati.

Hapa kuna njia kumi ambazo baba yangu aliepuka kifo wakati wa uhai wake:

1. Alipigwa na radi alipokuwa na umri wa miaka 14.

2. Alipata ugonjwa wa pleursy (kifua) alipokuwa mdogo kiasi kwamba ilimbidi daktari kupenyeza kisu kwenye ubavu wake na kwenye pafu ili kuiondoa bila ganzi yoyote.

3. Alipigwa risasi kichwani kwa bahati mbaya na mtu aliyekuwa na bunduki.

4. Alianguka kwenye bonde lenye kina kirefu katikati ya dhoruba ya theluji alipokuwa juu ya farasi. Farasi na wote wangekuwa wameganda hadi kufa ikiwa hakuja mtu kumtafuta na kuweza kumpata na kumtoa nje ya shimo (Cha kusikitisha Farasi hakufanikiwa kupona.)

5. Alitoka kwenye mwamba kwenye lori lake huku akisafiri kwenye

barabara yenye kupinda-pinda, iliyo na theluji juu ya barabara ya mlimani ambayo ilikuwa na barafu. Alianguka kifudifudi kama futi 50 na kuishia kwenye ukingo wa theluji uliovunja ubavu wake lakini aliweza kuendesha gari kupitia ukingo wa theluji na kuvuka mbuga hadi akapata barabara.

6. Alikuwa na mshtuko mkubwa wa moyo.

7. Aligongwa na treni iliyobomoa gari lake.

8. Alipigwa na radi mara ya pili—ingawa si kwa wakati mmoja.

9. Alishambuliwa na fahali mwenye hasira.

10. Alikaribia kuzama kwenye mto wakati farasi aliyekuwa amepanda alipoanguka naye mtoni na mguu wake ukawa umenaswa chini yake.

Siwezi kusema kwamba nilikuwa na mama anayeomba, kwamba ndiyo sababu baba yangu alinusurika uzoefu huu wa kuchungulia kaburi, lakini hakuna mtu anayeweza kuthibitisha kwamba hii sio sababu ya maombi. Niliona shimo upande wake lililotokana na ugonjwa wa pleura/Kifua. Na nikaona kovu ambapo risasi ilimpiga kichwani.

Nilimsindikiza hospitali muda mfupi baada ya kupata shambulio la moyo. Pia niliona gari alilokuwa akiendesha na kugongwa na treni. Nilikuwa na miaka kumi wakati huo, na hata katika umri huo mdogo na bila kumjua Bwana, nilifikiri ilikuwa ni muujiza. Gari liliharibiwa sana kiasi kwamba sikuweza kuelewa ni kwa vipi hakufa katika ajali hiyo. Treni iligonga gari upande wa abiria na upande wote wa kulia wa gari lake lilikuwa

limekunjwa upande wa dereva. Nakumbuka nilitazama gari hilo na nikishangaa jinsi baba yangu, ambaye alikuwa mtu mkubwa, angeweza kutoshea nafasi ndogo iliyoachwa kwa ajili yake. Na hakuwa na mkwaruzo mwilini mwake. Kwa kweli, katika matukio haya yote, hakuwa na uharibifu wa kudumu wa kimwili isipokuwa makovu na hakuna hata mfupa mmoja uliovunjika.

Hatari yoyote kati ya hizi ingeweza kumuua, lakini alikufa usingizini kitandani mwake mwenyewe alipokuwa na umri wa miaka 93, akiwa bado ana akili timamu na hakuna ugonjwa unaojulikana kwamba ulimuua. Ilikuwa ni njia ambayo siku zote alitaka kufa.

Haya yote yanatokeaje? Baba yangu hakuwa mtu wa kutumia vizuri nafasi. Yeye aliishi maisha ya tija kadri alivyojua, mara nyingi katika hali ngumu. Lo, na nilisahau kusema kwamba alinusurika sana kuangamia wakati anaishi na mama yangu ambaye alikuwa mgonjwa wa maradhi ya akili na mnyanyasaji hivi kwamba angekuwa amekufa tangu zamani. Angewezaje kuishi muda wote wa haya matukio ya karibu kufa? Naamini ni kwa sababu alikuwa na mama mwombezi (prayer warrior mother). Alikufa akiwa mzee, na watoto wake wote wanane waliendelea kuishi hadi uzee vilevile.

Baba yangu ndiye mfano wangu mkuu wa jinsi maombi ya mzazi anayeomba yanavyoweza kumlinda mtoto, na baadaye mtoto mzima, kwa maisha yao yote na kuwapitisha katika nyakati ngumu. Sala zako kwa ajili ya mtoto wako mtu mzima zinaweza kufanya vivyo hivyo.

## NGUVU YA MAOMBI

Bwana, ninaomba mkono wako wa ulinzi uwe juu ya watoto wangu wazima. Naomba kwamba wakutumaini Wewe kama ngao na mlinzi wao (Mithali 30:5). Walinde kimwili kutokana na ajali zote, magonjwa, udhaifu, vitendo vya ukatili na hatari za ghafla, na mipango ya uovu. Kuwa mlinzi wao wakati wowote wakiwa ndani ya gari, ndege, shule, maabara, basi, mashua, au vyombo vingine vya usafiri. Popote wanapotembea, naomba kwamba miguu yao isiteleze; kuwaongoza mbali kuelekea hatari (Zaburi 17:5). Waweke salama kila wakati. Ninaomba kwamba ungewazunguka na malaika Wako ili kuwalinda ili wasijikwae (Zaburi 91:12).

Wasaidie kusikia sauti yako uwaongoze, na uwafundishe kukutii Wewe ili wawe ndani ya mapenzi yako daima na mahali pazuri kwa wakati ufaao. Ninaomba kwamba "kumcha BWANA" kutakuwa ndani yao "chemchemi ya uzima" ambayo itatumika kuwageuza "kutoka kwenye mitego ya mauti" (Mithali 14:27). Nakuomba uweke macho Yako juu yao na wasiondoe macho yao mbali na Wewe. Wasaidie wajifunze kukaa katika kivuli Chako na chini ya mwavuli wa ulinzi wako (Zaburi 91:1). Ninaomba kwamba Wewe uwe "kimbilio lao na nguvu" na "msaada wao uliopo wakati wa taabu" (Zaburi 46:1). Naomba kwamba hapana silaha itakayofanyika juu yao itakayofanikiwa (Isaya 54:17). Kuwa na huruma kwao na uwape usalama "katika uvuli wa mbawa Zako" mpaka maafa yamepita" (Zaburi 57:1).

Wape hekima, busara, na ufunuo wanaohitaji ili kukaa salama na wasiingie

hatarini. Bwana, umesema katika Neno Lako kwamba ingawa watu waovu wanajaribu kuharibu mwenye haki hutaruhusu (Zaburi 37:32-33). Linda watoto wangu wakubwa kutoka kwa mipango yoyote ya uovu. Walinde na matatizo ya kisheria, kwa maana haki hutoka Kwako Wewe (Mithali 29:26). Kuwa nao wanapopita kwenye maji ya kina kirefu na zuia mto usiwafurikie. Wawezeshe wanapopita katika moto wasichomwe moto wala kuteketezwa kwa moto (Isaya 43:2). Bwana, ninaomba wanapopitia hayo mara, Wewe utakuwa mtetezi wao. Ninaomba kwamba wajifunze kukutazama Wewe ili uwe msaada wao (Zaburi 121:1-2). Nguvu za adui si kitu kwa uweza Wako mkuu. Wavike nguvu za vita na kuwaweka salama (Zaburi 18:39). Wasaidie "kuzitupilia mbali kazi za giza,…vaeni silaha za nuru" (Warumi 13:12). Naomba kwamba wao watajifunza kukulilia katika dhiki zao, nawe utawaokoa kutoka kwa dhiki yao (Zaburi 107:6).

Ninaomba kwamba mambo magumu wanayopitia yatumike kwa utukufu Wako na kwa kuimarisha uhusiano wao na Wewe. Wasaidie wasife moyo bali waamini kwamba wataona wema Wako katika maisha yao na katika kila hali (Zaburi 27:13). Haijalishi nini kitatokea, naomba kwamba hatimaye wataweza kusema, "Hili lilikuwa jambo la BWANA; ni ajabu machoni petu" (Zaburi 118:23). Wasaidie waelewe kwamba wanaweza "kulala kwa amani, na kulala usingizi; kwa Imani Kwako peke yako, Ee BWANA," uwajalie "wakae salama" (Zaburi 4:8). Katika Jina la Yesu ninaomba. Amen.

**NGUVU YA NENO**

Upitapo katika maji mengi nitakuwa pamoja nawe; na katika mito, haitakugharikisha. Upitapo katika moto, hautateketea, wala mwali wa moto hautakuunguza.

**ISAYA 43:2**

BWANA atakulinda utokapo na uingiapo tangu sasa; na hata milele.

**ZABURI 121:**8

Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, Sitaogopa mabaya; kwa maana Wewe U pamoja nami; Gongo Lako na fimbo yako vyanifariji.

**ZABURI 23:4**

Maskini huyu alilia, na BWANA akamsikia; kumuokoa na taabu zake zote.

**ZABURI 34:6**

BWANA ni jabali langu na ngome yangu na Mwokozi wangu; Mungu wangu, nguvu zangu, nitakayemwamini; ngao yangu na pembe ya wokovu wangu, ngome yangu. nitamwita BWANA astahiliye kusifiwa; hivyo nitaokolewa kutoka kwa maadui zangu.

**ZABURI 18:2-3**

## OMBA ILI WATOTO WAKO WAKUBWA WATAMBUE WANAVYOMHITAJI MUNGU

Nimeongeza sura hii mpya kwa toleo la hivi majuzi zaidi la kitabu hiki kwa

sababu, katika Miaka ile ya awali nilipoandika kwa mara ya kwanza Nguvu ya Kuombea WATOTO WAKO WAKUBWA, Nimegundua kuna kitu kwa vijana wengi ambacho kinaonekana kuenea na ni cha kutiliwa umakini. Na hilo ni kwamba wengi wao hawatambui namna wanavyomhitaji Mungu. Hapa nazungumzia hata wale ambao ni waumini. Bila shaka, watu wasioamini hawana fununu kwamba wanamhitaji Mungu kwa sababu hawamjui Mungu. Hivyo hawafanyi hivyo kwa vile wanakosa kuelewa wanapungukiwa na nini katika maisha yao. Lakini hata vijana Wakristo, ambao watu wazima ambao wamelelewa kanisani, au wamekuwa kanisani kwa muda, mara nyingi hawafanyi hivyo, yaani hawana njaa ya Mungu zaidi katika maisha yao, hitaji ambalo litasaidia kufanya uzoefu wa yote Mungu aliyo nayo kwa ajili yao.

Ingawa nimeona vijana wengi watu wazima wapo hai katika Bwana na kuendeleza njaa kwa ajili Yake na Neno Lake Mwenyezi Mungu, bado kuna wengi sana ambao hawahisi hitaji lao la Mungu. Kwa sababu ya yote niliyopitia katika maisha yangu ya awali kabla sijamjua Bwana nilikuwa na umaskini mkubwa, unyanyaswaji, huzuni, kukata tamaa, magonjwa, wasiwasi, na kukata tamaa.

Hatimaye nilipompokea Bwana nikiwa na umri wa miaka 28, nilijua singeweza kuishi bila Yeye tena. Kufikia wakati huo nilikuwa nimepoteza matumaini yote hata kufikia mwisho, kwa kukataa tamaa ya kuishi kwa njia hii, yaani siku nyingine tena ya maumivu ya kihisia. Nilikuwa napanga kujitoa uhai mara tu nitakapoweza kupata dawa za usingizi za kutosha

kufanya kazi hiyo kwa usahihi. (Dawa hizo hazikuwa rahisi kupatikana wakati huo kama ilivyo leo.)

Lakini natoa shukrani kwa rafiki yangu, na mchungaji wake. Kupitia kanisa nilikutanishwa na Mungu aliye hai wa upendo na amani, na nikaona Kwake njia ya kutoka gizani na ubatili na kuletwa katika maisha ya mwangaza na kusudi. Niliona kwamba Bwana alikuwa kila kitu ambacho mimi nilihitaji, na hamu yangu kubwa Kwake, iliongezeka siku hadi siku.

Ndio maana leo mimi lazima kabisa nipange wakati wa kuwa peke yangu na Bwana katika Neno Lake na katika maombi na kuabudu kabla sijaikabili siku. Siwezi kuishi kwa mafanikio wakati wowote hata kidogo bila kuhisi nguvu, amani, na usalama wa uwepo Wake Bwana ndani na karibu na mimi. Ninamtegemea Yeye kabisa. Mungu anataka sisi sote tumtegemee Yeye kabisa. Ninapoona watu ambao hawaonekani kuwa na hitaji kama hilo, huwa nashangaa-shangaa, Je! Wanaishi hivyo Kweli bila msaada, wanawezaje?

Je, anaishi vipi bila sauti Yake kuongea na mioyo yao kila wakati siku inapoendelea? Ni aina gani ya imani ya uwongo waliyo nayo ambayo hawafikirii kuwa wanamuhitaji Yeye kwa jambo lolote? Inakuwaje kwamba hawasumbuliwi na Ukweli kwamba wao hawana nguvu zozote zile za maana, na hivyo waombe kupata uwezo mkubwa zaidi kuliko ule walio nao, ili waweze kutimiza kitu kikubwa kuliko kile ambacho wanaweza kupata wakiishi bila kumhitaji Mungu?

Nashangaa ninapoona hata wale wanadamu wanaojiita Wakristo wana tabia ya kusema Nitatembea kutoka hapa hadi pale mwenyewe, Mungu nitakuita ikiwa nitakuhitaji. Hata hivyo, najua kwamba mtu ambaye amempokea Yesu na kubebwa kutoka kwa mengi pia hupenda sana. Unapojua mateso, utata, changamoto, malumbano, vita na maumivu ya Maisha yenye ombwe yaani maisha bila Yesu au utupu. Hakika unampenda sana Mwokozi ambaye anakuinua kutoka kwa yote. Unapojua maana ya kukata tamaa, unathamini sana wokovu. Na hiyo inaweza kuwa msaada mkubwa.

Vijana wengi hawaoni upwekwe au ombwe lolote kubwa katika maisha yao. Itakuwa vizuri endapo watoto wetu wakubwa wataachana na mambo mengi ndani ya maisha ambayo huwafanya wasifikirie kuwa wanamhitaji Bwana kwa chochote. Wanakuwa na ubize na kuwa kama wako sokoni kwenye makelele mengi, mpaka mambo yagote mwambani. Baadhi kimakosa wanaamini kwamba mahitaji yao yote yatatolewa kwa sababu ndivyo maisha yalivyokuwa hapo awali kwao. Mama, Baba, au mtu mwingine aliwapa kila hitaji lao, hivyo ni wazi kuwa ni hitaji la Mungu pia, wapate kila kitu wanachokitaka. Lakini Mungu hutupatia tu mahitaji yetu yote tunapokubali kwamba Yeye na upendo Wake, ndiyo haja yetu kubwa na zaidi.

Yeye Anataka tutambue utegemezi wetu Kwake ma kumtafuta kama jibu la kila hitaji letu. Lakini watoto wetu watu wazima bado hawatatambua hitaji lao kwa Mungu ikiwa wanafikiri kila hitaji litatimizwa na sisi wazazi au mtu mwingine.

Nimefanya kazi tangu nikiwa na umri wa miaka 14. Wazazi wangu walikuwa maskini na wasingeweza kunipa kila kitu, kwa hivyo ikiwa nilitaka au nilihitaji chochote, ilibidi nipate pesa za Kukilipia hicho kitu. Matokeo yake sasa naamini mimi nimefaidika Zaidi ya wale ambao hawakufanya hivyo, yaani hawakuwa na haja kufanya kazi kwa lolote. Kwa hivyo ikiwa wewe ni mzazi ambaye huwezi humudu kutoa mahitaji ya kila kitu kwawatoto, kamwe usijisikie vibaya juu ya hilo.

Ikiwa umewapa watoto upendo, kujali, na mafundisho ya Mwenyezi Mungu, basi wewe umewasaidia kuona kwamba kuna vitu vya thamani wanahitaji kuvifanyia kazi na kumtafuta Mungu hufungua mlango kwa ajili ya mengineyo. Ingawa mume wangu nami, sote tulikuwa na maadili ya kumtafuta-Mungu-na- kufanya kazi, ambapo tungeweza kumudu kutoa huduma kwa watoto zaidi kuliko tulivyowahi kupewa na wazazi wetu, tulijua fika kuwa tunapaswa kuwafundisha Watoto wetu kumtafuta Mungu kwa mwongozo na kuwasaidia kukuza ujuzi waliohitaji, na pia kufanya kazi kwa bidii na kwa mwongozo Wake, huku tukimtegemea Yeye kufungua milango ambayo wao walipaswa kupitia. Bado hata leo naomba waendelee kutambua hitaji lao zaidi la Bwana katika maisha yao na kuishi katika namna hiyo ya kumtegemea Yeye.

Wakati hatutambui hitaji letu la Mungu na kushindwa kuja Kwake kuimarishwa na kuhuishwa katika uwepo Wake, Yeye huruhusu mambo yatukie ambayo hutufanya tujue kwa uchungu juu ya ukosefu wetu. Ikiwa hatukai mkao mzuri kwa ukamilifu, tusipotafuta uwepo wa Bwana kila siku,

tunaweza kupotea na kutoja nje ya kivuli na ulinzi Wake, mahali ambapo mambo mabaya hutokea. Na hapo pia ni mahali hatari kuwepo. Hakika kuwa katika Bwana kunatufanya tuwe wema kwa wanadamu wenzetu, majirani wema, jamaa wema, wana jumuia wema, na salama kutwaliwa kwenda mbinguni! Je, ungependa mtu asiyemcha Mungu kuwa karibu nawe? Mimi nina hofu ya Mungu na hofu ya mtu mwovu!

Nimethibitisha maishani kwamba mtu yeyote ambaye hatatambua hitaji lake la Bwana, anaweza kujaribu kutimiza mahitaji yake kwa njia ambayo ni inaleta utupu tu moyono. Na wanaweza kunaswa juu yake na kushughulika nayo hadi kufikia hatua ya kuiabudu mali na kuiruhusu kuwatia ganzi kwa sauti ya Mungu ikinena na mioyo yao. Wanamkosa Mungu maishani mwao na hiyo inasikitisha, kwani Ndiye disaina wa maisha na bila Yeye, huwa siyo kamili, yana matobo mengi na mipasuko.

Kumtegemea Mungu kabisa sio tu mahali pa uhuru lakini pia mahali salama pa kuwa. Biblia inasema kuhusu watu wasiomtafuta Bwana, "Kwa sababu wanasema, 'Mimi ni tajiri, nimejitajirsha, wala sina haja ya kitu chochote' na wala hawajui ya kuwa wao ni wanyonge, wenye huzuni, mashaka, maskini, vipofu, dhaifu, na uchi. Bwana anawashauri wanunue kutoka Kwake dhahabu iliyosafishwa kwa moto, wapate kuwa tajiri; na mavazi meupe ya haki, wajifunike aibu ya uchi wako isifichuliwe; na wapakwe dawa ya macho ili wapate kuona. (Ufunuo 3:17-18).

Kwa maneno mengine, watu wengine wanafikiri wana kila kitu na hawahitaji kitu, lakini kwa hakika wao ni maskini, vipofu, na wenye huzuni

kwa sababu hawana utimilifu, utajiri, na usafi wa Bwana unaowaruhusu kuona mambo kwa mtazamo wake. Tunapojazwa na vitu vingine badala ya Mungu, tutakuwa na njaa daima. Tukijua tuna njaa na kutafuta kujazwa na Mungu, hatutakuwa kamwe na njaa ya kitu kingine chochote.

Moja ya zawadi ambazo Mungu hutupa ni ufahamu kuhusu sis wenyewe kwamba tunamhitaji kila siku na sio tu wakati tunakata tamaa. Hiyo ni kwa sababu tusipoelewa hilo, tutakata tamaa. Moja ya zawadi kubwa zaidi tunazoweza kutoa kwa watoto wetu  watu wazima ni kuomba wapate ufahamu kwamba wanamhitaji Mungu na kwamba bila Yeye hawawezi kufanya lolote kubwa au la kudumu-hawawezi kutoboa shimo na kutoka! Omba watoto wako wasiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia ambayo si ya Mungu. Maana Biblia inasema mtu akiipenda dunia, kumpenda Mungu hakumo ndani yake. Tamaa ya macho na kiburi cha uzima si Vyake Bwana na havitadumu (1 Yohana 2:15-17).

Usiogope kuruhusu mtoto wako apitie mambo fulani ili aweze kufikia hitimisho hilo. Kama wazazi tunapaswa kuwaombea usalama na ulinzi, lakini hatupaswi kuogopa mapambano wanayopitia ili kutambua kwamba wanamhitaji Bwana kila siku. Hilo si jambo baya. Kwa kweli, ni  zuri. Kile ambacho si kizuri ni kama wana vichwa vigumu kiasi kwamba wanakataa kutambua haja ya Mungu mpaka wasiwe na uwezo kwa namna fulani wa kujisalimisha na kufanya dhoruba ipite na hivyo wapate mateso yasiyoweza kurekebishwa yenye uharibifu au hasara.

Kuruhusu watoto wako kupata baadhi ya mambo bila kuwawekea dhamana

lazima ifanywe kwa maombi kwa uongozi wa Roho Mtakatifu. Kumbuka kwamba adui anataka waangamizwe. Kwa hiyo tafuta nia ya Mungu juu ya somo hilo. Endapo mtoto wako mkubwa anayewajibika kifedha kwa kawaida hawezi kulipa mkopo wa nyumba yake kwa sababu ya kuachishwa kazi au aina fulani ya ugonjwa mkubwa, shida ya kifedha, na una njia ya kusaidia hadi yeye avuke salama kwa vyovyote vile fanya hivyo.

Lakini hawezi kulipa mkopo wa nyumba kwa sababu ya uraibu wa kamari, unywaji pombe, mwenendo usio na nidhamu, kwa kutowajibika kushikilia kazi kwa ubora, au kutojali na pesa, basi yeye anaweza kuhitaji kupata matokeo ya tabia. Mwombe Mungu akuonyeshe Ukweli kuhusu hali hiyo na mapenzi Yake ni nini, Naye atakupa amani kwa njia moja au nyingine.

Najua inaweza kuonekana kuwa ngumu kuwaruhusu watoto wako watu wazima wapate shida fulani. Unahitaji kumwamini Mungu pamoja nao. Unahitaji kuwa nyuma yao katika maombi. Hiyo haimaanishi kutokuwa na upendo. Unapaswa kufanywa yote upendo kamili, ila hiyo inamaanisha kuwa na moyo wa Mungu kwa ajili yao. Unahitaji kujua mapenzi ya Mungu katika suala hilo.

Kumbuka mifano niliyotoa hapo awali kwenye kitabu kuhusu seti mbili za wazazi ambao waliwaacha watoto wao husika kwenda jela na nini matokeo ya kila mmoja wao. Seti moja ya wazazi waliomba na kupata uongozi wa Bwana na wengine hawakufanya hivyo. Lazima uwe na hakika kuhusu hili. Kuwa mwombezi wa maisha ya watoto wako wakubwa huwasaidia kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa sio tu kusikia kutoka kwa Mungu, lakini kujibu

kwa Mungu pia na kuwajibika Kwake! Na kwa sababu hakuna mtu atakayemuombea mtoto wako kwa bidii kama wewe unavyofanya, Mungu atasikia maombi yako. Yeye Anataka Watoto Wako Wakubwa waelewe ni kiasi gani wanamhitaji Yeye hata zaidi ya vile unavyotaka wewe. Baada ya yote, hakuna mtu anajua wazi zaidi, kiwango kamili cha matokeo ya kutofanya hivyo kuliko wewe.

Sikuzote Mungu Yuko tayari kufanya mengi zaidi kwa ajili yetu kuliko wengi wetu watakavyoruhusu au kumwalika afanye Waefeso 3:20,21 - Utukufu ni Wake Yeye, ambaye ana uwezo wa kutenda zaidi ya yale tunayoyaomba na kuyawazia, kwa kadiri ya nguvu Yake inayofanya kazi ndani yetu. Utukufu ni Wake katika kanisa na katika Kristo Yesu kwa vizazi vyote, milele na milele. Amina.. Biblia inasema, “Mungu wangu atawajazeni kila mnachohitaji kwa kadiri ya utajiri Wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu” (Wafilipi 4:19). Yeye Atatupatia kila kitu tunachohitaji, lakini kwanza lazima tukubali hitaji letu. Paulo alisema, “Si kwamba nasema haya kwa kuwa nina mahitaji; maana nimejifunza kuwa radhi na hali yo yote niliyo nayo.” (Wafilipi 4:11). Sababu anaweza kuwa Na hali iliyokuwa ikitokea katika maisha yake ambayo alitambua hitaji lake yaani namna anavyomhitaji Mungu na kwamba Mungu pekee Ndiye angetimiza mahitaji yake yote. Ni lazima kuomba kwa ajili ya sisi wenyewe, pamoja na watoto wetu watu wazima, kwamba tunatambua Mungu pekee Ndiye atatupa mahitaji yetu yote, na ndiyo maana hitaji letu la kwanza na kuu zaidi ni la Yeye zaidi katika maisha yetu.

## NGUVU YA MAOMBI

Bwana, ninaomba kwa ajili ya ……….. (jina la mtoto mzima) kwamba utamsaidia kutambua namna anakuhitaji kuliko kitu chochote. Usimruhusu aishi kana kwamba hana kusudi la Mungu katika maisha yake. Wewe kuwa msimamizi wa maisha yake. Msaidie yeye kuona kwamba kumpinga Mungu hakutampatia chochote cha kudumu, lakini Wewe, Yesu, unatoa kila kitu.

Usimruhusu kuwa adui Wako kwa kuwa rafiki wa dunia. Ninaomba kuwa ungezima mvuto wa kila mbegu kutoka kwa akili ya kilimwengu ambayo imepandwa ndani yake yake ili isiweze kukua. Ninaomba ungenyamazisha kila sauti ambayo haitokani na wewe inayosema upotovu moyoni mwake. Ninatamani kujua kuwa mtoto wangu ana Ukweli na hataingia kwenye roho ya udanganyifu (3 Yohana 4). Mshike aondokane na kuupenda ulimwengu kuliko yeye anavyokupenda Wewe (1 Yohana 2:15-17).

Ninaomba kwamba mtoto wangu mtu mzima atachukia uovu. Mwezeshe na kumzuia "miguu yake kutoka katika kila njia mbaya" ili yeye "apate kushika Neno Lako" kwa sababu yeye anakutazama Wewe ili kumfundisha njia sahihi ya kuishi (Zaburi 119:101). Umlinde na umwokoe kutoka mikononi mwa waovu. Ninaomba kwamba yeye hatakuwa "vuguvugu" kuhusiana na uhusiano wake na Wewe (Ufunuo 3:16). Usimruhusu kuridhika sana na maisha mbali na Wewe. Kamwe asifikiri wala kusema, "Sihitaji kitu" (Ufunuo 3:17). Msaidie kufahamu kwamba ikiwa yeye hataifanya sheria  Yako kuwa furaha yake, yeye kamwe hataishi kwa amani (Zaburi 119:92).

Msaidie kuelewa kwamba Unajua mahitaji yake kwa uwazi zaidi kuliko yeye) anavyotambua (Luka 12:29-30). Mfundishe kukutafuta Wewe akijua wewe Ndiye ficho lake na tumaini (Zaburi 119:114). Mtie nguvu kuchagua amri Zako na aondoke kutoka kwa wale ambao wangemwongoza mbali na Wewe (Zaburi 119:115). Ambapo yeye amepotoka kutoka Kwako, naomba mtendee kwa rehema Zako na umfundishe yeye njia Zako "kama desturi Yako kwa wale walipendao Jina Lako" (Zaburi 119:124,32).

Nisaidie kuishi kwa njia Yako na kwa utegemezi kamili Kwako ili yeye avuviwe kutembea katika njia hiyo hiyo (1 Yohana 5:2). Katika Jina la Yesu ninaomba. Amina.

**NGUVU YA NENO**

Kama vile ayala anavyotamani vijito vya maji, ndivyo nafsi yangu inavyokuonea Wewe shauku, Ee Mungu. Nafsi yangu ina kiu ya Mungu, Mungu aliye hai.

**ZABURI 42:1-2**

Mimi ni maskini na mhitaji; unifanyie haraka, Ee Mungu!

Wewe ni msaada wangu na Mwokozi wangu; Ee BWANA, usikawie.

**ZABURI 70:5**

Lolote mfanyalo, lifanyeni kwa moyo, kama kwa Bwana, wala si kwa wanadamu, mkijua kwamba mtapokea kwa Bwana ujira wa urithi; kwa

kuwa unamhudumia Bwana Kristo.

**WAKOLOSAI 3:23-24**

Ole wenu ninyi mlioshiba, kwa maana mtaona njaa. Ole wenu ninyi mnaocheka sasa, kwa maana mtaomboleza na kulia.

**LUKA 6:25**

Ee Mungu, Wewe ni Mungu wangu; mapema nitakutafuta; nafsi yangu inakuonea kiu; mwili wangu wakuonea shauku katika nchi kame na yenye kavu isiyo na maji.

**ZABURI 63:1**

## OMBA ILI WATOTO WAKO WATU WAZIMA WATEMBEE NA MUNGU KATIKA WAKATI WOTE UJAO

Hakuna wakati hauhusiki tena na watoto wako wakubwa na unaweza kutazama kisa cha maisha yao kikitokea kama filamu. Unafikiria tu unaweza kuacha kuwa na wasiwasi juu ya maisha yao ya baadaye mara wanapomaliza shule au wanapokuwa na kazi salama au mara tu wanapoweza kumudu kununua nyumba au mara wanapoweza kupanga mambo yao ya maisha au mara wanapokutana na mtu mzuri mtu wa kuoa au kuolewa nae au mara moja wanapokuwa wamefanikiwa au mara wanapopata watoto wao wenyewe au mara wanapopona au mara tu wanapopatana na Bwana au mara moja wanapowaondoa marafiki wabaya

au mara tu watakapokuwa huru kutoka kwa hiyo tabia haribifu au mara wanapogundua maisha au mara wanapoacha kufuata njia mbaya za maisha au mara wanapogundua Mungu aliwaumba kuwa nani.

Mtu mmoja aliwahi kuniuliza ikiwa kuwa na watoto wakubwa ni kifungo cha maisha. Nikasema nilihisi tu kama nilikuwa najitakia mambo kuwa magumu wakati nilipoacha kuomba. Wakati ninaomba, mimi niliona kama kazi ya kuwaweka mikononi mwa Mungu ni kazi ya miaka yote, ili mapenzi yake yaweze kufanyika katika maisha yao. Lakini kuna baadhi ya mambo sisi lazima tukumbuke daima kwamba yatatutia moyo kuendelea kuomba, jitahidi kupata amani huku ukingoja Mungu akujibu. Kumbuka Ahadi ya Mungu kwa mtoto wako Mkubwa Wakati ujao.

Neno la Mungu linasema nini juu ya maisha yajayo ya mtoto wako mtu mzima ndicho anachosema kwa ajili ya kesho yako pia. "Nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema BWANA; Ni mawazo ya amani na si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zijazo. Basi mtakwenda na kuniita, mtaniomba, Nami nitawasikiliza. Nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote" (Yeremia 29:11-13).

Angalia uhusiano kati ya ahadi ya kuwapa wakati ujao wenye furaha, uliojaa matumaini na maombi. Tena ni maombi ambayo yana ahadi. Mungu anasema kama ukimtafuta na kumtafuta kwa moyo wako wote, utampata na anakuwazia makubwa kwa ajili ya kesho yako.

Kama wazazi wa watoto wakubwa, hatuwezi kujiruhusu kukaa kwenye

mitazamo hasi. Tunapaswa kudhibiti mawazo na hofu zetu na tusiruhusu wasiwasi kupata nafasi mioyoni mwenu. Ikiwa hatufanyi hivyo, mawazo yetu yanayojali kuhusu wakati ujao wa mtoto wetu watu mzima yanaweza kutunyima furaha na kutufanya wagonjwa katika miili, akili na roho zetu. Itakuwa utumwa ambao sisi, basi, tutahitaji kuwekwa huru nao. Hatuhitaji kuishi kwa njia hiyo tunapoweza kuomba.

Mojawapo ya njia safi kabisa za maombi ni sifa. Tunaweza kuzima hofu ya yote yajayo kwa ibada. Tunapomwabudu Mungu, tunamgusa Yeye na ufalme Wake, na kwa kuitikia ibada yetu Roho wa Mungu hutugusa. Kusifu na kuabudu ndio njia ya uhakika ya kukaribisha uwepo wa Mungu katika maisha yetu na mioyo yetu. Uwepo wa Roho Mtakatifu unaweza kutupatia uhuru kutoka kwa hofu zote kuhusu siku zijazo. Kumbuka Kuwa Una Tumaini Katika Bwana Siku Zote na Matumaini yanatufanya tuendelee mbele, na wala tusikate, tamaa, naam tunajua vita ipo duniani katika wema na ubaya ila tunajipa moyo kwaana Kristo alimshinda Shetani. Ni nini hutuamsha asubuhi na kutufanya tuombe? Matumaini hayakita kwenye msingi wa matamanio ya kitu; bali ni kuamini ahadi za Mungu. “Tumaini halikatishi tamaa, kwa sababu upendo wa Mungu umemiminwa mioyoni mwetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi” (Warumi 5:5).

Upendo wa Mungu ndani yetu hutia moyo tumaini, ambalo huchochea maombi na ujasiri wa kuamini. Adui anajaribu kuiba tumaini letu kuhusu wakati ujao kwa uwongo wake, lakini tunaweza kumnyamazisha kwa Neno la Mungu na kupata furaha katika mchakato huo. “Umenijua njia za uzima;

Utanijaza furaha mbele za uso Wako" (Matendo 2:28). Hakuna kinachojenga imani yako na kukufanya ujisikie vyema kuhusu siku zijazo kuliko kusoma kile Mungu anasema.. Biblia inasema, "Tumaini linalodumu humfanya mtu Mwenye moyo mgonjwa, kusitawi kama mti wa uzima" (Mithali 13:12).

Kama mtoto wako mtu mzima amevunjika moyo kwa sababu shauku yake ya siku zijazo haikujibiwa na maombi yamechelewa, mwombe Mungu aujaze moyo wake tumaini katika Jina Lake, furaha katika uwepo Wake, na faraja ndani ya Neno Lake. Yeremia alisema unapomwamini Mungu na kuweka tumaini lako Kwake, utakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji na mizizi yake inaenea kando ya mto na kwa hiyo huna haja ya kuogopa wakati joto linawaka katika maisha yako. Si lazima kuhangaika wakati wa ukame (Yeremia 17:7-8). Ikiwa umewahi kuwa katika ukame wa kutisha, ikitokea unakuwa nje ya maji, unagundua kuwa maji ni bidhaa ya thamani na muhimu, kwani huna maisha bila hiyo. Wakati wewe au watoto wako watu wazima wako mahali pakavu, Mungu atawamiminia maji ya uzima na tumaini litapanda juu mioyoni mwenu.

Kumbuka kwamba Mungu ni Mwenye Rehema na Mwenye Huruma. Wakati fulani Yeremia alikuwa amepoteza tumaini kabisa. Mambo yalikuwa mabaya sana kiasi kwamba hakukumbuka kuwa na matumaini tena. Lakini baadae alikumbuka rehema za Mungu. "Hili nalikumbuka akilini mwangu, kwa hiyo nina tumaini. Ni kwa rehema za BWANA hatuangamii, kwa maana rehema Zake kazikomi. Ni mpya kila asubuhi;

Uaminifu wako ni mkuu. 'BWANA ni sehemu yangu,' nafsi yangu husema, 'Kwa hiyo ninamtumaini Yeye!' (Maombolezo 3:21-24).

Haijalishi ni nini kimetokea huko nyuma, Rehema za Mungu ni mpya leo. Unaweza kutubu dhambi leo. Mungu anaweza kufanya mambo yawezekane leo na pia anaweza kubadilisha mambo leo. Matumaini yanaweza kujaza moyo wako leo. Yeremia alizungumza juu ya umuhimu wa kumngojea Bwana. Hiyo ina maana kuwa na subira kumngoja Mungu ajibu maombi yako. "BWANA ni mwema kwa wale wanaompenda, umngojee. Ni vizuri kwamba mtu anapaswa kutumaini na kungojea wokovu wa BWANA kwa utulivu" (Maombolezo 3:25-26). Kumsubiri Bwana ni matarajio yenye matumaini ya kile ambacho Mungu anaenda kufanya. Ni kuamini juu ya kile Bwana anachoenda kufanya na kuona kwamba ni jambo la thamani kumngojea Bwana.

Yeremia pia alikumbuka kwamba Mungu ataonyesha huruma sikuzote. Mungu hataki tuteseke milele. "Bwana hatamtupilia mbali milele mtoto wako. Ingawa Mungu ataruhusu huzuni, bado Ataonyesha huruma kulingana na wingi wa rehema Zake. Kwa ajili Yake hawatesi wapendwa Wake, wala kuwahuzunisha wanadamu" (Maombolezo 3:31-31).

Si mapenzi Yake kwamba tuteseke, lakini anaruhusu mateso yatufundishe njia Yake. Kukumbuka kwamba Mungu ni Mwenye rehema na huruma kunakusaidia kuendelea kuomba, ukijua kwamba hivi karibuni ataonyesha rehema na huruma Yake kwako na watoto wako wakubwa. Kumbuka Kutuma Barua kwa Mwanao au Binti yako Kuhusu Mustakabali Wao na

mapenzi ya Mungu kwao.

Ikiwa wewe au mimi tungechukuliwa kwenda mbinguni leo, labda kungekuwa na mambo mengine ambayo tunatamani tungewaambia watoto wetu wakubwa. Unaweza kuandika yote au sehemu tuu ya yale ungependa kuwaambia kwa maneno yako mwenyewe, na uwape watoto wako watu wazima sasa au uweke katika mahali ambapo watayasoma baadaye. Mwambie Mungu akuonyeshe wakati sahihi kwao kuipokea. Natumai barua hii itakutia moyo kwa zaidi ya nilivyosema hapa.

Mpendwa,

Ninakuandikia barua hii kwa sababu nataka kukuambia kuwa tunakupenda wewe na tunajivunia wewe. Ninaona ukuu wote, karama, na talanta ambazo Mungu ameweka ndani yako, na tunajua atakutumia wewe kufanya mambo makuu kupitia wewe. Labda hatukuwa wazazi wakamilifu, na huenda hukuwa mtoto mkamilifu, lakini Mungu alijua tulikuwa wakamilifu kwa kila mmoja wetu. Na sote tunajua sasa kwamba hakuna aliye mkamilifu isipokuwa Bwana. Ninamshukuru Mungu kila siku kwa wewe na baraka ya ajabu uliyo nayo, na amekuwa daima Baraka kwa maisha yangu.

Nimekuwa nikikuombea na nitaendelea kukuombea maadamu niko hai kwamba utakuwa na maisha marefu na ya ajabu baadaye. Mungu anasema kwamba ikiwa unamwamini, basi hakuna mwanadamu ambaye anaweza kufikiria jinsi wakati ujao ulivyo mzuri kwa ajili yako. Lakini haifanyiki

bila maombi. Tunapaswa kuomba na kuendelea kuomba.

Ninaomba kwamba uhusiano wako na Mungu uwe wa karibu na wenye nguvu, na kwamba utakua katika upendo kwa Neno Lake na njia Zake. Naomba Mungu amimine Roho Wake upya juu yako kila siku, akuongoze, akufundishe, akufariji, akuponye na kukuweka huru, akuongezee imani yako, na kusema na moyo wako.

Ninaomba kwamba daima utahisi uwepo Wake na kamwe hutamfungia Mungu nje ya maisha yako. Kumbuka kwamba maisha ya kuishi na Mungu huwa hayakosi changamoto, kwa sababu daima utakuwa na adui anayejaribu kukuangusha na ukiwa na Mungu atakupa nguvu ya kukabiliana na changamoto hizo na hekima ya kusimama imara dhidi ya upinzani. Daima kumbuka kwamba, kama vile Mungu alivyo na mpango kwa ajili ya maisha yako ya baadaye, ndivyo na adui alivyo na mpango. Na adui daima atapinga mpango wa Mungu kwa maisha yako. Naomba kwamba Mpango wa Mungu utafanikiwa na wa adui utashindwa katika maisha yako.

Maadamu unatembea karibu na Bwana, ishi kwa utii kwa njia yake, endelea kusoma Neno Lake, kataa kumtilia shaka Mungu, mtukuze kwa sifa na ibada, ruhusu upendo Wake ukutie moyo katika mahusiano yako yote, mtafute kwa kila uamuzi unaofanya, jikabidhi Kwake kila siku, na usali kwa Mungu katika Jina la Yesu kuhusu kila kitu, huwezi kwenda mrama. Mwombe Mungu akusaidie kufanya yote hayo. Haijalishi nini kitatokea, usikate tamaa kwa Bwana, kwani Yeye kamwe hajakata tamaa juu yako.

Mungu habadiliki. Yeye ni YuleYule jana, leo, na hata milele (Waebrania 13:8).

Yeye Ameahidi mambo mengi kwako, yakiwemo matumaini na mustakabali mzuri. Kwa hivyo haijalishi kile kinachotokea kwako au katika maisha yako, ahadi hizo zitakamilika na kusimama daima. Kila siku weka mustakabali wako mikononi mwa Mungu, kwa sababu jambo muhimu Zaidi kuhusu maisha yako ya baadaye ni kile Anachosema Mungu na anachofanya Mungu juu yako. Yeye Ndiye maisha yako ya jana, leo na baadaye. Mustakabali wako utapatikana kwa kutembea na Yeye leo. Unapofanya hivyo, Mungu atakuwa anakutayarisha kila siku kwa ajili ya siku zijazo alizonazo kwa ajili yako. Usikate tamaa ikiwa mambo hayaonekani kutokea haraka kama wengine. Hiyo ni kwa sababu wakati Mungu anafanya mambo kutokea ndani maisha yako, Yeye pia anafanya kazi muhimu zaidi ndani yako wewe. Kuna masomo anataka ujifunze. Mwambie akusaidie ujifunze na kuyaelewa masomo hayo vizuri kama mwana au mzazi.

Ninaweza kuwa hai kwa muda mrefu au kesho nitakuwa nimeenda. Chochote kitakachotokea, nimeomba kuhusu kila kipengele cha maisha yako. Ninajua kwamba Nikifa, siku moja nitafufuliwa na kisha nitakuwa mbinguni pamoja na Bwana, lakini upendo wangu na maombi yangu yatakuwa pamoja nanyi siku zote. Nataka kuwa na uhakika kwamba siku moja nitakuona mbinguni pia. Nataka uweze kusema, “Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, imani nimeilinda. Hatimaye,

nimewekekewa taji ya haki, ambayo Bwana, Mwamuzi Mwenye haki, atanipa mimi siku hiyo, na si kwangu tu, bali na kwa wote waliopenda Kufunuliwa Kwake" (2 Timotheo 4:7-8).

Mungu anasema wewe mpokee Yesu moyoni mwako, kesho yako ya milele iko salama. Hakikisha maisha yako ya baadaye yanabaki salama kwa kutogeuka na kumwacha Bwana. Hatimaye, ninakuambia maneno haya ya tumaini kutoka kwa Bwana, "Inuka uangaze; kwa maana nuru yako imekuja! Na utukufu wa BWANA umekuzukia juu yako. Kwa maana tazama, giza litaifunika dunia, na giza nene litafunika kabila za watu; lakini BWANA atainuka juu yenu, na utukufu Wake utaonekana juu yako" (Isaya 60:1-2). Kumbuka hilo hata katika nyakati za giza za maisha yako, nuru ya Yesu ndani yako na juu yako haiwezi kamwe kuzima. Nakupenda siku zote. Mama/Baba

## NGUVU YA MAOMBI

Bwana, ninaomba ………….. (jina la mtoto) kuwa na siku zijazo nzuri, ndefu, zenye kufanikiwa, na salama kwa sababu kesho yake iko mikononi Mwako. Asante kwa kuwa mawazo yako kwake ni mawazo ya amani na kumpa tumaini siku zijazo (Yeremia 29:11). Mwongoze kila hatua ili kamwe asiondoke kwenye njia uliyo nayo kwa ajili yake. Uelekeze moyo wake Kwako ili kwamba yeye daima apende njia Yako na njia Zako zijae akilini. Mzuie yeye asitoke na kupoteza muda kwenye njia ambazo Wewe Hutabariki. Msaidie kukimbia mbio kwa njia ifaayo, ili amalize safari ya maisha yake kwa nguvu na kupokea tuzo uliyo nayo kwa ajili yake (1

Wakorintho 9:24).

Naomba kwamba yeye atapandwa imara katika nyumba yako ili asitawi ndani Yako na daima atastawi na kuzaa matunda hata uzeeni (Zaburi 92:13-15). Msaidie akumbuke kwamba Wewe “unaweza kufanya mambo makubwa sana zaidi ya yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yake” (Waefeso 3:20). Ninaomba kwamba hakuna kitakachomtenganisha yeye na upendo Wako, ambao hupatikana katika Kristo Yesu (Warumi 8:38-39).

Asante, Roho Mtakatifu, kwamba daima utakuwa naye ili kumuongoza na kumfundisha, na kumletea faraja katika nyakati ngumu. Ninaomba kwamba mustakabali wake uendelee kukua na kung'aa kila kukicha. Ninaomba kwamba mustakabali wake wa mwisho wa maisha yake iwe ni pamoja nawe mbinguni, na kwamba nami nitakuwa huko ili kumwona yeye tena. Ninaomba kwamba Wewe Mungu wa matumaini umjaze yeye na furaha Yako na amani ili yeye "azidi kuwa na tumaini kwa nguvu za Roho Mtakatifu" (Warumi 15:13). Katika Jina la Yesu ninaomba. Amina.

## NGUVU YA NENO

Amebarikiwa mtu yule anayemtegemea BWANA, ambaye BWANA ni tumaini lake. Kwa maana atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji, unaoeneza mizizi yake karibu na mto; wala haitaogopa wakati wa hari; lakini jani lake litakuwa bichi, wala halitanyauka wakati wa ukame, wala hautaacha kuzaa matunda.

**YEREMIA 17:7-8**

Mwangalie mtu mkamilifu, umtazame mtu mnyofu; maana siku zijazo za mtu huyo ni amani.

**ZABURI 37:37**

Bali njia ya wenye haki ni kama nuru inayong'aa, hata mchana mkamilifu.

**MITHALI 4:18**

Hakika kuna tumaini kwako wakati ujao, na tumaini lako halitakatiliwa mbali.

**MITHALI 23:18**

Jicho halijaona, wala sikio halijasikia, wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu Mambo ambayo Mungu amewaandalia wale wampendao.

**1 WAKORINTHO 2:9**




Mambo ya Kibiblia ambayo kila Mkristo anapaswa kuombea

Hata watoto wako wajifunzie kuombea wengine

Mei 14, 2024 | Blogu,

Kama ningewauliza waumini mia moja swali, "Je, mmeridhika na maisha yenu ya ya maombi?" Nadhani kungekuwa na wachache tu ambao wangesema kwa ujasiri kwamba wameridhika. Hiyo ni kwa sababu wengi wetu tunajitahidi kuomba. Tunajitahidi kupata muda. Tunajitahidi kubaki makini na macho katika maombi. Tunapofanya hivyo, muda wetu wa maombi mara nyingi huwa mfupi na wa juujuu, au tunajikuta tunaomba mambo yaleyale machache mara kwa mara. Je, kuna njia ya kubadilisha hili? Tunawezaje kukuza maisha ya maombi ya kina zaidi?

Vipi kama tungeangalia Biblia kwa mwongozo wa nini cha kuomba? Vipi kama tungeomba Maandiko? Wiki hii niliamua kuchimba zaidi ndani ya Biblia na nikatafuta kauli kuhusu maombi na kuhusu mambo ambayo Mungu anasema tuyafuate kama waumini. Haya ndiyo matokeo: Mambo 36 ya kibiblia ambayo kila Mkristo anapaswa kuombea.

Omba kwa ajili ya...

Jina la Mungu liheshimiwe na kutukuzwa (Mt.6:9).

Ufalme wa Mungu usonge mbele (Mt.6:10).

Ujuzi wa mapenzi ya Mungu (Kol.1:9), na utii Kwake (Mt.6:10).

Kukua kwa maarifa ya Mungu (Kol.1:10) yanayotokana na Neno Lake (Matendo 17:11).

Kumtegemea Mungu ili akupatie kila hitaji lako (Mt.6:11, Flp.4:19).

Furaha iliyojikita katika Yesu (Flp.4:4, 1 Thes.5:16).

Moyo usiogawanyika unaomcha Mungu (Zaburi 86:11, Mithali 9:1).

Chuki ya dhambi na uovu (Rum.16:19, Zab.97:10, Rum.12:21) na hamu ya haki (Mathayo 5:6).

Msamaha kutoka kwa Mungu unapotenda dhambi (1 Yohana 1:9).

Ushirika wa Karibu na Mungu (1 Yohana 1:6)

Moyo unaowasamehe wengine (Efe.4:32, Kol.3:13).

Mtazamo wa shukrani kwa wokovu wa Mungu (1 Petro 1:3-5) na matayarisho yake mengi (1 Wathesalonike 5:18, Zaburi 9:1-2).

Uwezo wa kuonyesha rehema na neema (Hosea 6:6, Mathayo 5:7).

Maadui zenu na wale wanaowatesa (Mathayo 5:44).

Moyo wa unyenyekevu na toba (Yakobo 4:6-10).

Utambuzi wa kujua mema na mabaya (Wafilipi 1:9-10, 1 Yohana 4:1).

Ukombozi kutoka majaribuni (Mt.6:13, 1 Kor.10:13, Mathayo 26:41).

Uhuru kutoka kwa uongo wa Shetani (Yohana 8:32, 44) na ushindi katika vita vya kiroho na vita (Waefeso 6:12).

Mguso wa uponyaji wa Mungu na/au neema ya kuvumilia mateso, chochote kile ambacho kingeleta utukufu zaidi kwa Yesu (Matendo 4:30, Yakobo 5:14-16, 2 Kor. 12:7-10).

Ujasiri katika kushiriki injili (Efe.6:18-19, Rum.1:16, Matendo 4:29).

Mungu kuondoa upofu wa kiroho wa wasioamini (Yohana 12:40, 2 Kor.4:3-4) na kuwaleta kwenye toba (2 Petro 3:9) na wokovu (Rum.10:1).

Mungu kuinua wafanyakazi zaidi kwa ajili ya shamba la mavuno (Mt.9:38).

Wamishenari (Rum.15:30-31) kwamba Mungu angewategemeza na kuwatumia watoto kuendeleza kuenea kwa injili.

Viongozi wa kanisa, kuhubiri kwa bidii na kufuata Ukweli (Ebr.13:7, Efe.6:19, 2

The.3:1).

Mamlaka zinazoongoza na viongozi kufanya maamuzi ya busara na ya haki ambayo yatawanufaisha waumini (1 Tim.2:1-4, Mit.21:1).

Imani kubwa zaidi kwa Mungu (Marko 9:24, Luka.22:32).

Hekima ya kuelewa nyakati na kujua jinsi ya kuishi kwa uaminifu kwa ajili ya Bwana (1 Mambo ya Nyakati 12:32, Yakobo 1:5).

Umoja na ukuaji katika kanisa (Yoh. 17:20-21, Matendo 2:47).

Kujitoa kwa kazi ya Mungu ya kujitakasa ili kukufanya ufanane zaidi na Kristo (Rum. 8:29, 2 Kor. 3:18, 1 The. 4:3).

Bidii katika kuwafundisha watoto wako Neno la Mungu na kumpenda na kumtumikia Mungu wa Neno (Kum. 6:4-7).

Uelewa wa kina wa upendo wa Kristo (Efe. 3:14).

Upendo wa kweli zaidi kwa wengine unaoonekana kwa maneno na matendo (Yohana 13:34-35, 1 Kor. 13:4-8).

Uvumilivu na uaminifu katika kumtumikia Mungu kwa wakati wako, talanta, na pesa (1 Kor. 15:58, Mathayo 25:21,23).

Utimilifu wa Roho Mtakatifu (Luka 11:13) ili kuzaa matunda ya Roho (Gal. 5:22-23).

Njaa na kiu ya Neno la Mungu (Mt. 4:4).

Uwezo wa kuvumilia mateso na magumu kwa uaminifu na furaha ya subira (Kol. 1:11, Yakobo 1:2-4)


MAMBO YA
36
AMBAYO KILA
MWAMINI
anapaswa kuombea
HATA WATOTO WAKO WAJIFUNZE KUOMBEA WENGINE
Kama ningewauliza waumini mia moja swali, "Je, mmeridhika na maisha yenu ya maombi?" Nadhani kungekuwa na wachache tu ambao wangesema kwa ujasiri kwamba wameridhika. Hiyo ni kwa sababu wengi wetu tunajitahidi kuomba. Tunajitahidi kupata muda. Tunajitahidi kubaki makini na macho katika maombi. Tunapofanya hivyo, muda wetu wa maombi mara nyingi huwa mfupi na wa juujuu, au tunajikuta tunaomba mambo yaleyale machache mara kwa mara. Je, kuna njia ya kubadilisha hili? Je, tunawezaje kukuza maisha ya maombi ya kina zaidi?
Vipi kama tungeangalia Biblia kwa mwongozo wa nini cha kuomba? Vipi kama tungeomba kutokana na Maandiko?
Wiki hii niliamua kuchimba zaidi ndani ya Biblia na nikatafuta kauli kuhusu maombi na kuhusu mambo ambayo Mungu anasema tuyafuate kama waumini.
Haya ndiyo matokeo: Mambo 36 ya kibiblia ambayo kila Mkristo anapaswa kuombea.
Omba kwa ajili ya...
1 Jina la Mungu liheshimiwe na kutukuzwa (Mt.6:9).
2 Ufalme wa Mungu usonge mbele (Mt.6:10).
3 Ujuzi wa mapenzi ya Mungu (Kol.1:9), na utii Kwake (Mt.6:10).
4 Kukua kwa maarifa ya Mungu (Kol.1:10) yanayotokana na Neno Lake (Matendo 17:11).
5 Kumtegemea Mungu ili akupatie kila hitaji lako (Mt.6:11, Flp.4:19).
6 Furaha iliyojikita katika Yesu (Flp.4:4, 1 Thes.5:16).
7 Moyo usiogawanyika unaomcha Mungu (Zaburi 86:11, Mithali 9:1).
8 Chuki ya dhambi na uovu (Rum.16:19, Zab.97:10, Rum.12:21) na hamu ya haki (Mathayo 5:6).
9 Msaamha kutoka kwa Mungu unapotenda dhambi (1 Yohana 1:9).
10 Ushirika wa Karibu na Mungu (1 Yohana 1:6)
11 Moyo unaowasamehe wengine (Efe.4:32, Kol.3:13).
12 Mtazamo wa shukrani kwa wokovu wa Mungu (1 Petro 1:3-5) na matayarisho yake mengi (1 Wathesalonike 5:18, Zaburi 9:1-2).
13 Uwezo wa kuonyesha rehema na neema (Hosea 6:6, Mathayo 5:7).
14 Maadui zenu na wale wanaowatesa (Mathayo 5:44).
15 Moyo wa unyenyekevu na toba (Yakobo 4:6-10).
16 Utambuzi wa kujua mema na mabaya (Wafilipi 1:9-10, 1 Yohana 4:1).
17 Ukombozi kutoka majaribuni (Mt.6:13, 1 Kor.10:13, Mathayo 26:41).
18 Uhuru kutoka kwa uongo wa Shetani (Yohana 8:32, 44) na ushindi katika vita vya kiroho na vita (Waefeso 6:12).
19 Mguso wa uponyaji wa Mungu na/au neema ya kuvumilia mateso, chochote kile ambacho kingeleta utukufu zaidi kwa Yesu (Matendo 4:30, Yakobo 5:14-16, 2 Kor. 12:7-10).
20 Ujasiri katika kushiriki injili (Efe.6:18-19, Rum.1:16, Matendo 4:29).
21 Mungu kuondoa upofu wa kiroho wa wasioamini (Yohana 12:40, 2 Kor.4:3-4) na kuwaleta kwenye toba (2 Petro 3:9) na wokovu (Rum.10:1).
22 Mungu kuinua wafanyakazi zaidi kwa ajili ya shamba la mavuno (Mt.9:38).
23 Wamishenari (Rum.15:30-31) kwamba Mungu angewategemeza na kuwatumia watoto kuendeleza kuenea kwa injili.
24 Viongozi wa kanisa, kuhubiri kwa bidii na kufuata Ukweli (Ebr.13:7, Efe.6:19, 2 The.3:1).
25 Mamlaka zinazoongoza na viongozi kufanya maamuzi ya busara na ya haki ambayo yatawanufaisha waumini (1 Tim.2:1-4, Mit.21:1).
26 Imani kubwa zaidi kwa Mungu (Marko 9:24, Luka.22:32).
27 Hekima ya kuelewa nyakati na kujua jinsi ya kuishi kwa uaminifu kwa ajili ya Bwana (1 Mambo ya Nyakati 12:32, Yakobo 1:5).
28 Umoja na ukuaji katika kanisa (Yoh. 17:20-21, Matendo 2:47).
29 Kujitoa kwa kazi ya Mungu na kujitakasa ili kutufanya ufanane zaidi na Kristo (Rum. 8:29, 2 Kor. 3:18, 1 The. 4:3).
30 Bidii katika kuwafundisha watoto wako Neno la Mungu na kumpenda na kumtumikia Mungu wa Neno (Kum. 6:4-7).
31 Uelewa wa kina wa upendo wa Kristo (Efe. 3:14).
32 Upendo wa kweli zaidi kwa wengine unaoonekana kwa maneno na matendo (Yohana 13:34-35, 1 Kor. 13:4-8).
33 Uvumilivu na uaminifu katika kumtumikia Mungu kwa wakati wako, talanta, na pesa (1 Kor. 15:58, Mathayo 25:21,23).
34 Utimilifu wa Roho Mtakatifu (Luka 11:13) ili kuzaa matunda ya Roho (Gal. 5:22-23).
35 Njaa na kiu ya Neno la Mungu (Mt. 4:4).
36 Uwezo wa kuvumilia mateso na magumu kwa uaminifu na furaha ya subira (Kol. 1:11, Yakobo 1:2-4)
MaarifaMtandaoni.com
RohoYaUnabii.Org


JE, TUOMBEE NINI?
KILA AHADI YA MUNGU NI JAMBO LA KUOMBEA
KUNA AHADI ZAIDI YA 10,000 KATIKA MAANDIKO,
KWENYE MAFUNGU 32,102 YA MAANDIKO
SOMA NA OMBEA HIZI AHADI!
MAKUNDI MATATU YA KUOMBEA
1
WEWE NA MAHITAJI YAKO
2
WENGINE NA MAHITAJI YAO
3
UFALME WA MUNGU UJE
NA MAHITAJI YA UFALME HUU!
Msifu Mungu kwa Jinsi Alivyo
Mshukuru Mungu kwa Yale Aliyoyafanya
Ombea Upendo na Neema ya Mungu Kwako
Omba Upende Majirani Zako
Zungumza na Mungu Kuhusu Mtu Mwenye Uhitaji
Ombea Mtu Ambaye Hajamjua Yesu
Omba Upende Adui Zako
Omba Utoe Wakati Wako, Pesa na Nguvu kwa Ufalme
Omba kwa ajili ya Kanisa Lako au Jumuiya ya Kikristo
Ombea Jiji Lako, Taifa na Viongozi wa raia
Ombea Fadhila
Omba kwamba Mungu aimarishe Ufalme Wake
Omba kwamba Mungu ainue Ufalme Wake katika Ulimwengu Huu
Omba kwa ajili ya Unyenyekevu
Omba kwa ajili ya Ufundishwaji
Omba kwa ajili ya Uwezo wa Kusamehe
Omba kwa ajili ya Utiifu
Ombea Akili Yako Ifanywe Upya
Omba kwa ajili ya Usafi wa moyo
Omba kwa ajili ya Uwajibikaji
Ombea Tumaini na Ujasiri
SOMA MAANDIKO. OMBEA AHADI.
ONEKANA KWA IMANI. POKEA KWA SHUKRANI.
MaarifaMtandaoni.com
RohoyaUnabii.com

# 31 Days OF PRAYER FOR YOUR ADULT CHILDREN

A COLLECTION OF BIBLICALLY BASED PRAYERS AND BLESSINGS FROM THE "PRAYING THE SCRIPTURES" BOOK SERIES BY JODIE BERNDT.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **1 SALVATION** | **2 IDENTITY & PURPOSE** | **3 FRIENDSHIPS** | **4 DIRECTION** | **5 SAFETY** | **6 FAVOR** | **7 WISDOM** |
| May ________ believe in their heart and profess with their mouth that Jesus is Lord. (Romans 10:9) | Show ________ that they are God's handiwork, created in Christ Jesus to do good works, which God prepared in advance. (Ephesians 2:10) | Surround ________ with a community of believers who will carry each other's burdens and not play the comparison game. (Galatians 6:2-4) | Instruct ________ and teach them in the way they should go; counsel them with your loving eye on them. (Psalm 32:8) | Keep ________ from all harm; watch over their coming and going, now and forevermore. (Psalm 121:7-8) | May your favor rest on ________. Establish the work of their hands and make their efforts successful. (Psalm 90:17) | Fill ________ with the knowledge of your will through all spiritual wisdom and understanding; may they please you in every way. (Colossians 1:9-10) |
| **8 GRATITUDE** | **9 JOY & PEACE** | **10 WORK ETHIC** | **11 LOVE FOR SCRIPTURE** | **12 TIME MANAGEMENT** | **13 KIND SPEECH** | **14 HONESTY & INTEGRITY** |
| Prompt ________ to give you thanks, knowing that wealth, honor, strength, power, and everything they have comes from you. (1 Chronicles 29:12-13) | Fill ________ with all joy and peace as they trust in you so that they may overflow with hope by the power of the Holy Spirit. (Romans 15:13) | Whatever ________ do, may they work with all their heart, as working for the Lord and not for human masters. (Colossians 3:23) | May ________ take delight in your decrees and never neglect your word. (Psalm 119:16) | Teach ________ to number their days; help them spend them wisely. (Psalm 90:12) | Let no unwholesome talk come out of ________'s mouth, but only what is helpful for building others up according to their needs. (Ephesians 4:29) | Cause ________ to walk in integrity and experience security, since those who take crooked paths will be found out. (Proverbs 10:9) |
| **15 APTITUDE** | **16 WAITING** | **17 TRANSFORMATION** | **18 COMPASSION & LOVE** | **19 RESTORATION** | **20 HEALTH & HEALING** | **21 PRAYERFULNESS** |
| May ________ show aptitude for every kind of learning, be well informed, quick to understand, and qualified to serve. (Daniel 1:4) | When ________ has to wait on your provision or timing, may they be strong and take heart and wait well. (Psalm 27:14) | Do not let ________ conform to worldly patterns; instead, may they be transformed by the renewing of their minds. (Romans 12:2) | Clothe ________ with compassion and humility. Equip them to be patient with others, quick to forgive, and marked by love. (Colossians 3:12-14) | When ________ falls, let them sense your loving presence. Restore their joy and give them a spirit that is willing to obey you. (Psalm 51:11-12) | Bring health and healing to ________; let them enjoy abundant peace and security. (Jeremiah 33:6) | Teach ________ to be joyful in hope, patient in affliction, and faithful in prayer. (Romans 12:12) |
| **22 TRUST** | **23 CHOICES** | **24 ANXIETY** | **25 ADDICTION** | **26 LEADERSHIP** | **27 MARRIAGE** | **28 STRENGTH** |
| Help ________ trust in you with all their heart instead of leaning on their own understanding. (Proverbs 3:5) | Work in ________, giving them the desire and the power to do what pleases you. (Philippians 2:13 NLT) | May ________ not be anxious or afraid, but instead cast their cares on you, knowing that you care for them. (1 Peter 5:7) | Keep ________ safe from the traps of drugs, alcohol, sex, or any other snares set by those who do wrong. (Psalm 141:9) | Make ________ wise. Equip them to lead many to righteousness so that they shine like the stars, for ever and ever. (Daniel 12:3) | Let ________ enjoy a marriage marked by mutual love, submission, self-sacrifice, caring, unity, and respect. (Ephesians 5:24-32) | Grant ________ strength when they are weary and increase their power when they feel weak. (Isaiah 40:29) |
| **29 GENEROSITY** | **30 PARENTING** | **31 BLESSING** | | | | |
| Prompt ________ to be rich in good deeds, generous, and willing to share. (1 Timothy 6:18) | As ________ raises a family, carry them close to your heart and lead them as they care for their young. (Isaiah 40:11) | Bless ________ and keep them. Make your face shine on them and be gracious to them. Give them peace. (Numbers 6:24-26) | | | | |

*May the Lord encourage your hearts and strengthen you in every good deed and word.* 2 THESSALONIANS 2:17

Jodie

www.jodieberndt.com

© JodieBerndt